# FASIRI HURU YA BIBLIA

## ***UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!***

### *Safari ya Nne ya Paulo ya Umisionari:*
### *1 Timotheo, Tito & 2 Timotheo*

NA BOB UTLEY,
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI
(UTAFASILI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO
AGANO LA KALE, VOL.09

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
2013

# ORODHA YA YALIYOMO

Vifupisho vilivyotumika katika Fasiri hii ........ i

Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ........ ii

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika ........ iv

Fasiri

Utangulizi wa Nyaraka za Kichungaji ........ 01

1 Timotheo 1 ........ 07

1 Timotheo 2 ........ 34

1 Timotheo 3 ........ 56

1 Timotheo 4 ........ 75

1 Timotheo 5 ........ 94

1 Timotheo 6 ........ 107

Utangulizi wa Tito ........ 124

Tito 1 ........ 126

Tito 2 ........ 142

Tito 3 ........ 162

2 Timotheo 1 ........ 174

2 Timotheo 2 ........ 193

2 Timotheo 3 ........ 212

2 Timotheo 4 ........ 221

Viambatisho

Maelezo mafupi ya muundo wa Visarufi vya Kiyunani ........ 235

Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi ........ 244

Farahasa ........ 248

Kauli ya Mafundisho ........ 257

# MADA MAALUM: ORODHA YA YALIYOMO


Masihi, 1:1 ........ 09

Timotheo, 1:2 ........ 10

Baba, 1:2 ........ 11

Adilisha, 1:4 ........ 14

Moyo, 1:5 ........ 15

Maoni ya Paulo  Juu ya sheria ya Mussa, 1:8 ........ 16

Wema na Uovu katika Agano Jipya, 1:9 ........ 17

Kujamiiana kwa Jinsia moja, 1:10 ........ 18

Shukurani, 1:12 ........ 20

Matumizi ya Paulo ya “Huper” ambatani, 1:14 ........ 24

Matumizi ya Paulo ya Kosmos, 1:15 ........ 25

Imani, Kuamini, kutumaini, 1:16 ........ 26

Milele, 1:17 ........ 29

Unabii wa Agano Jipya, 1:18 ........ 30

Maombi ya Kusihi, 2:1 ........ 35

Serikali ya Wanadamu, 2:2 ........ 38

“Kweli” katika maandiko ya Paulo, 2:4 ........ 41

Imani Juu ya Mungu mmoja, 2:5 ........ 42

Fidia, Komboa, 2:6 ........ 44

Maombi Yasiyo na Ukomo Ingawa yana Ukomo, 2:8 ........ 48

Wanawake Katika Biblia, 2:12 ........ 51

Mitazamo ya Kibiblia Juu ya Kileo na Ulevi, 3:3 ........ 60

Kanisa, 3:5 ........ 62

Shetani, 3:6 ........ 63

Kuhukumu (Je Wakristo Wahukumiane Wao kwa Wao?), 3:7 ........ 65

Mpango wa Mungu wa Ukombozi “Siri”, 3:9 ........ 66

Sifa za Wanawake Wafanyakazi wa Kanisa, 3:12 ........ 69

Mwili (sarx), 3:16 ........ 72

Kupaa, 3:16 ........ 73

Kurudi kwa Mara ya Pili Kulikocheleweshwa, 4:1 ........ 76

Ukanaji wa Imani (*Aphistem*), 4:1 ........ 77

Pepo (Pepo wachafu), 4:2 ........ 79

Dhambi Mpaka Mauti, 4:2 ........ 81
Utauwa, 4:7 ........ 85
Mpango wa Ukombozi wa YHWH wa Milele, 4:10 ........ 86
Muundo (*Tupos*), 4:12 ........ 88
Kuwekewa Mikono, 4:14 ........ 89
Hitaji la Ustahimilivu, 4:16 ........ 91
Mzee, 5:1 ........ 95
Kuzeeka kwa Mwanadamu, 5:1 ........ 96
Watakatifu, 5:10 ........ 101
Maonyo ya Paulo kwa Watumwa, 6:1 ........ 108
Wingi wa Mali, 6:8 ........ 111
Maneno ya Kiyunani kwa Majaribu na Visawe Vyake, 6:9 ........ 113
Umilele, 6:9 ........ 114
Uchaguzi/Kuamriwa kabla na Hitaji la Uwiano wa Kithiolojia, 6:12 ........ 116
Ukiri, 6:12 ........ 117
Amina, 6:16 ........ 120
Enzi Hii na Enzi Ijayo, 6:17 ........ 120
Nadharia ya Elimu ya Ujuzi, 1:1 ........ 128
Tumaini, 1:2 ........ 129
Umri na Utengenezaji wa Nchi, 1:2 ........ 129
Unyenyekevu (*Hupatasso*), 2:5 ........ 145
Kuamriwa Kabla (*Calvinism*) Dhidi ya Utashi Huru wa Kibinadamu (*Arminiasm*), 2:11 ........ 149
Haki, 2:12 ........ 152
Maneno ya Agano Jipya ya Kurudi kwa Kristo, 2:13 ........ 155
Utukufu, 2:13 ........ 157
Mamlaka (*Exousia*), 2:15 ........ 159
Arche, 3:1 ........ 164
Ubatizo, 3:5 ........ 167
Utatu, 3:6 ........ 168
Majina ya Uungu, 1:1 ........ 175
Kwanini Wakristo Wanateseka, 1:8 ........ 182
Wokovu(Njeo za Vitenzi vya Kiyunani), 1:9 ........ 182
Kuitwa, 1:9 ........ 183
Batili na Utupu (*Katargeo*), 1:10 ........ 184

Dhamana, 1:12 ........ 186
Siku Hiyo, 1:12 ........ 188
Utu wa Roho, 1:14 ........ 189
Mafundisho ya Kichungaji, 1:14 ........ 190
Agano, 2:1 ........ 194
Ustahimilivu, 2:11 ........ 198
Kutawala katika Ufalme wa Mungu, 2:12 ........ 200
Tabia za Mungu wa Israeli, 2:19 ........ 204
Jiwe Kuu la Pembeni, 2:19 ........ 204
Muhuri, 2:19 ........ 205
Jina la Bwana, 2:19 ........ 206
Utakatifu/Utakaso wa Agano Jipya, 2:21 ........ 207
Toba katika Agano la Kale, 2:25 ........ 209
Mafundisho ya Kanisa la Kwanza, 3:15 ........ 218
Wafu Wako Wapi?, 4:1 ........ 222
Ufalme wa Mungu, 4:1 ........ 224
Roho (Pneuma) katika Agano Jipya, 4:22 ........ 232

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

AB Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman
ABD Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman
AKOT Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens
ANET Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard
BDB A Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs
IDB The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick
ISBE International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr
JB Jerusalem Bible
JPSOA The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America)
KB The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner
LAM The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa
LXX Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
MOF A New Translation of the Bible by James Moffatt
MT Masoretic Hebrew Text
NAB New American Bible Text
NASB New American Standard Bible
NEB New English Bible
NET NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition
NRSV New Revised Standard Bible
NIDOTTE New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren
NIV New International Version
NJB New Jerusalem Bible
OTPG Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith
REB Revised English Bible
RSV Revised Standard Version
SEPT The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970
TEV Today's English Version from United Bible Societies
YLT Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young
ZPBE Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni— ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la ($UBS^4$). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
Juni 27, 1996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.
Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?
Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja

nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

## DHANIO


1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe

Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.


## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji”

(utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.




Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya “mwitikio wa msomaji”  (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: “Biblia inaangazia zaidi katika fasihi”. Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile

kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

1. **Mzunguko wa kwanza wa usomaji**
   a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
      1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
      2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
      3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
   b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
   c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
   d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
      1) Agano la kale
         a) Simulizi za waebrania
         b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
         c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
         d) Alama za siri za ki-sheria
      2) Agano jipya
         a) Simulizi (Injili, matendo)
         b) Hadithi za mafumbo (Injili)
         c) Barua/nyaraka
         d) Fasihi za mafunuo
2. **Mzunguko pili wa usomaji**
   a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
   b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
   c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.
3. **Mzunguko wa tatu wa usomaji**.
   a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
   b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
      1) Mwandishi
      2) Tarehe
      3) Wapokeaji
      4) Kusudu mahsusi la uandishi
      5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
      6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
   c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
   d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji
4. **Mzunguko wa nne wa usomaji**
   a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
      1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
      2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
      3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)

b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
    1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
    2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    1) Istilahi muhimu
    2) Istahili zisizo za kawaida
    3) Muundo muhimu wa kisarufi
    4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
        a) Vitabu vya thiolojia
        b) Biblia za marejeo
        c) Itifaki
    2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
    3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
    1) Soma biblia
    2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
    3) Tangulizi za biblia
    4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji #3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1 Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi
   b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
   c. Habari za kisarufi
   d. Usomaji wa neno
   e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
   a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
   b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
   c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
   d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi kiyunani, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
   a. Tofauti za mswada
   b. Maana ya maneno mbadala
   c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
   d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# UTANGULIZI WA NYARAKA ZA KICHUNGAJI

# 1 & 2 TIMOTHEO na TITO

**MAELEZO YA UFUNGUZI**

A. Maeneo ya kijiografia yaliyotajwa katika 1 Timotheo, Tito, na 2 Timotheo hayaendani kwenye mpangilio wa matukio huenda ya Matendo au nyaraka zingine za Paulo
   a. Kuitembelea Efeso (kama vile 1 Tim. 1:3)
   b. Kuitembelea Troa (kama vile 2 Tim. 4:13)
   c. Kuitembelea Miletusi (kama vile 2 Tim. 4:20)
   d. mpango wa kwenda Krete (kama vile Tito 1:5)
   e. mpango wa kwenda Uhispania (toka kwa Clement wa Rumi, mwaka wa 95 B.K na utangulizi wa orodha ya vitabu vya zamani vya Agano Jipya, mwaka 180-200 B.K)

   Kwa hiyo, nafikiria kuwa Paulo alikuwa amekwisha aachiwa toka gerezani (mwanzo mwa miaka ya 60, ambayo imeandikwa kwenye I Clement 5, ikiandikwa yapata mwaka wa 95 B.K) na kuchukua safari ya nne ya umisionari, baadaye alipumuzishwa na kuuwawa mwaka wa 68 (kujiuwa kwa Nero).

B. Kusudi la huu waraka kwa pamoja umefikiriwa kuwa ni wa kiutawala zaidi (kusanyiko la kanisa). Hata hivyo, katika *New International Biblical Commentary*, Vol. 13, na I na 2 Timotheo na Tito, Gordon Fee alinishawishi mimi kuwa tukio kwsa ajili ya waalimu wa uongo waliojitokeza ndani ya makanisa ya nyumbani ya huko Efeso (1 Timotheo) na kwenye kisiwa cha Krete (Tito).

C. Kwa namna nyingine barua zilianzisha kipengere cha utawala chenye kufanana Kwa namna Fulani Nyaraka za Kichungaji zilianzisha utaratibu wa kiutawala unaofanana na Essenes' *Manual of Discipline* cha Waesene. Miongozo kwa na yote ilikuwa muhimu zaidi katika mwanga wa mwanzo na kusambaa kwa tofauti toka katika mafundisho ya Kitume na muundo.

D. Ufanano kati ya Nyaraka za Kichungaji na misamiati ya Luka kwenye kitabu cha Luka na Matendo yawezakuwa ni kwa sababu ya ukweli kwamba Paulo alijitumia kama mwandishi (kama vile C. F. C. Moule, *The Problem of the Pastoral Epistles: A Reappraisal*). S. G. Wilson hata katika kitabu cha *Luke and the Pastoral Epistles* kuwa hivi vitabu vitatu vyawezakuwa ni jaribio la Luka kuandika kitabu cha tatu akielezea kikundi cha injili huko Rumi.

E. kwa nini hivi vitabu vitatu kuwekwa pamoja? Yawezekana vinashughulika wakati/mahali/masuala? 1 Timotheo na Tito wana kitu cha kufanya na kundi la kanisa. Ni kweli (1) misamiati yao; (2) walimu wa uongo wakitaka kuviunganisha hivi vitabu vitatu; na (3) ukweli kiurahisi haviendani na mpangilio wa matukio ya Matendo (kama yakiwekwa pamoja).

## MWANDISHI

A. Barua zenyewe zinadai kutoka kwa Paulo Mtume (kama vile 1 Tim. 1:1; 2 Tim. 1:1; na Tito 1:1) kwenda kwa wawakilishi wake wawili, Timotheo na Tito.

B. Suala la uandishi wa nyaraka za Kichungaji lilianza kubishaniwa katika karne ya 19 na 20. Kukataliwa kwa uandishi wa Paulo mara nyingi kunaegamia juu ya
   1. kuanzishwa kwa kundi la kanisa (lenye sifa za uongozi)
   2. kuanzishwa kwa watu waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee (kulikoandikwa katika karne ya pili)
   3. kuanzishwa kwa thiolojia (maelezo ya kanuni ya imani)
   4. tofauti ya misamiati na muundo (moja ya tatu ya maneno hayatumiki katika maandiko mengine ya Paulo)

C. utofauti waweza kuelezewa
   1. haya ni maandiko ya misho ya Paulo, yumkini akimtumia Luka kama mwandishi
   2. misamiati na muundo ni wa kujitegemea katika kila tukio
   3. mawazo ya wenye ujuzi yalikuwa ni maendeleo ya mawazo ya Kiyahudi ya karne ya kwanza (kama vile Magombo ya Bahariya Chumvi)
   4. Paulo alikuwa ni mwana thiolojia aliyeng'ara na mwandishi mbunifu akiwa na misamiati mingi

D. kuna ukuaji wa uelewa wa mifano ya kihistoria
   1. utumiaji wa Paulo wa mwandishi mwenye weredi wa Kikristo (katika suala hili, yumkini akawa Luka)
   2. utumiaji wa Paulo wa watenda kazi wenza (yaani., sehemu ya timu yake ya umisheni, kama vile 2 Tim. 4:11)
   3. utumiaji wa Paulo wa liturujia au nukuu za nyimbo (mhutasari mzuri unapatikana katika *Dictionary of Paul and His Letters*, ukahaririwa na Hawthorne and Martin, kuchapishwa na IVP, uk. 664).

      Maoni kuwa sehemu ya Nyaraka za Kichungaji zimenukuliwa toka vyanzo vingine vinasaidia kuelezea idadi ya *hapax legomena* (maneno yalliyotumika mara moja tu katika Agano Jipya), nahau zisizo za Paulo, na utumiaji wa kipekee wa maneno ya Paulo
      a. nyimbo za kumsifu Mungu (kama vile 1 Tim. 1:17; 6:15-17)
      b. orodha ya maovu (kama vile 1 Tim. 1:9-10)
      c. tabia njema za wake (kama vile 1 Tim. 2:9-3:1a)
      d. sifa kwa ajili ya wahudumu (kama vile 1 Tim. 3:1b-13)
      e. nyimbo za ukiri (kama vile 1 Tim. 2:5-6; 3:16; 2 Tim. 1:9-10; Tito 3:3-7)
      f. nyimbo (kama vile 1 Tim. 6:11-12,15-16; 2 Tim. 2:11-13; Tito 2:11-14)
      g. Agano la Kale *midrash* (kama vile 1 Tim. 1:9-10; 2:9-3:1a; 5:17-18; 2 Tim. 2:19-21; Tito 3:3-7)
      h. Kanuni
         1) "mwaminifu ni neno" (kama vile 1 Tim. 1:15; 2:9-3:1a; 2 Tim. 2:11-13; Tito 3:3-8)
         2) "ukitambua ya kuwa" (kama vile 1 Tim. 1:9-10; 2 Tim. 3:1-5)
         3) "mambo haya" (kama vile 1 Tim. 4:6,11; 2 Tim. 2:14; Tito 1:15-16; 2:1)
      i. nukuu toka kwenye ushairi wa Kiyunani (kama vile Tito 1:12 [Epimenides na/au Euripides])

E. inashangaza kuwa karne ya pili yenye kudhaniwa "mwandishi Paulo" angalitaja maelezo hasa kama majina ya watu (yaani., Hemenayo, 1 Tim. 1:20; 2 Tim. 2:17; Iskanda, 1 Tim. 1:20; Zena, Tito 3:13) matukio (ugonjwa wa Trofimu huko Mileto, 2 Tim. 4:20; au kazi ya mjane, 1 Tim. 5:9) ambayo hayakutajwa mahali popote katika maandiko ya Paulo. Vitu hivi haviendani na dhanio la usanifishaji wa uongo.

   Kwa ajili ya makala juu ya majina ya uongo yahusianayo na nyaraka za Agano Jipya, angalia *An Introduction to the New Testament*, na Carson, Moo, na Morris, kur. 367-371.

## TAREHE

A. kama hili ni kweli kuwa Paulo aliachiwa toka gerezani (baada ya kukifunga kitabu cha Matendo, yumkini mwaka wa 59-61 B.K), hivyo kuna mapokeo yeyote ya mwanzo ya kazi zake baada ya kutoka gerezani (yaani.,kuhubiri huko Hispania, kama vile Rum. 15:24,28)?
   1. Nyaraka za Kichungaji (kama vile 2 Tim. 4:10)
   2. I Clement 5
      a. Paulo akahubiri sehemu za mashariki na magharibi (yaani.,Hispania)
      b. Paulo aliuwawa chini ya "viranja" (yaani., Tigellinus na Sabinus, waliohudumu kwenye mwaka wa mwisho wa utawala wa Nero mwaka wa 68 B.K)
   3. utangulizi wa vitabu vya kale vya Agano Jipya (orodha ya vitabu vya kanuni za kanisa toka Rumi yapata miaka ya. 180-200 B.K)
   4. Eusebius' *Historical Ecclesiastical History* 2:22:1-8, inasema kuwa Paulo alifunguliwa toka gereza la Rumi

B. Inaonekana kuwa 1 Timotheo na Tito waliandikwa kwa karibu pamoja kabla ya Paulo kukamatwa tena. 2 Timotheo ni maandiko ya mwisho ya Paulo na kwa heri akiwa gerezani

C. Uwezekano wa maandiko ya Paulo yenye mfuatano wa matukio ukifuatisha F. F. Bruce na Murry Harris ukiwa na mwendano mdogo.

| | Kitabu | Tarehe | Mahali pa uandishi | Uhusiano na Matendo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wagalatia | 48 | Shamu ya Antiokia | Mdo. 14:28; 15:2 |
| 2. | 1 Wathesalonike | 50 | Korintho | Mdo.18:5 |
| 3. | 2 Wathesalonike | 50 | Korintho | |
| 4. | 1 Wakorintho | 55 | Efeso | Mdo. 19:20 |
| 5. | 2 Wakorintho | 56 | Makedonia | Mdo. 20:2 |
| 6. | Warumi | 57 | Korintho | Mdo. 20:3 |
| 7.-10. | Barua za gerezani | | | |
| | Wakolosai | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| | Waefeso | nwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| | Filemoni | mwanzoni mwa 60 | Rumi | |
| | Wafilipi | mwishoni 62-63 | Rumi | Mdo. 28:30-31 |
| 11.-13. | Safari ya nne ya umisheni | | | |
| | 1 Timotheo | 63 (au baadaye, | Makedonia | |
| | Tito | 63 lakini kabla | Efeso(?) | |
| | 2 Timotheo | 64 68 B.K) | Rumi | |

## WAPOKEAJI

A. Jina la, waraka wa kichungaji, lilikuja toka D. N. Berdot's commentary mwaka wa 1703 B.K. linazungumza juu ya tabia za kipekee na maudhui yaliyomo. Timotheo na Tito, hata hivyo, sio wachungaji, bali mitume walioteuliwa.

B. Hizi barua ziliandikwa kwenda kwa makanisa, lakini chini ya muundo wa fasihi wa barua kwenda kwa watenda kazi wenza wa Paulo, Timotheo na Tito. Paulo aliuhutubia umati wa watu kama alivyolihutubia kundi la viongozi wake. Dondoo za Paulo mbele ya umati wa watu zilikuwa ni

1. utangulizi rasmi ukitaja utume wake
2. wingi wa neno "ninyi" kwenye hitimisho la barua zake zote tatu
3. utetezi wa Paulo juu ya wito wake (kama vile 1 Tim. 2:7)
4. maandiko ya Paulo kwa Timotheo kuhusu mambo aliyokwisha yajua pindi akiwa na Paulo (kama vile 1 Tim. 3:15)

## MAHALI/KUSUDI

A. kusudi kuu lilikuwa ni kupingana na waasi waliokuwa wakiibuka (kama vile 1 Tim. 1:3-7). Uasi wenyewe wawezakuwa ni wa muunganiko wa Wayahudi na tabia za wale wenye ujuzi (zaidi kama waalimu wa uongo wa Efeso na Kolosai). Yumkini palikuwepo na makundi mawili tofauti.

B. Agano la Kale linatoa mwongozo maalum kwa ajili ya kikundi cha jumuiya ya wenye imani. Agano Jipya halina maelekezo maalum kuhusiana na kikundi au utaratibu wa kanisa. Barua za kichungaji (1 Timotheo, 2 Timotheo, and Tito) zinaonekana kufanana kwa karibu kama ilivyo miongozo ya Agano Jipya.

C. 1 Timotheo aliandikwa

1. akimwomba Timotheo kubaki huko Efeso (kama vile 1 Tim. 1:3)

2. kushughulika na waalimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 1:19-20; 4:1-5; 6:4-5,20-21)
3. kusaidia kuuweka pamoja uongozi (kama vile 1 Tim. 3)

D. Tito alikuwa na majikumu kama hayo kushughulika nauasi na makundi ya huko Krete (kama vile Tito 1:5)

E. 2 Timotheo alimkuta Paulo akiwa gerezani akiwa na matumaini kidogo ya kuachiwa (kama vile 2 Tim. 4:6-8, 16-18)

F. Kuna maana nzito "mafundisho kamili" (yaani., mafundisho kamili) yanayosikika kwenye barua hizi (kama vile 1 Tim. 1:10; 4:6; 6:3; 2 Tim. 1:13; 4:3; Tito 1:9; 2:1) au "yanayosikika kwenye imani" (kama vile Tito 1:13; 2:2). Mungu aliyaaminisha haya "mafundisho kamili" kwa Paulo (kama vile 1 Tim. 1:11); Paulo akayaaminisha kwa Timotheo (kama vile 1 Tim. 6:20), na Timotheo alipaswa kuyaaminisha kwa watu waaminifu (kama vile 2 Tim. 2:2).

## WALIMU WA UONGO

A. Ni vigumu kuwazungumzia waalimu wa uongo kwa sababu ya kukosa maelezo muhimu ya karne ya kwanza. Paulo anawaandikia wale wote wanaowafahamu hawa waalimu wa uongo kabla. Yeye, kwa hiyo, kwa upana hazungumzii thiolojia yao, lakini mara nyingi akiyalaumu maisha yao na mienendo yao (kama afanyavyo Yuda).

B. suala kuu lililotafasiriwa lenye kuhusiana ikiwa walikuwa
   1. Wayahudi
   2. Wayunani
   3. Wote pamoja
      Waalimu wa uongo wanaonekana kuwa wenye mchanganyiko wa Wayahudi na wele waliodai kuwa na ujuzi wa kipekee. Nikwa vipi hawa waliweza kuyapinga makundi ya kidini yaliyoungana?
      a. Dini ya Kiyahudi hujumuisha baadhi ya vipengere vya pande mbili (kama vile Magombo ya Bahari ya Chumvi)
      b. Nadharia ya wale wenye ujuzi wa karne ya pili walianzisha hizi mada zilizozoeleka za thiolojia/falsafa za mashariki ya karibu
      c. Dini ya Kiyahudi ya wale waliokuwa uhamishoni ilikuwa huru zaidi kuliko watafiti wa kisasa waliofikiriwa huko nyuma
      d. kuna mifano ya karne ya kwanza kwa ajili ya waasi walioungana wa Kiyahudi na wale wenye ujuzi katika kitabu cha Wakolosai

C. baadhi ya vipengere vya hawa waalimu wa uongo
   1. Dhana ya Kiyahudi
      a. walimu wa uongo
         1) walimu wa sheria (kama vile 1 Tim. 1:7)
         2) kusanyiko la waliotahiriwa (kama vile Tito 1:10)
      b. walimu wa uongo walioonya kuhusu hadithi za Kiyahudi (kama vile 1 Tim. 3:9; Tito 1:14)
      c. waalimu wa uongo walishughulika na sheria za chakula (kama vile 1 Tim. 4:1-5)
      d. waalimu wa uongo walihusika na unasaba (kama vile 1 Tim. 1:4; 4:7; 2 Tim. 4:4; Tito 1:14-15; 3:9)
   2. Dhana za wale wenye ujuzi (angalia Mada Maalum kwenye Tito 1)
      a. wenye kukataa mambo ya starehe na msamaha
         1) wakikataza mambo ya ndoa (kama vile 1 Tim. 2:15; 4:3)
         2) wakikataa vyakula Fulani (kama vile 1 Tim. 4:4)
      b. unyonyaji wa kingono (kama vile 1 Tim. 4:3; 2 Tim. 3:6-7; Tito 1:11,15)
      c. wakisisitiza juu ya maarifa (kama vile 1 Tim. 4:1-3; 6:20)

## UTAKATIFUSHAJI

A. Nyaraka za Paulo zilikusanywa pamoja kwenye kitabu kimoja kilichoitwa "kitabu cha Mitume" na baadaye kuzunguka kwenye makanisa yote. Machapisho tu ya Kiyunani ya nyaraka za Paulo yaliyokosa kuwa na I na 2 Timotheo na Tito (pia 2 Wathesalonike na Filemoni) ni machapisho ya kwenye mafunjo toka miaka ya 200 yaliyoitwa $P^{46}$ (toka kwa Chester Beatty papyri). Hata hili ni madhanio tu kwa sababu machapisho hayo bado hayaonekani kwenye kurasa mbalimbali za haya mafunjo. Machapisho mengine ya Kiyunani ndani yake yana kile kinachoitwa "Waraka wa Kichungaji."

B. vyanzo vya kale vyenye kunukuu, kudokeza, au vyenye kutaja nyaraka za Kichungaji
   1. viongozi wa kanisa la mwanzo
      a. Barnaba mwenye jina bandia ( 70-130 B.K) ananukuu 2 Timotheo na Tito
      b. Clement wa Rumi ( 95-97 B.K) anadokeza kwa 1 Timotheo na 2 Timotheo na kunukuu Tito 3:1
      c. Polycarp ( 110-150 B.K) anadokeza kwa 1 Timotheo, 2 Timotheo, na Tito
      d. Hermas (115-140 B.K) ananukuu 1 Timotheo na 2 Timotheo
      e. Irenaeus (130-202 B.K) ananukuu mara nyingi toka 1 Timotheo, 2 Timotheo, na Tito
      f. Diognetus (150 B.K) anamnukuu Tito
      g. Tertullian ( 150-220 B.K) ananukuu 1 Timotheo, 2 Timotheo, na Tito
      h. Origen ( 185-254 B.K) ananukuu 1 Timotheo, 2 Timotheo, na Tito
   2. orodha ya vitabu vya sheria za kikanisa vyenye kuwa na nyaraka za Kichungaji
      a. Muratorian Fragment (toka Rumi yapata mwaka wa 200 B.K)
      b. Barococcio (mwaka wa 206 B.K)
      c. Orodha ya Cheltenham (mwaka wa 360 B.K)
      d. Orodha ya Kitume ( 300 B.K)
      e. Barua ya Athanasius ( 367 B.K)
   3. matoleo ya mwanzo yenye kujumuisha nyaraka za kichungaji
      a. Kilatini cha kale (mwaka wa 150-170 B.K)
      b. Shamu ya kale (mwaka wa 200 B.K)
   4. baraza la mwanzo la kanisa lenye kuthibitisha nafasi iliyovuviwa ya nyaraka za kichungaji
      a. Nicea (mwaka wa 325-340 B.K)
      b. Carthage (mwaka wa 397 na 419 B.K)
      c. Hippo (mwaka wa 393 B.K)

C. Mchakato wa maridhiano kati ya makusanyiko ya mwanzo ya Wakristo na himaya ya Warumi ulianzisha sheria za kikanisa. Maridhiano hakika yaliathiliwa na misukumo ya ndani na nje ya kijamii. Mahitaji ya kimsingi kwa ajili ya kuyaingiza kwenye sheria za kanisa yalionekana kuwa ni
   1. uhusiano kwa Mitume
   2. mwendelezo wa ujumbe pamoja na maandiko mengine ya Kitume
   3. maisha ya wale waliokabiliana na haya maandiko
   4. makubaliano yaliyoendelea kwenye orodha ya maandiko yaliyokubalika kati ya haya makanisa ya mwanzo

D. Hitaji kwa ajili ya sheria za kanisa lilianzishwa kwa sababu ya
   1. kuchelewa kwa ujio wa mara ya pili
   2. umbali wa kijiografia kati ya makanisa na Mitume
   3. vifa vya Mitume
   4. kuinuka kwa mwanzo kwa waalimu wa uongo
      a. Dini ya Kiyahudi
      b. Falsafa za Kiyunani
      c. mchanganyiko wa vipengele vya Kiyahudi na watu wenye ujuzi (Wakolosai)
      d. Dini za siri za Wayunani na Warumi (mf. Mithra)

Hili lilitokea pale injili ilipoanza kutawanyika kwenye tamaduni mbalimbali.

E. Suala la utakatifushaji kihistoria linahusiana na uandishi. Makanisa ya mwanzo yalikubaliana na nyaraka za kichungaji kama maandiko ya Paulo. Dhanio langu kuhusu utakatifushaji linajumuisha uhusika wa Roho, sio tu kwenye uandishi wa maandiko, bali pia kwenye kuyakusanya na kuyatunza. Swali la kiuandishi la Paulo (ambalo nalidhania) haliathiri uvuvio na utakatifushaji.

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.
Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.
Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# 1 TIMOTHEO 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Salamu | Salamu | Salamu | Utangulizi | Mahubiri |
| 1:1-2 | 1:1 | 1:1 | 1:1 | 1:1-2 |
| | 1:2a | 1:2a | 1:2a | |
| | 1:2b | 1:2b | 1:2b | |
| Maonyo juu ya mafundisho ya uongo | Hakuna utetezi mwingine | Utetezi wa kweli | Maonyo juu ya mafundisho ya uongo | Kuwakomesha waalimu wa uongo |
| 1:3-7 | 1:3-11 | 1:3-7 | 1:3-7 | 1:3-7 |
| 1:8-11 | | 1:8-11 | 1:8-11 | 1:8-11 |
| Shukrani kwa ajili ya rehema | Utukufu kwa Mungu kwa ajili ya neema yake | | Shukrani kwa ajili ya rehema ya Mungu | Paulo akiwa kwenye wito wake |
| 1:12-17 | 1:12-17 | 1:12-17 | 1:12-17 | 1:12-17 |
| | Pigeni vita vizuri | | | Wajibu wa Timotheo |
| 1:18-20 | 1:18-20 | 1:18-20 | 1:18-20 | 1:18-20 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.
Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.
Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure),Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi(Textual Criticism),Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko(Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 1:1**
**[1] Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na Kristo Yesu, taraja letu;**

**1:1 "Paulo"** Wengi wa Wayahudi enzi za Paulo walikuwa na majina mawili ya mwanzo, moja la Kiyahudi, jingine la Kirumi (kama vile Mdo. 13:9). Jina la Paulo la Kiyahudi lilikuwa ni Sauli. Yeye, kama alivyokuwa mfalme wa kale wa Israeli, alikuwa ni wa kabila la Benjamini (kama vile Rum. 11:1; Fil. 3:5). Jina lake la Kirumi katika muundo wa Kiyunani alikuwa akiitwa, Paulo (Paulos), likimaanisha "mdogo." Hili linarejelea kwa

1. Umbo lake la mwili ambalo liligusiwa kwenye kitabu kilichotambuliwa na kanisa karne ya pili, *The Acts of Paul,* katika sura inayohusu Mthesalonike aitwaye "Paulo na Tekla"
2. maana yake binafsi ya kuwa mdogo kati ya watakatifu kwa sababu mwanazoni alilitesa kanisa (kama vile 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15)
3. jina alilopewa na wazazi wake pindi anazaliwa

Uchaguzi #3 ni wenye kufaa.

◙ **"mtume"** Huu mzizi ni moja ya VITENZI vya Kiyunani vilivyozoeleka kwa ajili ya neno "kutuma." Hili neno lina matumizi mbalimbali ya kithiolojia.

1. Walimu wa dini ya Kiyahudi walilitumia kama mtu aliyeitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu Fulani kwa Kiingereza kama "balozi" (kama vile 2 Kor. 5:20).
2. Injili mara nyingi ilitumia muundo wa KITENZI cha hili neno la Yesu kama aliyetumwa na Baba.katika kitabu cha Yohana neno linachukuliana na vidokezo vya Kimasihi (kama vile Yohana 4:34; 5:24,30,36,37,38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,8,18,21,23,25; 20:21).
3. Lilitumika kwa Yesu akiwatuma waamini (kama vile Yohana 17:18; 20:21).
4. Lilitumika kwenye karama maalum za uongozi katika Agano Jipya.
   a. kwa ule mzunguko wa mwanzo wa wanafunzi kumi na wawili (kama vile Mdo. 1:21-22)
   b. kikundi maalum cha wasaidizi wa Kitume na watenda kazi wenza
      1) Barnaba (kama vile Mdo. 14:4,14)
      2) Androniko and Yunia (KJV, Junia, kama vile Rum. 16:7)
      3) Apollo (kama vile 1 Kor. 4:6-9)
      4) Yakobo nduguye na Yesu (kama vile Gal. 1:19)
      5) Silvanusi na Timotheo (kama vile 1 The. 2:6)
      6) yumkini Tito (kama vile 2 Kor. 8:23)
      7) yumkini Epaphrodito (kama vile Fil. 2:25)
   c. karama zilizokuwa zikiendelea kanisani (kama vile Efe. 4:11)
5. Paulo alitumia hili jina kwa ajili yake mwenyewe kwenye nyaraka zake nyingi kama njia ya kutetea mamlaka aliyopewa na Mungu kama mwakilishi wa Kristo (kama vile 1 Kor. 1:1; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; 2 Tim. 1:1). Hata kwenye waraka wake binafsi wa 1 Timotheo, haya mamlaka ni ya muhimu.
   a. mamlaka yake yalimpa Timotheo mamlaka
   b. alikuwa akikabiliana na walimu wa uongo
   c. waraka wake dhahili ulisomwa kwa kanisa zima

◙ **"wa Kristo Yesu"** Haya maneno ni sehemu ya jina kamili "Bwana Yesu Kristo." Haya majina matatu kipekee yana umuhimu.

1. "Kristo" ni tafasiri ya Kiyunani ya Waebrania *Masihi* (mpakwa mafuta). Linatetea nafasi ya Yesu ya Agano la Kale kama Yule aliyeahidiwa na Mungu akitumwa kuweka enzi mpya ya haki.
2. "Yesu" ni jina alilopewa na malaika akiwa mtoto huko Yerusalemu (kama vile Mt. 1:21). Linaundwa na nomino mbili za Kiebrania: "YHWH," jina la agano kwa ajili ya Uungu, na "wokovu" (kama vile Kut. 3:14). Ni jina linalofanana na lile la Kiebrania Yoshua. Likitumika peke yake likimtambulisha mwanamme, Yesu

Mnazareti, mwana wa Mariamu (mf., Mt. 1:16, 25; 2:1; 3:13,15,16; Mdo. 13:23,33; Rum. 8:11; 1 Kor. 11:23; 12:3; Efe. 4:21; Fil. 2:10; 1 The. 1:10; 4:14).

3. "Bwana" (likitumika katika 1 Tim. 1:1 kwenye toleo la KJV au katika 1 Tim. 1:12) ni tafasiri ya Kiebrania ya neno *adon*, yenye kumaanisha "mmiliki, mme, bwana, au bwana." Wayahudi waliogopa kulitamka jina tukufu la YHWH ili wasije wakalitamka bure na kuvunja moja ya amri zile kumi. Pale waliposoma maandiko, walitamka *Adon* kwa ajili ya YHWH. Hii ndiyo sababu tafasiri zetu za Kiingereza zinatumia herufi kubwa kwenye majina yote BWANA kwa ajili ya YHWH katika Agano la Kale. Kwa kulibadilisha hili jina (*kurios* katika Kiyunani) kwenda, waandishi wa Agano Jipya wanatetea Uungu Wake na kuwa sawa na Baba (kitu kile kile kinafanyika kwa taratibu za kilugha kwenye 1 Tim. 1:2 kukiwa na KIVUMISHI kimoja chenye kurejelea Mungu Baba na Yesu mwana, kama vile 1 The. 1:1; 2 The. 1:1,2).

◙**"kwa amri ya Mungu"** Hii ni namna mojawapo ya fasihi ya kutetea mamlaka ya Kitume ya Paulo. Huduma ya Paulo ilikuwa ni kwa"mapenzi ya Mungu" (kama vile 2 Tim. 1:1) na "amri ya Mungu" (kama vile Tito 1:3). Hili yumkini linarejelea kwenye wito wa Paulo akiwa njiani akielekea Dameski na habari ya kufunuliwa na Anania (kama vile Mdo. 9:1-22; 22:3-16; 26:9-18). Paulo hakuwa anajitolea!

◙ **"Mungu Mwokozi"** Hili ni jina la Agano la Kale kwa ajili ya uangalizi wa YHWH na ukombozi wa Israeli (kama vile Isa. 19:20; 43:3,11; 45:15,21; 49:26; 60:16; 63:8),hasa kuja kwake Mtumishi Atesekaye (kama vile Isa. 52:13-53:12). Hili jina linatumika kwa Mungu Baba katika Tito 1:3; 2:10 na 3:4 na kwa Mungu Mwana, Yesu, katika Tito 1:4; 2:13 na 3:6. Hii ni namna nyingine kithiolojia ya kuhusianisha Baba na Mwana.

Hili lilikuwa ni moja ya majina kwa ajili ya YHWH lililotumiwa na Kaisari. Kaisari wa siku za Paulo alidai kuwa yeye ni "Bwana," "Mwokozi," hata "mungu." Wakristo waliyatunza haya majina kipekee kwa ajili ya Yesu na kwa sababu ya hili walionekana kama wasaliti kwenye serikali ya Kirumi na jamii na waliteswa na kuuwawa kwa maelfu katika karne ya kwanza na ya pili. Angalia maelezo kamili katika 2 Tim. 1:10.

◙ **"Kristo"** Angalia MADA MAALUM: MASIHI ifuatayo.

## MADA MAALUM: MASIHI

Ugumu katika kutafasiri neno hili ni kwa sababu ya matumizi tofauti kuhusiana na neno lenyewe "Masihi" au "aliyetiwa mafuta" (BDB 603, KB 645). Neno lilitumika katika kumwekea mtu mafuta maalumu kuonyesha wito wa Mungu na kumkabidhi majukumu ya uongozi.

1. Lilitumika kwa wafalme wa Kiyahudi (mf. 1 Sam. 2:10; 12:3; 24:6, 10;2 Sam. 19:21; 23;1; Zab. 89:51; 132:10, 17; Wim. 4:20; Hab. 3:13; "Malkia mtiwa mafuta" katika Dan. 9:25)
2. Lilitumika kwa makuhani wa Kiyahudi (yaani, "makuhani walitiwa mafuta," Kut. 29:7; mf. Law. 4:3, 5, 16; 6:15; 7:36; 8:12; bila shaka Zab. 84:9-10; na 133:2)
3. Lilitumika kwa makasisi, na Manabii (kama vile. Mwa. 26:7; 1 Nya. 16:22; Zab. 105:15, iliyomaanisha watu wa Agano kwa pamoja; yumkini Hab. 3:13)
4. Lilitumika kwa manabii (kama vile. 1 Fal. 19:16; yumkini 1 Nya. 29:22)
5. Lilitumika juu ya Koreshi (kama vile. Isa. 45 :1)
6. # 1 na # 2 umeunganishwa katika Zab. 110 na Zekaria 4.
7. Lilitumika kwa ujio maalumu wa Mungu, Ufalme wa Daudi kuleta enzi mpya ya haki
    a. uzao wa Yuda (kama vile. Mwanzo 49:10)
    b. nyumba ya Yesse (kama vile.2 Sam 7)
    c. utawala wa ulimwengu (kama vile. Zaburi 2; Isa. 9:6; 11:1-5; Mik. 5:1- 4 na kuendelea)
    d. Huduma kwa wahitaji (kama vile Isa. 61:1-3)

Mimi binafsi nimevutiwa na utambulisho wa neno "aliyetiwa mafuta" na Yesu wa Nazareti (kama vile.Yn. 1:41; 4:25) kwa sababu

1. kutambulishwa kwa ufalme wa milele katika Danieli 2 kipindi cha utawala wa nne

2. kutambulishwa kwa “mwana Adamu” katika Dan. 7:13 akipewa ufalme wa milele
3. maneno ya ukombozi wa Dan. 9:24, ambayo yanaashiria mwisho wa historia ya ulimwengu ulioanguka
4. matumizi ya Yesu ya kitabu cha Danieli katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24:15; Marko 13:14)

Lazima kukiri kuwa hii ni mada nadra katika Agano la Kale, bila shaka Dan. 9:25. Lazima pia ifahamike kuwa Yesu haingii sana katika maelezo ya jumla kuhusu Masihi katika Agano la Kale

1. hakuwa kiongozi katika Israeli
2. hakutiwa mafuta rasmi na kuhani
3. sio kama mwokozi wa Israeli
4. sio tu “mwana wa Adamu” lakini kwa mshangao “Mwana wa Mungu”

◙ **"tumaini letu"** Angalia MADA MAALUM: TUMAINI katika Tito 1:2.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 1:2**
**2 kwa Timotheo, mwanangu hasa katika imani. Neema na iwe kwako, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.**

**1:2 "kwa Timotheo"** Waraka wa Kichungaji ulifuata muundo halisi wa waraka wa Kiyunani: (1) toka kwa nani; (2) kwenda kwa nani; na (3) ombi.

## MADA MAALUM: TIMOTHEO

A. Jina lake linamaanisha "mtu amuheshimuye Mungu."
B. Alikuwa ni mtoto wa mama Myahudi na Baba Myunani na waliishi huko Lystra (kama vile Mdo.16:1). Tafasiri ya Kilatini ya Origen's commentary juu ya Rum. 16:21 inasema Timotheo alikuwa ni raia wa Derbe. Hili linawezekana kutokana na Mdo. 20:4.
C. Alikuwa amefundishwa imani ya Kiyahudi (au imani ya Kikristo) na mama yake na bibi yake (kama vile 2 Tim. 1:5; 3:14-15).
D. Inavyoonekana alimwamini Kristo kipindi cha safari ya kwanza ya Paulo ya umisheni (kama vile Mdo. 14:6-7).
E. Aliombwa kuambatana na kundi la Paulo na Sila kwenye safari ya pili (kama vile Mdo. 16:1-5), inavyoonekana ni kuzifanya kazi za Yohana aitwae Marko. Alithibitishwa kwa unabii (kama vile 1 Tim. 1:18; 4:14)
F. Alitahiriwa na Paulo ili atende kazi na Wayahudi na Wayunani (kama vile Mdo. 16:3).
G. Alikuwa ni mwenza wa Paulo aliyejitoa na akajakuwa Mtume wa kuaminika. Ametajwa kwa jina zaidi ya wasaidizi wengine wa Paulo (mara 17 katika waraka mmoja, kama vile Rum. 16:21; 1 Kor. 4:17; 16:10; Fil.1:1; 2:19,22; Kol. 1:5; 1 Tim. 1:2; 2 Tim. 1:2; Tito 1:4).
H. Paulo kwa upendo akamwita "mwanangu hasa katika imani" (kama vile 1 Tim. 1:2); "mwanangu mpendwa" (kama vile 2 Tim. 1:2); "mwanangu hasa katika imani tuishirikiyo" (kama vile Tito 1:4). Pia angalia hili "mwanangu mpendwa na mwaminifu katika Bwana" kwenye 1 Kor. 4:17.
I. Inavyoonekana alikuwa Rumi kipindi Paulo anaachiwa toka gerezani na akaambatana naye kwenye safari ya nne ya umisheni (kama vile Kol. 1:1; Filemoni 1:1).
J. Anaitwa "mtume" katika 1 The. 2:6 kwa maana ya karama alizokuwa nazo ndani ya makanisa (kama vile Efe. 4:11).
K. Nyaraka za Kichungaji mbili kati ya tatu zilikuwa zinamzungumzia yeye.
L. Mara ya mwisho ametajwa katika Ebr. 13:23 (lakini kimfuatano wa matukio katika 2 Tim. 1:2).

◙ **"mwanangu hasa"** Neno"wangu" haliko katika andiko la Kiyunani. "mwanangu" ni *teknon*, lenye kumaanisha mtoto halali. Paulo alijiona kama baba wa kiroho wa Timotheo (kama vile 2 Tim. 1:2; 2:1). Vile vile linarejelea kwa Tito (kama vile Tuto 1:4) na Onesimo (kama vile Filemoni 1:10) kwa mfanano wa vifungu.

◙ **"Neema, rehema na amani"** Tambua ukawaida na tofauti katika salamu za Paulo za ufunguzi:

1. "Neema iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile Rum. 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2; Gal. 1:3; Efe. 1:2; Fil. 1:2; 1 The. 1:2; Fil. 1:3)
2. "Neema iwe kwenu na amani toka kwa Mungu Baba" (kama vile Kol. 1:2)
3. "Neema iwe kwenu na amni" (kama vile 1 The. 1:1)
4. "Neema, rehema na amani toka kwa Mungu Baba na Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile 1 Tim. 1:2; 2 Tim. 1:2)
5. "Neema na amani toka kwa Mungu Baba na Kristo Yesu Mwokozi" (kama vile Tito 1:4)

Tambua kuwa aina mbalimbali, lakini vipengele vingine ni vya kawaida.

1. "Neema" inaanza katika salamu zote. Ni muundo uliowekwa Kikristo kwa ajili ya salamu ukiangazia juu ya tabia ya Mungu.
2. "amani" ni matokeo ya mwanadamu kuamini katika kumtumaini Mungu.
3. "Rehema" namna nyingine ya kuzielezea tabia za Mungu na ni namna ya kipekee ya uandishi wa Paulo, uliotumika tu katika I na 2 Timotheo. Neno hili lilikuwa likitumika katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ili kutafasiri neno la Kiebrania *hesed* (yaani., utii wa agano). Mungu ni wa rehema na kutumainiwa.
4. Baba ba Mwana wametajwa katika kila salamu (katika 1 Wathesolanike wametajwa katika kifungu kilichopita). Mara zote wamehusianishwa kisarufi. Hii ilikuwa ni njia mojawapo ya waandishi wa Agano jipya kutetea Uungu kamili wa Yesu wa Nazareti. Hili pia ni kweli kwa utumiaji wa majina ya Agano la Kale kwa ajili ya YHWH alivyotumia kwa Yesu (yaani., Bwana na Mwokozi).

◙ **"Baba"** Biblia inatumia aina mbalimbali za wanadamu (nadharia ya Mungu kuelezewa kwa lugha ya kibinadamu) kuuelezea uungu kama msaada kwenye ukomo wa muda, wa mwanadamu mwenye dhambi. Stiari ya kibiblia iliyozoeleka inahusianisha na familia:

1. Mungu kama Baba, kama mzazi (mama na baba), kama mtu wa karibu (*go'el*)
2. Yesu kama Mwana, kama ndugu, kama mme
3. waamini kama watoto, kama watoto walioasiliwa, kama bibi harusi

## MADA MAALUM: BABA

Agano la Kale linaanzisha neno mbadala la ndani la Mungu kama Baba. (tazama Mada Maalum: Ubaba wa Mungu):

1. Taifa la Israel daima linaelezwa kama “mwana” wa YHWH (kama vile. Hos. 11:1; Mal. 3:17)
2. Hata mwanzoni kabisa mwa kitabu cha Kumbukumbu la torati mfanano wa Mungu kama Baba umetumika (1:31)
3. Katika kumbukumbu la torati 32 Israeli inaitwa “Mwana wake” na Mungu anaitwa “Baba yake”
4. Ufananisho huu unatajwa katika Zab. 103:13 na kuendelea katika Zab. 68:5 (baba wa yatima)
5. Lilikuwa la kawaida katika manabii (kama vile. Isa. 1:2; 63:8; Israeli kama mwana, Mungu kama Baba, 63:16; 64:8; Yer. 3:4, 19; 31:9).

Yesu alizungumza Kiaramu, ikimaanisha kuwa kuna sehemu nyingi ambapo “Baba” anaonekana, ni *Pater* Yule wa Kiyunani, na linawezakuwa linaakisi neno *Abba* la Kiaramu (kama vile. Marko 14:36). Neno hili la kawaida “Baba” au “Papa” linaonyesha ukaribu uliopo wa Yesu na Baba. Udhihilisho wake huu kwa wafuasi wake pia kunahamasisha ukaribu wetu na Baba. Neno “Baba” lilitumika kidogo sana katika Agano la Kale kwa YHWH, lakini Yesu analitumia daima na kwa kulieneza. Ni uthibitisho mkubwa wa uhusiano mpya wa Waamini na Mungu kupitia kwa Kristo (kama vile. Mathayo 6:9)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 1:3-7**
**[3] Kama vile nilivyokusihi ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri kwenda Makedonia, ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine; [4] wala wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo, ziletazo maswali wala si madaraka ya Mungu yaliyo katika imani; basi ufanye hivyo. [5] Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki. [6] Wengine wakiyakosa hayo wamegeukia maneno ya ubatili; [7] wapenda kuwa waalimu wa sheria, ingawa hawayafahamu wasemayo wala mambo yale wayanenayo kwa uthabiti**

**1:3 "Efeso"**

1. Ulikuwa ni mji mkubwa wa jimbo la Kirumi la Asia Ndogo. Haukuwa ni mji mkuu, ingawa gavana wa Kirumi aliishi huko. Ulikuwa ni mji wa kibiashara kwa sababu ya kuwa na bandari nzuri.
2. Ulikuwa ni mji huru, ambao uliruhusiwa kuwa na serikali zake za mitaa na uhuru mwingi wa kisiasa, ikijumuisha kutokuwepo na ngome ya kijeshi.
3. Ulikuwa ni mji pekee ulioruhusiwa kundaa mashindano makubwa ya michezo ya Olimpiki.
4. Lilikuwa ni eneo la hekalu la Artemis (Diana katika Kilatini), ambalo lilikuwa ni moja ya maajabu saba ya dunia kwa siku hizo. Uilikuwa na ukubwa wa 425' kwa 220' likiwa na nguzo 127 ambazo zilikuwa na urefu wa 60’, ambazo 86 kati yake zilikuwa zimewekewa dhahabu (angalia Pliny's *Hist. Nat.* 36:95ff). Sura ya Artemis ilifikiriwa kuwa ya kimondo chenye kufanana na umbo la mwanamke mwenye matiti mengi. Hii inamaanisha kuwa palikuwepo na na makahaba wenye kupenda anasa ndani ya mji (kama vile Matendo 19). Ulikuwa ni mji wenye uovu, wenye tamaduni nyingi.
5. Paulo alitumia zaidi ya miaka mitatu akiwa ndani ya mji huu (kama vile Matendo 18:1na kuendelea; 20:13). Alikaa huko kwa muda mrefu kuliko sehemu zingine alizozizuru.
6. mafundisho ya zamani yanadai kuwa alikuja kuwa ni Mtume kwenye maeneo ya Yohana baada ya Mariamu kufariki huko Palestina.
7. Paulo na Timotheo wamekuwa wakizuru hapa pamoja baada ya Paulo kuachiwa toka gerezani huko Rumi. Ni taarifa ya kijiografia ya kwanza kuhusu safari ya nne ya Paulo ya umishionari. Tambua kuwa alikuwa akielekea Makedonia.
8. Eusebio (mwana historia wa kanisa wa karne ya tatu) anahusianisha yale mapokeo yaliyomsababishia Timotheo kupigwa mawe kwa sababu ya kubishana na wafuasi wa Diana.

◙ **"ili kwamba "** Hili ni neno *hina* (kishazi nia), linamaanisha "ili kwamba" (1 Tim. 1:10,18,20; 2:2; 3:15; 4:15; 5:7,16,20,21; 6:1,19).

◙ **"awakataze"** Hili ni neno la kijeshi "kutoa utaratibu wenye mkazo" (kama vile 1 Tim. 1:5,18; 4:11; 5:7; 6:13,17). Paulo anamwelekeza Timotheo kama mjumbe wa Kitume.

◙ **"wengine wasifundishe elimu nyingine"** Kwa kawaida Paulo, kama waandishi wengine wa karne ya kwanza, angejumuisha maombi ya shukrani, kipengere cha utangulizi kisichotarajiwa cha nyaraka za Kiyunani. Hata hivyo, katika kitabu cha Wagalatia na 1 Timotheo hali (yaani., kuwapinga waalimu wa uongo) walihitaji utofauti toka kwenye mfano mwingine. Kuna nadharia nyingi za kisomi kuwahusu hawa waalimu wa uongo. Wanaonekana kuunganisha dhana ya fikra za Kiyahudi na Kiyunani (kama walivyo waalimu wa uongo wa Kolosai). Katika muktadha huu (1:3-4) wanaainishwa kwa

1. mafundisho mengine
2. kuwa waangalifu na hadithi za kubuni
3. kuwa waangalifu na unasaba usio na mwisho
4. nadharia tupu

Baadhi ya watoa maoni wanahusianisha hili na vipindi vya wenye ujuzi au ulimwengu wa malaika (*plērōma*) kati ya mungu mzuri aliyeko juu na mungu/malaika wadogo, waliotengeneza vitu viovu. Angalia Mada Maalum: wenye ujuzi katika Tito 1:1.

Sababu za Kiyahudi ni dhahili katika:

1. "walimu wa sheria" (1 Tim. 1:7-10)

2. "hadithi za kutunga za Wayahudi" (Tito 1:14; 2 Tim. 4:4)
3. "kutokukubaliana kuhusu sheria" (Tito 3:9)
4. "wale wahusianao na tohara" (Tito 1:10)
5. yumkini asili ya Masihi katika Tito 3:9a

**NASB "wasifundishe elimu nyingine"**
**NKJV "kufundisha elimu nyingine"**
**NRSV "kufundisha mafundisho mapotoe"**
**TEV "kufundisha mafundisho ya uongo"**
**NJB "kueneza mafundisho ya uongo"**

Hii kauli ISIYO NA UKOMO YA WAKATI ULIOPO na neno ambatani *heteros* (nyingine ya aina tofauti) pamoja na *didakalin* (jambo lililofundishwa). KIVUMISHI cha neno *heteros* pia kimetumika kuelezea mafundisho yasiyo sahihi katika Mdo.17:21; 2 Kor. 11:4; na Gal. 1:6-7. 1 Timotheo 6:3 ni ufanano mzuri.

Katika *The New International Biblical Commentary*, uk. xiv, moja ya watoa maoni nimpendae, Gordon Fee, anadai kuwa huu mstari ni wa muhimu katika kuyatafasiri makusudi ya 1 Timotheo. Katika mtazamo huu sio hasa msingi wa "kiongozi cha kuliadabisha kanisa," bali ni kuwakanusha waalimu wa uongo/mafundisho (nami nakubaliana nalo).

**1:4 "wala wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo"** Kwa sababu ya rejeo za sheria za Kiyahudi (1 Tim. 1:7-10 na Tito 3:9b), kwenye tohara (Tito 1:10), na hadithi za Kiyahudi (Tito 1:14 na katika 2 Tim. 4:4), inaonekana dhahili kuwa hayo mafundisho yalikuwa ni ya asili ya Kiyahudi. Inawezekana kuwa yanarejelea kwenye mtizamo wa mwanzo wa Masihi (kama vile Tito 3:9a).

Irenaeus na Tertullian walidhani Paulo alikuwa akizungumza kinabii kwenye kipindi cha wale wenye ujuzi au ulimwengu wa kimalaika kati ya mungu mtakatifu na mungu na mungu mdogo (au *Elohim*/malaika) aliyevitengeneza vitu. Nadhalia ya wenye ujuzi ni muundo wa fikra zenye kujulikana toka kwenye maandiko ya kati ya karne ya pili. Angalia Mada Maalum Wenye Ujuzi katika Tito 1:1. Kutokana na maandiko haya tunatambua orodha pana ya ngazi ya kimalaika kati ya mungu mzuri aliyeko juu na viumbe vidogo vya kiroho. Hata hivyo, hii orodha ya watu wenye ujuzi kamwe hawaianishi kwenye Wakristo wa kisasa, Wayahudi, au fasihi ya wenye ujuzi kwa maneno "hadithi" au "unasaba."

Suala la wenye ujuzi kwa kiasi kikubwa limeendelezwa sana na uvumbuzi wa wana akiolojia wa maandiko ya wenye ujuzi kama vile Nag Hammadi. Maandiko haya sasa yanapatikana katika Kiingereza, *The Nag Hammadi Library* na James M. Robinson na Richard Smith.

**NASB "ziletezo uzushi mtupu"**
**NKJV "yasababishayo migogoro"**
**NRSV "yanayokuza madhanio hewa"**
**TEV "ambayo yanakuza mabishano tu"**
**NJB "ambayo yanaleta hofu tu"**

Inawezekana kujihusisha katika kujifunza Ukristo kitaaluma kile tunachosahau kwa nini tunajifunza neno la Mungu (kama vile Tito 3:8; Mt. 28:19-20). Kwa sababu vile tu andiko laweza kumaanisha hiki au kile haimaanisha kuwa linamaanisha hivyo. Angalia muundo wa kihistoria na muktadha mpana.

Hakika hii ndiyo sababu ya ule uchaji Mungu kuanzia nje ya mageuzi ya desturi. Fikra na moyo vyote lazima viwezeshwe na kutiwa nguvu na Roho wa Mungu.

**NASB "kuliko kusaidia kazi ya Mungu"**
**NKJV "kuliko kuleta maonyo ya kiungu"**
**NRSV "kuliko kuleta mafunzo ya kiungu"**

**TEV** **"hayatumikii makusudi ya Mungu"**
**NJB** **"badala ya kuendeleza mpango wa Mungu"**

Hili ni neno kwa ajili ya "mwangalizi wa nyumba" (*oikonomian*, linalopatikana katika toleo la MSS א, A, D[2], F, G) lililotumika katika utumishi wa waamini wa ujumbe wa injili. Linarejelea kwenye mpango mzuri wa Mungu kwa ajili ya wokovu wqa mwanadamu kupitia imani katika Kristo (kama vile Mwa. 3:15; 2 Kor. 5:21; Efe. 2:8-10; 2:11-3:13). Angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa YHWH katika 1 Tim. 4:10.

Toleo la NKJV la neno "kufundisha" (*oikodomēn*) linafuatisha toleo la MS D* na maandiko ya Kiyunani na Irenaeus na andiko la Kilatini lililotumiwa na Theodore. Toleo la UBS[4] linakipa kifungu "mwangalizi wa nyumbani" alama "A" katika viwango.

Toleo la NET Bible linaipa 1 Tim. 2:3-6; 2 Tim. 1:9-10 naTito 3:4-7 kama sehemu ya kithiolojia ya mpango wa ukombozi wa YHWH (uk. 2176).

## MADA MAALUM: KUADILISHA

Neno hili *oikodomeō* na muundo wa maneno yake mengine yanatumiwa mara kwa mara na Paulo. Kidhahiri lilimaanisha "kujenga nyumba" (kama vile Mt. 7:24), lakini lilikuja kutumika kisitiari kwa:

1. Mwili wa Kristo, kanisa, 1 Kor. 3:9; Efe. 2:21; 4:16
2. Kujenga
   a. ndugu wadhaifu, Rum. 15:1
   b. majirani, Rum. 15:2
   c. ninyi kwa ninyi, Efe. 4:29; 1 Wathesalonike 5:11
   d. watakatifu kwa ajili ya huduma, Efe. 4:11
3. tunajenga au kuonya kwa
   a. upendo, 1 Kor. 8:1; Efe. 4:16
   b. kuweka mipaka juu ya uhuru binafsi, 1 Kor. 10:23-24
   c. kukwepa kudhaniwa, 1 Tim. 1:4
   d. kuweka mipaka ya wazungumzaji katika huduma za kuabudu (waimbaji, walimu, manabii, wanenaji kwa lugha, na wakalimani), 1 Kor. 14:3-4,12
4. vitu vyote sharti vionywe
   a. mamlaka ya Paulo, 2 Kor. 10:8; 12:19; 13:10
   b. kauli za kimutahsari katika Rum. 14:19 na 1 Kor. 14:26

◙ **"yaliyo katika imani"** Kiukweli kuna tofauti kati ya "hadithi," "unasaba," "mitizamo," na imani. Imani inasimamia juu ya ukweli wa kihistoria wa injili, na sio nadharia. Imani huja kutokana na ahadi ya Mungu (kama vile Gal. 3:14,16,17,18,21,22,29), sio ushikiliaji wa kifalsafa wa mwanadamu (kama vile 1 Kor. 1:18-31). Mtu husimamia juu ya mafunuo, mwingine juu ya mtizamo wa mwanadamu. Mtu humweshimu Mungu na mwingine humtukuza mwanadamu mwenye fikra.

Hii haimaanishi kuyashusha thamani mafundisho ya Kimungu, bali ni kutofautisha mafunuo ya Kimungu toka kwa sababu ya mwanadamu, mtizamo, na uvumbuzi. Waamini wanaitwa kumpenda Mungu kwa "mawazo" yako yote (kama vile nukuu ya Yesu ya Kumb. 6:5 katika Mt. 22:36-37; Marko 12:28-30; Luka 10:27) na kuupitisha ukweli uu juu ya watoto wao (kama vile Kumb. 6:7,20-25).

**1:5 "upendo utokao katika moyo safi"** Lengo la lawama za Paulo kwa waamini katika 1 Tim. 1:5 zilikuwa na vitu vitatu vilivyoko pamoja.

1. upendo utokao katika moyo safi
2. upendo utokanao na dhamiri safi
3. upendo utokanao na imani halisi.

Katika Kiebrania neno "moyo" lilitumika kwa ajili ya nafasi ya uelewa, mihemuko, na mapenzi mema (kama vile Kumb. 6:5-6). Hili lilisimamia kwa watu wote.

## MADA MAALUM: MOYO

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania lēb (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*,, 2nd Ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
    a. Mungu anatujua mioyo (kama vile Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
    b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani,uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa,kama vile.Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile. Mt. 5:28; Matendo 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
6. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani,Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
    a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
    b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
    c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
    d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
    e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

◙ **"dhamira njema"** Hakuna katika agano la kale sehemu yeyote yenye kufanana na neno "dhamira" isipokuwa neno la Kiebrania "kifua" lenye kudokeza maarifa ya mtu mmoja na mienendo yake. Mwanzoni neno la Kiyunani lililorejea dhamira lilihusiana na milango mitano ya fahamu. Lilikujaanza kutumika kwa maana ya ndani (kama vile Rum. 2:15). Paulo alilitumia neno hili mara mbili kwenye majaribu yake katika Matendo (kama vile Mdo. 23:1 na 24:16). Inarejea kwenye maana yake kuwa kwa kutojua hakuziheshimu shughuli zozote tarajiwa kumwelekea Mungu (kama vile 1 Kor. 4:4).

Dhamira huendeleza uelewa wa mienendo ya mwamini na matendo yanayoendana juu ya (1) mtizamo wa Kibiblia; (2) Roho aishiye ndani yetu; na (3) maarifa ya neno la Mungu. Linakuja kuwa kweli kwa mapokezi binafsi ya injili.

Paulo anatumia hili neno mara mbili katika sura ya 1, mara moja katika uhusiano wa mwendelezo wake wa maana ya mapenzi ya Mungu (kama vile 1 Tim. 1:5) na mara moja katika kuhusiana na ukaidi wa kukataa wa walimu wa uongo (kama vile Tito 1:15), ukiwajumuisha Hymenaeus na Iskanda (kama vile 1 Tim. 1:19). Hawa waalimu wa uongo walikwisha sikia dhamiri zao zilikwisha nyauka (kama vile 1 Tim. 4:2).

◙ **"imani isiyo na unafiki"** Paulo anatumia KIVUMISHI mara tatu katika maandiko yake kuelezea (1) imani (kama vile 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 1:5) na (2) upendo (kama vile 2 Kor. 6:6 na pia 1 Pet. 1:22). Ina kidokezo cha asili, kweli, au kisicho na unafiki chenye maana sawa na "kisicho halisi" lenye kuelezea waalimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 1:19-20).

**1:6-7** Mistari hii zaidi inaainisha waalimu wa uongo katika namna za Kiyahudi

1. Waliondoka kwenye lengo la mafundisho ya kimaadili (kama vile 1 Tim 1:5)
2. waligeukia mbali katika

a. "majadiliano yasiyo na matunda" (NASB)
b. "maneno yasiyo na maana" (NKJV)
c. "mazungumzo yasiyo na maana" (NRSV)
d. "mtizamo tupu" (NJB)

3. walitaka kuwa waalimu wa sheria
4. hawakuelewa sheria
5. wakafanywa imara kuhusu madai ya vitu wasivyovielewa
6. Mistari ya 9c-10 inaonekana kuaksi Amri Kuu

Mwisho mbaya wa waalimu wa uongo huenda ni

1. upofu wao wa kiroho, ambao mara zote huelezewa kwa upofu kutokuwa wakweli
2. kwa ukaidi wao wanaikataa nuru, sio tu ujinga
3. wanaongoza wengine katika makosa na uharibifu

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 1:8-11**
**[8] Lakini twajua ya kuwa sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia iliyo halali; [9] akilifahamu neno hili, ya kuwa sheria haimhusu mtu wa haki, bali waasi, na wasio wataratibu, na makafiri, na wenye dhambi, na wanajisi, na wasiomcha Mungu, na wapigao baba zao, na wapigao mama zao, na wauaji, [10] na wazinifu, na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo; na likiwapo neno lo lote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima; [11] kama vile ilivyonenwa katika Habari Njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye, niliyowekewa amana.**

**1:8-11** Hii ni moja ya sentensi ndefu ya Kiyunani. Kwa wazi inafunua kusudi moja endelevu la sheria ya Musa, hasa kama inavyohusiana na maisha ya uadilifu.

**1:8 "Lakini twajua kuwa sheria ni nzuri"** Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA PAULO KUHUSU SHERIA YA MUSA

Ni nzuri na inatoka kwa Mungu (kama vile Rum. 7:12,16).

A. Si njia ya kuielekea haki na ukubalifu wa Mungu (inaweza hata kuwa laana, kama vile Gal. 3). Tazama Mada Maalumu: Sheria ya Musa na Mkristo.
B. Bado ni mapenzi ya Mungu kwa waaminio kwa sababu ni ufunuo wa Mungu Mwenyewe (mara nyingi Paulo amelinukuu Agano la Kale kuwasadikisha na /au kuwatia moyo waaminio).
C. Waamini wanafahamishwa naAgano la Kale (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 10:6,11), lakini hawaokolewi na Agano la Kale (kama vile Matendo 15; Warumi 4; Wagalatia 3; Waebrania). Ina fanya kazi ndani ya utakaso lakini si uthibitisho.
D. Inafanya kazi ndani ya agano jipya ili:
    1. kuonyesha dhambi (kama vile Gal. 3:15-29)
    2. kuwaongoza wanadamu ndani ya jamii waliokombolewa
    3. kumfahamisha Mkristo maamuzi ya kimaadili

Ni mpangilio maalumu unaomulika kithiolojia uliohusiana na Sheria, kutoka katika hali ya kulaaniwa (kama vile Gal. 3:10-13) na badala yake kuwepo baraka za kudumu, jambo ambalo linasababisha tatizo katika kujaribu kuuelewa mtazamo wa Paulo kuihusu Sheria ya Musa. Mwanadamu aliye ndani ya Kristo, James Stewart analionyesha fumbo la fikra na maadiko ya Paulo:
"Kwa kawaida ungetarajia kuwepo kwa mwanadamu anayejiendesha mwenyewe ili kuunda mfumo wa fikra na mafundisho yaliyoimarishwa na kama kitu kisichobadilishwa kama alivyotumia maneno yenye manufaa. Ungetarajia yeye kuulenga usahihi katika kutumia maneno yalioziongoza fikra zake. Ungedai kwamba neno, linapotumiwa na mwandishi wetu katika maana mahususi, linapaswa kuibeba maana hiyo kotekote. Lakini kwa kuangalia muundo huu yakupasa kutomtia moyo Paulo. Matumizi mengi ya maneno yake ni marahisi, si magumu. . . anaandika 'Basi torati ni njema', 'Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani' (Rum.

7:12,22) lakini ni dhahiri kwamba kipengele kingine cha *nomos* ndicho kinachomfanya kuzungumza hali hii pengine, 'Kristo alitukomboa katika laana ya torati' (kama vile Gal. 3:13)" (uk. 26).

◙ **"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA TATU yenye kumaanisha tendo muhimu, lakini lenye dharura. Sheria ya Musa lazima itumike katika kuendana na tabia na sio kama hoja ya kisheria (kama vile Rum. 2:27-29; 7:6; 2 Kor. 3:6).

**1:9 "bali waasi, na wasio wataratibu"** Paulo anahusisha orodha mbalimbali za dhambi katika maandiko yake (kama vile Rum. 1:29-31; 13:13; 1 Kor. 5:11; 6:9-10; Efe. 5:5; Kol. 3:5; 1 Tim. 6:4-5; 2 Tim. 3:2-4; Tito 3:3). Zinafanana na orodha ya mema ya wenye maadili wa Kiyunani. Hii orodha inaelezea wale wote ambao sheria bado ni muhimu kwao (yaani., watenda dhambi). Sheria kama mwakilishi wa Mungu kutenda dhambi kwa ukamilifu imeelezewa katika Wagalatia 3.

## MADA MAALUM : UOVU NA WEMA KATIKA AGANO JIPYA

Orodha ya vipengele vyote yaani maovu na maadili ni vinaendana kwa pamoja katika Agano Jipya. Mara nyingi hivi huakisi maeneo yote yaani katika Sheria za Kiyahudi na orodha ya tamaduni. Orodha za Agano Jipya za kuzilinganisha sifa pambanuzi zinaweza kuonekana katika:

| | | Uovu | Wema |
|---|---|---|---|
| 1. | Paulo | Rum. 1:28-32 | --- |
| | | Rum. 13:13 | Rum. 12:9-21 |
| | | 1 Kor. 5:9-11 | --- |
| | | 1 Cor. 6:10 | 1 Kor. 6:6-9 |
| | | 2 Kor. 12:20 | 2 Kor. 6:4-10 |
| | | Gal. 5:19-21 | Gal. 5:22-23 |
| | | Efe. 4:25-32 | --- |
| | | Efe. 5:3-5 | --- |
| | | --- | Flp. 4:8-9 |
| | | Kol. 3:5,8 | Kol. 3:12-14 |
| | | 1 Tim. 1:9-10 | --- |
| | | 1 Tim. 6:4-5 | --- |
| | | 2 Tim. 2:22a, 23 | 2 Tim. 2:22b,24 |
| | | Tito 1:7, 3:3 | Tito 1:8-9; 3:1-2 |
| 2. | Yakobo | Yakobo 3:15-16 | Yakobo 3:17-18 |
| 3. | Petro | 1 Pet. 4:3 | 1 Pet. 4:7-11 |
| | | 2 Pet. 1:9 | 2 Pet. 1:5-8 |
| 4. | Yohana | Ufu. 21:8; 22:15 | --- |

◙ **"wasio wataratibu"** Hii inamaanisha "mamlaka isiyotambulika." Walimu wa uongo walishakwisha kataa dhana za uadilifu za sheria ya Musa. Walishakwisha kuwa "sheria" wao wenyewe (hakuna dhamiri, kama vile 1 Tim. 4:2).

◙ **"waasi"** Hii inamaanisha "kutokuwa chini ya mamlaka." Walihitaji mamlaka iwe juu yao wenyewe.

◙ **"makafiri"** Hili linamaanisha "watu wasio na dini." Hawakuwa wapumbavu, lakini wenye kupofushwa.

◙ **"wenye dhambi"** Hili lina maana yenye kinyume na wacha Mungu. Walipinga yale yote Mungu alisimamia kwayo na kufatenda.

◙ **"wenye kukufuru"** Hii inamaanisha "kusimama juu ya patakatifu." Walidai kuwa wa kiroho sana, lakini kutokana na maisha yao waliyaonyesha ni ya kidunia.

◙ **"wale wawauao baba zao na mama zao"** Kama hii orodha inaaksi amri za Mungu, hivyo hili linaweza kuaksi kukosa utovu wa nidhamu/heshima ambayo inawafaa wazazi (kama vile Kut. 20:12; Kumb. 5:16).

◙ **"mauaji"** Katika amri za Mungu hili linarejelea kwenye mauaji yasiyo ya kisheria, yasiyo ya kukusudia (kama vile Kut. 20:13; Kumb. 5:17).

**1:10 "wazinifu"** Hii inamaanisha "wenye kuzini kingono" na laweza kurejea kwenye Kut. 20:14 na Kumb. 5:18. Tendo la ndoa pasipo mipaka mara nyingi limekuwa likiainishwa na waalimu wa uongo.

| | |
|---|---|
| **NASB, NJB** | **"wasenge"** |
| **NKJV, NRSV** | **"wafiraji"** |
| **TEV** | **"wakware"** |

## MADA MAALUM: KUJAMIIANA KWA JINSIA MOJA

Kuna shinikizo kubwa la destuli za kisasa kukubali kujamiiana kwa jinsia moja kama mtindo wa maisha sahihi na mbadala.
Biblia inalaani kitendo hiki kama mtindo wa maisha wenye uharibifu, nje ya mapenzi ya Mungu kwa ajili ya uumbaji wake.

1. inavunja amri ya Mwanzo 1 juu ya kuzaa na kuongezeka
2. Inaweka bayana tabia za ibada za kipagani na desturi (kama vile Mambo ya Walawi 18:22; 20:13; Rum. 1:26-27; na Yuda 7)
3. Inafunua uhuru wa kibinafsi kujitenga mbali na Mungu(kama vile 1 Kor. 6:9-10)

Hatahivyo kabla sijaachana na mada hii ngoja nielezee upendo wa Mungu na msamaha kwa wanadamu wote waasi. Wakristo hawana haki ya kuwa na chuki kuu wala kujivuna juu ya dhambi hii, haswa wakati I wazi kwamba sisi sote tunatenda dhambi. Maombi, kujaliana, ushuhuda na huruma vinafanya kazi zaidi katika eneo hili kuliko kushutumiana kwa ukali. Neno la Mungu na Roho wake watafanya kazi ya kulaani na kuhukumu ikiwa tutawaruhusu. Dhambi zote za zinaa, sio tu hii ni chukizo mbele za Mungu na zinatupeleka katika hukumu. Hali ya kutamani kujamiina ni zawadi na kipawa kutoka kwa Mungu kwa ajili ya ustawi wa mwanadamu, furaha na jamii imara. Lakini hamu hii yenye nguvu na iliyotolewa na Mungu mara kwa mara inageuzwa kuelekea katika ubinafsi na kujitaftia maslahi yake yenyewe, maisha ya "zaidi-kwa ajili yangu-kwa gharama yoyote" (kama vile Rum. 8:1-8; Gal. 6:7-8).

Mara kwa mara watu wanasema, "Mungu aliniumba hivi."Ni kweli kwamba bado hatujui chanzo cha usenge (yaani kijenetiki au kijamii) lakini vyovyote, Biblia lazima utuongoze juu ya chaguzi zetu; Chaguzi zina matokeo. Maandiko yana vipaumbele juu ya hisia au upendeleo binafsi. Sisi ni jamii ya kiimani tunaoongozwa kwa ufunuo wa kiungu na sio uhuru au haki za mtu mmoja mmoja.

Neno la kuhitimisha kama kiongozi wa kanisa sifahamu kwamba asilimia mashindano ya Wakristo juu ya suala hili. Tatizo sio ile hulka ila tendo. Baadhi ya wanafunzi wa kihuduma katika chuo changu wanahangaika na mambo mengine ya kingono (yana nguvu sana katika hatua hii ya maisha). Wale wanaochagua kuweka mipaka katika shauku zao (yaani kujizuia) katika eneo hili (yaani matamanio ya kingono) hakika ndio watu sahihi kwa ajili ya nafasi za huduma. Hili pia ni hivyo hivyo kweli kwa wale wanaohangaika na kujamiiana kwa jinsia moja. Suala la msingi hapa ni tendo na sio wazo. Kwanini baadhi wanavutwa kwa wengine wa jinsi moja bado ni fumbo. Kuna uchaguzi katika eneo hili (kama ilivyo katika maeneo mengine). Tunawajibika kwa chaguzi

zetu!

Mungu anawapenda watu na kutamani afya zao za kudumu na ustawi kwa wale wote waliofanywa kwa sura na mfano wake (Mwanzo 1:26-27; angalia Mada Maalumu: Kujamiiana kwa Jinsia moja). Yale mambo/matendo ambayo yanamuharibu afya ya mtu na furaha na pia jamii lazima yakemewe na kulaaniwa. Mungu anataka kutuona tukiwa katika ubora wetu! Sisi tunataka kutimizwa kwa matakwa yetu haraka haraka! Mungu aturehemu sisi sote.

◙**"waibao watu"** Huu ni ushahidi mwingine ya kuwa orodha nzima inafanana na amri kumi za Mungu. Hii ni tafasiri ya waalimu wa sheria ya Kiyahudi "usiibe" (kama vile Kut. 20:15; Kumb. 5:19). Walimu wa sheria za Kiyahudi wanadai kuwa linarejelea kwenye utekaji wa watumwa (kama vile Kut. 21:16; Kumb. 24:7), hata hivyo, kwa muktadha wa haraka inaonekana kuhusiana kwenye kujamiiana kinyume na matakwa ya mtu (yaani., kufanya ngono na binti mfungwa, kama vile Amosi 2:7, au kumtumia kijana wa kiume kwa ajili ya kufanya nae ngono kinyume na matakwa yake).

◙ **"na waongo na waapao kwa uongo"** Hili laweza kurejelea kwenye amri "usimshuhudie uongo jirani yako" (kama vile Kut. 20:16; Kumb. 5:20).

◙ **"na likiwapo neno lolote lisilopatana na maneno ya uzima"** Ikiwa tutaendelea kulinganisha hili kwenye amri kumi za Mungu hivyo hili linapaswa kurejelea kwenye "kutamani" (kama vile Kut. 20:17; Kumb. 5:21). Hata hivyo, Paulo anaonekana kuhitimisha orodha yake ya dhambi katika Rum. 13:9 na Gal. 5:21 katika maana ya pamoja (yaani, bila kumaanisha rejeo kwenye kutamani).

◙ **"mafundisho yenye uzima"** Tunapata neno la Kiingereza "usafi" toka kwenye neno la Kiyunani. Hili neno linatumika katika Agano Jipya mara kumi na moja; mara tisa katika nyaraka za Kichungaji. Linazungumza juu ya mafundisho ambayo humfanya mwamini awe hai kiroho. Dhana yenyewe (kupitia vifungu mbalimbali) ni yenye kurudia dhamira ya nyaraka za kichungaji (kama vile 1 Tim. 1:10; 4:6; 6:3; 2 Tim. 1:13; 4:3; Tito 1:9,13; 2:1,2,7). Katika muktadha huu unafanana na "injili ya utukufu" katika 1 Tim. 1:11.
Ugumu wa matumizi ya kisasa ya andiko hili linaendana na waamini wa leo wenye kuweza kuwaelezea "waalimu wa uongo." Ni namna gani mtu anaweza kutofautisha kati ya vipaumbele binafsi vya mtu na tamaduni dhidi ya masuala muhimu ya kimafundisho? Jibu lazima lisimamie kwenye mafundisho ya Kitume ya injili, hasa linapohusiana na mtu na kazi ya Kristo na namna watu wanavyofaidika na kazi ya Kristo na kuishi katika nuru ya injili ya kumfanana Kristo.
"mafundisho yenye uzima" ni moja ya maneno mbalimbali na vifungu vinavyoinua na kuelezea ukweli wa Mungu.

1. "Neno la Mungu" (kama vile 1 Tim. 4:5; 2 Tim. 4:2; Tito 2:5)
2. "neno la Bwana wetu" (kama vile 1 Tim. 6:3; 2 Tim. 1:13)
3. "neno la Kweli" (kama vile 2 Tim. 2:15)
4. "neno la imani" (kama vile 1 Tim. 4:6)
5. "mafundisho" (kama vile 1 Tim. 1:10; 11 Tim. 4:3; Tito 1:9, 2:1)
6. "kujiepusha" (kama vile 1 Tim. 6:20)
7. "ukweli" (kama vile 2 Tim. 1:14; 2:18, 25; 3:7,8; 4:4)
8. "injili" (kama vile 1 Tim. 1:11; 2 Tim. 2:8, 10, 11)
9. "imani" (kama vile 1 Tim. 6:21; 2 Tim. 4:7)
10. "maandiko" (kama vile 2 Tim. 2:15-16)

**1:11 "habari njema ya Utukufu"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "injili ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye." Hili linafanana na "mafundisho yenye uzima" ya 1 Tim. 1:10. Mungu amedhihilisha namna ya kujongea kwake na na watu wengine kwa namna ifaayo (injili) na namna isiyofaa (ushikiliaji sheria wa Kiyahudi). Agano Jipya katika Kristo ni mwamuzi wa mwisho kwa kile kimfaacho mwamini (kama vile Matendo 15).

Neno utukufu (*doxa*) ni gumu kulielezea. Katika Agano la Kale neno la Kiebrania *kabod*, ambalo ni neno la kibiashara, humaanisha "kuwa na uzito" na hivyo basi kuwa na thamani na kuheshimika. Lilikuwa na maana

maalum lilipotumika kwa YHWH (kama vile Kut. 16:7) likiendana na wingu la *shekinah* likiwakilisha uwepo Wake. Hili wingu lilikuwa nguzo ya moto.kwa hiyo, neno *kabod* ni dokezo lenye kushamiri (kama vile Kut. 24:17). Katika Agano la Kale lilikuja kuwa ni namna ya kurejelea kwa Mungu Mwenyewe (kama vile Isa. 59:19). Hii ndiyo sababu Yohana 1:14 ikaja kuwa ni ya muhimu zaidi. Yesu na/injili yake inatambulika kikamilifu na Mungu wa utukufu wa Agano la Kale, YHWH.

◙ **"Mungu wa utukufu"** Neno hili kwa ajili ya "utukufu" linatumika kwa ajili ya Mungu, hapa tu katika 1 Tim. 6:15. Ni neno lile lile lililotumika kwenye Heri za Mathayo 5 (yaani., "furaha," "kushangilia"). Maana ya nahau ni kuwa YHWH anasitahili kisifiwa.

◙ **"niliyowekewa amana"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ya neno pisteuō, ni neno la pamoja kwa ajili ya imani, amini, au kusadiki katika Agano Jipya. Hapa lintumika kwa maana ya "kuweka amana kwa ajili ya mwingine" (kama vile Luka 16:11; Rum. 3:2; 1 Kor. 9:17; Gal. 2:7; 1 The. 2:4; 1 Tim. 1:11; Tito 1:3; 1 Pet. 4:10).
Paulo aliamini kuwa Mungu amemfanya kuwa mtumishi kwa ajili kwa wale ambao angaliwapasha habari (kama vile 1 Kor. 9:17; Gal. 2:7; 1 The. 2:4; Tito 1:3).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 1:12-17**
**[12] Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake; [13] ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani. [14] Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na pendo lililo katika Kristo Yesu. [15] Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi. [16] Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele. [17] Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina.**

**1:12 "Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana Wetu"** Hili ni moja ya matukio machache wakati Paulo akielekeza maombi yake kwa Kristo badala ya kuyapeleka kwa Baba. Yumkini alifanya hivi kwa sababu alikuwa ni Yesu aliyemsikia pindi akiwa njiani kuelekea Dameski (kama vile Matendo 9:4-5; 22:7-8; 26:15). Paulo aliamini kuwa Yesu

1. angeweza kumtia nguvu (kama vile Flp. 4:13; 2 Tim. 4:17)
2. kumfikiria yeye kama mwaminifu/wa kuaminika
3. kumweka kwenye huduma (kama vile Mdo. 9:15).

Sehemu iliyobaki ya aya hii imetolewa kwenye mshangao wa Paulo kuwa Mungu angeweza kupenda, kusamehe na kumtumia mwenye dhambi kama yeye. Kama Mungu angalilifanya hili kwa Paulo, angaliweza kulifanya kwa mtu yeyote, hata kama ni kwa waalimu wa uongo na wale wote waliyovutiwa nao.

Aina hii ya wimbo wa kumsifu Mungu inayoonekana kupenya kwenye muktadha ni tabia ya uandishi wa Paulo. Akielezea thiolojia yake mara kadhaa ilisababisha alipuke kwa shangwe na shukrani. Paulo mara nyingi alitumia neno la Kiyunani *eucharisteō* au *eucharistia* kuelezea shukrani, lakini neno lenyewe hapa ni *charin*, ambalo limeundwa toka kwenye shina la neno "neema" (*charis*). Hili ni neno adimu kwenye maandiko ya Paulo (kama vile 1 Tim. 1:12; 2 Tim. 1:3). Hata hivyo, inavyoonekana yote yanatumika kwa kubadilishana kwenye waraka wa Wakorintho, kwa hiyo, yumkini yote ni visawe kwa ajili ya Paulo, yakitumika kidogo au kwa namna ya isiyotofauti.

## MADA MAALUM: SHUKRANI

I. Utangulizi
   A. Huu ni mwenendo sahihi wa mwamini kumwelekea Mungu

1. Hiki ndio chanzo cha sifa zetu kwa Mungu kupitia Kristo
    a. 2 Wakorintho 2:14
    b. 2 Wakorintho 9:15
    c. Wakolosai 3:17
2. Hili ni kusudio sahihi kwa ajili ya huduma, 1 Kor. 1:4
3. Hii ni dhamira endelevu ya mbinguni:
    a. Ufunuo 4:9
    b. Ufunuo 7:12
    c. Ufunuo 11:17
4. Hii ndio dhamira endelevu ya waumini
    a. Wakolosai 2:7
    b. Wakolosai 3:17
    c. Wakolosai 4:2

II. Vikorokoro vya Biblia

A. Agano la Kale

1. Maneno mawili ya msingi
    a. *yadah* (BDB 392, KB 398), ikimaanisha sifa
    b. *todah* (BDB 392, KB 1695), ikimaanisha sala ya shukrani. Mara nyingi lilitumika kwenye utoaji wa dhabihu (kama vile 2 Nya. 29:31; 33:16)
2. Daudi aliwachagua Walawi maalumu kwa ajili ya kumsifu na kumshukru Mungu. Hili liliendelezwa na Sulemani, Hezekia, na Nahemia.
    a. 1 Nyakati 16:4,7,41
    b. 1 Nyakati 23:30
    c. 1 Nyakati 25:3
    d. 2 Nyakati 5:13
    e. 2 Nyakati 7:6
    f. 2 Nyakati 31:2
    g. Nehemia 11:12
    h. Nehemia 12:24,27,31,38,46
3. Kitabu cha Zaburi ni mkusanyiko wa sifa na shukrani za Waisrael.
    a. Shukrani kwa YHWH kwa ajili ya uaminifu wake kwenye agano
        1) Zaburi 107:8
        2) Zaburi 103:1 na kuendelea
        3) Zaburi 138:2
    b. Shukrani ilikuwa ni sehemu ya kimchakato ndani ya hekalu
        1) Zaburi 95:2
        2) Zaburi 100:4
    c. Shukrani ilisindikizwa na utoaji dhabihu
        1) Zaburi 26:7
        2) Zaburi 122:4
    d. Shukrani ilitolewa kwa ajili ya matendo ya YHWH
        1) Kuwakomboa toka mikononi mwa maadui
            a) Zaburi 7:17
            b) Zaburi 18:49
            c) Zaburi 28:7
            d) Zaburi 35:18
            e) Zaburi 44:8
            f) Zaburi 54:6
            g) Zaburi 79:13
            h) Zaburi 118:1,21,29

i) Zaburi 138:1
2) Ukombozi toka gerezani (isitiari), Zaburi 142:7
3) Ukombozi toka katika mauti
a) Zaburi 30:4,12
b) Zaburi 86:12-13
c) Isaya 38:18-19
4) Aliwashusha chini waovu na kuwainua wenye haki
a) Zaburi 52:9
b) Zaburi 75:1
c) Zaburi 92:1
d) Zaburi 140:13
5) Anasamehe
a) Zaburi 30:4
b) Isaya 12:1
6) Hutoa kwa watu wake
a) Zaburi 106:1 na kuendelea
b) Zaburi 111:1
c) Zaburi 136:1,26
d) Zaburi 145:10
e) Yeremia 33:11

B. Agano Jipya
1. Neno kuu lililotumika kwa ajili ya shukrani na sala ya shukrani (baadhi ya nukuuu)
a. *eucharisteō* (kama vile 1 Kor. 1:4,14; 10:30; 11:24; 14:17,18; Kol. 1:3,12; 3:17)
b. eucharistos (kama vile Kol. 3:15)
c. *eucharistia* (kama vile 1 Kor. 14:16; 2 Kor. 4:15; 9:11,12; Kol. 2:7; 4:2)
d. *charis* (kama vile 1 Kor. 15:57; 2 Kor. 2:14; 8:16; 9:15; 1 Pet. 2:19)
2. Mfano wa Yesu
a. Alitoa shukrani kwa ajili ya chakula
1) Luka 22:17,19 (1 Kor. 11:24)
2) Yohana 6:11,23
b. Alitoa shukrani kwa ajili ya maombi yaliyojibiwa, Yohana 11:41
3. Mifano mingine ya shukrani
a. Kwa ajili ya zawadi ya Mungu ya Kristo, 2 Kor. 9:15
b. Kwa ajili ya chakula
1) Mdo. 27:35
2) Warumi 14:6
3) 1 Wakorintho 10:30; 11:24
4) 1 Timotheo 4:3-4
c. Kwa ajili ya uponyaji, Luka 17:16
d. Kwa ajili ya amani, Mdo. 24:2-3
e. Kwa ajili ya kukombolewa toka katika hatari
1) Mdo. 27:35
2) Mdo. 28:15
f. Kwa ajili ya matukio yote, Wafilipi 4:6
g. Kwa ajili ya wanadamu wote, hasa viongozi, 1 Timotheo 2:1-2
4. Sura nyingine za shukrani
a. Ni mapenzi ya Mungu kwa waamini wote, 1 Wathesolanike 5:18
b. Ni ushuhuda kwa ajili ya maisha yaliyojazwa na Roho, Waefeso 5:20
c. Kutojali ni dhambi
1) Luka 17:16-17

2) Warumi 1:21
d. Ni suluhisho kwa ajili ya dhambi, Waefeso 5:4
5. Shukrani za Paulo
a. Baraka zake juu ya kanisa
1) Kwa ajili ya kuitangaza injili
a) Warumi 1:8
b) wakolosai 1:3-4
c) waefeso 1:15-16
d) 1 wathesalonike 1:2
2) Kwa ajili ya neema iliyotolewa
a) 1 Wakorintho 1:4
b) 2 Wakorintho 1:11; 4:15
3) Kwa ajili ya kuipokea injili, 1 Wathesalonike 2:13
4) Kwa ajili ya ushirika wa kuieneza injili, Wafilipi 1:3-5
5) Kwa ajili ya ukuaji katika neema, 2 Wathesalonike 1:3
6) Kwa ajili ya maarifa ya uchaguzi, 2 Wathesalonike 2:13
7) Kwa ajili ya Baraka za kiroho, Wakolosai 1:12; 3:15
8) Kwa ajili ya wema katika utoaji, 2 Wakorintho 9:11-12
9) Kwa ajili ya furaha kwa waamini wapya, 1 Wathesalonike 3:9
b. Shukrani zake binafsi
1) Kwa ajili ya kuwa muumini, Wakolosai 1:12
2) Kwa ajili ya kukombolewa toka utumwa wa dhambi, Warumi 7:25; 2 Kor. 2:14
3) Kwa ajili ya kazi ya utoaji dhabihu kwa ajili ya watu wengine, Warumi 16:4; 2 Kor. 8:16
4) Kwa ajili ya baadhi ya matendo ambayo bado hayajatokea, 1 Wakorintho 1:14
5) Kwa ajili ya karama binafsi za kiroho, 1 Wakorintho 14:18
6) Kwa ajili ya ukuaji kiroho wa ndugu wengine, Filemoni 4-5
7) Kwa ajili ya nguvu ya huduma, 1 Timotheo 1:12

III. Hitimisho
A. Sala ya shukrani ni mwitikio wetu muhimu kwa Mungu mara tu tunapookolewa, haitolewi tu kwa ukubarifu wa maneno, bali kwa shukrani ya mfumo wa maisha
B. Sala ya shukrani katika vitu vyote ni lengo la maisha yaliyokomaa katika uangalizi wa Mungu (kama vile 1 The. 5:13-18)
C. Sala ya shukrani ni dhamira iliyopo ya maagano yote la kale na jipya. Je ni dhamira yako pia?

**1:13 "watukanaji"** Hili lazima lirejelee kwa imani ya Sauli na maelezo kuhusu Yesu kabla ya kuongoka kwake.

◙ **"wenye kuuzi watu, wenye jeuri"** (kama vile Matendo 8:1-3; 9:1,13,21; 22:4,19; 26:10-11; 1 Kor. 15:8-9; Gal. 1:13; Flp. 3:6)

◙ **"nalipata rehema"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Mungu /Kristo alikuwa na rehema juu ya Sauli yule mtesaji. Kama anaweza kupokea rehema, kumbe yeyote aweza kupokea rehema. Hili linafunua wazi tabia ya Mungu na namna upendo na rehema yake ilivyo juu ya wenye dhambi.

◙ **"kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga"** Katika Agano la Kale, dhambi ya upumbavu ingaliweza kusamehewa kwa kutoa dhabihu (kama vile Mambo ya Walawi16), ambapo kwa ajili ya dhambi ya makusudi hapakuwepo na uwezekanno wa msamaha kwa kutoa dhabihu, hata kwenye siku ya upatanisho. Kwa Warumi Paulo kwa wazi anadai kuwa Mungu anaushikilia uwajibikaji wa mwanadamu kwa ajili ya nuru waliyonayo. Mfano wa hii kweli ni kuwa kabla ya sheria ya Musa, Mungu hakumushikilia mwanadamu kwa kukiuka sheria zake (kama vile Matendo 17:30; Rum. 3:20,25; 4:15; 5:13,20; 7:5,7-8; 1 Kor. 15:56). Ukweli wa aina ile ile pia unaonekana kwa wale wote ambao hawajaisikia injili (kama vile Rum. 1:18-2:29). Wanawajibika kwa ajili ya mwanga walionao (tokea uumbaji,

Rum. 1:18-23 na ushuhuda wa ndani, Rum. 2:14-15). Hili huitwa "ufunuo wa asili" kama ulivyo kinyume na "ufunuo maalum" (yaani., Biblia).

**1:14 "neema ya Bwana wetu"** Maelezo ya msingi katika thiolojia ya Paulo kuhusu wokovu ilikuwa ni tabia ya Mungu, na sio utendaji wa mwanadamu. Mwanadamu aliyeanguka tumaini lake lipo tu kwenye tabia ya Mungu ya neema na rehema, iliyoelezewa katika Kristo (kama vile Efe. 1:3-14; 2:4,8-9).

**◙"ilizidi sana"** Hii kwa maana iliyo wazi "utele wa ajabu" (*huperpleonazō*). Ni uanishaji wa neno *hapax legomenon* ambalo ni ambatani na neno *huper* lililotungwa na Paulo. "ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema" (Rum. 5:2).

## MADA MAALUM: MATUMIZI YA PAULO YA NENO AMBATANI "*HUPER*"

Paulo alikuwa na upendeleo binafsi kwa ajili ya kuyaumba maneno mapya kwa kutumia KIWAKILISHI cha Kiyunani *huper*, ambacho kimsingi kinamaanisha "juu ya" ama "kuu." Hiki kilipotumika pamoja na KIMILIKISHI (CHA KUONDOA) kilimaanisha "badala ya" Pia kinaweza kumaanisha "karibia na" au "kuhusiana na" kama *peri* (kama vile 2 Kor. 8:23; 2 The. 2:18). Hiki kikitumika pamoja na HALI YA KUSHUTUMU kinamaanisha "kuzidisha wastani," "juu ya," au "zaidi ya" (kama vile A. T. Robertson, *A Grammar of the Greek New Testament in the Light of Historical Research*, kr. 625-633). Wakati Paulo alipotaka kutia mkazo alitumia KIWAKILISHI katika uambatani. Ifuatayo ni orodha ya matumizi maalum ya Paulo ya KIWAKILISHI hiki katika uambatani.

A. Hapax legomenon (kimetumika mara moja katia Agano Jipya pekee)
   1. *Huperakmos*, mmoja wa maisha kwanza yaliyopita, 1 Kor. 7:36
   2. *Huperauxanō*, kuongezeka sana, 2 The. 1:3
   3. *Huperbainō*, kupunja ama kukosa, 1 The. 4:6
   4. *Huperkeina*, mbele ya, 2 Kor. 10:16
   5. *Huperekteina*, kupita kadri, 2 Kor. 10:14
   6. *Huperentugchanō*, kuomba kwa kuugua, Rum. 8:26
   7. *Hupernikaō,* tunashinda tena zaidi ya kushinda, Rum. 8:37
   8. *Huperpleonazō*, kuwa katika hali ya kuzidi sana, 1 Tim. 1:14
   9. *Huperupsoō*, kuadhimisha mno, Flp. 2:9
   10. *Huperphroneō*, kunia yaliyo makuu, Rum. 12:3

B. Maneno yaliyotumika katika maandiko ya Paulo pekee.
   1. *Huperairomai*, kujivuna kwa mtu mwenyewe, 2 Kor. 12:7; 2 The. 2:4
   2. *Huperballontōs*, zaidi ya kipimo, kupita kiasi, 2 Kor. 11:2 (KIVUMISHI kiko hapa tu, lakini KITENZI ki katika 2 kor. 3:10; 9:14; Efe. 1:19; 2:7; 3:19)
   3. *Huperbolē*, kuzidi zaidi, kujilinda kuliko pitiliza, Rum. 7:13; 1 Kor. 12:31; 2 Kor. 1:8; 4:7,17; 12:7; Gal. 1:1
   4. *Huperekperissou*, zaidi ya vipimo vyote, Efe. 3:20; 1 The. 3:10; 5:13
   5. *Huperlian*, katika kiwango cha juu ama kuzidi wengine, 2 Kor. 11:5; 12:11
   6. *Huperochē*, maarufu, bora, 1 K. 2:1; 1 Tim. 2:2
   7. *Huperperisseuō*, kuzidi zaidi, Rum. 5:20 (KAULI YA KATI, to ninaujasiri mwingi, kupita kiasi, 2 Kor. 7:4)

C. Maneno yaliyotumiwa na Paulo na yaliyo haba katika waandishi wengine wa Agano Jipya
   1. *Huperanō*, juu sana, Efe. 1:21; 4:10; na Ebr. 9:5
   2. *Huperechō*, maarufu, bora, Rum. 13:1; Flp. 2:3; 3:8; 4:7; 1 Pet. 2:13
   3. *Huperēphanos*, kusingizia au majivuno, Rum. 1:30; 2 Tim. 3:2 na Luka 1:51; Yakobo 4:6; 1 Pet. 5:5.

Paulo alikuwa mtu wa hisia kali; wakati mambo au watu walipokuwa wema, walikuwa wazuri sana na walipokuwa wabaya walikuwa wabaya sana. KIWAKILISHI hiki kilimruhusu kueleza hisia zake zilizozidi kuihusu dhambi, mwenyewe, na Kristo na Injili.

◙ **"tukiwa na imani na upendo utokanao na Kristo Yesu"** Kuna masuala mbalimbali ya utafasiri yanahusiana na huu mstari.

1. Yapasa neno "Bwana" (1 Tim. 1:14) lirejelee kwa YHWH (kama vile 1 Tim. 1:17) au Yesu? Katika muktadha huu YHWH linafaa.
2. Je yapasa karama za Mungu za neema zihusiane na imani na upendo, ambazo pia ni karama zilizoko katika Kristo (kama vile TEV, NJB)?

Hakika kuongoka kwa Paulo (kama vile Matendo 9) lilikuwa ni tendo la neema. Paulo alichaguliwa na kulitendea kazi. Mwitikio wake haukuwa tendo la hiari! Mahitaji yake yalifikiwa katika neema ya Mungu na matendo ya Yesu. Paulo alipokea karama za mbinguni na kuishi kwazo na wengine.

Tambua kuwa utoaji wa Mungu kwa ajili ya wokovu huja tu kupitia Kristo. Ni jawabu la Mungu kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka katika kila eneo (kama vile 1 Tim. 1:15-17).

**1:15 "ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa"** Kifungu hiki kimetumika mara tano katika nyaraka za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 1:15; 3:1, 4:9; 2 Tim. 2:11; Tito 3:8). Kinatumika mara nyingi kama Yesu alivyotumia neno "amina, amina" (lililotafasiriwa "amini, amini" au "kweli, kweli") kuutambulisha ujumbe muhimu.

Wanazuoni wengi wanaamini kuwa kifungu hiki kilikuwa ni alama ya fasihi kwa ajili ya Paulo, kikinukuu wimbo, liturujia, au katekismu. Maeneo mengine aliyoyanukuu mwanzoni kama maelezo ya kimatamko ni 1:17; 3:16; 6:15-16; 2 Tim. 2:11-13.

◙ **"Kristo alikuja ulimwenguni"** Hili linamaanisha kuwepo kwa Kristo kabla (kama vile Yohana 1:1,15, 8:57-58, 16:28, 17:5; 1 Kor. 8:9; Fil. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8), ambalo lilikuwa ni suala kuu la kimafundisho linalohusiana na Uungu wake (Yeye alifanyika mwanadamu, wala haukuumbwa, kama vile Mith. 8:22). Hili laweza kuelezea dhana ya wenye ujuzi la hawa waalimu wa uongo. Angalia Mada Maalum: Wenye Ujuzi wa Kipeke katika Tito 1:1.

## MADA MAALUM: MATUMIZI YA PAULO YA NENO *KOSMOS*

Paulo analitumia neno *kosmos* kwa njia tofauti tofauti.

1. Mpangilio wa vitu vyote vilivyoumbwa (kama vile Rum. 1:20; Efe. 1:4; 1 Kor. 3:22; 8:4,5)
2. Sayari hii (kama vile 2 Kor. 1:12; Efe. 1:10; Kol. 1:20; 1 Tim. 1:15; 3:16; 6:7)
3. Wanadamu (kama vile Rum. 3:6,19; 11:15; 1 Kor. 1:27-28; 4:9,13; 2 Kor. 5:19; Kol. 1:6)
4. Kuwa pamoja na kutenda kwa wanadamu mbali na Mungu (kama vile 1 Kor. 1:20-21; 2:12; 3:19; 11:32; Gal. 4:3; Efe. 2:2,12; Flp. 2:15; kol. 2:8,20-23). Inafanana na matumizi ya Yohana (yaani., 1 Yohana 2:15-17)
5. Muundo wa ulimwengu wa sasa (kama vile 1 Kor. 7:29-31; Gal. 6:14; inafanana na Flp. 3:4-9, mahali ambapo Paulo anaelezea muundo wa Kiyahudi)

Kwa baadhi ya namna huu mwingiliano na ni vigumu kuainisha kila matumizi. Neno hili, kama yalivyo mengi katika mawazo ya Paulo, yaweza elezewa kwa mazingira ya haraka na sio maelezo yaliyotengenezwa awali. Misamiati ya Paulo ilikuwa ni myepesi (kama vile *James Stewart's A Man in Christ*). Hakuwa anajaribu kutengeneza msamiati wa kithiolojia, lakini akimtangaza Kristo.

◙ **"kuwaokoa wenye dhambi"** Hili ndilo kusudi la Yesu kuja (kama vile Marko 10:45; Luka 19:10; 1 Yohana 2:2). Pia huonyesha kanuni ya msingi ya injili kuhusiana na hitaji la mwanadamu aliyeanguka kwa ajili ya neema (kama vile Rum. 3:9-18,23; 6:23).

◙ **"wa kwanza wao ni mimi"** Kadri unavyomlikwa na nuru ya Mungu ndivyo uovu nao unakunyemelea kwa karibu (kama vile 1 Tim. 1:16; 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8). Paulo alijisikia kuhukumiwa kwa ajili ya mateso yake juu ya kanisa (kama vile Mdo. 7:58; 8:1; 9:1-2; 22:4,19-20; 26:10-11), lakini akajisikia kutiwa nguvu kwa neema ya Mungu, upendo, na kujitoa kwa ajili ya wenye dhambi kupitia kazi aliyoitimiliza Kristo (kama vile 1 Tim. 1:16).

**1:16**
**NASB** **"audhihilishe uvumulivu"**
**NKJV** **"kwa saburi"**
**NRSV** **"kwa uvumilivu mwingi"**
**TEV** **"kwa uvumilivu wote"**
**NJB** **"kwa ustahimilivu usiokuwa na mwisho"**

Hili ni ambatani ya neno la Kiyunani (*makros* na *thumos*) kwa ajili "kujizuia na ghadhabu." Hili neno mara nyingi linatumika kumhusu Mungu katika Agano la Kale la Kiyunani, lililoitwa tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani (kama vile Hes. 14:18; Zab. 86:15; 103:8; Yoeli 2:13; Nah. 1:3). Pia linamwainisha Mungu katika Agano Jipya (kama vile Rum. 2:4; 9:22; 1 Pet. 3:20; 2 Pet. 3:15). Pia lilimaanisha kuwaainisha watoto Wake (kama vile 2 Kor. 6:6; Gal. 5:22; Efe. 4:2; Kol. 1:11; 3:12; 2 Tim. 3:10; 4:2).

◙ **"kama mfano"** ushuhuda wa Paulo wa wokovu toka kuwa adui mkubwa wa Ukristo hadi kuwa Mtume wa kuaminiwa kwa watu wa mataifa unafunua kimo na upana na urefu wa neema ya Mungu. Kwa maana hiyo Paulo alikuwa mwalimu wa uongo halisia ambaye Mungu alimrehemu!

◙ **"kwa wale watakao mwamini kwa baadaye"** Yesu aliomba kwa wale watakao amini katika Yeye kwenye Yohana 17:20-26. Ingawa injili ya Yohana inatumia KIHUSISHI *eis* mara nyingi kuelezea jambo la imani ya mwanadamu, Paulo mara kadhaa ametumia kivumishi *epi* (kama vile Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; pia angalia Matendo 9:42; 11:17; 16:31) au uhusika wa MAHALI (kama vile Gal. 3:6; Matendo 18:8; 27:25). Kunaonekana kutokuwepo na tofauti yeyote ya kithiolojia kati ya (1) kuamini ndani ya (*eis*); kuamini katika (*en*); kuamini juu ya (*epi*); au matumizi ya UHUSIKA WA MAHALI pasipokuwa na KIHUSISHI (kama vile 1 Yohana 5:10).

Paulo, kama alivyo Yohana, wakati mwingine hutumia neno *hoti* (yaani, amini kuwa), ambalo husisitiza kadri ya imani (kama vile Rum. 6:8; 1 The. 4:14). Injili ni (1) mtu akaribishwae; (2) ukweli wa kuuamini; na (3) maisha ya kuishi.

## MADA MAALUMU: KUSADIKI, KUAMINI, AU IMANI

A. Hili ni aina ya neno muhimu katika Biblia (kama vile. Ebr. 11:1,6). Lilikuwa ni somo la Yesu katika mahubiri ya awali (kama vile. Mk. 1:15). Kiwastani kuna mahitaji mapya mawili ya agano: toba na imani (Mk. 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21)
B. Asili na historia yake ya maneno haya
   1. Neno “imani” katika Agano la Kale lilimaanisha mtiifu, mwaminifu au mwaminifu wa kutumainiwa na yalikuwa ni maelezo ya asili ya Mungu na si yetu.
   2. Linatokana na neno la Kiebrania (*emun, emunah*, BDB 53, yaani., Hab. 2:4), ambalo mwanzo kabisa lilimaanisha “kuwa na uhakika au imara.” Kuitumikia imani ni
      a. Kumkaribisha mtu (yaani., imani binafsi, sadiki, kama vile. E.1.hapo chini)
      b. Kuamini imani kuhusu mtu (yaani., maandiko, kama vile. E.5.hapo chini)
      c. Kuishi maisha kama ya mtu huyo (yaani., mfano wa Kristo)
C. Matumizi yake katika Agano la Kale
   Lazima isisitiziwe kuwa imani ya Ibrahim ilikuwa si kwa ajili ya Masiha ajaye, lakini ni kwa ahadi ya Mungu ya kwamba atapata mototo na uzao (kama vile Mwa. 12:2-5; 17:4-8; Rum. 4:1-5). Ibrahim aliikubali ahadi hii kwa kumwamini Mungu (angalia Mada Maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) na neno lake. Bado anamashaka na kuhusika juu ya ahadi hii, ambayo ilimchukua miaka kumi na mitano kutimizwa. Imani yake isiyo kamili, hata hivyo, alikubaliwa na Mungu. Mungu anapenda kufanya kazi na mwanadamu mwenye mapungufu anayejongea kwake na katika ahadi zake kwa imani, hata kama kwa kipimo cha chembe ya haradari (kama vile Mt. 17:20) au imani mchanganyiko (kama vile Marko 9:22-24)

D. Matumizi yake katika Agano Jipya
   Neno "kuamini" linatoka katika neno la Kiyunani *pisteuō* au nomino *pistis,* ambayo yanatafasiliwa kwa Kiingereza "kuamini" "amini" au "imani." Kwa mfano, nomino haijitokezi katika injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna uwalakini katika uhalisia wa uwajibikaji wa kundi kwa Yesu wa Nazareti kama Masihi. Mifano mwingine wa matumizi ya kubabiya ya neno hili "kuamini" ni katika Yohana 8:31-59 na Matendo 8:13, 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi ya uwajibikaji wa awali. Lazima ifuatishwe na mchakato wa uwanafunzi (kama vile Mt. 13:20-23, 31-32; 28:19-20)

E. Matumizi yake ikiwa na vivumishi
   1. *eis* inamaanisha "ndani ya." Muundo huu wa kipekee unasisitizia waumini kuweka imani zao kwa Yesu
      a) ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
      b) ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45,48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petr. 1:8)
      c) ndani yangu (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
      d) ndani ya mwanaye (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
      e) ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo. 19:4; Gal. 2:16)
      f) ndani ya nuru (Yohana 12:36)
      g) ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
   2. *ev* inamaanisha "katika" kama ilivyo katika Yohana 3:15; Marko 1:15; Mdo. 5:14
   3. *epi* ikimaanisha "katika" au "juu ya" kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Pet. 2:6
   4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
   5. *hoti* likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
      a) Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
      b) Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
      c) Yesu katika Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
      d) Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
      e) Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
      f) Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
      g) Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
      h) Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30
      i) Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye "Mimi ndiye" (Yohana 8:24; 13:19)
      j) Tutaishi naye (Rum. 6:8)
      k) Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

◙ **"uzima wa milele"** Uzima wa milele (*zōen aiōnion*) ni somo kuu lenye kujirudia kwenye thiolojia ya Yohana. Ni ukweli uliopo (mf., Yohana 3:16,36; 5:24; 6:47,54) vile vile pia ni tumaini la mbeleni lililotolewa kwa wale wote ambao wanamjua Baba kwa kumwamini Mwana (mf., Yohana 17:2-3).

Paulo anatumia neno hili kama namna ya kurejea kwenye maisha ya (1) enzi mpya; (2) ufalme wa Mungu; au (3) maisha ya ufufuko (kama vile Rum. 2:7; 5:21; 6:22,23; Gal. 6:8; 1 Tim. 1:16; Tito 1:2; 3:7). Ni Mungu pekee asiye na mwili wa nyama; ni Mungu pekee mwenye kutoa uhai. Hutoa uzima wa milele kwa wale wote wamwaminio mwana wake katika imani.

**1:17 "Mfalme"** Wimbo wa kumsifu Mungu unafanana na 6:15-16. Unaaksi lugha ya Sinagogi la baadaye ("mfalme wa ulimwengu") na Wayahudi wale waliokimbilia uahamishoni (neno "milele" lilitumiwa na Mungu kwa Filo wa

Iskandria). Ni wazi kuwa Paulo ananukuu imani au wimbo wa kanisa la mwanzo kama alivyofanya katika 1 Tim. 3:16; 6:15-16 na 2 Tim. 2:11-13.

◙ **"milele"** Hiki ni moja kati ya VIVUMISHI vinne vyenye nguvu ambavyo ni sawa na VIVUMISHI vilivyotumika katika kifungu "uzima wa milele" katika 1 Tim. 1:16 lakini hapa kinamwelezea Mungu. Kwa maana iliyo wazi ni "milele" (*aiōnion*), ambacho chaweza kuwa ni stiari ya milele au rejea ya dhana ya Kiyahudi ya enzi mbili:

1. zama ya sasa ya uovu inayoainishwa na uhuru binafsi na uasi (malaika na mwanadamu)
2. zama ijayo ya haki iliyoahidiwa iliyoletwa na Roho na kuanzishwa na Masihi.

Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 6:17.
Wasiwasi "iliyopo na isubiliwayo" ya uzima wa milele unaainisha wakati uliopo ambapo hizi enzi mbili za Kiyahudi ni zenye kuhusiana kwa sababu ya ufunuo mpya uhusianao na ujio mara mbili wa Masihi, moja kama mwokozi, na mwingine kama mfalme, Mfalme, Bwana, na Mwamuzi.

◙ **"asiyeweza kuona uharibifu"** Hii kwa maana iliyowazi ni "isiyoharibika." Kiistiari inarejea kwenye Yule aishiye milele (YHWH toka kwenye KITENZI cha Kiebrania "kuwa," kama vile Kut. 3:14, angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 2 Tim. 1:2). Ni Mungu pekee mwenye uzima ndani Yake (kama vile Rum. 1:23; 1 Tim. 1:17; 6:16). Uzima mwingine ni zawadi ya kupewa na utumishi. Hutuijia tu kupitia neema ya Baba, ambayo ni kazi ya Kristo (kama vile 2 Tim. 1:10), na huduma ya Roho.

◙ **"asiyeonekana"** Hili linatumika katika maana ya ulimwengu wa kiroho (kama vile Kol. 1:15) au yumkini YHWH kama Mungu asiyeonekana (asiye na sura, kama vile Kut. 33:20; Kumb. 4:15; 1 Tim. 6:16). Mungu ni Roho aishiye aliyekuwepo kwenye uumbaji wote!

◙ **"Mungu peke yake"** Hili linarejelea kwenye imani ya Kiyahudi ya Mungu mmoja (angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 2:5, kama vile Kumb. 6:4-6; Yuda 25). Huu muktadha unaaksi mtazamo pekee wa dunia Kibiblia. Biblia humwakilisha mwanadamu kwa mtizamo wa imani mbali na milango mitano ya fahamu.

1. Kuna Mungu mmoja na mmoja pekee (kama vile Mwa. 1:1; Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 4:35-39; 1 Sam. 2:2; 2 Sam. 7:22; 22:32; 1 Fal. 8:23; Zab. 86:8,10; Isa. 43:11; 44:6,8; 45:6-7,14,18,21-22; 46:5,9; Jer. 2:11; 5:7; 10:6; 16:20).
2. Ni Mungu wa kipekee, muumbaji, mwokozi (kama vile Mwanzo 1-2; 3:15; Zaburi 103-104).
3. Hutoa ahadi za matumaini na urejesho kwa maana ya Masihi (kama vile Isaya 53).
4. Imani katika Masihi huondoa uvunjifu wa uasi (yaani injili).
5. Yeye Yule aaminiye katika Masihi atakuwa na uzima wa milele (yaani injili).

Toleo la Textus Receptus, likifuatiwa na machapisho ya herufi kubwa א$^{c}$, D$^{c}$, K, L, na P, linaongezea neno "busara" (toleo la NKJV, "ni Mungu pekee aliye na busara"). Hili ongezeko haliko katika machapisho ya Kiyunani א$^{*}$, A, D$^{*}$, F, G, na H$^{*}$. Laweza kuwa ni nyongeza ya kiandishi toka Rum. 16:27. Toleo la UBS$^{4}$ hulipa andiko fupi alama "A" (yakini).

◙ **"na iwe heshima na utukufu"** Kimsingi hii ni maana ya neno la Agano la Kale *kabod* (cf. 1 Tim. 1:11).linatumika mara kadhaa katika kitabu cha Ufunuo likiwa na sifa zingine (kama vile 1 Tim. 4:9,11; 5:12,13; 7:12).
Katika Agano la Kale maneno ya Kiebrania yaliyozoeleka kwa ajili ya neno "utukufu" (*kabod*) mwanzoni kabisa yalikuwa ni maneno ya kibiashara yenye kurejea jozi ya vipimo vyenye kumaanisha "kuwa na uzito." Kile kilichokuwa na uzito ndicho kilikuwa na thamani. Mara nyingi dhana ya mng'ao iliongezwa kwenye neno kuelezea ukuu wa Mungu (kama vile Kut. 15:16; 24:17; Isa. 60:1-2). Yeye pekee anastahili heshima. Hapana mwanadamu awezaye kumwona akaishi (kama vile Kut. 33:17-23; Isa. 6:5). Mungu aweza kujulikana kupitia Kristo (kama vile Yer. 1:14; Mt. 17:2; Ebr. 1:3; Yakobo 2:1).
Neno "utukufu" kwa kiasi fulani ni tata.

1. laweza kufanana na "haki ya Mungu"
2. laweza kurejea kwenye "utakatifu" au "ukamilifu" wa Mungu
3. laweza kurejea kwenye taswira ya Mungu ambayo mwanadamu aliumbwa kwayo (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6), lakini baadaye ukaharibiwa kupitia uasi (kama vile Mwa. 3:1-22)

Mwanzoni lilitumika kwenye uwepo wa YHWH kwa watu wake (kama vile Kut. 16:7,10; Law. 9:23; Hes. 14:10).

◙ **"milele na milele"** Kwa maana iliyowazi hili neno ni "milele na milele," ni nahau kwa ajili ya pasipo na mwisho (kama vile Gal. 1:5; Fil. 4:20; 2 Tim. 4:18). Neno lile lile linatumika katika 1 Tim. 1:16 kwa ajili ya "uzima wa milele" na katika 1 Tim. 1:17 kwa ajili ya "ufalme wa milele."

## MADA MAALUM: MILELE (LAHAJA YA KIYUNANI)

Moja ya tungo ya kiyunani "katika nyakati" (kama vile Luka 1:33; Rum. 1:25; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 1 Tim. 1:17), ambayo inaweza kuaksi 'olam'. Angalia Robert B. Girdlestone, Synonyms of the Old Testament, kur. 319-321, na Mada Maalum: Milele ('*Olam*).

Tungo zingine zinazoweza kufanana "katika nyakati" (kama vile Mt. 21:19; Marko 11:14; Luka 1:55; Yohana 6:58; 8:35; 12:34; 13:8; 14:16; 2 Kor. 9:9) na "ya nyakati za nyakati" (kama vile Efe. 3:21). Kunaonekana kutokuwepo na utofauti kati ya lahaja hizi mbili za Kiyunani za "milele." Neno "nyakati" inaweza kuwa wingi katika namna ya kimafumbo ya tungo za kisarufi za kiualimu wa kiyahudi "wingi wa mfalme," au inaweza kurejerea dhana ya "nyakati" kadhaa katika namna ya Kiyunani ya "zama ya uovu," "enzi ijayo," au "zama ya haki" (angalia Mada Maalum: Enzi Hii na Enzi Ijayo).

◙ **"Amina"** angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 6:16.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 1:18-20**
**[18] Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri; [19] uwe mwenye imani na dhamiri njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani. [20] Katika hao wamo Himenayo na Iskanda, ambao nimempa Shetani watu hao, ili wafundishwe wasimtukane Mungu.**

**1:18 "agizo"** Paulo alitumia maneno mawili ya kijeshi katika aya hii: (1) "agizo" (1 Tim. 1:3,5,18) na (2) "kupigana vita vizuri" (1 Tim. 1:18; kama vile 2 Kor. 10:3-6; Efe. 6:10-17). Aya hii (yaani., 1 Tim. 1:18-20) inarudi kwenye suala la kithiolojia la waalimu wa uongo wa 1 Tim. 1:3-7.

| | |
|---|---|
| **NASB, TEV** | **"nawaamini"** |
| **NKJV** | **"nawakabidhi"** |
| **NRSV, NJB** | **"nawapeni"** |

Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO ya neno *paratithēmi*. Paulo alikabidhi kazi ya injili kwa Timotheo (kama vile 1 Tim. 6:20; 2 Tim. 1:14, kama Yesu alivyokwisha kabidhi ndani yake, kama vile 2 Tim. 1:12) kupitia juu ya wengine walio waaminifu (kama vile 2 Tim. 2:2).
Hili neno linatumika kwa

1. Yesu alijikabidhi mwenyewe Luka 23:46
2. Waamini walijikabidhi wao wenyewekwa Mungu katika Mdo. 14:23
3. Paulo akawakabidhi waamini kwa Mungu katika Mdo. 20:32
4. waamini anawakabidhi u kizazi kipya katika 2 Tim. 2:2

◙ **"kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyo tangulia juu yako"** Timotheo alipokea karama za rohoni na uthibitisho wa kinabii kwa kanisa la Lystra kipindi cha kuwekewa mikono (kama vile 1 Tim. 4:14). Hiki kifungu chaweza kumaanisha (1) "kutengenezwa kwa ajili yako" (kama vile toleo la NRSV) au (2) "kuniongoza kuja kwako" (kama vile toleo la RSV).

## MADA MAALUM:UNABII WA AGANO JIPYA

I. Sio sawa na Unabii wa Agano la Kale (BDB 611, KB 661; tazama Mada Maalumu:Unabii [Agano la Kale]), ambao una vidokezo vya upokeaji wa sheria za Kiyahudi na kunukuu mafunuo yaliyovuviwa toka kwa YHWH (kama vile Mdo. 3:18, 21; Rum. 16:26). Ni manabii tu waliweza kuandika maandiko.
   A. Musa aliitwa nabii (kama vile kumb. 18:15-21)
   B. Vitabu vya historia (Yoshua – Wafalme [isipokuwa Ruthu]) waliitwa "manabii wa mwanzo" (kama vile Matendo. 3:24)
   C. Manabii wanachukua nafasi ya makuhani wakuu kama chanzo cha habari kutoka kwa Mungu. (kama vile Isaya –Malaki)
   D. Mgawanyo wa pili wa kanuni za kanisa la Kiebrania ni "Manabii" (kama vile Mt. 5:17; 22:40; Luka 16:16; 24:25, 27; Rum. 3:21).

II. Katika Agano Jipya dhana ya unabii imetumika katika njia kadhaa tofauti tofauti.
   A. Kuwarejea manabii wa Agano la Kale na jumbe zao zilizovuviwa (kama vile Mt. 2:23; 5:12 11:13; 13:14; Rum. 1:2).
   B. Kuurejea ujumbe kwa mtu mmoja badala ya kikundi kichoungana (yaani, manabii wa Agano la Kale kimsingi waliongelea juu ya Israeli).
   C. Kuwarejea wote wawili Yohana mbatizaji (kama vile Mt. 11:9; 14:5; 21:26 Luka 1:76) na Yesu kama mpiga mbiu wa ufalme wa Mungu (kama vile Mt. 13:57; 21:11, 46; Luka 4:24; 7:16; 13:33; 24:19). Yesu pia alidai kuwa mkuu kuliko manabii (kama vile Mt. 11:9; 12:41; Luka 7:26).
   D. Manabii wengine katika Agano Jipya
      1. Maisha ya awali ya Yesu kama ilivyoandikwa katika injili ya Luka (yaani., kumbu kumbu za Maria)
         a. Elizabethi (kama vile Luka 1:41-42)
         b. Zakaria (kama vile Luka 1:67-79)
         c. Simoni (kama vile Luka 2:25-35)
         d. Ana (kama vile Luka 2:36)
      2. Ubashiri wa kejeli (kama vile. Kayafa, John 11:51)
   E. Inarejea juu ya mtu anayeitangaza injili (ikijumuishwa kwenye orodha ya kipawa cha utangazaji katika 1 Kor. 12:28-29; Efe. 14:11)
   F. Ikirejea juu ya vipawa vinavyoendelea kanisani (kama vile Mt. 23:34; Mdo. 13:1; 15:32; Rum. 12:6; 1 Kor. 12:10, 28-29; 13:2; Efe. 4:11) wakati mwingine hii inaweza kumaanisha kwa wanawake (kama vile Luka 2:36; Mdo. 2:17; 21:9; 1 Kor. 14:4-5).
   G. Ikirejea kwa sehemu mafunuo ya kitabu cha ufunuo (kama vile Ufu. 1:3; 22:7, 10, 18,19)

III. Manabii wa Agano Jipya
   A. Hawatoi ufunuo uliovuviwa kwa maana sawa kama manabii wa Agano la Kale waliofanya (yaani mafundisho ya Biblia). Usemi huu unawezekana kwa sababu ya Matumizi ya kifungu cha neno "Imani" (yaani., kwa maana ya injili iliyokamilika) iliyotumika katika Matendo 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 3, 20.
   Dhana hii iko wazi kutokana na fungu kamili la maneno lililotumika katika Yuda 3, "imani ya mara moja pasipo kujirudia imekabidhiwa kwa watakatifu." Imani ya "jumla pasipo kujirudia" inarejerea kwenye ukweli, mafundisho, dhana, maoni ya dunia juu ya mafundisho ya ukristo. Msisitizo huu unaotolewa mara moja tu ni msingi wa Kibiblia kwa ajili ya kuzuia uvuvio ulio wa kithiolojia wa maandiko ya Agano Jipya na pasipo kuruhusu maandiko mengine kufikirika kimafunuo (angalia Mada Maalumu: Uvuvio). Kuna maeneo mengi yenye utata, yasiojulikana katika agano jipya (Tazama Mada Maalumu: Fasihi za mashariki [mafumbo ya Kibiblia]), lakini waamini wanathibitisha kwa imani kuwa kila kitu "kinachohitajika" kwa ajili ya imani na utendaji inajumuishwa ikiwa na utosherevu wenye

uwazi wa kutosha katika Agano Jipya. Dhana hii inaelezwa kama "ufunuo pembe tatu."

1. Mungu amejidhihirisha mwenyewe katika historia kwa muda muafaka (UFUNUO)
2. Amechagua baadhi ya waandishi wa kibinadamu kuweka kumbu kumbu na kuelezea matendo yake (UVUVIO).
3. Alimtoa Roho Wake ili kufungua mawazo na mioyo ya watu wapate kuyaelewa maandishi haya, si kwa ubora tu bali kwa utoshelevu wa wokovu na maisha ya Mkristo yenye kufaa (NURU, tazama Mada Maalumu: nuru). Hoja iliyopo hapa ni kuwa uvuvio umewekewa ukomo kwa waandishi wa neno la Mungu. Hakuna maandiko mengine, maono au mafunuo yenye mamlaka. Sheria za kanisa zimefungwa. Tuna ukweli wote tunaouhitaji ili kuitikia vizuri kwa Mungu. Ukweli huu unaonekana vizuri katika makubariano ya waandishi wa Kibiblia dhidi ya waumini watiifu wa ki-Mungu wasiokubali. Hakuna mwandishi au mnenaji wa kisasa aliye na kiwango cha uongozi wa ki-Uungu kama ambao waandishi wa neno la Mungu waliokuwa nacho.

B. Kwa namna nyingine manabii wa Agano Jipya ni sawa na wale wa Agano la Kale.
   1. Utabiri wa matukio yajayo (kama vile Paulo, Mdo. 27:22; Agabo, Mdo. 11:27-28; 21:10-11; manabii wengine wasiotajwa Mdo. 20:23).
   1. Kutangaza hukumu (kama vile Paulo, Mdo. 13:11; 28, 25-28)
   2. Dalili za matendo ambayo dhahili yanaonyesha matukio (kama vile Agabo Matendo 21:11).

C. Mara zote wananena kweli ya injili, wakati mwingine kwa njia ya utabiri (kama vile Matendo 11:27-28; 20-23; 21:10-11) Lakini kimsingi huu sio mtazamo wenyewe. Unenaji wa unabii katika Wakorinto wa 1 kimsingi unaibainisha injili (kama vile 1 Kor. 14:24,39).

D. Ni Roho wa wakati ule ule akimaanisha kudhihirika wakati ule ule na utumiaji wa kiutendaji wa kweli ya Mungu kwa kila hali, tamaduni mpya au kipindi cha muda (kama vile 1 Kor. 14:3).

E. Walikuwa imara katika makanisa ya mwanzo ya Paulo (kama vile 1 Kor. 11:4-5; 12:28, 29;13:2, 8, 8,9; 14:1 3,4,5,6,22,24,29,31,32,37,39; Efe. 2:20; 3:5; 4:11; 1 The. 5:20) na wametajwa katika *Didache* (iliyoandikwa katika karne ya mwisho au karne ya pili tarehe haijulikani) na wakati wa mienendo ya Kikristo ya karne ya pili na tatu katika Afrika ya kaskazini.

IV. Je karama za Agano Jipya zimekoma?

A. Swali ni gumu kulijibu. Linasaidia kufafanua jambo kwa kuelezea kusudi la karama. Je wanamaanisha kuthibitisha mafundisho ya awali ya kuhubiri injili au ni njia endelevu ya kanisa kujihudumia lenyewe kwenye ulimwengu ulipotea?

B. Je mmoja aweza kuangalia kwenye historia ya kanisa kujibu maswali au Agano Jipya lenyewe? Hakuna kiashirio chochote kinachoonyesha katika Agano Jipya kuwa karama za rohoni zilikuwa za muda tu. Wale wote wanaojaribu kutumia 1 Kor 13:8-13 kuelezea habari hii wanatukanisha kusudi la mwandishi wa aya hii, ambayo inadokeza kuwa kila kitu kitatoweka isipokuwa upendo.

C. Nathubutu kusema kuwa tangu Agano Jipya, si historia ya kanisa, ndiyo yenye mamlaka, waamini wanapaswa kuthibitisha kuwa karama zinaendelea. Hata hivyo ninaamini kuwa mila zinaathiri tafsiri za maandiko. Baadhi ya maandiko yalioko wazi hayatumiki tena (yaani busu takatifu, Baibui, makanisa kukutana nyumbani n.k). kama mila zinaathiri maandiko, hivyo kwa vipi zisiathiri historia ya kanisa?

D. Hili ni swali ambalo haliwezi kujibiwa. Baadhi ya waumini wanatetea kuwepo na"ukoma" na wengine watetea "kusiwepo na ukomo". Katika eneo hili,kama ilivyo kwa mambo mengi yaliyo fasiliwa, moyo wa mwamini unabaki kuwa ndo kiini. Agano jipya ni tata na la kitamaduni zaidi. Ugumu unaweza kuamua ni maandiko yapi yanaathiliwa na mila/historia

na yapi yanaathiriwa kwa wakati wote na yapi kwa mila (kama vile Fee na Stuart, *How to read the Bible for all its Worth,* kur. 14-19 na 69-77 hapa ndipo pale mjadala wa uhuru na kuwajibika, unaopatikana katika Warumi 14:1-15, 13 na Kor. 8-10 unapokuwa wenye umuhimu mkubwa. Namna tunavyojibu swali ni muhimu katika njia mbili.

1. Kila mwamini anapaswa kutembea katika imani yake kwa mwanga walio nao. Mungu anaona mioyo yetu na nia.
2. Kila mwamini yampasa aruhusu waamini wengine kutembea katika uelewa wa imani. Lazima pawepo na uvumilivu ndani ya mipaka ya kibiblia. Mungu anatutaka tupendane kama anavyotupenda.

E. Kwa kuhitimisha suala hili, Ukristo ni maisha ya imani na upendo, na sio tu thiolojia kamili. Uhusiano wetu na Yeye unaosababisha kuwepo na uhusiano na wengine ni muhimu zaidi kuliko habari au imani kamili.

◙ **"uvipige vile vita vizuri"** Mara nyingi maisha ya Kikristo yanaonyeshwa kama tukio la kiriadha au vita, kama ilivyo hapa. Unabii unaohusiana na Timotheo ulimwezesha kuendelea kupigana vita vizuri kama vya Paulo (KAULI YA KATI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPO, kama vile 1 Tim. 6:12; 2 Tim. 2:3-4; 4:7; 2 Kor. 10:3-6; Efe. 6:10-17).

**1:19 "uwe mwenye imani na dhamiri njema"** Vita vizuri vinajumuisha kuwa na kuendelea kuwa na (KAULI TENDAJI TIMILIFU YA HALI YA KUENDELEA)

1. imani
2. dhamiri njema

Yote haya yametajwa katika 1 Tim. 1:5. Yanatajwa tena kwa sababu kupotea kwake ndio sababu ya washirika wengine wa kanisa wameshindwa kuendelea na imani. Imani ingaliweza kurejelea huenda kwenye (1) mafundisho ya Kikristo au (2) maisha ya Kikristo. Yote ni ya muhimu.

Tunajifunza toka 2 Tim. 2:17 kuwa Himenayo alikuwa akihusika kwenye kuyapotosha mafundisho (akidai kuwa ufufuo umekwisha tokea zamani) na wasiomcha Mungu (kama vile 2 Tim. 2:16). Jina jingine, Iskanda, lakini sio Yule mfua chuma aliyetajwa katika 2 Tim. 4:14 na Matendo 19 kwa sababu alikuwa ni adui wa injili.
Kwao kuikataa kweli na kutomjua Mungu haikuwa kwa sababu ya kudanganywa, bali walikataa kwa mapenzi yao (KAULI YA KATI [shahidi] YA HALI YA KUENDELEA YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ya neno *apōtheō*, kama vile Mdo. 7:39; 13:46; Rum. 11:1). Angalia maelezo juu ya dhamiri katika 1 Tim. 1:5.

◙ **"ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani"** Hili ni somo gumu na lenye mkanganyiko. Angalia MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1. Kuna mifano mingi ya uasi wa imani katika 1 Timotheo (kama vile 1 Tim. 1:19; 4:1-2; 5:14-15; 6:9-10,21; pia 2 Tim. 2:16-18; 3:1-8,13; 2 Pet. 2:1,20-21; Yuda 4). Angalia MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1.

**1:20 "nimempa shetani"** Hiki ni kifungu kigumu sana. Mifano ya Kibiblia ni

1. Mungu anamtumia shetani kumjaribu Ayubu (Ayubu 2:6)
2. Roho anamsukuma Yesu kwenye majaribu ya shetani (Marko 1:12)
3. Paulo anamsukumia kwa shetani ili kwamba aweze takasika na hatimaye kurejeshwa (1 Kor. 5:5)

Tambua kusudi lililoelezewa katika 1 Tim. 1:20 ni kuwafundisha wasije wakakufuru. Laweza kurejelea kwenye kuondolewa toka kwenye ushirika unaoamini. Adhabu ya Mungu ya kidunia mara zote huwa ni ukombozi. Mungu humtumia shetani aweze kuwajaribu wanadamu (kama vile Mwanzo 3; Ayubu 1-2; Zakaria 3). Kwa maana hiyo, Shetani ni chombo cha Mungu. Ni uasi wa shetani dhidi ya Mungu, shauku yake ya kuwa huru, ndiyo ilimfanya atende uovu, na sio kazi yake ya kujaribu. Angalia MADA MAALUM: SHETANI katika 1 Tim. 3:6.

Matumizi ya kifungu hiki kinadokeza kuna tumaini kwa ajili ya wale walimu wa uongo na wafuasi wao. Hata hivyo, stiari yenye kufanana iliyotumika kwa ajili ya waalimu wa uongo katika 1 Tim. 4:2 inamaanisha hakuna tumaini tena kwa ajili yao.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini Paulo anatetea utume wake kwenye waraka binafsi wa Timotheo?
2. Ni nini asili ya uasi wa imani huko Efeso?
3. Ni kwa namna gani Wakristo wanahusiana na sheria ya Musa?
4. Ni kwa namna gani Paulo anaitazama huduma yake? (mst.12)
5. Ni kwa nini anarudia rudia ushuhuda wake mara kwa mara? (1 Tim. 1:16)
6. Ni yapi yalikuwa maagizo ya Timotheo? (1 Tim. 1:18)
7. Ni kweli Hamenayo na Isakanda hawakustahili neema? (1 Tim. 1:19)
8. Nini maana ya "dhamiri njema?" (1 Tim. 1:19)
9. Inamaanisha nini kumkabidhi mtu kwa shetani? (1 Tim. 1:19

# 1 TIMOTHEO 2

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maelezo kuhusiana na maombi (2:1-3:1a) | Ombea wanaume | Utaratibu wa ibada | Ibada ya kanisa | Maombi ya liturujia |
| 2:1-7 | 2:1-7 | 2:1-7 | 2:1-7 | 2:1-7 |
| | Wanaume na wanawake katika kanisa | | | |
| 2:8-3:1 | 2:8-15 | 2:8-15 | 2:8-15 | 2:8 |
| | | | | Wanawake kwenye kusanyiko |
| | | | | 2:9-15 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Hiki kipengele kizima, 1 Tim. 2:1-3:13, kinashughulika na ibada ya kwenye hadhira na kusanyiko
   1. ibada ya kwenye hadhira (1 Tim. 2:1-15)
      a. kazi ya akina baba (1 Tim. 2:1-8)
      b. kazi ya akina mama (1 Tim. 2:9-15)
   2. kusanyiko la kanisa (1 Tim. 3:1-13)
      a. mchungaji (1 Tim. 3:1-7)
      b. shemasi (1 Tim. 3:8-10,12-13)
      c. wanawake wasaidizi (1 Tim. 3:11)

B. Mtazamo wa maombi ya waamini ni ukombozi wa "wote" (kama vile 1 Tim. 2:1). Shauku ya Mungu ni ukombozi wa "wote" (kama vile Yohana 3:16; 1 Tim. 2:4; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9). Yesu alitulipia adhabu ya dhambi zetu kwa ajili ya "wote" (kama vile Rum. 5:18-19). Ni mjumuisho wa kushangaza aina gani!

C. Kipengele hiki waweza kuwa ni mwongozo wa kanisa la mwanzo uliosanifiwa ili kusaidia makanisa kupanga na kuelekeza shughuli (kama vile 1 Tim. 3:14-15).

D. Sehemu iliyo ngumu katika sura hii kuweza kuitafasiri ni 1 Tim. 2:8-15. Sio vigumu kuweza kuelewa, lakini ni vigumu kuweza kujua namna ya kukitumia kwenye hali zetu za kitamaduni. Ni rahisi kuweza kutengeneza sehemu za Agano Jipya ambazo hatukubaliani nazo "kitamaduni" na, kwa hiyo, na sio la muhimu kwetu. Sijisikii vizuri kutotambulisha wazi andiko lililovuviwa kama tamaduni kwa sababu mbalimbali
1. Mimi ni nani nikanushe maandiko?
2. Nitajuaje kuwa mimi kuwa kwa kiasi kikubwa sishawishiwi na tamaduni zangu (upendeleo binafsi unaohusiana na hali ya kimazingira)?
3. Pana ishara yeyote ya kimaandiko, nahau, alama ambayo huchagua kile kinachoweza kuwa cha kitamaduni dhidi ya kile ambacho ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya makanisa yote ya enzi yote?
Kwanza, hapana alama za kimaandiko! Pili, lazima niruhusu maandiko yote yaweze kuelezea suala Fulani. Ikiwa maandiko yatawekwa pamoja juu ya mada lazima uwe ukweli wa wote. Kama maandiko yanaonekana kutoa hali au hoja mbalimbali, napaswa kuruhusu baadhi ya uhuru katika tafasiri (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth* by Fee and Stuart, kur. 70-76).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TIMOTHEO 2:1-7**
**[1] Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; [2] kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. [3] Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; [4] ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. [5] Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; [6] ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake. [7] Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume, (nasema kweli, sisemi uongo), mwalimu wa Mataifa katika imani na kweli.**

**2:1 "Kabla ya mambo yote"** Hii nahau ya Kiyunani inamaanisha "chenye umuhimu wa kwanza." Muktadha unadai kuwa hii inamaanisha kudhibiti na kuzuia athari za waalimu wa uongo.

◙ **"nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani"** Huu ni mfuatano wa maneno manne kwa ajili ya maombi (Flp. 4:6 ina matatu kati yake; Efeso 6:18 inayo mawili kati yake). Ni namna ya Paulo ya kusisitiza kuwa miundo yote ya maombi lazima yatolewe kwa watu wote, hasa walioko katika mamlaka. Katika Efe. 6:18 msisitizo wa aina ile ile juu ya kuomba kwa ajili ya wote umekuwa kidogo kwa waamini lakini hapa umejumuishwa pamoja.
Neno "maombi" (*enteuxis*) linajitokeza mahali hapa tu katika 1 Tim. 4:5.

◙ **"kwa niaba ya wote"** Neno "wote" linajitokeza mara tano katika mistari ya 1-7, linaonyesha kiwango cha maombi yetu na upendo wa Mungu. Baadhi wanaona msisitizo juu ya watu wote kama mwitikio wa jumuisho la waalimu wa uongo.

## MADA MAALUM:MAOMBI YA KUSIHI

I. Utangulizi
A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
1. Maombi binafsi, Mk. 1:35; Luka 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk. 11:17; Luka 19:46
3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luka 11:2-4
B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile. Yakobo 4:2)
D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.

E. Nafasi ya maombi ni mtu yeyote au kitu chochote kinachohusiana na waumini. Tunaweza kuomba, kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.

F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali

1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba

G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uwajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.

II. Taarifa za Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
    a. Ibrahim aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22ff
    b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israel
        1) Kutoka 5:22-23
        2) Kutoka 32:9-14,31-35
        3) Kutoka 33:12-16
        4) Kutoka 34:9
        5) Kumb. 9:18,25-29
    c. Samweli akiiombea Israel
        1) 1 Samweli 7:5-6,8-9
        2) 1 Samweli 12:16-23
        3) 1 Samweli 15:11
    d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18
2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizozitubia zinaathiri maombi yetu
    a. Zaburi 66:18
    b. Mithali 28:9
    c. Isaya 59:1-2; 64:7

B. Agano Jipya

1. Huduma ya kusihi/kuombea ya Mwana na Roho
    a. Yesu
        1) Warumi 8:34
        2) Waebrania 7:25
        3) 1 Yohana 2:1
    b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27
2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusihi
    a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
        1) Warumi 9:1ff
        2) Warumi 10:1
    b. Akiliombea kanisa
        1) Warumi 1:9
        2) Waefeso 1:16
        3) Wafilipi 1:3-4,9
        4) Wakolosai 1:3,9
        5) 1 Wathesalonike 1:2-3
        6) 2 Wathesalonike 1:11
        7) 2 Timotheo 1:3
        8) Filemon, uk. 4

c. Paulo analiomba kanisa limwombee
    1) Warumi 15:30
    2) 2 Wakorinthp 1:11
    3) Waefeso 6:19
    4) Wakolosai 4:3
    5) 1 Wathesalonike 5:25
    6) 2 Wathesalonike 3:1

3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusihi
    a. Kuombeana wao kwa wao
        1) Waefeso 6:18
        2) 1 Timotheo 2:1
        3) Yakobo 5:16
    b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
        1) Adui zetu, Mt. 5:44
        2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
        3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
        4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
        5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16

III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa

A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho
1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
2. Katika jina lake , Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Yuda 20
4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15

B. Visababishi
1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3
4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3

C. Mitazamo mingine
    a. Usitahimilivu
    b. Luka 18:1-8
    c. Wakolosai 4:2
1. Endelea kuomba
    a. Mathayo 7:7-8
    b. Luka 11:5-13
    c. Yakobo 1:5
2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7
3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zijulikanazo
    a. Zaburi 66:18
    b. Mithali 28:9
    c. Isaya 59:1-2
    d. Isaya 64:7

IV. Hitimisho la kithiolojia

A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

**2:2 "kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka"** Biblia haitufundishi juu ya haki ya Kiungu wa wafalme, lakini inafundisha mapenzi ya Kiungu kwa ajili ya serikali iliyoko madarakani (kama vile Rum. 13:1,2). Suala la kithiolojia sio ikiwa tunakubaliana na serikali yetu au serikali yetu ni ya haki. Waamini lazima wawaombee maafisa wa kiserikali kwa sababu woko katika mapenzi ya Mungu katika ulimwengu ulioanguka. Waamini wanatambua toka Rum.13:1,2 kuwa mamlaka yote hutolewa na Mungu, kwa hiyo, wafuasi wote, kama wafuasi wa Kristo tunaheshimu. Maelezo haya ni yenye nguvu zaidi pindi unapotambua Paulo anawaomba waamini kuwaombea viongozi wa kiserikali kama Nero!

◙ **"wenye mamlaka"** Neno hili ni *huperochē*. Angalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya Neno Ambatani *Huper* katika 1 Tim. 1:14.

## MADA MAALUM: SERIKALI YA WANADAMU

I. UTANGULIZI
   A. Ufafanuzi – serikali ni utaratibu wa kibinadamu wenyewe wa kutoa na kulinda kwa maana ya mahitaji (yaani, Mwanzo 4 na 11). Binadamu ni jamii ya viumbe hata kabla ya anguko (kama vile Mwa. 2:18).Familia, makabila, mataifa hutupatia jamii.
   B. Kusudi – Mungu anapendelea kuwa utaratibu wafaaa kwenye utawala huria.
      1. Sheria za Musa, hasa amri kumi za Mungu, ni mapenzi ya Mungu kwa wanadamu katika jamii. Inaleta ulinganifu wa ibada na Maisha.
      2. Hakuna mfumo wa muundo wa serikari unatetewa katika maandiko, ingawa Serikali ya kale ya makasisi wa Israeli ni mfumo tarajiwa wa huko mbinguni. Sio demokrasia wala ubepari ni ukweli wa kibiblia. Wakristo wanapaswa kutenda ipasavyo kwenye mfumo wa serikali yeyote walioikuta. Kusudi la mkristo ni uinjilisti na huduma, sio mapinduzi. Serikali zote ni za mpito
   C. Asili ya serikali ya mwandamu
      1. Roman katoliki wanadai kwamba serikali ya mwanadamu ni hitaji la asili. Aristotle anaonekana kwanza kudai wazo hili. Anasema, "mwanadamu ni mnyama wa kisiasa" na kwa hili alimaanisha kwamba serikali "ipo kwa ajili ya msaada wa maisha mazuri.
      2. Mprotestanti, hasa Martin Luther, anadai kuwa serikali ya mwanadamu ni ya asili toka kwenye anguko. Anaiita "ufalme wa Mungu wa mkono wa Kushoto." Alisema kuwa "Njia ya Mungu ya kutawala wanadamu wabaya ni kuweka watu wabaya katika utawala."
      3. Karl Marx anadai kuwa Serikali ndiyo njia ambayo wasomi wachache wanawaweka watu wengi chini ya utawala. Kwa yeye, serikali na dini huwa na jukumu sawa

II. NYENZO ZA KIBIBLIA
   A. Agano la Kale
      1. Israeli ni mfumo ambao utatumika mbinguni. Katika Israeli ya kale YHWH alikuwa mfalme. Serikali ya makasisi ni neno linalotumika kuelezea utawala wa Mungu wa moja kwa moja (kama vile 1 Sam. 1. 8:4-9).
      2. Utawala wa Mungu katika serikali ya mwanadamu unaweza kuonekana wazi katika kuteuwa kwake.
         a. wafalme wote, Dan. 2:21; 4:17,24-25
         b. Uongozi wa Musa, Dan. 2:44-45
         c. Nebuchadnezar (Babeli mpya), Yer. 27:6; Dan. 5:28
         d. Koreshi II (Uajemi), 2 Kor. 36:22; Ezra 1:1; Isa. 44:28; 45:1
      3. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa watiifu na wenye adabu hata kuvamia na kumiliki serikali…
         a. Danieli 1-4, Nebukadreza (Babeli mpya)
         b. Danieli 5, Belshazzar (Babeli mpya)
         c. Danieli 6, Dario (Uajemi)
         d. Ezra na Nehemia (Uajemi)
      4. Kurudishwa kwa Yuda kulikuwa ni kuomba kwa Koreshi na kutawala na uzao wake..

        a. Ezra 6:10; 7:23
        b. Wayahudi walipaswa kuomba kwa mamlaka ya kiraia, Mihnah, Avot. 3:2
  B. Agano Jipya
    1. Yesu alionyesha heshima kwa serikali ya kibinadamuu.
        a. Mathayo 17:24-27, Yeye alilipa kodi ya hekalu (dini na utawala wa kiraia ulikuwa na maaana ya kuwa mmoja,kama ile. Petro 2. 2:17)
        b. Mathayo 22:15-22; Marko 12:13-17; Luka 20:20-26, Alitetea nafasi ya kodi ya kirumi na hivyo mamlaka ya kiraia ya kirujmi.
        c. Yohana 19:11, Mungu aliruhusu utawala wa kiraia kufanya kazi.
    2. Maneno ya Paulo yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
        a. Warumi 13:1-5, waaminio lazima wawasilishe kwa utawala wa kiraia kwa kuwa walianzishwa na Mungu
        b. Warumi 13:6-7, waaminio lazima kulipa kodi na kuheshimu utawala wa kiraia.
        c. Timotheo 1. 2:1-3, waaminio lazima kuomba kwa utawala wa kiraia.
        d. Tito 3:1, waaminio lazima kunyenyekea kwa utawala wa kiraia.
    3. Maneno ya Petro yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
        a. Matendo 4:1-31; 5:29, Petro na Yohana kabla ya wakuu wa sinagogi (hii inaonyesha kuendelea mbele kibiblia kwa kutokutii kwa raia)
        b. Petro 2. 2:13-17, waaaminio lazima wawasilishe kwa utawala wa kiraia kwa mazuri ya jamii na kwa uinjilisti.
    4. Maneno ya Yohana yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
        a. Ufunuo 17,uzizi wa Babeli unawakilisha serikali ya wanadamu iliyoandaliwa na kufanya kazi mbali na Mungu.
        b. Ufunuo 18, uzinzi wa Babeli umeharibiwa.

III. HITIMISHO
  A. Serikali ya mwanadamu (katika ulimwengu ulioanguka) imewekwa na Mungu. Hii sio “haki ya kiungu ya wafalme,” bali kazi ya kiungu ya Serikali (yaani, amri sio machafuko). Hakuna mfumo wa mtu unaotetewa juu ya mwingine.
  B. Ni wajibu wa dini kwa waaminio kutii na kuomba kwa mamlaka ya kiraia.
  C. Ni sawa kwa waaminio kuunga mkono serikali ya wanadamu kwa kodo na mtazamo wa heshima.
  D. Serikali ya mwanadamu ni kwa lengo la utaratibu wa kiraia. Wao ni watumishi wa Mungu kwa kazi hii.
  E. Serikali ya mwanadamu sio mwisho. Ina kikomo katika mamlaka yake.Waaminio lazima kutenda kwa sababu ya dhamiri zao kwa kukataa mamlaka ya kiraia wakati inapita mipaka yake iliyowekwa na Mungu. Kama Augustino alionyesha katika *The City of God*, sisi ni raia wa falme mbili, moja ya muda na moja ya milele (kama vile. Wafil. 3:20). Tua wajibu kwa wote, lakini ufalme wa Mungu ni mwisho! Kuna yote mwelekeo wa kibinafsi na ushirika katika wajibu wetu kwa Mungu.
  F. Tunapaswa kuwatia moyo waminio katika mfumo wa kidemokrasia kushiriki kikamilifu katika mchakato wa serikali na kuutekeleza, wakati ikiwezekana, mafundisho ya maandiko.
  G. Mabadiliko ya kijamii lazima kuendelezwa na ubadilishaji wa mtu binafsi. Hakuna tawi halisi la theolojia linalojishughulisha na kifo, hukumu, pepo na jehanam la kudumu katika serikali. Serikali zote za mwanadamu, ingawa lazima na kutumiwa na Mungu, ni maonyesho ya dhambi ya shirika la mwanadamu mbali na Mungu. Dhana hii inaelezewa katika matumizi ya Johannine ya neno “ulimwengu (yaani, Yohana 1. 2:15-17).

◙ **"tuishi maisha ya utulivu na amani"** Hili linaonekana kumaanisha "amani" katika maana ya "pasipo majaribu" na "tulivu" kwa maana ya "mbali na machafuko." Waamini lazima waitumie imani yao kwa maisha yaliyo tulivu, ambacho ni kitu kigumu wakati wa msongo wa mawazo na mikanganyiko. Hawa waalimu wa uongo walikwisha iondoa amani na furaha kwa makanisa ya nyumbani huko Efeso. Paulo alitoa aina hii ya ushauri kwenye kanisa la

Thesolanike, ambalo lilikuwa na mkanganyo na moyo zaidi, sehemu ya matukio ya siku ya mwisho (kama vile 1 The 4:11; 2 The. 3:12). Katika uso wa machafuko ya kanisa, omba na uishi kwa upole, maisha ya Kimungu!

◙ **"katika utauwa na ustahivu"** Wakristo walikuwa wakiteswa na kutokueleweka na jamii ya wapagani. Njia mojawapo ya kulinyong'onyeza hili tatizo ilikuwa ni maisha ya waamini walioishi.

Neno "utauwa" limetumika mara kumi katika waraka wa Kichungaji (kama vile 1 Tim. 2:2; 3:16; 4:7,8; 6:3,5,6,11; 2 Tim. 3:5; Tito 1:1). Lina dokezo la kushangaza linalomwelekea Mungu likielezewa kwa maisha sahihi ya uadilifu. Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:7.

Neno "ustahivu" pia linatumika mara kadhaa katika waraka wa Kichungaji (kama vile 1 Tim. 2:2; 3:4,8,11; Tito 2:2,7). Linaelezewa katika maneno Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker kama "heshima, ustahivu, umuhimu, kuheshimika, utakatifu, utauwa" (uk. 47).

Wakristo lazima kuvuta/kukamata usikivu wenyewe kiuhakika (yaani. "kustahili heshima"), lakin sio kanushi (kama vile 1 Tim. 2:3; 1 Pet. 4:12-16).

**2:3 "hili ni zuri na linalokubalika"** Utauwa ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya wanadamu wote. Hii ni njia ya kurejelea kwenye urejesho "sura ya Mungu iliyopotea" ndani ya mwanadamu toka Mwa. 1:26-27. Siku zote Mungu anawahitaji watu wale wenye kuaksi tabia yake . siku zote swali limekuwa ni "namna gani" Agano la Kale linaonyesha kuwa mwanadamu aliyeanguka hawezi kuwa na utii au haki kwa nguvu zake mwenyewe. Kwa hiyo, agano jipya linasimamia juu ya matendo ya Mungu na uaminifu, na sio mwanadamu (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38). Mungu hurejesha na kuwahimiza wafuasi kupitia kitabu chake, Mwanae, na kupia Roho Wake. Hatuko sawa na Mungu tukisimamia kwenye utendaji wetu, lakini pale tu tunapomtambua kupitia wokovu, lengo la maisha yetu ni utakatifu (kama vile Mt. 5:20,48; Rum. 8:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10). Angalia MADA MAALUM: UTAKATIFU WA AGANO JIPYA/UTAKASO katika 2 Tim. 2:2.

◙ **"Mungu mwokozi wetu"** Angalia maelezo 2 Tim. 1:10.

**2:4 "ambaye hutaka watu waokolewe"** Waamini wanapaswa kuomba kwa ajili ya watu wote kwa sababu Mungu anawataka wote waokolewe. Huu ulikuwa ni ujumbe wenye kushangaza kwa kuwajumuisha waalimu wa uongo, ikiwa ni wale wenye ujuzi au Wayahudi, au zaidi yumkini katika nyaraka za Kichungaji. Huu ni ukweli mkubwa kuhusu upendo wa Mungu kwa ajili ya wanadamu wote (kama vile 1 Tim. 4:10; Ezek. 18:23,32; Yohana 3:16; 4:42; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:1; 4:14). Mstari huu unaonyesha kuwepo na mlingano mdogo, maamuzi ya kabla ya pande mbili yenye kusisitiza ukuu wa Mungu kwenye uondoaji wa hitaji la mwitiko wa mwanadamu. Ukweli uliokwisha semwa ni "hoja tano" za ufuasi wa Calvin, hasa "neema isiyopingika" na "upatanisho wenye ukomo," kutokufuata dhana ya agano la imani ya Kibiblia. Si vizuri kumshusha chini Mungu na kuwa kibaraka wa utashi huru wa mwanadamu, kama ilivyo sio vizuri kumshusha mtu chini na kuwa kibaraka wa mapenze ya Mungu. Mungu katika hali ya Ukuu wake amechagua kushughulika na mwanadamu aliyeanguka kwa njia ya agano. Siku zote huanzisha na kutengeneza agano (kama vile Yohana 6:44;65), lakini ameamuru kuwa mwanadamu ni lazima kuitikia na aendelee kuitika katika toba na imani (kama vile Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21).
Mara nyingi mazungumzo ya kithiolojia juu ya ukuu wa Mungu (yaliyoamliwa kabla) na mapenzi huru ya mwanadamu hudhoofika ndani ya ushindani wa kuyahakiki maandiko. Kwa uwazi Biblia inafunua ukuu wa YHWH. Hata hivyo, pia inafunua kuwa uumbaji wake wa hali ya juu, mwanadamu akaumbwa kwa mfano wake, amekwisha kupewa thamani binafsi kubwa, kuyafanya maamuzi ya kiadilifu. Mwanadamu lazima ashirikiane na Mungu katika kila eneo la maisha.
Neno "wengi" limetumika kudai kwamba Mungu amewachagua baadhi (waliochaguliwa) lakini sio wote; kwamba Yesu alikufa kwa baadhi ya watu , na sio kwa watu wote. Kwa usomaji mzuri wa maandiko yafuatayo unaonyesha kuwa haya yanatumika katika maana ya kufanana!

| **Isaya 53** | **Warumi 5** |
|---|---|
| 1. "wotel" (1 Tim. 2:6) | 1. "wote" (1 Tim. 2:18) |
| 2. "wengi" (1 Tim. 2:11-12) | 2. "wengi" (1 Tim. 2:19) |

◙ **"kuokolewa"** Hii ni KAULI TENDWA ISIO NA KIKOMO CHA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU (angalia Mada Maalumu katika 2 Tim. 1:9). Hili linadokeza kwamba wanadamu hawawezi kujiokoa wengine (SAUTI IRABU TENDWA) lakini Mungu yuko tayari, kupenda, na anaweza kufanya hivyo kupia Kristo.

◙ **"na kupata kujua yaliyo kweli**" Kifungu hiki kimetumika mara nyingi katika nyaraka za Kichungaji (kama vile 2 Tim. 2:25; 3:7; Tito 1:1). Inamaanisha kuelewa na kuitikia kwenye ujumbe wa injili (kama vile Efe. 4:13).

Huu ni muundo mpana wa Kiyunani wa *epi* + *gnōsis*, wenye kumaanisha "maarifa kamili na ya kiutendaji." Hii dhana ya ujumuishwaji kiukweli ilikuwa ni kuutetemesha msisitizo wa waalimu wa uongo juu ya tabaka la watu wenye uwezo na maarifa maalum. Uhusiano wa kweli kati ya vitu muhimu vya Wayahudi na Wayunani ndani ya waalimu wa uongo haujulikani. Lenye uhakika lina sehemu ya Kiyunani ambalo linakuza neno "hadithi," "unasaba," na "sheria" (angalia maelezo katika 1 Tim. 1:6-7). Pamekuwepo na mitazamo mingi zenye kuhusiana na sehemu ya Kiyunani. Hakika palikuwepo viashiria vya uovu ambavyo vilikuwa vikiainishwa zaidi na waalimu wa uongo wa Kiyunani kuliko wa Kiyahudi. Ni kwa kiasi gani muundo wa wenye ujuzi wa ngazi za kimalaika wanashiriki katika upotofu wa nyaraka za Kichungaji kiwastani haijulikani. Katika *Word Pictures in the New Testament*, juzuu ya. 4, uk. 567, A. T. Robertson anawatambua waalimu wa uongo kama "wale wenye ujuzi."

Kwa kutumia uvumbuzi wa wana akiolojia katika Nag Hammadi huko Misri sasa tunatambua mengi zaidi kuhusiana na mitazamo na thiolojia ya wenye ujuzi. Kuna tafasiri ya Kiingereza ya haya maandiko yaliyoandikwa *The Nag Hammadi Library* kikahaririwa na James M. Robinson and Richard Smith. Pia kuna uatafasiri wa kufurahisha wa maandiko haya katika Hans Jonas' book *The Gnostic Religion.*

◙ **"yaliyo kweli"** Neno "kweli" linatumika katika namna mbalimbali katika Agano Jipya:
1. kwa ajili ya Yesu kama mtu (kama vile Yohana 8:31,32, 14:6)
2. kumwelezea Roho (kama vile Yohana 16:13)
3. kuelezea "neno" (kama vile Yohana 17:17)

Ukweli wa Mungu hatimaye unaonekana katika Kristo, neno la uzima, ambalo kwa wingi limeandikwa katika Biblia, neno lililoandikwa; yote yameletwa nuruni kwetu kupitia mwakilishi ambaye ni Roho Mtakatifu. Kweli inayorejelewa hapa inafanana na "mafundisho ya kueleweka" ya 1 Tim. 1:9 na "injili ya utukufu ya Mungu mbarikiwa" ya 1 Tim. 1:10. Inarejelea kwenye habari njema za Yesu Kristo (kama vile 1 Tim. 4:3; 2 Tim. 2:25; 3:7; Tito 1:1).

## MADA MAALUM: "UKWELI" KATIKA MAANDIKO YA PAULO

Katika maana hii Yohana anaunganisha historia ya nyuma ya Waebrania na Wayunani ya neno *alētheia* yaani "ukweli" kama alivyofanya kwenye neno *logos* (kama vile 1:1-14). Waebrania (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) ikidokezwa hivyo ambavyo ni kweli, au uaminifu (mara nyingi linahusianishwa na maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno *pisteuō*). Katika Kiyunani lilihusianishwa na ukweli wa Pilato dhidi uongo; mambo ya kimbingu dhidi ya kidunia. Hili linakaa sawa kuhusiana na uwili wa Yohana. Mungu kwa uwazi ameridhihilisha hili (maana na asili ya neno *alētheia* ni kuweka wazi, kutokuficha, kudhihilisha wazi) Yeye mwenyewe katika Mwana. Hili limeelezewa katika njia tofauti.

1. Nomino, *alētheia*, kweli
   a. Yesu amejaa neema na kweli ya kutosha (kama vile Yohana 1:14,17 – maneno ya patano katika Agano la Kale)
   b. Yesu ndiye alikuwa mlengwa kwenye ushuhuda wa Yohana Mbatizaji (kama vile Yohana 1:32-34; 18:37 – nabii wa mwisho wa Agano la Kale)
   c. Yesu anaongea ukweli (kama vile Yn. 8:40,44,45,46 – ufunuo ni fumbo na kitu binafsi)
   d. Yesu ni njia, kweli, na uzima (kama vile Yohana 14:6)
   e. Yesu anawatakasa katika kweli (kama vile Yohana 17:17)
   f. Yesu (neno *Logos*, 1:1-3) ni kweli (kama vile Yohana 17:17)
2. Kivumishi, *alēthēs*, kweli, uaminifu
   a. Ushuhuda wa Yesu (kama vile Yohana 5:31-32; 7:18; 8:13-14)

b. Hukumu ya Yesu (kama vile Yohana 8:16)

3. Kivumishi, *alēthinus*, kweli
   a. Yesu ni nuru ya kweli (kama vile Yohana 1:9)
   b. Yesu ni mkate wa kweli (kama vile Yohana 6:32)
   c. Yesu ni mzabibu wa kweli (kama vile Yohana 15:1)
   d. Yesu ni shuhuda wa kweli (kama vile Yohana 19:35)
4. Kielezi*, alēthōs*, hakika
   a. Msamalia mwema anamshuhudia Yesu kama mwokozi wa ulimwengu (kama vile Yohana 4:42)
   b. Yesu ni chakula na kinywaji cha kweli, kama chakula cha manna kilivyopingwa katika siku za Musa (kama vile Yohana 6:55)

Neno ukweli na unyumbulisho wake pia unaelezea ushuhuda mwingine wa Yesu, kwa neno alēthēs

a. Ushuhuda wa Yohana Mbatizaji ni wa kweli (kama vile Yohana 10:41)
b. Ushuhuda wa Yohana (mwandishi wa Injili) ni wa kweli (kama vile Yohana 19:35; 21:24)
c. Yesu anaonekana kama nabii wa kweli (kama vile Yohana 6:14; 7:40)
d. Kwa mazungumzo mazuri kuhusu ukweli katika Agano la Kale angalia George E. *Ladd's A Theology of the New Testament*, kur.263-269

**2:5"kuna Mungu mmoja"** Msisitizo juu ya imani ya Mungu mmoja (kama vile Rum. 3:30; 1 Kor. 8:6; Efe. 4:6) waweza kupatikana katika 1 Tim. 1:17, ambao unaaksi Kumb. 6:4-6. Hata hivyo, Yesu mwana na Mungu Baba wanaonekana kuwa tofauti hapa. Ni muhimu kukumbuka madai ya Agano Jipya kuwa Yesu ni Mungu (kama vile Yohana 1:1; Kol. 1:14-16; Ebr. 1:2,3) lakini pia tabia tofauti toka kwa Baba. Mafundisho ya Utatu (angalia Mada Maalum katika Tito 3:6) yanatambua umoja wa roho wa Mungu mmoja na bado, ule upekee wa milele wa hawa watatu. Moja ya njia ya kuonyesha hili fumbo la kibiblia ni kulingnisha sura toka injili ya Yohana.

1. Yesu ni mmoja na Baba (Yohana 1:1; 5:18; 10:30,34-38; 14:9-10; 20:28).
2. Yesu amejigawa toka kwa Baba (Yohana 1:2,14,18; 5:19-23; 8:28; 10:25,29; 14:10,11,12,13,16; 17:1-2).
3. Yesu ni mwenye kutii kwa Baba (Yohana 5:20,30; 8:28; 12:49; 14:28; 15:10,19-24; 17:8).

Dhana ya Uungu wa Mwana na tabia ya Roho ziko wazi katika Agano Jipya, lakini halikufanyiwa kazi kikamilifu katika thiolojia ya imani kamili mpaka katika karne ya pili nay a tatu. Neno "utatu" sio la Kibiblia, lakini dhana kamili ni (kama vile Mt. 3:16-17; 28:19; Yohana 14:26; Mdo. 2:32-33,38-39; Rum. 1:4-5; 5:1-5; 8:1-4,8-10; 1 Kor. 12:4-6; 2 Kor. 1:21-22; 13:14; 4:4-6; 1 The. 1:2-5; 2 The. 2:13; Tito 3:4-6; 1 Pet. 1:2; Yuda 20-21).

Kisarufi cha 1 Tim. 2:5-6 kinatupatia sababu ya kithiolojia zenye kuhusiana na wokovu jumuishi wa Mungu.

1. Kuna Mungu Mmoja. Toka Mwa. 1:26-27 tunatambua kuwa watu wote wameumbwa kwa sura yake.
2. Kuna njia moja tu ya kwenda kwa Baba kupitia Masihi (kama vile Yohana 14:6), huenda akawa ametabiri katika Mwa. 3:15.
3. Kuna namna moja tu ya wokovu, matoleo ya dhabihu yaliyomalizika ya Mwana Kondoo wa Mungu asiye na dhambi, Yesu (kama Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21).

Kuna Mungu Mmoja anayetoa njia kwa ajili ya watu wote kuwa na ushirika naye (kama vile Mwa. 3:15). Yeyote ajaye, lakini aje kupitia njia yake, kupitia Mwana wake ambalo ndiyo tumaini tu kwa ajili ya ukubalifu.

## MADA MAALUM: IMANI KWA MUNGU MMOJA

M wanadamu amehisi kuwa kuna ukweli zaidi kuliko ule wa kimaumbile (yaani, yanayoathiriwa na mambo yaliyo nje ya uwezo, kama vimbunga, mfumo wa kupatwa kwa jua au mwezi, kimondo, hali ya hewa,matukio, vifo, n.k.). Wataalamu wa Elimu ya Mwanadamu wanatwambia kuwa walivikuta vitu ndani ya makaburi ya kale ya hominoids ambavyo vilikuwa kwa ajili ya maisha ya baadaye, ambavyo vilionekana kama nyongeza ya maisha haya. Utamaduni wa kwanza ulioandikwa ulikuwa Sumer (Tigri ya kusini, Mto wa Eufrate), ulianza mnamo 10,000 - 8,000 K.K. Hawa waliandika mashairi kuyaeleza maoni yao ya miungu na ushirika wao. Kisha, zaidi ya hayo kama wanadamu na udhaifu wao. Mila zao zilianza kuwepo katika mtindo wa masimulizi marefu kabla ya wao kuandika.

Kulikuwa na kukua kwa thiolojia kutokana na

1. imani juu ya vitu vyote ni hai
2. miungu wengi wa
3. mungu mkuu (au wa uwili)

Dhana ya "Mungu mmoja" (aliye mmoja na nafsi ya kwanza, Mungu wa maadili asiye na mahusiano ya mke), si "mungu mkuu" miungu wengi au mungu mzuri wa uwili w ki-Irani (Wafuasi wa Zoroaster, ni wa pekee kwa Israeli (Abrahamu na Ayubu, 2000 K K.). Ni mmoja pekee huko Misri (Amenhotep IV, pia anajulikana kama Akhenaten, 1367-1350 au 1386-1361 K.K. AMBAYE ALIABUDU Atemi, mungu jua, kama mungu pekee). Tazama J. Assmann, *The Mind of Egypt*, kr. 216-217.

Dhana hii inaelezwa katika vifungu kadhaa ndani ya Agano la Kale.

1. "hakuna aliye kama YHWH Elohim,wetu" Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 33:26; 1 Fal. 8:23
2. "hapana mwingine zaidi Yake," Kumb. 4:35,39; 32:39; 1 Sam. 2:2; 2 Sam. 22:32; Isa. 45:21; 44:6,8; 45:6,21
3. "YHWH ni mmoja" Kumb. 6:4; Rum. 3:30; 1 Kor. 8:4,6; 1 Tim. 2:5; Yakobo 2:19
4. "hakuna aliye kama Wewe," 2 Sam. 7:22; Yer. 10:6
5. "Wewe ni Mungu wa pekee," Zab. 86:10; Isa. 37:16
6. "kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwepo mwingine," Isa. 43:10
7. "hapana mwingine; zaidi ya mimi. . .hapana mwingine," Isa. 45:5,6,22
8. "Yeye ni chanzo cha vitu vyote," Isa. 45:7 (kama vile. Amosi 3:6)
9. "hapana mwingine, hapana Mungu tena," Isa. 45:14,18
10. "hapana mwingine zaidi ya mimi," Isa. 45:21
11. "hapana mwingine;. . .hakuna aliye kama mimi," Isa. 46:9

Lazima ikubalike kwamba haya mafundisho ya muhimu yamefunuliwa katika njia endelevu. Semi za kale zingeweza kueleweka kama "mungu mmoja" au Mungu mmoja wa matendo (kuna miungu wengine, yaani, Yoshua. 24:15; 1 Fal. 18:21), lakini Mungu mmoja kwetu (kama vile Kut. 15:11; 20:2-5; Kumb. 5:7; 6:4,14; 10:17; 32:12; 1 Fal. 8:23; Zab. 83:18; 86:8; 136:1-9).

Maandiko ya kwanza ambayo yalianza kudokeza juu ya umoja (Mungu mmoja wa kifalsafa) ni ya kale (kama vile Kut. 8:10; 9:14; 20:2-3; Kumb. 4:35,39; 33:26). Madai kamili na yenye mashindano yanapatikana katika Isaya 43-46 (kama vile 43:10-11; 44:6,8; 45:7,14,18,22; 46:5,9).

Kitabu cha Agano la Kale kinaishusha thamani ya miungu ya mataifa kama

1. uumbaji wa mwanadamu – Kumb. 4:28; 2 Fal. 19:18; Zab. 115:4-8; 135:15-18; Isa. 2:8; 17:8; 37:19; 40:19; 41:7,24,29; 44:10,12; 46:6-7; Yer. 10:3-5; Ufu. 9:10
2. pepo wabaya– Kumb. 32:17; Zab. 106:37; Isa. 8:19; 19:3c; 1 Kor. 10:20; Ufu. 9:20
3. majivuno, tupu – Kumb. 32:21; 2 Fal. 17:15; Zab. 31:6; Isa. 2:18; 41:29; Yer. 2:5; 10:8; 14:22; Yer. 2:5; 8:19
4. kisicho mungu – Kumb. 32:21; 2 Nya. 13:9; Isa. 37:19; Yer. 2:11; 5:7; 1 Kor. 8:4-5; 10:20; Ufu. 9:20

Kitabu cha Agano Jipya kinadokeza juu ya Kut. 6:4 katika Rum. 3:30; 1 Kor. 8:4,6; Efe. 4:6; 1 Tim. 2:5; na Yakobo 2:19. Yesu analinukuu hili kama amri ya katika Mt. 22:36-37; Marko 12:29-30; Luka 10:27. Kitabu cha Agano la Kale, pamoja na Agano Jipya, kinadai kwamba ukweli wa viumbe vingine vya kiroho (pepo wabaya, malaika), lakini muumbaji mmoja wa pekee/ Mungu mwokozi (YHWH, Mwa. 1:1).

Mungu mmoja wa Kibiblia anabainishwa na

1. Mungu ni mmoja na wa pekee (asili ya uhai wake ni dhahania, haidhihirishwi)
2. Mungu ni nafsi (kama vile Mwa. 1:26-27; 3:8)
3. Mungu ni wa maadili (kama vile Kut. 34:6; Neh. 9:17; Zab. 103:8-10)
4. Mungu aliwaumba wanadamu kwa sura na mfano wake (Mwa. 1:26-27) kwa ushirika (yaani., #2). Yeye ni Mungu mwenye wivu (kama vile Kut. 20:5-6)

Kutoka kitabu cha Agano Jipya

Mungu ana umilele wa aina tatu, uthihirisho wa nafsi (tazama Mada Maalum: Utatu)

1. Mungu amefuliwa kwa ukamilifu na utimilifu katika Yesu (kama vile Yohana 1:1-14; Kol. 1:15-19;

Ebr. 1:2-3)
2. Mpango wa Mungu wa milele kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka ni kujitoa dhabihu kwa Mwana Wake wa pekee (Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; Flp. 2:6-11; Webrania)

◙**"nampatanishi kati ya Mungu na mwanadamu"** Huu ni mfano wa uthibitisho wa Agano la Kale kuwa imani katika Yesu aliye binadamu na kazi ni njia pekee ya kuwa sawa na Baba (kama vile Yohana 10:1-18; 14:6). Hii mara nyingi hurejelea kama "kashfa ya kutojumuishwa kwenye injili." Huu ukweli uko nje ya wakati katika siku zetu za leo za uvumilivu (pasipo na masharti), lakini kama Biblia ni ufunuo binafsi wa Mungu, hivyo waamini lazima wathibitishe hii dhana ya kutojumuishwa. Hatusemi uwepo wa dini moja ndio suluhu ya yote, bali tunasema kuwa imani katika Kristo ndiyo suluhisho pekee la Mungu.
Matumizi ya neno "msuluhishi" lina madokezo ya kikuhani (kama vile Ebr. 8:6; 9:15; 12:24). Kuhani alisimama kati ya watu wahitaji na Mungu mtakatifu. Yesu ndiye kuhani wetu Mkuu (kama vile Ebr. 7-9). Yesu ni

1. Mwokozi
2. Mbadala wetu
3. Mshauri wetu
4. Mwombezi wetu

◙ **"Mwanadamu Kristo Yesu"** Msisitizo wa huu mstari ni kuwa Yesu ni mwanadamu kamili nab ado msuluhishi kati ya Mungu na Mwanadamu (kama vile Yohana 14:6). Walimu wa uongo wenye ujuzi wangaliweza kumkana Yesu mwanadamu (kama vile Yohana 1:14; 1 Yohana 1:1-3).
Yawezekana kuwa historia ya nyuma sio ya wale wenye ujuzi, bali ni uainishaji wa Paulo wa Adamu hadi Kristo (kama vile Rum. 5:12-21; 1 Kor. 15:21-22,45-49; Fil. 2:6). Yesu alionekana kama ni Adamu wa pili, mwanzo wa jamii mpya, sio ya Kiyahudi, sio ya Kiyunani, isiyo ya kiume, isiyo ya kike, sio mtumwa, sio bure, bali ya Kikristo (kama vile 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11).
Pia yawezekana kuwa 1 Tim. 2:5 na 6 ni maelezo ya kithiolojia ya neno "kweli," yanayopatikana katika 1 Tim. 2:4.

**2:6"ambaye alijitoa Mwenyewe"** Baba alimtuma Yeye lakini Yesu kwa kupenda Mwenyewe akaja na kuutoa uhai wake (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45; Yohana10:17,18).

◙**"kuwa ukombozi kwa ajili ya wote"** Hili linaaksi ukweli mkuu wa Isaya 53 (hasa 1 Tim. 2:6). Neno "mkombozi" limetokana na soko la watumwa na lilitumika kwa ajili ya kumnunua rafiki au ndugu toka utumwani au kwenye mateka ya kijeshi. Kisarufi cha hiki kifungu ni cha muhimu zaidi: (1) kuna muundo ambatani usio wa kawaida wa neno "mkombozi," likiwa na KIHUSISHI *anti* (badala ya), (2) KIHUSISHI "kwa ajili ya" ni KIHUSISHI cha Kiyunani cha neno *huper*, lenye kumaanisha "kwa niaba ya" (kama vile Tito 2:14). Msisitizo wa kithiolojia ni upatanisho mbadala wa Yesu Kristo kwa niaba yetu (kama vile 2 Kor. 5:21).

## MADA MAALUM: FIDIA/UKOMBOZI

I. AGANO LA KALE

A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.

1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).

2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
    a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
    b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)
    c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)

B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
    a. Kimaumbile
    b. Kijamii
    c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
    a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
    b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
    a. Baba
    b. Mme
    c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

II. AGANO JIPYA

A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisis ni wa Kristo.
2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laana" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
3. *Luō,* "kuweka huru"
    a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
    b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
        1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
        2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
        3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
    c. *Lutrōsis,* "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
        1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
        2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
        3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
4. *Apolytrōsis*
    a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
        1) Luka 21:28
        2) Warumi 8:23
        3) Waefeso 1:14; 4:30
        4) Waebrania 9:15

b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
    1) Warumi 3:24
    2) 1 Wakorintho 1:30
    3) Waefeso 1:7
    4) Wakolosai 1:14

5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.

1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambi kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!
6. Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

◙ **"kwa ajili ya wote"** Namshukuru Mungu kwa ajili ya neno "wote" lililotumika mara tano katika 1 Tim. 2:1-7! Ni muhimu zaidi kuwa tutambue kwamba kifo cha Yesu kilifunika dhambi za ulimwengu wote (kama vile Yohana 1:29; 3:16,17; 1 Tim. 4:10; Tito 2:11; Ebr. 2:9; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14). Kitu kinachomtuna mtu yeyote na kila mtu aweze kuokolewa sio dhambi zao, bali kutokuamini kwao kwa kazi aliyoimaliza Kristo Yesu (kama vile Yohana 1:12; Mdo. 17:30; 1 Tim. 4:10; 1 Yohana 5:10-13). Ukweli huu lazima ulinganishe maamuzi ya kabla (angalia Mada Maalum katika Tito 2:11).

**NASB "utakaoshuhudiwa kwa majira yake"**
**NKJV "kushuhudiwa kwa majira yake"**
**NRSV "huu ulikuwa ni ushuhuda wa majira yake"**
**TEV "ushahidi wa majira yake"**
**NJB "huu ni ushuhuda uliotolewa kwa wakati wake"**

Hiki kifungu ni mfanano kwenye 1 Tim. 6:15 na Tito 1:3. Mungu yupo katika udhibiti wa matukio ya kihistoria. Kristo alikuja kwa majira yake kuukomboa ulimwengu (kama vile Rum. 5:18-19).

Uwezekano mwingine ni kuwa laweza kuhusiana kwenye Rum. 5:6; Gal. 4:4; Efe. 1:10, ambapo hali Fulani ya kihistoria ya karne ya kwanza ya ulimwengu wa Wayunani na Warumi ukatoa muda muafaka:

1. *Pax Romana*, au amani ya Rumi, iliruhusu watu kusafiri toka nchi moja hadi nyingine kwa uhuru.
2. Lugha moja (*Koinē* ya Kiyunani) iliwaruhusu watu wote wa ulimwengu wa Mediteranian kuelewana wao kwa wao.
3. Hali ya kufilisika kwa wazi kwa dini za Kiyahudi na Kirumi kulisababisha watu kutafuta maana ya maisha. Walihitaji zaidi sehemu binafsi kuhusiana na mambo yao ya kiroho (hili pia linaonekana kwenye kuinuka kwa dini za siri).

**2:7"kwa ajili ya hili naliwekwa"** Huu ni msisitizo juu ya uchaguzi wa Paulo na kuitwa kwake na Mungu (mkabiliano wake akiwa njiani kuelekea Dameski), zaidi kama 1:1. Mungu anawahitaji watu wa mataifa kuelewa jumuisho lake la injili.

**◙"kuwa mhibiri na mtume. . .kama mwalimu"** Wakati mwingine hizi huorodheshwa tofauti kama karama za rohoni,kama ilivyo katika1 Kor.12:28 au Efe. 4:11. Katika orodha hii neno "mtume" laweza kurejelea kwa mhubiri (hasa utumiaji wa neno "unabii" katika 1 Wakorintho, kama vile 1 Kor. 11:4,5; 13:9; 14:1,3,4,5,24,31,39). Kwa maana hiyo kila karama za uongozi huu hutangaza injili ya aina ile ile ikiwa na misisitizo tofauti. Paulo anatumia tena maneno yale yale katika 2 Tim. 1:11 kuielezea huduma yake.

**◙"(nasema kweli, sisemi uongo)"** Wengi wa watoa maoni wamekwisha sema kuwa hii haitakuwa sawa kwenye barua binafsi iliyoandikwa na Paulo kwa mtenda kazi mwanza, Timotheo. Lakini sharti tukumbuke kuwa hizi barua zilimaanisha kusomwa wazi mbele ya kanisa (kama vile 1 Tim. 6:21b; 2 Tim. 4:22b; Tito 3:15b). Hizi barua zilikuwa ni barua za Paulo ya mapendekezo na uhamishaji wa mamlaka kwa mwakilishi wake wa kitume aliyetumwa kwa makanisa ya huko Efeso, yaliyokuwa yakihangaika na waalimu wa uongo.

**◙ "kama mwalimu wa mataifa"** Paulo alitambua kuwa Mungu alimwita yeye hasa kuitangaza injili ya Yesu Kristo kwa mataifa (kama vile Matendo 9:15; 22:21; 26:17; Rum. 1:5; 11:13; 15:16; Gal. 1:16; 2:7; Efe. 3:1-2,8; 2 Tim. 4:17). Huu ni uthibitisho mwingine wa wote wa upendo wa Mungu na ukombozi wa Kristo.

**◙"katika imani na kweli"** Hili laweza kurejea kwenye (1) mwonekano wa mpiga mbiu (2) kilichomo kwenye ujumbe. Katika 1 Tim. 1:14 "imani" inahusianishwa kwenye "upendo." Maneno haya yote yanamuelezea Yesu na yanamaanisha kufuatishwa na wafuasi wake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 2:8-15**

**[8] Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano. [9] Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; [10] bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu. [11] Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. [12] Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. [13] Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. [14] Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa. [15] Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi.**

**2:8"Hivyo nataka wanaume wasalishe kila mahali"** Kama Paulo alivyothibitisha heshima na ustahivu kwenye maisha ya wazi (kama vile 1 Tim. 2:1-7), sisi pia, katika ibada (kama vile 1 Wakorintho 11-14). Kifungu "katika kila mahali" yumkini linarejelea makanisa ya nyumbani yaliyoko karibu na Efeso. Maombi yaliyokubalika yanaelezewa kwa namna tatu katika mstari huu wa 8.

1. kuiinua mikono iliyotakata
2. pasipokuwa na hasira
3. wala majadiliano

Hizi sifa kwa uwazi zinamwonyesha Paulo akizungumza kwa waamini waminifu na kuwatenga waalimu wa uongo, walikuwa ni wazungumzaji mbadala (yumkini wajene vijana), na wafuasi wao.
Paulo anatumia hiki kifungu, "katika kila sehemu," mara nyingi (kama vile 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 2:14; 1 The. 1:8; 1 Tim. 2:8). Chaweza kuwa ni dokezo la Agano la Kale kwa Mal. 1:11, lenye kutoa unabii ibada za ulimwengu wa Masihi. Hili lingaliweza kuendana na matumizi ya neno "wote" in 1 Tim. 2:1-7.

◙**"akiinua mikono iliyotakata"** Hii ilikuwa ni hali ya kawaida ya maombi ya Wayahudi. Haya yalikuwa ,maombi kawaida ya Kiyahudi. Inaagiza kuwa maneno ya waamini na maisha lazima kukubaliana nayo (kama vile Yakobo 4:8).

◙**"pasipo ghadhabu"** Hili ni neno la Kiyunani *orgē*, lenye kumaanisha "upinzani uliokomaa" (kama vile Mt. 5:23-24; 6:15). Hasira kwa wengine huathiri uhusiano pamoja na Mungu (kama vile Mt. 5:21-24; Marko 11:25; 1 Yohana 2:9,11; 4:20-21).

**NASB** **"upinzani"**
**NKJV** **"mashaka"**
**NRSV, TEV,**
**NJB** **"majadiliano"**

Mwanafalsafa wa Kiyunani alitumia hili neno kwa ajili ya kipindi cha mafundisho au majadiliano. Katika Agano la Kale kuna dokezo lenye kinyume (kama vile Mt. 15:19; Marko 7:21). Hapa, linarejea kwenye muktadha wa mafundisho au mwonekano usio sawa, hasira, na usumbufu wa walimu wa uongo.

## MADA MAALUM: MAOMBI, YASIYO NA UKOMO INGAWA YANA UKOMO

A. Madokezo ya injili
   1. Waamini wanatiwa moyo kustahimili kwenye maombi na Mungu atafanya "mambo mazuri" (Mathayo, Mt. 7:7-11) au Roho wake" (Luka, Luka 11:5-13)
   2. Katika muktadha wa kanisa waamini wenye staha (wawili) wanatiwa moyo kuungana katika maombi (Mt. 18:19)
   3. Katika Muktadha wa hukumu ya dini ya Kiyahudi waamini wanatakiwa kuomba kwa imani pasipo na mashaka (Mt. 21:22; Marko 11:23-24)
   4. Katika muktadha wa ile mifano miwili (Luka 18:1-8, hakimu asiye haki na Luka 18:9-14, Mafarisayo na wenye dhambi) waaminio wanatiwa moyo kutenda kivingine toka kwa hakimu mtauwa na Farisayo mwenye kujihesabia haki. Mungu huwasikia wale wanyenyekevu na moyo wa kutubu (Luka 18:1-14)

B. Maandiko ya Yohana
   1. Katika muktadha mwanamme aliyezaliwa kipofu ambaye Yesu alimponya, upofu wa kweli wa Mafarisayo unafunuliwa. Maombi ya Yesu (kama ya mtu yeyote) yanajibiwa kwa sababu alimfahamu Mungu na kuishi ipasavyo (Yohana 9:31).
   2. Mazungumzo ya Yohana ya chumba cha juu (Yohana 13-17)
      a. Yohana 14:12-14 – maombi ya kuaminika yanachagizwa na
         1) Yale yatokayo kwa mwamini
         2) yakiombwa katika jina la Yesu
         3) akitamani kuwa Baba apate kutukuzwa
         4) kuzitunza amri (mst. 15)
      b. Yohana 15:7-10 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
         1) kudumu katika Yesu
         2) Neno lake lidumu ndani yao
         3) kutamani Baba apate kutukuzwa

4) kuzaa matunda mengi
5) kuzitunza amri (mst. 10)

c. Yohana 15:15-17 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
1) uchaguzi wao
2) uzaaji wao wa matunda
3) kuomba kwa jina la Yesu
4) kuitunza amri ile ya kupendana ninyi kwa ninyi

d. Yohana 16:23-24 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
1) kuomba kwa jina la Yesu
2) kutamani kuwa furaha yao ikatimie

3. Barua ya kwanza ya Yohana (1 Yohana)

a. 1 Yohana 3:22-24 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
1) kuzitunza amri zake (kur. 22,24)
2) kuishi istahilivyo
3) kuamini katika Yesu
4) kupendana ninyi kwa ninyi
5) kudumu katika Yeye na Yeye ndani yetu
6) kuwa na karama za rohoni

b. 1 Yohana 5:14-16 – maombi ya mwamini yanachagizwa na
1) kuwa na uhakika ndani yake Mungu
2) kutokana na mapenzi yake
3) waamini kuombeana wao kwa wao

C. Yakobo

1. Yakobo 1:5-7 – waamini wanaokabiliana na majaribu mbalimbali huhitajika kuomba kwa ajili ya hekima pasipo kuwa na mashaka
2. Yakobo 4:2-3 – waamini wanapaswa kuomba wakiwa na mienendo mizuri
3. Yakobo 5:13-18 – waamini wenye kukabiliwa na matatizo ya kiafya hutiwa moyo
   a. kuwaomba wazee waombe
   b. kuomba kwa imani
   c. kuomba kuwa dhambi zao zipate kusamehewa
   d. kuzikiri dhambi wao kwa wao na kuombeana wao kwa wao (sawa na 1 Yohana 5:16)

Jawabu la maombi yenye nguvu ni kumfanana Kristo. Hii ndiyo maana ya kuomba kwa jina la Yesu. Kitu kibaya ambacho Mungu anaweza kukifanya ni kuyajibu maombi yao ya ubinafsi! Kwa maana moja majibu yote hujibiwa. Kitu cha thamani kwenye maombi ni kuwa waamini hutumia muda wao wakiwa na Mungu, wakimwamini Mungu.

**2:9**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"vivyo hivyo"** |
| **NKJV** | **"katika maana hiyo"** |
| **NRSV, TEV** | **"pia"** |
| **NJB** | **"kwa namna hiyo"** |

Hili linaonyesha kwamba muktadha ni "namna gani mwanaume na mwanamke wahusike katika ibada ya wazi" (yaani., makanisa ya nyumbani, kama vile 1 Kor. 11-14). Kuna majadiliano mazuri juu ya neno hili katika F. F. Bruce, *Answers to Questions*,kur. 114-115.

◙ **"wanawake wajipambe kwa mavazi ya kusitiri"** Mavazi yanafunua moyo na fikra. Waamini wanapaswa kuvaa vizuri, sio tu wakiwa kanisani bali katika maeneo yote na kwa wakati wote kwa sababu ni Wakristo. Msisitizo wa kifungu hiki sio tu mwonekano wan je, lakini pia juu ya utauwa (kama vile 1 Tim. 2:10; 1 Pet. 3:3,4). Katika kila

eneo la maisha mwamini ni nuru ya ulimwengu na chumvi ya dunia (kama vile Mt. 5:13-16). Lazima tukumbuke ni akina nani tunawawakilisha!
Hata hivyo, hili halimaanishi kuwa waamini lazima wavae nguo mbaya. Tunapaswa kuvaa kana kwamba tuko kwenye jamii yeyote mwamini aishiyo. Uwe msafi, uwe na mwonekano mzuri, lakini katika yote muda wote uwe Mkristo.

◙**"adabu nzuri"** Angalia maelezo kamili katika 1 Tim. 3:2.

◙ **"si kwa kusuka nywele, wala dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani**" Hili linamaanisha kuwa faida la mwamini ilikuwa ni mali. Mtindo wa nywele wa Kiyahudi na Kirumi wa nyakati hizo ulikuwa mgumu, wa uharibifu, na wa aghali. Inavyoonekana wanawake wa Kikristo walikuwa wameingiziwa mafundisho yenye kuendana na ulimwengu au uhuru binafsi (yumkini wakikamatwa kwenye maandamano ya kutafuta uhuru wa mwanamke, ambayo yalianzia katika tamaduni za Kirumi, kama vile 1 Kor. 11:2-16). Hili laweza kuaksi kutokujumuishwa kwa walimu wa uongo waliowachagua wenye mali, watu mashuhuri, na wasomi.

**2:10 "kwa matendo mema"** Waamini lazima wakumbuke kuwa hawakuokolewa kwa kazi nzuri, bali kutenda kazi njema (kama vile Efe. 2:8-10; Tito 3:8; Yakobo 2:14-26). Maisha yetu hutupatia kuaminika kwenye ukiri wetu wa imani, ambao ndiyo madai ya kitabu kizima cha Yakobo na 1 Yohana.

Katika Muktadha huu "matendo mema" linahusiana na matarajio ya kawaida ya tamaduni za kifamilia (kama vile 1 Tim. 5:10; Tito 2:5).

◙**"kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu"** Hili kwa uwazi linazuiya muktadha kwa mwanamke aliyeolewa. Huu sio mwongozo wa pamoja kwa ajili ya jamii. Mavazi yafaayo kwa ajili ya wana wa Mungu ni uchaji Mungu. Urembo sio mavazi fulani, bali ni moyo uliobadilika. Kiukweli wanawake warembo na wa kuvutia ni wanawake wa Kimungu (katika sehemu zote za maisha yetu).

**2:11"mwanamke"** Hili lingaliweza kurejelea kwa wanawake wote wa Kikristo au wake (kama vile tafasiri ya Charles B. Williams, "mwanamke aliyeolewa" katika 1 Tim. 2:11 na). Muktadha lazima uelezee vizuri maana kusudiwa ya mwandishi.

◙ **"akitii kwa kila namna"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Mwanzoni hili lilionekana kuwa kinyume, lakini (1) wanawake hawakusomea sheria kwenye dini ya Kiyahudi au kuhudhuria kwenye shule kwenye ulimwengu wa Wayunani-Warumi. Hivyo, kwa maana hiyo hii ni hatua chanya kuwaelekea wanawake kujifunza neno la Mungu, (2) hili andiko ni lazima litazamwe katika nuru ya waalimu wa uongo ambao walikuwa wakiwawinda wanawake (kama vile 1 Tim. 5:13; Matendo 20:30; 2 Tim. 3:5-9; Tito 1:11). Yawezekana kuwa baadhi ya wanawake walikuwa wananenaji mbadala kwa ajili ya waalimu wa uongo kwenye ibada za hadhara kwenye makanisa ya nyumbani (Gordon Fee, *New International Biblical Commentary*, vol. 13).

◙**"ukitii kwa kila namna"** Hili pia linaonekana kuwa kinyume kwenye siku zetu za leo, lakini tukumbuke

1. Neno "kutii" lilitumika kwa Yesu. Alikuwa mtii kwa Baba yake (kama vile 1 Kor. 15:28); alikuwa mtii vile vile kwa wazazi wake wa kidunia (kama vile1 The. 5:21). Kwa maneno mengine alitimiza kazi zake za kijamii na kidini akionekana vizuri.
2. "kuwa mwenye kutii" ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini (kama vile Efe. 5:21). Ni moja ya kauli tano ZENYE HALI YA KUENDELEA ZA WAKATI ULIOPO ambazo huelezea kile kinachomaanishwa "kujazwa na Roho" (kama vile Efe. 5:18)
3. katika kifungu cha aina ile ile kwenye Waefeso Paulo anatumia mifano mitatu ya kifamilia kuonyesha utii wa kidugu ndani ya familia (1) wanawake kwa waume zao; (2) watoto kwa wazazi wao; na (3) watumwa kwa mabwana zao

   Kiuzingativu sehemu muhimu ya muktadha huu (yaani. Efe. 5:18-6:9) ni kuwa Paulo anaiwekea mipaka nguvu za wale walioko kwenye jamii waliokuwa na nguvu (yaani., waume, wazazi, na mabwana).

Katika siku za leo maandiko ya Paulo kuwahusu wanawake, watoto, na watumwa kimaanani alikuwa sahihi

4. Paulo hakuwakabili watumwa kama suala kbwa kwa sababu alitambua kuwa lilikuwa ni suala ambalo lingaliangamiza mafanikio ya kanisa na ushuhuda wake kwenye kipindi hicho cha historia. Nafikiri hiyo ni kweli kwa nafasi ya mwanamke kwenye jamii. Paulo alitetea usawa wa kiroho (kama vile Gal. 3:28; Kol. 3:11), kukirimiwa kwao (kama vile 1 Kor. 12:7-13), na kazi zao katika kuieneza injili (kama vile Warumi16). Lakini alitambua kuwa wanawake katika shughuli za kiuongozi wangekuwa (1) wangeeleweka vibaya kwa sababu ya ibada za kuzaa matunda na (2) wangekataliwa karibia na wote wazee wa kaya, wanaume waliofahamika kwenye jamii.

**2:12 "ruhusa ya kumtawala mwanaume"** Hiki KITENZI *authenteō* kimetumika mahali hapa tu katika Agano Jipya. Linaelezewa kama "Yule anayetenda kwa mamlaka yake mwenyewe" (*authentēs*, master*)* au "Yule atawalae." Angalia majadiliano katika Moulton and Milligan, *Vocabulary of the Greek Testament*, uk. 91. Hili linamaanisha kuwa wanawake waweza kuwa katika uongozi ikiwa hawatawali? Muktadha wa haraka hauungi mkono hili kwa ongezeko la kifungu "lakini wabaki kimya" (kama vile 1 Kor. 14:34). Maelezo ya Paulo kuhusu wanawake kuwa watii hayawezi kuelezewa kwa utumiaji wa hili *hapax legomenon*. Lazima lishughulike na mtazamo wa kitamaduni. Mungu anachagua kujifunua Mwenyewe ndani ya muundo maalum wa kitamaduni. Kila kitu kwenye utamaduni huo ulikuwa/sio mapenzi ya Mungu kwa ajili waamini wote katika tamaduni zote katika enzi zote (angalia Gordon Fee, *Gospel and Spirit* and *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukur. 83-86). Ukweli na nguvu ya injili moja kwa moja hubadili tamaduni za mwanadamu (yaani. utumwa, mfumo dume). Majivuno, utawala wa kinyonyaji ni uovu haijarishi ni kutoka kwa mwanaume au mwanamke. Kuna mipaka miwili ya kuepuka: (1) wanawake wanaweza kutofanya chochote (tamaduni za Mashariki ya Karibu ya Mbali) na (2) wanawake wanaweza kufanya chochote (nadharia ya ubinafsi wa magharibi ya sasa). Wahudumu wanaoamini (wanaume na wanawake) ndani ya tamaduni zao kuongeza upeo wa uinjilist na kufanyika uanafunzi, na sio hoja binafsi!

## MADA MAALUM:WANAWAKE KATIKA BIBLIA

I. Agano la Kale
   A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye
      1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
      2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
      3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
      4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)
   B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano
      1. Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
      2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
      3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
      4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu 6:1-2)
      5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
      6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
      7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
      8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 25:5-6).
      9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpya (Yoeli 2:28-29)
   C. Wanawake katika dhima ya uongozi
      1. Dada yake Musa, Miriamu, aliitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
      2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya Vibanda(Kutoka 35:25-26)
      3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vile Waamuzi. 4:4), aliyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)

4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "*Book of the Law*" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

II. Agano Jipya

A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenye haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).

B. Wanawake katika dhima ya uongozi

1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhurisha mbele za Mungu (Luka 1-2)
2. Anna, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?

A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?

1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyevuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.
2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenye masharti nay a kihistoria yaliyovuviwa.
   a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
   b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
   c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
      1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
      2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
      3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
      4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
      5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
      6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunuaa kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .

B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linanaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor. 14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile

za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuviwa?!

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1 Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunikwa, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile. Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu maandiko yenye utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa vilivyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeaathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi
   1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
   2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
   3. *Hard Sayings of the Bible by* Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667*)*

**2:13-15** Hoja ya Paulo katika muktadha huu unahusiana kithiolojia na Mwanzo 3. Pia inahusiana kuzidi kwa waalimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 1:3-11; 4:1-5; 5:11-13). Paulo anatumia Mwanzo 3 kufanya ufanano kama Hawa alivyodanganywa na nyoka kuangukia kwenye dhambi, uasi na kuwa na uhuru, hivyo baadhi ya wanawake hudanganywa kwa namna hiyo hiyo na waalimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 5:13; 2 Tim. 3:6-9).

Madhara ya anguko moja kwa moja yanahusiana na utii wa wanawake na shauku kwa ajili ya waume wao (kama vile Mwa. 3:16). Kitendo cha kuwa huru kilikuwa ni suala la kithiolojia. Je hili bado liko hata sasa? Je injili

moja kwa moja imeondoa dhana ya anguko la Mwanzo 3? Je tamaduni zetu za kisasa na wanawake viongozi waliofundishwa wanakanusha maelezo mazuri ya Paulo? Angalia Mada Maalum mwanzoni mwa 1 Tim. 2:12.

**2:14 "akaingia katika hali ya kukosa"** Kuna madhara mawili yaliyotolewa kwa Hawa kwa sababu ya makosa: (1) maumivu kipindi cha kujifungua na (2) kuwa na utii kwa mme wake. NJEO YA KITENZI ni KAULI TIMILIFU, ambayo inamaanisha kuwa hawa bado wako katika athari. Yesu aliianzisha enzi mpya, lakini waamini pia bado wanaishi kwenye enzi ya kale.

**2:15 "ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa"** Hiki ni kifungu kigumu na chenye kuhusika. Yumkini ni moja ya kifungu kigumu kabisa katika maandiko ya Paulo. Tunahitaji kukumbuka

1. uhusiano wake na Mwa. 3:13,16
2. mafundisho ya waalimu wa uongo
3. tofauti (yaani. "lakini"), ambao unahusiana na udanganyifu wa walimu wa uongo

Neno "kuhifadhi" au "kuokolewa" laweza kuhusiana huenda kwenye ukombozi wa kimwili tokana na tukio la kuzaliwa (kama vile toleo la New American Standard Version), ambalo linaonekana kuwezeshwa na utumiaji wa neno katika 1 Tim. 4:16 kwa ajili ya matusi ya waalimu wa uongo (baadhi yao ambao inavyoonekana wanatetea useja kama hali ya juu ya ukiroho, kama vile. 1 Tim. 4:3), au katika maana ya kiroho ya siku ya kiama ambayo hutengeneza zaidi matumizi katika Agano Jipya.

Utafasiri wa riwaya moja unasimamia juu ya maelezo ya sarufi za Kiyunani ambapo KIBAINISHI CHA WAZI ndani ya kifungu "kutokana na kujifungua," yumkini kinarejelea kwenye kufanyika mwili kwa Yesu Kristo:

1. huu muktadha unahusiana na Mwa. 3:15
2. KIHUSISHI *dia* chaweza kutafasiriwa "kwa namna ya"
3. kuna KIBAINISHI CHA WAZI kikiwa na "uzazi"
4. UMOJA na WINGI vimetumika kwa "mwanamke"

Hivyo Hawa akawa mwakilishi wa wanawake wote waliookolewa kwa ahadi ya Mungu ya uzao maalum (yaani., Yesu, ambao kithiolojia unafanana na uainishaji wa Adamu hadi Kristo wa Rum. 5:12-21; 1 Kor. 15:21-22,44-48; Fil. 2:6-7).

Muktadha wa haraka unaonekana kusisitiza kuwa wanawake kama watengenezaji wa mji ni tegemeo la kijamii kwenye kipindi cha Paulo, na kwa ajili ya jamii nyingi, za kale za za sasa. Wokovu wa mwanamke haukutokana na uongozi kwenye ibada za wazi au uhuru wa kitamaduni usiotarajiwa.

Kusema kweli huenda wokovu haukuja toka kwenye jamii iliyotarajiwa, bali ni kutokana na imani na matunda yake (kama vile 1 Tim. 2:15b). Wokovu umo ndani na kupitia Kristo. Wanawake wacha Mungu humwamini na hawahitaji kuwa na usikivu mwingi kwao wenyewe. Hata hivyo, katika tamaduni zetu "usikivu mwingi" hutokea pindi wanawake wanapowekewa mipaka. Kama watu tuliopotea tungaliweza kukatishwa tamaa na wanawake wa Kikristo waliohai kwenye karne ya kwanza, watu waliopotea leo wanakatishwa tamaa hasa na Wakristo wenye ubaguzi wa kijinsia na wenye kushikilia sana sheria. Lengo hasa ni uinjilist na kuwafanya watu kuwa wanafunzi, na sio uhuru binafsi au upendeleo binafsi (kama vile 1 Kor. 9:19-23).

**◙ "kama wakidumu katika imani, na upendo na utakaso na moyo wa kiasi"** Hii ni SENTENSI YENYE MASHARTI DARAJA LA KWANZA yenye kumaanisha kitendo muhimu cha tukio. Tukio ni kuendelea kwa wanawake kuamini katika imani, upendo, utakaso, na kuwa na kiasi. Angalia Mada Maalum: Saburi katika 2 Tim. 2:11.

Kwa ajili ya "kuwa na moyo wa kiasi" angalia maelezo kamili katika 1 Tim. 3:2.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana

1. Ni kwa namna gani ukweli wa kipengele hiki kinahusiana na waalimu wa uongo?

2. Tunahitajika kuwaombea maafisa wa serikali ambao sio Wakristo na wanaotenda pasipo haki na kinyume na njia za Mungu?
3. ni kweli Mungu anataka watu wote wapate kuokolewa? Ni kweli kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu?
4. Elezea maana ya neno"fidia."
5. Kwa nini vazi la Mkristo ni kitu muhimu cha kujadiliwa kwenye ulimwengu wetu wa leo?
6. ni kwa namna gani matendo mema yanahusiana na imani iokoayo?
7. ni ipi sehemu ya mwanamke kwenye kanisa la leo katika kuiangazia mistari ya 11-14?
8. Mstari wa 15 unamaanisha nini katika kuaangazia mafundisho yaliyobaki ya Agano Jipya?

# 1 TIMOTHEO 3

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Sifa za Maaskofu | Sifa za Wasimamizi | Matatizo ya Utawala | Viongozi katika Kanisa | Wazee katika Wajibu wao |
| 3:1b-7 | 3:1-7 | 3:1-7 | 3:1-7 | 3:1-7 |
| Sifa za Mashemasi | Sifa za Mashemasi | | Wasaidizi katika Kanisa | Mashemasi |
| 3:8-13 | 3:8-13 | 3:8-13 | 3:8-13 | 3:-13 |
| Siri za Dini yetu | Siri Kuu | | Siri Kuu | Kanisa na Siri ya Maisha yaliyotangulia |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura hii inaorodhesha aina mbali mbali za wahudumu.
    1. wachungaji (1 Tim. 3:1-7)
    2. mashemasi (1 Tim. 3:8-10,12-13)
    3. kazi za wajane (1 Tim. 3:11; 5:9-16) au shemasi wa kike (kama vile Rum. 16:1)

B. Vigezo hivi vinaweza kuwa katia utofauti wa moja kwa moja naaisha ya walimu wa uongo mafundisho.

C. Mstari wa 16 ni usemi wa kanuni za imani za awali au wimbo. Mara nyingi Pauloaliiunganisha aina hizi ya nyenzo (kama vile Efe. 5:19; Flp. 2:6-11; Kol. 1:15-16; 3:15-20; 2 Tim. 2:11-13). Muundo wa kiumbaji ni unaonekana dhahiri katika VITENZI VYA KAULI SITA TENDWAJI ELEKEZI ZA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU zilizounganishwa na UHUSIKA WA MAHALI au KISAIDIZI vifungu vya kisarufi.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 3:1-7**
**[1]Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. [2] Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; [3]si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; [4] mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; [5](yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?) [6] Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. [7] Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi.**

**3:1 "Ni neno la kuaminiwa"** Nahau hii inaweza kutenda kazi kama usemi wenye kuhitimisha na usemi wa ufunguzi (kama vile 1 Tim. 1:15; 3:1; 4:9; 2 Tim. 2:11; Tito 3:8). Hii ni ya pili miongoni mwa semi tano za "matumaini" katika Nyaraka za Kichungaji. Hizi zinafanya kazi kisarufi kama yalivyo matumizi ya Yesu ya utangulizi "amina" au "amina, amina" (inayotafsriwa kama "amini, amini" au "hakika, hakika"), wakiwasikiliza.

◙ **"mtu akitaka"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DALAJA LA KWANZA inayoonekana kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa makusudi yake ya kiuandishi.

◙ **"akitaka. . . atamani"** Haya ni maneno mawili yenye nguvu: (1) "chukua" (kama vile 1 Tim. 6:10; Ebr. 11:16) na (2) "huudhihirisha moyo wake" (kama vile Mt. 13:17; Luka 15:16). Kifungu hiki kinaniambia kwamba msisitizo wetu wa sasa ulio juu ya umuhimu wa aina ya wito wa Agano la Kale utokao kwa Mungu hadi kwa huduma yenyewe unaweza kuwa na mipaka sana. Shauku ya kuwa katika uongozi wa kanisa inajitosheleza. Shauku ya mioyo ya waamini inatoka kwa Bwana (kama vile Zab. 37:4).

**NASB " kazi ya askofu"**
**NKJV "nafasi ya askofu"**
**NRSV "kazi ya askofu"**
**TEV "kiongozi wa kanisa"**
**NJB "mzee atawalaye"**

Hili neno *episkopos*, na mara nyingi mi maneno yanayotafsriwa katika lugha ya Kiingereza "askofu" au "msimamizi." Hili linaonekana kiwa kisawe na maneno mengine ya mawili ya Agano Jipya yenye kuzungumzia kazi ya uongozi ndani ya kanisa. Haya maneno "mchungaji" "msimamizi," na "mzee" yote yanairejelea kazi moja (kama vile 1 Tim. 5:17; Matendo 20:17,28; Tito 1:5,7; 1 Pet. 5:1-2). Kanisa la Agano Jipya lina kazi mbili pekee: mchungaji na shemasi (kama vile Flp. 1:1). Inaonekana kwamba "mzee" alikuwa na historia ya Kiyahudi, ambapo "askofu" alikuwa na historia ya kuutawala mji.

**3:2 "asiyelaumika"** Hii ni sifa ya msingi ya muktadha mzima wa uongozi katika kanisa. Kifungu hiki kinamaanisha kuwa pasiwepo ukosoaji, kwa namna zote katika jamii ya waaminio (1 Tim. 3:2-6) na katika jamii ya wasio amini (1 Tim. 3:7). Dhima hii hii ya kutolaumiwa inarudiwa katika mistari 7,10; 5:7;na 6:14. Hakuna viongozi waliokamilika, bali kuna wacha Mungu, wenye kuheshimiwa, waamini wanokubalika. Tazama maelezo katika Tito 1:6.

**NASB, NKJV**
**NJB "mume wa mke mmoja"**
**NRSV "aliyeoa mke mmoja tu"**
**TEV "yampasa kuwa na mke mmoja tu"**

Kifungu hiki kimesababisha mjadala mwingi sana. Hili lilikuwa jambo dhahiri kwa kanisa huko Efeso katika karne ya kwanza (kama vile 1 Tim. 3:1,12; 5:7; na katika Krete, Tito 1:6). Hapa kuna nadharia za msingi zenye kutafsiriwa.

1. hii inarejelea ndoa za mitala

2. hii inarejelea ndoa baada ya talaka
3. hii inarejelea ndo ya mara ya pili baada ya kifo cha mke wa kwanza
4. hii inamrejelea mtu aliye mwaminifu na mwenye kumjali mkewe (njia nyingine ya kudai juu ya uhusiani mwema wa familia, kama vile. NEB)

Kwa namna iliyo dhahiri kifungu hiki kinayarejelea mahusiano ya familiya, na tatizo liwezalo kuzuka katika eneo la mahusiano ya familia na mtu kukosa sifa katika kanisa mama. Namba 1 haikuwa tatizo katika Dola ya Kirumi, bali ilikuwa na uwezekano wa kuwa tatizo katika Dini ya Kiyahudi (japo ilikuwa adimu katika karne ya kwanza); #2 ilikuwa tatizo kubwa katika Dola ya Kirumi, na pia ilikuwa tatizo katika dini ya Kiyahudi (Hillel dhidi ya Shammai); #3 ilikuwa hofu kuu katika kanisa la Mwanzo, hasa Tertullian, bado ni jambo gumu katika mzunguko wa ubatizo huko Ulaya. Hata hivyo, 1 Tim. 5:14 ni kifungu chenye kufanana ambapo wajane vijana wanaweza kuolewa tena pasipo kulaumiwa (kama vile Rum. 7:2-3; 1 Wakorintho 7).

Kuna uchaguzi zaidi, kwamba hitaji linairejelea ndoa dhidi ya useja. Walimu wa uongo walikuwa wakizuia ndoa (kama vile 1 Tim. 4:3). Hili linaweza kuwa kanusho la moja kwa moja la uelekeo wao wa ujane na kujinyima. Jambo hili halidai kwamba mtu asiye olewa hawezi kuwa kiongozi wa kanisa, bali ya kwamba useja hauwezi kuwa hitaji. Nafikiri huu ni mchaguzi bora zaidi nay a kwamba ni majibu ya matatizo yenye kutafsirika yenye kuhusiana na (1) "kutojikita katika ulevi" na (2) suala la wanawake katika 1 Tim. 2:8-15. Mambo haya lazima yatafsiriwe katika kuwamulika walimu wa uongo.

Ikiwa suala hili lina nguvu, nyumba ya wacha Mungu, talaka siyo suala <u>la</u> kiumakini pekee. Hata katika Agano la Kale taraka wakati mwingine suala la taraka lilikuwa uchaguzi sahihi: (1) YHWH analitarakisha taifa la Israeli lisilo aminifu na (2) makuhani walilazimishwa kuwatalakisha wake wasio waaminifu (tazama *Old Testament Perspective on Divorce and Remarriage* katika *Journal of the Evangelical Theological Society* Juzuu 40 #4, Des. 1997). Wanadamu wote wanakumbana na misukuosuko katika maisha ya nyumba zao katika maeneo fulani. Hofu kuu ni namna wanavyochukuliana na sifa hii kwa ugumu kiuhalisia ni uhaba wa uchaguzi katika mambo mengine katika muktadha huu kimaandishi pia. Ikiwa taraka huleta sifa fanya hivyo (a) kutojikita katika ulevi (kama vile "si. . .kujikita katika ulevi" kifungu cha 1 Tim. 3:8, ambacho si agizo la moja kwa moja kujinyima) na (b) "kuwalea watoto wake" kifungu cha 1 Tim. 3:4, ambacho kinawakosesha sifa wachungaji na mashemasi.

Kwa namna ya uaminifu, siwajui viongozi wengi wa Kikristo ambao kwa wakatai mwingine hukamilisha mahitaji haya katika maisha yao. Hivyo kabla ya kuwa na umakini sana wa dosari za uhusiano wa kukumbuka kuwa sifa hizi ni mapenzi ya Mungu kwa <u>wote</u>. Sitetei kushushwa kwa viwango vya utumishi, bali navitumia kama sehemu ya sheria, kwa maana ya hukumu. Kanisa linawahitaji wacha-Mungu, uongozi unaokubalika kijamii. Hata hivyo yatupasa wote kufanya uchaguzi kutokana na watenda dhambi walio chaguliwa! Makanisa ya sasa lazima yawatafute viongozi waliojihakikisha wao wenyewe kuwa waaminifu kwa wakati wote, na si viongozi wakamilifu.

Hoja moja zaidi ya zote, ikiwa orodha hii inachukuliwa kimaandiko, na sasa Yesu (kwa sababu alikuwa pekee) na Paulo (kwa sababu huenda alikuwa ametarakishwa) asingekuwa na viongozi wa kanisa. Mfanye mtu afikiri, sivyo ilivyo?

◙ **"mwenye kiasi"** Kiuhalisia "kuwa na utaratibu." Kwa sababu matumizi ya kilevi yanatajwa kwa upekee katika 1 Tim. 3:3, huenda kifungu hiki kinayarejelea matumizi ya kisitiari ya neno lenye kumaanisha "kuwa makini" (kama vile. 1 Tim. 3:11; Tito 2:2).

**NASB "mwenye kiasi"**
**NKJV "mwenye akili tulivu"**
**NRSV "mwenye akili"**
**TEV "wenye kujitawala"**
**NJB "makini"**

Neno hili *sōphrōn* linamanisha "kuwekuwa ulinganifu" katika mawazo wa wanafalsafa ya Kiyunani. Hili ni neno la Kiyunani lililofahamika sana ambalo lilidokeza juu ya kuepuka vitu vyenye kuzidi kipimo (yaani., kwa utetezi "maana sawa"). Hili lilitumika kwa mtu kutoa sauti yenye maana fulani (kama vile 1 Tim. 3:2; Tito 1:8; 2:2,5). Maneno yenye kuhusiana pia yanapatikana katika 1 Tim. 2:9,15; 2 Tim. 1:7; Tito 2:4,6,9,12,15.

Asili ya msingi (BAGD, uk. 802) inapatikana katika miundo kadhaa iliyo katika nyaraka za kichungaji.
KITENZI, *sōphroneō* – "kiasi," Tito 2:6
KITENZI, *sōphronizō* – "wawatie" (yaani., kumweka mtu katika umakini), Tito 2:4
NOMINO, *sōphronismos* – "wanafunzi" (yaani, kujitawala), 2 Tim. 1:7
NOMINO, *sōphrosunē* – "watiifu," 1 Tim. 2:9,15
KIELEZI, *sōphronōs* – "akili" (yaani., kwa makusudi, Tito 2:12
KIVUMISHI, *sōphrōn* – "ufahamu," "mwenye hekima," "yenye kufikirika," 1 Tim. 3:2; Tito 1:8; 2:2,5

**NASB, NRSV "mkaribishaji"**
**NKJV "wa tabia njema"**
**TEV "wa utaratibu"**
**NJB "mpole"**

Huu ni muundo wa neno la Kiyunani *kosmikos*. Huu unatumika katika Tito katika maana mbili: (1) kwa ukanushi wa kuepuka tama za kiulimwengu (2:12) na (2) na kwa namna ya uyakinifu ya mpangilio sahihi (2:10). Katika 1 Timotheo muktadha huu unamaanisha mpangilio mzuri au ushihi. Kile kilicho sahihi, chenye kuheshimiwa, na chenye kutegemewa na jamii ya nahali pale. Kwa hiyo, hiki ni kipengele cha 1 Tim. 3:7a, "yanipasa kuwa na sifa njema kwa wale walio nje ya *kanisa*."

◙ **"mkaribishaji"** Nyumba za kulala wageni za siku za Paulo zilikuwa maarufu sana kwa kazi ya ukahaba. Hivyo, Wakristo, na hasa viongozi wa Kikristo, iliwapasa kuziweka nyumba zao huru kwa ajili ya kutembelewa na wamisionari na mahitaji mengine ya jamii (kama vile 1 Tim. 5:10; Tito 1:8; Rum. 12:13; Ebr. 13:2; 1 Pet. 4:9; 2 Yohana 5; na 3 Yohana).

◙**"ajuaye kufundisha"** Yawapasa viongozi kuwa walimu wenye uwezo (kama vile 2 Tim. 2:24). Inatia shauku kwamba "kufundisha" kunaorodheshwa kama karama iliyojitenga katika 1 Kor. 12:28, lakini tendo lenye kuunganishwa na karama ya uchungaji katika Efe. 4:11. Kwa namna iliyo dhahiri kulikuwana na walimu, lakini pia wachungaji wote iliwapasa kuwa na uwezo wa kutenda kazi katika eneo hili, vivyo hivyo. Katika maana hii watu wote waliokirimiwa katika Waefeso 4 ni wahubiri wa injili, lakini katika maana tofauti na katika nikazo tofauti.

Baadhi ya wasoni wa kibiblia wanaifasiri sifa hii kama rejea la wale waliofundishwa au kuwaelimisha watu, au wale wenye "kufundishika"!

Mwisho, uwezo huu wa kufundisha unaweza kuhusiana walimu wa uongo wa Sheria (kama vile 1 Tim. 1:7) lakini ni wadanganyifu.

**3:3**
**NASB "si mtu wa kuzoelea ulevi"**
**NKJV "asiyetawaliwa na ulevi"**
**NRSV "asiye mlevi"**
**TEV "hapaswi kuwa mlevi"**
**NJB "asiye lewa sana"**

Inaonekana kuwa dokezo lenye kutokana na Agano la Kale la Kiebrania na Mith. 23:29-35. Lazima isisitizwe tena kuwa Biblia inaweka vikwazo dhidi ya ulevi, lakini haifundishi juu ya kujinyima kwa moja kwa moja (kama vile 1 Tim. 3:8; 5:23; Tito 1:7; 2:3). Kujinyima moja kwa moja kunatokana na kujitoa binafsi kwa waamini kwa Bwana Yesu kwa kujikita katika kuweka mipaka ya uhuru wa mwanadamu kwa sababu ya utamaduni katika eneo

wanalolihudumia (kama vile Rum. 14:1-15:13 na 1 Wakorintho 8-10). Kwa mjadala ulio mzuri zaidi tazama makala *Hard Sayings of the Bible* na Kaiser, Davids, Bruce, na Branch, kr. 673-674.

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA KUHUSIANA NA KILEVI NA MATUMIZI MABAYA YA KILEVI

I. Maneno ya Kibiblia

A. Agano la Kale
1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hiii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
2. *Tirosh* – Hiii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya," BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi huu unaongezwa katika ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

B. Agano Jipya
1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
2. *Neos oinos* (divai mpya) – neno linalofanana la Kiyunani sawa na tirosh (kama vile Marko 2:22).
3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, *asis)* – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

II. Matumizi ya Kibiblia

A. Agano la Kale
1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
2. Divai ni swehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
3. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2; Mit. 31:6-7).
4. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnoni– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amosi 4).
5. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
6. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mith. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
7. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).
   1. Kipindi cha uwazi kati ya Agano laKale na Agano Jipya
   2. Divai katika upatanisho ina msaada (Muhubiri 31:27-33).
   3. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa yalevyayo yanahitajika." (BB 58b).

C. Agano Jipya

1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji katika divai (Yohana 2:1-11).
2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima molja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
7. Divai ililaaniwa (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

III. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi
   1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
   2. Ulevi ni tatizo kubwa.
   3. Waamini katika baadhi ta tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).
B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka
   1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote.
      a. chakula– Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
      b. mambo yote yasiyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
      c. mambo yote ya halali – 1 Kor. 6:12; 10:23
      d. mambo yote yaliyo safi– Tito 1:15
   2. Mwanadamu aliyeanguka ametumia vibaya zawadi ya Mungu kwa kuzitumia nje ya mipaka ya Mungu aliyoitoa.
C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uumbaji wa vitu vinanyoonekana (tazama B. 1. Hapo juu).

IV. Utamaduni wa Karne ya kwanza ya Kiyahudi na Chachu

A. Chachu hunza ndani ya muda mfupi, takribani ndani ya masaa 6 baada ya barungi kusagwa
B. Desturi ya Kiyahudi inasema kwamba povu linapoonekana juu yake (dalili ya uchachu), hii huelekea kuwa sehemu ya divai iliyo na uchachu (Ma aseroth 1:7). Hiii iliitwa "divai mpya" au "divai tamu."
C. Chachu ya kwanza iliyo kali uilikamilishwa baada ya juma moja.
D. Chachu ya pili ilichukuwa sku zipatazo 40. Katika hatua hii tendo hili lilifikiriwa kama "divai kukuu" na ingweza kutolewa madhabahuni (Edhuyyoth 6:1).
E. Divai ambayo iliyobakizwa ndani ya machicha (divai kongwe) ilifikiriwa kuwa nzuri, lakini ilitakiwa kuchujwa vizuri kabla ya kutumiwa.
F. Divai ilifikiriwa kuwa kuukuu kwa usahihi baada ya kutunzwa vema kwa ajili ya kuchachushwa. Miaka mitatu kilikuwa kipindi cha muda mrefu ambapo divai ingetunzwa kwa usalama. Hii iliitwa "divai kuuku" na ilitakiwa kuchanganywa na maji.
G. Ni katika miaka 100 ya mwisho pekee ya ukame wa mazingira na ongezeko la madawa uchachu umetoweka. Ulimwengu wa kale usingeweza kustisha tendo la asili la kuchachusha.

V. Maelezo ya Kiufungaji

A. Hakikisha uzoefu wako, thiolojia, na fasiri ya kibiblia havimkashifu Yesu na ile karne ya kwanza ya Kiyahudi/Utamaduni wa ki- Kristo! Hawa kwa uwazi hawakujinyima moja kwa moja.
B. Mimi sitetei matumizi haya ya kilevi kwa jamii. Hata hivyo, wengi huchochea nafasi ya Biblia juu ya somo hili na sasa wanadai keki kuu iliyojikita katika utamaduni/ubaguzi wa kimadhehebu.
C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 zimetoa utambuzi na mwongozo uliojikita katika

upendo na heshima kwa waamini wenzetu na kuieneza injili ndani ya utamaduni wetu, si uhuru binafsi au ukosoaji wa hukumu. Ikiwa Biblia ni chanzo pekee cha imani na matendo, bila shaka yatupasa wote kufikiria upya juu ya jambo hili.

Ikiwa tunahimiza kujinyima moja kwa moja kama mapenzi ya Mungu, nini tunachokimaanisha juu ya Yesu, pamoja na zile tamaduni za sasa ambazo kwa hali ya mazoea hutumia divai (m.f. Ulaya, Israeli, Argentina).

◙**"si mpiga watu"** Kiuhalisia hili "si neno mpinzani" (kama vile Tito 1:7). Hili linawza kuhusiana na matumizi ya kilevi kama yenye kuharibu mahusiano binafsi (yaani., familia, kanisa la nyumbani, walimu wa uongo).

◙ **"awe mpole"** Kipengele hiki kinarejelea juu ya upendo wa mantiki, ambao unaandaliwa kwa ajili ya kufaidiwa na wengine (kama vile Efe. 5:21). Huu unaeleza juu ya wema, mtu mpole (kama vile Tito 3:2; Yakobo 3:17; 1 Pet. 2:18).

◙ **"si mtu wa kujadiliana"** Hili ni neno la Kiyunani lenye kumaanisha kupigana, mapambano, mgogoro, lakini lenye KIAMBATA HASI, yenye kukanusha maana. Hivyo, hii inamanisha yule yule asiyepigana au kuchochea machafuko (kama vile Tito 3:2). Ni rahisi kuona namna walimu wa uongo kifasihi walivyo walivyo wavurugaji katika sura ya 3 (na katika Nyaraka zote za Kichungaji).

**NASB "asiwe mwenye kupenda fedha"**
**NKJV "asiye na tamaa ya fedha"**
**NRSV "asiyependa fedha"**
**TEV "asiwe mpenda fedha"**
**NJB "asiwe mlafi wa mali"**

Hili ni neno ambatani lililotokana na neno "rangi ya fedha inayong'aa" na neno "upendo wa kindugu" lenye KIAMBISHI AWALI HASI ambacho ni sawa na "kutokupenda fedha" (kama vile 1 Tim. 6:6-10; Tito 1:7; Ebr. 13:5; 1 Pet. 5:2). Hii ni sifa nyingine ya waimu wa uongo. Tazama MADA MAALUM : WINGI WA MALI katika 1 Tim. 6:8.

**3:4-5 "mwenye kuisimamia nyumba yake vema"** Uongozi unaweza kuonekana kuanzia nyumbani. Jambo lo lote lililo gumu kati ya mume na mke au watoto na mababu zao au wakwe zao lilikuwa msingi wa kupoteza sifa katika utratibu wa kanisa hili la mwanzo. "Hakuna usimamizi wa matatizo" ndiyo hoja kuu. Ni kwa namna gani ataitawala nyumba yake na kuonyesha katika kuliongoza ya kanisa (kama vile 1 Tim. 3:5, swali la lililotengwa linatarajia jibu la "hapana"). Laulaa! Jambo hili lingewakosesha sifa wahudumu wengi wa sasa kama litachukuliwa kiuhalisia na kwa mujibu wa waraka. Sifa nyingi zilizo yakini pamoja sifa bainishi kanushi zilizotajwa katika 1 Tim. 3:2-3 yanafunuliwa katika mazingira ya myubani. "Ichunguze nyumba yako kwanza" ni ushauri nzuri kwa kamaai ya watendaji!

**3:5 "asiyejua"**Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DALAJA LA KWANZA yenye kudhaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au makusudi yake ya kiuandishi.

◙ **"Kanisa"**

## MADA MAALUM: KANISA (*EKKLESIA)*

Neno hili la Kiyunana, *ekklesia*, linatokana na maneno mawili, "nje ya"na "kuitwa." Neno hili linatumika kidunia (yaani., jamii iliyoitwa kwenye kikao, k.v Mdo. 19:32,39,41) na kwa sababu ya utumiaji wa maandiko ya kale ya Kiyunani ya neno hili kwa ajili ya "kusanyiko" la Israel (*Qahal,* BDB 874, KB 1078, k.v. Hes. 16:3; 20:4; Kumb. 31:30),na matumizi ya kidini. Kanisa la mwanzo walijiona wao kama mwendelezo wa Agano la Kale la watu wa Mungu. Walikuwa Waisrael wapya (k.v. Rum. 2:28-29; Gal. 3:29; 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6),

utimilizo wa kusudi la Mungu kidunia (k.v. Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH

Neno lililotumika kwa maana nyingi katika injili na matendo.

1. Mikusanyiko ya kidunia, Mdo. 19:32,39,41
2. Watu wa Mungu ulimwenguni katika Kristo, Mt. 16:18 na Waefeso
3. Kusanyiko la waumini wa mahali katika Kristo, Mt. 18:17; Mdo. 5:11 (katika aya hii, ni kanisa huko Yerusalem); Mdo. 13:1; Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; Filemoni uk. 2
4. Watu wa Israeli kwa ujumla, Mdo. 7:38, katika hotuba ya Stephano
5. Watu wa Mungu kwenye Miji, Mdo. 8:3; Gal. 1:2 (Yuda au Palestina)

Kanisa ni watu waliokusanyika, na sio jengo. Hapakuwepo na majengo ya kanisa kwa muda wa miaka mingi. Katika Yakobo (moja ya kitabu cha mwanzoni kabisa cha Wakristo) kanisa lilitajwa kwa neno "*synagōgē*" (kusanyiko). Neno kanisa limetokea tu kwa Yakobo (k.v. Yakobo 2:2; 5:14).

**3:6 "asiwe mtu aliyeongoka karibu"** Katika kitabu cha Tito hili limeachwa. 1 Timotheo aliandikwa ajili ya Efeso, ambayo ilikuwa imeliimarisha kanisa, abapo Tito iliandikwa kwa ajili ya Krete, ambapo hii ilikuwa kazi mpya. Hawa wote walikuwa waongofu wapya. Asili halisi ya neno hili llililotumika hapa inamaanisha "mmea mchanga." Hata hivyo, sababu iliyokuwa imekusudiwa kwa wakati huo haijulinani.

◙ **"asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi"** Majivuo ndilo lililokuwa tatizo kubwa kwa malaika na wanadamu (kama vile 1 Tim. 6:4; 2 Tim. 3:4). Hiki KITENZI (KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU) kinamaanisha "kufunikwa kwa moshi" Hiki KIMILIKISHI " cha neno Ibilsi" kinaweza kurejelea

1. hukumu inayosababishwa na Ibilisi (kama vile 1 Tim. 3:7)
2. aina hii hii ya hukumu aliyoipokea Ibilisi (kama vile NKJV, TEV, NJB)

Paulo anawataja maadui wa kiroho wa mwanadamu mara kadhaa katika 1 Timotheo (lakini si katika 2 Timotheo Tito):

1. Ibilisi (*diabolos,* 1 Tim. 3:6,7)
2. Shetani (*Santanas,* 1 Tim. 1:20; 5:20)
3. Pepo wachafu (*daimonion,* 1 Tim. 4:1)

Mtazamo wa kibiblia wa kiulimwengu ambao mwanadamu wenye kuonnyesha upinzani wa kiroho kwa mwanadamu (kama vile Efe. 2:2; 6:10-19) unaofumuliwa katika vitabu vyote Agano la Kale na Agano Jipya.

## MADA MAALUM: SHETANI

Hili suala gumu sana kutokana na sababu kadhaa.

1. Kitabu cha Agano la Kale hakimfunui adui mkuu apingaye mema, bali mtumishi wa YHWH (angaliA. B. Davidson, *OT Theology,* kr. 300-306), ambaye anampa mwanadamu uchaguzi wa bure na pia kumlaumu mwanadamu juu ya kutokuwa kwake mwenye haki. Kuna Mungu mmoja pekee (angalia Mada Maalum: Mungu aliye mmoja, uweza wa aina moja, sababu moja iliyo ndani ya Agano la Kale—YHWH (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6).
2. Hii dhana ya huyu adui mkuu wa Mungu wa kipekee ilikuwa katika kipindi cha ukimya wa fasihi ya Agano la Kale na Agano Jipya (pasipo sheria za kikanisa) chini ya ushawishi wa pande mbili za dini za Kiajemi (Dhana ya Zoroaster). Hii, katika kurudia, kwa kiwango kikubwa hizi ziliwashawishi viongozi wa dini za Kiyahudi na jamii ya Essene (yaani, Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi).
3. Kitabu cha Agano Jipya kiliikuza dhana ya Agano la Kale katika namna yaugumu wa kushangaza, lakini wa kipekee, wa aina nyingi.

Ikiwa moja ya mitazamo ya somo la uovu kutokana na kipengele cha theolojia ya kibiblia (kila kitabu au mwandishi au aina ya somo lililofundishwa na maelezo ya kimuhtasari yaliotengwa), tena ni mawazo tofauti sana ya uovu unaofunuliwa. Ikiwa, kwa vyo vyote, moja ya mitazamo ya somo la uovu kutoka mtazamo usio

wa kibiblia au mtazamo wa ziada wa kibiblia wa dini za ulimwengu au dini za mashariki, tena maendeleo mengi ya kitabu cha Aagano Jipya yanatabiriwa katika ule uwili wa Kiajemi na ukiroho wa utawala wa Wagiriki-Waroma.

Ikiwa wazo la awali lilijikita juu ya Andiko la mamlaka ya Kiungu (kama Mimi Niko!), kasha ukuaji wa kitabu cha Agano Jipya lazima uonekane kama ufunuo endelevu. Yawapasa Wakristo kujilinda dhidi ya kuyaruhusu mafunzo ya mila na desturi za Kiyahudi au fasihi ya mashariki (Dante, Milton) kwa ajili ya ushawishi wa dhana ya baadaye. Kuna siri fulani na utata katika eneo hili la ufunuo. Mungu amechagua kutovifunua vipengele vyote vya uovu, chimbuko lake (angalia Mada Maalum: Lusfa), uendelevu wake, sababu yake, lakini Yeye amelifunua ondoleo lake!

Katika neno la Agano la Kale "shetani" au "mshtaki" (BDB 966, KB 1317) anaweza kuhusiana na makundi matatu taliyojitenga.

1. washtaki wa mwanadamu (kama vile 1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 11:14,23,25; Zab. 109:6)
2. washtaki wa kimalaika (kama vile Hes. 22:22-23; Ayubu 1-2; Zek. 3:1)
3. washtaki wa kimapepo (kama vile 1 Nyak. 21:1; 1 Fal. 22:21; Zek. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha ukimya wa Agano la Kale na Agano Jipya tu ndipo yule nyoka wa Mwanzo 3 alipotambujlishwa kama Shetani (kama vile Book of Wisdom 2.23-24; II Enoch 31:3), na baadaye hili lilikuja kuwa uchaguzi wa sheria za Kiyahudi( *Sot* 9b na *Sanh*. 29a). Wale "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 walikuja kuwa malaika katika I Enoch 54:6. Nalitaja hili, si usahihi wa kitheolojia, bali hili linaonyesha maendeleo yake. Katika Kitabu cha Agano Jipya kazi hizi linapewa kundi la kimalaika, uovu wa kibinadamu (kama vile 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9). Chimbuko la uovu wa kibinadamu ni gumu au haliwezekani (linategemeana na hoja ya mtazamo wako) kuibainisha kutokana na kitabu cha Agano la Kale. Moja ya sababu ya hili ni kuwepo kwa Mungu wa Israeli Aliye mmoja (angalia Mada Maalum: Mungu Aliye Mmoja; pia nukuu 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Usababishi wote (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6) alikpewa YHWH ili kuonyesha upekee na ubora Wake (kama vile Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Chimbuko la uhakika wa habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo Shetani ni mmoja wa "wana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14 na Ezekieli 28, ambapo wafalme wenye majivuno waliokuwa karibu na mashariki (Babeli na Tiro) kwa hakika wanatumika kueleza juu ya majivuno ya Shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganywa kihisia kuhusu mtazamo huu. Ezekieli anatumia stiari za Bustani ya Edeni, si kwa mfalme wa Tiro pekee kama Shetani (kama vile Eze. 28:12-16), bali pia kwa mfalme wa Misri kama Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa mist. ya. 12-14, anaonekana kuufafanua uasi wa kimalaika kupitia majivuno. Ikiwa Mungu alitaka kuifunua kwetuj ile asili ya kipekee na chimbuko la Shetani, hii ni njia isiyo wazi na ni sehemu ya kulifanya hili. Yatupasa kujilinda dhidi ya uelekeo wa theolojia ya mfululizo wa kuchukulia mambo madogo madogo, sehemu za utata wa semi mbalimbali, waandishi, vitabu, aina na kuziunganisha kama vipande vya mafumbo ya Uungu.

Nakubaliana na Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, viambaisho XIII [kr. 748-763] na XVI [kr.770-776]) kwamba Sheria za Dini ya Kiyahudi kwa kiasi kikubwa zimepewa ushawishi na zile pande mbili za Kiajemi na kisiko la kimapepo. Hawa Walimu wa sheria za Kikyahudi si chimbuko zuri la ukweli ndani ya eneo hili. Kimsingi Yesu anaachana na mafundisho ya Masinagogi ndani ya eneo hili. Nafikiri kwamba ile dhana ya adui wa YHWH aliyekuwa katika umbo la kimalaika iliendelezwa kutokana na miungu mikuu miwili ya pande mbili za ki-Irani, *Ahkiman* na *Ormaza*, ambapo iliendelezwa tena na Walimu wa Sheria katika pande mbili za YHWH na Shetani.

Kuna uhakika wa ufunuo endelevu katika kitabu cha Agano Jipya kama sifa ya, lakini si kama wanavyoeleza Walimu wa Sheria za Kiyahudi. M fano mzuri wa utofauti huu ni "vita ya mbinguni." Anguko la Shetani kimantiki lina umuhimu, lakini ubatana haokutolewa (angalia Mada Maalum: Anguko la Shetani na Malaika

Zake). Hata kile kilichotolewa kinafunikwa katika aina ya ukiyama (kama vile Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa Shetani anaondolea kwa Yesu na kutupwa duniani, bado anafanya kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Katika eneo hili yatupasa kuzuia uchunguzi. Kuna nguvu binafsi ya ushawishi na uovo, lakini bado kuna Mungu mmoja pekee na bado tunawajibika kwa ajili ya chaguzi zetu. Kuna mapambano ya kiroho, wakati wote kabla na baada ya wokovu. Ushindi unaweza kuja tu na kubaki pale pale kupitia Mungu wa Utatu. Uovu emeshindwa na utaondoshwa kama vile Ufu. 20:10)!

**3:7 "imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje"** Uongozi lazima utazamwe kama eneo la uaminifu na udhahiri kwa jamii isiyoamini ambayo kanisa linajaribu kulipatia imani katika Kristo (5:14; 6:1; Tito 2:5,6,10; 1 Kor. 10:32; Kol. 4:5; 1 The. 4:12).

## MADA MAALUM : KUHUKUMU (JE! YAWAPASA WAKRISTO KUHUKUMIANA?)

Hukumu ni hakika (kama vile Mt. 12:36; Ebr. 9:27; 10:27; 2 Pet. 2:4,9; 3:7).

A. Yeye anayehukumu ni
   1. Mungu (kama vile Rum. 2:2-3; 14:10,12; 1 Pet. 1:17; 2:23; Ufu. 20:11-15)
   2. Kristo (kama vile Yohana 9:39; Mt. 16:27; 25:31-46; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1)
   3. Baba kupitia Mwana (kama vile Yohana 5:22-27; Mdo. 17:31; Rum. 2:16)

Hukumu sio somo zuri, lakini ni maudhui ya sasa katika Biblia. Imejikita katika misingi au miamba za kweli kibiblia.

1. Huu ni ulimwengu wa kimaadili ulioumbwa na Mungu mwadilifu (tunavuna tunachopanda, kama vile Gal. 6:7).
2. Uanadamu umeanguka; tumeasi.
3. Huu si ulimwengu ambao Mungu alikusudia uwepo.
4. Uumbwaji wote unaojielewa (malaika na wanadamu) tutatoa hesabu kwa muumbaji wao kwa zawadi ya uzima. Sisi ni mawakili.
5. Milele itaamuliwa kwa kudumu na matendo yetu na chaguzi tulizozifanya katika haya maisha.

B. Je Wakristo wahukumiane wao kwa wao? Jambo hili lazima lishughulikiwe katika namna mbili.
   1. waamini wanaonywa wasije wakahukumiana wao kwa wao (kama vile Mt. 7:1-5; Luka 6:37,42; Rum. 2:1-11; Yakobo 4:11-12)
   2. waamini waanaonywa kuwatathmini viongozi wao (kama vile Mt. 7:6,15-16; 1 Kor. 14:29; 1 The. 5:21; 1 Tim. 3:1-13; na 1 Yohana 4:1-6)

Baadhi ya vigezo kwa ajili ya tathmini sahihi inaweza kusaidia

1. tathmini lazima iwe kwa kusudi la kukiri (kama vile 1 Yohana 4:1 – "jaribu" ikiwa na mtizamo wa kuthibitisha; angalia Mada Maalum: Kujaribiwa [*peirazō* na *dokimazō*])
2. tathmini lazima ifanyike katika upole na unyenyekevu (kama vile Gal. 6:1)
3. tathmini lazima iweke shabaha kwenye upendeleo wa mambo ya kibinafsi (kama vile Rum. 14:1-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33)
4. tathmini lazima itambue wale viongozi walio na "sio weza kuvumilia kukosolewa" kutoka ndani ya kanisa au katika jamii (kama vile 1 Timotheo 3).

◙**"ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi"** Paulo alikuwa akizungunzia vita ya kiroho (kama vile 1 Tim. 6:9-10; Efe. 2:1-3; 4:14; 6:10-19). Wema ni ngao, lakini ubinafsi humfungulia mlango Ibilisi kufanya kutendakazi!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 3:8-13**
**8 Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana,si watu wanaotamani fedha ya aibu. 9 wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. 10 Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. 11 Vivyo hivyo wake zao na**

**wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. [12]Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. [13]Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu.**

**3:8 "mashemasi"** Mashemasi hawatajwi hata kidogo katika 2 Timotheo na Tito. Kazi na shughuli za shemasi haelezwi katika Agano Jipya. Wengi wanadhani kwamba Matendo ya Mitume 6 ni mwanzo wa jukumu hili lililojikita kikazi, lakini jambo hili linaonekana kuwa la kimashaka. Hapa wanatajwa, pamoja na wachungaji, kama wenye najikumu/kazi mbili katika kanisa mama (kama vile Flp. 1:1). Hili neno "shemasi" linamaanisha "kutimua vumbi," ambalo kistiari linamaanisha ktumika kwa ajili ya huduma. Hili linakuwa neno la jumla la kifungu "huduma" katika Agano Jipya (kama vile 1 Tim. 1:12; 4:6; 2 Tim. 1:18; 4:5, 11). Mashemasi ni watumishi, si watawala!

◙**"Vivyo hivyo"** Sifa za viongozi wa kanisa zinaelezwa kwa upana hadi kulizungumzia kundi jipya, kama walivyo "wanawake" katika 1 Tim. 3:11.

◙ **"na wawe wastahivu"** Tazama Maelezo katika 1 Tim. 2:2.

◙ **"si wenye kauli mbili"** Kifungu hiki kinamaanisha mambo tofauti tofauti ya makundi tofauti tofauti yanayopaswa kukubaliwa chini ya chini ya masingizio ya uongo. Huu ni muundo wa udanganyifu na uongo.

**NASB "si . . . kutumia mvinyo sana"**
**NKJV "si wenye kulewa sana"**
**NRSV "si wenye kuendekeza mvinyo"**
**TEV "wenye kiasi katika kipimo cha nvinyo wanazokunywa"**
**NJB "hawapaswi kuwa walevi"**

Huu ni uambatani wa neno *pros* na *echō*, maneno ambayo yanamaanisha"kuwa na nyongeza" au "kutimiza." Katika muktadha huu hili linaweza kuwa "kujitoa" (Harold K. Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised*, uk. 349). Kifungu hiki, kama 1 Tim. 3:3, hairejelei kujinyima moja kwa maoja, bali namna ya kutumia. Katika tamaduni nyingine, hata katika nyakati zetu, Wakristo hawana tatizo na usemi huu. Katika Marekani matumizi mabaya ya vileo yalisababisha maandamano yaliyodai mabadiliko yaliyochochea kuvifuata vifungu vya kibiblia. Ikiwa ndivyo tulivyo, kwa sababu yo yote ile, kwa makusudi tunadai nafasi ya kibiblia, tunakuwa watu wa tamaduni, si wa Biblia. Ni tatizo kuiongezea Biblia jambo lo lote (hata kwa shauku zilizo njema na sababu za kiuaminifu) kwa kuwa linauwa nje ya Biblia. Je! ni Biblia pekee iliyo chanzo cha imani na matendo? Ikiwa ni hivyo, lazina hii izihukumu tamaduni zote! Tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 3:3.

◙**"si watu wanaotamani fedha ya aibu"** Usemi huu unarejelea juu ya uaninifu wa kibiashara kwa hawa viongozi wa kanisa wenye kazi hizi zilizogawanyika mara mbili. Ikiwa fedha inawekwa kipaumbele (kama vile 1 Tim. 6:9-10) hapo Yesu hawezi kutenda kazi katika hali hiyo! Walimu wa uongo mara nyingi wanabainishwa katika Agano Jipya kama wenye ulafi na wanyanyasaji wa tendo la kujamiiana. Kumbuka, huu muktadha mzima unayaakisi matendo ya uasi.

**3:9 "wakiishika siri ya imani"** Siri hii inaonekaa kuwarejelea wote Wayahudi na Wayunani waliojumuiishwa katika familia ya Mungu (kama vile Efe. 2:11-3:13; Kol. 1:26,27). Hili neno "imani" lina KIBAINISHI CHA WAZI, ambapo maana yake inayarejelea mafundisho ya mwili wa Kristo.

## MADA MAALUM: MPANGO WA MUNGU KWA AJILI YA WOKOVU, "SIRI"

I. Katika Agano la Kale

Neno la kiaramaiki (BDB 1112, KB 1980), raz, humaanisha "kuficha," "kufanya siri." Danielinatumika mara kadhaa katika Danieli (kama vile Danieli 2:18,19,27,28,29,30,47; 4:9). Inakuwa dhamira kuu katika maandishi ya nyakati za mwisho na inatajwa mara kadhaa katika magombo ya bahari ya chumvi. Mungu anafunua shauri lake lililofichika kwa manabii (kama vile Mwanzo 18:17; Yeremia 23:18; Danieli 9:22; Amosi 3:7).
Katika jamii ya magombo ya bahari ya chumvi ufunuo wa Mungu uliingiliwa kupitia (1) ujumbe wa manabii wa Agano la Kale (*raz*), lakini pia (2) ukalimani (*pesher*) wa "mwalimu wa haki." Taratibu za upande mbili za ufunuo na ukalimani wenye tabia za maandiko ya siku za mwisho.

II. Katika Injili nne "siri" inatumika katika maarifa ya kiroho yatokanayo na mafumbo ya Yesu.
1. Marko 4:11
2. Mathayo 13:11
3. Luka 8:10

III. Paulo analitunia katika njia kadhaa tofauti tofauti.
1. Kufanya mioyo ya Israeli kuwa ngumu kuruhusu Mataifa kujumuishwa. Huku kujumuishwa kwa mataifa kutafanya kazi kama mbinu kwa Wayahudi kumkubali Yesu kama Kristo wa unabii (kama vile Rum. 11:25-32).
2. Injili kuifanya ijulikane kwa mataifa kwa kuwaambia kwamba wanajumuishwa katika Kristo na kupitia Kristo, (kama vile Rum. 16:25-27; Kol. 2:2).
3. Miili mipya ya waamini wakati wa kuja kwa mara ya pili (kama vile 1 Kor. 15:5-57; 1 The. 4:13-18).
4. Kuhitimishwa kwa mambo yote katika Kristo (kama vile Efe. 1:8-11).
5. Mataifa na Wayahudi kama warithi wenza (kama vile Efe. 2:11-3:13).
6. upendo wa kimahusiano ya karibu kati ya Kristo na kanisa unaoelezwa katika maneno ya kindoa (kama vile Efe. 5:22-33).
7. Mataifa yalijumuisha watu wa agano na kuishi kwa Roho wa Kristo ili kuweza kutengeneza makuzi ya kufanana na Kristo ya kwamba kurejesha taswira ya Mungu kwa mwanadamu (kama vile Mwanzo 1:26-27; 5:1; 6:5,11-13; 8:21; 9:6; Kol. 1:26-28).
8. Mwisho wa Mpinga Kristo (kama vile 2 The. 2:1-11).

IV. Tenzi za kanisa la kwanza au Katekisimu kuhusu siri za injili zinapatikana katika 1 Tim. 3:16.

V. Katika Ufunuo wa Yohna inatumika maana ya Yohana ya ishara za siku za mwisho.

◙ **"dhamiri safi"** Hili neno "dhamiri" linaonekana kumaanisha kwamba hawa viongozi wanaenenda na kuyazungumzia mapatano ya kweli ya injili. Tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 1:5.

**3:10 "Hawa pia na wajaribiwe kwanza"** Hii ni KAULI TENDWAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hili ni neno la Kiyunani *dokimazō*, ambalo linatumika pamoja na maana nyingine ya "mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu" (kama vile Rum. 2:18; 12:2; 14:22; 1 Kor. 3:13; 16:3; 2 kor. 8:22; 1 The. 2:4). Hili linatofautishwa na neno *peirazō,* lenye maana nyingine ya "kujaribu hadi kuyafikia maangamizi" (kama vile 1 Kor. 2:5; 10:9,13; Gal. 6:1; Flp. 1:10; 1 The. 3:5; 1 Tim. 6:9). Tazama Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani ya neno Kujaribu na Maana zake Nyingine katika 1 Tim. 6:9.

◙**"baadaye waitende kazi ya shemasi"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI

◙**"wakiisha"** Hii ni SENTENSI nyingine SHURUTISHI DALAJA LA KWANZA kama 1 Tim. 3:5.

◙ **"wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia"** Tazama Maelezo katika 1 Tim. 3:2.

**3:11 "Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu"** Usemi huu hauwarejelei wake za mashemasi (kama vile KJV na NIV), bali kazi zawanawake walio katika utumishi wa makanisa ya nyumbani. Sarufi-muundo ya Kiyunani inalitofautisha kundi lingine la watumishi wa kanisa (yaani,. "hivyo hivyo" ya 1 Tim. 3:8). Mashemasi wanatajwa katikaRum. 16:1 (kama vile Charles B. Williams' translation) na huenda Flp. 4:3. Sifa za wanawake hawa watumishi ni sawa na zile za watumishi wa kiume. Hawa walimaanishwa kuwa wasaidizi wa mashemasi katika hali mbali mbali ambapo mashemasi wa kiume wangeweza kukabiliana nazo vema (kuwabeba wanawake wagonjwa, kusaidia kuwaanda wanawake kabla na baada ya ubatizo, utaratibu wa kawaida wa kuwatembelea wanawake wazee, n.k.). Kutokana na maandishi ya makasisi wa kanisa la Kale tunafahamu kwamba kazi ya mashemasi iliboreshwa kwa haraka sana na ilikuwa ikitumika katika karne zote za kale. Tatizo lililo katika nyakati zetu ni namna tulivyo wapa mamlaka mashemasi kuwa miongoni mwa balaza tendaji, kwa sababu ya vifungu vingine vilivyo katika Timotheo, vinavyoonekana kuwatawala wanawake. Hata hivyo, mashemasi wanamaanishwa kuwa watumishina, hivyo, wanawake wanayo kazi sahihi. Huenda mashemasi wa kike walikuwa na kazi zilizofanana na "wajibu wa wajane" (kama vile 1 Tim. 5:9 na kuendelea), ambapo zaidi ya wajane stini ambao hawakuwa na familia walitumiwa na kanisa la kale kwa ajili ya huduma. Nafikiri kufanya machapisho kwa mara nyingine kuhusu maelezo yangu ya kimaandiko yanayotokana na Rum. 16:1 hapa inaweza kusaidia:

**NASB, NKJV “aliye mtumishi wa kanisa"**
**NRSV "shemasi wa kanisa"**
**TEV "anayelitumikia kanisa"**
**NJB "shemasi wa kike wa kanisa"**

Hili ni neno *diakonos*. Huu ni muundo wa JINSI YA KIKE UMOJA YENYE HALI YA KUSHUTUMU. Hili ni neno la Kiyunani lenye kumaanisha mhudumu/mtumishi. Neno hili linatumika (1) Kumhusu Kristo. 15:8; Marko 10:45; (2) kumhusu Paulo katika Efe. 3:7; Kol. 1:23,25; na (3) kuwahusu mashemasi katika Flp. 1:1; 1 Tim. 3:11.

Kuna ushahidi katika vipindi vyote yaani kipindi cha Agano Jipya na kipindi cha maandiko ya yaliyofuatia baada ya kanisa la kale kuhusu kazi ya mashemasi wa kike. Mfano mwingine wa wanawake walio katika huduma ya kanisa mama katika kitbu cha Agano Jipya ni "wajibu wa wajane" wa Kichungaji (kama vile Tim. 3:11; 5:3-16). Tafsiri za toleo la RSV, Amplified, na Wafilipi zina neno "mashemasi wa kike" katika Rum. 16:1. Toleo la NASB na NIV linacho kifungu hiki katika tambihi. Toleo la NEB lina kifungu "wazishikiliao kazi. "Waamini wote wanaitwa, wanakirimiwa, ni wahudumu kwa wakatai wote (kama vile Efe. 4:12). Wengine wanaitwa katika kazi za huduma ya uongozi.Mapokeo yetu lazima yatoe uelekeo wenyekuyaelekea Maandiko! Hawa mashemasi na mashemasi wa kike wa kale walikuwa watumishi, si wana-baraza la utendaji.

M. R. Vincent, *Word Studies*, juzuu. 2, uk. 752 na 1196, anasema kwamba *Apostolical Constitutions*, akienda mbali zaidi kutokana na karne ya pili au karne ya tatu, anatengeneza tofauti kati ya wajibu na dessturi za wanawake wasaidizi wa kanisa.

1. Mashemasi wa kike
2. wajane (kama vile 1 Tim. 3:11; 5:9-10)
3. mabikra (kama vile Matendo 21:9 na huenda 1 Kor. 7:34)

Wajibu huu ulihusisha

1. kuwahudumia wagonjwa
2. kuwahudumia wale wenye mateso ya kimaumbile
3. kuwatembelea walio gerezani kwa ajili ya kuchochea imani zao
4. kuwafundisha waamini wapya
5. kuwa saidia waamini wakati wa ubatizo
6. baadhi ya wake wa wasimamizi kuwasaidia wanashirika walio kanisani

◙ **"si wasingiziaji"** Huu ni mfano kamili wa matatizo yaliyosababishwa na walimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 5:13-15; 2 Tim. 3:1-7). Inawezekana kwamba kifungu hiki kinayerejelea mazungumzo yaliyohusu mafundisho ya walimu wa uongo. Hili neno lenye kutafsiriwa kama "umbea" mara nyingi lilitumika kumaanisha uovu (kama vile Yohana

6:70). Kiuhalisia hili lilimaanisha "muuaji" (NKJV, NRSV, NIV, kama vile 1 Tim. 3:11; 2 Tim. 3:3; Tito 2:3), si umbea (NASB, TEV, NJB).

◙ **"watu wa kiasi"** Tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 3:3.

◙ **"waaminifu katika mambo yote"** Kwa mara nyingine kipengele hiki kinaweza kuwaelekea moja kwa moja moja walimu wa uongo kuwatumia vibaya wanawake ndani ya makanisa ya nyumbani. Hawa viongozi/watumishi yawapasa kuwa waaminifu katika imani (hakuna KIBAINISHI katika 1 Tim. 3:13 pia) na katika chaguzi zake za maisha.

**3:12** Tafsiri za sasa zinaifupisha 1 Tim. 3:8-13 katika aya moja. Mashemasi huanza mjadala na (kama vile 1 Tim. 3:8) na kuhitiisha mjadala (kama vile 1 Tim. 3:13), bado katika 1 Tim. 3:11 mashemasi wa kike wanajadaialiwa. Ndiyo maana tafsiri nyingine zinawaita "wake za mashemasi." Hata hivyo, nafikiri kuwa wasaidizi wa mashemasi, au mashemasi wa kike, wanaweza kuwa sahihi zaidi kitanaduni. Watumishi wa kike (yaani.,"wajane") kwa upekee wanatajwa katika 1 Tim. 5:9-10.

Mstari wa 12 unafanana sana na sifa za msimamizi au askofu (yaani,. mchungaji) katika 1 Tim. 3:2-5.

## MADA MAALUM: SIFA ZA WANAWAKE WATENDAKAZI WA KANISA KATIKA 1 TIMOTHEO

A. wastahimilivu (1 Tim. 3:11)
B. si wasingiziaji (1 Tim. 3:11)
C. watu wa kiasi 1 Tim. 3:11)
D. waaminifu katika mambo yote (1 Tim. 3:11)
E. wasiosaidiwa na jamaa zao (1 Tim. 3:11)
F. amemwekea Mungu tumaini lake (1 Tim. 5:5)
G. hudumu katika maombi (1 Tim. 5:5)
H. wasiwe na lawama (1 Tim. 5:7)
I. umri wake amepata miaka sitini (1 Tim. 5:9)
J. mke wa mume mmoja (1 Tim. 5:9)
K. ameshuhudiwa kwa matendo mema (1 Tim. 5:10)
   1. ikiwa amelea watoto (1 Tim. 5:10)
   2. ikiwa amekaribisha wageni (1 Tim. 5:10)
   3. ikiwa amewaosha watakatifu miguu (1 Tim. 5:10)
   4. ikiwa amewasaidia wateswao (1 Tim. 5:10)
   5. ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema (1 Tim. 5:10)

M. R. Vincent, *Word Studies*, juzuu. 2, kr. 752 na 1196, anasema kwamba Badilikoli ya Ukanaji Imani, yalianza karne ya pili au ya tatu, unatengeneza tofauti kati ya majukumu na maagizo ya wanawake wasaidizi ndani ya kanisa.

A. mashemasi
B. wajane (kama vile 1 Tim. 3:11; 5:9-10)
C. mabikra (kama vile Matendo 21:9 na huenda 1 Kor. 7:34)

Majukumu haya yanahusisha

A. kuwajali wagonjwa
B. kuwajali wateswao
C. kuwatembelea walio gerezani kwa ajili ya imani
D. kuwafundisha waamini wapya
E. kuwasaidia wanawake wakatai wa ubatizo
F. kuwasaidia wanawake walio ndani ya kanisa

**3:13 "watendao"** Huu ni muundo wa KITENZI wa neno "shemasi." Hili ni neno la moja kwa moja lililo katika Agano Jipya lenye kumaanisha "mhudumu/mtumishi." Hili neno "shemasi" halimo ndani ya m stari huu wa Kiyunani.

◙**"hujipatia daraja nzuri"** Kifungu hiki si lazima kiwe kinairejelea nafasi ya uongozi wa juu (yaani,.mchungaji), bali uwezekano wa kuwepo heshima miongoni mwa jamii zao heshima ambayo kwa pamoja itawafanya kuishiriki injili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 3:14-16**
**[14] Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. [15] Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli. [16]Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili, Akajulika kuwa na haki katika roho, Akaonekana na malaika, Akahubiriwa katika mataifa, Akaaminiwa katika ulimwengu, Akachukuliwa juu katika utukufu.**

**3:14-15** Paulo anapanaga kumtembelea Timotheo katika Efeso. Roho anamwongoza kuwa anaandika hivyo ili mapenzi ya Mungu yatimie katika 1 Timotheo naye aweze kulibariki na kuliongoza kanisa lake kwa wakataia wote.

Mistari hii inaidhinisha Muktadha fasiriwa wa sura za 1-3 kama zinavyohusiana na ibada ya kusanyiko (kama ilivyofanya 1 Wakorintho 11-14). Pia nafikiri kuwa sura hizi ni matokeo na sifa zilizojikita katika uwepo wa walimu wa uongo. Huu si muundo usio na upande!

Hali hii hii ya kithiolojia inaonekana katika Mambo ya Walawi. Kitabu hiki si muunganiko wa sheria za afya au mila sambamba na matokeo ya utamaduni wa Kikanaani. Sheria nyingi ziliandikwa ili kuwaweka mbali Wakaani na Waisraeli na kijamii na kidini kama iwezekanavyo, vifungu hivi vinazitenga nyaraka za Kichungaji na Kiyahudi/Ujuzi wa walimu wa uongo.

**3:15 "Lakini nikikawia"** Hii ni SENTENSI SHURUTISHI DALAJA LA KWANZA, yenye kuamaanisa tendo lililo muhimu.

◙ **"katika nyumba ya Mungu"** Pauloanazitumia stiari zenye nguvu zilizounganishwa kulifafanua kanisa, kama vile "mwili," lakini familia/nyumba ni moja ndiyo inayotazamwa zaidi (Mungu kama Baba, Yesu kama Mwana, waamini kama watoto).

◙ **"kanisa"** Neno *Ekklesia* mi neno ambatani la Kiyunani linalotokana na" nje ya" na "kuita." Hili lilitumika katika lugha ya Koine ya Kiyunani kueleza aina fulani ya kusanyiko, kama vile kusanyoko la mji (kama vile Matendo 19:32). Kanisa la Kale la Kiyunani lilichagua kanisa hili kwa sababu neno hili lilikuwa likitumika katika Agano la Kale la Kiebrania, tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale, lililoandikwa mnamo 250 K.B. kwa ajili ya mabadiliko huko Iskandria, Misri. Neno hili lililtafsiri neno hili la Kiebrania *qahal*, ambalo lilitumika katika kifungu hiki "kusanyiko la Israeli" (Kutoka; Hes. 20:4). Waandishi wa agano Jipya walidai kwamba wao "waliitwa ki-Uungu tofauti na wengine" waliokwa watu wa Mungu wa nyakati zao. Waamini wa kale wa Kiyahudi hawakuiona tofauti ya mara kwa mara kati ya watu wa Mungu wa Agano la Kale na wao wenyewe, watu wa Mungu wa Agano Jipya. Waamini, hivyo, wanadai kwamba Kanisa la Yesu Kristo, si la sheria za Dini a Kiyahudi, huyu ni mrithi wa kweli wa Maandiko ya kweli ya Agano la Kale. Tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 3:5.

◙**"Mungu aliye hai"** Agano la Kale linadai kuwa kuna Mungu mmoja na wa pekee tazama MADA MAALUM : IMANI YA MUNGU MMOJA katika 1 Tim. 2:5, kama vile Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 4:35,39; 6:4; 32:39; 1 Sam. 2:2; Isa. 40:10-13; 44:6-8; 45:5-7). HiKI KIVUMISHI "hai" kinatokana na jina la agano (kama vile1 Tim. 4:10) lenye kumaanisha Mungu, YHWH, jina linalotokana na KITENZI cha Kebrannia "kisaidizi" (kama vile vile Kut. 3:14; tazama MADA MAALUM : MAJINA YA UUNGU katika 2 Tim. 1:2).

◙ **"nguzo na msingi wa kweli"** Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 28:16, Kuwepo kwa Mungu ni Yesu jiwe kuu la pembeni, ambalo pia linadokezwa katika 2 Tim. 2:19. Hiki ni cha tatu katika mlolongo wa vifungu bainishi vyenye kumuunganisha Mungu na kanisa.

1. "nyumba ya Mungu" (1 Tim. 3:15)
2. "kanisa la Mungu aliye hai" (1 Tim. 3:15)
3. "nguzo na kuiunga mkono ile kweli" (1 Tim. 3:15)

Hili neno kweli (*alētheia*) ni la kawaida sana katika maandishi ya Paulo (na yale ya Yohana). Mara nyingi hili liinarejelea dhima ya injili (kama vile Rum. 1:18,25; 2:2,8; 3:7; 15:8; 1 Kor. 13:6; 2 Kor. 4:2; 6:7; 7:14; 13:8; Gal. 2:5,14; 5:7; Efe. 1:13; 4:21; 5:9; Flpl. 1:18; Kol. 1:5,6; 2 The. 2:10,12,13; 1 Tim. 3:15; 4:3; 6:5; 2 Tim. 2:15,18,25; 3:7,8; 4:4; Tito 1:1,14). Tazama Mada Maalum : Kweli katika Maandiko ya Paulo katika 1 Tim. 2:4.

**3:16**
**NASB "alidhihirishwa katika mwili"**
**NKJV "pasipo mabishano"**
**NRSV, NJB "pasipo shaka"**
**TEV " hakuna awezaye kupinga"**

Hili neno la Kiyunani mara nyingi linatumika kuonyesha kuungama au kuungama juu ya imani (tazama MADA MAALUM : UKIRI katika 1 Tim. 6:12). Hii ni ishara ya kimaandishi kuwa mfululizo ufuatao ni udhihirisho wa msingi ya imani ya kale.

◙**"shaka siri ya utauwa ni kuu"** Neno "Siri"katika maandiko ya Paulo mara nyingi huduma ya Mataifa (kama vile Efe. 2:11-3:13), neno ambalo linaweza kuwa nsingi wa 1 Tim. 3:16. Tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 3:9. Kwa neno "Uungu" tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 4:7.

Kifungu hiki kinatoa utangulizi wa usemi wa ungamo la awalia au wimbo wa Kikristo. Nyingine kati ya hizi inapatikana katika 2 Tim. 2:11-13. Mkondo wa kimuundo unaweza kuwa

1. A B C D E F (kweli iliyofunuliwa kumhusu Kristo)
2. AB, BA, AB (tofauti kati ya nchi na mbingu au fedheha na furaha)
3. ABC, ABC (kweli zilizofunuliwa kumuhusu Kristo na kanisa lake)

Mikondo Pingani ndani ya Biblia zinakuwa dhahiri kwa hali ya ujifunzaji wa sasa. Toleo la Companion Bible published na Kregel mnamo 1990 na Kenneth E. Bailey's *Poet and Peasant* linautumia mtazamo huu kwa mapana.
Paulo anaonekana kunukuu kuhusiana na mstari wa wimbo wa awali au yawzekana ni litrujia ya kanisa. Mstari huu unakazia juu ya ubinadamu wa Yesu na huduma yake kwa ulimwengu mzima. Huu haukuhusishwa katika mikazo mitatu ya kithiolojia inayotokana na Paulo: (1) msalaba; (2) ufufuo; na (3) Kuja mara ya Pili. Paulo anavinukuu vyanzo kadhaa katika I, 2 Timotheo na Tito ambavyo vinaeleza misamiatai ya kupekee na matumizi tofauti ya maneno ya kitheolojia yanavyotumika kwa utofauti katika maandiko ya Paulo

**NASB "alidhihirishwa katika mwili"**
**NKJV "Mungu alidhihirishwa katika mwili"**
**NRSV "Aliyefunuliwa katika mwili"**
**TEV "Aliyefunuliwa katika mwonekano wa kibinadamu"**
**NJB "Aliyefanywa katika mwili"**

Kifungu hiki kinazungumzia tendo la Yesu Kristo kutwaa mwili (kuzaliwa) huko Bethlehemu: maisha yake, mafundisho, kifo, na ufufuo, ambayo yalimfunua Baba (kama vile Yohana 1:14-18). Pia kuna kuna hitimisho lenye nguvu ya uwepo wake wa kabla (kama vile Yohana 1:1-5; 8:57-58; 2 Kor. 8:4; Flp. 2:6; Kol. 1:17). Hiki ni kina cha kweli ya Injili yenye kumhusu Yesu Kristo, ya kwamba yeye alikuwa Mungu kamili na mwandamu kamili (kama vile Yohana 1:14; Flp. 2:6-8; Kol. 1:14-16; 1 Yohana 4:1-6).
Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani ambapo kiwakilishi rejeshi *hos* (MSS א, A, C, F, G; toleo la UBS[4] linakipa kiwakilishi hiki daraja "A" [yakini]) kinabadilishwa na kuwa *theos*. Mabadiliko haya yanaweza kuwa yametokea

1. pamoja na mkanganyiko juu ya OC (vifupisho vya herufi kubwa za Kiyunani kwa yule ambaye) kifupi kilichosomwa kama H C (kifupisho cha herufi kubwa za Kiyunani za neno " Mungu") au
2. mabadiliko ya kithiolojia ya kimakusudi yaliyofanywa na waandishi wa nyaraka (kama vile MSS $\aleph^c$, $A^c$, $C^2$, na $D^2$) waliokuwa wakitaka kufanya mabadiliko zaidi ya kipekee dhidi ya waasi wa kiuasilishaji (kama vile Bart D. Ehrman, *The Orthodox Corruption of Scripture*, uk. 77-78)

## MADA MAALUM:MWILI (sarx)

Neno hili limetumiwa mara kwa mara na Paulo kwa Wagalatia na makuzi yake kithiolojia katika Warumi. Wasomi wana tofautiana juu ya namna gani dokezo la maana ya maneno haya ibainishwe. Kuna uhakika wa baadhi ya mipishano katika maana. Lifuatalo ni jaribio tu la kunukuu uwanja mpana wa maana ya neno.

A. mwili wa binadamu, Yohana 1:14; Rum. 2:28; 1 Kor. 5:5; 7:28; 2 Kor. 4:11; 7:5; 12:7; Gal. 1:16; 2:16,20; 4:13; Flp. 1:22; Kol. 1:22,24; 2:5; 1 Tim. 3:16
B. kushuka kibinadamu, Yohana 3:6; Rum. 1:3; 4:1; 9:3,5,8; 11:14; 1 Kor. 10:18; Gal. 4:23,29
C. mwanadamu, Rum. 3:20; 7:5; 8:7-8; 1 Kor. 1:29; 2 Kor. 10:3; Gal. 2:16; 5:24
D. kuzungumza kibinadamu, Yohana 8:15; 1 Kor. 1:26; 2 Kor. 1:12; 5:16; 10:2; Gal. 6:12
E. udhaifu wa kibinadamu, Rum. 6:19; 7:18; 8:5-6,9; 2 Kor. 10:4; Gal. 3:3; 5:13,16,19-21; Kol. 2:18
F. ghasia ya wanadamu kumwelekea Mungu, inayohusiana na matokeo ya Anguko, Rum. 7:14; 13:14; 1 Kor. 3:1,3; Efe. 2:3; Kol. 2:18; 1 Pet. 2:11; 1 Yohana 2:16

Inasisitizwa ya kwamba "mwili" hautazamwi kama uovu katika Agano Jipya, ni katika fikira za Kiyunani. Kwa wanafalsafa wa Kiyunani "mwili" ulikuwa chanzo cha matatizo ya wanadamu; kifo kilimweka huru mtu kutoka kwenye matakwa yake. Lakini katika Agano Jipya, "mwili" ni uwanja wa mgogoro wa mapambano ya kiroho (kama vile Efe. 6:10-18), tena usio na upande. Mwingine anaweza kutumia umbile lake la mwili kwa mazuri au mabaya.

**NASB** **"Akajulikana kuwa na haki katika roho"**
**NKJV, NJB** **"Akathibitika katika Roho"**
**NRSV** **"Akadhihirishwa katika roho"**
**TEV** **"Akaonekana kuwa nuru ya Roho"**

Kfungu hiki kimekuwa kikielezeka katika namna kadhaa.

1. Je! Hiki kinamaanisha kuwa huyu hakuwa na hatia au alithibitika (yaani., alionekana kuwa mwenye haki)?
2. Je! Hiki kinamaanisha kuwa Roho Mtakatifu alikuwa akitenda kazi katika huduma ya Yesu (NASB)?]
3. Je! Hiki kinamaanisha kwamba roho wa Yesu alikuwa amethibitishwa na Baba (kama vile Mt. 3:17; 17:5) ambapo Yesu aliishi maisha kama mwanadamu wa kawaida NRSV)?

Baadhi ya wanathiolojia wanaliona neno "Roho" kama lenye kuurejelea Uungu wa Yesu, ambao umethibitika kupitia ufufuo wake (kama vile Rum. 1:4; 1 Pet. 3:18).

◙ **"Akaonekana na malaika"** Malaika walishuhudia alichokifanya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (kama vile 1 Kor. 4:9; Efe 2:7; 3:10; 1 Pet. 1:12). Hata hivyo, kipengele hiki kinaweza kumrejelea malaika aliyemtumikia Yesu, kwa vyo vyote vile katika tukio la jaribu lake (kama vile Mt. 4:11; Marko 1:13), katika Bustani ya Gethsemane (kama vile Luka 22:43, ambalo ni andko lenye mashaka), au punde baada ya ufufuo (kama vile Luka 24:4,23; Yohana 20:12).

Kifungu hiki ni kifupi sana na kina utata kwamba nadharia kadhaa zimekuwa zikitolewa na watoa maoni na zote ni dhahanio tu:

1. malaika waliomtumikia Yesu (hapo juu)
2. malaika waliokutazama kupaa kwake (malaika wa Mungu na /aua malaika walioanguka kama vile 1 Pet 3:19-20,22)

3. malaika walioitazama furaha ya kusimikwa kwake kimbingu

◙ **"Akahubiriwa katika mataifa"** Hili ni tendo la kuihubiri njili ulimwengu mzima (kama vile Luka 24:46-47) tendo ambalo lingewatisha sana Wayahudi wa karne ya kwanza, lakini kiukweli hii ndiyo hoja kamili (kama vile Mt 8:18-20). Hii ndiyo siri ya kumcha Mungu (kama vile Efe. 2:11-3:13).

**NASB, NKJV "Akaaminiwa katika ulimwengu"**
**NRSV, TEV,**
**NJB "akaaminiwa katika ulimwengu"**

Haukuwa ujumbe wa kiulimwengu tu, bali kulikiuwa na mwitikio wa kiulimwengu, na sasa Kanisa linaundwa na Wayahudi na watu wa Mataifa (kama vile Efe. 2:11-3:13). Huu umekuwa mpango wa Mungu wa mara kwa mara. Mungu mmoja wa kweli ameitimiza ahadai yake ya Mwa. 3:15. Toba binafsi na imani (tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 1:16) sasa katika injili, katika maisha haya, mbingu zilizo wazi kwa "ndio wale" (kama vile Yohan 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13). Tazama Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya neno *Kosmos* katika 1 Tim. 1:16.

◙ **"Akachukuliwa juu katika utukufu"** Kifungu hiki kinaonekana kukurejelea kupaa kwake. Inashangaza kwamba kifo cha Yesu, ufufuo, na kurudi kwake vimeachwa, bali ikiwa huu ni wimbo wa Kikristo, huenda ulinukuliwa pembeni, sasa unaeleweka. Pia, kwa usahihi ni mkondo ambao ni wa kizani (kingamo) unaofuatishwa unaendana na fasiri ya mtu (kama vile 1 Tim. 3:16). Wimbo huu /kanuni ya imani uliohusianishwa na usemi wa ufunguzi ungeukanusha kwa nguvu ujuzi usiyo sahihi. Mtu aitwaye Yesu alitukuzwa (kama vile mkondo wa upinzani #2)! Hata hivyo, kwa kufuata toleo la NRSV mistari mitatu ya mwisho inaweza kulirejelea Kanisa (kama vile mkondo wa ukingamo #3). Kwa maelezo kamili tazama maelezo yahusuyo "utukufu" tazama 1:17.

## MADA MAALUM : KUPAA

Yesu alipaa kwenda mbinguni (kama vile Flp. 2:6-7; 2 Kor. 8:9). Na sasa amerejeshwa katika utukufu Wake wa awali (kama vile Yohana 1:1-3; 17:5; Efe. 4:10; 1 Tim. 3:16; I Yohana 1:2). Yeye amekaa mkono wa kuume wa Mungu (kama vile Zab. 110:1; Luka 22:69; Mdo. 2:33; Rum. 8:34; Efe. 1:20; Kol. 3:1; Ebr. 1:3; 8:1; 10:12; 12:2; 1 Pet. 3:22). Huu ni uthibitisho wa ukubalifu wa Baba kwa uhai na maisha yake!
Kuna idadi tofauti tofauti ya maneno ya Kiyunani yaliyotumika kuelezea juu ya kupaa kwa Yesu mbinguni:

1. Mdo. 1:2,11,22; *analambanō*, kunyakuliwa (kama vile 1 Tim. 3:16)
2. Mdo. 1:9, *epairō*, kutazama juu, kuinua, kunyakua
3. Luka 9:51, *analēpsis* (kwa mtindo wa #1)
4. Luka 24:51, *diistēmi,* kusambaa

Katika Injili ya Yohana kuna vidokezo mbali mbali vya akurudi minguni kwa Yesu (kama vile Yohana 7:33; 8:14,21; 12:33-34; 13:3,33,36; 14:4,5,12,28; 16:5,10,17,28; 26:7)

1. Yohana 3:13; 20:17, *ana BeBēken*, amekwenda zake
2. Yohana 6:62, *anabainō*, kupaa

Tukio hili halikuchukuliwa kumbukumbu katika Injili ya Mthayo au mwishoni mwa Ijili ya Marko katika 16:8, lakini moja wa maongezeko ya waandishi wa baadaye inaeleza tukio katika Marko 16: 19 (yaani, *analambanō* ). Katika Matendo Kuna vidokezo kadha wa kadha kumhusu Yesu kurudi huko mbinguni.

1. Petro – Mdo. 2:33; 3:21
2. Stefano – Mdo.7:55-56
3. Paulo - Mdo. 9:3,5, 22:6-8; 26:13-15

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa usomaji wa fasihi, ikimaanisha kuwa unahusika katika ufasiri wako mwenyewe wa biblia. Kila mmoja wetu anapaswa kutembea katika mwanga tulionao. Wewe, biblia na Roho Mtakatifu ni kipaumbele katika ufasiri. Hatuwezi kuwaachia watoa maoni.

Maswali yametolewa kukusaidia wewe kufikiri mambo makubwa ya sehemu hii ya kitabu. Yanamaanisha kuchokonoa mawazo, na wala sio kumalizia.

1. Kuna aina ngapi za huduma?
2. Kwa nini wachungaji, maaskofu, na wazee wanahitwa kwa majina tofautitofauti katika Agano Jipya?
3. Je! Agano Jipya lina mashemasi wa kike? Ikiwa ni hivyo, kazi zao zilikuwa zipi? Kwa nini mstari wa 16 unafikiriwa kuwa wimbo wa Mkristo kumhusu Kristo?
4. Nini maana ya haiba? Kwa nini ni muhimu?

# 1 TIMOTHEO 4

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| USB[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Unabii wa Ukanaji Uongo Imani | Ukanaji Mkuu wa Imani | Walimu wa Uongo | Walimu wa Uongo | Walimu wa |
| 4:1-5 | 4:1-5 | 4:1-5 | 4:1-5 | 4:1-11 |
| Mhudumu Mwema wa Yesu Kristo | Mtumishi mwema wa Yesu Kristo | | Mtumishi Mwema wa Yesu | |
| 4:6-10 | 4:6-10 | 4:6-10 | 4: 6-10 | |
| | Kuwa Mwangalifu Katika huduma yako | | | |
| 4:11-16 | 4:11-16 | 4:11-16 | 4:11-16 | |
| | | | | 4:12-16 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KUHUSU 4:1-16

A. Kama zilivyo sura za1-3, sura ya 4-6 lazima ifasiriwe katika kuwatazamia walimu wa uongo.
B. Sura ya 4 inauaksi uongozi usiyo yakini (1 Tim. 4:1-5) na uongozi yakini (1 Tim. 4:6-10).
C. Mistari ya 11-16 ni ujumbe binafsi unaotoka kwa Paulo hadi kwa Timotheo ujumbe wenye mwendelezo kupitia 1 Tim. 6:2.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1TIMOTHEO 4:1-5**
**[1]Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; [2] kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto**

**dhamiri zao wenyewe; [3]wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli. [4]Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukrani; [5] kwa kuwa kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba.**

**4:1 "Basi Roho anena waziwazi"** Kifungu hiki kinaweza kuakisi juu ya
1. Unabii wa Agano la Kale
2. Paulo kama mpokeaji na mwenye uvuvio wa moja kwa moja toka kwa Roho (kama vile Matendo 20:33)
3. Vifungu vilivyovuviwa kutoka katika kwa wengine waliovuviwa, viongozi wa sasa (kama vile Matendo 21:11)

**4:1 "Basi Roho anena waziwazi"** Kifungu hiki kinaweza kuakisi juu ya
1. unabii wa Agano la Kale
2. Paulo kama mpokeaji na mwenye uvuvio wa moja kwa moja toka kwa Roho (kama vile Matendo 20:33)
3. Vifungu vilivyovuviwa kutoka katika kwa wengine waliovuviwa, viongozi wa sasa (kama vile Matendo 21:11)

**NASB, NRSV,**
**TEV "nyakati za nyaraka"**
**NKJV "nyakati za nyaraka"**
**NJB "nyakati zilizopita"**

Paulo, kama manabii wengine wa Agano la Kale, alikuwa akizungumza kuhusu matukio ya nyakati zake, lakini akiyahusianisha na yale ya siku zilizopita kabla ya Kuja mara ya Pili. Paulo anafundisha juu ya kukawia huku *Parousia* katika 2 Wathesalonike 2. Hivyo, ubainishaji huu wa uasi na mafundisho yasiyo ya kweli yote haya yanaelezwa katika siku zake (kama vile 2 Tim. 3:1) pamoja na wakati kati ya ujio wa Kristo wa mara ya kwanza na ule wa pili (kama vile 2 Pet. 3:3; Yuda 1:18).
Mara nyingi Agano Jipya linazifafanua sana siku hizi zijazo au nyakati za mwisho kama manabiii wa Agano la Kale walivyozihatarisha siku zao na kututumainia utendaji wa matukio ya siku za mwisho (kama vile Mt. 24:10-12; Matendo 20:29-30; 2 The. 2:3-12; 2 Tim. 3:1-9; 4:3-4; 1 Yohana 2:18-19; 4:1-3).

## MADA MAALUM: KUKAWIA KWA UJIO WA MARA YA PILI (kuja upesi kwa Kristo dhidi ya kukawia *Parousia*)]

Waamini wengi wamekuwa wakifundishwa kwamba Yesu yu karibu kuja, ghafula, na pasipo kutarajia (kama vile Mt. 10:23; 24:34; Marko 9:1; 13:30; Ufu. 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; tazama Mada Maalum: Kurudi Upesi). Bali kila kizazi cha waamini che tarajio nacho kimekuwa kikikosea! Upesi huu (ukaribu) wa kurudi kwa Yesu ni tumaini lenye kuhaidiwa kwa nguvu kwa kila kizazi, bali ukweli wa mtu (na kwa yule ateswaye).
Waamini lazima waishi kana kwamba Yeye anarudi kesho, ni lakini mpango na utekelezaji wa Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:19-20) ikiwa atakawia.
Baadhi ya vifungu katika Injili (kama vile Mt. 24:45-51; 25:5,19; Marko 13:10; Luka 17:2; 18:8; 19:11-27) na 1 na 2 Wathesalonike zimejikita katika kukawia Kuja kwa mara ya Pili (*Parousia*). Kuna baadhi ya matukio ya kihistoria ambayao lazima yatokee kwanza:
1. uinjilishaji wa kiulimwengu (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
2. ukanaji mkuu wa imani (kama vile 2 The. 2:3)
3. ufunuo wa "Dhambi ya mwanadamu" (kama vile Mt. 24:15; 2 The. 2:3,8-12; Ufunuo 13)
4. mateso makuu (kama vile Mt. 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata uliokusudiwa (kama vile Mt. 24:42-51; Marko 13:32-36)! Kila siku ishi kana kwamba ni wakati uliopita lakini panga na jifunze kwa ajili ya huduma ijayo!

**NASB "watajitenga"**
**NKJV "wataondoka"**
**NRSV "watakanusha"**
**TEV "wataacha"**
**NJB "watarudia"**

Huu ni uambatani wa neno *apo* (kutokana) na *istēmi* (simama). Hapa neno hili linatumika katika maana ya usaliti, katika Luka 8:13, na Ebr. 3:12. Katika 2 Tim. 2:19 hili linamaanisha "kujinyima kutokana na." Katika muundo huu KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI UJAO. Moja ya uthibitisho wa wokovu wa kweli ni mtu kwendelea kukaa kanisani (kama vile 1 Yohana 2:18). Tazma MADA MAALUM: HITAJI LA USTAHIMILIVU katika 1 Tim. 4:16.

## MADA MAALUM : UKANAJI WA IMANI *(APHISTĒMI)*

Neno la Kiyunani *aphistēmi* lina uwanja mpana wa elimu-maana. Hata hivyo, Neno la Kiingereza "uasi" limetokana na neno hili na athari za matumizi yake kwa wasomaji wa sasa. Muktadha, kama iliyo kawaida, ndio ufunguo, sio maelezo ya wakati uliopo.

Hili ni neno lililounganishwa kutokana na KIHUSISHI *apo*, ambacho kinamaanisha "kutokana na" au "mbali na" na *histēmi*, "kukaa," "kusimama," au "kupachika." Angalia matumizi yafuatayo (yasiyo ya kitheolojia):

1. kuondoa kimwili
   a. kutoka Hekaluni, Luka 2:37
   b. kutoka katika nyumba, Marko 13:34
   c. kutoka kwa mtu, Marko 12:12; 14:50; Matendo 5:38
   d. kutoka katika vitu vyote, Mt. 19:27,29
2. kuondoa kisiasa, Matendo 5:37
3. kuondoa kimahusiano, Matendo 5:38; 15:38; 19:9; 22:29
4. kuondoa kisheria (talakisha), Kumb. 24:1,3 (LXX ) na Agano Jipya, Mt. 5:31; 19:7; Marko 10:4; 1 Kor. 7:11
5. kuondoa deni, Mt. 18:7
6. kuonyesha kutokuhusika kwa kuondoka, Mt. 4:20; Yohana 4:28; 16:32
7. kuonyesha kutokuhusika kwa kutoondoka, Yohana 8:29; 14:18
8. kuruhsu au kutoa kibali, Mt. 13:30; 19:14; Marko 14:6; Luka 13:8

Katika maana ya kitheolojia KITENZI pia kina matumizi mapana:

1. kufuta, kusamehe, kuifuta hatia ya dhambi, Kut.32:32 (70) (LXX); Hes. 14:19; Yak. 42:10 na Agano Jipya, Mt. 6:12,14-15; Marko 11:25-26
2. kujiondoa toka dhambini, 2 Tim. 2:1
3. kukataa kwa kujiondoa toka kwenye
   a. Sheria, Mt. 23:23; Matendo 21:21
   b. imani, Ezek. 20:8 (LXX ); Luka 8:13; 2 The. 2:3; 1 Tim. 4:1; Ebr. 3:12

Waamini wa sasa wanauliza maswali mengi ya kitheolojia ambayo waandishi wengi wa Agano Jipya wasingalifikiri kuyahusu. Moja ya haya yangeliweza kuhusiana na uelekeo wa sasa wa kuitenga imani (uthibitisho) kutoka kwenye imani (utakaso).

Kuna watu katika Biblia walihusishwa miongoni mwa watu wa Mungu na jambo lililotokea na kusababisha wao kuondoka.

I. Agano la Kale
   A. Wale walioisikia taarifa ya wale wapelelezi kumi na wawili (kumi), Namba 14 (kama vile Heb. 3:16-19)
   B. Kora, Namba 16
   C. Wana wa Eli, 1 Samueli 2, 4

D. Sauli, 1 Samueli 11-31
E. Manabii wa uongo (mifano)
    1. Kumb. 13:1-5 18:19-22 (nji za kumtambau nabii wa uongo)
    2. Jeremia 28
    3. . Ezekieli 13:1-7
F. Manabii wa uongo
    1. Ezekieli 13:17
    2. Nehemia 6:14
G. Uovu wa viongozi wa Israeli (mifano)
    1. Yeremia 5:30-31; 8:1-2; 23:1-4
    2. Ezekieli 22:23-31
    3. Mika 3:5-12

II. Agano Jipya

A. Hili neno la Kiyunani kifasihi linamaanisha "kuasi". Vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipya vinathibitisha uchochezi wa uovu na mafundisho ya uongo kabla ya Ujio wa Pili (kama vile Mat. 24:24; Marko 13:22;

Matendo 20:29,30; 2 The. 2:9-12; 2 Tim. 4:4). Neno hili la Kiyunani linaweza kuyaaakisi maneno ya Yesu katika Mfano wa Udongo unaopatikana katika Mathayo13; Marko 4; na Luka 8. Kwa kudhaniwa walimu hawa wa uongo si Wakristo, bali waamini wachanga (kama vile Ebr. 3:12).

Swali la kitheolojia ni hili walimu wa uongo wanawapeleka wapi waamini? Hili ni vigumu kulijibu kwa kuwa kulikuwa na walimu wa uongo katika makanisa anzilishi (kama vile 1 Yohana 2:18-19). Mara nyingi tamaduni au madhehebu yetu yanajibu swali hili pasipokuwa na marejeo ya maandiko ya Biblia mahususi (isipokuwa njia ya kuhakiki kwa nukuu mstari ulio nje ya muktadha ili kwa uangalifu kuhakiki madhara yaliyomo).

B. Imani Thabiti
    1. Yuda, Yohana 17:1
    2. Simoni mchawi, Matendo 8
    3. Wale waliozungumziwa katika Mat. 7:13-2
    4. Wale waliozungumziwa katika Mathayo 13; Marko 4; Luka
    5. Wayahudi wa Yohana 8:31-59
    6. Alexanda na Himenayo, 1 Tim. 1:19-20
    7. Wale wa 1 Tim. 6:21
    8. Himanayo na Fileto, 2 Tim. 2:16-18
    9. Dema, 2 Tim. 4:10
    10. Walimu wa uongo, 2 Petro 2:19-22; Yuda 1:12-19
    11. wapinga Kristo, 1 Yohana 2:18-19
C. Imani isiyo kuwa na matunda
    1. 1 Wakorintho 3:10-15
    2. 2 Petro 1:8-11

Mara chache tunafikiri juu ya haya maandiko kwa kuwa mfumo wa injlili yetu (Ufuatao mtazamo wa Calvn, Arminian, n.k.) unaamuru mwitikio wa kimamlaka. Tafadhari usinihukumu kabla kwa kuwa nafundisha somo langu. Shauku yangu ni hatua ya kiufasiri. Tunapaswa kuipa nafasi Biblia ili izungumze nasi na si kuiumba katika mpangilio wa thiolojia iliyopita. Mara nyingi hii inaumiza na kushtua kwa kuwa thiolojia zetu zilizo nyingi ni za kimadhehebu, kitamaduni, kimahusiano (mzazi, rafiki, mchungaji), si za kibiblia (tazama Mada Maalumu: Nini maana ya neno "Kupokea," "Kuamini," "Kiri/Ungama,"na "Itia"?). Wengine walio miongoni mwa watu wa Mungu wanarudi nyuma na kutokuwa miongoni mwa watu wa Mungu (mf. Rum. 9:6).

◙ **"imani"** Hili neno (yenye huendana na KIBAINISHI) linatumika katika Nyaraka za Kichungaji kwa ajili ya mwli wa kweli ya Kristo aliyefumuliwa (kama vile 1 Tim. 3:9; 4:6; 5:8; 6:10,12,21; 2 Tim. 2:18; 3:8,10; 4:7; Tito 1:5,13; 2:2). Hapa si muhimu neno hili lirejelee juu ya wokovu wao kama ilivyo kwa walimu wa uongo.

◙ **"wakisikiliza roho zidanganyazo"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU yenye kukazia tendo endelevu. Ukanaji huu wa imani unaendelea kuamini na kwendelea kuyasadiki mafundisho ya shetani.

**4:2**
**NASB "kwa unafiki wa watu wasemao uongo"**
**NKJV "wakizungumza uongo kwa unafiki"**
**NRSV "kupitia unafiki wa wadanganyifu"**
**TEV "wakieneza kwa udanganifu"**
**NJB "wakishawishiwa kwa unafiki wa wadanganyifu"**

Hawa wanadai kuwa "walimu wa Sheria" (kama vile 1 Tim. 1:7). Kuna jambo la wazi la Dini ya Kiyahudi lililohisishwa. Kwa uhalisia wao hawa wanaelezwa katika 1 Tim. 1:3-7; 4:2-3,7 na 6:3-10,20-21

1. wanafundisha elimu nyingine (1 Tim. 1:3; 6:3)
2. wanaziangalia hadithi na nasaba (1 Tim. 1:4)
3. wamegeukia maneno ya ubatili (1 Tim. 1:6)
4. wapenda kuwa waalimu wa sheria, ingawa hawayafahamu wasemayo wala mambo yale wayanenayo (1 Tim. 1:7; 6:4)
5. kwa unafiki wa watu wasemao uongo (1 Tim. 4:2)
6. wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe (1 Tim. 4:2)
7. wakiwazuia watu wasioe (1 Tim. 4:3)
8. na kuwaamuru wajiepushe na vyakula (1 Tim. 4:3)
9. hadithi za kizee (1 Tim. 4:7)
10. husuda, na ugomvi, na matukano, na shuku mbaya (1 Tim. 6:4)
11. ana wazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno (1 Tim. 6:4)
12. majadiliano ya watu walioharibika akili zao (1 Tim. 6:5)
13. wanayaona maarifa ya uongo (1 Tim. 6:20-21)
14. wameikosa Imani (1 Tim. 4:1; 6:21)

**NASB "roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani"**
**NKJV "roho zidanganyazo na mafundisho ya shetani"**
**NRSV "roho zidanganyazo na mafundisho ya shetani"**
**TEV "roho za uongo . . . mafundisho ya uongo"**
**NJB "roho zidanganyazo na mafundisho yanayotokana na shetani"**

Mtazamo wa Paulo juu ya hawa walimu wa uongo ni hasi sana. Yeye anayalinganisha mafundisho yao na kazi ya Shetani (tazama Mada Maalumu:Shetani katika 1 Tim. 3:6, kama vile 1 Tim. 2:14; 3:6-7) na ile ya pepo wachafu. Katika namna nyingi mtazamo wa Paulo juu ya hawa waasi unafanana na mtazamo wa Agano la Kale juu ya Ibada ya Ustawi wa Wakanaani. Mungu aliwaamuru Waisraeli kuwaangamiza watu hawa moja kwa moja kwa sababu wangeichafua imani. Maonyo kama haya yanapatikana katika hapa (kama vile 2 The. 2:9-10; Yakobo 3:15; 1 Yohana 2:18-19).

## MADA MAALUM: PEPO WACHAFU (ROHO CHAFU)

A. Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.

B. Mifano hii wakati mwingine ilileta matokeo ya kuabudu miungu mingi (miungu wengi). Kwa kawaida mapepo (*genii*) ilikuwa miungu midogo au nusu miungu (mizuri au miovu) ambao ilileta matokeo kadha wa kadha katika maisha ya watu binafsi.
   1. Machafuko na migogoro huko Mesopotamia,
   2. Mpangilio na kazi huko Misri,
   3. Kanaani, tazama W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel,* Toleo la Tano, kur. 67-9

C. Agano la Kale halielezi sana au kukuza jambo la miungu wadogo, malaika, au pepo, huenda ni kwa sababu ya msistizo wake mkali unaozungumzia Imani ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalumu : Mungu mmoja_ Imani ya Mungu mmoja kama vile Kut. 8:10; 9:14; 15:11; Kumb. 4:35,39; 6:4; 33:26; Zab. 35:10; 71:19; 86:8; Isa. 46:9;Yer. 10:6-7; Mik. 7:18). Haliizungumzii miungu ya uongo ya mataifa ya wapagani (*Shedim*, BDB 993, kama vile Kumb. 32:17; Zab. 106:37) na halitaji majina au kufananisha baadhi yao.
   1. *Se'im* (mazimwi au majitu yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14)
   2. *Lilith* (jike, pepo apotoshaye kizinifu nyakati za usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
   3. *Mavet* (neno la Kiebrania liliotumika kumtaja mungu mwovu wa Wakanani, Mot, BDB 560, KB560, kama vile Isa. 28:15,18; Yer. 9:21; na kwa kadri iwezekavyo Kumb. 28:22)
   4. *Resheph* ( mahali, moto, au mawe yenye kutiririsha mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kumb. 32:24; Zab. 78:48; Hab. 3:5)
   5. *Dever* (uharibifu, BDB 184, cf. Zab. 91:5-6; Hab. 3:5)
   6. *Az'aze*l (jina halina uhakika, lakini huenda akawa pepo wa jangwani au jina la mahali, BDB 736, KB 736, kama vile Law. 16:8,10,26)

(Mifano hii inachukuliwa kutoka *Encyclopedia Judaica*, juzuu l. 5, uk. 1523.).Hata hivyo, hakuna imani ya Mungu wawili au uhuru wa malaika kutoka kwa YHWH katika Agano la Kale. Ibilisi chini ya YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), hayuko huru, ni adui anayejiongoza (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306).

D. Dini ya Kiyahudi iliendelezwa kipindi cha uhamisho wa Babeli (586-538 b.k). Kitheolojia iliathiriwa aina mbili za Kiajemi zilizochukua nafasi kwa wafuasi wa Zoroaster, mungu mkuu na mzuri aliitwa Mazda au Ormazd na mpinga uovu aitwaye Ahriman. Huyu aliruhusiwa ndani ya dini ya Kiyahudi baada ya uamisho na kuwa mfano wa aina mbili kati ya YHWH na malaika zake na Ibilisi malaika zake au pepo.

Theolojia ya dini ya Kiyahudi yenye kutoa mfano wa uovu inaelezwa na kunakiliwa vema katika Edersheim ya Alfred *The Life and Times of Jesus the Messiah,* juzuu. 2, kiambatisho XIII (kur. 749-863) na XVI (kur. 770-776). Dini ya Kiyahudi ilitoa mifano ya uovu katika njia tatu.
   1. Ibilisi au Malaika wa maangamizi
   2. kusudi la uovu (yetzer hara) ndani ya mwandamu
   3. Malaika wa Mauti

Edersheim anayabainisha haya kama
   1. Mshitaki
   2. Mjaribu
   3. Mwadhibishaji (juzuu 2, uk. 756)

Kuna tofauti zinazodhihirika kitheolojia kati ya dini ya Kiyahudi iliyokuwepo baada ya uhamisho na nanma uwaslilishaji na maelezo ya uovu inavyofanyika ndani ya Agano Jipya.

E. Agano Jipya, haswaa Injili, linadai uwepo na upinzani wa uovu wa viumbe vya kiroho kwa mwanadamu na kwa YHWH (katika dini ya Kiyahudi, Ibilisi alikuwa adui wa mwanadamu, lakini si kwa Mungu). Hawa wanayapinga mapenzi ya Mungu, amri, na ufalme.

Yesu alikabiliana na kuvifukuza hivi viumbe vya kimapepo, pia viliitwa (1) roho chafu (kama vile. Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu kama vile. Luka 7:21; 8:2), kutoka kwa wanadamu. Yesu kwa udhihilisho alitengeneza tofauti kati ya maradhi (kimwonekano na kiakili) na hali ya kimapepo. Aliithibitisha nguvu Yake na mtazamo wa ndani wa kiroho kwa kuwatambua na kuwafahamu hawa pepo wabaya. Mara nyingi walimtambua na kumwita, lakini Yesu aliukataa ushuhuda wao, alihitaji wawe kimya, na kuyafukuzia mbali.

Utambuzi wa pepo hawa ni ishara ya kuvunja ufalme wa Ibilisi.

Kuna upungufu wa ajabu wa habari ndani ya barua za Kitume za Agano Jipya kuhusiana na somo hili. Utambuzi huu kamwe haukuorodhesha karama za kiroho, wala methodolojia au hatua yake iliyotolewa kwa ajili ya vizazi vijavyo vya huduma au waamini.

F. Mwovu yu dhahiri; mwovu ni mtu binafsi; mwovu yupo. Si asili yake wala kusudi lake linalofunuliwa. Biblia inatetea ukweli wake na kwa ukali inapinga ushawishi wake yule mwovu. Ndani ya ukweli hakuna hatima yenye mitazamo yenye uwili ndani yake. Mungu yu ndani ya utawala wake mwenyewe ; mwovu anaangamizwa na kuhukumiwa na ataondolewa kutoka katika uumbaji.

G. Watu wa Mungu yawapasa kumpinga mwovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawawezi kutawaliwa na naye (kama vile 1 Yohana 5:18), bali wanaweza kujaribiwa na ushuhuda na ushawishi wake kuangamizwa (kama vile Efe. 6:10-18). Mwovu ni sehemu ya mtazamo wa ulimwengu kwa wakristo uliofunuliwa. Wakristo wa sasa hawana haki ya kueleza wazi kwa mara nyingine (kutafasiri upya maandishi ya Rudolf Baltmann); kuyaua maovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), wala kujaribu kuelezea kwa ukamilifu katika namna ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea kote, lakini umeangamizwa. Waamini wanahitaji kuenenda ndani ya ushindi wa Kristo!

**NASB "wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe"**
**NKJV "wenye dhamiri zilizotiwa muhuri wa chuma chenye moto"**
**NRSV "wenye dhamiri zilizotiwa muhuri kwa chuma cha moto"**
**TEV "dhamiri zinekufa, kama vile zimechomwa kwa chuma cha moto"**
**NJB "dhamiri zimechomwa kama zilizotupwa katika chuma cha moto chekundu"**

Kifungu hiki kinalirejelea jambo moja kati ya mambo haya.

1. Hawa walimu wa uongo walikuwa nje ya tendo la toba (kama vile Efe. 4:19; Tito 1:15). Hapa tunalipata neno la Kiingreza "unguzae" kutokana na hili neno la Kiyunani.
2. Kifungu hiki kinaiurejelea moto wa Shetani wenye kuonyesha umiliki wake (mf., Ufu. 13:16,17; 14:11; 16:2; 19:20; 20:4).

Kwa kuwa watu hawa wanekataa kuiona kweli, sasa hawawezi kuioa kweli (kama vile 2 Kor. 4:4). Hii ni dhambi ya Injili isiyosameheka na dhambi katika mauti ya 1 Yohana 5.
Tazama maelezo kuhusu "dhamiri" katika 1 Tim. 1:5.

## MADA MAALUM : DHAMBI KATIKA MAUTI

A. Uzingatiaji wa kanuni za ufasiri
  1. Utambulisho sahihi unapaswa kuhusishwa na kuiweka vizuri kihistoria ya 1 Yohana
    a. uwepo wa mafunuo ya walimu wa uongo (tazama Mada Maalum: Mafunuo) katika makanisa (kama vile 1 Yohana 2:19,26; 3:7; 2 Yohana 7; tazama Mada Maalum: Mafunuo)
      1) "*Cerinthian*." Watu wa mafunuo walifundisha kwamba Yesu aliyekuwa mwanadamu alipokea roho wa Kristo katika ubatizo wake na kwamba roho ya Kristo iliondoka kabla ya kifo chake pale msalabani (kama vile 1 Yohana 5:6-8)
      2) "*Docetic*." Watu wa mafunuo walifundisha kuwa Yesu alikuwa ni Roho wa Kiungu, na wala si Mwanadamu kamili halisi (kama vile 1 Yohana 1:1-3)
      3) Mafunuo yanadhihilisha kuwa katika maandiko ya karne ya pili yaliangazia kuhusu maoni ya aina mbili tofauti kuhusu mwili wa binadamu
        a) kwa vie wokovu ulikuwa ni ukweli uliobainishwa katika fikra mwili wa mtu haukuwa na maana katika ulimwengu wa kiroho. Kwahiyo, chochote ungetaka kingekuwa. Haya daima huitwa mafunuo kwa njia ya neema au mafunuo huru.
        b) kundi lingine lilihitimisha kuwa kwa vile mwili ulikuwa na uovu wa asili (yaani, wazo la Kiyunani), tamanio lolote la kimwili sharti likataliwe. Hivyo haya uitwa mafunuo ya "kujinyima."
    b. walimu hawa wa uongo walikwisha ondoka kanisani (kama vile 1 Yohana 2:19), lakini athari zao bado

zipo!

2. utambulisho mzuri sharti uhusishwe na mazingira ya fasihi za kitabu kizima
   a. 1 Yohana kiliandikwa ili kupambanisha mafundisho ya uongo na kuwahakikishia waamini wa kweli
   b. makusudi haya mawili yanaweza kuonekana katika majaribio ya waamini wa kweli
      1) kimafundisho
         a) Yesu alikuwa mwanadamu halisi (kama vile 1 Yohana 1:1-3; 4:14)
         b) Yesu alikuwa Mungu halisi (kama vile 1 Yohana 1:2; 5:20)
         c) wanadamu ni wenye dhambi na wanawajibika kwa Mungu mtakatifu (kama vile 1 Yohana 1:6,10)
         d) wanadamu pia wanasamehewa na kufanya kuwa wenye haki kwa
            i. kifo cha Yesu (kama vile 1 Yohana 1:7; 2:1-2; 3:16; 4:9-10,14; 5:6-8)
            ii. imani kwa Yesu (kama vile 1 Yohana 1:9; 3:23; 4:15; 5:1,4-5,10-12,13)
      2) Kivitendo (chanya)
         a) Mtindo wa maisha wenye utii (kama vile 1 Yohana 2:3-5; 3:22,24; 5:2-3)
         b) Mtindo wa maisha wenye upendo (1 Yohana 2:10; 3:11,14,18,23; 4:7,11-12,16-18,21)
         c) Mtindo wa maisha unaofanana na Kristo (hatendi dhambi, kama vile 1 Yohana 1:7; 2:6,29; 3:6-9; 5:18)
         d) Mtindo wa maisha wenye ushindi dhidi ya maovu (kama vile 1 yohana 2:13,14; 4:4; 5:4)
         e) Neno Lake linadumu ndani mwao (kama vile 1 Yohana 1:10; 2:14)
         f) Wana Roho (kama vile 1 Yohana 3:24; 4:4-6,13)
         g) Hujibiwa maombi (kama vile 1 Yohana 5:14-15)
      3) Kivitendo (hasi)
         a) Mtindo wa maisha ya dhambi (kama vile 1 Yohana 3:8-10)
         b) Mtindo wa maisha yenye chuki (kama vile 1 Yohana 2:9,11; 3:15; 4:20)
         c) Mtindo wa maisha usio na utii (kama vile 1 Yohana 2:4; 3:4)
         d) Kupenda ulimwengu (kama vile 1 Yohana 2:15-16)
         e) kumkana Yesu (kumkataa Baba na Mwana,kama vile 1 Yohana 2:22-23; 4:2-3; 5:10-12)
3. Utambulisho mzuri lazima uunganishwe kwenye kipengele maalumu katika andiko muhimu (kama vileYohana 5:16-17)
   a. Je neno “ndugu” katika 1 Yohana 5:16 linahusiana na wale wote watenda dhambi zisizowapeleka katika mauti na wale watendao dhambi zinazowapeleka katika mauti?
   b. Ni wapi wakosaji mara moja wanakuwa wanajumuiya ya kanisa (ama vile 1 Yoh.2:19)
   c. Nini umuhimu wa kimaandiko wa:
      1) Hakuna KIFUNGU kinachoafikiana na “dhambi”
      2) Kitenzi “anaona” ni kama kilivyo kwenye DARAJA LA TATU SHURUTISHI kikiwa na KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU?
   d. Ni kwa namna gani mmoja wa waombaji wa Kikristo (kama vile Yakobo 5:15-16) aweza kurejesha uzima wa milele, *zōē,* kwa mwingine pasipo mwenye dhambi mwenyewe kutubu?
   e. Ni kwa vipi 1 Yohana 5:17 inahusiana na aina hiyo ya dhambi ( mpaka mauti, kutokuyafikia mauti)

A. Matatizo ya kithiolojia
   1. Ni lazima mtafasili ajaribu kuhusianisha andiko hili na
      a. Dhambi “isiosameheka” kwenye injili (angali Mada Maalumu: Dhambi Isiosameheka)
      b. Dhambi “inayoondoka mara moja” kwenye Waebrania 6 na 10

Muktadha wa 1 Yohana unaonekana kufanana na dhambi isiosameheka ya Wafarisayo katika siku zile za Yesu (kama vile Mt. 12:22-37; Marko 3:22-29) vile vile Wayahudi wasioamini wa Waebrania 6 na 10. Makundi yote haya matatu (Mafarisayo, Wayahudi wasioamini, na walimu wa mafunuo ya uongo) waliisikia injili wazi, lakini wakakataa kumwamini Kristo.

2. Ni lazima maswali ya kisasa ya kimadhehebu yawe kipimo cha kithiolojia cha kuliangalia andiko hili? Uinjilisti umesisitiza mno juu ya uanzishwaji wa mambo ya Ukristo na kuacha ushuhuda wa imani ya kweli juu ya mtindo wa maisha unaoendelea. Maswali ya kisasa ya kithiolojia yangaliwashangaza Wakristo wa karne ya kwanza. Tunataka kitu “fulani” kinachoendana na “uhakiki wa maandiko” ya Kibiblia yaliyochaguliwa na

mapungufu yetu ya kimantiki au upendelea wa kimadhehebu.
Maswali yetu ya kithiolojia, vipimo, na makandokando yanatazamisha kutokuwepo kwetu kwa ulinzi. Tunahitaji zaidi habari na maelezo ya kina kuliko yale yatolewayo na Biblia, kwa hiyo mpangilio wetu wa kithiolojia unachukua kipande kidogo cha andiko na kupeperusha mfumo mkubwa wa mantiki za kimagharibi, na mafundisho maalumu!
Maneno ya Yesu katika Mathayo 7 yalijitosheleza kwa ajili ya kanisa la mwanzo! Yesu alikuwa akiwatafuta wanafunzi, na sio maamuzi, imani ya muda mrefu ya mtindo wa maisha, na sio imani ya kimhemuko ya muda mfupi (kama vile Mt. 13:10-23; 28:18-20; Yoh. 8:31-59). Ukristo sio kitendo cha nyuma kilichojitenga, lakini ni kitendo cha toba kinachoendelea, imani, utii, na ustahimilivu. Ukristo sio tiketi ya kwenda mbinguni, sio kitu kilichonunuliwa huko nyuma, au bima ya moto iliyochukuliwa kumlinda mtu toka kwenye mtindo wa maisha ya ubinafsi, maisha yasio ya kiungu! Angalia Mada Maalumu: Utume

3. Dhambi mpaka inarejea mauti ya kimwili au mauti ya milele? Yohana ametumia *zōē* katika mazingira haya kudokeza tofauti iliyopo inayorejerea mauti ya milele. Inawezekana kuwa Mungu anawarejesha nyumbani wana wanaotenda dhambi? Uhusishaji wa mazingira haya ni kwamba (1) maombi ya waumini wenza na (2) toba binafsi ya mtu mkosaji inajumuishwa kurejesha waumini, lakini kama wakiendelea katika mtindo wa maisha ule uletao fedheha kwa jamii inayoamini, ndipo matokeo yanawezakuwa kwenye "muda usio muafaka" au kuondoka mapema katika maisha haya (kama vile *When Critics Ask* by Norman Geisler and Thomas Howe, uk. 541).

**4:3 "wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula"** Hapa kuna mambo mawili yahusuyo ya walimu wa uongo yahusuyo kujinyima. Jambo la kwanza, kuzuia ndoa, linahusiana na msingi wa Kiyunani (Ujuzi wa uongo) au huenda ni ushawishi wa Asili ya Kiyahudi (Jamii ya Magombo ya Bahari ya Chumvi). Ndoa ni zawadi toka kwa Mungu (kama vile Mwa. 2:24) na mapenzi ya Mungu (kama vile Mwa. 1:28; 9:1,7). Ndoa ni kawaida; useja ni wito na karama maalum toka kwa Mungu (kama vile Mt. 19:11-12; 1 Wakorintho 7).
Jambo la Pili, kujinyima vyakula fulani, linaonekana kuhusiana msingi fulani wa Kiyahudi (kama vile Mambo ya Walawi 11), lakini ungerejelea vizuizi vya waaujuzi wa uongo. Dhana zote zinashughulikiwa kithiolojia katika Mwa. 1:28-31. Kumekuwa na tabia ya mara kwa natraniongoni mwa watu wa kidini kuipinga kwli ya kiulimwengu, kufikiri kuwa useja kama hali nzuri zaidi ya kiroho na kulitazamia tendo la kujinyima chakula na kinywaji na kujizuia kwa ujumla kama hali ya juu ya kiroho (kama vile Mt. 15:11; Marko 7:17-23; Rum. 14:1-15:13; 1 Kor. 8:8; 10:23-33; Kol. 2:8-23). Orodha ya sifa za uongozi katika sura ya 3 huenda inahusiana na mafundisho ya hawa walimu wa uongo. Tambua kuwa mambo yote mawaili yaani ndoa na mvinyo yanaruhusiwa (kama vile 1 Tim. 3:2,12; 5:9 na 3:3,8; 5:23).

◙ **"walio na imani wenye kuijua hiyo kweli"** Huu ni muundo wa kisarufi usio wa kawaida (yaani., KIVUMISHI na KIAMBATA, kama vile Michael Magill, *NT TransLine*, uk. 785). Muundo huu wenye kufanana unajitokeza katika Tito 1:15. Waamini hawa wanabainishwa kama

1. waanini – ITANGULIAYO NOMINO, KIELEZI CHA MUDA, WINGI, JINSIA YA KIUME, KIVUMISHI
2. wale waliokwisha kujulikana – TIMILIFU, TENDAJI, KAULI ENDLEVU JINSIA YA KIUME WINGI

Hapa ukweli (tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 2:4) ni kwamba uumbaji unatoka kwa Mungu na anapaswa kushukuliwa kwa ajili ya tendo hili. Kujinyima huaribu ukweli.

**4:4 "Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri"** Kuhusiana na kweli hii yenye kustaajabisha juu ya utauwa wa mambo yote tazama Mwa. 1:31; Rum. 14:14,20; 1 Kor. 6:12; 10:26; Tito 1:15. Hata hivyo, yatupasa kuweka ulinganifu wa kweli hii kwamba japo mambo yote yanaweza kuwa mema na safi kwa wale wenye kulijua chimbuko lao katika Mungu, si mambo yote yalionyalo kanisa (kama vile 1 Kor. 6:12 na 10:23). Hivyo, sisi kama Wakristo tuweke mipaka ya uhuru wetu kwa ajili ya wengine walio nje ya utukufu wa Kristo (kama vile Rum. 14:1-15:13; 1 Wakorintho 8-10).
Hili neno "kataliwa" kiuhalisia linamaanisha "kuweka kando." Moffatt analitafsiri kama "haramishwa." Iweni makini kuhusu utamaduni na/au mapokeo ya kimadhehebu (kama vile Isa. 29:13; Kol. 2:8-23).

**4:5** Neno la Mungu lililonenwa kuhusu uumbaji (kama vile Mwa. 1:3,6,7,14,20,24) na kuukiri utauwa halisia wa mambo yote (kama vile Mwa. 1:31). Mwamini humshukuru Mungu (kama vile 1 Tim. 4:4b) kwa ajili ya uumbaji wake na utoaji wake (kama vile Rum. 14:6; 1 Kor. 10:30-31).

◙ **"kuomba"** Neno hili (*enteuxis*) linatumika mara mbili tu katika Agano Jipya, mara hizi zote ziko katika 1 Timotheo kama vile 1 Tim. 2:1 na 4:5). Hili linadokeza juu ya tendo la kukutana na mtu kwa kusudi la kimatembezi. Mara nyingi linatafsiriwa kama"kusihi" (kama vile 1 Tim. 2:1); katika muktadha huu, "shukrani" inaonekana kuwa bora zaidi. Kumbuka kwamba ni muktadha wenye kubainisha maana ya maneno, si mafundisho!

**ANDIKO LA NASB (LILLOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 4:6-10**
**6 Uwakumbushe ndugu mambo hayo, nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoevu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata. 7 Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae; nawe ujizoeze kupata utauwa. 8 Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye. 9 Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa; 10 kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio.**

**4:6 "Uwakumbushe ndugu mambo hayo"** Neno *Hupotitēmi*, ambalo ni KAULI YA KATI linamaanisha "kupendekeza." Litambue bembelezo ambalo Paulo alikuwa akilisistiza kwa Timotheo kuwakosoa washirika wa kanisa (kama vile sura ya 5). Itambue tofauti iliyopo katika 1 Tim. 4:11, ambapo ambapo anatoa maagizo makali ya kushughulikia matatizo yanayoukumba ushirika huao. Yote yanaendana na eneo walilopo.

◙ **"nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoevu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri "** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO (ingawa iko katika mfumo huu inaweza kuwa KAULI YA KATI, ambayo ingewasistiza waamini kujifunza kuhusu imani yao wenyewe). Wahudumu wanapandwa katika misingi ya Ukristo wa kweli (Navichagua vifungu hivi viwili vya kipekee kama vya kivisawe).Hii ni dhana ya mafundisho ya kweli, si mafundisho ya kimapepo yaliyokuwa yakitolewa na walimu wa uongo! Makusudi ya Maandiko yanatajwa vema katika 2 Tim. 3:15-17, kama lilivyo jukumu la kila mwanini katika 2 Tim. 2:15, hasa kwa upande wa mafundisho ya uongo (kama vile 2 Tim. 2:14-18).

◙ **"yale uliyoyafuata"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Timotheo aliifuatisha nukuu ya uaminifu. Neno hili kwa vyo vyote vile linaweza kumaanisha

1. kufuatisha (kama vile 2 Tim. 3:10)
2. kufanya uchunguzi wa karibu (kama vile Luka 1:3)

**4:7 "Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae"** Nyara za Kichungaji zinaipinga (KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPO [yenye ushahidi] SHURUTISHI) mijadala dhahania pamoja na kujinyima kulikofundishwa na walimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 1:4; 4:7; 2 Tim.2:14-18,23; Tito 1:14; 3:9). Hiki KITENZI cha kipekee (*paraiteomai*) kinatumika katika 1 Tim. 4:7; 5:11; 2 Tim. 2:23, na Tito 3:10.

Hiki kifungu "kizee" (*graōdēs*) kinatumika mahali hapa pekee katika Agano Jipya. Harold K. Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised*, uk. 82, anazungumza kwa maana ya kuwa hiki kinamaanisha "upumbavu" na "upuuzi." Hiki kinatafsiriwa "simulizi za wanawake wazee" katika toleo la NRSV, NJB na "hekaya za wanawake wazee" katika toleo la NKJV.

Kwa kuwa pia namwamini Gordon Fee kwamba wanawake walikuwa wakitawaliwa na walimu wa oungo na walikuwa wakitumiwa kama wazungumzaji kupitia maoni yao katika makanisa ya nyumbani, na mtu anashangaa

1. Je! Kulikuwa na wanawake wazee watataua waliokuwa walimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 5:6)?
2. Je! Hii ni njia ya kuyaainisha matatizo yaliyowakumba wanawake?
3. Je! Hii ilikuwa nahau ya utamaduni wa utawala wa kibaba?

◙ Hili neno "hadithi" (NRSV, NJB) katika 1 Tim. 4:7 limekuwa likieleweka vibaya. Makala nzuri iko katika G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, sura ya 13, kr. 219-242. Hadithi zina uwezekano wa kuwa na maana nyinginezo.

◙ **"nawe ujizoeze kupata utauwa"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Neno "Maagizo," au "katika mafundisho," ni stiari ya kiziara ambapo tunalipata neno la Kiingereza "chumba cha mazoezi." Mafunzo ya kiriadha ni mfano mzuri wa bidii, kujitoa, kipaumbele cha juhudi kwetu ili kutusisimua sisis kama Wakristo katika ulimwengu wa roho ambao ni wa muhimu sana (kama vile 1 Kor. 9:24-27; 2 Tim. 2:5; 4:7; Ebr. 12:1-3).

◙ **"utauwa"**

## MADA MAALUM : UTAUWA

Hili ni neno la msingi katika barua za Kichungaji (yaani 1 Timotheo; 2 Timotheo; Tito). Linarejerea kwa vyote mafundisho na mtindo wa kila siku unaomaanishwa na injili. Inaelezea sio upekee bali kinachotarajiwa. Ni neno ambatani kutoka "njema" (*eu*) na "kuabudu" (*sebomai*). Ibada ya kweli ni kuishi kila siku kwa namna ya fikra sahihi (kama vile 1 Tim. 4:16a). Tazama mara ambazo neno hili linatumika katika Barua za Kichungaji:

1. nomino (*eusebeia*), 1 Tim. 2:2; 3:16; 4:7,8; 6:3,5,6,11; 2 Tim. 3:5; Tito 1:1
2. kielezi (*eusebēs*), 2 Tim. 3:12; Tito 2:12
3. kitenzi (*eusebeō*), 1 Tim. 5:4
4. Neno linalohusiana *theosebeia*, 1 Tim. 2:10
5. neno kanushi (KIAMBISHI AWALI HASI, yaani *asebeia*), 2 Tim. 2:16; Tito 2:12

**4:8** Mwili ni sehemu ya utumishi wetu katika maisha, lakini hauwekwi kipaumbele. Utauwa ndiyo kipaumbele! Kipenele hiki kingeweza kurejelea juu ya

1. mazoezi ya kimwili
2. maagizo ya kimwili
3. tendo la kujinyama anasa

Kile kiletao mabadiliko katika mwili ni muhimu, bali kile kiletahoo mabadiliko katika roho ni cha milele! Zoezi la kweli ni "nguvu kazi" na "mapambano" ya 1 Tim. 4:10! Huduma husababisha natokeo ya injili, bali kujinyima anasa hutoa msistizo wa mtu binafsi.

**4:9 "Ni neno la kuaminiwa"** Kifungu hiki kwa vyo vyote chaweza kuendana na mstari wa 8 au 10. Paulo anakitunia kifungu hiki mara kwa mara kusistiza semi muhimu katika Nyaraka za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 1:15; 3:1; 4:9; 2 Tim. 2:11; Tito 3:8), kama Yesu alivyolitumia neno "Amini, amini" au Paulo alivyokitumia kifungu "ndugu zangu sipendi msiwe na habari," katika maandiko yake ya awali (kama vile Rum. 1:13; 11:25; 1 Kor. 10:1; 12:11; 2 Kor. 1:8; 1 The. 4:13).

**4:10 "twajitaabisha na kujitahidi"** Hizi zote ni stiari za kiriadha. Herufi, ambayo kutokana na hiyo tunalipata neno la Kiingereza "masumbuko" au "sumbua," pia inapatikana katika Flp. 2:16; 1 Tim. 6:12; na 2 Tim. 4:7.
Kuna tofauti ya machapisho katika kifungu hiki:

1. MSS $א^{c}$, D, L, P, pamoja na Vulgate, Peshitta, na tafsiri za ki-Kikoptiki zenye kifungu "mateso ya fedheha" (NKJV)
2. $א^{*}$, A, C, F, G, K, na 075 yana neno"jitihada" (NASB, NRSV, TEV, NJB, NIV)

Toleo la UBS[4] linalipa neno hili "jitihada" daraja "C", kwa maana kwamba kamati ilikumbana na ugumu katika kuamua kati ya tofauti hizi.

**NASB "kwa sababu tunamtumaini "**
**NKJV "kwasababu tunatumaini katika hili"**
**NRSV "kwasababu tunalo tumaini lililokwishakuwapo"**

**TEV "kwasababu tumeliweka tumaini"**
**NJB "ya kwamba tumeliweka tumaini katika hili"**

Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Waamini wanaamini katika kitu kilichotulia, cha uhakika, sifsa ya Mungu isiyobadilika kama tumaini pekee (kama vile Zab. 102:26-27; Mal. 3:6; Ebr. 1:11-12; 13:8; Yakobo 1:17). Uhakika wa wokovu wetu umejikita katika sifa ya YHWH (kama vile 1 Tim. 6:17; Rum. 15:12; 2 Kor. 1:10).

◙**"Mungu aliye hai"** Nafikiri kuwa kifungu hiki cha Kiyunani kinamuakisi Mungu wa Agano la Kale aliyefanya agano. Hii ni asili ya maana ya neno "YHWH," ambalo linatokana na KITENZI cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kut. 3:14; tazama MADA MAALUM : MAJINA YA UUNGU katika 2 Tim. 1:2). YHWH anaishi daima, ndiye aishie pekee.

◙ **"aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio"** Hili jina "Mwokozi" linatumika mara kwa mara katika Nyaraka za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 1:1; 2:3; 2 Tim. 1:10; Tito 1:3-4; 2:10-13; 3:4,6). Katika sura za mwanzo za 1 Timotheo linatumika kumtaja Mungu kama Mkombozi, kwa uwezekano, wa wanadamu wote (kama vile 1 Tim. 2:4,6; Luka 2:11; Yohana 1:29; 4:42; Rum. 5:18-19; 2 Pet. 3:9). Tazama maelezo kamili katika 2 Tim. 1:10. Huenda ni kwa sababu ya vifungu hivi vichache "hasa kwa waamini" (ambapo mtu anazeweza kutarajia kithiolojia "pekee") hili linaweza kutumika katika maana yake ya Agano la Kale ya neno *Elohim*, ambaye ni "mlinzi" au "mtoaji" wa maisha yote ya duniani (kama vile Mt. 5:45; Matendo 17:28).

## MADA MAALUM : MPANGO WA YHWH WA UKOMBOZI WA MILELE

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31),wale wote walio umbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maangano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israeli, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.
Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anaunganisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani., iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israeli, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abrahamu ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israel. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihilisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Abraham, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, “kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu”). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama

vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakfisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43, 60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
    a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
    b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
    c. Mika 4:1-3
    d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa "agano jipya" (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna "moyo mpya," "mawazo mapya," na "roho mpya." Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimarisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.
1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani., ulioamuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni "fumbo la Mungu," lililofichika lakini sasa limedhihilishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya linaangazia juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israel ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumai utapata wasaa wa kusoma Mada Maalum: kwa nini ahadi za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti toka ahadi za Agano Jipya. Waweza kupata katika mtandao www.freebiblecommentary.org.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 4:11-16**
**11Mambo hayouyaagize na kuyafundisha. 12 Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi. 13Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha. 14Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee. 15Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. 16Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.**

**4:11 "uyaagize"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ya neno lenye maana ya "maagizo makali ya kijeshi" (kama vile 1 Tim. 1:3,18).

◙ **"na kuyafundisha"** Hii ni KAULI nyingine TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATAIA ULIOPO. Paulo anamsistiza Timotheo kuatilia maanani haya. Kanisa hili lilikuwa limevurugwa na walimu wa uongo na wawakilishi wao (yaani,. Huenda ni wajane vijana, kama vile 2 Tim. 3:6-7, au wajane wazee, kama vile 1 Tim. 4:7).

**4:12 "Mtu awaye yote asiudharau ujana wako"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO pamoja na KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI ambayo mara nyingi inamaanisha kustisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato. Hili neno "ujana" katika utamaduni wa Kirumi na Kiyunani hili lingeweza kumrejelea mtu mwenye umri zaidi ya miaka ya 40. Huenda walimu wa uongo waliuchagua umri wa Timotheo kama njia ya kuyashambulia au kuyakanusha mafundisho yake (kama vile 1 Kor. 16:11). Timotheo alikuwa kwa niaba ya utume wa Paulo. Paulo anamsistiza sana Tito katika namna ile ile iliyo katika Tito 2:15.

◙ **"bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi"** Ilimpasa Timotheo kuonyesha (KAULI YA KATI ULIOPO [yenye ushshidi] SHURUTISHI) kujizatiti kwake kwa ajili ua uongozi na maisha yake (kama vile 1 Tim. 4:6c na 7b). Ilimpasa kuishi kinyume hasa dhidi ya walimu wa uongo!

Kuna tofauti ya kimachapisho katika kifungu hiki. Toleo Textus Receptus liaongeza neno "katika pendo," "katika roho." Neno hili linapatikana katika machapisho ya herufi kubwa K, L, na P na pia katika machapisho ya jinsi ya kiume yaliyofuatia. Hata hivyo, hili limo katika MSS א, A, C, D, F, G, na Vulgate, ki-Shamu, na tafsiri za Koptiki, ambapo linamaanisha kuwa lilliongezwa na waandishi waliofuatia.

◙**"kielelezo"**

## MADA MAALUM : MUUNDO (*TUPOS)*

Neno *tupos* lina elimu-maana pana.

1. Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek New Testament*, uk. 645
   a. Sampuli
   b. mpango
   c. Mtindo au namna ya kuandika
   d. Amri ya serikali ama agizo litolewalo na mtawala
   e. Sentensi ama uamuzi
   f. Mfano wa mwili wa binadamu kama sadaka ya kuondoa nadhiri kwa Mungu anayeponya
   g. Kitenzi kilichotumika kwa maana ya kuongeza agizo au mwongozo wa sheria
2. Louw and Nida, *Greek-English Lexicon*, juzuu. 2, uk. 249
   a. Kovu (kama vile Yohana 20:25)
   b. Sura (kama vile Matendo 7:43)
   c. Fanya kwa mfano (kama vile Hebr. 8:5)
   d. Mfano (kama vile 1 Kor. 10:6; Flp. 3:17)
   e. Umboasili (kama vile Rum. 5:14)
   f. Aina (kama vile Matendo 23:25)
   g. Maudhui (kama vile Matendo 23:25)
3. Harold K. Moulton, *The Analytical Greek Lexicon Revised,* p. 411
   a. Kipigo, chapa, alama (kama vile Yohana 20:25)
   b. Eleza kinaganaga
   c. Sanamu (kama vile Matendo 7:43)
   d. Kanuni, mpango (kama vile Rum. 6:17)
   e. Muundo, kusudi (kama vile Matendo 23:25)
   f. Umbo, enye kufanana na kitu kingine (kama vile. 1 Kor. 10:6)
   g. Umbo tarajiwa, aina (kama vile Rum. 5:14; 1 Kor. 10:11)
   h. Sampuli mfano (kama vile. Matendo 7:44; Hebr. 8:5)
   i. Mfano adilifu (kama vile Flp. 3:17; 1 The. 1:7; 2 The. 3:9; 1 Tim. 4:12; 1 Pet. 5:3)

Kumbuka, msamiati hauweki maana; ni matumizi tu ya maneno kwenye sentensi/aya ndiyo yanaweka maana (yaani, muktadha). Kuwa mwangalifu kugawanya rasmi kundi la fafanuzi kwa neno na kulitumia kila mahali neno hilo linapotumika katika Biblia, muktadha huamua maana!

**4:13 "Hata nitakapokuja"** (kama vile 1 Tim. 3:14)

◙ **"ufanye bidii"** Hii ni KAULI nyingine TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Paulo anasistiza kazi tatu za kusanyiko kwa Timotheo kama kiongozi mkuu katika ibada za ushirika.

1. usomaji wa maandiko kwa pamoja

2. mahubiri
3. mafundisho

Kanisa la mwanzo liliuchukua msingi wa muundo wa ibada toka kwenye Sinagogi (kama vile Matendo 13:15; 15:21).

**4:14 "Usiache"** Hii ni KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye KIAMBATA HASI ambacho mara nyingi kinamaanisha kusitisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato. Je! mstari huu unamaanisha kuwa Timotheo aliikataa karama yake au hakupaswa kuikataa karama yake? Nafikiri ni kwa nujibu wa waraka.

◙ **"karama ile iliyomo ndani yako"** Kila mwanini amepewa karama ya kiroho ya mazungumzo (kama vile 1 Kor. 12:7,11,18). Katika muktadha huu, karama ya kiroho ya Timotheo ilikuja kutambuliwa na viongozi wa kanisa mama huko Listra (kama vile Matendo 16:2) na kuidhinishwa katika huduma malum ya kujitolea (kama vile 1 Tim. 1:18). Karama ya kiroho inatolewa na Mungu wa Utatu (kama vile 1 Kor. 12:4-6) kwa waamini pekee kwa ajili ya mambo yaliyo mema ya mwili wa Kristo (kama vile 1 Kor. 12:7,11). Wakati sahihi wa karama hautajwi bayana, idadi kamili ya karama haielezwi wazi, na ni njia kamili iliyotumika haiwekwi wazid. Jambo lililo dhahiri ni kwamba waamini wote wanakirimiwa kwa ajili ya huduma (kama vile Efe. 4:12).

◙ **"kuwekewa mikono"** Kifungu hiki kinaonekana kuwa tendo la kujitoa kwa dhati la Kanisa la Agano Jipya (kama vile Matendo 6:6; 13:3; 2 Tim. 1:6), ambalo walilichukua kutoka Agano la Kale (kama vile Hes. 8:10; Kumb. 34:9).

## MADA MAALUM: KUWEKEA MIKONO KATIKA BIBLIA

Hii ishara ya kujumuishwa inatumiwa sana katika njia mbalimbali katika Biblia.

1. kula kiapo (yaani mkono katika uvungu wa paja [kama vile Mwanzo 24:2,9; 47:29])
2. kuchukua uongozi wa familia (kama vile Mwanzo 48:14,17,18)
3. kutambua kifo cha dhabihu ya mnyama kama mbadala
    a. Makuhani (kama vile Kutoka 29:10,15,19; Law. 16:21; Hes. 8:12)
    b. kuwalaza watu (kama vile Law. 1:4; 3:2,8; 4:4,15,24; 2 Nyakati. 29:23)
4. mtu wa kukaa pembeni kumtumikia Mungu kwa ajili ya jukumu maalumu au huduma (kama vile Hes. 8:10; 27:18,23; Kumb. 34:9; Mdo. 6:6; 13:3; 1 Tim. 4:14; 5:22; 2 Tim. 1:6)
5. kushiriki katika kurusha mawe kwa kimahakama kwa kumpiga mwenye dhambi (kama vile Law. 24:14)
6. mkono katika mdomo wa mtu huashiria ukimya au tafakari (kama vile Waamuzi. 18:19; Ayubu 21:5; 29:9; 40:4; Mika 7:16)
7. Mkono wa mtu ukiwa katika kichwa chake humaanisha huzuni/ombolezo (2 Sam. 13:19)
8. kupokea Baraka za afya, furaha na utauwa (kama vile Mt. 19:13,15; Marko 10:16)
9. ikihusiana na uponyaji wa mwili (kama vile Mt. 8:3; 9:18,20; Marko 5:23; 6:5; 7:32; 8:23; 16:18; Luka 4:40; 13:13; Mdo. 9:17; 28:8)
10. kupokea Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 8:17-19; 9:17; 19:6, angalia Kumb. 34:9)

Kwa kushangaza kuna ukosefu wa mfanano katika vifungu ambavyo kihistoria vimekuwa vinatetea kuwekwa wakfu kwa viongozi kwa ajili ya kazi ya injili (yaani kuwekwa wakfu, angalia Mada Maalum: Kuwekwa Wakfu).

1. Katika Mdo. 6:6 Ni mitume wanaoweka mikono yao kwa ajili ya huduma ya watu saba ya kanisa la mahali pamoja.
2. Katika Mdo. 13:3 Ni Mitume na Walimu wanaoweka mikono juu ya Barnaba na Paulo kwa ajili ya huduma ya kimishenari.
3. Katika Mdo. 1 Tim. 4:14 Ni viongozi wa kanisa la nyumbani (wazee) waliojumuishwa katika wito wa kwanza na kuwekwa rasmi.
4. Katika 2 Tim. 1:6 Ni Paulo anayeweka mikono yake juu ya Timotheo.

Mtawanyiko na utata unaonyesha kukosekana kwa mpangilio katika kanisa la karne ya kwanza. Kanisa la kwanza lilikuwa zaidi katika kuendelea na kubadilika badilika na mara zote likitumia karama na vipawa vya roho vya waamini (kama vile Wakorintho 12; 14). Agano Jipya kwa ufupi tu limeandikwa kutetea au kushusha mfano

wa serikali (Angalia mtawanyiko huu katika Mdo. 15) au taratibu za kuwekwa wakfu. Mpangilio wa desturi za kikanisa ni muhimu lakini sio kibiblia. The Uuungu wa uongozi ni zaidi kiumuhimu kuliko mfumo ya uongozi (yaani dola).

◙ **"uliyopewa kwa unabii"** Je! kipengele hiki kinamaanisha kuwa karama ya kiroho ya Timotheo ilikuwa imetolewa

1. wakati alipowekwa wakfu kwa ajili ya huduma (kama vile 1 Tim. 1:14)
2. kwa maana ya unabii na kuwekea mikono (kama vile 2 Tim. 1:6)
3. Ya kwamba manabii waitambue karama yake na kumweka wakfu kwa ajili ya huduma (kama vile 1 Tim. 1:18)

Nafikiri #3 ni bora zaidi.

**NASB, NKJV "ya wazee"**
**NRSV "ya baraza la wazee"**
**TEV "wazee"**
**NJB, NIV "baraza la wazee"**

Yanipasa kukiri kwamba naleta mkanganyiko wa andiko hili. Ninao msingi wa kithiolojia dhidi ya "ukasisi/ulei" mara dufu ambao umeendelezwa katika Ukristo. Naamini kwamba waamini wote wameitwa na kukirimiwa kwa ajili ya ukomavu na huduma (kama vile 1 Kor. 12; Efe. 4:11-12). Waamini ni watakatifu na ni wa huduma!

Dhana ya Marekebisho ya "makuhani wa mwanini," iliyotajwa na Martin Luther kwa mara ya kwanza, inakosa hoja ya kibiblia — waamini wote wanatenda kazi kama makuhani (kama vile Kut. 19:5-6; Hes. 16:3). Kibiblia hii lazima iwe "ukuhani wa waamini"!

Na sasa katika kulizungumzia hili nimetambua kwamba Mungu huwaita waamini kwa ajili ya kuwaongoza waamini. Hakuna swali kwamba wengine wanaitwa na kuwakifishwa kwa ajili ya kuongoza, kuelekeza, kutia hamasa, kutia moyo, na kuwakusanya watu wa Mungu.

Hata hivyo, viongozi hawa si waamini maalum, au waamini waliopendelewa, bali ni viongozi watumishi (kama vile Mt. 18:1-4; 20:20-28; 23:11). Desturi za sasa zinalenga kizifedhehesha kweli kazaa za kibiblia:

1. waamini wote ni watumishi wa wahudumu
2. waamini wote wamekirimiwa kwa ajili ya huduma

Desturi za sasa zimeendelezwa kutokana na ukubalifu wa karama usio rasmi na shauku ya yenye kutenda kazi kwa ajili ya kazi ya huduma fulani katika maelezo, kiwango cha juu cha usomi! Dhana hii lazima ibadilishwe; mfano huu lazima uthamanishwe upya; uendelezwaji huu wa kibiblia lazima ubadilishwe. Ukristo wa sasa unejikita sana katika desturi na katika usomi kuhusu hii misingi midogo ya kibiblia. Na sasa mamlaka iko wapi, katika vifungu dhahiri vya Agano Jipya au desturi za kimadhehebu?

**4:15**
**NASB "Uyatafakari hayo"**
**NKJV "Uyazingazitie mambo haya"**
**NRSV "Uyatendee kazi mambo"**
**TEV "uyatendee kazi mambo haya"**
**NJB "Litunze hili**

Hii ni KAULI nyingine TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Katika Agano la Kale la Kiebrania neno hili lilitumika kumaanisha tendo la kupatanisha (kama vile Isa. 33:18; Matendo 4:25). Katika Agano Jipya neno hili linaonekana kuwa na maana dhahiri ya tendo la kutumia nguvu nyingi.

**NASB "ukae katika hayo"**
**NKJV "jikite katika hayo"**

**NRSV, TEV** **"jitolee kwa ajili ya ayo"**
**NJB** **"kazi yako"**

Hii ni KAULI nyingine SHURUTISHI. Hii inamaanisha "kujiingiza katika mafundisho haya." Haya na yawe kipaumbele katika maisha yako na huduma. Kweli ya Mungu huitaji tabia fulani iliyo dhahiri na yenye kuthibitika katika maisha yetu katika namna fulani ambayo wengine wanaweza kumuona Kristo ndani yetu!

◙ **"ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote"** Kumbuka kwamba ilimpasa Timotheo kuishi na waamini na wasio waanimi ili isiwepo nafasi ya kuipinga injili au huduma yake (kama vile 1 Tim. 3:2,7,10; 5:7,8,14; 6:14). Ukinzani halisi wa mwendelezo huu katika utauwa unaonekana ndani ya walimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 2:16 na 3:9).

**4:16 "Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako"** Hapa bado kuna KAULI nyingine TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Ilimpasa Timotheo kuutumia muda wake kwa ukomavu na uendelezji wake wa kiroho. Hili ni neno jema kwa wachungaji wa nyakati zetu (kama vile 1 Tim. 4:6c; 7b; 12b).

◙ **"Dumu katika mambo hayo"** Hii ni KAULI nyingine TENDAJI SHURUTISHI. Pia ilimpasa Timotheo kuwa mfano wa ustahimilivu kwa sababu walimu wa uongo na wafuasi wao kwa namna iliyo dhahiri walikuwa hawastahimiliki. Wokovu unaungamanishwa si si katika ukiri wa awali wa toba, imani na utauwa, bali pia kuendelea katika mambo hayas. Ustahimilivu ni uthibitisho wa wokovu wa kweli! Katika biblia Ukristo ni namna mtu anavtyoanza, anavyoishi, na namna anavyomaliza haya yote ni ya kweli!

## MADA MAALUM : HITAJI LA UVUMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kilahaja (angalia Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milingnyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Msharike walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana na au kukushifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwitikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahusuyo uhakika
   a. semi za Yesu katika Inili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
   b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 Thes. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
   c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahusuyo umuhimu wa ustahimilivu
   a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
   b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
   c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
   d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
   e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kma vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba,

katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, The Word of Truth, Eerdmans, 1981 (kr. 348-365)
2. Howard Marshall, Kept by the Power of God, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, Life in the Son, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumika, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashujghulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumika kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabuj cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5
- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 Thes. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote vya nyakati: kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito.

◙ **"maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia"** Kifungu hiki kinaweza kuhusiana na mstari wa 10 au walimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 2:15). Mara nyingi Paulo anahofu kwamba kwa kujilinda mwenyewe kungemfanya kuwa na woga ambapo angepoteza sifa (kama vile 1 Kor. 9:27).

Tazama MADA MAALUM : WOKOVU (VITENZI VYA NYAKATI ZA KIYUNANI) katika2 Tim. 1:9.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! walimu wa uongo ni Wakristo? Waliendelea kuwa Wakristo
2. Kwa nini tendo la kujinyima na kujitesa lilikuwa hatari kwa Kanisa?
3. Je! Mstari wa 10 unamaanisha nini? Je! kila mtu ataokolewa nyakati za mwisho?
4. Ni kwa namna gani Timotheo ilimpasa kuwa kuushinda ujana wake?

# 1 TIMOTHEO 5

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Majukumu ya Kuwajali wengine | Kuwajali watu wa Kanisa | Mchungaji na Kundi | Majukumu ya Kuwajali Waaminio | Shughuli za Kichungaji |
| 5:1-2 | 5:1-2 | 5:1-2 | 5:1-2 | 5:1-2 |
| | Waheshimu Wajane | | | Wajane |
| 5:3-16 | 5:3-16 | 5:3-8 | 5:3-8 | 5:3-8 |
| | | 5:9-16 | 5:9-10 | 5:9-16 |
| | | | 5:11-16 | |
| | Waheshimu Wazee | | | Wazee |
| 5:17-23 | 5:17-23 | 5:17-22 | 5:17-22 | 5:17-22 |
| | | 5:23 | 5:23 | 5:23 |
| 5:24-6:2a | | 5:24-6:2a | 5:24-25 | 5:24-25 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kwa ufahamu mpana wa mazingira ya kihistoria ya kitabu, maneno haya ya ushauri wa kichungaji yawezekana pia yanachagizwa na matendo ya walimu wa uongo
   1. matatizo na wajane (1 Tim. 5:3-16)
   2. matatizo na wazee (1 Tim. 5:17-25)
   3. matatizo na watumwa (1 Tim. 6:1-2a)
   4. matatizo na walimu wa uongo (1 Tim. 6:2b-10)
      a. mafundisho
      b. wingi wa mali
B. Kuna maneno matatu yanayotumika katika kipengele hili kwa namna mbili tofauti
   1. "mzee"
      a. mwanaume mzee (1 Tim. 5:1)
      b. kiongozi wa kanisa la nyumbani (1 Tim. 5:17)
   2. "mjane"
      a. mwanamke anayesalia katika ndoa aliyesaidiwa na kiongozi wa kanisa (1 Tim. 5:3-8)
      b. kipengele maalumu cha mfanyakazi wa kike wa kanisa aliyeajiliwa na kanisa (1 Tim. 5:9-16)
   3. "heshima"

a. adhama (1 Tim. 5:3, 17)
b. mshahara (1 Tim. 5:3, 17)
c. au vyote

C. Kwa namna fulani Sura ya 5 inahusiana na sura ya 3. Ile "wazee" ya 1 Tim. 5:17 inarejerea "waangalizi" wa 1 Tim. 3:1 na ya wajane "orodha" (kunja) ya 1 Tim. 5:9 inarejerea "wanawake" wa 1 Tim. 3:11.

Natambua kwamba tofauti hii kati ya wajane wanaosaidiwa na kanisa (1 Tim. 5:3-8) na wajane wanaolitumikia kanisa inaonekana kukuzwa, lakini hizi hapa ni sababu za kuwa na maoni haya.

1. Sifa za wajane ni ngumu (kama vile 1 Tim. 5:5,9-10). Je hii inamaanisha kwamba kanisa linasaidia wajane maalum tu?
2. Ile "orodha" ya 1 Tim. 5:9 inaonekana kuwa orodha maalumu ya wajane.
3. Ile "orodha" (kama vile 1 Tim. 5:9) au ahadi (kibayana "imani ya kwanza") katika 1 Tim. 5:12 inamaanisha zaidi ya ahadi ya kutooa. Kwanini kuolewa tena kuwe tatizo? Ingemuondoa mjane kutoka katika uhitaji wake kwa kanisa lakini vipi kama ingekuwa mkataba kwa ajili ya ajira ya kanisa? Kwa namna hii kanisa lilisaidia wahitaji (yaani mishahara)**,** lakini bado pia walipata huduma (yaani kutumikia wanawake wengine).
4. Mjadala wa "wazee," ambao unaanza katika 1 Tim. 5:17, inahusisha msaada uliolipiwa na kanisa.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 5:1-2**
**1 Mzee usimkemee, bali umwonye kama baba; na vijana kama ndugu; 2wanawake wazee kama mama; wanawake vijana kama ndugu wa kike; katika usafi wote.**

**5:1 "usimkemee"** Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU IKIWA NA KIAMBATA KANUSHI ambayo siku zote inamaanisha kuanza kitendo. Hili ni neno lenye nguvu la Kiyunani (linalotumika hapa tu), ambalo kibayana linamaanisha "kupiga kofi" (kama vile 1 Tim. 3:13). Wakristo lazima watende tofauti, lazima watende katika upendo wakiwa na mtazamo wa usuluhishi. Ushauri huu unaweza kuaksi onyo la Agano la Kale kuheshimu wazee katika Law. 19:32.

◙**"Mzee"** Hili neno kibayana "mzee" (*presbuteros*). Kuna namna mbili ambayo neno hili linatumika katika muktadha huu:

1. kwa ajili ya mwanaume mzee (1 Tim. 5:1)
2. kwa nafasi ya uongozi katika makanisa ya makanisa ya nyumbani (1 Tim. 5:17 kama vile 1 Pet. 5:1,5)

## MADA MAALUM: MZEE

I. Matumizi ya Agano la Kale
   A. lilitumika na malaika wa Mungu aliyetengeneza baraza la kimalaika (BDB 278, KB 278, kama vile Isa. 24:23). Msamiati huo huo unatumika juu ya viumbe vya kimalaika katika Ufunuo (kama vile Ufunuo 4:4, 10; 5:5,6,8,11,14; 7:11,13; 11:16; 14:3; 19:4).
   B. Lilitumika na viongozi wa makabila wakati wa Agano la Kale (kama vile Kut. 3:16; Hes. 11:16). Baadaye katika Agano Jipya neno hili linatumika kwa kikundi cha viongozi kutoka Yerusalemu waliokuwa wakitengeneza mahakama ya Kiyahudi, baraza la Sinagogi (kama vile Mt. 21:23; 26:57). Katika Siku za Yesu hili baraza la watu sabini liliendeshwa na ukuhani ulioharibika (yaani wasiotoka katika uzao wa Haruni bali mabwana wa Kirumi walionunuliwa).

II. Matumizi ya Agano Jipya
   A. Lilitumika na viongozi wa wa maeneo wa kanisa la Agano Jipya. Lilikuwa ni moja ya maneno kati ya matatu yaliyokuwa na matumizi ya kufanana (mchungaji, mwangalizi, na mzee, kama vile Tito 1:5,7; Mdo. 20:17,28). Petro na Yohana wanalitumia kujijumuisha wenyewe katika kundi la uongozi (kama

vile 1 Petro 5:1; 2 Yohana 1; 3 Yohana 1).

B. Kuna mzaha juu ya neno mzee (*presbuteros*) katika 1 Pet. 1:1 na 5. Neno inavyoonekana lilitumika kama cheo cha uongozi (kama vile mstari wa 1) na maelezo ya umri (kama vile mstari wa 5). Matumizi ya neno hili yanashangaza ukizingatia kwamba msingi ni maelezo ya kikabila ya uongozi wa Kiyahudi, wakati "askofu" au "mwangalizi" (*episcopos*) yalikuwa maelezo ya uongozi wa mji wa Kiyunani. 1 Petro anatumia majina ya Kiyahudi kuzungumza na waaminio wa mataifa.

Petro anajiita mwenyewe "mzee mwenzenu," Neno *presbuteros* pamoja na KIELEZI *syn*, ambacho kinamaanisha "ushirika wa pamoja." Petro haelezei mamlaka yake ya Kitume (kama vile 2 Yohana 1, ambapo Mtume mwingine anajiita mwenyewe "mzee"), lakini anaonya (yaani "Nakuonya," KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO) viongozi wa maeneo kutenda na kuishi kwa utaratibu kwa kuzingatia

1. Mfano wa Kristo
2. Ukaribu wa kurudi kwake

Makanisa ya kwanza hayakuwa na nafasi za kiuongozi ambazo walikuwa wakilipwa bali walitambua karama walizopewa na Mungu juu ya huduma na uongozi ndani ya kanisa la mahali. Ukiri huu wa kipawa ulitakiwa kuwianishwa na heshima ya kidesturi kwa "hekima-ya uzeeni," hasa kati ya jamii ya wayahudi waaminio. Hivyo Petro anazungumza na aina zote mbili za uoungozi.

Pia tambua kwamba "wazee" ni WINGI. Hii inaweza kurejerea kwa (1) hesabu ya viongozi wa makanisa ya nyumbani (kama vile Mdo. 20:17) au (2) karama tofauti za kiroho kati ya mwili wa viongozi (kama vile Efe. 4:11), ambalo hasa linazungumza kiuwazi kwamba huduma ni mali ya waaminio wote. Hii inaendana na dhana ya "ufalme wa makuhani" (kama vile 1 Pet. 2:5,9).

C. lilitumika kwa wanaume wazee katika kanisa, sio lazima wawe viongozi tu (kama vile 1 Tim. 5:1; Tito 2:2).

## MADA MAALUM: KUZEEKA KWA MWANADAMU

I. Utangulizi

A. Nukuu kutoka Christian Life Commission magazine juu ya "A Future for the Family," 1973, p. 16, cha L. D. Johnson, entitled "Hebrew-Christian Geriatrics":

"Mitazamo yetu juu ya uzee, inayoaksiwa na tabia zetu ukitofautisha na mazungumzo yetu, inapendekeza kwamba tuifuate Biblia zaidi kwa shauku kuliko kuitii tu. Yawezekana hakuna jamii kati ya watu waliostaarabika wanaonesha kutojali wazee kama sisi. Sisi ni waumini wa Ujana. Tunajitoa kwa ajili ya vijana, tunawajali na kuwalinda kupita kiasi, tunawashirikisha, tunawatamani na kujipumbaza wenyewe tukijaribu kuwaiga wao. Thamani yetu kubwa kupita vyote kwa vijana ni umri wetu mdogo. Na bado ushenzi wa aina hiyo uliogeuzwa chini juu wa mfumo wetu wa thamani unaendelea kuwa dhahiri. Moja kati ya sita kati ya mmoja wetu katika ulimwengu wa magharibi yuko umri zaidi ya sitini na asilimia inapanda."

B. Tamaduni zetu zimetofautiana kwa sehemu kubwa sana katika namna wanavyowachukulia wazee wao:

1. Desturi za kimagharibi wameonesha heshima kubwa sana na kujali wazee wao.
2. desturi za Wamarekani wenye asili ya India wamewatelekeza wazee wao wafe.

C. Kuna baadhi ya miongozo ya kibiblia ya kutusaidia sisi katika eneo hili.

II. Nyenzo za Kibiblia

A. Agano la Kale

1. Umri ni Baraka ya kiungu kwa ajili ya kutembea katika agano.

a. Mithali 16:31
b. Mwanzo 15:15
c. Kutoka 20:12; Kumb. 6:2; 22:6-7; 25:15
d. Ayubu 5:17-26 (hasa mstari wa 26)
e. Zaburi 91:14-16
f. Zaburi 92:1-15 (hasa mistari ya 14-15)

2. Hata umri wenye baraka bado una matatizo ya aina yake
   a. Jedwali la maelezo ya umri wa uzee inapatikana katika Muh. 12:1-5
   b. Isaka alikuwa haoni vizuri, Mwa. 27:1
   c. Yakobo alikuwa haoni vyema, Mwa. 48:10
   d. Eli hakuwa haoni vizuri, 1 Sam. 3:2
   e. Barzillai alikuwa na tatizo la kutosikia vyema na kupoteza ladha ya chakula, 2 Sam. 19:31-35
   f. Daudi alikuwa na mzunguko mbaya wa damu, 1 Wafalme 1:1-4
   g. alikuwa na macho yasiyoona vyema, 1 Wafalme 14:1
3. Mungu huwa hatuachi sisi, hata katika uzee.
   a. Zab. 37:23-26
   b. Zab. 71:9,18
   c. Zab. 73:24
4. Umri kwakuwa ni ishara ya Baraka za Mungu, unatakiwa kuheshimiwa.
   a. Walawi 19:32
   b. Ruth. 4:15
   c. Mith. 23:22
   d. Kukosa heshima kutafanya kuhukumiwa.
      (1) Kumb. 28:50
      (2) 1 Samweli 2:31-32
      (3) Isaya 3:5
      (4) Omb. 4:16; 5:12
   e. Hekima ya Sulemani, 2:10
   f. Hekima ya Bin Sira (Ecclesiasticus) 8:6
5. Umri wenye Baraka huleta hekima na utambuzi
   a. 1 Wafalme 12:8
   b. Ayubu 12:12,20
   c. Ayubu 15:10
   d. (Ecclesiasticus 25:6)
   e. Kuna upekee
      (1) Ayubu 32:6 na kuendelea
      (2) Muh. 4:13
6. Ni umri upi unaoitwa uzee?
   a. Walawi 27:1-8, miaka 60
   b. Zab. 90:10, umri wa kawaida - 70, umri mzuri – 80
   c. Isaya 65:20, miaka 100
   d. Ecclesiasticus 18:9 – miaka 100

B. Agano Jipya - 1 Timotheo
1. nafasi ya wajane, 5:3 na kuendelea (yaani wajane juu ya miaka 60 waajiliwe na kanisa)
2. mtazamo juu ya mtu mzee, 3:1-2
3. waaminio wanawajibika kutunza familia zao, 3:8

III. Baadhi ya Mapendekezo ya kufanyia kazi

A. Wafundishe watoto wako kuheshimu watu wazee (utahitaji hili siku moja wewe mwenyewe!).
B. Fanya uwe mradi wa familia kuwasiliana na wajumbe wazee wa familia yako. Ikiwezekana wapigie simu au waandikie ndugu hao hasa wakati wa mapumziko.
C. Fanya ziara kwa jirani mzee au nyumba wanakotunzwa. Watie moyo na kanisa lako kutengeneza eneo kwa ajili ya wazee na kuwatembelea mara kwa mara.
D. Tafta muda kwa ajili ya watoto wadogo kupata muda na bibi na babu zao kiasili au hata kwa "kuasilisha."
E. Hamasisha makanisa mengine kutengeneza Huduma kwa ajili ya Watu wa makamu na wenye umri mkubwa. Tafta mtu wa kuratibu.
F. Wewe mwenyewe binafsi anza kupanga sasa na kujiandaa kwa ajili ya kustaafu.

◙**"bali umwonye kama baba"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Msisitizo wa Paulo kwa ajili ya Timotheo kuwajali watu wa makanisa ya nyumbani kama wanafamilia wa karibu (kama vile Marko 3:31-35). Heshima na adhama "wakina baba na wakina mama" inaweza kuaksi Amri Kumi (kama vile 1 Tim. 5:4).

**5:2 "wanawake vijana kama ndugu wa kike; katika usafi wote"** Kwasababu ya (1) Umri wa Timotheo na (2) unyanyasaji wa kingono wa walimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 3:6), Paulo hasa alikuwa makini kuweka kiashiria cha usafi kwa mahusiano ya wanawake vijana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 5:3-8**
**[3]Uwaheshimu wajane walio wajane kweli kweli. [4]Lakini mjane akiwa ana watoto au wajukuu, na wajifunze kwanza kuyatenda yaliyo wajibu wao kwa jamaa zao wenyewe, na kuwalipa wazazi wao. Kwa kuwa hili lakubalika mbele za Mungu. [5] Basi yeye aliye mjane kweli kweli, ameachwa peke yake, huyo amemwekea Mungu tumaini lake, naye hudumu katika maombi na sala mchana na usiku. [6]Bali, yeye asiyejizuia nafsi yake amekufa ingawa yu hai. [7]Mambo hayo pia uyaagize, ili wasiwe na lawama. [8]Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.**

**5:3 "Uwaheshimu wajane"** Neno "heshima" katika 1 Tim. 5:3 na 17 inaweza kuashiria mshahara au mapato yaliyotolewa na kanisa
1. kwa wajane walio wahitaji (kama vile 1 Tim. 5:3-8)
2. kwa wasaidizi wanawake maalumu (kama vile 1 Tim. 5:9-16)
3. kwa wazee (kama vile 1 Tim. 5:17-22)

Inaonekana kwamba kanisa kwa kufuata Agano la Kale na Sinagogi (kama vile Kumb. 24:17-22; Kut. 22:22-24; Isa. 1:17; Mdo. 6:1 na kuendelea; 9:39,41), walijali wajane. Ilikuwa hofu ya Paulo kwamba wale waliokuwa wakisaidiwa na kanisa walikuwa wahitaji wa kweli au hawakuwa na familia zao wenyewe za kuwasiadia (kama vile 1 Tim. 5:4,16). Walimu wa uongo waliwanyonya wajane (kama vile 1 Tim. 5:6,15). Paulo aliwaonya kanisa kusaidia wajane wa kweli.

**5:4 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YA DARAJA LA KWANZA LENYE MASHARTI (kama ilivyo katika 1 Tim. 5:8). Kulikuwa na wajane waliokuwa wameachwa na familia zao wenyewe (kama vile 1 Tim. 5:8,16).

◙**"Kwa kuwa hili lakubalika mbele za Mungu"** Hii yawezekana inarejea kwa Amri Kumi kuhusu kuheshimu baba na mama (kama vile Kut. 20:12), kwa namna hii ni mama mjane. Katika Agano la Kale Mungu anawatetea wadhaifu kijamii na wasio na nguvu. Kilio cha kutetea "mjane, yatima na mgeni" inafanyika tabia hapa kama tungo ya Kumbu kumbu la Torati (ikirudiwa katika Yeremia).

Waaminio wanaonesha upendo wao kwa YHWH kwa kuheshimu neno Lake na mapenzi kwa kuendeleea kutunza ushirika wa kifamilia na majukumu.

**5:5"Basi yeye aliye mjane kweli kweli, ameachwa peke yake"** Hii ni tungo ile ile nadra ya kisarufi kama 4:3 (KIVUMISHI NA KAULI ENDELEVU, kama vile Tito 1:15). Mtu anaweza kushangaa ikiwa hii ilikuwa alama ya kisarufi ya mwandishi ambayo Paulo aliitumia katika barua za Kichungaji. Paulo anatoa miongozo dhahiri katika siku zake juu ya sifa ya kupata msaada kutoka kwa kanisa (lakini sio katika "orodha" ya 1 Tim. 5:9):

1. NJEO YA WAKATI TIMILIFU – ana na anaendelea kuishi peke yake
2. NJEO YA WAKATI TIMILIFU – anaendelea kuwa mwanamke mtauwa
3. NJEO YA WAKATI TIMILIFU – anaendelea kukimbia tama za duniani kwa namna ya maombi endelevu

Anna (Luka 2:37) na Dorcas (Mdo. 9:36) (ingawa haitajwi kibayana juu ya yeye kuwa mjane), angekidhi hivi vigezo.

**5:6**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"bali yaya anayejishughulisha katika starehe"** |
| **NKJV** | **"bali yeye aishiye katika starehe"** |
| **NRSV** | **"aishiye katika starehe"** |
| **TEV** | **"ajitoaye mwenyewe katika starehe"** |
| **NJB** | **"yeye anayefikiri tu katika starehe"** |

Kwasababu hali ya kimila hii inaweza kurejerea

1. wajane wakigeukia ukahaba kama namna ya kupata kipato
2. unyasanyasi wa kingono wa walimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 3:5-7)

Hii inaonekana kuwa onyo kali (kama vile 1 Tim. 5:15).

Neno hili hili linatumika katika Yakobo 5:5.

◙**"amekufa ingawa yu hai"** Hii inarejerea hali ya kifo cha kiroho (KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI MTIMILIFU). Mstari huuu unaelezea wajane katika makanisa ya nyumbani ya Efeso! Walimu wa uongo sio tu kwamba walileta juu yao wenyewe "vifo," lakini sasa wanalazimika kiroho kwa ajili ya "vifo" vya wengine.

**5:7**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"yaagize mambo haya"** |
| **NKJV** | **"mambo haya yaamuru"** |
| **NRSV** | **"amuru mambo haya"** |
| **TEV** | **"wape maelekezo haya"** |
| **NJB** | **"waelekeze katika hili"** |

Neno hili linarejerea "amri kali za kijeshi" (kama vile 1 Tim. 1:3,18; 4:11). Haya hayakuwa mapendekezo! Hivi havikuwa vitu vya kiupendeleo vya kibinafsi.

◙**"uyaagize, ili wasiwe na lawama"** Ile "wao" inaonekana kurejerea ndugu wa wajane waishio na familia. Hii ilikuwa na ni wito sahihi kwa ajili ya waaminio wote. Yeyote anayeshindwa kukidhi mahitaji yake mwenyewe hasa familia yake ya karibu ameikana imani yake mwenyewe na katika macho ya jamii ni mbaya kuliko asiyeamini (1 Tim. 5:7,8). Hii inaaksi mafundisho ya Yesu katika Marko 7:9-13. Hii inaonekana kuhusiana na msisitizo wa kuendelea juu ya kutovumilia ukosoaji, vyote kwa waaminio na wasioamini (kama vile 1 Tim. 3:2,7,10; 5:7; 6:14). Wakristo lazima siku zote waishi ili kuwavuta wengine kuiijia imani katika Kristo. Upande chanya wa hili unaonekana katika mstari wa 4, wakati hii ni hasi. Angalia MADA MAALUM: SIFA ZA WAFANYAKAZI WA KANISA WA KIKE katika 1 Tim. 3:12.

**5:8 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YA DARAJA LA KWANZA LENYE MASHARTI ikimaanisha baadhi ya waaminio wameacha familia zo (kama vile 1 Tim. 5:4,16)

◙**"ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini"** Naamini hii inarejerea ushuhuda wa mtu katika jamii (kama vile 1 Tim. 5:7; 3:4-5), sio kwa ajili ya wokovu. Hata wasioamini wanasaidia familia zao wenyewe. Hatahivyo kuna maandiko mengine yanayotumia neno hili hili "kukataa" na kumaanisha kukataliwa moja kwa moja na

Mungu (kama vile 2 Tim. 2:12; Tito 1:16; 2 Pet. 2:1; Yuda 4). Katika muktadha huu inaweza kwa sehemu fulani kuhusiana na matendo au mafundisho ya walimu wa uongo "walioanguka katika imani" (kama vile 1 Tim. 1:19-20; 4:1-2; 6:9-10,20-21) au wafuasi wao (kama vile 1 Tim. 5:6,15). Angalia MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 5:9-16**
**9Mjane asiandikwe isipokuwa umri wake amepata miaka sitini; naye amekuwa mke wa mume mmoja;**
**10naye ameshuhudiwa kwa matendo mema; ikiwa amelea watoto, ikiwa amekaribisha wageni, ikiwa amewaosha watakatifu miguu, ikiwa amewasaidia wateswao, ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema.**
**11Bali wajane walio vijana ukatae kuwaandika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo, wataka kuolewa; 12 nao wana hukumu kwa kuwa wameiacha imani yao ya kwanza. 13Tena, pamoja na hayo, hujifunza kuwa wavivu, wakizunguka-zunguka nyumba kwa nyumba; wala si wavivu tu, lakini ni wachongezi na wadadisi, wakinena maneno yasiyowapasa. 14Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, wawe na madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu. 15Kwa maana wengine wamekwisha kugeuka na kumfuata Shetani. 16Mwanamke aaminiye, akiwa ana wajane, na awasaidie mwenyewe, Kanisa lisilemewe; ili liwasaidie wale walio wajane kweli kweli.**

**5:9 "Mjane asiandikwe isipokuwa umri wake amepata miaka sitini"** Hii ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA KANUSHI. Hapa ni sifa nyingine kwa ajili ya wajane waliokuwa sehemu ya timu ya huduma. Neno "orodha" ni neno la Kiyunani "orodha ya kisheria" Wajane' Orodha ya wajane inaweza kufanana na dhana ya "mashemasi wa kike" (kama vile 1 Tim. 3:11; Rum. 16:1). Hata hivyo "Katiba za Kitume," zilizoandikwa mwanzoni mwa karne ya pili ilitaja vipengele vitatu vya wahudumu wa kike: wanawali, mashemasi wa kike na wajane.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kuwa mke wa mume mmoja"** |
| **NKJV** | **"mpaka awe kwamba alikuwa mke wa mume mmoja"** |
| **NRSV** | **"na amekuwa katika ndoa mara moja"** |
| **TEV** | **"kwa kuongezea awe ameolewa mara moja"** |
| **NJB** | **"ambaye amekuwa na mume mmoja"** |

Kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya nini kinamaanishwa na tungo hii (kama vile 1 Tim. 3:1,12). Lakini ni dhahiri kwamba chochote kinachomaanishwa, lilikuwa ni jambo la makanisa ya nyumbani ya Efeso na Krete (kama vile 1 Tim. 3:1,12; 5:9; Tito 1:6). Familia zenye nguvu za kitauwa zilikuwa (na ndivyo zilivyo) ushuhuda wa nguvu kwa ulimwengu uliopotea.

Kwa mjadala kamili angalia 3:2. Katika 1 Tim. 5:14 wajane vijana wanaonywa kuhusu kuolewa tena. Hii inaonekana kumaanisha kwamba ndoa ya pili ilionekana kama dhambi (kama vile Rum. 7:2-3; 1 Kor. 7). Katika mizunguko ya ya Wabatisti wa Ulaya hii "mume wa mke mmoja" au "mke wa mume mmoja" imekuwa ikifasiriwa kama kukataliwa kibiblia kwa ndoa ya pili hasa kwa wachungaji. Hatahivyo hii haikuwa hivyo kwa mila na desturi za mashariki ya kati. Hii nadharia inaaksi ukuaji wa upole wa kanisa la kwanza lakini zuio wa Agano Jipya. Mtazamo wa Wayunani (yaani mwili ni uovu) ulileta athari chanya kwa makanisa ya kwanza ya Mataifa.

**5:10"ameshuhudiwa kwa matendo mema"** Kuna matendo mazuri matano ya kibayana yanayotajwa (yote ni SENTENSI YA DARAJA LA KWANZA LENYE MASHARTI) kwa ajili ya kumbukumbu ya 1 Tim. 5:10. Angalia Mada Maalum: Sifa za wafanyakazi wanawake wa kanisa katika 1 Tim. 3:12. Hizi kazi njema zinaaksi kazi ya mwanamke itarajiwayo katika jamii yake.

◙**"ikiwa"** Huu ni mfuatano wa SENTENSI YA DARAJA LA KWANZA LENYE MASHARTI katika 1 Tim. 5:10, ambayo kila moja inaashiria sifa za mjane anayetakiwa kuajiliwa na kanisa.

◙**"amelea watoto"** Hii haimaanishi kwamba mwanamke asiye na watoto hatakiwa kupewa msaada bali kwamba kama likuwa na watoto lazima wawe watauwa. Huu ni msisitizo unaojirudia rudia (kama vile sura ya 3) juu ya familia yenye nguvu, yenye utauwa na aminifu.

◙**"ikiwa amekaribisha wageni"** Hii hairejerea kwa kumkaribisha yoyote katika nyumba ya mtu bali kumpa hifadhi kiongozi wa Kikristo anayesafiri.

◙**"ikiwa amewaosha watakatifu miguu"** Hili lilikuwa ni tendo la watumishi wa nyumbani kupokea wageni. Yesu alifanya hivi kwa ajili ya wanafunzi wake mwenyewe ili kuwafundisha unyenyekevu (kama vile Yohana 13). Hapa inaonekana kuwa sitiari kwa ajili ya huduma ya kipole (na yawezekana ukarimu wa kimila unaotegemewa).

## MADA MAALUM: WATAKATIFU (*hagios*)

Huu ni usawa wa Kiyunani wa neno la Kiebrania *kadosh* (NOMINO, BDB 871; KITENZI, BDB 872, KB 1066-1067; tazama Mada Maalum: Takatifu), lililo na maana ya msingi ya kumweka mtu katia usawa, kitu fulani, au baadhi ya sehemu tofauti na matumizi ya YHWH yaliyojitenga. Hili linadokeza dhana ya Kiingereza ya "wekwa wakfu." Israeli lilikuwa "taifa takatifu" la YHWH (kama vile 1 Pet. 2:9, ambayo inanukuu Kut. 19:6). YHWH anaweka mbali na ubinadamu kwa kutumia asili Yake (milele, Utatakatifu usioumbwa) na sifa Yake (ukamilifu wa maadili). Yeye ni kipimo ambapo vitu vyote vinapimwa na kuhukumiwa. Yeye yu kila mahali, Mtakatifu, Mtakatifu wa Watakatifu.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa ushirika, lakini anguko (Mwanzo 3) lilisababisha kikwazo cha mahusiano na maadili kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi. Mungu alichagua kuurejesha ufahamu Wake wa uumbaji; hivyo, Anawaita watu Wake kuwa "watakatifu" (kama vile Law. 11:44; 19:2; 20:7,26; 21:8). Kwa imani uhusianao wa YHWH na watu Wake ukawa mtakatifu kwa nafasi zao za kiagano ndani Yake, lakini pia wanaitwa kuishi maisha matakatifu (tazama Mada Maalum: Utakaso, kama vile Mt. 5:48; Efe. 4:1,17; 5:2-3,15; 1 Pet. 1:15).

Huku kuishi kitakatifu kunawezekana kwa sababu waamini wamekubaliwa kwa utimilifu na kusamehewa kupitia (1) Maisha ya Yesu na (2) kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ndani ya fikra na mioyo yao. Hili linahimarisha hali ya ukinzani kwa waamini:

1. kuwa watakatifu kwa sababu ya haki ya Kristo iliyowekwa ndani yao (kama vile Warumi 4)
2. walioitwa kuishi kitakatifu kwa sababu ya uwepo wa Roho (tazama Mada Maalum: Utakaso)

Waamini ni "watakatifu" (*hagioi*) kwa sababu ya

1. mapenzi ya yule Aliye Mtakatifu (Baba, kama vile Yohana 6:29,40; 1 Pet. 1:15-16)
2. kazi ya Mwana aliye Mtakatifu (Yesu, kama vile 2 Kor. 5:21; 1 Pet. 1:18-21)

uwepo wa Roho Mtakatifu akaaye ndani (kama vile Rum. 8:9-11,27)

Mara nyingi katabu cha Agano Jipya kinawarejelea watakatifu kama WINGI (isipokuwa mara moja katika Flp. 4:21, lajkini muktadha unalifanya neno hili kuwa WINGI). Kuokolewa ni kuwa sehemu ya familia, mwili, ujenzi! Imani ya kibiblia huanza na mapokezi binafsi, bali suala li ndani ya ushirika wa pamoja. Kila mmoja wetu amekirimiwa kama vile 1 Kor. 12:11) kwa ajili ya afaya, ukuaji, na manufaa ya Mwili wa Kristo—kanisa (kama vikle 1 Kor. 12:7). Tumeokolewa ili kutumika! Utakatifu ni sifa ya familia!

Hili linakuwa adimu kwa waamini (kama vile Matendo ya Mitume 9:13,32,41; 26:10; Rum. 1:7; 1 Kor. 1:2; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; Flp. 1:1; Kol. 1:2) na njia ya kuonyesha huduma kwa wengine (kama vile Rum. 12:13; 16:2; Efe. 1:15; Kol. 1:4; 1 Tim. 5:10; Ebr. 6:10). Paulo alichukua wakati wa kipekee wa kujitoa kwa makanisa Mataifa kwa watu wahitaji waliokuwa ndani ya Kanisa Mama ndani ya Yerusalemu (kama vile Rum. 15:25-26; 1 Kor. 16:1; 2 Kor. 8:4; 9:1).

◙**"ikiwa amewasaidia wateswao"** Hapa tena hii inarejerea kwa huduma ya faraja kwa waaminio lakini ingehusisha wahitaji, walioumizwa, majirani waliopotea. Kila sifa inafunua moyo wa utumishi wa wajane hawa viongozi.

**5:11 "ukatae kuwaandika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo, wataka kuolewa"** Lazima tukumbuke thiolojia chanya ya ndoa ambayo inawasilishwa katika Biblia (kama vile Mwanzo 1 na 2). Tungo hii inaonekana kuhusiana na kiapo ambacho wajane hawa walikula walipofanyika wasaidizi wa kanisa la nyumbani (kama vile 1 Tim. 5:12). Hii sio kauli juu ya ndoa bali maoni ya kuchosha kuhusu kufanya viapo katika jina la Kristo na sio kuitunza (yaani kama talaka inavyofanya pia).

**5:12 "wana hukumu"** Toleo la King James lina "shutumu" (NKJF lina "hukumu"). Hii ni kali sana kwa fasiri ya neno la Kiyunani *krino*. Kiapo kwa Mungu ilikuwa nadhiri makini (kama Law. 27 na Hes. 30), bali sio suala la wokovu.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"wameweka kando viapo vyao vya kwanza"** |
| **NKJV** | **"wametupa imani yao ya kwanza"** |
| **NRSV** | **"kwa kuvunja ahadi zao za kwanza"** |
| **TEV** | **"okwa kuvunja nadhiri zao za kwanza"** |
| **NJB** | **"kwa kutokuwa waaminifu kwa nadhiri zao za kwanza"** |

Neno la Kiyunani *pistis*, ambalo mara nyingi linafasiriwa "imani," "tumaini," au "amini," lina kisawe cha Agano la Kale la uaminifu au kutumainika. Hivi ndivyo ilivyotumika hapa katika namna ya kipaumbele cha nadhiri kinachohusiana na kumtumikia Kristo (kibayana, "imani ya kwanza").

**5:13 "wakizunguka-zunguka nyumba kwa nyumba"** Yawezekana wajane walisaidia katika kujali kwa kila siku na kugawa chakula kwa kila wiki (kama ilivyokuwa katika sinagogi) kwa wajumbe wote wa makanisa ya nyumbani tofauti tofauti. Wanaweza kuwa walitembelea nyumba kwa nyumba kuwajulia hali waaminio.

◙**"lakini ni wachongezi na wadadisi"** Neno la kwanza lililotumika katika 3 Yohana 10 ya shutuma za uongo zilizoletwa dhidi ya viongozi wa kanisa. Tatizo linatolewa maana katika Tito 1:11. Tatizo halikuwa uchongezi bali uzushi!

Neno la pili lilitumika juu ya miujiza au uchawi katika Mdo. 19:19. Hatahivyo, katika muktadha huu inamaanisha wanawake wanaofanya kazi ya kuangalia mambo ya wengine (NJB "wadadisi/wachochezi").

◙ **"wakinena maneno yasiyowapasa"** Katika muktadha huu wa barua za Paulo walimu wa uongo kuwadanganya wanawake vijana (kama vile 2 Tim. 3:5-7), Inawezekana kwamba walikuwa wanaeneza mafundisho ya uongo kutoka nyumba moja mpaka nyingine au kutoka nyumba ya mtu wa kanisani kwa mwingine (kama vile Tito 1:11). Hii ndiyo sababu Paulo hakuwaacha wazungumze kwa uwazi katika makanisa ya nyumbani (kama vile 1 Tim. 2:9-15) na hakuwaruhusu kuwa wasaidizi wa kanisa.

**5:14 "Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe"** Ndoa (kwa hili ndoa ya pili) sio jambo ovu au lisilo la kiroho (kama vile 1 Kor. 7:8,39-40). Kutengeneza familia ni wito wa kiungu (kama vile 1 Tim. 2:15).

◙**"iliwasimpe adui nafasi ya kulaumu"** Ile "adui" ni UMOJA; Inarejerea kwa

1. Shetani (kama vile 1 Tim. 5:15)
2. majirani wakristo wapinga upagani (Tanbihi ya NJB, *Jerome Biblical Commentary*, p. 356)
3. mwalimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 3:6-7)

Wajane hawa waliokuwa waliokuwa na hisia kali za kujamiiana kulifungua mlango kwa vyote mashambulizi ya kishetani na ukosoaji kutoka kwa jamii nzima (waaminio na waisioamini).

Neno "nafasi" ni neno la kijeshi "mwinuko wa "au"ngome ya kijeshi" (kama vile Rum. 7:8,11). Mwili unaoonekana sio muovu bali uwanja wa majaribu. Hisia za kujamiiana sio tatizo. Ni wanadamu walioanguka kuchukua vitu vizuri vya kimungu zaidi ya mipaka ya mipaka iliyotolewa na Mungu.

**5:15 "wengine wamekwisha kugeuka na kumfuata Shetani"** Yawezekana Timotheo ilikuwa na uhusiano na Paulo juu ya matukio ya kibayana kama wajane yanayotajwa katika mstari 6 au 13. Walimu wa uongo walikuwa

wamewawekea malengo wajane hawa vijana kuwa wazungumzaji wasaidizi (kama walikuwa na viongozi baadhi wa kiume, kama vile 1 Tim. 1:20). Nyuma ya walimu wa uongo walikuwa/wana matendo ya uovu. Angalia MADA MAALUM: SHETANI katika 1 Tim. 3:6.

**5:16 "ikiwa"** Hii ni SENTENSI YA DARAJA LA KWANZA LENYE MASHARTI. Paulo anataka familia za Kikristo kuwajibika (KAULI TENDAJI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO). Pia anataka kutoa kwa wale wote wasiokuwa na familia (kama vile 1 Tim. 5:4,8).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ikiwa mwanamke aliye mwamini"** |
| **NKJV** | **"ikiwa yoyote mwanamke anaamini au mwanaume"** |
| **NRSV** | **"ikiwa mwanamke yoyote aaminiye"** |
| **REV, REB** | **"bali mwanamke yoyote wa Kikristo"** |
| **NJB** | **"ikiwa mwamini mwanamke"** |

Kwa dhahiri kuna tofauti za kiandiko.

1. *pistē* – mwanamke aaminiye, MSS א, A, C, F, G, P
2. *pistos* – mwanaume aaminiye, Baadhi ya Old Latin na Vulgate MSS na andiko la Kiyunani iliyoandikwa na Augustine
3. *pistos ē pistē* – mwanaume aaminiye na mwanamke, MS D na vingi vidogo
4. *pistas* – wanawake waaminio, baadhi Old Latin na Vulgate MSS

Toleo la UBS[4] inatoa mbadala #1 a ikitoa alama "B" (karibia na hakika).

◙**"kanisa"** Angalia dokezo katika 1 Tim. 3:15 na Mada Maalum katika 1 Tim. 3:5.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 5:17-22**
**17 Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha. 18 Kwa maana andiko lasema, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Na tena, Mtenda kazi astahili ujira wake. 19 Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu. 20 Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope. 21 Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, na mbele za malaika wateule, uyatende hayo pasipo kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lo lote kwa upendeleo. 22 Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine. Ujilinde nafsi yako uwe safi.**

**5:17 "wazee"** Neno "mzee" (*presbuteros*) ilikuwa na maelezo ya kiungozi wakati neno "mwangalizi" (*episkopos*, kama vile 1 Tim. 3:1) yalikuwa maelezo ya Kiyunani ya mji wa jiji ya uongozi. Maneno haya mawili yanatumika kwa mfanano kwa Agano Jipya (kama vile Mdo. 20:17, 28 na 1 Pet. 5:1-2, ambapo mzee inatumika juu ya wachungaji na pia Tito 1:5,7, ambapo mzee na mwangalizi inatumika juu ya kiongozi Yule yule).

Agano Jipya haiwezi kutumika dola ya kiungu ya kanisa. Inaweka kumbukumbu miundo mitatu iliyokuzwa.

1. baraza la maaskofu (Yakobo na kiongozi wa kimamlaka)
2. baraza la wazee (kundi la wazee likipitiwa upya)
3. makutano (makongamano yakipigiwa kura)

WINGI hapa na katika Mdo. 20:17 na Tito 1:5 na yawezekana kuelekeza kanisa la nyumbani. Kanisa la kwanza halikutenganisha majengo mpaka karne ya tatu. Hakukuwa na nyumba ya mtu mmoja ya kutosheleza waaminio, hivyo nyumba mbali mbali za wakristo kuzunguka miji mikubwa ilifungua milango yao kwa jamii ya Wakristo ajili ya kukutana kwa mara kwa mara. Mbinu hii pia ililinda kanisa kutokukamatwa wote kwa mara moja.

Hakika kwa jinsi gani uongozi wa mji ulio na nyumba kadhaa ulikuwa umepangiliwa haijulikani. Kadiri kanisa lilivyokuwa likikua, utaratibu ulitakiwa. Muundo wa utaratibu huo sio jambo la msingi kama utauwa wa viongozi.

◙**"kustahili heshima maradufu"** Hii ni KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Inaweza kurejerea mshahara (kama vile. Gal. 6:6) au kujikuza (kama vile 1 Thes. 5:12-13). Muktadha ufuatao wa 1 Tim. 5:18 unapendekeza mshahara.

◙**"hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha"** Wazee siku zote wanatajwa katika WINGI katika Agano Jipya, jambo ambalo inaonekana kumaanisha makanisa kadhaa ya nyumbani katika miji mikubwa kama Efeso (kama vile Mdo. 20:17 na kuendelea). Wachungaji walikuwa na uwezo wa kufundisha lakini pia kuhubiri (kama vile 1 Tim. 3:2; 2 Tim. 2:24; Efe. 4:11).

Baadhi ya viongozi wana karama moja na wengine wanazo zaidi. Viongozi lazima wawe na shabaha juu ya karama zao na kuruhusu Wakristo wengine kuchukua nafasi. Baadhi ya waumini wengine wamekirimiwa vipawa vya uongozi, mara kwa mara katika namna kadhaa. Wale wanaofanya kazi katika maeneo kadhaa wanahitaji kupewa thawabu kwa ajili ya bidii na kulindwa na kanisa katika maeneo yao ya ufanisi. Sisi kama mwili wa Kristo tunafurahi katika karama ya vipawa vyao lakini pia wanahitaji kukumbuka kwamba tunahitajiana sana (kama vile 1 Kor. 12:7)!

**5:18 "Kwa maana andiko lasema"** Hii ni nukuu kutoka Kumb. 25:4. Inanukuliwa pia kutoka 1 Kor. 9:6-7,14. Huu upekee wa 1 Tim. 5:18 ni kwamba Agano la Kale linanukuliwa kwa msimamo ule ule kama nukuu ya Agano Jipya ambayo tunajikuta tumefungwa ndani yake katika Luka 10:7 ("afanyaye kazi astahili mshahara wake"). Hii inaonesha mtazamo wa Paulo sio tu juu ya uvuvio wa Agano la Kale bali ubora wa sifa za usawa unaokuwa wa Agano Jipya (pia tazama namna gani Petro anavyofanya jambo hilo hilo kwa maandiko ya Paulo, kama vile 2 Pet. 3:15-16).

Paulo kukiri dhana yauongozi wa kulipwa inashangaza sana.

1. Kufuatia urithi wa Kiyahudi, mara kwa mara hakuchukua hela kutoka kwa wale ambao aliwafundisha (Filipi na Thesalonike ilikuwa ni maeneo ambayo hayakuguswa).
2. Jambo hili hili lilikuwa limetumika na walimu mwa uongo kumshambulia Paulo (kama ilivyo katika Korintho, kama vile 2 Kor. 11:7-9; 12:13).
3. Kuna uwezekano pia kuwepo baadhi ya muunganiko na kauli hii ya kimuhtasari na mafundisho ya walimu wa uongo lakini hakika hakitajwi.

**5:19 "Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA KANUSHI ambayo siku zote inamaanisha "kuzuia kitendo kilicho kwenye mchakato." Hii inarejerea matatizo na mashitaka yaliyosababishwa na walimu wa uongo.

Dhana yenyewe inatoka katika maandiko ya Musa (kama vile Hes. 35:30; Kumb. 17:6; 19:15).

**5:20 "Wale wadumuo kutenda dhambi"** Tazama KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATIU ULIOPO. Katika muktadha huu inarejerea viongozi wanaoendelea kutenda dhambi (kama vile 1 Kor. 3:10-15). Hii sio lazima kuwa kitendo cha mara moja. Paulo anazungumzia taratibu sahihi za kushughulikia waaminio watendao dhambi katika Rum. 16:17-18; 1 Kor. 5; Gal. 6:1-5; 1 The. 5:14; 2 The. 3:6-15; 1 Tim. 1:20; 5:19-20; na Tito 3:10-11.

◙**"uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope"** Hii inahusiana na kuzungumza mbele ya hadhara (yaani mbele ya wazee wengine au mbele ya kanisa zima) matendo ya kinidhamu (kama vile Gal. 2:14; Yakobo 5:16) ambayo viongozi wengine walizichukua wakati wengine walifanya

1. kuingilia mamlaka yao
2. kushikilia na kukuza kukuza mafundisho ya uongo
3. kujiingiza katika matendo yasiyopendeza

"kemea" ni neno linalojitokeza sana katika barua za kichungaji (kama vile 2 Tim. 4:2; Tito 1:9,13; 2:15).
Ile "pumzika" inaweza kurejerea kwa

1. makanisa mengine ya nyumbani
2. viongozi wengine wa maeneo
3. waaminio wengine

**5:21 "Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, na mbele za malaika wateule"** Hiki kiapo kikuu kinapatikana mara kadhaa katika barua za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 5:21; 6:13; 2 Tim. 4:1; na katika namna ya kimahusiano katika 2 Tim. 2:14). Paulo alikuwa makini juu ya mamlaka na asili ya mafundisho yake.

◙**"malaika wateule"** Kwa namna fulani inashangaza kwamba"malaika wateule" wanatajwa badala ya Roho Mtakatifu. Hii inatumika katika namna ya

1. wale wanaowahudumia wateule wa Mungu na wale waliopo pamoja nao (kama vile Zaburi 138:1; 1 Kor. 4:9; Mt. 18:10; Luka 9:26; na Ebr. 1:14)
2. Wale malaika maalum walio karibu na kiti cha enzi cha Mungu wanaojongea karibu na uwepo wake (katika fasihi ya kiualimu wa kiyunani, malaika saba wako katika uwepo)

Tungo hii inatofautiano moja kwa moja na Shetani (kama vile 1 Tim. 5:15).

◙**"uyatende hayo pasipo kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lo lote kwa upendeleo"** Timotheo anatakiwa asifanye kisasi na uchungu wala upendeleo! Neno "kudumu" ni neno la Kiyunani "linda." Kama Mungu anavyotulinda sisi (kama vile 2 The. 3:2; Yuda 1:24) na urithi wetu (kama vile 1 Pet. 1:4-5), tunatakiwa kulinda kweli Yake! Tunatakiwa pia kujilinda wenyewe dhidi ya mafundisho ya uongo (kama vile 2 Tim. 4:15; 2 Pet. 3:17; 1 Yohana 5:21).

Tazama hali ya kiagano ya kujirudia rudia: Mungu hulinda/hutunza; waaminio lazima kutunza/kulinda kweli Yake na sisi wenyewe! Inawezekana maelekezo haya kwa Timotheo yanahusiana na upendeleo na upendeleaji ulioneshwa na walimu wa uongo wakidai kuwa kundi maalum la wasomi au kuwa na uwezo wa maarifa ya kipekee au uhuru maalumu.

**5:22 "Usimwekee mtu mikono kwa haraka"** Mstari huu una KAULI TENDAJI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO zaidi ya tatu. Imefasiriwa kwa njia mbili: (1) kurejerea kuwekwa wakfu (kama vile 1 Tim. 3:10; 4:14) au (2) kurejerea kukubaliwa na kurudishwa kazini kwa mzee aliyetubu ambaye alikuwa amekemewa hadharani (kama vile 1 Tim. 5:20). Namba 2 inaonekana kushabihiana na muktadha wa mstari was 24 na 25 na muktadha wa kihistoria wa walimu wa uongo. Angalia MADA MAALUM: KUWEKEWA MIKONO katika 1 Tim. 4:14.

◙**"usizishiriki dhambi za watu wengine"** Hii pia inaweza kurejerea (1) kuwekwa wakfu kwa haraka (kama vile 1 Tim. 3:6) au (2) kurejesha wazee katika uongozi kwa haraka. Kumbuka muktadha ni shughuli za walimu wa uongo waliokuwa wakijipenyeza katika makanisa. Matendo yetu yaweza kufasiriwa na baadhi kama ukiri au ukubalifu wa makosa ya wengine (kama vile 2 Yohana 11).

◙**"Ujilinde nafsi yako uwe safi"** Hii kibayana "kujiweka safi wenyewe" (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, kama vile 1 Tim. 4:12; 5:2). Dhambi ni

1. mtazamo
2. tendo
3. ushirika

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 5:23**
**[23]Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara.**

**5:23 "Tokea sasa usinywe maji tu"** Hii inaonekana kuwa oni lenye utata kwa Timotheo (NET Bible, ukur. 2182, #14). Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI CHA WAKATI ULIOPO ikiwa na KIAMBATA CHA ME, ambayo siku zote ikimaanisha kuzuia kitendo kilicho katika mchakato. Paulo anamsihi Timotheo kubadili mazoea ya shughuli zake za kila siku. Amri "jiweke katika hali ya usafi" katika 1 Tim. 5:22 haiathiriwi na unywaji wa mvinyo! Kuwa mwangalifu na desturi za kimadhehebu ambazo zinaenda zaidi ya maandiko!

Timotheo alikuwa anajizuia kunywa mvinyo. Paulo anatajwa kwamba Mvinyo kwa kiwango kidogo isingekuwa tatizo kwa kiongozi wa kiroho. Lazima tukumbuke kwamba ulimwengu wa Kimediteranean ulikunywa mvinyo kila siku. Hii ingeweza kumaanisha (1) kuongeza mvinyo uliochachishwa kusafisha macho yako au (2) kunywa mvinyo kidogo kutoka muda mpaka muda tumbo likichemka. Mvinyo sio tatizo; kutumia vibaya na kutumia vibaya ni matatizo. Biblia inakataza dhidi ya ulevi (kama vile Mith. 23:29-35; Isa. 5:11,22; 28:1-8), lakini haifundishi kujizuia (kama vile 1 Tim. 3:3,8). Katika siku zetu na jamii kujizuia lazima kuhusiane na dhana ya kiroho inayopatikana

katika Rum. 14:1-15:13; 1 Wakorintho 8 na 10:23-33). Hatahivyo waamini lazima wapingane na miundo yote ya upole (kama vile Kol. 2:20-23)! Angalia Mada Maalumu: Mitazamo ya kibiblia juu ya kilevi na ulevi katika at 1 Tim. 3:3.

◙**"kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara"** Je hizi ni tungo mbili za maelezo tofauti tofauti au wanarejerea tatizo moja? Je huu mstari inamaanisha kuwa Timotheo alikuwa mtu mdhaifu kimwili? Kazi ya Timotheo ilikuwa na changamoto na ngumu. Ikiwa alikuwa dhaifu wa mwili, inamfanya mfano zaidi na mtu wa kuheshimu mtu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 5:24-25**
**24Dhambi za watu wengine zi dhahiri, zatangulia kwenda hukumuni; wengine dhambi zao zawafuata. 25Vivyo hivyo matendo yaliyo mazuri ya dhahiri; wala yale yasiyo dhahiri hayawezi kusitirika.**

**5:24-25** Mistari hii inaweza kuwa 1 Tim. 5:22. Kwa matunda yake mtawatambua (kama vile Mt. 7). Katika muktadha. Wao ni shahidi kwa mafundisho yao na mitindo yao ya maisha (dhambi ambazo ni dhahiri) na dhambi zingine (yaani dhambi zilizojificha au mitazamo/dhamira) zitafunuliwa siku ya hukumu.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha nafasi za wafanyakazi walipwao na kanisa la maeneo wanaotajwa katika sura ya 5.
2. Orodhesha sifa za mjane wa kweli aliyetakiwa kupokea fedha kutoka kanisa.
3. Namna gani mistari 7,8, na 14 inahusiana na 1 Timotheo 3?
4. Namna gani mstari wa 20 inahusiana na mistari ya 24 na 25?
5. Je Biblia inafundisha kujizuia na Unywaji wa Pombe?

# 1 TIMOTHEO 6

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Majukumu ya Kuwajali wengine | Heshimu Mabwana | | Majukumu ya kuwajali Waaminio | Watumwa |
| (5:1-6:2a) | 6:1-2 | (5:1-6:2a) | (5:1-6:2a) | 6:1-2a |
| Mahubiri ya uongo Na mali za kweli | Tamaa na Makosa | Maelekezo ya Mwisho | Mahubiri ya uongo na Utajiri wa kweli | Walimu wa kweli na Walimu wa Uongo |
| 6:2b-10 | | 6:2b-10 | 6:2b-5 | 6:2b-10 |
| | 6:3-10 | | | |
| Vita vizuri vya Imani | Ukiri mwema | | Maelekezo binafsi | Kazi ya Timotheo inakumbushwa |
| 6:11-16 | 6:11-16 | 6:11-16 | 6:11-16 | 6:11-16 |
| | Maelekezo kwa Matajiri | | | Wakristo Matajiri |
| 6:17-19 | 6:17-19 | 6:17-19 | 6:17-19 | 6:17-19 |
| | Ilinde Imani | | | Onyo la Mwisho Na Hitimisho |
| 6:20-21a | 6:20-21 | 6:20-21a | 6:20-21a | 6:20-21 |
| 6:21b | | 6:21b | 6:20b | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Somo la walimu wa uongo linarudi (kama vile 1 Tim. 1:3-11,19-20; 4:1-5; 6:3-11,17-19). Barua hii nzima inazungumzia matatizo yaliyosababishwa na mafundisho na mambo ya kimaadili yaliyoibuliwa na wazushi.
B. Mistari ya 1-2 inaonekana nje ya eneo, lakini yawezekana yanahusiana pia na jumbe za walimu wa uongo kuhusu watumwa wakristo na haki zao mpya na uhuru. Toleo la UBS[4] na TEV yote yanaona muundo wa kipengele hiki cha kitabu kama Paulo anavyomtia moyo Timotheo namna gani ya kushughulika na makundi mbali mbali ndani ya kanisa.
    1. wanaume wazee na wanawake wazee (1 Tim. 5:1-2)
    2. wajane (1 Tim. 5:3-11)
    3. wazee (1 Tim. 5:17-25)
    4. watumwa (1 Tim. 6:1-2)

C. Kinachoshangaza 1 Timotheo haimaliziki kwa mfuatano wa salamu. Paulo alikaa muda mrefu katika Efeso kuliko mji mwingine wowote na alikuwa na matokeo ya ajabu ya kiuinjilisti. Alifahamu waaminio wengi waamifu katika katika mji huu. Kwa nini amsalimie Timotheo tu?
   Barua hii kidhahiri inakusudiwa kusomwa kwa kusanyiko la kansa au katika makanisa ya nyumbani ("ninyi" ni WINGI katika 1 Tim. 6:21). Hatahivyo ilikuwa pia ni barua ya kibinafsi pamoja na ushauri na maelekezo hasa kwa ajili ya Timotheo, msaidizi wake wa Utume.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 6:1-2**
**1 Wo wote walio chini ya kongwa, hali ya utumwa, na wawahesabie bwana zao kuwa wamestahili heshima yote, jina la Mungu lisitukanwe wala mafundisho yetu. 2 Na wale walio na bwana waaminio wasiwadharau kwa kuwa ni ndugu; bali afadhali wawatumikie, kwa sababu hao waishirikio faida ya kazi yao wamekuwa wenye imani na kupendwa. Mambo hayo uyafundishe na kuonya.**

**6:1 "Wo wote walio chini ya kongwa, hali ya utumwa"** Ukristo ulijiweka wenyewe katika desturi za nyakati zake wenyewe kuhusiana na utumwa. Theluthi mbili ya ulimwengu wa Kirumi walikuwa watumwa. Ilikuwa ni kweli, haki, upendo wa Mungu katika Injili ambao mwishowe uliumaliza utumwa. Paulo alichagua kushughulikia mitazamo ya kibinadamu kwa kutumia mazingira yao ya kidesturi badala ya kupindua mila hizo kwa kumwaga damu (Kama alivyofanya zaidi juu ya nafasi ya wanawake).

### MADA MAALUM: MAONYO YA PAULO KWA WATUMWA

1. Utosheke, lakini kama patakuwepo na fursa kwa ajili ya kunufaika na uhuru wenyewe, chukua (1 Kor. 7:21-24).
2. Katika Kristo hapana mtumwa wala (Gal. 3:28; Kol. 3:11; kama vile 1 Kor. 12:13).
3. Tenda katika Bwana, naye atakulipa (Efe. 6:5-9; Kol. 3:22-25; kama vile 1 Pet. 2:18-20).
4. Katika Kristo watumwa huwa ndugu (1 Tim. 6:2; Filemoni 1:16-17).
5. Watumwa wa ki-Mungu huleta heshima kwa Mungu (1 Tim. 6:1; Tito 2:9).

Maonyo ya Paulo kwa wamiliki wa watumwa:

Watumwa wa Kikristo na mmiliki wa watumwa wana Bwana mmoja, kwa hiyo, kwa hiyo, wanapaswa kuwatenda wengine kwa heshima (Efe. 6:9; Kol. 4:1).

Utumwa ni moja ya iana ya kitamaduni (kama vile tamaduni za wazee wa kaya) ambao walikuwa ndio nguzo ya ulimwengu wa karne ya kwanza. Agano Jipya halileti changamoto wala mwelekeo. Hata hivyo, kweli ya injili, kwa muda iliathiri mabadiliko katika mwelekeo wa utamaduni.

◙**"wawahesabie bwana zao kuwa wamestahili heshima yote"** Inavyoonekana mstari wa 1 unarejerea watumwa wa Kikristo watumikiao mabwana wasio wakristo, wakati mstari wa 2 unarejerea watumwa Wakristo watumikiao mabwana wakristo. Mtumwa mkristo anatakiwa kuenenda mbele ya waaminio na wasioamini kwa namna ya kuleta heshima kwa Mungu na Injili ya Yesu Kristo (kama vile Efe. 6:6-7). Mstari wa 1 una mwelekeo ule ule kama 3:2;7;10; 5:7,8,14; na Tito 2:5,ambayo inamaana "kutoweza kuvumilia ukosoaji." Pia angalia 1 Tim. 6:14 ya sura hii hii.

**6:2 "Na wale walio na bwana waaminio wasiwadharau"** Hii kibayana ni "kudharau,"ambayo ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO pamoja na KIAMBATA KANUSHI ikimaanisha kusitisha kitendo kinachoendelea au kilicho katika mchakato. Tungo hii inahusiana na dhana za kimafundisho kwamba kila kitu ambacho sisi kama waaminio tunafanya lazima kiwe cha ubora wa hali ya juu sana kwa ajili ya Kristo (kama vile 1 Kor. 10:31; Efe. 6:6-7; Kol. 3:17; 1 Pet. 4:11).

Neno "mabwana" sio neno la kawaida kwa ajili ya mmiliki wa watumwa, *kurios* (kama vile Efe. 6:5,98; Kol. 3:22; 4:1), bali *despotēs*. Siku zote linatumika na Mungu Baba na Mwana lakini katika barua za Kichungaji zinatumika

mara kwa mara kwa mabwana wa watumwa wa duniani (kama vile. 1 Tim. 6:1,2; 2 Tim. 2:21; Tito 2:9). Paulo anaweza kuwa alitumia mwandishi tofauti.

◙ **"uyafundishe na kuonya"** Kuna KAULI TENDAJI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO mbili jambo linalomaanisha jukumu endelevu (kama vile 1 Tim. 4:11). Tungo hii inahitimisha onyo la kwanza (kama vile NASB, NKJV) au kutambulisha kile kinachofuata (kama vile NRSV, TEV, NJB).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 6:3-10**
**[3] Mtu awaye yote akifundisha elimu nyingine, wala hayakubali maneno yenye uzima ya Bwana wetu Yesu Kristo, wala mafundisho yapatanayo na utauwa, [4] amejivuna; wala hafahamu neno lo lote; bali ana wazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno, ambayo katika hayo hutoka husuda, na ugomvi, na matukano, na shuku mbaya; [5] na majadiliano ya watu walioharibika akili zao, walioikosa kweli, huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida. [6] Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. [7] Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; [8] ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. [9] Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. [10] Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi.**

**6:3"ikiwa"** Hii ni SENTENSI YA DARAJA LA KWANZA LENYE MASHARTI (inayodhaniwa kuwa kweli) kuendelea kwa muktadha wa fasihi kutoka 1 Tim. 6:3 mpaka 1 Tim. 6:5. Kulikuwa na walimu wa uongo waliokataa mafundisho ya Paulo (kama vile 1 Tim. 1:3-7; 4:1-3).

◙**"akifundisha elimu nyingine"** Hili ni neno la Kiyunani *heteros*, ambalo linamaanisha "nyingine ya namna tofauti." Mafundisho ya uongo yalikuwa muunganiko wa nadharia ya sheria ya Kiyahudi na Falsafa ya Kiyunani sawasawa na ile inayopatikana katika Kolosai na Efeso.

◙**"wala hayakubali maneno yenye uzima"** Angalia dokezo katika 1 Tim. 1:10.

◙**"ya Bwana wetu Yesu Kristo"** Paulo anaelezea kwamba asili ya "maneno yenye uzima" ni mafundisho ya Kristo ambayo alipewa Paulo. Hawa walimu wa uongo walikataa wote Kristo na mafundisho ya Mitume.

◙**"wala mafundisho yapatanayo na utauwa"** Angalia dokezo katika 1 Tim. 2:2. Mafundisho ya Kristo siku zote yalikuwa na utauwa kama lengo lao (kama vile 1 Tim. 3:16). Walimu hawa wa uongo walijaribu kutenganisha ukweli na uzima, kuhesabiwa haki na utakaso, ELEKEZI (ukweli wa injili) kutoka SHURUTISHI (utauwa wa kiinjili, angalia Mada Maalumu katika 1 Tim. 4:7). Angalia MADA MAALUM: UTAKATIFU/UTAKASO WA AGANO JIPYA katika 2 Tim.2:21.

**6:4**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"mwenye majivuno"** |
| **NKJV, NJB** | **"mwenye kujisifu"** |
| **TEV** | **"asumbuliwaye na majivuno"** |

Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Neno kibayana "apofushwaye na moshi" kwa namna ya majivuno (kama vile 1 Tim. 3:6; 6:4; 2 Tim. 3:4). Angalia MADA MAALUM: UOVU NA WEMA katika Agano Jipya katika 1 Tim. 1:9.

◙**"bali ana wazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno"** Kumekuwepo na msisitizo unaoendelea juu ya Timotheo kutohusishwa katika mijadala hii ya kijinga ya walimu wa uongo (kama vile. 1 Tim. 1:3,4; 4:7; 2 Tim. 2:14; 4:4; Tito 1:14). Nashangaa namna hii ingekuwa siku ya leo?

Neno "kuhuzunishwa" ni kibayana "kuumwa." Ilikuja kutumika kisitiari juu ya shauku kubwa ya kutamani kitu. Walimu hawa wa uongo hawakuwa wakitafuta utauwa bali maarifa ya siri juuu ya maeneo yasiyofunuliwa au maeneo nyeti ya kweli. Walitaka kubishana juu ya mambo yasiyodhahiri ya kimafundisho jambo lililosababisha hoja na migawanyo ya kimajivuno.

Kadiri ninavyokua ninajua kufahamu kwamba sijui na ndivyo ninavyozidi kuwa na furaha juu ya uelewa wangu mdogo! Kweli kuu ya Ukristo ziko wazi na zinarudiwa! Japo bado kwa namna fulani tunakazana kujua "yote" maelezo na maana na utando wa vifungo vya kithiolojia vinavyojumuisha fasiri ngumu zisizo wazi, za nyakati za mwisho na jumbe za kinabii. Tunaona utukufu katika mifumo yetu ya maelezo mengi badala ya uhusiano wetu na Kristo. Inaweza kuwa ngumu zaidi kwa Mwanathiolojia mwenye msimamo na kufuata mifumo kupita katika tungu la sindano kuliko mtu tajiri!!

Hubiri kweli zilizo wazi! Jadili mambo yanayo fika ukingoni mwa fahamu kwa upendo! Kuwa mwenye neema kwa wote! Ukomavu utatufanya sisi tuwe watu tusio hukumu na wafananao zaidi na Kristo.

**6:5 "watu walioharibika akili"** Aidha (1) muktadha mzima unarejerea walimu wa uongo au (2) mistari michache ya kwanza inawarejerea wao na inayobaki inarejerea madhara yaliyosababishwa katika makanisa ya nyumbani kwa mafundisho yao (kama vile Arichea na Hatton's *A Handbook on Paul's Letters to Timothy and Titus*, UBS). Nafikiri wajane vijana na pia yawezekana baadhi ya watumwa (kama vile 1 Tim. 6:1-2), walikuwa wazungumzaji wasaidizi wa walimu wa uongo (kama vile Gordon Fee's *First and Second Timothy and Titus* katika New International Biblical Commentary Vol. 13).

◙**"walioikosa kweli"** Tungo hizi mbili za mwisho ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU, ikimaanisha hali ya utulivu wa akili na moyo inayoleta na jambo la nje yawezekana yule muovu (angalia Mada maalumu katika 1 Tim. 3:6). Yeye ni baba sio tu wa uongo bali wa madhanio ya kidini na majisifu ya kithiolojia. Angalia Mada Maalum: Kweli katika 1 Tim. 2:4.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"wanaodhani kuwa utauwa ni jambo la kujipatia faida"** |
| **NKJV** | **"wanaodhani kuwa utauwa ni namna ya kujipatia faida"** |
| **NRSV** | **"wakidhania kwamba utauwa ni namna ya kujipatia faida"** |
| **TEV** | **"wanafikiri kwamba dini ni njia ya kufanyika tajiri"** |
| **NJB** | **"fikiria kwamba dini ni njia ya kutengeneza faida"** |

Hii inaonekana kujumuisha moja ya vitu viwili: (1) walimu wa uongo walifundisha thiolojia ya mafanikio na umiliki mali au (2) waliwalipisha watu kwa ajili ya mafundisho yao (kama vile Tito 1:11; 2 Pet. 2:3). Namba 2 yawezekana ina mwelekeo wa ufanano ulio sawa zaidi.

Toleo la King James linaongeza tungo mwishoni mwa 1 Tim. 6:5, "katika hayo jitoe," Lakini hii inatokea tu katika sahihisho la karne ya tano ya maandiko ya Kiyunani D. Haitokei katika maandiko zaidi ya kale ya א, A, $D^*$, F, or G. Toleo la $UBS^4$ linatoa andiko fupi alama ya "A" (hakika).

Kwa "utauwa" angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:7.

**6:6 "pamoja na kuridhika"** Neno hili kimsingi linajumuisha kutoridhika kwa hali ya kiburi, bali kutiwa moyo na utoshelevu wa Roho Mtakatifu ambako hakutokani na mazingira au mali binafsi bali kumtegemea Mungu katika Kristo (kama vile Flp. 4:11-13).

**6:7 "Kwa maana hatukuja na kitu duniani"** Hii inaweza kuwa maelezo ya vifungu kadhaa vya Agano la Kale (kama vile Ayubu 1:21; Zab. 49:17; Muh. 5:15). Inaweka msingi kwa ajili ya kauli katika 1 Tim. 6:6. Mistari ya 6 na 8 ni sawa na kauli zinazopatikana kwa Wanafalsafa wa Kiyunani wa Stoiki. Paulo alikuwa anajua juu ya wanaharakati wa kimaadili hawa. Nyingi za orodha zake za dhambi na wema pia zinapatikana na kufanana kwa waandishi wa Kiyunani hawa. Angalia mada maalum: Matumizi ya Paulo ya *Kosmos* katika 1 Tim. 1:15.

Toleo la KJV linaongeza "na ni hakika" kwa "kwasababu." Nyongeza hii inatokea katika MSS $א^2$ na $D^2$, pamoja pia na baadhi ya Old Latin, Vulgate, na matoleo ya Kishamu. MS D na baadhi Old Latin, Vulgate, na matoleo ya kishamu yana "kweli" kabla ya "kwasababu." Toleo la $UBS^4$ linatoa andiko fupi alama ya "A" (hakika).

**6:8** Waaminio wanahitaji kuridhika na namna Mungu anavyowapatia mahitaji yao ya kila siku (kama vile Mith. 30:8; Mt. 6:11). Matumizi ya Paulo ya neno "faida" katika 1 Tim. 6:5 iliwasababishia yeye kutoa maelezo juu ya tamaa za walimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 6:6-10 na 17-19).

## MADA MAALUM: WINGI WA MALI

I. Mtazamo wa kitabu cha Agano la Kale kwa ujumla
   A. Mungu ndiye mmiliki wa vitu vyote
      1. Mwanzo 1-2
      2. 1 Nyakati 29:11
      3. Zaburi 24:1; 50:12; 89:11
      4. Isaya 66:2
   B. Wanadamu ni wasimamizi wa mali kwa ajili ya makusudi ya Mungu
      1. Kumbukumbu 8:11-20
      2. Mambo ya Walawi 19:9-18
      3. Ayubu 31:16-33
      4. Isaya 58:6-10
   C. Wingi wa mali ni sehemu ya ibada
      1. zaka za aina mbili
         a. Hesabu 18:21-29; Kumb. 12:6-7; 14:22-27
         b. Kumb. 14:28-29; 26:12-15
      2. Mithali 3:9
   D. Wingi wa mali huonekana kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajiri ya agano la uaminifu
      1. Kumbukumbu 27-28
      2. Mithali 3:10; 8:20-21; 10:22; 15:6
   E. Onyo dhidi ya mali katika kuwagharimikia wengine
      1. Mithali 21:6
      2. Yeremia 5:26-29
      3. Hosea 12:6-8
      4. Mika 6:9-12
   F. Wingi wa mali sio dhambi kuwa nayo isipokuwa ikiwekwa kama kipaumbele
      1. Zaburi 52:7; 62:10; 73:3-9
      2. Mithali 11:28; 23:4-5; 27:24; 28:20-22
      3. Ayubu 31:24-28

II. Mtazamo wa kipekee wa kitabu cha Mithali
   A. Mali imewekwa katika nafasi ya juhudi ya mtu binafsi
      1. uzembe na uvivu umelaaniwa – Mithali 6:6-11; 10:4-5,26; 12:24,27; 13:4; 15:19; 18:9; 19:15,24; 20:4, 13; 21:25; 22:13; 24:30-34; 26:13-16
      2. kufanya kazi kwa bidii kumeungwa mkono – Mithali 12:11,14; 13:11
   B. Umaskini dhidi ya mali umetumika kueleza juu ya haki dhidi ya unyonge – Mithali 10:1na kuendelea; 11:27-28; 13:7; 15:16-17; 28:6,19-20
   C. Hekima (kumjua Mungu na nenp lake na kuishi katika maarifa haya) ni bora kuliko utajiri- Mithali 3:13-15; 8:9-11,18-21; 13:18
   D. Maonyo na makaripio
      1. Maonyo
         a. jihadhari na kudhamini deni la jirani yako (dhamana) –Mithali 6:1-5; 11:15; 17:18; 20:16; 22:26-27; 27:13
         b. jihadhari na kupata utajiri kwa njia ya uovu – Mithali 1:19; 10:2,15; 11:1; 13:11; 16:11; 20:10,23; 21:6; 22:16,22; 28:8

        c. jihadhari na mkopo – Mithali 22:7
        d. jihadhari na utajiri wa muda mfupi – Mithali 23:4-5
        e. mali hazifaidii kitu siku ya ghadhabu – Mithali 11:4
        f. utajiri una "marafiki" wengi– Mithali 14:20; 19:4
    2. makaripio
        a. ukarimu huungwa mkono – Mithali 11:24-26; 14:31; 17:5; 19:17; 22:9,22-23; 23:10-11; 28:27
        b. afadhali haki kuliko utajiri – Mithali 16:8; 28:6,8,20-22
        c. maombi kwa ajili ya uhitaji, na sio utoshelevu – Mithali 30:7-9
        d. kumpa mhitaji ni kumpa Mungu – Mithali 14:31

III. Mtazamo wa kitabu cha Agano Jipya

A. Yesu
1. mali hutengeneza jaribu pekee la imani ndani yetu wenyewewe rasilimali na zetu badala ya Mungu na rasilimali Zake
    a. Mathayo 6:24; 13:22; 19:23
    b. Marko 10:23-31
    c. Luka 12:15-21,33-34
    d. Ufunuo 3:17-19
2. Mungu atatupa mahitaji yetu ya kimwili
    a. Mathayo 6:19-34
    b. Luka 12:29-32
3. kupanda kunahusiana na kuvuna (kiroho pamoja na kimwili)
    a. Marko 4:24
    b. Luka 6:36-38
    c. Mathayo 6:14; 18:35
4. toba huithiri mali
    a. Luka 19:2-10
    b. Mambo ya Walawi 5:16
5. unyanyasaji wa kiuchumi umelaaniwa
    a. Mathayo 23:25
    b. Marko 12:38-40
6. Humu ya nyakati za mwisho inahusiana na matumizi yetu ya mali – Mathayo 25:31-46

B. Paulo
1. Maoni ya kiutendaji kama ule wa Mithali (kazi)
    a. Waefaso 4:28
    b. 1 Wathesalonike 4:11-12
    c. 2 Wathesalonike 3:8,11-12
    d. 1 Timotheo 5:8
2. Maoni ya kiroho kama yale ya Yesu (mambo ni ya muda mfupi, iweni na utoshevu)
    a. 1 Timotheo 6:6-10 (kuridhika)
    b. Wafilipi 4:11-12 (kuridhika)
    c. Waebrania 13:5 (kuridhika)
    d. 1 Timotheo 6:17-19 (ukarimu na kuamini Mungu, si utajiri)
    e. 1 Wakorintho 7:30-31 (kubadiklika badilika kwa mambo)

IV. Hitimisho

A. Hakuna theolojia ya kimfumo iliyo ya kibiblia kuhusiana na mali.
B. Hakuna kifungu cheye uhakika kuhusiana na suala hili, hivyo, mitazamo ya kiundani lazima ikusanywe kutokana na vifungu mbalimbali. Jihadhari na kutokutumia maoni yako katika maandiko haya yaliyojitenga.
C. Kitabu cha Mithali, ambacho kiliandikwa na watu wenye hekima (busara), wana mtazamo

tofauti kuliko aina nyingine za miundo ya kibiblia. Kitabu cha Mithali ni cha kiutendaji na kina tazamio binafsi. Hiki kina ulinganifu na lazima kiwe na ulinganifu na Maandiko mengine (kama vile Yer. 18:18)

D. Katika hizi siku tulizonazo tunahitaji kuchambua maoni na utendji wake kuhusiana na mali katika nuru ya Biblia. Vipaumbele vyetu vimepotea ikiwa ubepari au ukomonisti ni mwongozo wetu wa pekee. Ni kwa nini na ni kwa namna gani kufanikiwa kwa mtu ni maswali muhimu sana kuliko kuliko kile mtu alichojilimbikizia.

E. Kujilimbikizia mali lazima kuwe na ulinganifu na ibada ya kweli na utumishi unaostahili kama vile 2 Wkakorintho 8-9).

**6:9 "Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu"** Waaminio wanaleta vitu vingi juu yao wenyewe kwa sababu ya tamaa ya vitu vya duniani na umaarufu (kama vile Mith. 23:4; 28:20; Mt. 6:19-34).

"Majaribu" ni neno la Kiyunani *peirasmos*.

## MADA MAALUMU: MANENO YA KIYUNANI YAHUSUYO KUPIMA NA VIDOKEZO VYAKE VINGINE

Kuna manaeno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumpima mtu kwa kusudi fulani.

1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

Neno hili ni neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhihilisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale).

Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya

a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28
c. imani yetu – Yakobo 1:3
d. hata Mungu –Ebr. 3:9

Matokeo ya majaribu hayajafikiriwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7; Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

a. kuwa wa thamani
b. kuwa wazuri
c. kuwa halisi
d. kuwa wa maana
e. kuwa wa kuheshimiwa

*2. Peirazō, Peirasmus*

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mt. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mt. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
c. Matumizi
   1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mat. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
   2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).
   3) Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

◙**"na tanzi,"** Kuna aina tatu.

1. tanzi – MSS א, A, D[2], H
2. mitego – midogomidogo 33, 1175, na Peshitta na toleo la Koptiki
3. mitego ya ibilisi – MSS D[*], F, G, na toleo la Old Latin

Toleo la UBS[4] linatoa mbadala wa #1 alama ya "A" (hakika).

◙**"zisizo na maana, zenye kudhuru"** Dhana hii inatumika mara kadhaa katika Agano Jipya (kama vile Mt. 7:13; Rum. 9:22; Flp. 1:28; 3:19; 2 The. 2:3; 2 Pet. 2:1; 3:7; Ufu. 17:8-11). Ni sitiari kwa kukatisha uzima wa mwili kwa nguvu. Neno hili halihusiani na dhana ya kithiolojia ya kuondoa (angalia Edward Fudge, *The Fire That Consumes* kwa ajili ya hoja kali za uondoaji), ambayo inaelezea kwamba wale waliopotea kiroho huwa hawa dhuriki/kuteseka na utengano wa kudumu, lakini kwa namna fula kupoteza hali ya kuishi. Waondoaji watalitafsiri hili kibayana. Hii inaelezewa kuwa zaidi "ubinadamu" wa Mungu kuliko kuzimu ya milele. Hatahivyo neno hili hili (*aiōnion*) ambalo linaelezea mbingu ya milele katika Mt. 25:46, linaelezea kuzimu ya milele.

## MADA MAALUM: UMILELE (*aiōnios)*

Robert B. Girdlestone, katika kitabu chake *Synonyms of the Old Testament*, ana maoni ya kushangaza juu ya neno "umilele":

> "Kivumishi *aiōnios* kimetumika zaidi ya mara arobaini katika Agano Jipya. Kwa kuzungumzia uzima wa milele, ambao unachukuliwa kwa sehemu kama zawadi tuliyonayo sasa, kwa sehemu kama ahadi kwa ajili ya ubaadaye. Pia inafanya kazi kwa uwepo wa Mungu usio na ukomo katika Rum. 16.26; kwa thamani ya ondoleo la dhambi lisilokuwa na ukomo la Kristo katika Ebr. 9.12; 13.20; na nyakati zilizopita katika Rum. 16.25; 2 Tim. 1.9; Tito 1.2.
>
> Neno hili linatumika kurejerea moto wa milele, Mt. 18.8; 25.41; Yuda 1:7; adhabu ya milele, Mt. 25.46; hukumu ya milele au shutuma, Marko 3.29; Ebr. 6.2; uharibifu wa milele, 2 The. 1:9. Neno katika vifungu hivi inamaanisha hitimisho na kwa dhahiri ikiashiria kwamba wakati hukumu hizi zikitolewa, muda zaidi zwa uangalizi, mabadiliko au nafasi ya kurudisha nafasi ya mtu ya kwanza, vitakuwa vimekwisha ondoka kikamilifu na milele. Tunaelewa kidogo juu ya wakati wa baadaye, kuhusu mahusiano ya maisha ya mwanadamu na maisha mengine. Ikiwa upande mmoja, sio sawa kuongeza neno la Mungu, upande mwingine lazima tusiondoe; na ikiwa tutayumba yumba katika fundisho la adhabu ya milele kama inavyowekwa katika maandiko, lazima tukubaliane kusubiri tukishikiria injili ya upendo wa Mungu katika Kristo wakati tukitambua kwamba kuna historia isiyojulikana ambayo hatuna uwezo wa kuielewa" (kur. 318-319).

**6:10 "Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha"** Hii inaweza kuwa ni mithali ijulikananyo sana; ni kupenda pesa ndio tatizo! Wayunani wana KIBAINISHI CHA WAZI pamoja na "mzizi" inayomaanisha ni moja ya matatizo mengi (kama vile 2 Tim. 2:25-26; 3:2-5,7-9). Pesa ni chombo na sio lengo. Inaweza kufanyika mungu (sanamu, kama vile Mt. 6:24; Luka 16:9-13).

Toleo la fasiri ya NASB, kama NKJV na NRSV, inajaribu kuilainisha Wayunani (kifasihi. "kwa kuwa mzizi wa uovu yote") kutia chumvi kwa kuongozea "aina" (NKJV, NRSV, "ya aina"). Pesa sio majaribu pekee (kama vile Kol. 3:5), lakini ni moja muhimu sana (kama vile 1 Tim. 3:3).

◙ **"wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani"** Je "imani" hapa inazungumzia juu ya wokovu au kuishi kwa utauwa? Katika muktadha huuu walimu wa uongo wameiacha imani na wanajaribu kuwashawishi wengine (kama vile Marko 13:22). Tamaa na unyanyasaji wa kifedha (pamoja na unyanyasaji wa kingono pamoja na kudai kuwa na maarifa maalumu au ufahamu) ni tabia inayojirudia rudia ya walimu wa uongo. Ikiwa fedha ni kilele, inafanyika kuwa mungu. "Sanamu" katika Mt. 6:24 inakuzwa katika toleo la NASB kwasababu inadhaniwa kuaksi cheo cha mungu wa fedha kutoka Shamu. Kupenda fedha kunafanyika ibada ya sanamu. Inaweza

kusabaisha matokeo ya hatari katika haya maisha na maisha yajayo (kama vile 1 Tim. 4:1; 5:8; 2 Tim. 2:25-26; Tito 1:16).

Ni ngumu kutambua tofauti kati ya mwalimu wa uongo aliyepotea na mwamini aliyepumbazwa. Mara kwa mara wana mwonekano sawa, wanafikiri sawa na wanatenda kwa kufanana. Ni Mungu tu ajuaye moyo. Yeye atafanya uamuzi wa mwisho. Maneno ya Yesu katika Mathayo 7 ("mtawatambua kwa matunda yao") na 13 (mfano wa udongo) inasumbua mifumo yetu uipendayo ya thiolojia. Angalia MADA MAALUMU: UKANAJI WA IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 6:11-16**
**11 Bali wewe, mtu wa Mungu, uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole.**
**12 Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. 13 Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato, 14 kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo; 15 ambako yeye kwa majira yake atakudhihirisha, yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana;**
**16 ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele. Amina.**

**6:11 "uyakimbie mambo hayo"** Timotheo anamuriwa (KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, kama vile 2 Tim. 2:22) kuyakimbia mambo haya katika 1 Tim. 6:3-10 (yaani mkanganyo usiokwisha na/au kupenda fedha). Hii ni kinyume na vitu alivyotakiwa kuhubiri na kufundisha (kama vile 1 Tim. 6:2b), ambayo yanatajwa katika 1 Tim. 5:1-6:2a. Ukristo unajumuisha maamuzi ya mwanzo na yanayoendelea!

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | |
| **TEV** | **"wewe mtu wa Mungu"** |
| **NKJV** | **"Mtu wa Mungu"** |
| **NJB** | **"kama mtu uliyejitoa kwa Mungu"** |

Hiki kilikuwa ni cheo cha heshima kutoka Agano la Kale kilichotumika na Musa (yaani Kumb. 33:1; Yos. 14:6), Eliya, Elisha, Samweli, Daudi, na manabii wasiotajwa (yaani 1 Sam. 2:27; 1 Falme. 12:22; 13:1). Katika 2 Tim. 3:16,17 Inatumika kwa waminio wote waliowezeshwa kwa neno la Mungu. Walimu wa uongo sio watu wa Mungu wala hawajawezeshwa kwa neno la Mungu

◙**"ukafuate"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO ya amri inayoendelea. Ya kwanza ("kukimbia") ni kanushi, ya pili ni SHURUTISHI ("ukafuate") chanya. Zote ni muhimu kwa mafundisho ya uzima na haki binafsi.

◙ **"Haki"** Hii lazima irejeree kuishi maisha ya utauwa (kama vile Yakobo 3:13-18), sio kukata (kimahakama) haki katika Warumi 4. Warumi 1-8 (muhtasari wa kimafundisho) kuzungumzia nafasi yetu katika Kristo (yaani kuhesabiwa haki). Barua za kichungaji (barua dhidi ya mafundisho ya uongo) inazungumzia juu ya kumiliki kwetu umiliki (yaani utakaso, angalia Mada Maalum katika 2 Tim. 2:21).

Kwa "haki" Angalia MADA MAALUM: HAKI katika Tito 2:12.

Hii ni orodha ya sifa za kufanana na Kristo ni sawasawa na kinyume cha mitindo ya maisha ya walimu wa uongo. Kwa matunda yao mtawatambua (kama vile Mathayo 7).

◙**"utauwa"** Hii ni mada inayojirudia rudia (kama vile 1 Tim. 3:10; 4:7-8; 6:3,5-6; 2 Tim. 3:5, angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:7). Milele (angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:7) maisha yana tabia zinazoonekana waziwazi. Kumjua Mungu ni (kutamani kuwa) kama Mungu (kama vile Mt. 5:48).

| | |
|---|---|
| **NASB, NJB** | **"ustahimilivu"** |
| **NKJV** | **"uvumilivu"** |
| **NRSV, TEV** | **"ustahimilivu"** |

Neno la Kiyunani *hupomonē* lina fasiri kadhaa ya kingereza. Katika *A Greek-English Lexicon of the New Testament*, Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker wanasema kwamba neno hili linarejerea kustahimili kazi ngumu na mateso (ukur. 846). Timotheo alitakiwa kukabiliana (1) matatizo; (2) wale waliosababisha matatizo; na (3) wale walioathiriwa na matatizo na ustahimilvu usiokoma. Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:16.

◙**"upole"** Sio tu kwamba Timotheo alitakiwa kustahimili na kug'ag'ania bali alitakiwa kufanya hivyo kwa uaminifu, upendo, roho ya upole (kama vile 1 Tim. 3:3; 2 Tim. 2:25; Tito 3:3; Gal. 6:1; Yakobo 1:21; 3:13,17; 1 Pet. 2:18; 3:4).

**6:12 "Piga vita vile vizuri vya imani"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI (yenye ushahidi) YA WAKATI ULIOPO. Kitenzi KINACHOFANANA na NOMINO vinatumika hapa kuimarisha hali ya afya (kama vile 1 Tim. 1:18; Ebr. 12:1-3) au kijeshi (kama vile Efe. 6:10-18) sitiari (Paulo pia "alipigana vita vizuri," kama vile 2 Tim. 4:7). Tunapata neno la Kingereza "mateso" kutoka katika sitiari hii.

◙**"shika uzima ule wa milele"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU (kama vile 1 Tim. 6:19). Hii ni sitiari ya mwanamichezo ashindaye anayepokea tuzo au taji. Hii inaonesha hitaji la mwanadamu kuanitikia kwa mwanzo (kama vile. 1 Tim. 6:12b) na kuendelea kuitikia katika imani. Tungo inayofuata inaonesha Mungu kutunza nguvu (kama vile. 1 Tim. 6:12c). Hizi mbili zote ni kweli na vipengele sawia vya kiagano vya wokovu; ni kweli kinzani ila za kweli! Uzima wa milele ni njia ya kurejerea hitimisho la tumaini la injili (yaani kutukuzwa, kama vile Rum. 8:30).

◙**"ulioitiwa"** Msisitizo huu juu ya uteuzi wa Mungu na kutunza nguvu (kama vile 1 Kor. 1:9) lazima uunganishwe na ushirikiano wetu wa kila siku wa imani yetu. Kuamriwa kwanza na ustahimilivu lazima ushikiliwe pamoja kama pande mbili za sarafu moja.

## MADA MAALUM: UCHAGUZI/MAJAALIWA NA UHITAJI WA USAWA KITHIOLOJIA)

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile Warumi10:11,13).

Umuhimu wa huu muvatano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja (fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihilisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye

10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhimu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kithiolojia ya "agano" inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daima huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu (k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maneneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa theolojia!

◙**"ukaungama maungamo mazuri"** Hili ni neno la Kiyunani *homologeō,* ambalo linazungumzia juu ya ukiri wa wazi au ukiri (kama vile 1 Yohana 1:9). Hii inaonekana kurejerea ubatizo wa Timotheo kama ukiri wake wa wazi wa imani. Waamini wa kale walirudia kanuni "Yesu ni Bwana" (kama vile Rum. 10:9-13) kama ukiri wao binafsi na wa wazi wa imani katika Yesu. Tungo hii ya kimuhtasari ilimaanisha ubinadamu Wake, uungu, kuchukua chambi na kutukuzwa (kama vile Flp. 2:6-11). Angalia Mada Maalum: Je Inamaanisha Nini "Kupokea," "Kuamini," "Kukiri/Kukiri," Na "Kuitia?"

## MADA MAALUMU: KUTUBU (AGANO JIPYA)

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (Nacham, BDB 636, KB 688, mf., Kut. 13:17; 32:12,14; Shuv, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Flm. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama Mada Maalumu: Toba [Agano la Kale]) na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipya katika kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinanahusiana, lakini tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kitheolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoeō*, kama vile mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 and Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba Mungu hutoa toba (kama vile Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanalitazama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru.

Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuelewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swali ni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelevu na kuwa ndni ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeukia kitu/kifikra!

◙**"mbele ya mashahidi wengi"** Hii inaweza kurejerea kwa

1. kuwekwa wakfu kwa Timotheo (kama vile. 1 Tim. 5:14; 2 Tim. 1:6)
2. Ukiri wake wa wazi mbele ya kanisa la eneo (kama vile Mdo. 16:1-2)
3. yawezekana zaidi, ubatizo wake.

**6:13 "Nakuagiza mbele za Mungu"** Mistari ya 13-16 yote ni sentensi moja katika Kiyunani. Kama Timotheo alivyomkiri Yesu wazi (kama vile Mt. 10:32-33), sasa Paulo anamuagiza pia katika uwepo wa Mungu (kama vile 1 Tim. 5:21; 2 Tim. 4:1).

Paulo "anaagiza" au kumwamuru Timotheo mara kwa mara katika barua za Kichungaji. Wakati mwingine hizi zinarejerea kwa vitu ambavyo Timotheo anatakiwa avifanye (kama vile 1 Tim. 1:3,18; 4:11; 5:21; 6:13; 2 Tim. 4:1) na wakati mwingine kitu gani anatakiwa kuwaambia wengine (kama vile 1 Tim. 5:7,21; 6:17; 2 Tim. 2:14).

KIWAKILISHI NOMINO "ninyi" kiko katika KITENZI JINA "kutunza" ya 1 Tim. 6:14. Baadhi ya MSS iliingiza hii baada ya KITENZI "Nakuagiza" katika 1 Tim. 6:13 (MSS א [2], A, D, H). Inaondolewa katika MSS א[*], F, G. UBS[4] haiwezi kuamua ipi ni ya asili. Kidhahiri kama ilivyo utofauti mwingi wa Kiyunani, haiathiri maana ya sentensi ndefu kutoka katika mstari wa 13 mpaka mstari wa 16.

◙**"anayevihifadhi hai vitu vyote"** Mungu ndiye asili na chanzo cha uhai wote (kama vile 1 Tim. 6:16; 1:17; 2 Tim. 1:10). Hakuna uzima wala uhai kwa mwingine isipokuwa Yeye. Cheo cha Agano la Kale YHWH, kutoka katika kitenzi cha Kiebrania "kisaidizi" (kama vile Kut. 3:14), ni mzaha juu ya dhana hii. Mungu ndiye pekee awezaye kutoa na kuhifadhi uhai wa kimwili na wa milele.

Neno hili lina visawe vyote (1) kutoa uzima/uhai (kama vile 1 Sam. 2:6; 1 Tim. 6:13) na (2) kuhifadhi uhai/uzima (kama vile Waamuzi 8:19; 1 Sam. 27:9,11; 1 Wafalme. 21:31; Luka 17:33; Mdo. 7:19). YHWH anafanya vyote viwili kupitia Kristo.

◙**"na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato"** Yesu anaitwa "shahidi Mwaminifu" (kama vile Ufu. 1:5; 3:14). Neno "mbele" (*enōpion*) linaweza kumaanisha (1) "mbele ya" au (2) "katika kipindi cha." Hivyo hii inaweza kumrejerea maisha yote ya Kristo ya ushuhuda au hasa juu ya mashitaka Yake (kama vile Mt. 27:2; Yohana 18:33-37).

**6:14 "kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama"** Hii inaweza kujerea 1 Tim. 6:11 na 12. Timotheo alitakiwa kuishi katika utii na usafi tofauti na walimu wa uongo. Angalia Mada maalum katika 1 Tim. 3:2.

◙ **"hata kufunuliwa kwake"** Katika 2 Tim. 1:10 na Tito 2:11 neno hili (*epiphaneia*) linatumika juu ya kuja mara ya kwanza lakini hapa katika 2 Thes. 2:8; 2 Tim. 4:1,8; Tito 2:13 linatumika juu ya Kuja kwa Mara ya Pili. Kuja kwa Mara ya Pili kumekuwa siku zote kisababishi kizuri cha kuishi maisha ya Kikristo. Angalia Mada Maalumu katika Tito 2:13.

**6:15 "ambako yeye kwa majira yake atakudhihirisha"** Tungo hii hii inatumika katika 1 Tim. 2:6 na Tito 1:3 of juu ya Kuja mara ya kwanza kwa Yesu. Ile "Yeye" inaelezea Mungu maarifa ya Baba na utawala juu ya kuja mara ya kwanza na ya Pili kwa Masihi (kama vile Mt. 24:36; Mdo. 1:7). Toleo la Fasiri ya Jerome Biblical Commentary (ukur.357) linapendekeza kwamba 1 Tim. 6:15-16 ni nukuu kutoka kwenye tenzi za Kikristo (kama vile. 1 Tim. 1:17; 3:16; 2 Tim. 2:11-13).

◙**"yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana"** Maombi haya yanafanana na 1 Tim. 1:17. Tungo hizi za maelezo kwa kuanza na kimuktadha inarejerea Mungu Baba:

1. "iliyobarikiwa" (1 Tim. 1:1)
2. "mwenye utawala pekee" (1 Tim. 1:17; kama vile Ecclesiasticus 46:5)
3. "Bwana wa Mabwana" (Kumb. 10:17; Zab. 136:3)

Cheo "Mfalme wa Wafalme" inafanana na "Bwana wa Mabwana" na inatumika na Yesu katika Ufu. 17:14; 19:16. kiasili inarejerea mfalme wa Mesopotamia lakini ikitumika na Wayahudi wakati wa kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya kurejerea kwa YHWH.

**6:16 "ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti"** Hili ni neno "mauti" likiwa na KIAMBISHI AWALI HASI (kama vile 1 Kor. 15:53-54). Hii inaonekana kuwa maana ya msingi ya cheo cha Agano la Kale "YHWH," aishiye milele, Yeye pekee aishiye (kama vile Kut. 3:14-16). Tazama maana ya imani kwa mungu mmoja (angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 2:5), "Yeye pekee amilikiye"! YHWH ni asili na chanzo cha uzima na hakuna mwingine!

◙**"amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa"** Walimu wa kiyahudi waliita "wingu la utukufu" ile *Shekinah*, ambayo inatoka neno la Kiebrania "kukaa" (ikiwa na maana "kukaa pamoja kwa kudumu," kama vile Kut. 24:17; 23:20).

◙**"wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona"** Katika Agano la Kale utakatifu wa Mungu ulikuwa mzuri sana kiasi kwamba hakuna mwanadamu mwenye dhambi ambaye alikuwa na uwezo wa kumwona Mungu (kama vile Mwa. 16:13; 32:30; Kut. 20:19; 33:18-20; Waamuzi. 6:22-23; 13:22; Isa. 6:5; Yohana 6:46; 1 Yohana 4:12). Katika Agano Jipya waamini wamemuona yeye Kweli akifunuliwa katika Yesu (kama vile 1 Yohana 1:18; 6:46) ana watamwona Yeye binafsi siku moja (kama vile Mt. 5:8; Ebr. 12:14; Ufu. 22:40).

◙**"Heshima na uweza una yeye hata milele"** Paulo mara kwa mara anaingia katika kumsifu Mungu Baba (kama vile 1 Tim. 1:17). Mwana ni chombo cha Baba cha uumbaji, ufunuo, ukombozi na hukumu. Hata hivyo, ufalme wa milele unamilikiwa na Baba kupitia Mwana (kama vile Dan. 7:13; 1 Kor. 15:25-28).

◙**"Amina"** Hii ni nahau ya Kiebrania ya ukiri.

## MADA MAALUMU: AMINA

I. AGANO LA KALE
   A. Neno "Amina" linatoka kwenye neno la Kiebrania lenye maana ya
      1. "ukweli" (emun, emunah, BDB53)
      2. "Uaminifu" (emun, emunah, BDB 53)
      3. "imani" au "uaminifu"
      4. "amini" (dmn, BDB 52)
   B. Asili yake ya neno inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu Yule asio imara, unaotereza (kama vile Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yeremia 23:12) au kizuizi (kama vile Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kiisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kama vile. Hab. 2:4)
   C. Utumiaji maalumu (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika agano la kale)
      1. Nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)
      2. Kuthibitika, Kut 17:12
      3. Uimalifu, Kut. 17:12
      4. Uthabiti, Isa. 33:6
      5. Ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Pro. 12:22
      6. Thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
      7. Stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160
   D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti
      1. Bathach (BDB 105), imani
      2. Yra(BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile Mwa. 22:12)
   E. Kwa maana ya kuamini au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambao ulitumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile. Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).
   F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu

mwenyewe (kana vile Kut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab. 108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile. Hab. 2:4). Biblia ni historian na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile. Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

II. AGANO JIPYA

A. Utumiaji wa neno "amina" kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida kwenye Agano Jipya (kama vile Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Fil. 4:20; 2 The. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).
C. Yesu ndiye yeye aliyelitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu 3:14 ( pia angalia 2 Kor 1:20, yamkini jina la heshima la Mungu kutoka Isa. 65:16)
E. Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama "imani","sadiki","kuamini"(angalia mada maalumu: Sadiki, Kuamini au Imani).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 6:17-19**
[17] **Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha.** [18] **Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo;** [19] **huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.**

**6:17-19** Mtu anaweza kushangaa ikiwa 1 Tim. 6:17-19 lilikuwa ni wazo la baadaye au ikiwa Paulo alipokea taarifa juu ya kanisa la nyumbani katika Efeso. Inawezekana kwamba Paulo aliandika 1 Tim. 6:17-21 mwenyewe kama ilivyokuwa desturi yake ya kufunga barua zake (kama vile 2 Thes. 3:17-18).

**6:17 "Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune"** Kama mstari wa 9 unaonya juu ya tamaa mbaya ya fedha, mstari wa 17 unaonya wale walio na fedha dhidi ya kuweka imani yao katika hizo na wakacha kuweka kwa Kristo (kama vile Mt. 6:19-21; 13:22; 19:23-30; Yakobo 1:9-11; 5:1-6).

## MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI IJAYO

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kilicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

| **Yesu** | **Paulo** | **Webrania** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| | | **(Paulo)** |
| Mt. 12:32; 13:22,39 | Warumi 12:2 | Ebr.1:2; 6:5; 11:3 |
| Marko 10:30 | 1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18 | |
| Luka 16:8; 18:30; 20:34-35 | 2 Kor. 4:4 | |
| | Wagalatia 1:4 | |
| | Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12 | |
| | 1 Timotheo 6:17 | |
| | 2 Timotheo 4:10 | |
| | Tito 2:12 | |

Katika thiolojia ya Agano Jipya zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyekevu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale liilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipya wa uliopo tayari, lakini bado!

◙**"wala wasiutumainie utajiri usio yakini"** Hii ni KAULI TENDAJI YA KITENZI JINA CHA WAKATI TIMILIFU. Wanadamu wanajaribu kutumaini mali zao sio mali za Mungu (kama vile 1 Tim. 4:10; 5:5). Baadhi ya maneno makali ya Yesu yalikuwa yameelekezwa kwa wenye mali (kama vile Luka 18:18-30).

◙**"bali wamtumaini Mungu"** Kuna tofauti kadhaa.

1. juu ya Mungu – א, F, G
2. juu (yule anayejulikana) Mungu – MSS A, I, P
3. juu ya Mungu aliye hai – MS $D^*$
4. juu ya (anayejulikana) Mungu (anayejulikana) aliye hai– MS $D^2$

Toleo la UBS[4] linatoa uchaguzi wa #1 alama ya "A". Muundo wa maelezo yanachukuliwa kutoka 4:10.

**6:18 "waelekeze***"* Hapa ni maelekezo yenye tungo tatu kwa wale walio na mali za duniani.

1. kuendelea kutenda mema (kama vile. 1 Tim. 5:10; 2 Tim. 2:21; 3:17; Tito 3:1,8,14)
2. kuwa tayari kushirikisha
3. kuwa mkarimu (kama vile 2 Wakorintho 8-9)

**6:19** Mstari huu unakumbusha juu ya mahubiri ya Mlimani hasa sura ya 6 (kama vile Luka 12:15). Umetumia sitiari mbili: (1) kutunza hazina za kweli za utajiri (2) kujenga msingi imara na wa uhakika. Wenye hekima wanafanya vyote! Kwa waaminio wao wanashikilia uzima wa kweli (yaani uzima wa milele, kama vile 1 Tim. 6:12).

**NASB** **"uzima kweli kweli"**
**NKJV** **"uzima wa milele"**
**NRSV** **"uzima ambao kiukweli ni uzima"**
**TEV** **"uzima ambao ni uzima wa kweli"**
**NJB** **"peke wa hivyo ni hakika"**

Aina ya fasiri za Kingereza zinahusisha uchaguzi wa

1. *ontōs* – MSS א, A, D*, F, G
2. *aiōniou* – MS D²
3. zote mbili – ndogo ndogo 69, 296, 467, na 1175 (wanakili hawa lazima walikuwa na maandiko ya Kiyunani ambayo yalikuwa na chaguzi zote mbili)

Toleo la UBS⁴ linatoa uchaguzi #1 na alama ya "A".

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 TIMOTHEO 6:20-21**
***20*** **Ee Timotheo, ilinde hiyo amana; ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo na maana, na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo;** ***21*** **ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani. Neema na iwe pamoja nanyi.**

**6:20-21** Mistari hii ya hitimisho (pia yawezekana 1 Tim. 6:17-19) inaweza kuwa iliandikwa na Paulo mwenyewe kuthibitisha barua (kama vile 2 Thes. 3:17-18).

**6:20 "ilinde hiyo amana"** Kile KITENZI ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Neno "waliopewa amana" inahusiana na neno la Kibenki "kuweka pesa," ambayo inatumika mara tatu katika barua za kichungaji "Injili" (kama vile 1 Tim. 1:11, angalia dokezo kamili katika 1 Tim. 1:18) au taarifa ya ukweli wa Mkristo (kama vile Mdo. 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 1:3,20). Waaminio ni mawakili wa injili (kama vile 1 Kor. 4:1-2; 2 Tim. 1:12,14).

◙**"ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo na maana, na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo"** "kuepuka" ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO iliyotumika kama SHURUTISHI. 1 Timotheo ni barua kimsingi juu ya uzushi, sio utaratibu wa kikanisa. Miongozo katika kitabu moja kwa moja inahusiana na matatizo yaliyosababishwa na walimu wa uongo na sio lazima kuwa miongozo kwa ajili ya makanisa yote ya kijumla ya wakati wote katika maeneo yote.

◙**"elimu"** Walimu wa uongo katika Barua za kichungaji ni muunganiko wa "wasomi wa sheria wa Kiyahudi" na wenye ujuzi Wayunani (kwa mfanano ule ule tu wa Kolosai na Efeso). "Maarifa," siku zote siri au hasa maarifa yaliyofunuliwa kwao ndivyo vilikuwa madai ya walimu hawa. Walimu hawa wa Uongo walitenganisha ukweli n uzima, kuhesabiwa haki na utakaso na kugeuza wokovu kuwa siri, maarifa maalumu yaliyotalakishwa kutoka katika utauwa.

**6:21**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani"** |
| **NKJV** | **"ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani"** |
| **NRSV** | **"ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani "** |
| **TEV** | **"kwa wengine wamedai kuwa nayo na matokeo yake wamekosa njia ya imani"** |
| **NJB** | **"kwa kufanya hili, wengine wamekosa lengo la imani"** |

Neno hili hili limetumika katika 1 Tim. 1:6 kuelezea walimu wa uongo; pia tazama 1 Tim. 1:19; 4:1-2; 5:15; 6:10. Kuna maonyo makali mengi katika kitabu hiki!

Kumbuka kuwa Ukristo ni (1) kukaribisha mtu; (2) mafundisho ya kuaminiwa; na (3) maisha yanaorandana na kilichoaminiwa na kuishi hivyo! Ikiwa kimoja kati ya hivi kitaondolewa katika kusisitizwa au kuachwa kando, basi matatizo makubwa yatatokea (kama vile Mt. 7:21-27).

◙ **"Neema na iwe pamoja nanyi"** Ile "nanyi" ni WINGI (MS D). Hii inaonesha kwamba barua ingawa ilikuwa imeandikwa kwa mtu mmoja (umoja "nanyi" katika MSS א, A, F, G), ilitakiwa kusomwa kwa wazi. Tazama Paulo anaomba kwa ajili yao neema ya Mungu na maarifa ya kweli (kama vile 1 Tim. 6:20)! Huu umaliziaji wa WINGI huu upo katika barua zote za Kichungaji (kama vile 2 Tim. 4:22; Tito 3:15).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Kanisa la Kikristo halikushambulia suala la utumwa? (Vifungu vingine vya Paulo ambavyo vinashughulikia watumwa ni 1 Kor. 7:21-24; Gal. 3:28; Efe. 6:5-9; Kol. 3:22-25; Filemoni 1:16,17; Tito 2:9; 1 Pet. 2:18).
2. Nini mistari ya 1 na 2 kinazungumzwa juu ya mahusiano kati ya mwajiliwa na mwajiri wa siku zetu za leo?
3. Nini maana ya uvumi?
4. Kuna tofauti gani kati ya walimu wa uongo na tofauti katika fasiri?
5. Je kuwa na pesa ni uovu?
6. Elezea kadiri unavyoweza thiolojia ya walimu wa uongo.

# UTANGULIZI WA TITO

I. Historia fupi

A. Tito ni sehemu ya mkusanyiko wa barua za Paulo zijulikanazo kama "Barua za kichungaji." Hii ni kwasababu 1 Timotheo, Tito, na 2 Timotheo inashughulikia maonyo ya wafanyakazi wenza katika

1. namna ya kukabiliana na walimu wa uongo
2. namna ya kuimarisha uongozi katika makanisa ya nyumbani
3. namna ya kutia moyo utauwa

Mtiririko dhahiri wa kimantiki wa vitabu hivi ni: 1 Timotheo na/au Tito baadaye, 2 Timotheo. Tito anashughulikia mambo yale yale kama 1 Timotheo. Tito inaweza ikawa iliandikwa kwanza kwasababu utangulizi wake ni mrefu na unahusisha thiolojia kama ilivyo kwa Warumi.

B. Safari za kijiografia za Paulo na wafanya kazi wenza hawa hawashabihiani katika safari za Paulo katika Mdo. Hivyo wengi (mimi nikijumuishwa) nadhania kwamba huu ni ushahidi kwamba Paulo aliachiwa kutoka gerezani na kuanzisha safari ya kimisioanari ya nne.

C. Tarehe kwa ajili ya safari hii ya kimisioanari inaweza kuwa kati ya mwanzoni mwa miaka ya 60 B.K mpaka 68 B.K. kwasababu Paulo alikamatwa na kuwekwa kizuizini chini ya Nero na Nero alijiua mwenyewe mnamo mwaka 68 B.K (wengi wanadhania katika mashitaka yake mnamo mwaka 65 B.K).

II. Mtu aitwaye Tito

A. Tito alikuwa mmoja wa wafanyakazi wa Paulo walioaminiwa sana. Hii inawekewa ushahidi na ukweli kwamba Paulo alimtuma kwa makanisa yenye migogoro ya Korintho na Krete.

B. Alikuwa mtu wa Mataifa kwa asilimia zote (Timotheo alikuwa chotara wa Kiyunani), aliyeongoka kupitia mahubiri ya Paulo. Paulo alikataa kumtahiri (kama vile Gal. 2:3).

C. Anatajwa katika barua za Paulo mara kwa mara (kama vile 2 Kor. 2:13; 7:6-15; 8:6-24; 12:18; Gal. 2:1-3; 2 Tim. 4:10) na inashangaza sana kwamba Luka hamtaji yeye katika Mdo. Baadhi ya fasiri zinaweka nadharia kwamba

1. anaweza kuwa alikuwa ndugu wa Luka (yawezekana kaka) na kujumuisha jina lake ingeweza kuonekana tendo la ubaguzi wa kimila kwa upande wa Luka
2. Tito ni chanzo kikubwa cha taarifa juu ya maisha ya Paulo na huduma na hivyo kama Luka asingeweza kutajwa

D. Alikuwa msindikizaji wa Paulo na Barnaba sehemu zote muhimu za Baraza la Yerusalemu zilizoandikwa katika Mdo. 15, ambapo jambo la uhusiano mpya wa waamini wapya Mataifa kwa mujibu wa Sheria ya Musa lilizua mabishano na mjadala na kumalizwa.

E. Kitabu hiki kinajikita katika ushauri unaotolewa na Paulo kwenda kwa Tito juu ya huduma yake huko Krete. Tito anatenda kazi kama mjumbe msaidizi rasmi wa Paulo.

F. Taarifa za mwisho katika Agano Jipya juu ya Tito ni kwamba alitumwa kuhudumu huko Damaltia (kama vile 2 Tim. 4:10).

III. Walimu wa Uongo

A. Kwa dhahiri kundi la walimu wa uongo huko Krete ambao walipinga injili ya Paulo.

B. Mafundisho yao ya kithiolojia yalipelekea mgogoro na mtindo wao wa maisha ya utauwa ambao unategemewa kwa waaminio wote.

1. rejea kwa maisha ya utauwa: Tito 1:1,16; 2:7,14; 3:1,8,14
2. muhtasari wa sifa za kitabia: Tito 2:11-14; 3:4-7

C. Kuna ladha ya dhahiri ya Kiyahudi kwa fundisho hili la uongo (kama vile Tito 1:10,14; 3:8-9). Vumi hizi ni muunganiko wa sheria za Kiyahudi na madhanio ya Kiyunani (nadharia ya ujuzi wa pekee, angalia Mada Maalum katika Tito 1:1). Zinafanana na walimu wa Uongo zinazosemwa katika 1 Timotheo, Kolosai, na Efeso. Shabaha ya Barua za Kichungaji upo juu ya uvumi na haizungumzii utaratibu wa kanisa.

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# TITO 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Salamu | Salamu | Salamu | Salamu za wazi | Maelezo |
| 1:1-4 | 1:1-3 | 1:1-3 | 1:1-3 | 1:1-4 |
| | 1:4a | 1:4a | 1:4a | |
| | 1:4b | 1:4b | 1:4b | |
| Kazi zaTito huko Krete | Wazee wenye sifa | Mwakilishi | Kazi za Tito huko Krete | Kuweka wazee |
| 1:5-9 | 1:5-9 | 1:5-9 | 1:5-9 | 1:5-9 |
| | Kazi za wazee | | | Kinyume cha Walimu wa uongo |
| 1:10-12a | 1:10-16 | 1:10-16 | 1:10-16 | 1:10-14 |
| 1:12b-16 | | | | |
| | | | | 1:15-16 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure),Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi(Textual Criticism),Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko(Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 1:1-3**
1 **Paulo, mtumwa wa Mungu, na mtume wa Yesu Kristo; kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu, na ujuzi wa kweli ile iletayo utauwa;** 2 **katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele;** 3 **akalifunua neno lake kwa majira yake katika ule ujumbe niliowekewa amana mimi kwa amri ya Mwokozi wetu Mungu;**

**1:1 "Paulo"** wayahudi wengi siku za Paulo walikuwa na majina mawili ya mwanzo,moja la kiyahudi, moja la kirumi (kama vile Mdo. 13:9). Jina la Paulo la kiyahudi ni Sauli. yeye, kama mfalme wa zamani wa Israeli,alikuwa wa

kabila la Benyamini (kama vile.  Rum. 11: 1; Fil. 3:5).  Jina lake la kirumi kwa muundo wa Kiyunani,Paulo (Paulo),linamaanisha “dogo.”Hili linarejelea

1. kimo chake cha mwili ambacho kinadokeza karne ya pili vitabu visivyo vya kikanoni, *The Acts of Paul,* juu ya sura iliyoitwa Thesalonike "Paulo na  Thekla"
2. maana yake binafsi ya mtumishi mdogo kwa sababu hapo mwanzo alilitesa kanisa (kama vile. 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15)
3. ni jina alilopewa na wazazi wake alipozaliwa

Chaguo #3 linaonekana ni bora zaidi.

◙ **"mtumwa wa Mungu"** hiki ni cheo cha heshima kilichotumika kwa viongozi wa Agano la kale (kama vile Kumb. 34:5; Yos. 1:1-2; 14:7; 24:29; 2 Sam. 7:5,8; 2 Fal. 10:10; Zab. 89:3; 105:42; Isa. 20:3; Dan. 6:20; 9:11). Paulo kwa kawaida alitumia tungo “mtumwa wa Kristo” (kama vile. Rum. 1:1; Gal. 1:10; Fil. 1:1). Hata hivyo, hapa alikuwa "mtumwa wa Mungu." Hili jambo linalenga kwamba hawa walimu wa uongo kwa jinsi gani walikuwa na uhusiano na Uyahudi.

1. Mungu ametajwa mara tano kwa uwazi kwenye nyaraka hii (kama vile. Tito 1:1-4).
2. hii yumkini pia ikaelezwa kwanini jina la "mkombozi" limetumika mara tatu kwa ajili ya Mungu Baba kama lilivyotumika mara tatu kwa ajili ya Kristo.
3. ni dhahili kutoka  2 Tim. 1:10,14; 3:8-9 kwamba alikuwa na asili ya Kiyahudi iliyoleta mabishano huko Krete.

◙ **"mtume"** hii ni wazi "aliyetumwa,"ambalo linahusisha walimu wa kiyahudi ambao wa mmojawapo wa wajumbe wenye mamlaka. Tazama mada maalumu katika 1 Tim. 1:1. Hili linafanana na dhana yetu ya mjumbe (kama vile. 2 Kor. 5:20). Haya pia ni madai ya Paulo na kuimarisha mamlaka yake katika kristo, kama jina lililopita la “mtumwa wa Mungu”. Aliimarisha utambulisho wake na hivyo kumtia nguvu Tito. Nyaraka hii inaweza kusomwa kwa kanisa zima kama WINGI wa 1 Tim. 6:21; 2 Tim. 4:22; na Tito 3:15 inaonyeshwa wazi kabisa.

◙ **"kwa ajili ya imani"** NOMINO haina KIBAINISHI CHA WAZI; hivyo basi, inaweza kurejelea

1. binafsi anamwamini kristo
2. waaminifu walio hai (maana ya Agano la kale)
3. mafundisho ya mwili wa kristo (kama vile Mdo. 6:7; 18:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; 6:10; Flp. 1:27; Yuda 3,20)

Umisionari wa Paulo zaidi ulikuwa wa

1. kuimarisha imani kwa wale waliookolewa
2. kuwaleta wale waliookolewa milele kuja kwenye imani binafsi ("kuita walioitwa")

Wote ni muhimu, lakini kile kinachosisitizwa hapa kina mashaka.
Paulo ametumia *kata* mara kadhaa kwenye sura iliyo wazi.

1. kulingana na imani, Tito 1:1
2. kulingana na utakatifu, Tito 1:1
3. kulingana na amri, Tito 1:3
4. kulingana na imani ya kawaida, Tito 1:4
5. kulingana na kuchaguliwa, Tito 1:5 (neno lililochanganywa)
6. kulingana na mafundisho, Tito 1:9

Kwa wazi kuna kiwango cha ukweli na tabia (kama vile. Tito 3:5,7).

◙ **"wateule wa Mungu"** hii ni wazi “kulingana na imani ya aliyechaguliwa”. Kwenye Agano la kale uchaguzi ulitumika kumtumikia Mungu, ambapo katika Agano jipya umetumika kama kuokolewa Mungu (kama vile. Rum 8:29-30; 9:1 na kuendelea; Efe. 1:4-11; 2 Tim. 1:9). Maana hii ya uchaguzi imeelezwa vizuri katika Mdo 13:48. Kanisa limechaguliwa na Mungu (kama vile Rum. 8:32; Kol. 3:12; 2 Tim. 2:10). Kanisa sio mwili mpya, lakini ni uenezi wa watu wa Mungu wa Agano la kale. Tazama mada maalumu:Uchaguzi (Kuamriwa kabla) katika 1 Tim. 6:12.

◙ **"ujuzi"** Hili ni neno la kiyunani lililochanganywa *epiginōskō,* ambalo linamaanisha wingi wa ufahamu wa ujuzi. Hii ni nahau ya kweli ya mabadilishano (kama vile Yn. 8:32; 1 Tim. 4:3; 2 Tim. 2:25; 1 Yn. 2:21; 3 Yn. 1). Hii ilikuwa ni tofauti kwa walimu wa uongo ambao mkazo wao ulikuwa kwenye ujuzi wa siri ambao haukusimuliwa kwenye maisha ya utakatifu. Tungo kama hii imetumika kwenye 1 Tim. 2:4, lakini ikiwa na mkazo wa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya wanadamu wote!

## MADA MAALUM:UJUZI WA KIPEKEE

Walimu wenye mafunuo ya uongo waliamini kwamba viumbwavyo, ulimwengu (maada) ni ovu, na kwahiyo katika upinzani wa ulimwengu wa roho, na kwamba roho tu ndiyo njema. Walijenga Mungu muovu na viumbe ya Agano la Kale kuelezea uumbaji wa ulimwengu (maada) na kumfanya Yesu Kristo kama Mungu kamili wa kiroho.

Imani za Walimu wajuzi wa uongo zinapingana kiukubwa na mafundisho yanayokubaliwa na mkristo. Ukristo unatufundisha kwamba wokovu unapatikana kwa kila mtu, sio wateule wachache na kwamba inakuja kutoka neema kupitia imani katika Yesu Kristo (Waefeso 2:8-9), na kutoka katika masomo au kazi. Chanzo cha ukweli ni Biblia tu, Ukristo unaelezea.

Walimu wa uongo walimngawanya kwa Yesu. Mtazamo mmoja ni kwamba alitokea tu kuwa na umbo lake la kibinadamu lakini kwamba alikuwa katika roho tu. Mtazamo mwingine uliweka wazi kwamba roho yake ya kiungu ilikuja juu ya mwili wake katika Ubatizo na kuondoka kabla ya kusulubiwa. Ukristo, kwa upande mwingine unashikilia kuwa Yesu alikuwa mwanadamu kamili na Mungu kamili na asili hizi zote zilikuwepo na muhimu kutoa sadaka ya kupendeza kwa dhambi ya ubinadamu.

◙ **"kweli ile iletayo utauwa"** hii tofauti kubwa na ya kipekee kwa walimu wa uongo. Wanatilia mkazo ujuzi kama viongozi wa kuongoza kundi. Ukweli ni lazima usimuliwe kwenye maisha ya kila siku (kama vile. 1 Tim. 2:2). Utauwa au ucha-Mungu (*eusebeia*) ni dhana ya kwaida kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile 1 Tim. 2:2; 3:16; 4:7,8; 6:3,5,6,11; 2 Tim. 3:5; Tito 1:1; muundo uliochanganywa, *theosebeia*, kwenye 1 Tim. 2:10; na KIVUMISHI *eusebōs* kwenye 2 Tim. 3:10; Tito 2:12). Tazama mada maalumu katika 1 Tim. 4:7.
Hii ni wazi inaakisi makosa ya walimu wa uongo. Waaminio sio tu wanaitwa kwenda mbinguni wanapofariki, lakini kufanana na kristo sasa (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 Thes. 3:13; 4:3). Kusudi la injili halitatimia mpaka wote tumfahamu mwokozi na kuakisi tabia yake. Tazama mada maalumu: kweli katika maandiko ya Paulo katika 1 Tim. 2:4.

**1:2 "katika tumaini la uzima wa milele "**KIHUSISHI *epi* kinadokeza "kupumzika kwenye." Toleo la RSV na TEV yana "ambao msingi." Kuna utata wa wa neno hili "tumaini" juu ya kukamilisha mpango wa Mungu wa milele wa wokovu.

Uzima wa milele kwenye maandiko ya Paulo mara zote ni maisha ya enzi mpya, maisha ya matukio ya siku za mwisho (kama vile Rum. 2:7; 6:22,23; Gal. 6:8; 1 Tim. 1:16; Tito 1:2; 3:7). Kwenye maandiko ya Yohana yanarejelea ukweli wa sasa ambao msingi wake uko kwenye kumwamini Kristo kama mwokozi (kama vile. Yn 3:15; 10:28; 12:25; 17:2-3; 1 Yn. 1:2; 2:25; 3:15; 5:11,13,20). Yote ni kweli. Enzi mpya ilianza na ujio wa kwanza wa Kristo. Waaminio tayari ni sehemu hii ya enzi mpya. Enzi mpya itakamilishwa katika ujio wa pili.

Tazama MADA MAALUMU:UMILELE katika 1 Tim. 6:8.

## MADA MAALUM: TUMAINI (*elpis*, kwa Paulo)

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano., 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

◙ **"Mungu asiyeweza kusema uongo"** Imani yetu inakaa kwenye uaminifu na kutumainiwa kwa Mungu juu ya ahadi zake (kama vile. Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Rum. 3:4; 2 Tim. 2:13; Ebr. 6:18). Tumaini letu linakaa kwenye tabia ya Mungu isiyobadilika (kama vile. Zab. 102:27; Mal. 3:6; Ebr. 13:8; Yakobo 1:17).

◙ **"aliuahidi tangu milele"** hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. SAUTI YA KATI inatilia mkazo jambo, Mungu (kama vile Rum. 4:21; 2 Tim. 1:9). Tungo hii "tangu milele" ni wazi "milele kabla ya nyakati" (tazama mada maalumu katika 1 Tim. 4:10). Hii yumkini ikarejelea ahadi za ukombozi wa Mungu na kuona mbele zaidi kabla ya uumbaji (kama vile Mt. 25:34; Yn. 17:24; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:19-20; Ufu. 13:8).

## MADA MAALUM: UMRI NA UTENGENEZAJI WA NCHI (DUNIA)

I. Sehemu hii ya kujifunza ina upendeleo kwasababu ya makisio kwamba yanatakiwa yafanywe kwa hata kutafta kufikiri sahihi kuhusu somo. Makisio lazima yawe na shabaha ya kutathminika kwa kutofautiana kwa maoni yanayoelezewa na wanaanga, wanajiolojia na sayansi zinazofanana na hizo ukilinganisha na uelewa wa kithiolojia na fasiri.

II. Katika sayansi madhanio yake ya dhahiri ni:
   A. kwamba kiwango cha mabadilio (yaani kimwili, kikemikali na kibaiyolojia) kunakowekwa kumbukumbu na kupimwa duniani leo hakubadiliki huko nyuma (nadharia ya kuendana saresare, "ya sasa ni msingi kwa ya kale")
   B. Kuwekwa tarehe ya upimaji wa mionzi (kunakoitwa tarehe kamili), ambayo ndiyo msingi wa kufuatana kwa kuwekewa tarehe kwa matukio ya dunia na anga lote kuwawekea msingi wa kitanda kiovu cha makisio kadhaa:
      1. yaani utengenezaji wa asili wa miamba(yaani uhusiano wa chembe chembe mama na

mwana za kiatomiki zisizo imara)

2. maisha yasiyo kamili ya elementi hizi
3. joto pia linaathiri viwango vya kiasilimia vya mwamba mama na vizaliwa katika sampuli ( yaani muda wa utengenezwaji na/au vyumba vya ujiuji wa kivolkeno)
4. Chanzo cha asili na muda wa uumbaji wa elementi za utoaji wa mionzi hakijulikani. Nadharia za kisasa zinzsema kwamba namna ambavyo elementi ni nzito zinatengenezwa na mkutano wa nyuklia za joto katika sekunde na kizazi cha tatu cha nyota na kuenea kwa njia ya kulipuka kwa nyota.

C. kwamba ya sita ilikisia mfuatano wa kanuni za jiolojia (ziitwazo tarehe zinazohusiana) zinazoathiri elimu juu ya mabaki ya wanyama na mimea:
   1. sheria ya nafasi ya juu ya Dhambi na mfuatano usiosumbuliwa wa miamba ya mashapo, safu ya sakafuni (chini) juu na safu ya kati chini yake ni kuu kuu (ya zamani)
   2. Kanuni ya asili ya mlalo-safu ya miamba ya mwando ilirundikwa karibia na uwanda wa mlalo
   3. Kanuni ya uhusiano wa mkato-wakati miamba ikikatwa au kusawazishwa na mpasuko, lazima ziwe zenye umri kubwa zaidi ya mpasuko
   4. kanuni ya ujumuisho wa miamba S mikubwa iliyopakana yenyewe kwa yenyewe, moja siku zote utakuwa na vipande vya kubebana moja chini katika safu ya juu ambayo inathibitisha makisio ya #1
   5. kanuni ya uwiano wa mimbaS ya maumbo sawa lakini kutoka katika maeneo tofauti tofauti lazima yalinganishwe na kufananishwa, wakati hili haliwezi kufanyika hivyo mabaki ya wanyama na mimea yanatumika kuonesha tarehe zinazofanana za uumbaji
   6. kanuni ya mabaki S ya viumbe haikutangulia moja baada ya nyingine katika namna inayoeleweka na mfuatano wa uashiria:
      a. utawanyikaji mpana wa mabaki ya viumbe
      b. kuwepo kwa ukomo wa muda mfupi wa muda wa kijiolojia

III. maoni kadhaa ya wanasayansi

A. Wanasayansi wengi wanatambua kwamba sayansi ya kweli ni mbinu ya kitafiti ambayo inatafuta kupatanisha kweli zinazojulikana na makosa katika nadharia zinazojabika. Baadhi ya vitu kwa asili yake vyenyewe havijaribiki.

B. Baadhi ya maoni kutoka kwa wanasayansi kuhusu makisio ya kisayansi katika eneo hili

1. "Mafundisho (yaani nadhania ya U-yunifomu) haitakiwi kuchukuliwa kiuhalisia. Kusema kwamba michakato ya kijiolojia wakati wa nyuma haikuwa kama ile inayotokea leo sio kupendekeza kwamba zilikuwa siku zote na umuhimu za kimahusiano na kufanya kazi vizuri kabisa kwa kiwango kilekile" (Tarbuck na Lutgens, *Earth Science,* 6th ed. Ukrasa wa 262).
2. "Ni muhimu kutambua kwamba tarehe ya ukwel; wa upimaji wa mionzi inaweza kupatikana tu ikiwa madini yataendelea katika mfumo uliofungwa wakati wa kipindi cha uundwaji wake; hiii ni kwamba tarehe sahihi haiwezekani mpaka kulikuwa hakuna kuongezeka ama kupungua kwa mwamba aisotopu mama au mtoto" (*Earth Science,* 6th ed. Ukurasa wa 276).
3. "Tunachelea kusisitiza kwamba uyunifomu huu ni madhanio kwamba tunatengeneza asili, hivyo ni fundisho kuliko sheria ya kuthibitishwa kimantiki" (Dott na Balten, *Evolution of the Earth*, 4th ed. Ukurasa wa 44).
4. "Kuendelea kuoza bila kukoma kunaweka tabia ya kiwango cha kuoza kutoa mionzi na kutawala uhusiano kati ya taarifa za ki-isotopu na mrejeo wa nyakati za radio isotopu. Kwa matokeo, usahihi wa

baadhi ya mbinu bora za uwekaji wa tarehe kama vile mbinu ya 40Ar/39Ar, inaweza kuwa utaratibu wa ukubwa au mbaya zaidi kuliko usahihi wake ("Progress and challenges in geochronology" cha Renne, Ludwig na Karner katika *Science Progress* (2000), 83 (1), 107).

5. "Watu bila mafunzo ya kisayansi hawawezi kuelewa kwamba mbinu yoyote ya upimaji wa mionzi ya uwekaji wa tarehe inaweza tu kuaminiwa kwa sampuli pamoja na umri karibu na nusu umri wa elementi inayoulizwa (Hugh Ross, *Reasons to Believe* newsletter).

IV. Makisio sio ya upekee wa jamii ya kisayansi lakini kwa uwazi pia yanatukia katika jamii ya kidini

A. Wanadamu wanaletwa karibu kna kanuni ya uletaji umoja au mfano kupatanisha maana zao za uzoefu na kutoa uthabiti wa kihisia. Katika sayansi kanuni hii ya uunganishaji pamoja imekuwa "mabadiliko"

1. Theodosius Dobzhansky, "Changing man," *Science*, 155, 409-415, "Mabadiliko ni mchakato ambao umezalisha maisha kutoka pasipo kuwa na maisha, ambayo imeleta mwanadamu kutoka katika wanyama na ambalo linaweza kuendelea kufanya vitu vya kushangaza katika siku za usoni."
2. Brian J. Alters and Sandra M. Alters, *Defining Evolution*, ukurasa wa 104, "mabadiliko ni msingi wa muktadha wa sayansi za kibaiyolojia... mabadiliko ni muundo unaoelezeka, nadharia inayounganisha. Ni sharti kusoma biolojia kama nadharia ya ki-atomiki ilivyo lazima kujifunza kemia."

B. Kwa wakristo wengi wenye kushikilia msimamo nadharia ya uunganishaji (yaani ufasiri) imefanyika ufasiri halisi wa Mwanzo 1-3. Hii ni kweli kwa wanahalisia wa dunia changa (*Creation Research Society* inaweka tarehe ya dunia kama miaka 10,000) na wanahalisia wa nchi kuu kuu (*Reasons to Believe* wanaweka tarehe ya dunia katika ufahamu wa jiolojia ya kisasa miaka bilioni 4.6). Tafsiri ya mtu ya maadiko inakuwa kioo ambacho kupitia kwacho vitu vingine vyote vinaonekana na kutathminiwa. Mtu hawezi kupasua makisio yanajikita juu ya maoni ya mtu, kwa kuwa maarifa ya kibinadamu katika ya viwango fulani ni kufikirika na kukisia kabla. Hatahivyo, tathmini ya madhanio ya mtu ni muhimu kwa ajili ya tathmini sahihi ya kauli za "kweli" yao.

C. Ukristo wa kimsingi ni kujaribu kujivika wenyewe hoja za "kisayansi" pale ambapo jambo jambo kuu ni tafsiri za kimbinu. Hii ni kumaanisha kwamba "sayansi ya mabadiliko ya sasa" sio ya kufikirika kabla au kwamba hitimisho lake halichongwi na mtazamo wa kiulimwengu wa kabla. Lazima tuwe makini na kuwa na ufafanuzi wa vyote. Hapo panaonekana kuwa na ushahidi wa pande mbili. Lazima nijiulize mwenyewe kwa mtazamo gani kwamba navutiwa nao kiasili, kihisia au kielimu (yaani makisio ya kujirishisha wenyewe)?

V. Hitimisho binafsi

A. Kwakuwa mimi ni mwana thiolojia na sio mwanasayansi, ilikuwa muhimu kwangu kusoma na kufananisha kadiri nilivyoweza kutoka katika sayansi za mfanano mmoja. Kibinafsi sisumbuliwi na "mabadiliko" lakini na "asilia" (maana moja iliyofanywa maarufu na Carl Sagan ni, "Ulimwengu ni vile ulivyokuwa na vile utakavyokuwa"). Natambua kwamba huu ni ubaguzi na upendeleo lakini nadharia yangu ya kuweka pamoja ni uasilia wa kupita kawaida na uumbaji maalumu lakini sikatai au kujiskia kutishwa na nadharia ya mabadiliko. Mtazamo wangu wa msingi ni kwamba kuna Mungu ambaye alianzisha na anaongoza mchakato kwa ajili ya kusudi! Kwangu mimi "uumbaji wenye akili" inakuwa nadharia ya kimantiki (kama vile M. J. Behe, *Darwin's Black Box* na William A. Demski, ed. *Mere Creation: Science, Faith and Intelligent Design*). Ni "kutawanyika" kwa mabadiliko "kutokuwepo kwa wakili" wa asili ambao

unanisababishia maumivu binafsi na kuchanganyikiwa. Mchakato ni sehemu ya maisha. Lazima niwe na hakika kwamba sishikilii kile ambacho kinaleta faraja bila tathmini. Nimejaribu kubainisha makisio yangu:

1. Mwanzo 1-3 (na kwa namna hiyo zaidi kitabu cha Ufunuo), hakikusudiwa na mwandishi wake wa asili aliyevuviwa kuchukuliwa kibayana. "Namna yote yalivyoanza" na "kwa namna gani vyote vitakavyoisha" imefumbwa (na lazima iwe kwa mwanadamu aliyeanguka) katika aina za kifasihi.
2. Mabadiliko yako wazi katika viwango fulani ("mabadiliko mlalo," "mabadiliko madogo madogo," mabadiliko nadani ya viumbe) lakini sio sababu kiunganishi pekee. Kuna fumbo na jambo la kushangaza hapa! Binafsi najisikia vizuri na Biblia (yaani ufunuo maalumu) unaoniamba "nani" na "kwa nini" na asili (yaani ufunuo wa asili), ambayo ni utafiti wa sayansi ya kisasa unaoniambia "namna gani" na "lini" ikijikita kwenye mifano, vielelezo na nadharia.
3. Hata kilele cha uhalisia wa "mabadiliko ya kiimani juu ya Mungu kama mtawala wa dunia" hauwezi kusababisha mimi kukataa makisio yangu yoyote ya imani. Angalia Darrel R. Falk, *Coming to Peace with Science: Bridging the World's Between Faith and Biology* naFrancis S. Collins,*The Language of God*.Ninayo madhanio ya imani (kama wewe ulivyo nayo)! Mtazamo wangu wa kiulimwengu wa Kibiblia jii ya Ukristo.Taswira yangu ya kiulimwengu inakua na kubadili uelewa wangu.

B. Umri "halisi" wa dunia sio jambo kubwa katika thiolojia yangu isipokuwa:
   1. Dhana inayoonekana ya "Big Bang (kutokea ghafla)" kwa mpangilio wa kiulimwengu wa maada ambayo inaelezea mwanzo wa ulimwengu unaonekana kuweka ukomo wa uwezekano wa muda usio na kikomo kwa maendeleo ya kimabadiliko (yaani uasili).
   2. Kuanza na kuhitimishwa katika kumbukumbu za mabaki ya viumbe "uingizaji wa ulinganifu" ambayo inaelezea kwamba nafasi ya mabadiliko inatokea katika kuchepusha (yawezekana matendo ya uumbaji ya Mungu yanayoendelea) na sio muhimu mabadiliko ya kihatua baada ya muda.
   3. Dunia ya kuu kuu na uumbaji maalum wa ubinadamu ni kielelezo kinachopendekezwa, nachagua kushikilia mpaka nielewe zaidi kutoka katika kujifunza Biblia, elimu ya viumbe wa kale. Utaratibu wa haya unaonesha ubaguzi (lakini sisi sote huwa tunao)!
   4. Sayansi sio adui kwangu, wala mwokozi! Inafurahisha sana kuishi katika hiki kizazi cha kuongeza maarifa! Inafariji sana kama mwamini kuwa na maarifa ya utafsiri wa neno la Mungu! Muingiliano wa imani na mantiki au Biblia na Sayansi na sifa ni uwezekano mzuri sana!

VI. Makisio ya sasa kama kwa kizazi cha dunia

A. Kuweka tarehe kwa miamba ya mwezini na vimondo kwa utumiaji wa mionzi imekuwa endelevu kwa miaka Bilioni 4.6. Zinajumuisha elementi ileile kama sayari za mfumo wa nyota hivyo kuhitimisha ni kwamba jua letu, vimondo na asteroidi vilifanyika wakati huu. Miamba ya zamani zaidi imetambuliwa kwa kutumia mionzi miaka Bilioni 3.8.

Tarehe ya kuumbwa kiungu kwa jozi ya kwanza ya binadamu (Homo sapiens) ni jambo gumu sana lakini ni utofauti wa nyuzi makumi elfu yawezekana 40,000. Angalia Fazale Rana na Hugh Ross, *Who was Adam?.*
Muda unakuwa ni jambo tu kwa wale sisi tulioumbwa katika mfululizo wa mpangilio wa muda fulani. Mungu haathiriwi na upitaji wa muda. Naamini dunia na mazingira yake yaliumbwa kwa muda kwa ajili ya kusudi maalumu ya utoaji wa "sehemu" kwa Mungu kufanya ushirika na uumbwaji wake wa juu walioumbwa na

yeye katika sura na mfano. Chanzo pekee kwa imani hizi ni Biblia iliyovuviwa. Nashikilia na kuruhusu sayansi ya kisasa kuongeza uelewa wa vipengele vya shughuli za Mungu za uumbaji!

**1:3**
**NASB, NKJV,**
**NRSV "kwa majira yake"**
**NJB "kwenye majira yake"**
**TEV "kwa majira muafaka"**

Tungo hizi ni WINGI (yaani., "milele kabla ya nyakati") na yumkini ikaaksi tukio zima la Kristo , (kama vile. 1 Tim. 2:6; 6:14-15; Gal. 4:4). Hii yumkini ikarejelea

1. kusambaa kote kwa lugha ya kigiriki ya Koine
2. amani ya kisiasa ya Rumi
3. matarajio ya kidini baada ya ulimwengu kupoteza heshima na manufaa kwenye miungu ya kale ya Kiyunani

◙ **"akalifunua"** hii inamaanisha "nuru ya wazi iliyoretwa" au "kufunuliwa wazi". Yesu amefunuliwa wazi kwenye injili na mahubiri ya mitume (kama vile. 2 Tim. 1:10).

◙ **"neno lake"** hii inaweza kurejelea (1) ujumbe wa injili juu ya Kristo au (2) Kristo mwenyewe (kama vile Yn. 1:1; Ufu. 19:13).

◙ **"niliowekewa amana mimi"** Paulo anaweka maana ya ndani zaidi ya utumishi wake wa injili (kama vile 1 Kor. 9:17; Gal. 2:7; 1 Thes. 2:4; 1 Tim. 1:11) na pia utumishi wa waaminio wote (kama vile. 1 Kor. 4:1-2 na 1 Pet. 4:10).

◙ **"mwokozi wetu Mungu"** hili ni jina la kawaida kwa ajili Mungu kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile Tito 1:3; 2:10; 3:4). Tazama muhtasari kamili katika 2 Tim. 1:10. Hata hivyo, kwenye kila muktadha pia umetumia Yesu (kama vile.1:4; 2:13; 3:6).ni jina (kama alivyo "Bwana") lililonenwa na Kaisari wa Rumi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 1:4**
**[4] kwa Tito, mwanangu hasa katika imani tuishirikiyo. Neema na iwe kwako na amani zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Mwokozi wetu.**

**1:4 "kwa Tito"** nyaraka hii inamwelezea Tito, lakini pia ilisomwa mbele za watu kwa makanisa yote (kama vile. WINGI wa "wewe" katika Tito 3:15). Tito alikuwa mtume mdogo mwamiminifu wa Paulo kwa mataifa. Sio jambo la kawaida kwamba hakutajwa kwenye kitabu cha matendo ya mitume (tazama utambulisho II. C.).

◙**"mwanangu hasa"** Paulo aliyatumia maneno haya sawa na kwa ajili ya Timotheo kwenye 1 Tim. 1:2 na "mwanangu" kwenye 2 Tim. 1:2 kwa Onesimo kwenye Filemoni 1:10. Ni sitiari inayofanana na kubadilika kwa Paulo na marafiki.

◙ **"imani tuishirikiyo"** "tuishirikiyo" haikutumika hapa na kidokezo cha najisi kama kwenye Mdo. 10:14 na 11:8, lakini kwenye kidokezo cha ulimwengu au kawaida. Tungo sawa imetumika kwenye Yuda 1:3. Ina maana ya kawaida kwamba ni kwa ajili ya wanadamu wote na inapatikana kwa wanadamu wote. Hii yumkini ikawaongoza wasio amini katika Mungu kwa viongozi walimu wa uongo na wenye kujitenga.

◙ **"Neema na iwe kwako na amani zitokazo kwa Mungu Baba"** maneno haya mawili mara nyingi yalikuwa ni muundo wa maombi ya wazi ya Paulo. Inawezekana kwamba "neema" (*charis*) ni mchezo wa maneno wa "salamu" (*charein*, kama vile Yakobo 1:1; Mdo. 15:23), neno linalofanana na la kiyunani kwamba lilifungua

nyaraka nyingi za Kiyunani. Paulo alichukua desturi ya kawaida wazi, *charein,* na kuibadilisha kuwa ya kikristo pekee *charis.*

Neno “amani” yumkini likaaksi salamu ya kawaida ya Kiebrania "*Shalom.*" kama ni hivyo basi, Paulo aliunganisha salamu za kiyunani na kiebrania kuwa salamu ya Kikristo.
Toleo la Textus Receptus (kama vile. Toleo la KJV) na machapisho ya kiyunani A, $C^2$, na K, yanaongeza "rehema" kwa neema na amani. Hii inawezekana ni usimilishaji kutoka 1 Tim. 1:2 na 2 Tim. 1:2. Muundo mfupi unapatikana kwenye machapisho א, $C^*$, D, F, G, na P kama vile toleo la kilatini la Vulgate. Toleo la $UBS^4$ linatupatia usomaji mfupi alama ya "A" (hakika).
Kwa ajili ya "Baba" tazama mada maalumu katika 1 Tim. 1:2.

◙ **"Kristo Yesu mwokozi wetu"** tungo hii inahusiana na Mungu Baba, YHWH wa Agano la kale, na Yesu Masihi kwa kutumia neno “mwokozi” (kama vile Tito 1:3-4; 2:10,13; 3:4,6). Yametumika kwa Mungu kwenye Tito 1:3 na Yesu kwenye Tito 1:4. Kutumia majina ya Agano la kale ya Mungu ni kumtumia Yesu ambayo ni njia ya kawaida kwa waandishi wa Agano jipya kutetea uungu wa Yesu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 1:5-9**
**5 Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; 6 ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. 7 Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno ,kwa kuwa ni wakili wa MUNGU;asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake,asiwe mwepesi wa hasira,asiwe mlevi wala mgomvi,asiwe mpenda mapato ya aibu. 8 bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; 9 akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga.**

**1:5 "kwa sababu hii"** kazi ya Tito ilikuwa ni (1) kupangilia mambo ambayo yamepungua au ambayo hajakamilika, na (2) kuwachagua wazee (kama vile. Mdo 14:23). Tatizo sio kurejesha muundo uliokwepo, ambao unathibitishwa kuwa mdogo, lakini kuimarisha muundo. Hapa tunaona aina tofauti ya muundo wa kisiasa zaidi ya 1 Timotheo 3, ambao unaelezwa kuimarisha kanisa la Efeso.tambua uteuzi wa Tito, sio kura ya baraza. Tambua tungo "kila mji." Kumbuka Timotheo na Tito wote ni mitume wadogo, sio wachungaji wa mahali au viongozi wa mkoa .

◙ **"Krete"** huu ni mji wa asili kwa Wafilisti na desturi za kabla ya Uyunani ndogo. Mdo 27:7-13 inaeleza kwamba Paulo alitembelea kisiwa hiki akiwa safarini kuelekea Rumi, lakini hakuna kumbukumbu kwamba alihubiri mahali hapo. Hii ni kwa nini wafasiri wengi (pamoja na mwandishi huyu) wanaamini nyaraka hizi za kichungaji zinaksi safari ya nne ya umisheni baada ya Paulo kufunguliwa toka kifungo na Rumi mwanzoni mwa miaka ya 60.

◙ **"ili"** Hii ni *hina* (sehemu ya kusudi) hivyo maelezo ya nyaraka za Paulo (kama vile Tito 1:9,13; 2:4,5,8,10,12,14; 3:7,8,13,14).
Paulo alimtaka Tito;

1. kutengeneza (KAULI YA KATI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) yaliyopungua
2. kuweka (KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) wazee

◙ **"kuweka"** KITENZI hiki “kuweka” kinamaanisha "kuweka kwenye mamlaka ya." KITENZI kama hiki kimetumika kwa mitume "kuwachagua watu saba” kwenye Mdo. 6:3.ni kazi ya mamlaka.
Paulo alimwelekeza Tito kuweka wazee kwenye haya makanisa mapya kama alivyofanya yeye na Barnaba walivyofanya kwenye Mdo. 14:23. Paulo hakumwelekeza Timotheo kufanya kazi hiyo kwa sababu makanisa ya Efeso ni kazi ambayo ilikwisha imarishwa (kama vile 1 Timotheo 3).

◙ **"wazee"** Neno *presbuteroi* ni kisawe na "wasimamizi" (kama vile. Tito 1:7) na "wachungaji" (kama vile. Mdo 20:17,28; Tito 1:5,7). Neno hili lina mpangilio wa kiyahudi, ambapo "wasimamizi" lina mpangilio wa wasimamizi wa kisiasa wa mji wa Kiyunani. Tambua sifa kwenye 1 Tim. 3:6 kwamba asiwe mtu aliyeongoka karibu asije akaanguka. Hii inadokeza haya makanisa mapya yaliyoanzishwa. Tazama MADA MAALUMU:WAZEE katika 1 Tim. 5:1.

◙ **"kama vile nilivyokuamuru"** hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Tito alikuwa anatenda kama mbadala wa mtume Paulo.

**1:6 "ikiwa"** hii ni KAULI YA DARAJA LA KWANZA. Paulo alihakikisha kunakuwa na watu waliofundishwa kila mji.

**NASB "hakushitakiwa"**
**NKJV, NRSV "sio na lawama"**
**TEV "pasipo lawama"**
**NJB "tabia isiyoshutumiwa"**

Huu ni ufunguo wa sifa zote, hasi na chanya, ya vyote 1 Timotheo na Tito (kama vile. Tito 1:6,7; 1 Tim. 3:2,7,10; 5:7; 6:14). Hili sio neno sahihi la kiyunani linalopatikana kwenye 1 Timotheo 3, lakini kisawe kimetumika hasa kwa namna ile ile. Huduma ni lazima iwe na mashahidi wazuri kwa ile jamii inayoamini na kwa jamii isiyoamini (kama vile. Tito 2:5,8,10; Mdo. 2:47; 4:4,31; 5:13,42). Tazama mada maalumu katika 1 Tim. 3:2.
Sifa hizi ni lazima zitafsiriwe kwenye nuru ya makusudi mawili: (1) viongozi ni lazima wakubaliwe na waaminio na wasioamini; uinjilisti ni lengo la mwisho na (2) viongozi ni lazima waonekane tofauti na walimu wa uongo . ni vigumu sana hasa kuelewa namna ya kutumia hizi sifa kwa tamaduni tofauti na muda wa nyakati. Waaminio ni lazima waangalie dhidi ya sheria ngumu za kihistoria, bado wangali wazi kuzipokea kanuni za Mungu. Kwa ufahamu wangu na makanisa ya kisasa ya magharibi ni kwamba:

1. wanahariri andiko moja au zaidi ya sifa hizi, lakini wakikana au wakiwashusha wengine thamani
2. wanaongeza hizi sheria na kudai ni mamlaka ya kibiblia kwa ajili ya nyongeza
3. wanatafsiri hizi sheria kwenye nuru ya siku zetu badala ya desturi ya karne ya kwanza, ambayo imevurugwa na walimu wa uongo
4. wanachukua tungo tata na kuzigeuza kuwa mafundisho ya sheria kwamba ulimwengu uyatumie

Tafadhari angalia mjadala kamili zaidi kwenye 1 Timotheo 3, www.freebiblecommentary.org.

◙ **"naye ni mume wa mke mmoja"** Tungo hii imesababisha mjadala zaidi. Ni dhahiri kwamba pia ni jambo muhimu kwa kanisa la Efeso (kama vile 1 Tim. 3:1,12; 5:7). Hii inaweza kurejelewa kwa;

1. mitala
2. kuoa tena baada ya kuachana
3. ndoa ya pili baada kufiwa mwenza
4. mtu ambaye ni mwaminifu na anaemjali mke wake na familia

Kanisa la mwanzo liliweka heshima kubwa kwenye mahusiano ya familia,na tatizo lolote kwenye hili eneo lilibatilisha nafasi ya uongozi kwenye kanisa.

1. Kwanza halikuwa tatizo kwenye utawala wa Kirumi lakini lilikuwa ni tatizo kwenye jamii ya kiyahudi (Yakobo, Elkana, Daudi, Suleimani).
2. Pili lilikuwa ni tatizo kubwa kwenye utawala wa Kirumi kama vile tatizo ndani ya Uyahudi ambao msingi wake ni mjadala wa waalimu wa sheria ya kiyahudi kati shule zenye kupenda utamaduni za Shammai na shule za kutaka mabadililko za Hillel.
3. Tatu ilikuwa na maana kubwa kwa kanisa la awali, hasa Tertullian, na bado ni tatizo katika ulaya; hata hivyo kwenye 1 Tim. 5:9 (kama vile Rum. 7:1-2; 1 Kor 7) wajane wanaweza kuolewa tena bila kulaumiwa.
4. Nne inasimulia kushushwa thamani ya ndoa na walimu wa uongo (kama vile. 1 Tim. 4:3). Kwa maana hii kuna njia nyingine ya kudai mahitaji ya familia, bado sio muhimu kwa mtu ambaye hajaoa (kumbuka Yesu na Paulo hawakuwa na wanawake).

◙ **"ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii"** hili limejadiliwa kwenye 1 Tim. 3:4-5). Uongozi bora unaweza kuonekana kwenye maisha ya nyumbani. Tofauti ngumu ya aina yeyote kati ya mume na mke au watoto na babu/bibi ulikuwa ni msingi uliozuiliwa kwenye utaratibu wa kanisa hili la awali. "hakukubaliana na shutuma" ilikuwa ni hofu yao kuu. Namna mtu alivyoongoza nyumba yake ingeonyesha vile angeongoza kanisa. Wengi wetu tunaofundishwa huduma tuwe na hofu juu ya sifa hizi! Mara nyingi wahubiri wadogo hawatii hata uwepo wa ucha-Mungu nyumbani na wazazi wacha-Mungu. Yumkini ni ukosefu wetu wa mafundisho kwenye jambo hili linaloweza kuaksi kwenda kwenye sifa zingine vizuri zaidi.

◙ Inawezekana Tito 1:6 inatumia mtoto wa mchungaji, au sifa zake mbili zaidi kwa ajili ya mchungaji? Njia zote zinalenga kwenye mtindo wa maisha ya kila siku na mtazamo unaoelekea kwenye mamlaka. Nafikiria kwa upana sifa zilizotajwa kwamba zinarejelea kwa kiongozi anaetazamiwa.

**1:7 "askofu"** neno hili *episkopon* kwa kawaida limetafsiriwa "mwangalizi" au "askofu." Muktadha unaonyesha kwamba unarejelea mtu Yule yule (kama vile Tito 1:5,7 na Mdo. 20:17,28). Neno hili ni la mji wa Kiyunani, utaratibu wa usimamizi wa kisiasa. Tazama muhtasari katika 1 Tim. 3:2.

◙ **"kama wakili wa Mungu"** hii inarejelea mtumishi wa nyumbani (kama vile. 1 Kor. 4:1; 9:17). Neno hili la kifamilia linasimuliwa kwa sifa kwenye Tito 1:6. Mchungaji kama mtu wa familia anaaksi ni kwa namna gani ataliongoza kanisa. Kuna tabia tano zisizofaa kwenye Tito 1:7 na tabia sita zifaazo kwenye Tito 1:8. Tazama MADA MAALUM: UOVU NA WEMA katika Agano jipya katika 1 Tim. 1:9.

**NASB, NKJV "asiwe wa kujipendeza nafsi yake"**
**NRSV, TEV "asiwe mwenye kujisifu"**
**NJB "asiwe mwenye kujisifu kamwe"**

Huu ni mchanganyo wa neno kutoka *autus* (binafsi) na *edomai* (furaha).inaelezea kwamba mtu ambaye ni mwenye kujipendeza, mkaidi, kujisifu, akijifurahisha (kama vile 2 Pet. 2:10).

◙ **"asiwe mwepesi wa hasira"** hili ni neno *orgē*, ambalo linarejelea hasira za haraka. Ni kinyume cha maneno "utulivu"na kimya " kwenye orodha ya sifa katika 1 Tim. 3:3. Hii inaelezea sifa za kiwango cha hasira au hasira kubwa za haraka.

**NASB, NRSV "asiwe mlevi"**
**NKJV "asiyependa mvinyo"**
**TEV "au mlevi"**
**NJB "wala mlevi sana"**

Hili linaonekana ni dokezo kutoka tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania ya Mit. 23:29-35. Ni lazima itiliwe mkazo tena kwamba Biblia inashutumu dhidi ya ulevi lakini haifundishi nidhamu binafsi kwa ujumla (kama vile. Mwa. 27:28; Zab. 104:14,15; Mhu. 9:7; Mit. 31:6-7). Nidhamu ya jumla inatoka kwa muumini mmoja mmoja aliyejitoa kwa Bwana Yesu ambayo msingi wake unamzuia mtu uhuru wake binafsi kwa sababu ya upendo kwa wengine pamoja na utamaduni ambao yeye anasimamia (kama vile Rum. 14:1-15:13; 1 Kor. 8-9; 10:23-33). Tazama mada maalumu: Mitazamo ya kibiblia Juu ya Kileo (uchachushwaji) na ulevi (wa kupindukia) katika 1 Tim. 3:3.

**NASB "asiwe mgomvi"**
**NKJV, NRSV,**
**TEV, NJB "asiwe mkali sana"**

Hii ni dhahiri "asiwe mbishaji." Hii yumkini inasimulia matumizi zaidi ya pombe au aina ya mtu binafsi (kama vile 1 Tim. 3:3).

**NASB** " asiwe mpenda mapato ya aibu"
**NKJV** "asiwe na tamaa ya fedha"
**NRSV** "au tamaa kwa ajili ya mapato ya aibu"
**TEV** "au tamaa kwa ajili ya fedha"
**NJB** "wala mwenye tamaa"

Tatizo kama hili liliaksi walimu wa uongo kwenye Tito 1:11. Tazama muhtasari kamili katika 1 Tim. 3:8.

**1:8 "mkaribishaji"** Hii ni dhahiri "kupenda wageni." Nyakati za Paulo nyumba za kulala wageni zilkuwa ni maarufu kwa umalaya, hivyo, Wakristo, na hasa uongozi wa Kikristo, wawe na nyumba zao kwa ajili ya kutemelewa na wamishionari na kwa ajili ya mahitaji ya jamii (kama vile. 1 Tim. 5:10; Rum. 12:13; Ebr. 13:2; 1 Pet. 4:9; 3 Yn 1:5).

◙ **"mpenda mema"** yote maneno mawili ya kwanza ya Tito 1:8 yamechanganywa *phileos* na *agathos*. Hii ni tungo ya kawaida iliyothibitishwa kwenye desturi za Wagiriki na Warumi. Yamepatikana mara nyingi kwenye minara yao ya ukumbusho. Kinyume chake yanapatikana kwenye 2 Tim. 3:3, ambayo yanaelezea sifa za walimu wa uongo.

**NASB, NJB** "mwenye kiasi"
**NKJV** "mwenye utaratibu"
**NRSV** "mtu makini"
**TEV** "mwenye nidhamu"

Neno hili katika miundo yake mbalimbali ni la kawaida kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile. 1 Tim. 2:9,15; 3:2; 2 Tim. 1:7; Tito 1:8; 2:2,4,5,6,9,12,15). Neno linaaksi zuio la mipaka. Linadokeza maisha ya uwiano.
Tazama muhtasari kamili katika 1 Tim. 3:2.

**NASB** "mwenye haki"
**NKJV** "mtakatifu"
**NRSV, NJB** "anayesimamia haki"
**TEV** "anayesimamia patakatifu"

Sifa hizi hazikutajwa kwenye 1 Timotheo 3. Mara zote zinahusiana pamoja kwenye desturi za Uyunani. Ni maneno ambayo yanaaksi mahusiano kati ya wajibu mbele za Mungu na wajibu mbele za mwanadamu.

◙ **"mwenye kudhibiti nafsi yake"** hii inaelezea mahubiri ya Paulo mbele za Felix na Drusilla kwenye Mdo 24:24 na kuendelea. Na imetumika kwenye muunganiko na mojawapo ya sitiari inayofaa ya Paulo kwenye 1 Kor. 9:25. Pia imetumika kwa sifa ya Wakristo waliokomaa kwenye Tito 2:2 na 2 Pet. 1:6. NOMINO imejitokeza kwenye orodha ya matunda ya Roho kwenye Gal. 5:23. Inamuaksi mtu ambae, kupitia kwa Roho, anaweza kutawala hisia na kuweka utaratibu wa mvuto kwa dunia iliyoanguka, majaribu ya shetani (pepo wabaya) na dhambi ya asili. Hii inawaelezea waaminio ambao wanaongozwa na Kristo.

**1:9**
**NASB, NKJV** "akilishika lile neno la imani "
**NRSV** "lazima alishike neno la kutumainiwa"
**TEV** "lazima aushike ujumbe ambao unaweza kuaminiwa"
**NJB** "ashike ujumbe usioweza kubadilishwa"

Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Waaminio wana muunganiko na mfuatano wa kitume, historia ya Ukristo. Ni lazima washikilie na kushikamana na Agano la kale na jipya ambalo ni ufunuo binafsi wa mtu na Mungu pekee wa kweli. Ni wa kwao, na wetu, ni mwongozo pekee kwa ajili ya imani na mazoezi!

**NASB, NRSV** **"vile vile kama alivyofundishwa "**
**NKJV** **"kama alivyofundishwa"**
**TEV** **"kama inavyokubaliana na mafundisho"**
**NJB** **"ya utamaduni"**

Viongozi wa kanisa ni lazima wapitie kwenye kweli za kitume walizofundishwa bila kuzibadilisha.

◙ **"apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima"** huduma, kwa maandalizi binafsi, karama za kiroho, na upendo lazima ufanye kazi na waaminio na wasio amini. Kazi yake inahusisha kufundisha, kuhubiri, na ufinyanzi (yaani. Kuishi nje ya) injili na kusahihisha mafundisho ya uongo (kama vile. 2 Tim. 4:2).
Kwa ajili ya “mafundisho ya uvumi” tazama muhtasari katika 1 Tim. 1:10.

◙ **"na kuwashinda wenye kupinga"** mistari michache inayofuatia (kama vile Tito 1:10-16) inaelezea shauku na matendo ya hawa walimu wa uongo. Kuna kipengele cha wazi cha Kiyahudi (kama vile Tito 1:10,14).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 1:10-16**
**[10] Kwa maana kuna wengi wasiotii, wenye maneno yasiyo na maana, wadanganyaji, na hasa wale wa tohara, ambao yapasa wazibwe vinywa vyao. [11] Hao wanapindua watu wa nyumba nzima, wakifundisha yasiyowapasa kwa ajili ya mapato ya aibu. [12] Mtu wa kwao, nabii wao wenyewe, amesema, Wakrete ni waongo siku zote, hayawani wabaya, walafi wavivu. [13] Ushuhuda huo ni kweli. Kwa sababu hiyo uwakemee kwa ukali, ili wapate kuwa wazima katika imani; [14] wasisikilize hadithi za Kiyahudi, wala maagizo ya watu wajiepushao na yaliyo kweli. [15] Vitu vyote ni safi kwa hao walio safi; lakini hakuna kilicho safi kwao walio wanajisi, wasioamini; bali akili zao zimekuwa najisi, na nia zao pia. [16] Wanakiri ya kwamba wanamjua Mungu, bali kwa matendo yao wanamkana; ni wenye machukizo, waasi, wala kwa kila tendo jema hawafai.**

**1:10**
**NASB** **"wengi wasiotii"**
**NKJV, NJB** **"mkaidi"**
**NRSV** **"watu wasiotii"**
**TEV** **"aliye muasi"**

Hili ni neno "kuwa na jambo” (*hupotassō*) na KIAMBISHI AWALI HASI (kama vile Tito 1:6). Hili linamaanisha “kutokuwa chini ya mamlaka." Hili linasimulia kimuktadha kwa "wote wasiotii" kwenye Tito 1:9. Wameelezewa kwenye Tito 3:9-11.

**NASB** **"wenye maneno yasiyo na maana"**
**NKJV, NRSV** **"wenye kusema yasiyofaa na yasiyo na maana"**
**TEV** **"wakiwadanganya wengine na maneno yasiyo na maana"**
**NJB** **"wakiongea upuzi na kujaribu wengine wauamini"**

Maneno haya mawili yamepatikana hapa pekee kwenye Agano jipya. Tatizo la mwanzo la nyaraka za kichungaji ni walimu wa uongo (maneno haya yanaelezewa kwenye Tito 1:10) na misimamo yao. Nini tunaamini na jinsi tunaishi kwenye kipengele cha muhimu cha Ukristo.

◙ **"hasa wale wa tohara"** tungo hii inatukumbusha moja ya thiolojia yenye upinzani ya Paulo katika baraza la Yerusalemu (Mdo. 15) na katika makanisa ya Galatia (Gal. 2:12 nakuendelea). Haina shaka ni namna gani hawa

wanasheria wa mwanzo wa kiyahudi, ambao walidai kwamba watu ili wawe wayahudi ni muhimu kutunza sheria za Musa kabla ya kuweza kumwamini Yesu na kuwa Wakristo, inasimuliwa kwa walimu wa uongo wa Wakolosai, Efeso, na nyaraka za kichungaji. Hapa baadae inaonekana muungano wa wanasheria wa kiyahudi na mawazo ya wanafilosofia wa Kiyunani (wajuzi). Tazama utangulizi wa 1 Timotheo, C. Walimu wa uongo na mada maalumu katika 1 Tim. 1:8.
Pamoja na kifo cha mitume na kuenea haraka kwa Ukristo, vikundi vidogo vilijiimarisha kupitia mashariki ya kale ya karibu na ulimwengu wa kimediterania. Agano la kale linatupatia mwongozo namna gani ya kuwatambua hawa walimu wa uongo, hasa katika Mathayo 7 na kitabu cha 1 Yohana, ambalo linalenga kwenye mtindo wa maisha ufaao na mafundisho ya kweli.

**1:11 "yapasa wazibwe vinywa vyao"** hii ni KAULI TENDAJI YA KITENZI JINA YA WAKATI ULIOPO ya kuchanganywa "kuziba mdomo" (yaani. tulia, kinywa wazi, au kimya). Viongozi wa kanisa ni lazima waangalie nani anaongea kwenye makanisa. Kanuni zile zile ni kweli siku za leo. Kidini na shule zilizo na uhuru hazimpi yeyote na kila mtu haki ya kuelezea kusanyiko la watu wa Mungu!

◙ **"Hao wanapindua watu wa nyumba nzima"** Hii inaweza kurejelea kwa makanisa (kama vile. Rum. 16:5; 1 Kor. 16:19; Kol. 4:15; 1 Tim. 3:15) au kudhulumu wajane na wale waliosemwa kwenye (kama vile. 2 Tim. 3:6).

◙ **"kwa ajili ya mapato ya aibu"** hii inaonyesha asili ya kweli ya walimu wa uongo (kama vile 1 Tim. 1:7; 6:5,10; 2 Pet. 2:3,14; Yuda 1:16). Viongozi wa kanisa wa 1 Timotheo 3 lazima wawe huru kwenye jaribu hili (kama vile. 1 Tim. 3:3,8; 6:9-10).
Walimu wa uongo na makundi ya imani potofu yanaweza kutambulika haraka kwa tabia hizi tatu.

1. utumiaji mbaya wa fedha
2. unyanyasaji wa uhuru wa jinsia
3. kutangaza ni wa kipekee na kuonyesha ufunuo

Ikiwa viongozi wako wa kidini wanataka fedha yako, mke wako, na kutangaza kwamba Mungu amesema nao-kimbia!

**1:12 "Mtu wa kwao, nabii wao wenyewe"** Epimenides aliyeishi kwenye karne ya 6 B.K. na alitokea Krete. Paulo anashuhudia kwa maneno kwamba mojawapo ya mashairi yao yanaonyesha upotoshwaji na ushawishi kwenye kisiwa hiki. Paulo anadokeza kutoka kwa wanafilosofia wa Ugiriki na mashairi kama mara tatu kwenye maandiko yake (kama vile Mdo .17:28; 1 Kor. 15:13; Tito 1:12). Katika mji wake wa Tarso ulifahamika kwa taasisi zake za elimu. Paulo alikuwa msomi wa hali ya juu kwa desturi zote za Kiyunani na Kiebrania.
Paulo yumkini alimuita Epimenides nabii kwa sababu aliandika ukweli juu ya wakaazi wa Krete au inawezekana kwa sababu Wakrete walimwona ni mnenaji aliyevuviwa na miungu ya Uyunani. Alifahamika kama mmoja wa watu wa Krete wenye hekima.

◙ **"Wakrete ni waongo siku zote"** huu ni muundo wa kishari wenye mizani sita. Wakrete waliamini na kujigamba kwamba mungu Zeus alikuwa amezikwa kwenye kisiwa chao. Neno "Krete" linamaanisha “mwongo." Kwenye muktadha huu sifa hizi zinaonekana zikisimulia kwa walimu wa uongo, sio makanisa au makutano ya watu.

◙ **"walafi wavivu"** maana ya msingi wa tungo hii ni tamaa (kama vile Flp. 3:19).

**1:13 "Kwa sababu hiyo uwakemee kwa ukali"** hii kwa dhahili inamaanisha "kuwakata kwa upanga." Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Neno hili imara limetumika hapa pekee kwenye Agano jipya.karipio lingine imara la onyo dogo linaweza kuonekana kwenye 1 Tim. 5:25; 2 Tim. 4:2; Tito 2:15.

◙ **"ili wapate kuwa wazima katika imani"** hii inaonyesha nidhamu ya kuokolewa, sio kuadhibiwa (kama vile. 1 Kor. 5:5; Ebr. 12:5-13). VIWAKILISHI kwenye Tito 1:13 vinarejelea kwa walimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 2:25-26).

Neno “wazima”ni dhana iliyojirudia kwenye nyaraka za kichungaji, ambayo inarejelea kitu chenye afya (kama vile. 1 Tim. 1:10; 2 Tim. 1:13; 4:3; Tito 1:9,13; 2:1,2,8).

**1:14 "hadithi za Kiyahudi"** hadithi hizi yumkini zilikua na uhusiano wa nadharia ya kiyahudi juu ya uzao wa Masihi (kama vile. Tito 3:9; 1 Tim. 1:4; 2 Tim. 4:4). Kwa ajili ya mjadala mzuri wa vidokezo tofauti vya “hadithi” Tazama G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible,* uk. 219-242.

◙ **"na maagizo ya watu "** hili, kwenye muktadha, linaonekana kurejelea mapokeo ya fasihi simulizi ya wayahudi, baadae kuweka utaratibu katika kitabu cha sheria na maadili ya kiyahudi huko Babeli na Palestina (kama vile. Isa. 29:13; Marko 7:7-8; Kol. 2:16-23).

◙ **"wajiepushao na yaliyo kweli"** hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hawa walimu wa uongo waliendelea kuiacha injili. Tazama mada maalumu: ukweli katika maandiko ya Paulo katika 1 Tim. 2:4.

**1:15 " Vitu vyote ni safi kwa hao walio safi "** "vitu vyote" ni kauli ya kwanza kwa Kiyunani ili kutilia mkazo. Ukweli huu ni vigumu kwa baadhi ya waaminio kuuelewa (kama vile. 1 Tim. 4:4; Marko 7:15-23; Luka 11:41; Rum. 14:14,20; 1 Kor. 10:23-33)! Hii inawezekana inasimulia kwa wale walijinyima anasa za mwili hivyo ni kawaida kwa utamaduni wa filosofia wa dini za Kiyunani (kama vile. 1 Tim. 4:3; Kol. 2:20-22). Wakristo halali mara nyingi wamepoteza uwiano wa kibiblia kwenye jambo hili (kama vile Rum. 14:1-15:13)!

◙ **"lakini hakuna kilicho safi kwao walio wanajisi, wasioamini"** VITENZI VINAVYOHUSIANA kwanza ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU YA HALI YA KUENDELEA na ya pili ni KAULI TIMILIFU TENDWA ELEKEZI YA HALI YA KUENDELEA, ambavyo vinaongelea hali ya kuimalisha kilichoumbwa na nguvu za asili zilizo nje, hapa inawezekana mwovu. Aina hii ya mtu hugeuza kila kitu na kila mtu kwa shauku yake binafsi (mfano, Mdo. 20:29).

**1:16 " Wanakiri ya kwamba wanamjua Mungu"** "Mungu” limewekwa mwanzoni kwenye sentensi ya Kigiriki ili kutilia mkazo. Walimu hawa wa uongo hukiri kwamba ni wa kidini! Wanatangaza utauwa msingi wake ni kanuni za wanadamu (kama vile Isa. 29:13; Kol. 2:16-23), lakini kwa ukweli, hao ni najisi. Baadhi wanaona hili kama ushahidi mwingine wa kipengele cha kiyahudi cha upotoshwaji kwa sababu ya neno “Mungu” kidogo zaidi ya Kristo. Kwa ajili ya “kukiri” tazama MADA MAALUMU:UKIRI katika 1 Tim. 6:12.

◙ **"bali kwa matendo yao wanamkana"** hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Mtindo wa maisha ya waaminio unatupatia ushahidi wa mabadiliko yao ya kweli (kama vile. Mt. 7:16,20; 1 Yohana na Yakobo).

◙**"machukizo"** neno hili limetumika mara nyingi kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya kiebrania kama "kuchukiza mno" (kama vile Ufu. 17:4) na mara nyingi linahusiana na kuabudu sanamu. Kwa dhahiri linamaanisha “kunuka" (kama vile. Ufu. 21:8).

◙ **"waasi, wala kwa kila tendo jema hawafai"** tungo hii inashangaza (kama vile 1 Kor. 3:10-15; 2 Pet. 1:8-11)!
Neno hili “waasi” pia limetumika kwenye Tito 3:3 kuelezea namna waaminio waliishi kabla ya rehema za Mungu/ kristo kawabadilisha (3:4)!
Neno “hawafai” kwa wazi linamaanisha “kushindwa kufauli” (*dokimos* na KIAMBISHI AWALI HASI, kama vile. 1 Kor. 9:27; 2 Tim. 3:8). Tazama mada maalum: Maneno ya Kiyunani kwa “jaribio” katika 1 Tim. 6:9.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, inamaanisha kwamba una wajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini sifa zilizotajwa juu ya viongozi kwenye 1 Tim. 3:1-13 zinatofautiana na zilizotajwa kwenye Tito 1?
2. Ni kwa jinsi gani sifa zilizoaksi desturi karne ya kwanza ya Wayunani na Warumi zinasimulia siku za leo, kanisa la leo?
3. Ni kwa namna gani orodha hii iliathiriwa kwa mafundisho na mtindo wa maisha ya walimu wa uongo?
4. Eleze orodha nzima kwenye sentensi moja ambayo inafafanua kiongozi wa Kikristo.
5. Je ujumbe huu unaaksi mamlaka ya kanisa tofauti zaidi kwenye 1 Timotheo?
6. Aina gani ya walimu wa uongo waliokuwa Krete? Walikuwa Wakristo au hapana?
7. Taja mistari inayoaksi kipengele cha wayahudi cha walimu wa uongo.
8. Taja mistari inayoaksi kipengele cha falsafa ya Uyunani ya walimu wa uongo.
9. Eleza kanuni za ulimwengu kwenye Tito 1:15.

# TITO 2

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Mafundisho ya Uzima | Sifa ya kanisa la uzima | Mchungaji na kundi la kondoo (2:1-3:11) | Mafundisho ya uzima | Baadhi ya maagizo ya maadili |
| 2:1-10 | 2:1-10 | 2:1-2 | 2:1-5 | 2:1-10 |
| | | 2:3-5 | | |
| | | 2:6-8 | 2:6-8 | |
| | | 2:9-10 | 2:9-10 | |
| | Kufundishwa sifa Nzuri | | | Msingi wa maisha ya maadili ya mkristo |
| 2:11-15 | 2:11-15 | 2:11-14 | 2:11-14 | 2:11-14 |
| | | 2:15-3:8a | 2:15 | 2:15 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KATIKA MISTARI 1-10

A. Paulo anayaonya makundi tofauti ya watu
   1. watu wazee (Tito 2:1-2)
   2. wazee wa kike. Tito 2:3 (kama vile. 1 Tim. 2:9-15)
   3. wanawake vijana (Tito 2:4-5)
   4. vijana wanaume (Tito 2:6)
   5. Tito, Tito 2:7-8,15 (kama vile. 1 Tim. 4:12-13)
   6. watumwa (Tito 2:9-10)

B. Katika Tito 2 sifa za viongozi wa kanisa zinapatikana kwenye kitabu cha Tito 1:5-9 na 1 Timotheo 3 zinaendelea zaidi kwa jinsi zote na umri wa waaminio wote.

C. kusudi la kuishi maisha ya ucha-Mungu kwa Wakristo limeelezwa kwa wazi kwenye Tito 2:11-14, ambayo ni sentensi moja kwa Kiyunani.

D. Tito 2 ni picha halisi ya mtindo wa maisha ya walimu wa uongo unaopatikana kwenye Tito 1:10-16.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 2:1-3**
1 **Lakini wewe nena mambo yapasayo mafundisho yenye uzima;** 2 **ya kwamba wazee wawe wenye kiasi,**

**wastahivu, wenye busara, wazima katika imani na katika upendo na katika saburi. [3] Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema;**

**2:1 "lakini wewe"** KIWAKILISHI CHA UMOJA "wewe" ni mkazo. Hii inaonyesha tofauti kubwa sana kati ya walimu wa uongo na Tito, kiongozi wa kweli/mwalimu (kama vile. 1 Tim. 6:11; 2 Tim. 3:1,14).

◙ **"nena"** hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile. 1 Tim. 4:13; 2 Tim. 4:2). Injili na kuhusishwa kwake lazima inenwe.

◙ **"mambo yapasayo mafundisho yenye uzima"** mafundisho yenye uzima (mafundisho imara) ni dhana inayojirudia (kama vile Tito 1:9,13; 2:1,2,8; 1 Tim. 1:10; 2 Tim. 1:13; 4:3). Tambua kwamba kwenye muktadha huu mafundisho ya uzima sio kanuni, lakini mazoezi ya mtindo wa maisha, watu wamfanane Kristo. Hatuwezi kutenganisha haki kutoka kwenye utakatifu!

**2:2 "wazee"** hili ni sawa na neno lililotafsiriwa "wazee" kwenye Tito 1:5 na 1 Tim. 5:1,17, lakini muktadha huu mahitaji yake ni tafsiri tofauti (kama vile Filemoni 9). Kwa desturi hii inarejelea wanaume wa umri wa miaka 60 na zaidi. Tazama MADA MAALUMU: WAZEE katika 1 Tim. 5:1.

**NASB, NRSV "wenye kiasi"**
**NKJV, TEV "wenye utulivu"**
**NJB "wenye akiba"**

Hii ni dhahili "kuwa mtulivu," ambao unaweza kurejelea kileo (kama vile. Tito 1:6,7). Neno pia limetumia sitiari kuitadharisha akiri au kuwa makini (kama vile. 1 Tim. 3:2,11).

◙ **"busara"** neno hili limetumika kwenye Tito 2:2,4,5,6 na 12. Tazama muhtsari wa "busara" katika 1 Tim. 3:2.

**NASB, NJB "heshima"**
**NKJV "mkweli"**
**NRSV "hekima"**
**TEV "heshima"**

Neno hili limetumika mara kadhaa kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile. Tito 2:2,7; 1 Tim. 2:2; 3:4,8,11; na muundo wa neno kwenye 2 Tim. 2:2; 3:4). Kulingana na kamusi ya Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker, limeweza kutafsiriwa "heshima, hadhi, ukweli, heshima, utakatifu, au uaminifu" (kama vile. uk. 47).
Neno hili linasimuliwa kwenda Kilatini "Augustus" (kama vile. Mdo 25:21,25; 27:11). Linarejelea kuheshimu au kumwabudu mtu, mfalme mkuu, na linaeleza namna ya kuwajibika au kuhisi uwepo wake.

◙**"wazima"** Hii ni sitiari inayojirudia ni neno lililotumika kutoka Tito 2:1, "uzima." Wakristo wanatakiwa kuwa wazima na imara kwenye imani yao, kwenye upendo wao, na uvumilivu wao (kama vile 1 Tim. 6:11; 2 Tim. 3:10), kama kwenye mafundisho yao. kwa Paulo, kuishi na kuamini haviwezi kutengana — kama kinyume cha walimu wa uongo.

◙ **"wastahivu"** Tazama mada maalumu katika 1 Tim. 4:16 na kwenye muundo tofauti 2 Tim. 2:11.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 2:3-5**
[3] **Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema;** [4] **ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao;** [5] **na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe.**

**2:3 "mwenendo wa utakatifu"** hili ni neno lililochanganywa la *hieros*, ambalo kwamba ni takatifu au tukufu (kutoka *hierou,* kwa ajili ya hekalu) na *prepei*, ambalo kwamba linafaa au kustahili. Wanawake Wakristo wazee wawe na mwenendo wa ucha-Mungu, watembee kwenye njia zilizo takatifu (kama vile. 1 Tim. 2:10).

**NASB** "wasiwe wasingiziaji "
**NKJV, NRSV,**
**TEV** "wasiwe na uzushi"
**NJB** "wasiwe wasingiziaji-waongo**

Neno lililotumika hapa (*diabolos*) ni sawa na lile lililotumika kwa shetani, “msingiziaji" (kama vile. Yn 6:20; 1 Tim. 3:6. Tazama MADA MAALUM:SHETANI katika 1 Tim. 3:6). Hata hivyo, ni WINGI na halina KIBAINISHI (yaani. 1 Tim. 3:11; 2 Tim. 3:3). John Calvin anasema kwamba "kuwa na maneno mengi ni ugonjwa wa wanawake, na inaongezwa na umri."
Tatizo linarejelewa sio tu kwa mchongezi lakini inawezekana upokeanaji wa taarifa za uongo (kama vile. 1 Tim. 5:13). Wanawake wajane wadogo yumkini walikuwa wanenaji badala ya walimu wa uongo ndani ya nyumba na kwenye makanisa ya Efeso (kama vile. 2 Tim. 3:5-7). Kwa vyovyote tungo hii (kama vile. 1 Tim. 3:11; 2 Tim. 3:3) inarejelea tatizo lile lile lenye mashaka.

◙ **"wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ENDELEVU YA HALI YA KUENDELEA. Hii ni kauli imara zaidi kuliko Tito 1:7 au 1 Tim. 3:3,8. Ulevi (tazama mada maalum katika 1 Tim. 3:3) lazima lilikuwa ni tatizo katika Krete, ambalo linaonyesha kwamba uongozi wa Agano jipya yumkini ukaliongezea nguvu au halikutiliwa mkazo kwenye tamaduni fulani.

◙ **"bali wafundishao mema"** kwa sababu ya 1 Tim. 2:12 hii ni dhahili inamaanisha walimu nyumbani au mshauri wa Wanawake vijana. Mistari ya 4-5 inatupatia maudhui ya mafundisho. Tazama mada maalumu katika 1 Tim. 3:3.

**2:4 "wawatie wanawake vijana akili"** neno la asili sōphrōn linapatikana kwenye Tito 2:4,5,6, na 12. Kimsingi linamaanisha “watiwe akili." Wajitetee wenyewe, maisha ya uwiano.

◙ **“wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao"** haya maneno mawili ya Kiyunani yanapatikana pekee hapa kwenye Agano jipya. Mapenzi ya Mungu kwa ajili ya mwanamke aliyeolewa ni kwamba ampende mme na mtoto. Walimu wa uongo walikuwa ni waleta vurugu kwenye nyumba (kama vile. Tito 1:11; 2 Tim. 3:6).

**2:5** sifa za wanawake vijana kama wafanya kazi wa nyumbani wenye utii zilitazamwa kwenye jamii ya karne ya kwanza ya utamaduni wa Mediterranea (kama vile. 1 Tim. 2:10). Je ujumbe huu ulitumiwa kwa wanawake walioolewa nyakati zote kwa desturi zote? Hili sio swali rahisi! Wakristo wa sasa ni lazima wakubali baadhi ya tafsiri za uhuru hapa bila kung’ang’ania mafundisho. Tafadhali soma *How to Read the Bible For All Its Worth* by Fee and Stuart na *The Gospel and Spirit* by Gordon Fee.

◙ **"wenye kiasi"** tazama muhtasari kamili katika 1 Tim. 3:2.

◙ **"safi"** neno hili linapatikana hapa pekee kwenye nyaraka za kichungaji. Paulo ametumia "bikira safi" (yaani, kanisa) kwenye 2 Kor. 11:2.

**NASB** "wafanya kazi wa nyumbani"
**NKJV** "wafanya kazi nyumbani"
**NRSV** "waangalizi wazuri nyumbani"
**TEV** "wanawake wangalizi wazuri"
**NJB** "namna ya kuzilinda nyumba zao"

Kuna tatizo la machapisho ya Kiyunani kwenye tungo hii (tazama BAGD, uk. 561). Machapisho mengi ya mwanzoni (א*, A, C, D*, F, G, I),mababa wengi wa kanisa la mwanzo, na baadae machapisho kidogo yana neno la kawaida,wafanya kazi wa nyumbani (*oikourgos*, "nyumba" + "mfanyakazi"), lakini baadhi ya maandiko ya kale (א$^{c}$, D$^{c}$, H, L, P) yana mtunzaji wa nyumba (*oikouros*, "nyumba" + "mlinzi"), ambayo inafanana na kwenye 1 Tim. 5:14, *oikodesmoteu* (msimamizi wa nyumba, "nyumba" + "bwana").
Neno hili, *oikourgous*, ni neno adimu sana (Bruce M. Metzger, *Commentary on the Greek New Testament*, uk. 654. Moja ya fundisho kuu la ukosoaji wa maandiko ni kwamba maneno mengi yasiyo ya kawaida au tungo inawezekana ni ya asili kwa sababu waandishi waliyabadili ili yafanane na kitu fulani.

◙ **"kuwatii waume zao wenyewe"** neno "kuwatii" au "kujiweka chini" linatokana na neno la kijeshi linalorejelea kuwa chini ya amri. Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO (kama vile. Efe. 5:21na kuendelea; Kol. 3:18; 1 Tim. 2;11-12; 1 Pet. 3:1). Hata hivyo, tambua kwamba Paulo, kwenye Efe. 5:21, anaunganisha utii unaojazwa na Roho (kama vile. Efe. 5:18) na kuwafanya wote wawili kuwajibika kwa wakristo wote. Tafadhali soma muhtasari katika 1 Tim. 2:11-12.

## MADA MAALUM: KUJITOA *(HUPOTASSŌ)*

Tafasiri hii ya mandiko ya kale yanatumia neno hili kwa maneno 10 tofauti ya Kiebrania. Maana yake halisi kufuatana na Agano la kale ilikuwa "kuamuru" "amri iliyo sawa" neno hili limechukuliwa kutoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya miaka ya 70.

1. Mungu anaamuru (kama vile Law. 10:1; Yn. 2:1; 4: 6-8)
2. Musa anaamuru (kama vile Kut. 36:6; Kumb. 27:1)
3. Amri za wafalme (kama vile 2 Nya. 31: 13)

Katika Agano jipya, maana hii inaendelea hadi katika Mdo. 10:48, ambapo Mtume anaamuru. Hata hivyo, mitazamo mipya imeibuka katika Agano Jipya.

1. Suala la hiari linaibuliwa (mara nyingi IRABU YA KATI)
2. Tendo la mtu pekee kujizuia linaweza kuonekana kwa Yesu kutii kwa Baba (Luk. 2: 51)
3. Waumini wanatii katika sura ya kijadi ili kwamba injili isiathiriwe sana.
    a. Waumini wengine (kama vile Efe.5:21)
    b. Wake za wanaoamini (kama vile Kol. 3:18; Efe. 5:22- 24; Tit.2:5; 1Petr.3:1.
    c. Waumini katika serikali za kipagani (kama vile Rum. 13:1-7; 1Pet. 2: 13).

Waumini wanatenda kutokana na msukumo wa upendo, kwa Mungu, kwa Kristo, na kwa Ufalme, kwa faida ya wengine. Kama *agapaō* (upendo), kanisaliliingiza neno hili kwa maana mpya iliyohusiana na mahitaji ya Ufalme na ya wengine. Neno hili tena linachukuliwa kama uzuri wa kutokuwa mbinafsi, usiohitaji amri, bali kwa ushirika mpya wa kujitoa kwa Mungu na Masihi Wake. Waumini wanatii na kukubali kwa manufaa ya wote na Baraka za familia ya Mungu.

◙ **"ili neno la Mungu lisitukanwe"** mtindo wa maisha ya waaminio ni wa maana sana. Hii ni dhana inayojirudia kwenye nyaraka za kichungaji, "usishitakiwe kwa makosa" (kama vile. Tito 2:8,10; 1 Tim. 3:2,7,10; 5:8,14; 6:1; Tito 1:6-7,8,10). Maisha ya waaminio na neno yatawaleta wengine kwa Kristo. Kweli, uzima, mafundisho ya uzima hayawezi kutenganisha haki kutoka kwenye utakatifu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 2:6-8**
**[6] Vivyo hivyo na vijana waume uwaonye kuwa na kiasi; [7] katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu, [8] na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa, ili yule mwenye kupinga atahayarike, kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu.**

**2:6**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kiasi"** |
| **NKJV** | **"wenye utaratibu"** |
| **NRSV, TEV** | **"kujitawala"** |
| **NJB** | **"kiasi"** |

Vijana waume wamepewa mwongozo mmoja pekee ("kuwa na kiasi," kama vile. Tito 2:2,4,5). Ni SHURUTISHI pekee kwenye Tito 2:2-6. Tazama muhtasari kamili wa neno hili la Kiyunani katika 1 Tim. 3:1. Inaelezea sifa nyingi za msingi wa mwongozo wa maisha kwa falsafa ya Kiyunani (yaani, "maana ya haki").

**2:7 "katika mambo yote"** ni sarufi yenye mashaka kama "katika mambo yote" ya Tito 2:7 inasimulia mstari huu na mwongozo mwingine kwa ajili ya vijana waume, au inasimulia mkazo "peke yako" wa Tito 2:7, ambayo inamrejelea Tito.

◙ **"ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO imetumika kama SHURUTISHI (kama vile. 1 Tim. 4:12).
Kwa "mfano" (*tupos*) tazama Mada Maalumu: Muundo katika 1 Tim. 4:12.

◙ **"cha matendo mema "** huu ni mkazo unaojirudia (kama vile. Tito 1:16; 2:7,14; 3:1, 8, 14). Mabadiliko ya mtindo wa maisha ni ushahidi wa na kuvutia ujumbe wa Wakristo.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"na katika mafundisho mema"** |
| **NKJV** | **"katika mafundisho huonyesha mema"** |
| **NRSV** | **"kwenye mafundisho yako onyesha mema"** |
| **TEV** | **"kuwa mwaminifu . . .kwenye mafundisho yako"** |
| **NJB** | **"kwa uaminifu . . .unapofundisha"** |

Hii inaonyesha na kuelezea njia za Tito ya kufundishia (tofauti na shauku ya maisha machafu ya walimu wa uongo), sio tu maudhui ya mafundisho na mahubiri yake. Tito alipita kwenye ukweli wa kitume alioupokea kutoka kwa Paulo. Ikiwa inarejelea maudhui, inawezekana ni mkazo wa ufufuo (kama vile. Rum. 2:7; 1 Kor. 15:42,53,54).
Kuna matatizo kadhaa ya machapisho ya Kiyunani yanayosimulia tungo hii. Kwenye *A Textual Commentary on the Greek New Testament* Bruce M. Metzger anasema neno aphthorian (siopotoshwa)

1. Yana unga mkono machapisho mazuri (yaani., א*, A, C, D*)
2. Yanafaa muktadha
3. Yanaelezea aina mbalimbali
4. Ni chaguo kuu lisilo la kawaida

Chaguo kuu (yaani, א$^c$, D$^c$, L, na baadae machapisho madogo) ni *adiaphthorian* (mwaminifu) (uk. 654).

**2:8 "maneno yenye uzima"** Hili ni eneo lile lile lililojirudia lililotumika kwenye Tito 2:1 na 2 ambalo linamaanisha "uzima" (sitiari yenye utofauti kwa ujumbe usio na uzima wa walimu wa uongo).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ustahivu"** |
| **NKJV** | **"hekima"** |
| **NRSV** | **"umakini"** |

**TEV "ukweli"**
**NJB "kwa dhati"**

Tazama muhtasari kamili katika Tito 2:2.

◙**"yasiyoweza kuhukumiwa makosa"** Huu ni mwongozo wa ujumla kwa ajili ya viongozi wa Wakristo na waaminio wote (kama vile. Tito 1:6-7,8,10; 1 Tim. 3:2,7,10; 5:8,14; 6:1). Tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 3:2.

◙ **"mwenye kupinga"** kwenye muktadha huu inaweza kurejelea (1) walimu wa uongo wa Tito 1:10-16 au (2) jamii ya wasioamini ambao walikosoa Ukristo kutoka ujinga wa kipagani. Maisha wa waaminio lazima yatulize makundi haya yote na kuwavutia kwenye injili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 2:9-10**
**9 Watumwa na wawatii bwana zao, wakiwapendeza katika mambo yote; wasiwe wenye kujibu, 10 wasiwe waibaji; bali wauonyeshe uaminifu mwema wote, ili wayapambe mafundisho ya Mwokozi wetu Mungu katika mambo yote**.

**2:9 "Watumwa na wawatii bwana zao"** "wawatii" hii ni KAULI YA KATI YA KITENZI JINA YA WAKATI ULIOPO (kama vile Efe. 6:5-9; Kol. 3:22-24: 1 Tim. 6:1-2). KITENZI "sihi sana" kinadokezwa kutoka Tito 2:6. Kama wanawake, watumwa wanasisitizwa kuwa na tabia ya ucha- Mungu sambamba na muundo wa desturi ya mamlaka kwa ajili ya Kristo. Tatizo sio kwamba ni uhuru binafsi, lakini uinjilisti! Tazama Mada Maalum: Maonyo ya Paulo kwa watumwa katika 1 Tim. 6:1.

◙**"katika mambo yote"** tungo hii imerudiwa mwishoni mwa mstari wa 10. Ina maana kwamba waaminio wanaelewa maisha yao, kwenye maeneo yote, yanaaksi katika Mungu. Hii ni dhana inayofanana ya kithilojia ya utii kwa wote inayopatikana kwenye Efe. 5:21 na utii wa wanawake wacha-Mungu kwenye Tito 5:22-6:9 (kama vile. H. E. Butt's *The Velvet Covered Brick*).

◙ **"wakiwapendeza"** haielezei, lakini inadokeza, haimanishi kwa bwana wa watumwa pekee, lakini sana zaidi kwa Mungu (kama vile Rum. 12:1-2; Efe. 6:7-8).

**NASB "wasiwe wenye kujibu"**
**NKJV "wasijibu"**
**NRSV, TEV "wasiongee"**
**NJB "pasipo majibizano"**

Kwa namna gani waaminio wanaweza kukabiliana na mahali pa shida na hali ikawa nzuri, wakiwa mashahidi imara kwa imani yao katika Kristo (kama vile Efe. 6:5-9).

**2:10 "wasiwe waibaji"** hili lazima lilikuwa ni tatizo la kawaida kwa watumwa (kama vile Efe. 4:28).

◙ **"waonyeshe"** Neno hili linamaanisha wathibitishe kitu kwa kuonyesha. Maisha ya watumwa waaminio lazima yalete utukufu kwa Mungu na nguvu ya injili inayobadilisha maisha! Jamii moja inaona jambo hili sio muhimu, lakini ni mtindo wa maisha ya mmojawapo!

◙ **"Mwokozi wetu Mungu"** hiki ni cheo kilichotumika na kwa ajili ya Kaisari. Hizi ni sifa za tungo za nyaraka za kichungaji kwa ajili ya Uungu (kama vile. Tito 1:3-2:10; 3:4). Cheo kile kile kilichotumika pia ambacho kimerudiwa kwa Yesu (kama vile Tito 1:4; 2:13; 3:6). Tazama muhtasari kamili katika 2 Tim. 1:10.

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA ZA TITO 2:11-14

A. Muhtasari huu wa kifungu (Tito 2:11-14) unatupatia sababu ya kiteolojia ya maisha wanayoishi Wakristo wacha-Mungu. Mjadala huu unafanana Tito 3:4-7 na 2 Timotheo 1:8-10.
B. Tito 2:11 inarejelea ujio wa kwanza wa Masihi, kuwa na mwili (kama vile. Tito 3:4; 2 Tim. 1:10). Tito 2:13, imetumia neneo lile lile, "kuonekana," inarejelea ujio wa Kristo mara ya pili (kama vile. 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 4:1,8). Ujio wa kwanza unaelezewa kwa neema ya Mungu; ujio wa pili unaelezewa kwa haki ya Mungu!
C. Tito 2:12 ni maelezo ya sifa za viongozi wacha-Mungu kwenye sura ya 1:5-9 na Wakristo wote kwenye sura ya 2:1-10.
D. Tito 2:13 inapangilia aina ya sifa za injili za Paulo "tayari" (ufalme wa Mungu upo sasa) na "bado" (ufalme wa Mungu ujao). Hofu hii ni kweli ya mjadala wa Paulo juu ya maisha ya Wakristo.
E. ni Yesu pekee anarejelewa kwenye Tito 2:13 (kama vile Toleo la NASB, RSV, NEB, NIV) au ni rejea mbili kwa Mungu Baba na kwa mwana Yesu (kama vile Toleo la KJV, ASV, tafsiri ya Moffatt na 2 Petro 1:1)? Kuna sababu kadhaa kwa nini inaonekana inarejelea Uungu wa Yesu, kuvikwa nguo lilitumika kwa ajili Kaisari wa Rumi:
   1. KIBAINISHI kimoja pekee chenye NOMINO mbili
   2. mstari wa 14 pekee unamsimulia Kristo
   3. Maneno "mkuu" na "kuonekana"hayakutumika kamwe kwenye Agano Jipya inarejelea kwa Mungu Baba.
   4. Kuna vifungu kadhaa vingine kwa Paulo na baadhi ya wandishi wa Agano Jipya ambavyo vimejaa Uungu wa sifa za Yesu.
   5. Wengi wa mababa wa kanisa la awali waliona pia kama inarejelea kwa Yesu. Ilifahamika, hata hivyo, matoleo ya awali yalitunza tungo kuangalia kama zinarejelea YHWH na Yesu.
F. Mstari 14 unaelezea kanisa kama Israeli katika maneno yaliyotumika kwenye Agano. Kwa baadhi ya maana ya kanisa ni ukomavu ambao Mungu anautaka kwa ajili ya Israeli (kama vile. Rum. 2:28-29; Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Bado Israeli ni kusudi pekee la upendo wa Mungu na anaeitunza (kama vile Rum. 11).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 2:11-14**
**11 Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; 12 nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; 13 tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; 14 ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.**

**2:11 "maana"** mistari 11-14 ina muunganiko na 1-10, kutupatia msingi wa kithiolojia kwa ajili maisha ya ucha-Mungu.

◙ **"neema ya Mungu imefunuliwa"** hii inarejelea Yesu kuwa na mwili (kama vile. 2 Tim. 1:10; Tito 3:4-7). Maisha, mafundisho, na kifo cha Yesu yamejaa upendo wa Baba, neema na rehema. Tunapomuona Yesu, tunamwona Mungu (kama vile Yn. 1:1-14; 14:8-11; Kol. 1:15-19; Ebr. 1:1-3).
Neno epiphany (kudhihirishwa kwa Kristo kwa Mataifa/imefunuliwa) limetumika kwenye Tito 2:13 kwa ajili ya ujio wa Kristo mara pili (kama vile. Tito 2:11,13; 3:4; 2 Thes. 2:8; 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 1:10; 4:1,8). Tazama Mada Maalumu: maneno ya Agano Jipya kwa ajili ya ujio wa Kristo katika Tito 2:13.

◙ **"iwaokoayo wanadamu wote "**Mungu alimtuma Kristo afe kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote (tazama mada maalumu katika 1 Tim. 4:10), lakini ni lazima kila mmoja akubali kwa kutubu, imani, utiifu, na uvumilivu. Vifungu vifuatavyo vinaaksi dira ya kazi ya Kristo kwa ulimwengu.

1. "kwa ulimwengu" (Yn. 1:29; 3:16; 6:33,51; 2 Kor. 5:19; 1 Yn. 2:2; 4:14)
2. "kwa watu wote" (Rum. 5:18; 1 Kor. 15:22; 1 Tim. 2:4-6; Ebr. 2:9; 2 Pet. 3:9)

Tazama muhtasari kamili katika 1 Tim. 2:4 na mada maalumu katika 1 Tim. 4:10.

Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wa sura yake (kama vile Mwa. 1:26-27). Katika Mwa. 3:15 aliahidi kuwakomboa wanadamu wote. Alielezea mpango wake wa pekee kwa ulimwengu pale alipotoa wito kwa Ibrahimu (kama vile Mwa. 12:3) na Israeli (kama vile Kut. 19:5). Agano la kale liliahidi kwa Israeli (wayahudi dhidi ya mataifa) kama ilivyo sasa ulimwenguni kwa waaminio na wasioamini (kama vile. Efe. 2:11-3:13). Mwaliko wa Mungu ulimwenguni ni wokovu, msisitizo wa kila mmoja, na kuongozwa na nguvu za Roho.

## MADA MAALUMU: MAJAALIWA (CALVINISM) DHIDI YA UTASHI HURU WA KIBINADAMU (ARMINIANISM)

Tito 2:11 Ni mlinganyo wa vifungu vingine vya Agano Jipya kwenye uchaguzi. Nilifikiri inaweza kuwa ya msaada wa kitheolojia kusaidia kutoa maelezo yangu ya kiufafanuzi kutoka kwa Warumi 8:29 na sura ya 9, pamoja na Waefeso 1.

I. Warumi 8:29 – Paulo anatumia "naliwajua kabla" (*proginōskō*, "kujua kabla") maradufu, hapa na 11:2. Katika 11:2 inamaanisha upendo wa Agano la Mungu kwa Israeli kabla ya wakati kuanza. Kumbuka kwamba neno "kujua" kwa kiebrani linahusiana na uhusiano binafsi,wa ndani, sio kumwambia ukweli kuhusu mtu fulanii (kama vile. Mwanz. 4:1; Yer. 1:5). Hapa ilikuwa imejumuisha katika mlolongo wa matukio ya milele (kama vile. Rum. 8:29-30). Neno hili lilihusishwa na kuamuliwa kabla. Hata hiyo, ni lazima ieleweke kwamba maarifa ya Mungu ya mambo yajayo sio msingi wa uchaguzi kwa sababu ikiwa ni hivyo, basi uchaguzi utakua umeegemea katika mwitikio wa baadaye wa binadamu uliyeanguka, ambao utakua utendaji wa kibinadamu. Neno hili pia linapatikana katika Matendo 26:5; Pet 1. 1:2,20 na Pet 1. 3:17.

A. "aliowajua tagu asili" (*proginōskō*, "kujua kabla")

Maneno "aliowajua tangu asili" na "aliwachagua tangu asili"yote ni maneno ambatani pamoja na kihusishi "kabla" na, kwa hiyo inapaswa kutafsiriwa, "kujua kabla ," "kuweka mipaka kabla," au "alama kabla ." Vifungu ya uhakika juu ya kuamuliwa kabla katika Agano Jipya ni Warumi. 8:28-30; Waef. 1:13-14; na Warumi 9. Maandiko haya ni dhahiri kusisitiza kwamba Mungu ni Mfalme.Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu yote. Kuna mpango wa ki-Uungu uliowekwa tayari ili kufanywa kwa wakati. Hata hivyo, mpango huu sio wa kiholela wala kuchagua. Inategemea sio tu juu ya Ufalme wa Mungu na ujuzi wa asili, lakini kwa tabia yake isiyobadilika ya upendo, huruma, na neema isiyostahili. Tazama Mada Maalumu: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele.

Tunapaswa kua makini na ubinafsi wetu wa magharibi (Amerika) au moyo wetu wa uinjilisti wa kuulemba ukweli huu wa ajabu. Tunapaswa pia kulindwa dhidi ya kukingamizwa ndani ya historia, kitheolojia kati ya Augustine dhidi ya Pelegius au Calvinism dhidi ya Arminianism.

B. "imeamriwa kabla" (*proorizō*, "kuweka mipaka kabla")

Kuamriliwa kabla sio mafundisho yenye maana ya kupunguza upendo wa Mungu, neema, na huruma wala kuwatenga wengine kutoka kwenye injili. Ilikuwa na maana ya kuimalisha wanaoamini kwa kuunda maoni yao ya ulimwengu. Mungu ni kwa ajili ya binadamu wote (kama vile. Yohana 1:12; 3:16; Tim 1. 2:4; Petro 2. 3:9; Yohana 1. 2:2; 4:14).Yeye ni mdhibiti wa jumla wa vitu vyote. Nani au nini kinachoweza kututenganisha na yeye (kama vile. Warumi. 8:31-39)? Mungu anaona historia yote mambo yaliyopita kama yapo sasa; binadamu ni kiumbe aliyefungwa na muda. Mtazamo wetu na uwezo wa akili ni wenye mipaka/kikomo. Hakuna kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, Ni muundo wa Agano. Huu ni mfano mwingine uliotolewa katika mvutano wa lahaja. Mafundisho ya kibiblia yanatolewa kwa mtazamo tofauti. Mara nyingi huonekana fumbo la maneno. Ukweli ni mlinganyo kati ya jozi zilizo kinyume. Hatupaswi kuondoa mvutano kwa kuchukua moja ya ukweli. Hatupaswi kutenganisha ukweli wowote wa Kibiblia ndani ya

chumba.

Ni muhimu kuongeza kwamba lengo la uchaguzi sio mbinguni tu wakati tunapokufa,lakini mapenzi ya Kristo sasa. (kama vile Warumi. 8:29-30; Wakorintho 2. 3:18; Gal. 4:19; Waefeso. 1:4; 2:10; 4:13; The. 1. 3:13; 4:3; 5:23; The 2. 2:13; Tito 2:14; Pet 1. 1:15). Tumechaguliwa kuwa "watakatifu wasio na lawama." Mungu huchagua kutubadili ili wengine waweze kuona badiliko na kuitikia kwa imani kwa Mungu katika Kristo. Majaaliwa sio pendeleo la kibinafsi, bali ni wajibu wa Agano. Huu ni ukweli mkuu wa kifungu hiki. Hili ni lengo la Ukristo. Utakatifu ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwamini. Uchaguzi wa Mungu ni mapenzi ya Kristo (kama vile. Waefeso 1:4), sio msimamo maalumu. Mfano wa Mungu ulotolewa kwa binadamu katika uumbaji (kama vile. Mwanzo. 1:26; 5:1,3; 9:6), ni kurejeshwa.

C. "kubali kugeuzwa kwa mfano wa mwanawe"—Lengo kuu la Mungu ni kurejesha picha iliyopotea kwenye anguko. Waamini wamewekwa mbele kwa mapenzi ya Kristo kama vile. Waefeso. 1:4).

II. Warumi 9

A. Warumi 9 ni mojawapo ya kifungu cha Agano Jipya juu ya Ufalme wa Mungu (mwingine kuwa Waef. 1:3-14), wakati sura ya 10 inasema kuwa uhuru wa binadamu ni dhahiri na hujirudia mara kwa mara (kama vile. "kila mtu" Rum. 9:4; "kila mtu" 9:11,13; "wote" 9:12 [maradufu]). Paulo kamwe hakujaribu kupatanisha mvutano huu wa kitheolojia. Wote ni wa ukweli! Mafundisho mengi ya Biblia yanawasilishwa kwa fumbo la maneno au jozi za lahaja. Mifumo mingi ya theolojia ni yenye mantiki na nusu ya ukweli. Augustinianism na Calvinism dhidi ya nusu-Pelegianism na Arminianism zina misingi ya ukweli na yenye makosa. Mvutano wa kibiblia kati ya mafundisho ni bora kwa maandishi ya ushahidi, yenye kutangazwa kama imani ya kanisa, ya kimantiki, ya mfumo wa kitheolojia ambayo inasisitiza Biblia kwenye mstari wa ramani iliyoelezea kabla.

B. Ukweli huo huo (unapatikana katika Warumi. 9:23) umeelezwa katika Warumi. 8:29-30 na Waefeso. 1:4,11. Sura hii ni maelezo yenye nguvu zaidi ya uweza wa Mungu katika Agano Jipya. Haiwezi kuwapo na migogoro kwa vile Mungu ndiye muhusika wa jumla wa uumbaji na Ukommbozi. Ukweli huu mkubwa haupaswi kamwe kufutwa au kupunguzwa. Hata hiyo, ni lazima pawepo na mlinganyo na uchaguzi wa Mungu wa agano kama njia ya kuhusianisha na uumbaji wa mwanadamu, uliofanywa kwa mfano wake. Kama vile Mwanzo 15 isiyokuwa na masharti na haihusiani kabisa na majibu ya mwanadamu, lakini maagano mengine yenye masharti juu ya majibu ya binadamu (mf., Edeni, Nuhu, Musa, Daudi).Mungu ana mpango wa ukombozi kwa uumbaji wake;hakuna mwanadamu anayeweza kuathiri mpango huu. Mungu amechagua kuruhusu watu binafsi kushiriki katika mpango wake. Nafasi hii ya ushiriki ni mvutano wa kitheolojia kati ya Ufalme( Warumi 9) na mapenzi ya Kibinadamu (Warumi 10).

Sio sahii kuchagua msisitizo mmoja wa Biblia na kupuuza mwingine. Kuna mvutano kati ya mafundisho kwa sababu watu wa mashariki wanawasilisha kweli katika lahaja na jozi kujaza mvutano. Mafundisho lazima yafanyike katika mahusiano na mafundisho mengine. Ukweli ni kweli za Musa.

III. Waefeso 1

A. Uchaguzi ni mafundisho ya ajabu. Hata hivyo si wito kwa upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa ajili ya huduma; katika agano jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia haipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa Kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguzi wa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile. 10:11,13).

Umuhimu wa mvutano huu wa kitheolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni "ndiyo" ya Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo).Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu (uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!

Mafundisho huja huja kutokana na kweli zingine, sio kama moja, lisilohusiana na ukweli. Mfuatano mzuri ungalikuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika namna ya kimashariki na sio kimagharibi. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho ( Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu aliye dhahili: usalama dhidi ya uvumilivu;Yesu aliye sawa na Mungu baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu; Uhuru wa kikristo dhidi ya wajibu wa kikristo kwa mwenzi wa agano, nakadharika).

Dhana ya kitheolojia ya "agano" inaunganisha Uweza wa Mungu (ambaye daima huchukua hatua kwa kuweka mswada) wenye mwanzo muhimu na mwendelezo wa mwitikio wa imani ya toba kutoka kwa mtu. Kuwa mwangalifu na uhakiki wa maandiko wa upande mmoja na kupuuza mwingine! Kuwa mwangalifu wa kuthibitisha mafundisho yako pendwa au mfumo wa theolojia.

B. "alivyotuchagua" katika Waef. 1:4 ni KAULI YA KATI ELEKEZI CHA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ambayo inasisitiza somo. Hii inalenga katika uchaguzi wa Mungu kabla ya wakati. Chaguo la Mungu halipaswi kueleweka kwa maana ya kiislamu ya falsafa za maamuzi.Mungu aliahidi kuwakomboa wanadamu walioanguka (kama vile. Mwanzo. 3:15). Mungu alimwita na kumchagua Ibrahimu kuchagua wanadamu wote (kama vile. Mwanzo. 12:3; Kutoka. 19:5-6).

Mungu mwenyewe alichagua wanadamu wote ambao wangetenda imani katika kristo. Mungu daima huchukua maamuzi mwenyewe katika wokovu (kama vile. Yohana 6:44,65). Nakala hii na Warumi 9 ni msingi wa Kibiblia kwa mafundisho ya majaaliwa yaliyosisitizwa na Augustine na Calvin.Mungu alichagua wanaoamini si tu kwa wokovu (kuhesabiwa haki), lakini pia kwa utakaso (kama vile. Wakolosai 1: 10-12).

Hii inaweza kuhusiana na (1) nafasi yetu katika Kristo (kama vile. Wakorintho 2. 5:21) au (2) Nia ya Mungu kuzalisha tabia yake katika wana wake (kama vile. Waef. 2:10; Warumi. 8:28-29; Wagalatia. 4:19). Mapenzi ya Mungu kwa wana wake ni kuwaona wote mbinguni siku moja na kufanana na Kristo sasa!

"katika yeye" ni dhana muhimu ya Waef . 1:4. Baraka za Mungu, neema, na wokovu hupitia kwa njia ya kristo (kama vile. Yohana 14:6). Angalia kurudia rudia kwa umbo hili la kisarufi (ENEO LA MAHALI) katika Waefeso. 1:3, "katika kristo"; 1:4, "katika yeye"; 1:7, "katika yeye"; 1:9, "katika yeye"; 1:10, "katika kristo," "katika yeye"; 1:12, "katika kristo" na 1:13, "katika yeye" (maradufu).Yesu ndiye mwanadamu aliyechaguliwa na wote wanawezekana kuchaguliwa ndani yake. Wote wa Mungu Baraka za Baba zinapatikana katika Kristo.

Maneno "kabla ya msingi wa Dunia" pia hutumiwa katika Mt. 25:34; Yohana 17:24; Pet 1. 1:19-20 na Ufu. 13:8. Inaonyesha nafsi tatu kwa moja ya shughuli ya ukombozi wa Mungu hata kabla ya Mwanzo. 1:1. Binadamu anakikomo kwa maana za wakati; kila kitu kwetu ni cha muda uliopita, wa sasa,na wa baadaye, lakini si kwa Mungu.

Lengo la kuamua kabla ni utakatifu sio pendeleo. Wito wa Mungu sio wa wachache waliochaguliwa wa wana wa adamu, bali kwa wote! Wito ulikuwa ni kile Mungu alichotaka mwanadamu kuwa kama yeye mwenyewe (kama vile. 1 Wathesalonike 5:23; 2 Wathesalonike 2:13);katika sura yake (kama vile. Mwanzo. 1:26-27). Ili kugeuza majaaliwa kuwa katika kanuni ya theolojia badala ya maisha takatifu kuwa janga. Mara nyingi theolojia yetu huzungumza kwa sauti zaidi kuliko maandiko ya Kibiblia.

Neno "wasio na lawama" (*amōmos*) au "bila lawama" linatumika

1. Yesu (kama vile. Waebrania. 9:14; Pet 1. 1:19)
2. Zekaria and Elisabeti (kama vile. Luka 1:6)
3. Paulo (kama vile. Wafilipi. 3:6)
4. wakristo wote wa kweli (kama vile. Wafiipi. 2:15; Wathesalonike 1. 3:13; 5:23)

Mapenzi ya Mungu yasiyowezekana kubadilika kwa kila Mkristo sio baadaye mbinguni tu, lakini ni mapenzi ya kristo sasa (kama vile. Warumi 8:29-30; Wagalatia 4:19; Pet 1. 1:2). Wanaoamini wanapaswa kuitazamisha tabia ya Mungu kwa ulimwengu uliopotea kwa dhumuni la Uinjilisti.

Kisarufi maneno "katika upendo" katika Tito 2:2 yanaweza kwenda pamoja na Tito 2:4 au 5. Hata hivyo wakati maneno haya yanatumika katika maeneo mengine katika Waefeso daima yanahusu upendo wa Kibinadamu kwa Mungu (kama vile. Waefeso. 3:17; 4:2,15,16).

C. Katika Waefeso. 1:5 neno "alitangulia kutuchagua" ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA

USIOTIMILIFU. Neno hili la Kiyunani ni neno ambatani kwa “kabla” na “alama kabla.” Inahusu mpango wa ukombozi wa Mungu uliotanguliwa kabla (kama vile Luka 22:22; Matendo 2:23; 4:28; 17:31; Warumi 8:29-30). Majaaliwa ni moja ya ukweli kadhaa kuhusiana na wokovu wa mwanadamu. Ni sehemu ya kikolezo cha kitheolojia au mfululizo wa ukweli unaohusiana. Haikuwa na maana ya kusisitizwa katika kutengwa! Kweli ya Kibiblia imetolewa katika mfululizo wa mvutano wa anguko, jozi za fumbo la maneno. Ufuasi wa kimadhehebu umejaribu kuondoa mvutano wa kiibiblia kwa kusistiza kweli moja tu ya ukweli wa lahaja (majaaliwa dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu ; usalama wa mwamini dhidi ya uvumilivu wa watakatifu; dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari; kutokuwa na dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo; utakaso wa mara moja dhidi ya utakaso wa kuendelea;imani dhidi ya kazi; Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo; Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu wa asili).

Uchaguzi wa Mungu haukutegemea ujuzi wa mbele wa utendaji wa mwandamu, lakini kwa tabia yake ya neema (kama ile. Waef. 1:7,9,11). Alitamani kwamba wote (hapana mmoja kama mwenye mafunuo) angeokolewa (kama vile Ezek. 18:21-23,32; Yohana 3:16-17; Tim 1. 2:4; 4:10; Tito 2:11; Pet 2. 3:9; Yohana 1. 2:2; 4:14). Neema ya Mungu (tabia ya Mungu) ni muhimu kitheolojia kwa kifungu hiki (kama ile. Waef. 1:6a, 7c, 9b), kama huruma ya Mungu ni muhimu kwa kifungu kingine juu ya kuamuliwa kabla kwa mambo, Warumi 9-11.

Tumaini pekee la wanadamu walioanguka ni neema na huruma ya Mungu (kama vile. Isay. 53:6 na nyingine kadhaa za Agano la Kale zilizotajwa katika Warumi. 3:9-18). Ni muhimu sana kwa kutafsiri sura hizi za kwanza za kitheolojia ili kutambua kwamba Paulo anasisitiza mambo hayo ambayo hayahusiani kabisa na utendaji wa mwanadamu: kuamuliwa kabla kwa mambo (Waefeso 1), neema (Waefeso 2), na mpango wa ukombozi wa milele wa Mungu (Ajabu, Waefeso 2:11- 3:13). Hii ilikuwa ni kusawazisha mkazo wa walimu wa uongo juu ya sifa ya binadamu na kiburi.

**2:12 "nayo yatufundisha"** hii kwa dhahili inamaanisha nidhamu au mafunzo kwa mtoto (kama vile 1 Tim. 1:20; 2 Tim. 2:25; 3:16). Neema ni kama upendo binafsi wa mzazi (kama vile Ebr. 12:5 na kuendelea).

◙ **"kukataa ubaya"** huu ni mchezo wa maneno kati ya *asebeia* (kukataa mabaya, KIAMBISHI AWALI HASI) na *eusebia* (utauwa, tazama mada maalumu katika 1 Tim. 4:7). Yumkini yakaaksi “njia mbili” maarifa ya fasihi ya Agano la kale (kama vile Yos. 24:14-15; Zab 1; Mit. 4:10-19; Mt. 7:13-14). Tunatoka kwa shetani kwa sababu Kristo yeye alitukomboa sisi kutoka kwa shetani; tunayageukia mema kwa sababu Kristo amepangilia mfano. Neema inatufundisha somo chanya na hasi sisi wote!

◙ **"tamaa za kidunia"** (kama vile. Tito 3:3; 1 Tim. 6:9; 2 Tim. 2:22; 3:6; 4:3)

◙ **"kwa kiasi"** tazama muhtasari kamili katika 1 Tim. 3:2.

◙ **"haki"** tazama mistari 2,4,5,6 na mada maalumu ifuatayo.

## MADA MAALUM:HAKI

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (KITENZI, BDB 842, KB 1003; NOMINO JINSI YA KIUME, BDB 841, KB 1004; NOMINO JINSI YA KIKE, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae . Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko, hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

A. <u>kutangaza</u> haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
B. <u>kwa kutoa haki</u> huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)
C. <u>kumtoa</u> Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
D. <u>kurejesha</u> ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

A. Toba
B. Imani
C. Utii kwenye stadi ya maisha
D. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [ utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio

wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!
lli kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

A. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
    1. Warumi 3:26
    2. 2 Wathesalonike 1:5-6
    3. 2 Timotheo 4:8
    4. Ufunuo 16:5
B. Yesu ni haki
    1. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
    2. Mathayo 27:19
    3. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
C. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
    1. Mambo ya Walawi 19:2
    2. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
D. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
    1. Warumi 3:21-31
    2. Warumi 4
    3. Warumi 5:6-11
    4. Wagalatia 3:6-14
    5. Iliyotolewa na Mungu
        a. Warumi 3:24; 6:23
        b. 1 Wakorintho 1:30
        c. Waefeso 2:8-9
    6. Iliyopokelewa kwa imani
        a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
        b. 2 Wakorintho 5:7,21
    7. kupitia matendo ya Mwana
        a. Warumi 5:21
        b. 2 Wakorintho 5:21
        c. Wafilipi 2:6-11
E. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
    1. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    2. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
    3. Waefeso 1:4; 2:10
    4. 1 Timotheo 6:11
    5. 2 Timotheo 2:22; 3:16
    6. 1 Yohana3:7
    7. 1 Petro 2:24
F. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
    1. Matendo 17:31
    2. 2 Timotheo 4:8
G. Kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11
H. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi wake wawe watakatifu
    a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    b. Warumi2:13; 5:1-5; 6:1-23

c. Waefeso 1:4; 2:10
d. 1 Timotheo 6:11
e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
f. 1 Yohana 3:7
g. 1 Petro 2:24

I. Mungu atauhukumu ulimwengu kwa haki
a. Matendo 17:31
b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni tabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

A. agizo la Mungu
B. zawadi ya Mungu
C. tendo la Kristo
D. ni maisha yapaswayo kuishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!
Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasisitiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

A. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
B. injili ni ukweli (msisitizo wa Augustine na Luther)
C. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.
Yatupasa kumkaribisha Yesu!
Yatupasa kuiamini injili!
Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

◙ **"ulimwengu huu wa sasa"** tazama mada maalumu katika 1 Tim. 6:17.

**2:13 "tukilitazamia"** hii ni KAULI YA KATI YA WAKATI ULIOPO ambayo inamrejelea mtu kuendelea kutazamia ujio wa Kristo.

◙ **"tumaini lenye baraka"** hii ni rejea nyingine ya ujio wa Kristo.

◙ **"mafunuo"** tazama mada maalumu hapa chini.

## MADA MAALUM: MISAMIATI YA AGANO JIPYA YA KURUDI KWA KRISTO

Msisitizo wa matukio ya siku za mwisho ya siku maalum ya kuja ambayo wanadamu watakutana na Yesu (kama Mwokozi na Mtoa hukumu) yanatolewa maelekezo yake kadhaa.

1. "siku ya Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:8)
2. "siku ya Bwana" (kama vile 1 Kor. 5:5; 1 The. 5:2; 2 The. 2:2)
3. "siku ya Bwana Yesu" (kama vile 2 Kor. 1:14; MS א ina ". . .Bwana Yesu" katika 1 Kor. 5:5)
4. "siku ya Yesu Kristo" (kama vile Fil. 1:6)

5. "siku ya Kristo" (kama vile Fil. 1:10; 2:16)
6. "Siku Yake (Mwana wa Adamu)" (kama vile Luka 17:24)
7. "siku ambayo mwana wa Adamu atadhihirishwa" (kama vile Luka 17:30)
8. "ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo" (kama vile 1 Kor. 1:7)
9. "wakati Bwana Yesu atakapodhihirishwa kutoka mbinguni" (kama vile 2 The. 1:7)
10. "katika uwepo wa Bwana Yesu wakati wa kuja kwake" (kama vile 1 The. 2:19)

Kuna angalau njia nne ambazo waandishi wa Agano Jipya wanamaanisha kurudi kwa Yesu.

1. *epiphaneia*, ambayo inamaanisha mg'ao wa kumetameta ambako kithiolojia (japo sio kiasili) kunafanana na "utukufu." Katika 2 Tim. 1:10; Tito 2:11 na 3:4 inamaanisha kuja kwa Yesu kwa mara ya kwanza (yaani kuzaliwa) na kuja kwake mara ya Pili. Inatumika katika 2 The. 2:8 ambayo inajumuisha maneno yote matatu ya kuja kwa mara ya Pili: 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 4:1,8; Tito 2:13.
2. *parousia*, ambayo inamaanisha uwepo na kwa asili ikimaanisha utembeleo wa kifalme. Linatumika sana neno hili (kama vile Mt. 24:3,27,37,39; 1 Kor. 15:23; 1 The. 2:19; 3:13; 4:15; 5:23; 2 The. 2:1,8; Yakobo 5:7,8; 2 Petro. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28).
3. *apokalupsis* (au *apocalypsis*), ambayo inamaanisha kufunuliwa kwa kusudi la kufunuliwa. Ni jina la kitabu cha mwisho katika Agano Jipya (kama vile Luka 17:30; 1 Kor. 1:7; 2 The. 1:7; 1 Petro 1:7; 4:13).
4. *phaneroō*, ambalo linamaanisha kuleta mwanga au kwa ufasaha kufunua au kudhihirisha. Neno linatumika mara nyingi katika Agano Jipya kwa vipengele vingi vya ufunuo wa Mungu. Ni kama *epiphaneia*, Linaweza kurejerea kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo (kama vile 1 Petro 1:20; 1 Yohana 1:2; 3:5,8; 4:9) na kuja kwake mara ya Pili (kama vile Mt. 24:30; Kol. 3:4; 1 Petro 5:4; 1 Yohana 2:28; 3:2).
5. Neno lililozoeleka la "kuja," *erchomai*, pia linatumika mara kwa mara kwa kurudi kwa Kristo (kama vile Mt. 16:27-28; 23:39; 24:30; 25:31; Mdo. 1:10-11; 1 Kor. 11:26; Ufu. 1:7,8).
6. Pia linatumika pamoja na tungo "siku ya Bwana" (kama vile 1 The. 5:2), ambalo ni cheo cha siku ya Mungu ya amaungu kwa Agano la Kale (ufufuo) na hukumu.

Agano Jipya lote limeandikwa ndani ya mtazamo wa kiulimwengu wa Agano la Kale ambalo linaelezea

a. uovu wa sasa, kizazi cha uasi
b. kizazi kijacho cha haki/utauwa
c. kizazi kitakacholetwa na wakala wa roho kupitia kazi ya Masihi (Mpakwa Mafuta)

Dhanio za kithiolojia za ufunuo unaoendelea unatakiwa kwasababu ya waandishi wa Agano Jipya kidogo wamerekebisha mategemeo ya Israeli. Badala ya kuja kijeshi na kiuzalendo (Israeli) kwa Masihi, kuna kuja mara mbili. Kuja kwa kwanza ni kuzaliwa kwa uungu na kutungiwa mimba na kuzaliwa kwa Yesu wa Nazareth. Alikuja ila sio kijeshi, sio kwa ajili ya hukumu "mtumwa atesekaye" wa Isaya 53; pia mwendesha farasi (si farasi wa vita au farasi wa kifalme), wa Zekaria 9:9. Kuja kwa mara ya kwanza kunaanzishwa na kizazi cha Kimasihi, ufalme wa Mungu duniani (angalia Mada Maalum: Ufalme wa Mungu). Kwa namna moja, lakini, katika nyingine kuna kuwa bado mbali sana. Ni mvutano huu wa kuja mara mbili kwa kimasihi (angalia Mada Maalum: Masihi) ambao, katika namna, ni kupandana kwa vizazi vya kiyahudi (angalia Mada Maalum: Kizazi hiki na kizazi kijacho) ambacho kilikuwa hakionekani au kwa sehemu hakiko katika hali ya kuonekana kutoka katika Agano la Kale. Kiukweli huku kuja kwa mara mbili kunaweka mkazo katika kujidhatiti kwa YHWH kukomboa binadamu wote (kama vile. Mwanzo 3:15; 12:3; Kutoka 19:5 na kuhubiri kwa manabii, hasa Isaya na Yona).

Kanisa halisubiri kutimilizwa kwa unabii wa Agano la Kale kwasababu nabii nyingi zinamaanisha kuja kwa mara ya kwanza (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth*, ukurasa 165-166). Kile waaminio wanachokibashiri ni kuja kwa utukufu wa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana aliyefufuka, kutimilizwa kwa kizazi kipya cha haki duniani kama ilivyo mbinguni kwa kihistoria kunakotarajiwa (kama vile Mt. 6:10). Uwasilishwaji wa Agano la Kale si kwamba haukuwa wa kweli bali haukuwa umekamilika (angalia Mada Maalum: Kwa nini Ahadi za Kiagano za Agano la Kale zinaonekana kuwa Tofauti na Ahadi za Agano Jipya?). Atakuja tena kama manabii walivyotabiri katika nguvu na mamlaka ya YHWH.

Cheo "Kuja kwa Mara ya pili" si neno la Kibiblia, lakini dhana ni ya kimtazamo wa ulimwengu na muundo wa Agano Jipya lote zima. Mungu atayaweka mambo yote sawa kwa sawa. Ushirika kati ya Mungu na

mwanadamu ulifanya sura yake irejeshwe. Uovu utahukumiwa na kuondolewa. Kusudi la Mungu halitakuja kuondolewa wala kufeli!
Kanisa la kwanza liliabudu siku zote Sabato na siku ya kwanza ya wiki (yaani Jumapili, siku ya ufufuo). Sinagogi lilizungumzia kukua kwa uamsho wa Wakristo kwa kuwataka waumini wao kumkataa Yesu kama Masihi (yaani Mapokeo kumi na nane). Kwa wakati huu (yaani mwaka 70 B.K. ) Wakristo walikutana siku ya Jumapili.

◙ **"ya utukufu "**Tungo hii "ya utukufu" inaweza kufahamika kwa njia mbili: (1) "utukufu uliofunuliwa" (kama vile. Toleo la NKJV) au (2) "kuonekana utufuku" (kama vile Toleo la NASB, NRSV, TEV na NJB). Utukufu mara nyingi unahusiana na uwepo wa Mungu kwenye Agano la kale (hasa *Shekinah* wingu la utukufu kipindi cha kutangatanga jangwani).Utukufu linatokana na neno la Kiebrania kabod ambalo linarejelea fahari kuu. Maneno mawili ya Kiyunani yanahusiana na ujio wa pili pia yanarejelea nuru au furaha: *epiphaneia,* (kama vile. Mt. 25:31) na phanerōō (kama vile. Mat. 24:30). Yesu alizungumzia utukufu wake na wa Baba yake kwenye Yn. 17:1-5,22,24.

## MADA MAALUMU: UTUKUFU (AGANO LA KALE)

I. Maana yake kubwa

Kuna maneno yapatayo ishirini yaliyo litafasiri neno "utukufu" (*doxa)* na agano la kale la Kiyunani, lakini neno la Kiebrania lililo muhimu sana ni *kabod* (BDB 458-459, 455-458). Maana yake ya msingi ni ile ambayo ni nzito. Lilikuwa ni neno la kibiashara lililotumika kwenye ununuzi wa miamala (yaani .vipimo). likaja kuwa na elimu-maana kubwa ambapo dhana ya uzito ikajitokeza katika kilo, watu wenye nazo, mahali na vitu.

II. Utumiaji wa neno YHWH

A. Ikaja kuwa ndIo njia ya kuelezea uwepo binafsi wa YHWH. Ilijumuisha nguvu zake, uweza (yaani, uliopita mipaka) akiwa na u-mtu wake na uwepo katika umbo la kirahisia.
B. Ilidokeza YHWH katika uumbaji, kama vile Zab. 19:1; 29:3,9; 104:31
C. Lilitumika katika udhihilisho wa wazi wa Mungu kwa mwanadamu likijiungamanisha na utengenezaji wa agano la watu wake. Yeye ni "utukufu wa Israel", kama vile 1Sam. 15:29
  1) Safari yao ya kutoka Misri kama vile Hes. 14:22 (ilitabiliwa katika Mwa. 15:12-21)
  1) Katika wingu la utukufu lililowafunika na kuwaongoza kama vile Kut. 16:7,10
  2) Utoaji wa sheria zake katika mlima Sinai
  3) Matendo yake ya utoaji na hukumu wakati wa kutangatanga nyikani
    a. Uwasi wa awali uliohusiana na taarifa ya wapelelezi kumi na mbili, kama vile Hes. 14:9-10
    b. Uingiliaji kati wa Musa kwa niaba yao kama vile Hes. 14:20-21
    c. Uasi wa Kola kama vile Hes. 16:19
    d. Mgogora wa maji, kama vile Hes. 26:6
D. Ombi la Musa kutaka kumwona Mungu, kama vile Kut. 33:18-23
E. Lilitumika na YHWH mwenyewe
  1) 1 Nya. 29:11
  2) Zab 106:20; Yer. 2:11; Hos. 4:7; Rum. 1:23
  3) Isa. 42:8; 45:7; 48:11; 58:8; 60:1-2,19 (Ufunuo 21:23; 22:5)
  4) Zak. 2:5,10
F. Lilitumika katika muunganikano wa uwepo wa YHWH na/ katika
  1) Hema takatifu, kama vile Kut. 16:7,10; 29:43; 40:34-35; Law. 9:6,23
  2) Hekalu, kama vile 1 Fal. 811; 2 Nya. 5:14; 7:1-3; Isa. 6:3; Hag. 2:3,9
  3) Sanduku la agano, kama vile 1 Sam. 4:22; Zab. 63:2; 78:61
G. Lilitumika katika ufalme wa YHWH, kama vile 1 Nyakati 29:12-13; Zab. 24:7-10; 45:3
H. Lilitumika na YHWH katka hali ya kuadilisha (yaani, haki), kama vile Zab. 29:3; 97:6; Isa. 42:8; 48:11; 58:8; Hab. 2:14

III. Lilitumika kwa wanadamu na mataifa

A. Binadamu

1) Likiendana na “nafsi” (yaani, *nephesh)* kama vile Mwa. 49:6; Zab. 16:9; 108:1
2) Mali, kama vile Mwa. 31:1; Zab. 49:16,17; Isa. 10:3; 61:6; 66:11-12
3) Heshima, kama vile Mwa. 45:13; Zab. 8:6; Hag. 2:7
4) Sifa njema, kama vile Ayu 19:9; 29:20; Zab. 4:2; 49:17
5) Uzuri, kama vile 1 Nya. 29:12,28; 2 Nya. 17:5; 18:13; 32:27

B. Mataifa
1) Misri,
2) Efraim, kama vile Hos. 9:11
3) Samaria, kama vile Hos. 10:5

C. Wafalme
1) Ahausuero, kama vile Esta 1:4
2) Israel, kama vile Zab 21:6
3) Antiochus IV, kama vile Dan. 11:39

D. Majeshi ya mataifa
1) shamu, kama vile Isa. 8:7
2) Israeli, kama vile Isa. 17:4
3) Kedari, kama vile Isa. 21:16

IV. Lilitumika kwenye maelezo ya siku za mwisho
A. YEHOVA atarudi kwenye hekalu lake jipya, kama vile Ezek. 43:2,4,5; 44:4
B. YHWH atauvutwa ulimwengu wote kwake, kama vile Isa. 40:5; 59:19; 60:1-3; 66:18-19
C. YHWH ataishusha Yerusalemu “mpya” kama vile Isa. 66:10; Zak. 12:7

V. Kusudi la uumbaji ni kumtukuza YHWH
A. Aliumba kwa ajili ya utukufu wake, kama vile Isa. 43:7
B. Utukufu ni juu yake, kama vile 1 Nya. 16:29
C. Imba/sifu utukufu wake, kama vile Zab. 66:2; 96:8; 115:1
D. Yote tuyatendayo twayatenda katika yeye, kwa ajili ya utukufu wake, kama vile 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 4:15; Efe. 5:22; 6:5; 1 Petr. 2:12
E. Maelezo ya kwanza ya katekismu

◙ **"Mungu mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo"** Yesu hapa hana utata kwa cheo alichopewa cha Mungu! Kaisari alidai cheo kama hiki (yaani, Ptolemy I). Maneno “kuonekana” (ambayo kimuktadha yanasimulia ujio wa pili wa Kristo) na "kuu" kamwe hayakutumika kwa YHWH. pia, hakuna KIBAINISHI Na “mwokozi”. Sintaksi ya Koine ya Kigiriki inasidia hiki cheo kwa ajili ya Kristo kwa sababu kuna KIBAINISHI kimoja pekee chenye NOMINO mbili, vinavyounganika pamoja (tazama NET Bible). Yesu ni Mungu (kama vile. Yn 1:1; 8:57-58; 20:28; Rum. 9:5; Fil. 2:6; 2 Thes. 1:12; Ebr. 1:8; 2 Pet. 1:1,11; 1 Yn. 5:20). Masihi Kwenye Agano la kale (tazama mada maalumu katika 1 Tim. 1:1) alitarajiwa awe mtu mwenye nguvu za kiroho kama vile waamuzi. Uungu wake ulimshangaza kila mtu (tazama MADA MAALUMU:IMANI JUU YA MUNGU MMOJA katika 1 Tim. 2:5)!

**2:14"ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu"** hii inafuata teolojia ya Marko 10:45; 2 Kor. 5:21; na Ebr. 9:14.inarejelea kuwakilishwa, upatanisho mbadala (kama vile. Isa. 53; Gal. 1:4; 1 Tim. 2:5-6; Ebr. 9:12-15; 1 Pet. 1:18-19). Mungu Baba “alituma” lakini mwana “alijitoa nafsi yake”!

◙ **"ili atukomboe "** maneno "fidia" na "komboa" yana asilio ya Agano la kale (toleo la NASB limechapisha Tito 2:14 kama dondoo la Agano la kale).maneno yote yanarejelea kwa mtu aliyetolewa kutoka utumwani kama Israeli alivyokombolewa kutoka Misri. Hii pia inadokeza kwamba waaminio wamewekwa huru kutoka nguvu za dhambi kupitia kwa Kristo (kama vile Warumi 6). Tazama MADA MAALUMU: FIDIA/KOMBOA katika 1 Tim. 2:6.

◙ **"kujisafishia"** rejelea kwenye mada maalumu "haki" katika Tito 2:13. Swali la kiteolojia ni kwa namna gani atawasafisha watu? Je ni kipawa huru toka kwa Kristo, kitolewacho kwa agizo la kiroho au ni katika mamlaka, kutubu, utiifu, uvumilivu katika imani? Je yote ni Mungu au mwanadamu anaitikia mamlaka?

Kwangu mimi, tangu nitazame Biblia kama ukweli uliopo kwenye fumbo la maneno, yote ni matendo huru ya Mungu mtakatifu na yanahitajika kwanza na kuendelea matendo ya kila mmoja aliyeanguka (tazama mada maalumu katika Tito 2:11)! Huu ni muunganiko kwenye dhana ya "maagano" (tazama mada maalumu katika 2 Tim. 2:1).

◙ **"watu wawe milki yake mwenyewe"** haya ni maneno ya maagano kwenye Agano la Kale (yaani. Kut. 19:5; Kumb. 14:2; 1 Pet. 2:5,9,10; Ufu. 1:6). Kanisa ni Israeli ya kiroho (kama vile. Gal. 6:16; Rum. 2:29). Kanisa lina mamlaka ya kiwafundisha injili wanadamu wote (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8) kwa kushirikiana katika injili na injili iliyo hai!

◙**"wale walio na juhudi katika matendo mema"** shabaha ya Ukristo sio tu kwenda mbinguni waaminio wanapofariki lakini sasa kumfanana Kristo (kama vile. Gal. 4:19; Efe. 1:4 2:10). Watu wa Mungu wanaelezewa kuwa na shauku ya kutamani matendo mema (kama vile. Yakobo na 1 Yohana.

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 2:15**<br>**[15] Nena maneno hayo, onya na kukaripia kwa mamlaka yote; asikudharau mtu awaye yote.** |

**2:15 "nena maneno hayo, onya na kukaripia"** kuna KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO tatu: endelea kufundisha (kama vile. Tito 2:1), endelea kuonya, na endelea kukaripia (kama vile. 2 Tim. 3:16). Viongozi wa kanisa ni lazima wawatie moyo watakatifu na kuwatambua walimu wa uongo!

◙ **"kwa mamlaka yote"** Yesu alisema wawe na mamlaka yote (*exousia*) mbinguni na duniani (kama vile. Mat. 28:18). Aliwakilisha mamlaka yake kwa mitume wake (Paulo akiwa wa mwisho, aliyezaliwa nje ya wakati ufaao). Paulo aliwakilisha mamlaka yake (*epitaē*) kwa Timotheo na Tito kama mwakilishi binafsi.

Tangu kifo cha hawa mashahidi, Agano jipya limeandikwa (kama vile Agano la Kale) lina mamlaka "kwa ajili ya kizazi cha baadae cha waaminio wote" (kama vile. 2 Tim. 3:15-17).

## MADA MAALUM: MAMLAKA (exousia)

I. Matumizi ya Luka – Inatia shauku kuyachunguza matumizi ya Luka ya neno *exousia* (mamlaka, uweza, au haki ya kisheria).
   1. Katika Luka 4:6 Shetani anadai kuwa na uwezo wa kumpa Yesu mamlaka.
   2. Katika Luka 4:32,36 watu wa Kiyahudi walistaajabishwa namna Yesu alivyofundisha, kwa kutumia mamlaka yake binafsi.
   3. Katika Luka 9:1 Aliwapa uweza na mamlaka Mitume Wamke.
   4. Katika Luka 10:19 Aliwapa mamlaka wamisionari wake sabini.
   5. Katka Luka 20:2,8 kiini cha swali la mamlaka ya Yesu kinaulizwa.
   6. Katika Luka 22:53 uovu umeruhusu mamlaka ya kushtumu na kumuua Yesu.

Ijapokuwa si katika Luka, utangulizi wa injili ya Mathayo kuhusu Agizo Kuu (Mt. 28:18), "nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani,"huu ni usemi wa mamlaka yaYesu unaoshangaza.
Yesu alidai kuwa na mamlaka kwa sababu
1. maneno ya Mungu yaliyonenwa kwake katika
   a. ubatizo wake (Luka 3:21-22)
   b. kubadilika kwake (Luka 9:35)
2. utimilifu wa unabii wa Agano la Kale
   a. kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10)
   b. uzao wa Yese (kama vile 2 Samueli 7)
   c. kuzaliwa kwake katika Bethlehemu (kama vile Mika 5:2)

d. kuzaliwa kwake wakati wa dora ya nne (Rumi) ya Danieli 2
e. alivyowasaidia maskini, vipofu, wahitaji (Isaya)
3. kupunga kwake pepo kulifunua uweza wake na mamlaka juu ya Shetani na ufalme wake.
4. kuwaansha waliolala mauti kulionyesha uweza wake juu ya maisha ya kimwili na mauti.
5. miujiza yake yote aliufunua uweza wake na mamlaka mpangilio, utofauti, na muonekano.
   a. Asili
   b. Ulishaji
   c. Uponyaji
   d. kumbukumbu za kiakili
   e. uvuaji wa samaki

II. Matumizi ya Paulo ya neno "mamlaka" yalihusiana na wanawake wa ki-Kristo.

Suala hili la mamlaka pia limejadilikwa katika 1 Wakorintho 11 katika uhusianao wa wanawake kufunika vichwa. Ufuatao ni muundo wa maelezo yangu yalioypo hapa.

**1 1 Kor. 11:10 "Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani"** Matumizi ya mamlaka katika 1 Wakorintho yanaweza kueleweka katika njia kadhaa. Jambo la msingi (katika muktadha huu) ni "mamlaka" (exousia) gani yanayozungumziwa. Kwanza, lazima ieleweke kwamba neno exousia mara nyingi lilihusiana na neno dunamis (uweza). Otto Betz ina makala yenye kuvutia kuhusuj neno exousia katika New International Dictionary of New Testament Theology, juzuu 2, kr. 606-611. Hapa kuna mifano mitano.
"Sifa zake za Agano la Kale kwamba maneno *exousia* na *dunamis* yote yalihusikana na kazi ya Kristo, matukio ya mpangilio mpya wa nguvu ya umbile la kiulimwengu na kuwawezesha waamini" (uk. 609).

"Hili neno exousia kwa waamini. Mamlaka ya muumini wa ki- Kristo inapatikana katika utawala wa Kristo na kuzivunja nguvu zote. Hili linamaanisha vyote uhuru na huduma" (uk. 611).

"Huyu yuko huru kwa kila kitu (1 Kor. 6:12; 10:23 *exestin*); dai hili, ambalo lilikuwepo tangu awali kupitia kwa wanaushawishi wa kimathehebu huko Korintho, lilipendelewa na Paulo ambaye alilithibitisha kwa usahii kabisat" (uk. 611).

"Katika utendaji, hata hiovyo, uhuru huu usiozuiliwa kinadharia unaongozwa kwa kwa fikra za kile chenye kuwasaidia Wakristo wengine na kusanyiko kama kama kitu kamili cha mtazamo wa ukweli kwamba ukombozi kamili bado unakuja (1 Kor. 6:12; 10:23)" (uk. 611).

"'Mambo yote ni ya kisheria [*exestin*] kwangu mimi,' lakini si mambo yote yenye kusaidia. 'Mambo yote ni ya kisheria [*exestin*],' lakini si mambo yote yenye kujenga. Mtu asiyatafute yaliyo mema tu, bali mema kwa ajili ya jirani yake" (1 Kor. 10:23 na kuendelea). Nukuu iliyo ndani ya nukuuu hizi bila shaka ndio wito wa wa wanasheria huko Korintho. Paulo anawakabili kwa kuukubali ukweli wao, lakini kwa kuonyesha kwamba si ukweli kamili" (uk. 611).

Mara nyingi Paulo anatumia maneno haya mawili ndani ya barua zake kwa kanisa la Korintho.
1. *exousia*, 1 Kor. 7:37; 9:4,5,6,12 (mara mbili),18; 11:10; 2 Kor. 13:10
2. *dunamis*, 1 Kor. 1:18; 2:4,5; 4:19,20; 5:4; 15:24,43; 2 Kor. 4:7; 6:7; 8:3 (mara mbili); 12:9; 13:4 (mara mbili)

Haki na uweza yalikuwa mambo makuu kwa wate wanasheria na wanahaki. Paulo anajaribu kutembea katika mstari uliyonyooka katika ya kingo zote. Katika muktadha huu wanawake wa ki-Kristo wanasisitizwa kuyakubali maagizo ya Mungu ya uumbaji yaliyotolewa (yaani, Kristo-mwanadamu-mwanamke) kwa makusudi ya ufalme wa baadaye. Paulo anaeleza juu ya makubaliano halisi (kama vile Mwa. 1:26-27; 2:18) katika mistari ya 1 Kor. 11:11-12. Hili ni la hatari kithiolojia
1. kutenga mstari mmoja katika muktadha huu
2. kutumia mabadiliko ya mawasiliano ya madhehebu ya kifumo katika suala hili la mahusiano ya

wanaume na wanawake/waume kwa wake wa karne ya kwanza kwa kila utamaduni katka kila karne

3. Kuukosa ulinganifu wa Paulo baina ya uhuru wa Mkristo na agano la wajibu wa ushirika wa Mkristo.

Wanawake wa ki-Kristo walipata wapi uhuru wa kushiriki kama viongozi katika ibada za kusanyiko (yaani, kanisa la nyumbani)? Hakika si kutoka katika sinagogi. Ni mwelekeo gani wa kiutamaduni utokanao na jamii ya Kirumi ya karne ya kwanza? kwa hakika hililinawezekana na katika mtazamo wangu hili linasaidia kueleza juu ya mitazamo yangu ya sura hii. Hata hivyo, pia inawezwekamna kwamba nguvu ya injili, ujrejesho wa "sura na mfano wa Mungu" halisi uliopotea katika Anguko, hiki ndicho chanzo. Kuna kiwango cha ubora mpya wenye kuogopesha katika maeneo yote ya maisha ya mwanadamu na jamii. Lakini usawa huu unaweza kurudishwa ndani ya bima kwa ajili ya matumizi mabaya binafsi. Upanuzi huu usiofaa ndiyo Paulo anaoujelezae.

F. F. Bruce, Answers to Questions, kwa ujkweli amenisaidia kufikiri kupitia mambo mbalimbali ya kimkanganyiko yalihusu mapokeo ya kanisa la Ukristo wa sasa wa magharibi. Kama ulivyo ufafanuzi wa maandiko matakatifu mara nyingi nimekuwa nikifikiria kwamba wanawake kujifunika ilimaanisha kuonyesha karama ya Mungu (au usawa wa pade mbili wa Mwa. 1:26,27), si mamlaka wa mume wake. Hata hivyo, Nisingeipata tafsri hii miongoni wa vyanzo vya kibiblia nivitumiavyo, hivyo, Nilisita kuliweka hili katika maoni au kulihubiri/kulifundisha. Bado nakumbuka msisimko na uhuru niliokuwa nikiusikia wakati F. F. Bruce alipofikiria kitu kile kile (tazama Answers to Questions, uk. 95). Nafikiri waamini wote wanaitwa, kwa wakati wote, wamekirimiwa kuwa watumishi wa Kristo (kama vile Efe. 4:11-12)!

◙ **"asikudharau mtu awaye yote"** hii ni KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPO inayokanusha SHURUTISHI (kama vile. 1 Tim. 4:12). Hii yumkini ikarejelea

1. Wote waliokuwa ndani ya kanisa walioangalia umri wa Tito au mwakilishi wa mamlaka.
2. Wote waliohusiana na walimu wa uongo, inawezekana hata msemaji mkuu.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je sura hii inaongelea ujio wa kwanza wa Kristo au ujio wake wa pili?
2. Ni nini umuhimu wa mstari wa 13?
3. Taja kazi tatu za mhubiri kwenye Tito 2:15.
   a.
   b.
   c.
4. Je Tito 2:15 inafunga sura ya 2 au inaanza mjadala wa sura ya 3?

# TITO 3

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Kudumu kutenda Matendo mema | Neema za warithi wa Neema | Mchungaji na Kundi (2:1-3:11) | Mwenendo wa Mkristo | Maelezo ya Jumla Kwa Waaminio |
| 3:1-7 | 3:1-8 | 2:15-3:8a | 3:1-8a | 3:1-3<br>3:4-8a |
| 3:8-11 | Kataa Uasi | | | Ushauri Binafsi kwa Tito |
| | 3:9-11 | 3:8b-11 | 3:8b-11 | 3:8b-11 |
| Maelekezo binafsi Na Salamu | Jumbe za Mwisho | Maelezo ya Mwisho | Maelekezo ya Mwisho | Mapendekezo Ya Kutendea Kazi, Kwaheri na Baraka Njema |
| 3:12-14 | 3:12-14<br>Kwaheri | 3:12-14 | 3:12-14 | 3:12-14 |
| 3:15 | 3:15 | 3:15a<br>3:15b | 3:15a<br>3:15b | 3:15 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA TITO 3

A. Sura hii inatengeneza maudhui kwa ajili ya kitabu kizima.
   1. Tabia za Mkristo inatiliwa mkazo katika Tito 1:16; 2:7,14; 3:1-2, 8
   2. mafundisho ya Mkristo yanawekwa kimutahsari katika Tito 2:11-14 na 3:4-7
   3. Waaminio wanatakiwa kuishi sawasawa kwasababu wamepatanishwa na Mungu. Tunatakiwa kuchukua tabia za familia ya Baba yetu. Hitimisho la Mkristo sio tu kwenda mbinguni tutakapokufa bali kufanana na Kristo sasa (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 Thes. 3:13; 4:3). Kusudio la maisha yetu mapya ni kufikia waliopotea kwa Injili (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Lakini Paulo anataka kuwa hizi ni nasaha zake kwa "maisha mema" hayachanganywi pamoja na "kazi za haki."

B. Utatu wote unatenda kazi juu ya wokovu wa mwanadamu (angalia Mada Maalum katika Tito 3:6)
   1. upendo wa baba (Tito 3:4)
   2. kufanywa upya na Roho na ubatizo wa Roho (Tito 3:5)
   3. upatanisho wa Mwana (Tito 3:6)

C. Tito 3:9-11 ni maonyo endelevu ya Paulo dhidi ya walimu wa uongo na kuwaonya kutenda matendo mema ambayo ndiyo tabia hasa ya Nyaraka za Kichungaji (kama vile Tito 1:10-16; 1 Tim. 1:3-7).

D. Tito 3:12-15 inatengeneza hitimisho binafsi la utiaji moyo na maelekezo kwa Tito.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 3:1-11**
**1 Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema; 2 wasimtukane mtu ye yote, wasiwe wagomvi, wawe wema, wakionyesha upole wote kwa watu wote. 3 Maana hapo zamani sisi nasi tulikuwa hatuna akili, tulikuwa waasi, tumedanganywa, huku tukitumikia tamaa na anasa za namna nyingi, tukiishi katika uovu na husuda, tukichukiza na kuchukiana. 4 Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake kwa wanadamu, ulipofunuliwa, alituokoa; 5 si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu; 6 ambaye alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; 7 ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu. 8 Ni neno la kuaminiwa; na mambo hayo nataka uyanene kwa nguvu, ili wale waliomwamini Mungu wakumbuke kudumu katika matendo mema. Hayo ni mazuri, tena yana faida kwa wanadamu. 9 Lakini maswali ya upuzi ujiepushe nayo, na nasaba, na magomvi, na mashindano ya sheria. Kwa kuwa hayana faida, tena hayana maana. 10 Mtu aliye mzushi, baada ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili, mkatae; 11 ukijua ya kuwa mtu kama huyo amepotoka, tena atenda dhambi, maana amejihukumu hatia yeye mwenyewe.**

**3:1 "Uwakumbushe"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO USIO TIMILIFU ikiwa na maana ya "kuendelea kukumbusha." Hii kidhahiri inaunganishwa na 2:15. Tito ni kuwakumbusha wao juu wa kile amacho tayari wanakijua (kama vile 2 Tim. 2:14; 2 Pet. 1:12; 3:1-2; Yuda 1:5). Angalia MADA MAALUM: WEMA NA UOVU katika Agano Jipya katika 1 Tim. 1:9.

◙**"kunyenyekea"** Hii ni KAULI YA KATI YENYE KITENZI JINA YA WAKATI ULIOPO ikiwa na maana ya "endelea kujiweka chini ya mamlaka." Lilikuwa ni neno la kijeshi kwa mfuatao wa amri. Neno hilo hilo linatumika juu ya Wake za Wakristo katika Tito 2:5 na Watumwa Wakristo katika Tito 2:9. Pia linatumika kwa Wakristo wote katika Efe. 5:20. Kimsingi ni mmatazamo wa maisha kwa ajili ya Wakristo katika maeneo yote. Angalia Mada Maalum: Utii (*hupotassō*) katika Tito 2:5.

◙**"kwa wenye uwezo na mamlaka"** Maneno haya mawili, *exousia* (angalia Mada maalumu katika Tito 2:15) na *archē* (angalia Mada Maalum hapa chini), kuwa na uwanja mpana wa kimaana wa ulimwengu wa Kimediteranean. Kuna hatahivyo, muingiliano wa baadhi ya maana katika namna ya mamlaka au nguvu juu ya nyingine.

1. *Exousia* inatumika juu ya mamlaka ya umma katika Rum. 13:1 na Tito 3:1. 1 Timotheo 2:2 na 1 Pet. 2:13-17 yanafanana kithiolojia, japo maneno haya mawili ya Kiyunani hayatumiki.
2. *Exousia* na *archē* yanatumika kwa ajili ya mamlaka ya kiroho na nguvu katika Efe. 2:2 na Kol. 2:15. katika Efe. 3:10 na 6:12 maneno haya mawili "katika maeneo ya kimbingu," ambalo ni pekee kwa Waefeso na inarejerea ulimwengu wa roho ufanyao kazi katika historia ya mwanadamu.
3. Kuna baadhi ya maandiko ya Paulo ambayo yanaunganisha mamlaka ya umma na ya kiroho (yaani, 1 Kor. 15:24; Efe. 1:21; na Kol. 1:16). Angalia MADA MAALUM: SERIKALI YA KIBINADAMU katika 1 Tim. 2:2.

## MADA MAALUMU: *ARCHĒ*

Neno la Kiyunani archē linamaanisha "mwanzo" au "asili" ya kitu.

1. mwanzo wa mpangilio ulioumbwa (kama vile. Yohana 1:1; Ebr. 1:10)
2. mwanzoni mwa injili (kama vile Mk. 1:1; Flp. 4:15; 2 The. 2:13; Ebr. 2:3; 1 Yohana 1:1)
3. mwanzo wa jicho la kwanza la ushahidi (kama vile. Luka 1:2)
4. mwanzo wa dhambi (miujiza, kama vile. Yohana 2:11)
5. mwanzo wa mafundisho (kama vile Ebr. 5:12)
6. mwanzo wa udhihirisho uliojikita katika kweli ya injili (kama vile. Ebr. 3:14)
7. mwanzo, Kol. 1:18; Ufu. 3:14

Ilikuja kutumika juu ya "utawala" au "mamlaka"

1. juu ya wanadamu rasmi watawalao
    a. Luka 12:11
    b. Luka 20:20
    c. Warumi 13:3; Tito 3:1
2. juu ya mpangilio wa mamlaka
    a. Warumi 8:38
    b. 1 Kor. 15:24
    c. Efe. 1:21; 3:10; 6:12
    d. Kol. 1:16; 2:10,15
    e. Yuda 1:6

◙**"na kutii"** Hii ni KAULI TENDAJI YENYE KITENZI JINA YA WAKATI ULIOPO. Ni neno ambatani na mzaha juu ya "tii" (*peithomai*) pamoja na "watawala" (*archē*). Linapatikana hapa na katika Mdo. 27:21 katika Agano Jipya. Dhana ya utii na unyenyekevu inarudiwa katika maonyo ya Paulo kwa wanawake wa Kikristo, watoto na watumwa katika Efe. 5:21-6:9 na Kol. 3:18-25.

◙**"na kuwa tayari kwa kila kazi njema"** Tungo hii katika muktadha inaweza kurejerea kwa huduma ya mamlaka ya umma na/au huduma kwa jamii kwa wanadamu wenza. Hatahivyo tungo inayofanana hivyo inaonekana katika 2 Tim. 2:21 na 3:17, ambapo muktadha unarejerea maisha ya utauwa kwa ujumla (kama vile Tito 2:14; 2 Kor. 9:8; Efe. 2:10). Walimu wa uongo wa Tito 1:16 hawana sifa kwa kazi yoyote njema, ya kawaida au ya Mungu.

**3:2** Sentensi hii inaorodhesha vitu vinne ambavyo Mkristo anatakiwa avifanye kwa majirani zake. Wakristo walikuwa kundi dogo katika jamii. Namna wanavyoenenda ilikuwa ushuhuda wa muhimu sana. Pia hii orodha inaaksi kile kilichokuwa kinafanywa na walimu wa uongo na waamini wa kweli ambavyo hawatakiwi kufanya.
Huu ni ushauri mzuri kwa waaminio wa kisasa wanaojihusisha na matendo ya kisiasa. Namna tunavyotenda ni muhimu kufanana namna tunavyosema! Hakuna Kusudi kubwa linalozidi Uinjilishaji!

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kutomsengenya mtu"** |
| **NKJV, NRSV** | **"kutomsema mtu vibaya"** |
| **TEV** | **"kutomsema mtu kwa mabaya"** |
| **NJB** | **"sio kuwasengenya watu wengine"** |

Hii neno kibayana ni "kukufuru" (kama vile 1 Tim. 1:13,20; 2 Tim. 3:2; 1 Pet. 4:4; 2 Pet. 2:2,10,11,12). Linatumika mara nyingi kumaanisha kumzungumza vibaya Mungu (kama vile Mt. 26:65). Lililkuja kutumika na Paulo kuelezea kwamba Injili haitakiwi kuzungumzwa vibaya kwasababu ya mienendo ya Wakristo (kama vile Rum. 14:16; 1 Kor. 10:30 na hapa). Namna gani Waamini wanaishi ni muhimu kwa ushuhuda wa kiinjili wa kanisa.

◙**"wawe wema"** Hili kama maneno mengine matatu yanarejerea namna waaminio wanatakiwa kuwa na mahusiano na wale wasioamini bado. Angalia dokezo katika 1 Tim. 3:3.

◙**"upole"** Angalia dokezo katika 1 Timotheo 3:3.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kuwajali watu wote"** |
| **NKJV, NRSV** | **"kuonesha matendo mema kwa kila mtu"** |
| **TEV** | **"kuonesha mtazamo wa upole kwa kila mtu"** |
| **NJB** | **"siku zote kuwa wapole kwa watu wa aina zote"** |

Tena tungo inarejerea matendo a waminio kwa wasioamini. Katika 2 Tim. 2:25 inahusiana na matendo yetu kwa waaminio (kama vile 1 Tim. 6:11).

Maudhui ya "kila mtu" is ni tabia ya Barua za Kichungaji. Mungu anapenda watu wote; Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote; Wakristo lazima wawe na mwitikio chanya kwa watu wote (kama vile 1 Tim. 2:1,4,6; 4:10; Tito 2:11).

**3:3 "Maana hapo zamani"** Matendo yanayoelezewa katika mstari huu yanatoa sifa ya mwanadamu aliyeanguka (Mwanzo 3; Rum. 1:19-3:31), hata Wakristo kabla hawajaokolewa (kama vile Rum. 1:29-31; 2 Kor. 6:9-11; Efe. 2:3; 4:17-21; Gal. 5:19-21).

◙**"hatuna akili"** Hili ni neno kwa "kuwaza" au "kufikiria" hali ya hasi tu (kama vile Luka 6:11; 24:25; Rum. 1:14,21; Gal. 3:1,3; 1 Tim. 6:9; 2 Tim. 3:9). Ni neno lenye nguvu kwa kufikiria vibaya na isivyo sawa.

◙**"wasiotii"** Hili ni neno "kuamini" katika hali hasi. Lilitumika juu ya

1. Mfalme Agrippa katika Mdo. 26:19
2. Wapagani katika Rum. 1:30; Efe. 2:2; 5:6
3. Wayahudi katika Luka 1:17; Rum. 11:30,32; Ebr. 4:6
4. walimu wa uongo katika Tito 1:16; 2 Tim. 3:2

◙**"tumedanganywa"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ambayo kibayana inamaanisha "kudanganywa" au "kushawishiwa." Kiasili inarejerea kwa watangaji (yaani sayari ambazo hazikufata njia inayotakikana ya sayari zingine) za anga la usiku na kuja katika Kingereza "planet (sayari)." Ilikuja kutumika kisitiari kwa kile ambacho kiko katika makosa. Neno hili kama yale mengine yaliyotangulia mawili yalitumika na Paulo kuelezea dhambi ya mwanadamu katika Rum. 1:27 na 2 Thes. 2:11. Pia tambua matumizi yake katika 1 Tim. 4:1-2; 2 Tim. 3:13; 1 Pet. 2:25; 2 Pet. 2:18; 3:17; na Yuda 11.

SAUTI IRABU inamaanisha kitendo cha mjumbe wa nje, hapa shetani au mapepo.

◙**"tukitumikia"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO ambayo kibayana inamaanisha "kutenda kama watumwa" kwa tamaa za kibinadamu (kama vile Rum. 6:6,12).

◙**"namna nyingi"** Hiki ni kivumishi "mbali mbali,"kinachotumika kwa upinde wa mvua. Ilitumika juu ya vitu vyenye pande nyingi (yaani, [1] katika 1 Pet. 1:6 na Yakobo 1:2 ya mashitaka mengi ambayo yanawakabili waaminio na [2] katika 1 Pet. 4:10 yenye pande nyingi, asili ya neema ya Mungu yenye pande nyingi).

◙**"tamaa"** Hili ni neno ambatani kutoka "juu ya" (*epi*) na "akili au nafsi" (*thumos*). Inarejerea shauku kubwa kwa ajili ya kitu fulani, mara kwa mara kwa namna hasi. Neno hili linatumika katika Rum. 1:24 kuelezea mwanadamu aliyeanguka.

◙**"anasa"** Tunapata neno la Kingereza "hedonism (anasa)" kutoka katika hili neno la Kiyunani (kama vile Luka 8:14; Yakobo 4:1-3). Anasa binafsi zinaweza kufanyika teso!

◙**"tukiishi katika uovu na husuda"** Haya ni maelezo mengine kutoka Rum. 1:29 juu ya tabia ya mwanadamu aliyeanguka.

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"wenye chuki, wenye kuchukiana"** |
| **NRSV** | **"wasio na haya, wenye kuchukiana"** |
| **TEV** | **"wengine walituchukia nasi tukawachukia"** |
| **NJB** | **"wenye kuchukiana na tukijichukia wenyewe"** |

Matumizi haya ya maneno mawili ya Kiyunani kwa chuki (KIVUMISHI *stugētos* na KAULI ENDELEVU *miseō*). Orodha hii ya matatizo inamkumbusha mtu juu ya Mathayo 7, "kwa matunda yao mtawatambua"! Muktadha huu unaelezea waaminio hawa kabla ya kuongoka lakini tukitegemea kuwa hawakuendelea hivyo baada ya uongofu. Bado inaelezea walimu wa uongo na wafuasi wao wasiojitambua.

**3:4-7** Hii ni moja ya sentensi ya Kiyunani ndefu, ambayo inatoa maana ya Injili (inafanana na 2:11-14). Inaweza kuwa hata kutoka katika tenzi, tungo au nyimbo (angalia Nestle-Aland Greek NT 26th and 27th editions).

**3:4"Lakini wema"** Aisee! Ni utofauti mzuri wa namna gani neema inatenda! Tunapata neno la Kingereza "philanthropy (ukarimu)" Kutoka katika neno hili ambalo linatokana na maneno mawili ya Kiyunani: "upendano wa kindugu" (*phileō*) na "mwanadamu" (*anthropos*). Katika Agano Jipya neno hili linapatikana hapa tu katika Mdo. 28:2. Mungu anapenda watu waliofanywa kwa sura yake (yaani Mwa. 1:26-27), hata walioanguka (kama vile Rum. 5:8).

◙**"wake Mwokozi wetu Mungu"** Haya ni maelezo ya YHWH (kama vile 2 Wafalme. 13:5; Zab. 106:21; Isa. 19:20; 43:3,11; 45:15,21; 49:26; 60:16; Luka 1:47). Hii inaweza kuaksi cheo cha kisasa kwa ajili ya Mfalme (kama vile 1 Tim. 1:1). Hii ni Tungo ya tabia ya Barua za Kichungaji. Tazama kwamba Yesu anaitwa cheo hicho hicho katika Tito 3:6 (kama vile 1 Tim. 1:1; 2:3; 4:10; Luka 2:11; Yohana 4:42; Mdo. 5:31; 13:23; 2 Tim. 1:10). Linganisha Tito 1:3-4; 2:10-13; 3:4-6. Njia mojawapo ya kuunganisha Baba na Mwana nilikuwa ni kwa kutumia cheo kile kile kwa wote! Moyo halisi wa Mungu muumbaji upo katika kuokoa, kukomboa, kusamehe, kurejesha, kuunganisha viumbe vyake vilivyoasi (kama vile Yohana 3:16; Rum. 5:8). Angalia dokezo kamili katika 2 Tim. 1:10.

◙**"ulipofunuliwa"** Hii inarejerea kuja kwa Mara ya Kwanza kwa Yesu. Neno hilohilo linatumika katika Tito 2:13 kwa ajili ya Kuja kwa Mara ya Pili kwa Yesu (kama vile 1 Tim. 6:14). Angalia Mada Maalum: Misamiati ya Agano Jipya kwa Kurudi kwa Kristo katika Tito 2:13. Wokovu wa Mungu uliohaidiwa (yaani Masihi, angalia Mada Maalumu katika 1 Tim. 1:1) alizaliwa Betlehemu (kama vile Tito 2:11).

**3:5"alituokoa"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU ambayo inamaanisha kitendo kilichokwisha kumalizika wakati uliopita. Hiki ni Kitenzi KIKUU CHA SENTENSI NDEFU ya Kiyunani kutoka Tito 3:4 mpaka Tito 3:7. Angalia Mada Maalum: Njeo za kitenzi cha Kiyunani zinazotumika kwa ajili ya wokovu 2 Tim. 1:9.

◙**"si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi"** Tungo hii inawekwa ya kwanza katika sentensi ya Kiyunani kwa ajili ya msisitizo. Wokovu haujajikita katika juhudi za mwanadamu bali Mungu (kama vile Tito 3:20,2-28; 4:4-5; Rum. 9:11; Gal. 2:16; Efe. 2:8-9; Flp. 3:9; 2 Tim. 1:9). Huu ni mvutano wa kithiolojia kati ya "imani tofauti na matendo" na "imani inayoonekana katika matendo" (kama vile Efe. 2:8-10; Yakobo 2:14-26**)**. Walimu wa uongo wa wenye ujuzi wayahudi wa kichungaji walikuwa wakisisitiza juu ya kutimiza mwanadamu kuwa na kigezo!

◙**"ya haki "** Waaminio lazima waitafute haki (yaani kufanana na Kristo) baada ya wokovu (kama vile 1 Tim. 6:11), lakini wanadamu walioanguka hawawezi kukaribia Mungu mtakatifu kwa vigezo vya haki yao wenyewe (kama vile Isa. 64:6 na mfululizo wa nukuu za Agano la Kale katika Rum. 3:10-18). Angalia MADA MAALUM: HAKI katika Tito 2:12.

◙**"bali kwa rehema yake"** Tumaini pekee la mwanadamu aliyeanguka liko katika rehema za neema ya Mungu mwenye upendo. Ni tabia Yake na tendo lake la kimakusudi ambalo limepelekea sisi kupata nafasi ya msamaha na urejesho (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Mal. 3:6; Efe. 2:4-7; 1 Pet. 1:3). Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:10.

◙**"kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili"** Hii kibayana ni "kupitia utakazo wa uamsho." Neno kuosha (*loutron*) linatumika mara mbili katika Agano Jipya (Efe. 5:26 na hapa). Ilikuwa kwa nadra likitumika katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani. Inaweza kurejerea

1. sehemu ya kuogea
2. maji ya kuoshea
3. tendo la kuosha

Katika Mambo ya Walawi ilikuwa ishara ya kusafishwa au kufanywa msafi mtu au vitu (kama vile Magombo ya Bahari ya Chumvi). Katika Efe. 5:26 kuoga kulirejerea ibada ya kuoga kabla ya ndoa.

Neno "regeneration (kufanywa upya)" (*palingenesia*) ni neno nadra, linalopatikana katika Mt. 19:28 na hapa. Ni neno ambatani kutoka "tena" (*palin*) na "kuzaliwa" (*genesis*). Hivyo linarejerea kuzaliwa upya kunakoletwa na kazi iliyokwisha malizika ya Kristo na kuomboleza kwa Roho. Namna ya ubatizo mpya ni ubatizo wa maji, msaidizi ni Roho Mtakatifu (kama vile Tito 3:5-6) Njia ni kufa na kufufuka na Kristo (kama vile Tito 3:6), na msingi wake wote ni upendo na rehema za Baba (kama vile Tito 3:4). Hili si andilo linalokubaliana na ubatizo wa kufanywa upya. Ubatizo lilikuwa ni tendo la ukiri wa wazi (kama vile Mdo. 2:38) Na ishara ya mwamini ya kufa, kuzikwa na kufufuka pamoja na Kristo katika tendo la kiishara (kama vile Rum. 6:3-9; Kol. 2:12). Katika kanisa la mwanzo ubatizo ilikuwa ni nafasi ya ukiri wa wazi wa imani ("Yesu ni Bwana" kama vile Rum. 10:13). Shabaha ni tendo la Roho Mtakatifu (yaani kuzaliwa na kufanywa upya).

## MADA MAALUM: UBATIZO

I. Ubatizo katika maisha ya Kiyahudi
II. Ubatizo ulikuwa utaratibu wa kawaida miongoni mwa Wayahudi wa karne ya kwanza na ya pili.
   1. maandalizi ya kuabudu hekaluni (yaani, utaratibu wa kujitakasa)
   2. ubatizo wa kujibatiza mwenyewe kwa kubadili dini

Ikiwa mtu alikuwa na historia ya kuwa mtu wa Mataifa ilimlazimu kuwa mtoto kamili wa Israeli, huyu ilimpasa kutimiza majukumu matatu:

   a. tohara, ikiwa ni mwanamume
   b. kujibatiza mwenyewe kwa kuzama majini, katika uwepo wa mashahidi watatu
   c. dhabihu ndani ya Hekalu

   3. Tendo la utakaso (kama vile Mambo ya Walawi 15)

Makundi ya kimadhehebu ya karne ya kwanza ya ki- Palestina, kama vile Essenes, kwa uwazi kabisa ubatizo lilikuwa jambo la kawaida, zoezi lililorudiwa rudiwa. Hata hivyo, kuifanya dini ya kiyahudi iwe rasmi, Ubatizo wa Yohana wa toba ungeweza kuwa wa kungemnyenyekeza mtoto wa asili kuyafanya Mataifa kuzikubali taratibu hizi.

◙**"kufanywa upya"** Hili ni neno nadra linalotumika mara mbili tu katika Agano Jipya, hapa na Rum. 12:2. Inamaanisha kumsababisha mtu au kitu kuwa kipya. Neno linalofanana linapatikana katika Kol. 3:10. Kisarufi ni neno sawasawa na "kuzaliwa upya." Kuna KIELEZI kimoja tu (*dia*) kwa ajili ya yote mawili. Hivyo hii sio kazi mbili ya neema laki namna mbili ya kazi moja. Hii inamaanisha kwamba ni tukio moja linaloongozwa na Roho Mtakatifu. Hii ingekuwa sawasawa na Yohana 3:5-8 na 1 Pet. 1:23.

**3:6 "alitumwagia"** Hii ingeweza kurejerea kwa Baba (kama vile Tito 3:4) au Roho Mtakatifu (kama vile Tito 3:5). KITENZI kile kile chenye utata ule ule kinatumika katika Mdo. 2:17-18,33; 10:45, ambayo inachukuliwa kutoka kwa Yoeli 2:28-30.

◙**"kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu"** Cheo "Mwokozi" inamaanisha Mungu Baba katika Tito 3:4 Sasa inafanya kazi kwa Mwana. Mabadilishano yale yale yanafanywa juu ya vyeo na kupatikana katika Tito 1:3 na 4; na 2:10 na 13.

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

A. Injili
   1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
   2. Yohana 14:26
B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
C. Paulo
   1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
   2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
   3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
   4. Gal. 4:4-6
   5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
   6. 1 The. 1:2-5
   7. 2 The. 2:13
   8. Tit. 3:4-6
D. Petro – 1 Pet. 1:2
E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
   1. Jina *Elohim* liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
   2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
A. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
   1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
   2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
   3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   4. Zakaria 3:1-2
B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
D. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origen-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa

Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho

**3:7 "ili kwamba"** Hii ni kauli ya kimakusudi (*hina*) kama 3:8, 13 na 14.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"tukihesabiwa haki kwa neema Yake"** |
| **NKJV, NRSV** | **"tukisha hesabiwa haki kwa neema Yake"** |
| **TEV** | **"kwa neema Yake tuweze kupatanishwa na Mungu"** |
| **NJB** | **"kuhesabiwa haki na Mungu"** |

Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU (kama vile Rum. 1:16-17; 3:24) inayohusiana na neno "haki." Angalia dokezo kamili katika Tito 2:12. SAUTI IRABU inamaanisha kwa usaidizi wa Roho. "kuhesabiwa haki kwa imani" ni sitiari ya kimahakama (kisheria) inayotumiwa mara kwa mara na Paulo kusisitiza neema ya kwanza ya Mungu (kama vile 1 Tim. 1:2,14; 2 Tim. 1:2; Tito 1:4). "hesabia haki" na "kuhesabiwa haki," ni maneno yaliyozoeleka katika Wagalatia na Warumi, yanatokea mara mbili katika barua nyingine za Paulo (1 Kor. 6:11 na hapa). Waaminio wamesamehewa na kukubaliwa kwasababu ya Yeye alivyo na kile alichokifanya sio kwasababu ya walo walivyo na vile walivyofanya!

◙**"tumefanywa warithi"** Hiki ni kille cha utumizi wa sitiari za kifamilia zinazotumika kuelezea waaminio (kama vile Rum. 4:13; 8:14-17: Gal. 3:29; 4:7; Ebr. 6:7; Yakobo 2:5).

◙ **"uzima wa milele"** Tazama muhtasari katika Tito 1:2.

**3:8 "Ni neno la kuaminiwa"** Hili ni andiko la kawaida la ishara tano za uthibitisho wa thiolojia ya Paulo kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile. 1 Tim. 1:15; 3:1; 4:9; 2 Tim. 2:11). Kwa dhahiri kile ambacho mistari hii inarejelea majadiliano kati ya wafasiri; wengi wana uhakika na Tito 3:4-7.

◙ **"uyanene kwa nguvu"** Tazama muhtasari katika 1 Timotheo 1:7.

◙ **"ili"** Hili ni *hina* (sehemu ya kusudi) lingine, kama Tito 3:7, 13, na 14.

◙ **"wale waliomwamini Mungu"** ii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI ENDELEVU YA HALI YA KUENDELEA, ambayo inaelezea tendo lililopita na matokea yanayoendelea ambayo yanaimarika kwa pamoja. Kwa kawaida kwenye Agano jipya makusudi ya imani ni Yesu, lakini mara nyingi KIWAKILISHI (yeye) kutumia uungu ni utata na inaweza kurejelea kwa Baba au kwa Mwana. Tazama MADA MAALUM: KUAMINI, KUTUMAINI, IMANI, NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE (אמן) katika 1 Tim. 1:16.

◙ **"wakumbuke kudumu katika matendo mema"** neno “wakumbuke” ni muundo KITENZI “kuwa na shauku” au “kuwa makini”, ambalo linapatikana hapa kwenye Agano jipya pekee. KITENZI JINA “kushikilia” ni kutoka kwenye neno lililotafsiriwa kawaida “simamia” (kama vile 1 Tim. 3:4,5,12). Waaminio ni lazima mara zote wafikilie juu ya na kuendelea kuishi maisha ya ucha-Mungu kwa ajili ya injili. Paulo anathibitisha tena kwamba watu wana haki ya kuwa na Mungu mbali na kazi njema binafsi za mtu, lakini pia malengo ya Mungu kwa kila mwamini ni kazi njema kwa kila mtu (kama vile Efe. 2:8-10 na Yakobo 2:14-23). Shauku ni shukrani bila sababu, rehema za Mungu zisizostahili; matokeo yake ni kufanana na Kristo; lengo ni uinjilisti.

◙ **"kwa wanadamu"** tena, kwa ujumla mkazo ni kwamba Mungu anawapenda wanadamu wote na anatamani wote waokolewe (Yn. 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Mlango wa njia unaoelezewa kwa wasioamini katika Mungu ni maisha ya mabadiliko kwa waaminio (kama vile. Mt. 5:16; 1 Pet. 2:12).

**3:9 "Lakini ujiepushe"** hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, yenye maana ya "kuendelea kuwa mbali au kuepuka" (kama vile. 2 Tim. 2:16).

◙ **"maswali ya upuzi "** hili ni neno la kwanza la andiko la Kiyunani kwa ajili ya kutilia mkazo (kama vile. 1 Tim. 6:4-5; 2 Tim. 2:14,23). Timotheo ni mwakilishi wa kitume wa Paulo. Hakuwa na haja ya kujadili au kufikilia lakini kutoa ukweli wa kitume na mamlaka.

◙ **"nasaba"** aina ile ile ya walimu wa uongo waliokuwa Efeso (kama vile. 1 Tim. 1:4) walikuwa Krete. Hii nasaba inawezekana ni Wayahudi, wanakisiwa kuwa na uhusiano wa kimasihi, sio kwa kiwango cha ujuzi wa watakatifu (*eons*).

◙ Kuna mfuatano wa NOMINO kwenye Tito 3:9 unaounganishwa kwa "na" (*kai*), ambao yumkini unarejelea kipengele tofauti au mwelekeo kwa ujumla (yaani, "maswali," "nasaba," "magomvi," na "mashindano").

◙ **"juu ya sheria"** hii inaonyesha kipengele cha wayahudi kwenye mafundisho haya ya uongo (kama vile. Tito 1:10,14; 1 Tim. 1:3-7). Tazama mada maalumu: maono ya Paulo juu ya sheria za Musa katika 1 Tim. 1:8.

◙ **"Kwa kuwa hayana faida, tena hayana maana."** Thiolojia ya maneno ya bure na kukisia mara zote hayasaidii mwili wa Kristo. Tito, kama Timotheo, anaongea kwa mamlaka ya kitume ya Paulo.

**3:10 "mkatae"** hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, nyingine kama Tito 3:9. Neno sawa na, "kukataa, kataa, au kana," yametumika kwenye 1 Tim. 4:7; 5:11 na 2 Tim. 2:23. Dhana ile ile iliyotumika kwenye Rum. 16:17; Gal. 1:8-9; 2 The. 3:6-14.

Kwenye mazungumzo yetu tunayojaribu na jumuia moja ya watu hatuwapi ishara yeyote au salamu kwamba wanaweza kuona kama kukubaliwa au uthibitisho (kama vile 2 Yohana 10)!

**NASB " Mtu aliye mzushi "**
**NKJV "Mtu aliye na matatizo"**
**NRSV "yeyote asababishaye matatizo"**
**TEV "kwa wale wote wasababishao matatizo"**
**NJB "ikiwa mtu anashindana na kile unachofundisha"**

Hili ni neno la Kiyunani *hairetikos* (ambalo limejitokeza hapa kwenye Agano jipya pekee), ambalo tunapata neno la Kiingereza "heretic (mzushi)." Neno hili asili linamaanisha "kuchukua upande" au "kuchagua mmoja." yametumika kwenye Agano Jipya

1. ya "madhehebu" kwenye Mdo. 5:17; 24:14
2. ya "kikundi kidogo ndani ya kundi zima" kwenye 1 Kor. 11:19; Gal. 5:20
3. ya "mafundisho" kwenye 2 Pet. 2:1

◙ **"baada ya kumwonya mara ya kwanza na mara ya pili,"** hii inahusiana na baadhi ya vifungu vya Agano Jipya kwenye nidhamu ya kanisa (kama vile Mt. 18:15-17; Gal. 6:1; 2 Thes. 3:15; Yakobo 5:19). Yumkini ikaaksi Law. 19:17.

**3:11"ukijua ya kuwa mtu kama huyo"** hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI ENDELEVU YA HALI YA KUENDELEA. Matendo yao yalikuwa dhahili na kuendelea kuonyesha uhalisia wao (kama vile Mathayo 7).

◙ **"amepotoka"** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDWA ELEKEZI YA HALI YA KUENDELEA. Muundo huu unapatikana hapa kwenye Agano Jipya pekee. Huu ni mchanganyo wa neno kutoka *ek* (kutoka) na *strephō* (kugeuka), hivyo ikimaanisha kugeuka kutoka. Huu ni mzaha wa neno kugeuka kwa Kristo (kuongoka) kwa Mt. 18:3 (*epistrephō*), ambayo inaaksi neno la agano la kale kwa ajili ya kugeuka (*shub*) kwa Mungu (Mt. 13:15; Marko 4:12; Luka 22:32; Yohana 12:40; Mdo. 3:19; 25:27; Yakobo 5:19-20). Walimu hawa wa Uongo sasa wanageuka kutoka kwa Mungu (kama vile Tito 1:14, *apostrephō*) kwenda kwenye uzushi na mafundisho ya uongo.

SAUTI IRABU inamaanisha msaidizi wa nje. Katika muktadha huu inatakiwa awe shetani au mapepo. Juu ya "Shetani" Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 3:6 na juu ya "mapepo" angalia Mada maalum katika 1 Tim. 4:2.

◙**"tena atenda dhambi"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO ambayo inamaanisha tabia, tendo linaloendelea, tabia iliyo katika mtindo wa maisha (kama vile 1 Tim. 5:20, pia tazama NJEO YA WAKATI ULIOPO katika 1 Yohana 3:6,9).

◙**"maana amejihukumu"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Muundo unapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Matendo yetu na maneno yanafunua mioyo yetu (kama vile 1 Tim. 5:24; Mathayo 7).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 3:12-14**
**[12] Wakati nitakapomtuma Artema kwako au Tikiko, jitahidi kuja kwangu huku Nikopoli; kwa maana huku nimekusudia kukaa wakati wa baridi. [13] Zena, yule mwana-sheria, na Apolo, uwasafirishe kwa bidii, wasipungukiwe na cho chote. [14] Watu wetu nao wajifunze kudumu katika matendo mema, kwa matumizi yaliyo lazima, ili wasiwe hawana matunda.**

**3:12 "Artema"** Mtu huyu hajulikani kwetu ila si kwa Mungu.

◙**"Tikiko"** Anatajwa katika Mdo. 20:4; Efe. 6:21-22; Kol. 4:7-8 na 2 Tim. 4:12. Ndiye mpelekaji wa barua za Paulo Gerezani. Hawa watu wawili walitakiwa kuchukua nafasi ya uongozi ya Tito huko Krete ili kwamba aweze kuungana na Paulo wakati wa Kipupwe.

Hii inaonesha kwamba barua ingawa iliandikwa kwenda kwa Tito ilikuwa imekusudiwa kutoa taarifa, kuelekeza na kutia moyo kanisa zima la Krete. Kauli nyingi za Paulo kwenda kwa Tito hazituoneshi sana kwamba Tito alitakiwa kuondoka haraka baada ya barua kuwa imepokelewa labda kama ilikuwa dhahiri kwa Wakristo kwamba Paulo alikuwa alikuwa nazungumza nao kupitia maneno yake kwa Tito.

◙**"jitahidi kuja kwangu huku"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Paulo hakutaka kuwa peke yake (kama vile 2 Tim. 4:9,21), Nafikiri ni kwasababu alikuwa na tatizo kali la macho yawezekana kwasababu ya wakati wa nyuma wa uongofu wake njiani Dameski (kama vile Mdo. 9:3-9,12,17-18). Naamini "mwiba mwilini" (kama vile 2 Kor. 12:7) yawezekana lilikuwa tatizo la macho. Tazama kauli isiyokuwa ya kawaida katika Gal. 4:15. Pia katika Gal. 6:11 Paulo anazungumza juu ya mwandiko wake mwenyewe kuwa mkubwa sana. Aliandika mistari ya mwisho miwili kuthibitisha hilo (kama vile 2 The. 2:2; 3:17; 1 Kor. 16:21; Kol. 4:18; Filemoni 19).

◙**"Nikopoli"** Kuna miji kadhaa kwa jina hili ambayo inamaanisha "mji wenye ushindi." Huu yawezekana ulikuwa mji wa pwani karibu na eneo la mapigano ya Actium.

**3:13**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"fanya bidii kusaidia. . .njiani kwao"** |
| **NKJV** | **"tuma. . .katika safari yao kwa haraka"** |
| **NRSV** | **"fanya bidii kutuma. . .wakiwa njiani"** |
| **TEV** | **"jitahidi kwa nguvu zote kusaidia. . .waanze safari yao"** |
| **NJB** | **"saidia kwa shauku njiani kwao"** |

Hiki ni KIELEZI *spoudaiōs*, ambacho kinamaanisha "kwa juhudi" au "shauku" au "kwa bidii" (kama vile Luka 7:4 na neno linalofanana la Flp. 2:28). Limeunganishwa na KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO *propempō*, ambalo linamaanisha kufanya maandalizi yote yanayotakiwa kwa ajili ya safari (kama vile 3 Yohana 6; na Mdo. 15:3). Inavyoonekana Zena na Apollo walikuwa wakifanya juhudi ya kimisheni. Paulo anaomba msaada huo huo kusaidia makanisa ya nyumbani huko Rumi katika Rum. 15:24.

◙**"Zena, yule mwana-sheria"** Ikiwa alikuwa Myahudi au mwanasheria wa Kiyunani haijulikani.

◙"**Apolo"** Alikuwa muhubiri machachali kutokea Alexandria aliyekuwa amesaidiwa kuelewa kikamilifu injili na Prisilla na Akilla (kama vile Mdo.18:24,28; 19:1; 1 Kor. 1:12; 3:5,6,22; 4:6; 16:12). Hawa watu wawili yawezekana walikuwa wasambazaji wa barua za Paulo kwenda kwa Timotheo.

**3:14 "Watu wetu nao wajifunze kudumu katika matendo mema"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile Tito 1:16; 2:7,14; 3:18), kuwatia moyo wamisionari katika majukumu yao ya uinjilishaji (kama vile Tito 2:7,14; 3:8).

◙**"ili wasiwe hawana matunda"** Neno "wasiokuwa na matunda" ni tata. Nafikiri linafanana na lile la Paulo "bure" (kama vile *eikē* katika 1 Kor. 15:2; Gal. 3:4; 4:11 au *kenos* katika 1 Kor. 15:10,58; 2 Kor. 6:1; Gal. 2:2; Flp. 2:16; 1 The. 2:1; 3:5), ambayo inarejerea uanzishwaji wa makanisa yenye mguso na mtazamo wa umisheni wa uinjilishaji. Paulo alianzisha makanisa katika maeneo kadhaa aliyoyachagua kwa ajili ya kusudi la uinjilishaji wa eneo lote zima. Ikiwa kwa sababu yoyote makutano haya ya kwanza yalipoteza muono wa kusudi la "agizo kuu" basi kupandwa kwake kungekuwa bure!

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 3:15a**<br>**15 Watu wote walio pamoja nami wakusalimu** |

**3:15 "Watu wote walio pamoja nami wakusalimu"** Paulo mara kwa mara japo si siku zote (kama vile 1 Timotheo), anahitimisha barua zake kwa salamu (1) kutoka kwa timu ya watu wanaofuatana naye (2) kwa waaminio wa kanisa au maeneo anayowaandikia.

◙**"katika imani"** Neno Imani linaweza kutumika ju ya fundisho kama katika Mdo. 6:7; 13:8; 14:22; Gal. 1:23; 3:23; Flp. 1:27; Yuda 3,20 au njia ya uhusiano binafsi wa mtu na Mungu kupitia Kristo (kama vile Yohana 1:12; 3:16). Inaweza pia kutumika katika namna ya uaminifu au kutumainia kwa Agano la Kale. Angalia MADA MAALUM: KUAMINI, KUTUMAINI, IMANI, NA UAMINIFU KATIKA AGANO LA KALE (אמן), kuamini na kutumaini katika 1 Tim. 1:16. Tungo hii inarejerea ukweli kwamba walimu wa uongo huko Krete walikataa mamlaka ya Kiyume ya Paulo na mafundisho.

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) TITO 3:15b**<br>**15 Neema na iwe pamoja nanyi nyote.** |

◙**"Neema na iwe pamoja nanyi nyote"** Ile "ninyi" ina WINGI. Barua hii ilitakiwa kusomwa katika makanisa ya nyumbani huko Krete kama ilivyokuwa Barua zote za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 6:21; 2 Tim. 4:22).

◙Toleo la King James linahitimisha na "Amina," lakini hii haipo katika maandiko ya kale ya Kiyunani ya P[61], א[*], A, C, or D[*]. Yawezekana baadaye waandishi walitambua matumizi yake katika Rum. 16:27; Gal. 6:18; Flp. 4:20; 2 Thes. 3:18; 1 Tim. 6:16; na 2 Tim. 4:18 na kuongezwa hapa kama walivyofanya katika Warumi 15:33; 16:20,24; 1 Kor. 16:24; 2 Kor. 13:14; Efe. 6:24; Flp. 4:23; 1 Thes. 5:28; 1 Tim. 6:21; 2 Tim. 4:22; na Tito 3:15. Toleo la UBS[4] linatoa uondoaji waka alama ya "A" (hakika).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Wakristo wawe na utii kwa serikali ya umma? Je vipi ikiwa mamlaka ya utawala siyo ya Kikristo?
2. Nini msisitizo mkubwa wa Tito 3:4-7?

3. Je ubatizo ni muhimu kwa ajili ya wokovu? Kwanini? Kwanini sio?
4. Kwanini waaminio waheshimu na kutii mamlaka ya kiserikali?
5. Uzushi ni nini?
6. Bainisha kauli za kithiolojia za Tito 3:5-7.
7. Je "matendo mema" ya Tito 3:8 na 14 yanajumuisha nini?
8. Je walimu wa uongo ni Wayahudi au Wenye Ujuzi? Kwanini?

# 2 TIMOTHEO 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS4 | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Salamu<br>1:1-2 | salamu<br>1:1<br>1:2a<br>1:2b | salamu<br>1:1<br>1:2a<br>1:2b | Utangulizi<br>1:1<br>1:2a<br>1:2b | salamu na Shukurani<br>1:1-2 |
| Uaminifu kwa ajili Ya Injili<br>1:3-14 | Imani ya Timotheo na urithi<br>1:3-7 | Shukurani na Maonyo<br>1:3-7 | Shukurani na Kutia moyo<br>1:3-7 | 1:3-5 |
| | | | | Kipawa ambacho Timotheo amekipokea<br>1:6-11 |
| | Kutoionea haya Injili | Hamasiho la kuonesha ujasiri<br>(1:8-2:13) | | |
| | 1:8-12 | 1:8-14 | 1:8-10 | |
| | Kuwa Mwaminifu Kwa Imani<br>1:13-18 | | 1:11-14 | |
| | | | | 1:12 |
| 1:15-18 | | 1:15-18 | 1:15-18 | 1:13-14<br>1:15-18 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 1:1-2**
**1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu; kwa ajili ya ahadi ya uzima ulio katika Kristo Yesu; 2 kwa Timotheo, mwanangu mpendwa. Neema na iwe kwako, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.**

**1:1 "Paulo"** Sauli wa Tarso kwa mara ya kwanza aliitwa Paulo katika Mdo. 13:9. Inawezekana kwamba Wayahudi wengi wa nje walikuwa na jina la Kiebrania (Sauli) na jina la Kiyunani (Paulo). Ikiwa ndivyo hivyo, sasa kwa nini ghafla"Paulo" inatokea ghafla Mdo. 13? Yawezekana (1) wengine walianza kumuita kwa jina hili au (2) alianza kujiiita mwenyewe kwa jina "mdogo" au "wa hadhi ya chini." Jina la Kiyunani *Paulos* lilimaanisha "mdogo." Nadharia kadhaa zimekua juu ya asili ya jina la Kiyunani: (1) desturi ya karne ya pili inadai kwamba Paulo alikuwa

mfupi, mnene, mwenye kipara, mwenye miguu ya matege na mwenye nyusi nyingi na macho yaliyojitokeza nje, wakitoa kutoka katika kitabu kisicho cha kikanoni ambacho Thessalonika inaita *Paul and Thekla*, ni chanzo kinachowezekana cha jina; (2) Paulo anajiita mwenyewe "mdogo wa mitume" kwasababu alilitesa kanisa (kama vile Mdo. 9:1-2; 1 Kor. 15:9; Efe. 3:8; 1 Tim. 1:15). Wengine wameona huu "udogo" kama asili ya cheo alichojiita. Hatahivyo katika kitabu kama Wagalatia ambapo alisisitiza kujitegemea kutoka katika kujilinganisha na wale Kumi na Mbili wa Yerusalemu, hii inaweza ikawa haihusiani (kama vile 2 Kor. 11:5; 12:11; 15:10).

◙**"mtume"** Hii ilitoka katika neno la Kiyunani "kutuma" (*apostellō*). Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 1:1. Yesu alichagua wanaume Kumi na Mbili wawe pamoja naye kwa namna maalum na akawaita "Mitume" (kama vile Luka 6:13). Neno hili mara kwa mara lilitumika na Yesu kwa kutumwa kutoka kwa Baba (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34; 5:24,30,36,37,38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8,18,21,23,25; 20:21). Katika vyanzo vya Kiyahudi, mtume alikuwa mtu aliyetumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, sawasawa na "balozi" (kama vile 2 Kor. 5:20).

◙**"Kristo"** Hii ni neno sawasawa la Kiyunani la Kiebrania *messiah,* lililomaanisha "aliyepakwa mafuta." Ilimaanisha "Yule aliyeitwa na kuwezeshwa na Mungu kwa ajili ya kusudi fulani." Katika makundi matatu ya viongozi wa Agano la Kale — makuhani, wafalme na manabii — walipakwa mafuta. Yesu alitimiza nafasi tatu zote za ofisi hizi (kama vile Ebr. 1:2-3). Yeye ni Yule aliyehaidiwa ambaye alitakiwa kuanzisha nyakati mpya ya haki. Angalia MADA MAALUM: MASIHI katika 1 Tim. 1:1.

◙**"Yesu"** Neno hili la Kiebrania lilimaanisha "YHWH anaokoa," "YHWH ni wokovu,"au "YHWH huleta wokovu." Ni sawasawa na jina la Agano la Kale "Yoshua." "Yesu" inatoka katika jina la Kiebrania, *hosea*, ikiwekwa na kiambishi tamati cha jina la agano la Mungu, "YHWH." Ilikuwa jina lililotolewa na Mungu kupitia malaika kwa Maria (kama vile Mt. 1:21).

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El* (BDB 42, KB 48)
   1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, "kuwa shupavu" au "kuwa mwenye nguvu" (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
   2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra),akaitwa "baba wa miungu" na "bwana wa mbinguni"
   3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
      a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana BDB 42 & 751 II), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
      b. *El-Roi* ("Mungu aonaye" au "Mungu ajifunuaye Mwenyewe" BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
      c. *El-Shaddai* ("Mungu Mkuu" au "Mungu mwenye huruma zote" au "Mungu wa mlima"), BDB 42 & 994) Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
      d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
      e. *El-Berit* (Mungu wa Agano"), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46
   4. *El* inalinganishwa na
      a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
      b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, "Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
      c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
      d. "wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
      e. "rehema" katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
      f. "mkuu na mzuri" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
      g. "maarifa" katika I Sam. 2:3

h. “kimbilio langu” katika II Sam. 22:33
i. “mlipa kisasi wangu” katika II Sam. 22:48
j. “mtakatifu” katika Isa. 5:16
k. “muweza” katika Isa. 10:21
l. “wokovu wangu” katika Isa. 12:2
m. “mkuu na mwenye nguvu” katika Yer. 32:18
n. “anayepatiliza: katika Yer. 51:56

5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH,* kurudiwa)

B. *Elyon* (BDB 751, KB 832)

1. Maana yake ya msingi ni “juu,” “aliyetukuzwa,” au “kuinuliwa” (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme.
18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
    a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
    b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
    c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
    d. *El* - Hes. 24:16
    e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya “Mungu aliye Juu”) katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
    a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
    b. Balaamu, Hes. 24:15
    c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
    d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)

1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104).
Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.
7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
    a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa “wingi wa ukuu,” mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
    b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7.

c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)

1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
   a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
   b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).
   Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.
2. Katika Mwanzo 4:26 inasema"*wanadamu* wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
   a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
   b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
   c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
   d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
   e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
   f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
   g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo. 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
   h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
      (1) *Yah* (mfano Hallelu – yah, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)
      (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
      (3) *Yo* (majina mfano Joeli)
3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania "mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
   a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa ), Mwanzo. 22:14
   b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 & 950, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Kutoka. 15:26

c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 & 651,Kutoka. 17:15
d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 & 872, *Piel* HALI YA KUENDELEA),Kut. 31:13
e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022), Waamuzi. 6:24
f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi ,BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu, BDB 217 & 944, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Zab. 23:1
h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6
i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa,BDB 217 & 1027), Ezek. 48:35

◙**"kwa mapenzi ya Mungu"** Tungo hii hii ya utangulizi inatumika katika 1 Kor. 1:1; 2 Kor. 1:1; Efe. 1:1; na Kol. 1:1. Paulo alishawishiwa kwamb a Mungu alikuwa amemchagua yeye kuwa Mtume. Namna hii maalum ya wito ilianza kwa kuongoka alipokuwa njiani akielekea Dameski (kama vile Mdo. 9:1-22; 23:3-16; 26:9-18). Paulo mara kwa mara alielezea mamlaka yake aliyopewa na Mungu na wito ili kuthibitisha maandiko yake kuwa ni ya kipekee kutoka kwa Mungu (yaani yaliyovuviwa, kama vile 2 Tim. 3:16; 1 Kor. 2:9-13; 1 Thes. 2:13).

**NASB, NKJV "kwa ahadi ya uzima"**
**NRSV "kwa makusudi ya ahadi ya uzima"**
**TEV "kutangaza uzima uliohaidiwa"**
**NJB "kulingana na ahadi ya uzima"**

Paulo alikuwa naeleza kwamba wokovu wake, wito na uwezeshwaji wa kihuduma umejikita juu ya uzima wa Mungu wa uzima halisi, uzima wa milele kupitia Kristo
(kama vile 2 Tim. 1:1,2,9,13). Paulo anaelezea dhana hii ya Mungu kuwa na yeye kutoa uhai mara kadhaa katika nyaraka za Kichungaji (kama vile 2 Tim. 1:1; 1 Tim. 6:15-16,19; Tito 1:2).

**1:2 "kwa Timotheo mwanangu mpendwa"** Hii ni sitiari ya Paulo kuwa baba wa kiroho wa Timotheo katika injili (kama vile 2 Tim. 2:1; Tim. 1:2; Tito 1:4). Hii ni aya ya ufunguzi inayoonesha upendo wa pande zote mbili. Angalia MADA MAALUM: TIMOTHEO katika 1 Tim. 1:1.

◙**"neema, rehema na amani"** Tazama ufanano na tofauti katika salamu za ufunguzi wa Paulo wa ufanano
1. "neema iwe kwenu na amani kutoka kwa Mungu na Bwana Yesu Kristo" (Rum. 1:7; 1 Kor. 1:3; 2 Kor. 1:2; Gal. 1:3; Efe. 1:2; Flp. 1:2; 1 Thes. 1:2; Filemon 1:3)
2. "Neema iwe kwenu na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu" (Kol. 1:2)
3. "Neema kwenu na amani" (1 Thes. 1:1)
4. "Neema, rehema na amani itokayo kwa Bbaba na Kristo Bwana wetu" (1 Tim. 1:2; 2 Tim. 1:2)
5. "Neema na amani kutoka kwa Baba na Kristo Yesu Bwana wetu" (Tito 1:4)

Tazama kuna aina mbali mbali lakini baadhi ya viashiria ni vya kawaida
1. "Neema" inaanza salamu. Ni aina iliyofanywa Kikristo ya ufunguzi wa Kiyunani cha kawaida wa kati. Inaweka shabaha juu ya tabia ya Mungu.
2. "amani" ni matokeo ya wanadamu kutumaini katika Mungu anayetumainika, kuamini katika uaminifu wake.
3. "Rehema" ni namna nyingine ya kuelezea tabia ya Mungu na ni ya kipekee kwa I na 2 Timotheo. Neno hili lilitumika katika Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani kufasiri neno la Kiyunani *hesed* (yaani upendo wa agano na uaminifu). Mungu ni wa neema na Mwaminifu.
4. Baba na Mwana wanatajwa katika kila salamu (katika 1 Wathesalonike wanatajwa katika tungo iliyopita). Siku zote zinaunganishwa kisarufi. Hii ilikuwa njia moja wapo ya waandishi wa Agano Jipya ya kuelezea Uungu kamili wa Yesu wa Nazareti. Hii ilikuwa pia kweli ya matumizi ya vyeo vya Agano la Kale kwa ajili ya YHWH (yaani Bwana na Mwokozi).

◙**"kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu."** Tungo ya ufunguzi ambayo inafuatia "neema, rehema na amani" ina KIELEZI (*apo*) ikiunganishwa na Baba na Mwana katika mahusiano (kama vile 1 Tim. 1:2; Tito 1:4 na 2 Tim. 1:2). Hii ilikuwa mbinu iliyotumiwa na Paulo kuelezea Uungu wa Yesu.

"Baba" halitumiki katika namna ya kuzaa kwa kujamiiana au kwa mtiririko wa namna hiyo bali uhusiano wa kifamilia wa ukaribu zaidi. Mungu alichagua maneno familia kujifunua mwenyewe kwa binadamu (kama vile. Hosea 2-3, ambapo Mungu anaoneshwa kama mwenye upendo, mpenzi mwaminifu na Hosea 11 anaoneshwa kama baba mwenye upendo).

Uungu wa Ufunuo sio Kianzilishi au Kisababishi cha Kwanza cha Falsafa ya Kiyunani bali Baba wa Kristo Yesu. Biblia sio Falsafa iliyojengewa mantiki za kibinadamu bali ufunuo wa Kimungu unaojifunua wenyewe bila kugungduliwa na uchambuzi wa kibinadamu. Angalia MADA MAALUM: BABA katika 1 Tim. 1:2.

◙**"Bwana"** Mungu alifunua jina lake la Agano — YHWH — kwa Musa katika Kutoka. 3:14. Ilikuwa kutoka KITENZI "kisaidizi" cha Waebrania. Wayahudi baadae walikuwa na hofu kutamka jina takatifu hili wakati wakisoma maandiko isije ikatamkwa bure na kuvunja moja ya Amri Kumi (kama vile Kut. 20:7; Kumb. 5:11). Hivyo waliweka mbadala wa neno lingine, *Adon*, lililomaanisha, "mume, mmiliki, Bwana, Mkuu." Hiki ni chanzo cha neno la tafsiri ya Kingereza YHWH kama BWANA. Angalia MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU katika 2 Tim. 1:1.

Wakati waandishi wa Agano Jipya walipoita Yesu "Bwana" (*kurios*), walikuwa wakielezea Uungu. Huu ukiri ulifanyika kanuni ya ubatizo wa kanisa la kwanza, "Yesu ni Bwana" (kama vile Rum. 10:9-13; Flp. 2:6-11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 1:3-14**

**[3] Namshukuru Mungu, nimwabuduye kwa dhamiri safi tangu zamani za wazee wangu, kama vile nikukumbukavyo wewe daima, katika kuomba kwangu usiku na mchana. [4] Nami natamani sana kukuona, nikiyakumbuka machozi yako, ili nijae furaha; [5] nikiikumbuka imani uliyo nayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, nami nasadiki wewe nawe unayo. [6] Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu. [7] Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi. [8] Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu; [9] ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, [10] na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili; [11] ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa niwe mhubiri na mtume na mwalimu. [12] Kwa sababu hiyo nimepatikana na mateso haya, wala sitahayari; kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile. [13] Shika kielelezo cha maneno yenye uzima uliyoyasikia kwangu, katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu. [14] Ilinde ile amana nzuri kwa Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu.**

**1:3 "Namshukuru Mungu"** Ilikuwa halisi ya barua Kimediteranean kujumuisha maombi ya shukurani mwanzoni mwa barua. Paulo siku zote alifuata utaratibu huu (kama vile Rum. 1:8; 1 Kor. 1:4; Efe. 1:15-16; Flp. 1:3-4; Kol. 1:3-4; 1 The. 1:2; 2 The. 1:3; Filemoni 4).

◙**"ambaye namtumikia. . .tangu zamani za wazee wangu"** Paulo haukuujua Ukristo kuwa tofauti au imani mpya kutoka Agano Jipya (kama vile Mdo. 24:14; 26:5-6,22; Rum. 4; 2 Kor. 11:22; na Flp. 3:5). Katika Gal. 6:15-16 anatumia cheo cha Agano la Kale "Waisraeli wa Mungu" kuelezea kanisa. Katika Rum. 2:28-29 anaelezea kwamba watoto wa kweli wa Ibrahimu ni wa imani na sio wazao wa kikabila (kama vile Rum. 9:6). Hakuna Myahudi wala Myunani (kama vile Rum. 3:22; 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol. 3:11)!

◙**"kwa dhamiri safi"** Angalia dokezo katika 1 Tim. 1:5.

◙**"nikukumbukavyo"** Paulo anakumbuka maisha ya Timotheo, familia na wito kwa huduma. Anatumia neno *mneia* katika njia nne 2 Tim. 1:3-6.

1. katika 2 Tim. 1:3 Paulo anamkumbuka Timotheo bila kukoma katika maombi yake

2. katika 2 Tim. 1:4 anatumia MUUNDO ENDELEVU kumkumbusha Timotheo juu ya kutengwa kwake kimachozi
3. 2 Tim. 1:5 anatumia muundo AMBATANI (*hupo* + *mneia*) kumkumbusha Timotheo juu ya uzingatifu wa kifamilia ya imani
4. katika 2 Tim. 1:6 anatumia muundo KITENZI AMBATANI cha neno (*ana* + *mneia*) kumkumbuka Timotheo juu ya wito wake na uwezeshwaji wake wa kihuduma

Inasaidia kithiolojia na kutia moyo kutazama nyuma ya maisha yetu na mkono wa Mungu ambao ulikuwa ukijumuisha kila hatua (imani ya familia, imani binafsi, wito na kuwezeshwa kihuduma na marafiki wa kimungu na wanasiri).

**1:4** Paulo na Timotheo alikuwa na uhusiano mzuri na huduma ya Kristo. Urafiki wao ulihamasisha na kuwaimarisha wao kwa ajili ya huduma (kama vile 2 Tim. 4:9,21).

**1:5 "imani isiyo na unafiki"** Kibayana hii ni "isiyo na unafiki." Inatumika katika namna ya "imani safi" (kama vile 1 Tim. 1:5).

◙**"ndani yako"** Haijulikani kuitoka katika muktadha (na 3:15 kama vile katika Mdo. 16:1) ikiwa hii inarejerea kwa dini ya Kiyahudi (bibi wa Timotheo na yawezekana mama) au Ukristo (Uongofu wa Timotheo). ni dhahiri kuwa inarejerea Imani kwa YHWH Mpango Wake wa Ukombozi (angalia Mada Maalumu katika 1 Tim. 4:10).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"Nina uhakika kwamba"** |
| **NKJV** | **"nashawishika iko ndani yako pia"** |
| **NRSV** | **"Nina uhakika inaishi ndani yako pia"** |
| **TEV** | **"Nina uhakika kwamba unacho pia"** |
| **NJB** | **"naamini inakaa ndani yako pia"** |

Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Tungo hii katika Kiyunani ni ukiri wa ujasiri endelevu katika kazi ya Roho katika maisha ya Timotheo na huduma (kama vile Flp. 1:6).

**1:6 "uichochee"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO ambayo inamaanisha hitaji linaloendelea la kuchochea mwale. Kuna kipengele cha maamuzi ya kipawa (angalia MADA MAALUM: AGANO katika 2 Tim. 2:1)! Hii haimaanishi kwamba Timotheo aliruhusu mwale wa wito wa Mungu na kipawa kuwaka chini na kuwezeshwa.

◙**"kipawa cha Mungu"** Mzizi wa neno "kipawa" (*charisma*), ambayo inatoka katika "neema" (*charis*). Hii inaweza kumaanisha Roho Mtakatifu au, vizuri zaidi katika muktadha huu, kwa vipawa vyake vya huduma. Kila mwamini ana kipawa kitokacho kwa Mungu au vipawa kwa ajili ya huduma (1 Kor. 12:7,11,18). Karama ya Timotheo ilitambuliwa na Paulo na kanisa lake la nyumbani (kama vile 1 Tim. 4:14).

◙**"kwa kuwekewa mikono"** Hii haiwezi kuwa andiko la kuhakikiwa kwa "kurithi Utume." Angalia dokezo kamili katika 1 Tim. 4:14. Kuwekewa mikono kulitumika kwa sabababu kadhaa katika Biblia. Angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 4:14.

**1:7 "Kwa maana Mungu hakutupa roho ya"** Maandiko ya Kiyunani ya kale ya Agano Jipya kuliandikwa kwa herufi kubwa (uncials), kwa hiyo kutumia herufi kubwa kwa fasiri za kisasa katika jambo la utafasiri. Hakuna KIAMBATA CHA WAZI katika andiko la Kiyunani. Pia hakuna ufanano la Agano Jipya kwa herufi ndogo "r" (kama vile Rum. 8:15; 1 Kor. 2:12) bado kati katika muktadha ya Roho Mtakatifu hasa inataja. Nyingi za fasiri za kisasa zina "roho..." (yaani matoleo ya, KJV, ASV, NKJV, NASB, RSV, NRSV, NEB, REB na NIV). Hatahivyo, wengine wanadhani Roho Mtakatifu anarejerewa hapa (kama vile TEV, NJB na fasiri za William za Agano Jipya). Kwa kusema ukweli inaweza kuwa utata wa kimakusudi (kama vile NEB na NJB).

Mungu amempatia kila mwamini kipawa kikubwa, kama ilivyo pia karama za Roho kwa ajili ya huduma lakini pia jasiri na shauku yenye nguvu kutumikia kushirikiana kwenda kufanana na Kristo.

Robert Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, lina mjadala mzuri wa matumizi ya neno "roho" katika Agano Jipya (kurasa. 61-63).

1. roho wachafu
2. roho ya mwanadamu
3. Roho Mtakatifu
4. vitu kwamba Roho inayozalishwa na kwa kupitia roho za kibinadamu
   a. "sio roho ya utumwa" dhidi "roho ya uasilishaji," Rum. 8:15
   b. "roho ya upole," 1 Kor. 4:21
   c. "roho ya imani," 2 Kor. 4:13
   d. "roho ya hekima na ufunuo katika maarifa Yake," Efe. 1:17
   e. "sio roho ya woga" dhidi "nguvu, upendo na nidhamu," 2 Tim. 1:17
   f. "roho ya kukosea" dhidi ya "roho ya kweli," 1 Yohana 4:6

**NASB, NJB** **"roho ya hofu"**
**NKJV** **"roho ya hofu"**
**NRSV** **"roho ya kuogopa"**
**TEV** **"Roho. . .hatufanyi kuwa waoga"**

Kuna eneo moja hasi na vipengele vitatu vya karama ya Mungu.

**NASB** **"nidhamu"**
**NKJV** **"ufahamu mwema"**
**NRSV** **"nidhamu binafsi"**
**TEV, NJB** **"kiasi"**

Angalia dokezo kamili katika 1 Tim. 3:2.

**1:8-14** Hii ni sentensi moja ya Kiyunani.

**1:8 "haya"** Huu ni ufunguo wa msingi katika sura hii ya kwanza (kama vile 2 Tim. 1:8,12,16; pia dokezo Marko 8:38; Rum. 1:16). Huu ni muundo wa kisarufi ni KAULI TENDWA TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU (yenye ushahidi); haijalishi kwamba Timotheo alikuwa na aibu lakini baada ya maonyo asianze kuwa na aibu.

Paulo anaweza kuwa angeelezea dhana ya Agano la Kale la dhambi likileta matatizo na haki kuleta baraka (kama vile Kumb. 27-28; Ayubu, Zab. 73). Paulo hakuwa anateseka kwa ajili ya dhambi bali kwa ajili ya Kristo.

◙**"ushuhuda wa Bwana wetu wala mimi mfungwa Wake"** Paulo alimuonya Timotheo kuendelea kuhubiri mateso ya Kristo (kama vile Mwa. 3:15; Isa. 53; Mdo. 3:18; 26:23) na pia kutambua pamoja na Paulo kama mfungwa wa kiroho wa injili na mfungwa wa mwili! Hubiri habari njema licha ya gharama au madhara (kama vile Gal. 4:17; 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:23-29)!

◙**"ukijiunga pamoja nami"** Kwasababu ya thiolojia ya Paulo juu ya waamini karibu na utambulisho pamoja na (kama vile Rum. 6; Gal. 2:20) na kuteseka (kama vile Rum. 8:17; 2 Kor. 1:5; Flp. 3:10; pia katika 1 Pet. 4:13), Paulo mara kwa mara KIELEZI *syn* ambayo inamaanisha "Ushirika katika ushirikiano."

1. kuteseka na (1:8 na 2:3)
2. kufa na (2:11)
3. kuishi pamoja na (2:11)
4. kutawala na (2:12)

◙**"mateso ya injili"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU (kama vile 2 Tim. 2:3, 9; 4:5; Rum. 8:17; 1 Pet. 3:14; 4:12-19). Tungo ya msingi ni "kwa ajili ya injili," sio kwa uovu wetu wenyewe (kama vile. 1 Pet. 2:15-16). Wakristo wa sasa lazima watambue kwamba Mateso kwa ajili ya Injili ni utaratibu wala haina

mjadala wala kukwepa (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-2; 17:14; Mdo. 14:22; Rum. 5:3-4; 2 Kor. 4:16-18; 6:4-10; 11:23-28; Flp. 1:29; 1 Thes. 3:3; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4).

## MADA MAALUM: KWANINI WAKRISTO WANATESEKA?

1. kwasababu ya dhambi binafsi (hukumu ya muda). Hii haimaanishi kwamba matatizo yote na mazingira magumu ni matokeo ya dhambi (kama vile Ayubu; Zaburi 73; Luka 14:1-5; Nehemia 9; Yohana 9; Mdo. 5:1-11; 1 Kor. 11:29-30; Gal. 6:7).
2. Kukuza hali ya kufanana na Kristo (Ebr. 5:8). Hata Yesu, ukizungumza kibinadamu alitakiwa akomae na ndivyo inavyowapasa wafuasi wake (kama vile Rum. 5:3-4, 8:28-29; 2 Kor. 12:7-10; Flp. 3:10; Ebr. 12:5-12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 1:7).
3. Kukuza ushuhuda wenye nguvu na wenye uhalisia (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-22; 1 Pet. 2:18-21, 3:13-17).
4. Kama ishara ya kuzaa kwa uchungu kwa Zama mpya (kama vile Mt. 24:6; Marko 13:8).

Vitabu viwili ambavyo vimenisaidia mimi kushughulikia kutokuwepo na usawa na uovu wa ulimwengu ulioanguka ni Hannah Whithall Smith, *The Christian's Secret of a Happy Life* na John W. Wenham, *The Goodness of God.*

Mwamini lazima akumbuke kwamba matatizo na mateso sio kwamba ni ishara ya hasira ya Mungu au kukataliwa. Vitu vibaya hutokea kwa wafuasi waamiifu katika ulimwengu ulioanguka(kama vile. 1 Pet. 4:12-19). Ahadi za Mungu na kujitoa kwa Kristo ni ishara za upendo wa Mungu (kamavile Rum. 5:8). Maandiko lazima yachukue nafasi juu ya hali za muda!

**1:9 "aliyetuokoa sisi na kutuita"** Hizi ni KAULI TENDAJI ENDELEVU ZA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU mbili zinazounganishwa na "na" (*kai*). Katika Rum. 8:29-30 ule "wito" unakuja kabla ya "kuokoa," ikirejerea utawala wa Mungu (uchaguzi), lakini hapa wito unarejerea kwa huduma (ikiwa na wito, kama vile 2 Tim. 1:6-8 na Mada Maalumu katika 2 Tim. 1:9).

Hii ni sawasawa na ufanano wa Agano Jipya kwa lugha ya kiagano ya Agano la Kale iliyotumiwa na Israeli. Waaminio katika Yesu ni watu wa agano wa Mungu.

## MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI VILIVYOTUMIKA )

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

**WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI TIMILIFU)**

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11(inajumuisha WAKATI TIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

**WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (TIMILIFU)**

- Waefeso 2:5,8

**WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPO)**

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

**WOKOVU KAMA UKAMILISHO UJAO (WAKATI UJAO katika NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)**

- Warumi 5:9, 10; 10:9,13

- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28
- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum 10:9-13),lakini hili lazima liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (kama vile Rum. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (kama vile 1Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu.Hili linaweza kuelezwa kama

1. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
2. Wokovu endelevu–utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
3. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

◙**"kwa wito mtakatifu"** Hii inaweza kurejerea kwa Mungu kama mtakatifu lakini yawezekana katika muktadha wa Mapenzi ya Mungu kwa watu watakatifu wa kiagano wa Mungu. Mapenzi ya Mungu siku zote yamekuwa kwa ajili ya watu wake "waliofanywa kwa sura yake" (kama vile Mwanzo 1:26-27) kuaksi Sura yake kwa ulimwengu (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6)! Kazi ya Masihi imerejeza sura ya Mungu iliyopotea katika uasi wa Adamu na Hawa katika Mwanzo 3. Lengo la Ukristo ni Kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:29; Gal. 4:19; Efe. 1:4).

## MADA MAALUMU: KUITWA

Siku zote Mungu anachukua uwezo wa kuanzisha jambo katika mwito, uchaguzi, na akiwatafuta waumini waje kwake (kama vile. Yohana 6:44,65; 15:16; 1 Kor. 1:1-2; Efe. 1:4-5,11). Neno "kuitwa" limetumika kwa maana nyingi za kithiolojia.

A. Katika Agano la Kale "uitaji wa jina" mara nyingi ulikuwa katika mazingira ya kuabudu (kama vile. Mwa. 4:26; 12:8; 21:33; 26:25; Kut. 34:5).
B. Wenye dhambi wanaitwa kwenye wokovu kwa neema ya Mungu (yaani., Kut. 34:6-7) kupitia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kwa kusadikishwa na Roho ((yaani., *klētos*, kama vile. Rum. 1:6-7; 9:24, ambayo kithiolojia inafanana na 1 Kor. 1:1-2 na 2 Tim. 1:9; 2 Petr. 1:10).
C. Wenye dhambi wanaliitia jina la Bwana ili waokolewe (yaani., *epikaleō*, kama vile. Mdo. 2:21; 22:16; Rum. 10:9-13). Maelezo haya ni nahahu ya Kiyahudi katika taratibu za kuabudu.
D. Waumini huliita jina lake nyakati za migogora na msongo wa mawazo (yaani., Mdo.7:59).
E. Waumini wameitwa kuishi maisha yanayomfanana Yesu i.e., *klēsis*, kama vile. 1 Kor. 1:26; 7:20; Efe. 4:1; Fil. 3:14; 2 Thes. 1:11; 2 Tim. 1:9).

Waumini wameitwa kwenye kazi ya huduma (kama vile. Mdo. 13:2; 1 Kor. 12:4-7; Efe. 4:1).

◙**"sio kwa kadiri ya matendo yetu"** Hii ilikuwa pointi kubwa ya mahubiri Paulo kwa watu wa dini ya Kiyahudi wa Mdo. 15 na kitabu cha Wagalatia. Walimu wa uongo wa Barua za kichungaji pia wana mtazamo wa Kiyahudi wa na tendo kusaidia kuhesabia haki. Katazo hili la matendo kupatia haki ni maudhui yanayojirudia rudia katika maandiko ya Paulo (kama vile Rum. 3:20; 27-28; 4:4-5; 8; 9:11; Gal. 2:16; 3:11; Efe. 2:8-9; Flp. 3:9; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5).

◙**"kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema"** Mapenzi ya Mungu na tabia haviwezi kutenganishwa. Amefanya kwa niaba ya mwanadamu aliyeanguka akijikita kwa Yeye alivyo (kama vile Efe. 1:4-5, 11). Injili inaaksi moyo wa Baba, matendo ya Mwana mpendwa na nguvu ya Roho. Wokovu lilikuwa ni wazo la Mungu, uanzishwaji wake ni Mungu na mtoaji ni Mungu!

◙**"Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele"** Injili haikuwa "mpango B." Siku zote ilikuwa mpango wa Mungu kumkomboa mwanadamu aliyefanywa kwa sura na mfano Wake na ulifanywa kwa ajili ya mahusiano na Yeye. Kama Mwanzo 3 inavyoandika juu ya uasi wa mwanadamu, pia inaandika ahadi za Mungu na mpango (Mwa. 3:15; Rum. 16:25-26; Efe. 2:11-3:13, angalia Mada maalum katika 1 Tim. 4:10).

Huu mpango uliopangwa hapo kabla kupitia Kristo mara kwa mara unarejerea katika mahubiri ya Mitume katika Mdo. (kama vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29 na kama pia maneno yake Yesu mwenyewe katika Marko 10:45; Luka 22:20). Yawezekana inaelezewa katika Tito 1:2 (angalia Mada Maalum: Umilele katika Tito 1:2) na Ufu. 13:8.

Israeli ilikuwa ni hatua ya kwanza tu katika mipango ya Mungu juu ya ulimwengu kufanya ukombozi (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5-6). Masihi siku zote amekuwa ni tumaini pekee kwa mwanadamu mdhambi!

**1:10 "kwa kufunuliwa kwake"** Neno *epiphany (kudhihirishwa katika mwili)* hapa kunarejerea kuja kwa Kristo kwa mara ya Kwanza (kama vile 1 Tim. 6:14; Tito 2:11), lakini katika 2 Tim. 4:1 na Tito 2:13 neno hilo hilo linatumika juu ya Ujio wake wa Mara ya Pili. Angalia Mada Maalum: Misamiati ya Agano Jipya kwa Kurudi kwa Kristo katika Tito 2:13.

◙**"mwokozi wetu Kristo Yesu"** Mwokozi ni cheo cha Agano la Kale la YHWH (kama vile Zab. 106:21; Isa. 43:3,11,15,21; 49:26; 60:16; 63:8; Hos. 13:4; Luka 1:47). Katika Agano Jipya inaweka sifa kwa Yesu kama Masihi wa Mungu (kama vile Luka 2:11; Yohana 4:42; 13:23; Efe. 5:23; Flp. 3:20; 1 Yohana 4:14).

Ni katika Barua za Kichungaji tu vyeo vyote viwili vinatumika kwa ukaribu sana kwa wote Mungu Baba na Mungu Mwana.

A. Mungu
   1. Mungu mwokozi wetu (1 Tim. 1:1)
   2. Mungu mwokozi wetu (1 Tim. 2:3)
   3. mwokozi wa wanadamu wote (1 Tim. 4:10)
   4. Mungu mwokozi (Tito 1:3)
   5. Mungu mwokozi (Tito 2:10)
   6. Mungu mwokozi (Tito 3:4)

B. Kristo
   1. mwokozi wetu (2 Tim. 1:10)
   2. Bwana Yesu Kristo mwokozi wetu (Tito 1:4)
   3. Mungu wetu mkubwa na Mwokozi, Kristo Yesu (Tito 2:13)
   4. Yesu Kristo mwokozi wetu (Tito 3:6)
   5. Bwana wetu na mwokozi Yesu Kristo (1 Pet.1:11)
   6. Bwana na Mwokozi Yesu Kristo (2 Pet. 2:20)
   7. Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo (2 Pet. 3:18)

Barua za Kichungaji zilizoandikwa kati kati ya miaka ya mwishoni mwa miaka ya sitini zilikuwa pia mrejesho dhidi ya madai ya Mfalme wa Rumi kuwa vyote Mungu na mkombozi (na pia matumizi ya vyeo hivi katika dini za siri). Kwa Wakristo majina haya yalikuwa yanawekwa akiba kwa ajili ya YHWH na Masihi Wake.

◙**"aliyeibatili mauti"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: BATILI NA UTUPU (*katargeō*)

Hili neno (*katargeō*) lilikuwa ni moja ya maneno pendwa ya Paulo. Aliyatumia takribani mara ishirini na tano lakini lilikuwa na utofauti mpana.

A. Mzizi wa kiasili wa neno unatoka kwenye neno *argos* linalo maanisha
   1. Isio tendaji
   2. Isio na kazi
   3. Isiotumika

4. Isiofaa
5. Isiofanya kazi

B. Neno ambani likiwa na *kata* lilitumika kuelezea
1. Isiofanya kazi
2. Isiofaa kabisa
3. Iliyo imebatilishwa
4. Lililofanyikia mbali
5. Ambalo lilikuwa halifanyi kazi kabisa

C. Limetumika mara moja tu katika Luka kuelezea lisilozaa matunda, kwa hiyo ni mti usiofaa(kama vile. Lk 13:7)

D. Paulo analitumia kwa maana ya kitamathari kwa njia mbili za msingi
1. Mungu anafanya vitu visivyotumuka ambavyo havina faida kwa mwanadamu
   a. Asili ya dhambi ya mwanadamu-Rum. 6:6
   b. Sheria za Musa ukilinganisha na ahadi ya Mungu ya “mbegu”-Rum. 4:14; 3:17;5:4,11; Efe. 2:15
   c. Nguvu za kiroho-1 Kor. 15:24
   d. “Mtu asiye wa sheria”-2 The. 2:8
   e. Mauti ya mwili– 1 Kor. 15:26; 2 Tim. 1:10 (Ebr. 2:14)
2. Mungu anaweka ktu kingine cha zamani (Agano, zama) kwa kipya
   a. Vitu vinavyohusiana na sheria za Musa – Rum. 3:3,31; 4:14; 2 Kor. 3:7,11,13,14
   b. Mshabihiano wa ndoa uliotumia sheria – Rum. 7:2,6
   c. Mambo ya zama hizi – 1 Kor. 13:8,10,11
   d. Mwili huu – 1 Kor. 6:13
   e. Viongozi wa zama hizi – 1 Kor. 1:28; 2:6

Neno hili linatafasiliwa kwa njia mbali mbali, lakini maana yake kuu ni kukifanya kitu kisichofaa, batili na utupu, kisichofanya kazi, kisicho na nguvu, lakini sio muhimu kuwa hakiishi, kilichoharibiwa au angamizwa

◙**"na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili;"** Neno "uzima" limetumika mara kadhaa katika barua za Kichungaji na linaweza kumaanisha
1. uzima wa milele (1 Tim. 1:16; 6:12; Tito 1:2; 3:7)
2. uzima wa kweli (1 Tim. 6:19)
3. uzima wa sasa na maisha ya enzi ijayo (1 Tim. 4:8)
4. ahadi ya uzima katika Kristo (2 Tim. 1:1)
5. uzima na kutokufa kupitia Kristo (2 Tim. 1:10)

Kuna maneno mawili yanayoendana yanayotumika katika Barua za Kichungaji kuelezea zama mpya za uzima zisizo na ukomo:
1. "yenye uharibifu" ikiwa na KIBAINISHI HASI (2 Tim. 1:10; Tito 2:7; Rum. 2:7; 1 Kor. 15:52-54)
2. "mauti" ikiwa na KIBAINISHI HASI (1 Tim. 6:16 na 1 Kor. 15:53-54)

Hii sio dhana ya Kiyunani ya kila mwanadamu kuwa na sifa ya "nafsi" iliyokuwepo hapo kabla na isiyokufa. Hali ya kutokufa ya waamini inaanza na imani yao ya toba katika Kristo. Mungu ni chanzo pekee cha kutokufa roho (kama vile 1 Tim. 1:17; 6:16). Anatoa bure kupitia Kristo (na Kristo pekee).

◙**"kwa ile Injili"** Neno hili la Kiyunani kwa asili lilimaanisha "thawabu kwa ajili ya kuleta habari njema." Ilikuja kipekee kurejerea kwa upekee ndani ya Kristo juu ya ujumbe wa wa ajabu wa msamaha na ukubalifu kupitia maisha ya Yesu, mafundisho, kifo na ufufuo. Baadaye lilifanyika kuwa neno litumikalo kuelezea vitabu juu ya maisha ya Yesu (yaani Injili nne). Yesu ni habari njema ya upendo wa Mungu na mpaji kwa ajili ya dhambi.

**1:11 "ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Katika mstari huu Paulo anaelezea kipawa chake alichopewa na Mungu na majukumu yanayohusiana na injili (kama vile 1 Tim. 2:7).

◙**"muhubiri"** Hii sio sana kama kipawa kama ilivyo jukumu (kama vile TEV). Kuhubiri hakujawahi kutajwa kama kipawa lakini katika namna ni kipengele muhimu cha karama za viongozi wote (kama vile Efe. 4:11), ambazo zote zinajumuisha tangazo. Hii NOMINO inatoka kutoka KITENZI *kērussō,* ambayo ilimaanisha kwa umma kutangaza au kutoa tangazo. Ilikuja kuwa namna ya kiufundi kama njia ya kurejere mahubiri ya Kitume (*kērygma*) hasa kama inavyotokea katika mahubiri yaliyoandikwa ya Petro na Paulo katika kitabu cha Mdo. Angalia Mada Maalum: Mafundisho ya kanisa la kwanza katika 2 Tim. 3:15.

◙**"mtume"** "Mtume" inatoka kutoka moja ya neno la Kiyunani "kutumwa" (*apostellō*). Yesu alichagua kumi na mbili ya wanafunzi Wake kuwa pamoja naye kwa namna maalum na kuwaita "Mitume" (kama vile Luka 6:13). Ule muundo wa KITENZI inatumika mara kwa mara kwa Yesu akitumwa kutoka kwa Baba (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34; 5:24,30,36,37,38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,3,18,21,23,25; 20:21). Katika vyanzo vya Kiyunani, neno lilitumika na mtu aliyetumwa kama mwakilishi maalum wa mwingine ambaye ni sawa na "balozi."

Neno hili lilikuwa maana maalumu ya kimamlaka. Ilitumika na wale waliojua Kristo wakati maisha yake ya kimwili na huduma (kama vile Mdo. 1:21-26). Paulo alidai kwamba yeye pia yeye pia alikuwa amemuona Bwana katika maono ya Dameski na wito (kama vile Mdo. 9). Watu hawa kipekee waliitwa na kuwezeshwa na Roho kuandikwa na kuelezea matukio, mafundisho na miujiza ya Yesu ya duniani.

Neno lilikuja kutumika juu ya karama inayoendelea katika kanisa (kama vile 1 Kor. 12:28; Efe. 4:11). Kazi hasa haijawahi kuwekwa bayana; inaweza kuwa kupanda kanisa katika maeneo mapya au uongozi wa kimkoa (kama vile Mdo. 14:4,14; 18:5; 1 Kor. 4:9; Gal. 1:19; Flp. 2:25; 1 The. 2:6).

◙**"mwalimu"** Hii inatajwa kama karama ya kiroho katika Mdo.13:1; Rum. 12:6-7; 1 Kor. 12:28; na Yakobo 3. Inaunganishwa pamoja na kipawa cha mchungaji katika Efe. 4:11 na 1 Tim. 3:2; 2 Tim. 2:24. Wakati ilipotumika kama karama iliyotenganishwa, inaweza kurejerea mafunzo ya waaminio katika mafundisho (kama vile 2 Tim. 2:15; 3:16-17).

Toleo la KJV na NKJV yameongeza neno "kwa mataifa." Hii haitokei katika maandiko ya Kiyunani א* na A, lakini inatokea katika MSS א [2], C, D, F, G, na maandiko mengine ya kale. Inatokea katika 1 Tim. 2:7 na yawezekana nyongeza ya waandishi wa kale. Toleo la UBS[4] inatoa ujumuishi wa alama ya "B" (karibia na hakika).

**1:12 "kwasababu hiyo nimepatikana na mateso haya"** Hii lazima ihusiane 2 Tim. 1:8. Paulo alijua gharama kibinafsi ya uongozi wa kiroho (kama vile 2 Kor. 4:7-12; 6:3-10; 11:24-28).

◙**"wala msitahayari"** Hii ni rejea ya maonyo ya Paulo kwa Timotheo 2 Tim. 1:8 na mstari wa 16. Matatizo ya Paulo walikuwa katika namna ushahidi wa mafanikio yake katika kutangaza injili (kama vile Gal. 6:17)!

◙**"kwa maana najua"** Tazama msisitizo upo katika uhusiano binafsi, sio mazingira.

◙**"niliyemwamini"** Hii KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU ambayo kibayana "nimeamini na kuendelea kuamini." Inarejerea kwa tajiriba ya wokovu wa Paulo njiani Dameski (kama vile Mdo. 9).

Kwa "kuamini" angalia Mada Maalum katika 1 Tim. 1:16.

◙**"na kusadiki"** Hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Inarejerea ujasiri katika Mungu hata kati kati ya dhiki na kufungwa ambayo alipitia.

## MADA MAALUM: DHAMANA YA MKRISTO

Dhamana ni (1) kweli ya kibiblia, (2) uzoefu wa imanai ya mwamini, na (3) uthibitisho wa mtindo wa maisha.

A. Misingi ya kibiblia ya dhamana ni
   1. Tabia za Mungu Baba na kusudi
      a. Kutoka 34:6-7 (tazama Mada Maalum: Tabia za Mungu wa Israeli)

b. Nehemia 9:17
c. Yohana 3:16; 10:28-29 (tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele)
d. Warumi 8:38-39
e. Waefeso 1:3-14; 2:5,8-9
f. Wafilipi 1:6
g. 2 Timotheo 1:12
h. 1 Petro 1:3-5

2. Kazi ya Mungu Mwana
   a. Maombi yake ya kikuhani, Yohana 17:9-24, hasa mst. wa 12; Waebrania 7-9
   b. Kujitoa kwake kama dhabihu (kama vile. Isa. 52:13-53:12)
      1) Marko 10:45
      2) 2 Wakorintho 5:21
      3) 1 Yohana 2:2; 4:9-10
   c. Kusihi kwake katika hali endelevu
      1) Warumi 8:34
      2) Waebrania 7:25
      3) 1 Yohana 2:1

3. Uwezesho wa Mungu Roho Mtakatifu
   a. Wito wake, Yohana 6:44,65
   b. Hatima yake
      1) 2 Wakorintho 1:22; 5:5
      2) Waefeso 1:13-14; 4:30
   c. Dhamana yake binafsi
      1) Warumi 8:16-17
      2) 1 Yohana 5:7-13

B. Umuhimu wa mwitikio wa kimaagano wa mwamini ni (angalia Mada Maalum: Agano)
1. Toba na imani ya mwanzo na endelevu (tazama Mada Maalum: Je! "Pokea," "Amini," "Kiri/Ungama," na "Kusihi" kunamaanisha nini?)
   a. Marko 1:15
   b. Yohana 1:12
   c. Matendo 3:16; 20:21
   d. Warumi 10:9-13
   e.
2. Kumbuka kwamba lengo la wakovu ni kumfanana Kristo
   a. Warumi 8:28-29
   b. 2 Wakorintho 3:18
   c. Wagalatia 4:19
   d. Waefeso 1:4; 2:10; 4:13
   e. 1 Wathesalonike
   f. 2 Wathesalonike 3:13; 4:3; 5:23
   g. Tito 2:14
   h. 1 Petro 1:15
3. kwa kukumbuka kwamba dhamana inakamilishwa na mtindo wa maisha
   a. Yokobo
   b. 1 Yohana
4. kwa kukumbuka kwamba dhamana inakamilishwa kwa imani thabiti na ustahimilivu (tazama Mada Maalum: Ustahimilivu)
   a. Marko 13:13

b. 1 Wakorintho 15:2
c. Waebrania 3:14; 4:14
d. 2 Petro 1:10
e. Yuda 1:20-21

◙**"aweza kukilinda"** Tungo "Anaweza" ni maelezo mazuri ya maelekezo (kama vile Rum. 16:25; Efe. 3:20 na Yuda 1:24). Mungu si kwamba anaweza lakini anawezekana kulinda ukiri wetu wa imani katika Kristo (kama vile 1 Pet. 1:4-5) na mtindo wetu wa uaminifu wa maisha! Sio tu ni wokovu ulioanzishwa na Mungu, Mungu alianzisha na hitimisho la tukio la Mungu lakini hivyo pia ni maisha ya Mkristo.

◙**"kile nilichokiweka amana kwake"** Mungu analinda ukiri wa waamini (kama vile 1 Pet. 1:4-5). Hatahivyo waaminio lazima walinde uwakili wao wa injili (angalia dokezo kamili katika 1 Tim. 1:18, kama vile 1 Tim. 6:20; 2 Tim. 1:14). Ukristo ni agano pamoja na faida na upendeleo lakini pamoja na hitaji na majukumu!

◙**"siku hiyo"** Hii ni njia ya Agano la Kale la kurejerea nyakati za mwisho (kama vile 2 Tim. 1:18). Agano la Kale kwa uwazi ulifunua uingiliaji wa hewa wa Mungu katika historia ya wanadamu. Hatahivyo kutoka katika ufunuo endelevu wa waamini wa Agano Jipya sasa wanajua kuna Kuja mara ya Pili, kuvaa mwili (uanzilishwaji wa Ufalme wa Mungu) na Ujio wa Pili (hitimisho la Ufalme wa Mungu).

## MADA MAALUM: SIKU HIYO

Kifungu, "siku hiyo" au "kwenye siku hiyo," ni namna ya manabii wa karne ya nane kuzungumzia juu ya ujirio wa Mungu (uwepo), kwa ajili ya hukumu na urejesho.

| **Hosea** | | **Amosi** | | **Mika** | |
|---|---|---|---|---|---|
| chanya | hasi | chanya | hasi | chanya | hasi |
| 1:11 | 1:5 | | 1:14(2) | | 2:4 |
| | 2:3 | | 2:16 | | 3:6 |
| 2:15 | | | 3:14 | 4:6 | |
| 2:16 | 4:5 | | 5:18 (2) | | 5:10 |
| 2:18 | 5:9 | | 5:20 | | 7:4 |
| 2:21 | 6:2 | | 6:3 | 7:11(2) | |
| | 7:5 | | 8:3 | 7:12 | |
| | 9:5 | 9:11 | 8:9 (2) | | |
| | 10:14 | | 8:10 | | |
| | | | 8:13 | | |

Kipengere hiki kiuhalisia kinazungumzia juu ya manabii. Mungu anakwenda kutenda dhidi ya dhambi kwa wakati, lakini pia hutoa siku toba na msamaha kwa wale wanaopenda kubadili mioyo na matendo yao (yaani., kupokea roho mpya, mawazo mapya, na roho mpya, kama vile Ezek. 36:22-27)! Kusudi la Mungu la ukombozi na urejesho utatimilizwa! Atakuwa na watu watakaoaksi tabia Zake. Kusudi la uumbaji (ushirika kati ya Mungu na mwanadamu) utatimilizwa!

**1:13**
**NASB** **"kuendelea kushikilia"**
**NKJV** **"kushikilia"**
**NRSV** **"kushikilia"**

**TEV** **"kushikilia"**
**NJB** **"kutunza"**

Hii imezoeleka sana "Nina" (*echō*), lakini lina uwanja mpana wa kimaana kaka fasiri zinavyooneshwa. Muundo ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Timotheo lazima aendelee kug'ag'ania ukweli wa kitume uliowekwa kwake na Paulo (kama vile 2 Tim. 1:14; Tito 1:9).

◙**"kielelezo"** Neno "ya kati" (inayojulikana)" katika Kiyunani ilimaanisha "kuchora" na alikuwa mchoro wa mchoraji (yaani mchoro). Paulo alikuwa amempatia Timotheo mpango wote mzima wa Kithiolojia.

◙**"maneno ya uzima"** Hii ni mada inayojitokeza katika barua za Kichungaji ambayo itarejerea kwa mafundisho yenye afya (kama vile 1 Tim. 1:10; 4:6; 6:3; 2 Tim. 1:13; 4:3,4; Tito 1:9,13; 2:1,2). Mstari huu kibayana inaaksi uwepo na matatizo yaliyosababishwa na walimu wa uongo.

◙**"katika imani na upendo"** Hii inarejerea namna ambayo viongozi wanatakiwa kuwashikilia, kurithisha na kulinda ukweli wa Injili (kama vile 1 Wakorintho 13).

**1:14"ilinde ile amana kwa Roho Mtakatifu"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Tambua kwamba waamini lazima walinde, lakini Roho Mtakatifu ni namna na nguvu kwa kile ambacho kimefanywa!

◙**"akaaye ndani yetu"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Kuna sintofahamu kati ya kazi ya Roho na Mwana. G. Campbell Morgan anasema kwamba jina bora kwa Roho ni "Yesu mwingine." Ifuatayo ni ubainisho wa ulinganifu wa kazi na vyeo vya vya Mwana na Roho:

1. Roho anaita "Roho ya Yesu" au maelezo yanayofanana (kama vile Rum. 8:9; 1 Kor. 15:45; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).
2. wote wanaitwa kwa jina hilohilo
   a. "kweli"
      (1) Yesu (Yohana 14:6)
      (2) Roho (Yohana 14:17; 16:13)
   b. "wakili"
      (1) Yesu (1 Yohana 2:1)
      (2) Roho (Yohana 14:16; 16:7)
3. Wote waaminio wa ndani
   a. Yesu (Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17; Kol. 1:27)
   b. Roho (Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
   c. Baba (Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)

## MADA MAALUMU: UTU WA ROHO

Kwenye Agano la Kale "Roho wa Mungu" (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile. Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa "ambaye" (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)

8. Anaweza kupingwa (kama vile Matendo 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)
10. Humtukuza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Matendo 15:28
2. Rum. 8:26
3. 1 Kor. 12:11
4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu:Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

**NASB "hazina ambazo mmepewa kwenu"**
**NKJV "hicho kitu chema kilichowekwa kwenu"**
**NRSV "hazina njema ambazo nyie ni mawakili wake"**
**TEV "vitu vyema ambavyo vimewekwa kwenu"**
**NJB "hazina za thamani ambazo mmekabidhiwa"**

Hii inarejerea kwa utunzaji mwingine. Hii yawezekana ni mzaha juu ya neno *pistis*, ambalo linafasiriwa katika kingereza kama imani, tumaini na imani. Waamini wameaminishwa (angalia dokezo kamili katika 1 Tim. 1:18) imani yao kwa Mungu (kama vile 2 Tim. 1:12). Mungu badala yake ameawaaminisha kwa ujumbe wa injili (kama vile 1 Tim. 6:20). Waamini ni mawakili wa ujumbe wa injili. Siku moja tutatoa hesabu kwake Yeye (kama vile 2 Kor. 5:10) juu ya namna gani tunatunza na kutumia hazina hii ya ukweli!

## MADA MAALUM: MAFUNDISHO YA KICHUNGAJI

Kwa muda wa kuandikwa kwa mafundisho ya kichungaji (yaani, 1 Timotheo, Tito, 2 Timotheo) mnamo miaka ya 60 (Paulo alinyongwa mnamo mwaka 67 B.K), tayari katika namna ya kweli za injili zilikuwa zimekuzwa katika namna ya mafundisho. Tambua namna Paulo anavyorejerea kwenye hili "mafundisho yaliyokuzwa" (angalia Mada maalum: Mafundisho ya Kanisa la Kwanza), ambayo yalikuwa ulinzi wa kanisa dhidi ya walimu wa uongo.

1. "mafundisho yenye uzima"
   a. 1 Tim. 1:10
   b. 2 Tim. 4:3
   c. Tito 1:9; 2:1
2. "misemo ya kiuaminifu"
   a. 1 Tim. 1:15; 3:1; 4:8-9
   b. 2 Tim. 2:11-13
   c. Tito 1:9; 3:5-8
3. "mafundisho"
   a. 1 Tim. 4:16; 6:1
   b. 2 Tim. 3:10
   c. Tito 2:7

4. "mafundisho mazuri"
    a. 1 Tim. 4:6
5. "mafundisho ya utauwa"
    a. 1 Tim. 6:3
    b. Tito 1:1
6. "maneno ya uzima"
    a. 1 Tim. 6:3
    b. 2 Tim. 1:13
7. "kile mlichokabidhiwa"
    a. 1 Tim. 6:20
    b. 2 Tim. 1:12,14 (yaani, "amana njema")
8. "imani"
    a. 1 Tim. 1:5,19; 3:9,13; 4:1,6; 5:8; 6:10,12,21
    b. 2 Tim. 3:10; 4:7
    c. Tito 1:13; 2:2

Utungaji wa mafundisho ya injili lazima uwe wa
1. kuongozwa – 1 Tim. 6:20; 2 Tim. 1:14
2. kutunzwa – 2 Tim. 4:7
3. kushikiliwa kwa nguvu zote – Tito 1:9
4. ukabidhiwe kwa watu waaminifu – 2 Tim. 2:2

Waaminio wote wamekabidhiwa na injili (mafundisho). Lazima tuyalinde, tuyatunze na kuyarithisha!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 1:15-18**
**15 Waijua habari hii, ya kuwa wote walio wa Asia waliniepuka, ambao miongoni mwao wamo Figelo na Hermogene. 16 Bwana awape rehema wale walio wa mlango wake Onesiforo; maana mara nyingi aliniburudisha, wala hakuuonea haya mnyororo wangu; 17 bali, alipokuwapo hapa Rumi, alinitafuta kwa bidii akanipata. 18 Bwana na ampe kuona rehema machoni pa Bwana siku ile. Na jinsi alivyonihudumia kwa mengi huko Efeso, wewe unajua sana.**

**1:15 "walio wa Asia"** Hii ni utiaji chumvi. Paulo anasisitiza kwamba wengi zaidi walikuwa na hofu na waliacha ushirika nae.

◙**"waliniepuka"** Baadhi ya wasaidizi wa Paulo (kama vile 2 Tim. 4:10,16) walimuacha yeye katika kifungo (kama vile 2 Tim. 1:8,16) lakini sio lazima kuacha imani yao katika Kristo. Hii yawezekana ilihusiana na mashitaka yaya Paulo ya Kirumi.

◙**"Figelo na Hermogene"** Hakuna kinachojulikana juu ya Figelo au Hermogene.

**1:16-18** Mistari ya 16-18 ni maombi yaliyorefushwa (KAULI TENDAJI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU WA KIUCHAGUZI).

**1:16 "Onefilo"** Huyu ni mwamini mmoja na familia yake (au kanisa la nyumbani) ambaye hakumwacha Paulo (kama vile 2 Tim. 4:19). Katika namna zisizokuwa za kibayana sana (kihisia na kifedha) mtu huyu alimtia moyo Paulo wakati alipokuwa gerezani na pia alitoa mahitaji yote ya Kihuduma katika Efeso (kama vile 2 Tim. 1:18).

**1:18 "Bwana. . .Bwana"** Katika Kiebrania kuna utofauti ulio wazi kati ya YHWH (BWANA) na Adon (Bwana, kama vile Zab. 110:1). Katika Kiyunani yote yanatafsiriwa kama *kurios.* Inaonekana kwamba maombi haya yabnaelekezwa kwa Masihi na
kurejerea kwa "siku ya YHWH," Nahau/lahaja ya Agano la Kale (siku ya Baraka au hukumu). Angalia MADA MAALUM:MAJINA YA UUNGU katika 2 Tim. 1:2.

Hii inaonekana maka maombi ya ajabu kwetu sisi. Baadhi ya Wafasiri wamefikiria kwamba Onefiro alikuwa amekufa, ikiwa ndivyo haya ni maombi tu katika Biblia kwa niaba ya waliokufa. Paulo alikuwa anaomba kwamba Mungu aibariki "nyumba" (yaani familia au kanisa la nyumbani) kwasababu ya huduma yake ya uaminifu (kama vile Kumb. 7:9; 5:10 na dhana hiyo hiyo katika 1 Kor. 7:14).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je Paulo aliuona Ukristo kama imani tofauti ya Agano la Kale au mwendelezo wake??
2. Nini makusudi ya kuwekea mikono?
3. Orodhesha vitu vya muhimu kithiolojia katika 2 Tim. 1:9.
4. Je kwa namna gani Yesu alisababishiwa mauti?
5. Ni kwa namna gani neno "kulinda" linatumika kitofauti tofauti katika 2 Tim. 1:12 na 2 Tim. 1:14?
6. Kwanini wafanyakazi wenzake na Paulo walimtelekeza? Je hii inamaanisha kwamba walikuwa si waumini tena?

# 2 TIMOTHEO 2

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Askari Mzuri wa Kristo kuukabili | Kuwa na Nguvu katika Neema | Rufani ya Kuonyesha Kutiwa moyo | Askari Mwaminifu wa Kristo | Namna Timotheo Anavyopaswa<br><br>Ugumu |
| 2:1-7 | 2:1-13 | 2: 1-7 | 2: 1-7 | 2:1-2 |
| | | | | 2:3-7 |
| 2:8-13 | | 2:8-13 | 2:8-13 | 2:8-13 |
| Mtendakazi aliyekubaliwa | Watenda kazi asiokubaliwa na Wasiokubaliwa | Mchungaji na Kundi | Mtenda kazi Aliyekubaliwa | Mapambano dhidi hatari toka kwa Walimu waUongo |
| 2:14-26 | 2:14-26 | 2:14-19 | 2:14-19 | 2:14-18 |
| | | | | 2: 19 |
| | | 2:20-30:9 | 2:20-26 | 2:20-21 |
| | | | | 2:22-26 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 2:1-7**
**1 Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. 2 Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine. 3 Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. 4 Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari. 5 Hata mtu akishindana katika machezo hapewi taji, asiposhindana kwa halali. 6 Yampasa mkulima mwenye taabu ya kazi kuwa wa kwanza wa kupata fungu la**

**matunda. [7] Yafahamu sana hayo nisemayo, kwa maana Bwana atakupa akili katika mambo yote.**

**2:1 "Basi wewe"** Kifungu hiki kinaonekana kuhusiana na 2 Tim. 1:15-18, ambapo Paulo anawatofauisha wale waliomwacha panoja na wale walioendelea kuwa waaminifu.

◙ **"mwanangu"** Mazungunzo haya yanamrejelea Paulo kama baba wa Timotheo katika injili (kama vile 2 Tim. 1:2; 1 Tim. 1:2; Tito 1:4).

◙ **"uwe hodari"** Hiki weza kuwa

1. KAULI TENDWA SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, "endelea kuwa hodari" (*Word Pictures in the Greek New Testament* na A. T. Robertson; *A Grammatical Analysis of the Greek NT* na Zerwick na Grosvenor; na *Analytical Greek New Testament* na Barbara na Timothy Friberg)
2. KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO, "endelea kuwa hodari" (*The Analytical Greek Lexicon Revised* na Harold K. Moulton na the Charles B. Williams translation).

Je! mwamini anashiriki katika kuwezesha, au Mungu anafanya uwezesho? Huu ni mvutano kati ya ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya wanadamu. Katika Agano Jipya hivi vyote vinahusika katika wokovu na maisha ya Mkristo. Mungu hushughulika na mwanadamu aliyeanguka katika uhusiano na agano. Kuna vyote haki na majukunu, mahitaji na upendeleo! Neema (yaani., uanzilishi wa ki-Ungu) mara nyingi ni kipaumbele , bali jukumu la mwanadamu linatawaliwa!

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihirisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni “kukata/kuchinja”(BDB 144) ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano(kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahiri cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abrahamu (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israel toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika “agano jipya” (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3 N

2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini "agano jpya" (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10;). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio namna ya wokovu (yaani., Yakobo na Yohana. Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekana kwa wazi kwa katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi).

**2:2 "mambo yale uliyoyasikia kwangu"** Timotheo anapitia katika mafundisho ya kitume ya Paulo, si katika mawazo yake aua nadharia zake (kama vile 2 Tim. 1:13, tazama Mada Maalum katika 2 Tim. 1:14).

◙ **"mbele ya mashahidi wengu"** Kifungu hiki kinaweza kumaanisha

1. mwan zo wa kuhubiri kwa Timotheo (kama vile 2 Tim. 1:6; 1 Tim. 4:14)
2. Timotheo alichokisikia Paulo akikifundisha pia alikithibitisha kwa manabii/walimu wengine/
3. Timotheo alimsikia Paulo akihubiri/akifundisha kweli ile ile mara nyingi

◙ **"hayo uwakabidhi"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Hili ni neno ni sawa na lile lililotumika katika 2 Tim. 1:12,14 na 1 Tim. 1:18.T azama maelezo katika 2 Tim. 1:12 na 1 Tim. 1:18.

**NASB, NKJV "watu waaminifu"**
**NRSV "kwa watu waaminifu"**
**TEV, NJB "kwa watu wenye kuaminika"**

Hii nahau ya Kiyunani *pistis* inayotafsiriwa katika lugha ya Kiingereza kama"imani,"amini" au "sadiki." Hapa inatumika kama KIVUMISHI, *pistos*, katika Agano la Kale katika maana ya wenye kusadikika, waaminifu, wenye kutumainika viongozi muhimu wa kanisa wenye kuona mbali. Hii ni kanuni ya kuachia madalaka na kugawa nadalaka. Yesu aliutumia muda wake katika kuwachagua wachache ili wawafikie wengi kupitia kwao. Vitabu viwili vyenye kushangaza sana ambavyo vinaipanua nadharia hii ni *The Master Plan of Evangelism* na *The Maser Plan of Discipleship*, vyote vimeandikwa na Robert E. Coleman.

◙ **"watakaofaa"** Wahubiri /walimu wenye ujuzi/wenye uzoefu wa Kikristo wanatokana na

1. Mungu mwenyewe, kama vile 2 Kor. 2:17; 3:5-6
2. kuipokea/kuiamini kwao ile kweli ya Kitume

Uzoefu hautokani na akili ya mtu au elimu au mtu alivyo. Yatupasa kuwa wanenaji waaminifu wa neno/kweli ya Mungu!

**2:3 "Ushiriki taabu pamoja nami"** HII NI KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Hii imekuwa ni dhima ya mara kwa mara (kama vile 2 Tim. 1:8,12; 2:3,9; 4:5). Tazama maelezo kamili katika 2 Tim. 1:8. Mara nyingi huduma husababisha mapambano toka kwa ndugu aliyepotea, mamlaka ya kiraia au tamaduni.

◙ **"kama askari mwema"** Mara nyingi Paulo anayatolea ufafanuzi maisha ya Mkristo kwa kutumia stiari za mapigano (kama vile 4) au mashindano (kama vile mst. wa 3) (kama vile Rum. 13:12; 2 Kor. 6:7; 9:7; 10:4; Efe. 6:11-17; Fil. 2:25; Filemoni 2; 1 Tim. 1:18; 6:12; 2 Tim. 4:7).

**2:4 "Hakuna apigaye vita . . . ajitiaye katika shughuli za dunia . . .mkulima"** Paulo anaitumia mifano mitatu yenye kuhusiana na kazi ili kueleza juu ya kumtia moyo Timotheo.

◙ **"ajitiaye katika shughuli za dunia"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO yenye kusistiza matendo endelevu kwa upande wa kiima. Si kwamba mambo yasiyo ya kiroho ni mabaya, hayawezi kuwa kipaumbele au hatima (kama ile 2 Pet. 2:20). Viongozi lazima waushikilie mtazamo wa huduma!

**2:5 "akishindana"** Hii ni SENTENSI AMRISHI DALAJA LA KWANZA yenye kuzungumzia tendo lenye umuhimu.

◙ **"asiposhindana kwa halali"** Kifungu hiki kinatumika kumaanisha ubingwa, riadha za wakati wote. Ikiwa mshindani atajiondoa katika sheria, huyo hatafaa (kama vile 1 Kor. 9:24-27).

**2:6 "mkulima mwenye taabu ya kazi"** Paulo anaitumia mifano mitatu ya juhudi za ubingwa

1. ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari
2. mtu akishindana katika machezo hapewi taji
3. mkulima mwenye taabu ya kazi kuwa wa kwanza wa kupata fungu la matunda

Haya yote yanahusisha moyo wa kujituma, juhudi, uvumilivu ma mateso! Wote hawa hupokea thawabu zao kulingana na haya (kama vile Mit. 27:18).

**2:7 "Yafahamu sana hayo nisemayo"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye kumaanisha "kuendelea kufikiri juu ya jambo hili kwa umakini." Utambue ubunifu endelevu kati ya jukumu la mwanadamu na utoaji wa Mungu wa neema.

◙ **"Bwana atakupa akili katika mambo yote"** Bwana, kwa maana ya Roho Mtakatifu, atawapa uelewa watu wake (kama vile Yohana 14:16; 16:13). Hili linaweza kuakisi Agano Jipya la Yer. 31:31-34 (hasa 2 Tim. 2:33-34).

Kwa hakika hili halirejelei hali maalum, maarifa kamili katika kila eneo la maisha, bali maarifa timilifu na kamili ya injili na maana zake. Roho huwapa waamini maarifa yote wanayoyahitaji kwa ajili ya kuishi maisha ya kumpendeza Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 2:8-13**

**[8] Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu, wa uzao wa Daudi kama inenavyo injili yangu. [9] Nami katika hiyo nimeteswa hata kufungwa kama mtenda mabaya; lakini neno la Mungu halifungwi. [10] Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule, ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele. [11] Ni neno la kuaminiwa. Kwa maana, Kama tukifa pamoja naye, tutaishi pamoja naye pia; [12] Kama tukistahimili, tutamiliki pamoja naye; tutamiliki pamoja naye, yeye naye atatukana sisi; [13] Kama sisi hatuamini, yeye hudumu wa kuaminiwa. Kwa maana hawezi kujikana mwenyewe.**

**2:8 "Mkumbuke"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Paulo anamkumbusha Timotheo mara nyingi (kama vile 2 Tim. 1:3,4,5,6; 2:8,14). Hili ni tukio maalum lenye kusistiza mafundisho yanayohusiana na thiolojia ya Kikristo inayohusiana na Kristo.

◙ **"Yesu Kristo, aliyefufuka katika wafu"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU yenye kumaanisha kwamba Yesu alifufuliwa na Baba na ya kwamba yeye alibaki akiwa mfufuliwa. Ufufuo wa Yesu ilikuwa ishara kwamba aliikubali kwa ukamilifu kazi aliyoifanya Mwana duniani, mafundisho na shabihi kwa ajili ya dhambi. Ufufuo wa Yesu ni moja ya kiini cha nguzo ya Ukristo (kama vile 1 Kor. 15).

Ufufuo wa Yesu pia ni sehemu muhimu ya mahubiri ya kwanza (*kerygma*, tazama Mada Maalum katika 2 Tim. 3:15) ya Petro na Paulo katika Matendo, yenye kuonyesha kweli kuu za injili zilizo rudiwa rudiwa katika kanisa la mwanzo:

1. yampasa Masihi kuteswa
2. Yesu aliukamilisha unabii wa Agano la Kale
3. enzi mpya za Roho zimekuja katika Yesu
4. Yesus alikufa kwa ajili ya dhambi, ambao ndio mpango wa Mungu uliokuwa uekusudiwa
5. Yesu alifufuliwa katika wafu na kukaa mkono wa kuume wa Mungu
6. Yesu atakuja tena
7. Ye yote atakayemwabudu katika toba na imani ataokolewa

Tanbihi (2,d) kuhusiana na ukurasa wa 365 wa Jerusalem Bible (1966) inatengeneza maelzo mazuri, "fikra za Kiyunani zinazopatikana katika ufufuo hasa zenye kukubaliwa, Matedo 17:37; 1 Kor. 15:12."

**2:9 "nimeteswa"** Hii ilikuwa tabia ya kuhubiri injili katika karne ya kwanza. Paulo alifahamu kuwa itakuwa hivyo na atamwita Timotheo ili aungane naye (kama vile 2 Tim. 1:8; 2:3; 4:5).

◙ **"hata kufungwa kama mtenda mabaya"** Paulo alitiwa gerezani kwa sababu ya kuhubiri injili na alitarajia kukatwa kichwa punde (kama vile 2 Tim. 4:6). Kumtumikia Mungu katika ulimwengu ulioanguka inagharimu (kama vile 2 Kor. 4:7-15; 6:1-10; 11:23-30)!

◙ **"lakini neno la Mungu halifungwi"** Nimelipa jina toleo hili "Paul Bound, but the Gospel Unbound" kutokana na mstari huu. Ukinya wetu pekee ndiyo ututiao gerezani "neno la Mungu"!

◙ **"wa uzao wa Daudi "** Kifungu hiki kinauzungumzia utu wake wa kweli (kama vile Mt. 1:1; Rum. 1:3) na utimilifu wa unabii (kama vile 2 Sam. 7:14 na kuendelea).

◙ **"kama inenavyo injili yangu"** Haya ni maneno halisi ya Paulo yaliyo katika Rum. 2:16; 16:25. Kifungu hiki kinayarejelea mahubiri ya injili ya kitume.

**2:10 "nastahimili mambo yote"** Hii inamaanisha "kujitolea, kutenda, kudumu katika juhudi." Paulo anachagua kukaa chini ya huduna ya injili kwa ajili ya wengine.

◙ **"kwa ajili ya wateule "** Mungu anawaja waliyo wake (kama vile Tito 1:1; Ufu. 13:8). Kwa uwazi kabisa kifungu hiki kinawarejelea wale wote ambao waliohitikia a wale ambao hawakuihitikia (kama vile Rum. 11:25-26) injili.

◙ **"ili wao nao waupate wokovu ule"** Wokovu huu ni kupitia Kristo pekee na maisha ya milele (kama vile 1 The. 5:9; 2 The. 2:13-14).

◙ **"pamoja na utukufu wa milele"** Wokovu wa Agano Jipya unabainishwa na mbambo ambayo anaondolewa kwa mtu na anayopewa mtu.

A. Yanayoondolewa
   1. Dhambi
   2. Shetani na nguvu za kimapepo
   3. Makosa
   4. udanganyifu
B. Anayopewa
   1. amani ya sasa pamoja na Mungu
   2. makusudi katika maisha ya sasa
   3. karama kwa ajili ya huduma
   4. kujazwa roho na maisha ya sasa yenye kuongozwa naye
   5. utimilifu wa baadaye

6. makao ya baadaye huko mbinguni
7. utukufu wa baadaye pamoja na Kristo
8. kutwala baadaye pamoja na Kristo
9. Mwili wa baadaye kama ilivyo Kristo

◙ **"utukufu"** Utukufu huu unarejelea wokovu wa mwisho uitwao "kutukuzwa" katika Rum. 8:28-30. Tazama maelezo kamili katika 1 Tim. 1:17.

**2:11 "tukifa"** Hili ni neno la mwisho kati ya yale matano "semi za kusadiki" katika Nyaraka za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 1:15; 3:1; 4:9; Tito 3:8). Hili (2 Tim. 2:11-13) linaonekana kuwa nukuu kutoka katika kanuni ya imani au wimbo.

1. mtiririko wa vishazi "kama" (SENTENSI AMRISHI DALAJA LA KWANZA, kama vile 2 Tim. 2:11,12,13 mara mbili)
2. hivi viwili vya kwanza ni yakini; hivi viwili vya mwisho ni kanushi
3. vishazi vya tatu na vya nne vina mstari wa ziada

◙ **"tukifa pamoja naye "**Hii ni moja ya ambatani kadhaa wa neno *syn* katika 2 Timotheo. Hili linazungumzia stiari ya kibiblia ya ubatizo wa kuzamishwa (kama vile Rum. 6:1-11; Gal. 2:20). Huu muundo halisi unajitokeza hapa tu, katika Marko 14:31, na 2 Kor. 7:3.

◙ **"tutaishi pamoja naye pia"** Hili ni neno lingine ambatani *syn* ambatani lililo adimu (kama vile Rum. 6:8; 2 Kor. 7:3). Hili linarejelea jasiri wa waamini kujiamini kunakohusiana na uhusiano pamoja na Yesu, sasa si kwa imani tuu bali siku moja (na kwa kila siku) uso kwa uso**.**

Vishazi vya vitatu vya kwanza vya neno "kama" vyenye kuhitimisha katika VITENZI VYA WAKATI UJAO vyenye dhahanio la (yaani., wakati wa mwisho) muundo wa siku za mwisho. Agano Jipya lote lina kifungu hiki hiki tayari lakini bado kuna mvutano. Ufalme wa Mungu umekuja (umesimikwa) katika Yesu lakini umekamilishwa. Waamini wanakumbana vipengele vingi vya Ufalme huu sasa, bali wengine wamewekwa akiba kwa ajili ya Kuja Mara ya Pili.

◙ **"Kama tukistahimili"** Huu utunzi wa kisarufi (SENTENSI AMRISHI DALAJA LA KWANZA) unadhani kuwa waamini watastahimili.

## MADA MAALUMU: USTAHIMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Mashariki walielekea kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwitikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahusuyo uhakika
    a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
    b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
    c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)

2. maandiko yahusuyo umuhimu wa ustahimilivu
    a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
    b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
    c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
    d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
    e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kithiolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumika, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumika kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumiwa vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika Agano

Jipya 3:5

- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote ni vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

**2:12 "tutamiliki pamoja naye"** Hili ni neno lingine *syn* ambatani linalopatikana hapa na katika 1 Kor. 4:8. Paulo anaupenda sana uambatani huu. Muda, mahali, na washiriki hawajulikani.

## MADA MAALUM:KUTAWALA KATIKA UFALME WA MUNGU

Dhana ya kutawala tukiwa na Kristo ni sehemu ya namna kubwa ya kithiolojia inaitwa "ufalme wa Mungu." Huu ni mwito toka dhana ya Agano la Kale la Mungu Yeye kama Mfalme wa kweli wa Israel (kama vile 1 Sam.8:7). Kiishara anatawala (1 Sam. 8:7; 10:17-19) kupitia kizazi cha kabila la Yuda (kama vile Mwa. 49:10) na familia ya Yese (kama vile 2 Samwel 7).

Yesu ni ahadi ya utimilifu wa unabii wa Agano la kale kuhusiana na Masihi. Aliuanzisha Ufalme wa Mungu akiwa na mwili wa kibinadamu pale Bethlehemu. Ufalme wa Mungu ukaja kuwa ni nguzo kuu ya mafundisho ya Yesu. Ufalme wa Mungu ukawa kamili ndani yake (kama vile Mt. 10:7; 11:12; 12:28; Marko 1:15; Lk 10:9,11; 11:20; 16:16; 17:20-21).

Hata hivyo, ufalme ulikuwa wa wakati ujao (matukio ya siku za mwisho). Ulikuwepo lakini ukawa haujatimilizwa (kama vile. Mt. 6:10; 8:11; 16:28; 22:1-14; 26:29; Lk 9:27; 11:2; 13:29; 14:10-24; 22:16,18). Kwa mara ya kwanza Yesu akaja kama mtumwa mwenye mateso (kama vile. Isa. 52:13-53:12); mwenye kunyenyekea (kama vile. Zak. 9:9), bali atarudi kama Mfalme wa Wafalme (kama vile. Mt. 2:2; 21:5; 27:11-14). Dhana ya "kutawala" kwa uhakika ni sehemu ya "Ufalme" wa thiolojia. Mungu amekwisha kuwapatia ufalme wafuasi wa Kristo (angalia Lk 12:32).

Dhana ya kutawala pamoja na Kristo ina mitizamo mbali mbali pamoja na maswali

1. Je sura zile zinazodai kuwa Mungu amewapa waamini "ufalme" kupitia Kristo zinarejea juu ya "kutawala" (kama vile Mt. 5:3,10; Lk 12:32)?
2. Je maneno ya Yesu kwa wanafunzi wa mwanzo kwenye karne ya kwanza katika mazingira ya Kiyahudi yanarejea kwa waamini wote (kama vile. Mt. 19:28; Lk 22:28-30)?
3. Je misisitizo ya Paulo juu ya kutawala katika maisha haya ya sasa yanakinzana au yanawiana na maandiko ya hapo juu (kama vile. Rum. 5:17; 1 Kor. 4:8)?
4. Ni kwa namna gani mateso na utawala vinahusiana (kama vile. Rum. 8:17; 2 Tim. 2:11-12; 1 Pet. 4:13; Ufu. 1:9)?
5. Dhana ya kujirudia ya ufunuo unachangia pamoja utawala wa Yesu uliotukuzwa, lakini huo utawala wa
   a. Kidunia, Uf. 5:10
   b. Utawala wa miaka 1000, Uf. 20:4-6

Milele, Uf. 2:26; 3:21; 22:5 na Dan. 7:14,18,27.

◙ **"tutamiliki pamoja naye"** Hili ni onyo lenye nguvu (tazama MADA MAALUM:UKANAJI IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1)! Kumbuka hizi zilikuwa zama za mateso, unyanyasaji, na kifo (kama vile Mt. 10:32-33; Luka 9:26; 1 Tim. 5:8; Tito 1:16; 2 Pet. 2:1; Yuda 4).

**2:13 "Kama sisi hatuamini, yeye hudumu wa kuaminiwa"** Kifungu hiki kinashangaza sana. Bado amri ni ya DALAJA LA KWANZA (yenye kudhahaniwa kuwa ya kweli; mtu angetarajia kuwa hii ingekuwa DALAJA LA TATU (tendo lenye umuhmu).

Ni katika namna gani mwamini si mwaminifu? Je! hili linamaanisha

1. kusitasita chini ya mateso au jaribu
2. kuwafuata walimu wa uongo
3. maisha yasiyo yaki-Mungu

Kifungu hiki kinaweza kuakisi dhana ya Agano la Kale ya uaminifu wa Mungu katikati ya uaminifu endelevu juu ya Israeli (kama vile Mal. 3:6). Hatimaye tumaini la waamini li katika sifa na ahadi ya Mungu isiyobadilika. Uaminifu wa YHWH ni jina linalojieleza (Kumb. 7:9; Isa. 49:7; 1 Kor. 1:9; 10:13; 2 kor. 1:18; 1 The. 5:24; 2 The. 3:3) na sifa (Zab. 36:5; 40:10; 89:1,2,5,8; 92:2; 119:90; Ebr. 6:17-18; 1 Pet. 4:19) ambayo inafunuliwa kwa ukamilifu katika Krisro (Ebr. 6:13-20). Kwa sababu ya kuiacha imani (tazama Mada Maalum: Ukanaji wa Imani katika 1 Tim. 4:1) haumaanishi kwamba Mungu amewaacha (tazama MADA MAALUM: DHAMANA katika 2 Tim. 1:12)! Mapenzi huru ya matendo katika kila ngazi. Neema ya Mungu na uaminifu wake havihatarishwi kwa sababu ya walimu wa uongo na wafuasi wao wasio waaminifu!

◙ **"hatuamini, yeye hudumu wa kuaminiwa"** Hiki kinadai kwamba kama ilivyo sifa ya Mungu ya kutobadilika (yaani, Zab. 102:27; Mal. 3:6), ndivyo ilivyo, Yesu habadiliki (kama vile Ebr. 13:8). Ni asili ya Uungu isiyobadilika ya rehema ambayo ndiyo msingi wa tumaini lla waamini, ujasiri, na dhamana!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 2 : 14-19**
**[14] Uwakumbushe mambo hayo, ukiwaonya machoni pa Mungu, wasiwe na mashindano ya maneno, ambayo hayana faida, bali huwaharibu wasikiao. [15] Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli. [16] Jiepushe na maneno yasiyo na maana, ambayo si ya dini; kwa kuwa wataendelea zaidi katika maovu, [17] na neno lao litaenea kama donda-ndugu. Miongoni mwa hao wamo Himenayo na Fileto, [18] walioikosa ile kweli, wakisema ya kwamba kiyama imekwisha kuwapo, hata kuipindua imani ya watu kadha wa kadha. [19] Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii, Bwana awajua walio wake. Na tena, Kila alitajaye jina la Bwana na auache uovu.**

**2:14 "Uwakumbushe"** Hil ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Tazama maelezo katika 2 Tim. 1:3 kuhusu "uwakumbuke."

◙ **"mambo hayo"** Hili lingeweza kurejelea 2 Tim. 2:11-13 au 14-19. Walimu wa uongo wanabainishwa katika 2 Tim. 2:14, 16, na 23 kama walivyo katika 1 Tim. 1:4,6; 6:4,20.

**NASB "ukiwaonya machoni pa Mungu"**
**NKJV "ukiwaonya machoni pa Bwana"**
**TEV "waonye machoni pa Mungu"**
**NJB "waambie katika jina la Mungu Mungu"**

Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani kati ya "Mungu" (MSS א, C, F, G, I) na "Bwana" (MSS A, D). Matumizi ya kifungu kama hiki "Mungu" yanajitokeza katika 2 Tim. 4:1 na 1 Tim. 5:4,21 (tazama Metzger, uk. 647), kwa hiyo, *Theos* huenda ni halisi. Toleo la UBS[4] linakipa daraja "B" (kwa namna fulani ni yakini). Kama zilivyo nyingi tofauti hizi, hizi hazitengenezi tofauti ya kithiolojia.

Hili ni neno ambatani *dia* + *marturomai*, ambalo linamaanisha "wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso" (kama vile Luka 16:28; Matendo 2:40; 8:25; 10:42; 18:5; 20:21,24; 23:11; 28:23; 1 Tim. 5:21; 2 Tim. 2:14; 4:1).

Ilimpasa Timotheo kuyatumia mamlaka yake yote kama uwakilishi wa kiutume wa Paulo na Mzungumzaji wa Mungu kwa ajili ya kukabiliana na walimu wa uongo katika utauwa, si dhahanio (kama vile 2 Tim. 2:14-26).

◙ **"wasiwe na mashindano ya maneno"** Kulikuwa na sehemu ya mgawanyiko uliokuwepo (kama vile 2 Tim. 2:16; 1 Tim. 1:3-4; 4:7; 6:4,5,20; Tito 3:9).

Timotheo anatahadharishwa kutojihusishwa katika mazungumzo ya kithiolojia pamoja na walimu wa uongo kutokana sababu kadhaa.

1. hayakuwa na maana kwa sababu fikra zao zikuwa zimepotoka na kutiwa giza (kama vile 2 Tim. 2:14; 1 Tim. 4:2; 6:5; Tito 3:11)
2. yaliwasababisha waamini wengine waliyoyasikiliza kwa makini mazungumzo hayo kuanza kusitasita (kama vile 2 Tim. 2:14,18; 1 Tim. 6:20-21)
3. yalipelekea kukosekana kwa utauwa (kama vile 2 Tim. 2:16,19; 1 Tim. 6:3)
4. yalienea kama donda-ndugu (kama vile 2 Tim. 2:17)

◙ **"bali huwaharibu wasikiao"** "Uharibifu" ni neno la Kiyunani ambapo tunalipata neno la Kiingereza "machafuko." Kiuhalisia neno hili lilimaanisha "kupindua" (kama vile Pet. 2:6) au "akazipindua" (kama vile Mt. 21:12).

**2:15 "Jitahidi kujionyesha"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA KITENZIJINA CHA WAKATI USIO TIMILIFU. Huu ni wito wa tendo muhimu wa hiari (kama vile Rum. 6:13; Efe. 4:3).

◙ **"umekubaliwa"**Hili ni neno la kimetali ambalo linakuwa nahau ya "waliokubaliwa wawe dhahiri kwenu" stiari ya kuthibitisha kitu fulani kama ni halisi (kama vile 1 Kor. 11:19; 2 Kor. 10:18). Tazama Maalum: Maneno ya Kiyunani ya neno "Kujaribu" na Maana zake za Karibu katika 1 Tim. 6:9.

◙ **"na Mungu"** Mungu ndiye apasaye kuyakubali mafundisho yetu, nahubiri, na maisha yetu.

◙ **"mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari"** Toleo la Spiritless Bible inafundisha na maisha ya kila siku yasiyomfanana Kristo yatasababisha waamini kuona haya watakaposimama mbele za Bwana (kama vile 2 Kor. 5:10). Paulo alihofia kuahibishwa mbele za Bwana, bali mbele za wanadamu (kama vile 2 Tim. 1:8,12,16).

◙ **"ukitumia kwa halali"** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO lenye kumaanisha "unyoofu" Hili linapatikana hapa pekee katika Agano Jipya. Mara nyingi hili lilitumika katika kutenganisha kutengeneza barabara, kuchimba mtaro, au mwashi atengenezaye umbo fulani kwa kutumia jiwe (kama vile Mit. 3:6; 11:5 katika Agano la Kale la Kiebrania).

Hili neno linatumika kistiari kutembea kwa unyoofu. Neno la Mungu ni nyoofu (mwenye haki) huendana na kweli. Hilii neno "nyoofu" ni neno la utungaji wa Agano la Kale la neno "tete la mto" ambalo lilitumka kusimika kuta kwa wima, mitaa, n.k. YHWH alilitumia neno hili kuieleza sifa yake binafsi. Hili linatafsiriwa kama "sawa" au "haki" (na miundo yote inayohusiana, tazama Mada Maalum katika Tito 2:12). Mungu ni mwongozaji wa kweli au sawa ambapo kila kitu kinatambulikana kwake. Kweli ya kitume inaiakisi sifa ya Mungu; maisha ya kitume yanaiakisi sifa ya Mungu. Walimu wa uongo walishindwa katika yote!

◙ **"halali neno la kweli"** Katika Efe. 1:13; Kol. 1:5 na Yakobo 1:18 yanairejelea injili. Hapa kifungu hiki kinairejelea kweli ya ki- Kitume iliyofikishwa na Paulo na iliyofuatishwa na Timotheo na aliyokubaliwa na kufuatishwa na waaini waliokomaa. Kiabu kizuri chenye kufafanua vema mahubiri ya Kitume, kuhubiri na nyaraka katika Agano Jipya tazama *Birth of a New Testament* na William L. Bevins (Union Baptist University, Carson City, TN). Tazama Mada Maalum : Kweli katika Maandiko ya Paulo katika 1 Tim. 2:4.

**2:16 "Jiepushe na maneno yasiyo na maana"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hii ndiyo dhima kuu katika Nyaraka za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 6:20; Tito 3:9).

◙ **"wataendelea"** Waamini yawapasa kuwa wanyoofu katika haki na kweli (kama vile 2 Tim. 2:15) bali walimu wa uongo na wafuasi wao wanatengeneza njia zisizo za utauwa na udanganyifu (kama vile 2 Tim. 3:9,15).

**2:17**
**NASB, NRSV** **" neno lao litaenea kama donda-ndugu "**
**NKJV** **"ujumbe wao utakuwa kama kansa"**

**TEV** **"mafundisho kama hayo ni kama uchungu ulao"**
**NJB** **"maneno ya aina hii ueneza ueneza ubaya kama donda-donda"**

Ni kwa namna gani nahau hii ya walimu wa uongo inavyothibitishwa! Uasi huenea kama kansa ikuayo, hata miongoni mwa waamini, na matokeo yake yanatisha kama sitiari (kama vile 1 Tim. 6:20-21).

◙ **"Himenayo"** Tazama maelezo katika 1 Tim. 1:20.

◙ **"Fileto"** Hili ni tajo pekee la mtu huyu katika Agano Jipya.

**2:18 "walioikosa ile kweli"** Kiuhalisia hiki ni kifungu "ameikana Imani," ambacho ni stiari inayotokana ufundi wa kulenga shabaha (kama vile 1 Tim. 1:19; 4:1; 5:8; 6:10,21). Neno la jumla la dhambi (*hamartia*) linamaanisha kukosa alama. Kipengele hiki kinahusiana na msistizo ulio katika sura inayohusu napito ya unyoofu (kama vile 2 Tim. 2:15-16). Mungu ni "mnyoofu" (yaani., kuokana na stiari ya kibiashara yenye kutumia matete ya mto, tazama Mada Maalum katika Tito 2:12), ambayo ni sawa "haki au "usawa." Watu wake lazima waiakisi sifa yake, bali walimu hawa wa uongo na wafuasi wake kwa uwazi wanainarishwa uthibitisho wao unaotokana na kweli ya ki-Kitume ya kwamba wameiacha njia nyoofu (yaani., "Njia" ambalo lilikuwa jina la awali la kanisa). Tazama MADA MAALUM: UKANAJI IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1.

◙ **"wakisema ya kwamba kiyama imekwisha kuwapo"** Hii ni KAULI TENDAJI YA KITENZI JINA YA WAKATI TIMILIFU (kama vile 1 Kor. 15:12). Fasiri muhimu ni

1. Uwili wa Kiyunani, ambao ulipinga kipengele cha kimwili cha uzima wa milele
2. Msistizo wa falsafa ya Kiyunani juu ya kichocheo cha ki-Ungu ndani ya kila mtu aliyeunganishwa na Mungu katika kifo
3. Msadukayo –kama ukanaji wa maisha ya kimwili baada ya kifo
4. ufufuo ulikuwa ni kwa ajili ya Kristo pekee
5. ufufuo tayari umekwisha tokea (kama vile 2 The. 2:1-2)
6. ufufuo wa waamini kwa maisha mapya unatokea katika wokovu (kama vile Yohana 5:25; Rum. 6:1-11; Kol. 2:12-13)

Toleo la UBS[4] ina kifungu "hii" katika mabano ili kuonyesha uwezekano kwamba andiko halisi, lenye kuzifuatisha MSS א, F, G, na toleo la Georgi (kar ne ya 5), pamoja na andiko la Kiyunani linalotumiwa na Koreshi wa Iskandria (444 B.K), linaweza kuwa limeondolewa.

Hata kama kuna tofauti kama ilivyo hii, andiko la kweli halikupotea bali ni moja ya chaguzi. Andiko lililovuviwa la Mitume bado linapatikana kwa wasomaji wa sasa. Hakuna upotevu wa ile kweli, maana, aua mafundisho.

Ujuzi wa uongo kwa nanmna iliyo dhahiri uliifanya kweli hii kuwa dai la kithiolojia. Hili linaelezwa na kupingwa na

1. Polycarp (69-155 B.K) kwa Wafilipi 3:5
2. Justin Martyr (aliyeuawa mnamo 162-168 B.K) – *Dialogue with Trypho* 80
3. Irenaeus (aliyeandika *Adv. Haer* mnamo 180 B.K) – *Against Heresies* I.23.5; II.31.2
4. Tertullian (160-220 B.K)
   a. *Prescriptions Against Heretics* 33:7
   b. *Of the Resurrection of the Flesh* 19

**NASB** **"walioikosa ile kweli"**
**NKJV** **"waliiweka mbali imani"**
**NRSV, TEV** **"waliikosa imani "**
**NJB** **"wameikosa imani yao"**

Hii KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO inayotokana na "kupindua" (kama vile Yohana 2:15) au "kuangusha" ambalo lilikuja kutumika kistiari kumaanisha"angamiza" au "kuharibu" (kama vile Tito 1:11 na matokeo katika 1 Tim. 1:19; 6:21). Kwa usahihi kipengele hiki kinamaanisha au kugusia katika uhusiano na ukanaji

wa imani (tazama Mada Maalum katika 1 Tim. 4:1) haujulikani, bali majanga ya kiroho! Maneno ya Mathayo 7, "kwa matendo yao mtawatambua" (kama vile 2 Tim. 2:19), ni ya kweli!

Hili neno "imani" linaweza kueleweka katika namna tatu

1. mkaribishaji
2. kweli zinazomhusu watu wa kumwamini
3. maisha kama ya yule tunayotakiwa kuyaishi

**2:19 "Lakini msingi wa Mungu"** Watu wa Mungu kama jengo lililojengwa juu ya Kristo kama msingi ni stiari zilizopendelewa sana na Paulo (kama vile 1 Kor. 3:10 na kuendelea; Efe. 2:20 na kuendelea; 1 Tim. 3:15). Katika muktadha huu na maelezo haya yairejelea kweli ya Mungu yenye kubaki kwa hakika na ngumu katika kuwatofautisha walimu wa ongo. Tumaini la walimu wa uongo li katika sifa ya Mungu na katika kuzisadiki ahadi zake.

## MADA MAALUM: TABIA ZA MUNGU WA ISRAELI

1. Mwenye huruma (BDB 933, KB 1216) – Kut. 34:6; Kumb. 4:31; 2 Nya. 30:9; Zab. 86:15; 103:8; 111:4; Neh. 9:17,31; Yoeli 2:13; Yona. 4:2
2. Mwingi wa fadhili (BDB 337, KB 333) – Kut. 34:6; 2 Nya. 30:9; Zab. 86:15; 103:8; 111:4; Neh. 9:17,31; Yoeli 2:13; Yona. 4:2
3. Si mwepesi wa hasira (BDB 74 MUUNDO WA MANENO BDB 60) – Kut. 34:6; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoeli 2:13; Yona. 4:2
4. Amejaa huruma (BDB 912 I MUUNDO WA MANENO BDB 338) – Kut. 34:6-7; Zab. 86:15; 103:8; Neh. 9:17; Yoeli 2:13; Yona. 4:2
5. Mwaminifu (au "kweli," BDB 54, angalia Mada Maalum: Kusadiki, Amini, Imani, na Uaminifu katika Agano la Kale) – Kut. 34:6; Kumb. 7:9; Zab. 86:15; Isa. 49:7; Yer. 42:5
6. Mwenye kujaa msamaha (BDB 699, KB 757) – Neh. 9:17
7. Hatawasahau ninyi (BDB 736 I, KB 806) – Neh. 9:17,31
8. Hughairi mabaya (BDB 636, KB 688, *Niphal* KAULI ENDELEVU + BDB 948) – Yoeli 2:13; Yona. 4:2
9. Mungu Mkuu (BDB 42, 152) – Neh. 1:5; 9:32
10. Mungu Mkuu na mwenye kuogofya (BDB 152, 431) – Neh. 1:5; 4:14; 9:32
11. Atunzaye maagano (BDB 1036, 136) – Neh. 1:5; 9:32
12. Mwenye rehema kwa wampendao (BDB 338) – Neh. 1:5; 9:32 (angalia Mada Maalum: Wema (*hesed*)

Haya yote yanaelezea hisia za Mungu dhidi ya watu wake, Israeli. Tabia yake haibadiliki (kama vile Mal. 3:6), kwa hiyo, haya pia yanatumika pia kwa wale wafuasi wake waaminifu (yaani., 2 Kor. 1:3).

◙ **"umesimama"** Hii ni KAULI TENDAJI ELEKEZI YA WAKATI TIMILIFU. Toleo la United Bible Societies *A Handbook on Paul's Letters to Timothy and Titus*, uk. 210, linaorodhesha chaguzi nne kama utambulisho wa "msingi huu."

1. Kriso mwenyewe, jiwe kuu la pembeni (kama vile sa. 28:16; Rum. 9:33; 1 Kor. 3:10-12)
2. ujumbe wenye kumhusu Kristo (kama vile Efe. 2:20)
3. Kanisa, mwili wa Kristo
4. Ile Kweli (mafundisho ya umakini)

## MADA MAALUM: JIWE KUU LA PEMBENI

I. Matumizi ya Agano la Kale
   A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu kinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
   B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanza 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).

C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).

D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).

1. linalowekwa la kwanza, ambalo lililuwa linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia liliitwa" jiwe kuu la pembeni"
2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia uzito wa jengo la kuta nzima.

II. Matumizi ya Agano Jipya

A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko 12:10-11; Luka 20:17)

B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)

C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo

D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

II. Kauli za Kithiolojia

A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!

B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.

C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).

D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).

E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

◙ **"wenye muhuri hii"** Huenda hili ni dokezo la

1. mila za kale za makusudi za usanifu wa jengo lililo juu ya jiwe kuu la pembeni
2. rejeleo ibada ya nta ya muhuri (ama vile Yohana 3:33; 6:27; Rum. 4:11; 15:28; 1 Kor. 9:2; 2 kor. 1:22; Efe. 1:13; 4:30; Ufu. 7:3-8)

## MADA MAALUMU: MUHURI/LAKIRI

Muhuri au lakiri yaweza kuwa ni njia ya kale ya kuonyesha

1. Ukweli (kama vile Yohana 3:33)
2. Umiliki (kama vile Yohana 6:27; 2 Tim. 2:19; Ufu.. 7:2-3; 9:4)

3. Ulinzi (kama vile Mwa. 4:15; Mt. 27:66; Rum. 4:11; 15:28; 2 Kor. 1:22; Efe. 1:13; 4:30; Ufu. 20:3)
4. Yaweza kuwa pia ni dalili za ukweli wa ahadi ya Mungu (kama vile Rum. 4:11 and 1 Kor. 9:2)

Kusudi la muhuri huu katika Ufunuo 7:2-4; 9:4 ni kuwatambua watu wa Mungu ili kwamba ghathabu ya Mungu isiwadhuru. Muhuri wa shetani pia huwatambua walio wake, wale walio chombo cha ghathabu ya Mungu. Katika kitabu cha Ufunuo “dhiki kuu” (yaani., *thlipsis)* mara zote inarejerea wasio waumini wakiwatesa waumini, wakati ghathabu/hasira (yaani., *orgē* au *thumos*) mara zote huwa ni hukumu ya Mungu juu ya wale wasioamini ili kwamba wapate kutubu na kuirudia imani katika Kristo. Kusudi hili chanya la hukumu laweza kuonekana katika agano la laana/Baraka katika kitabu cha Mambo ya Walawi 26; Kumbukumbu la Torati 27-28;30; Zaburi 1

◙ **"Bwana awajua walio wake"** Hili naweza kuwa dokezo la Hes. 16:5 katika Aagano la Kale Kiebrania, mazingira yamatendo ya kihistoria na migawanyo, panoja na Yohana 10:14,27.

◙ **"Kila alitajaye jina la Bwana"** Huu unaweza kuwa utata uliokusudiwa. Je! neno "Bwana " linamrejelea YHWH au Yesu?Katika Agano la Kale, kuliitia jina la YHWH ilikuwa stiari ya kuabudu. Waandishi wa Agano Jipya wanachukua matumizi haya ya neno "jina" kama njia ya

1. kuueleza Uungu wa Yesu
2. kumkubali yeye kama Mwokozi na Bwana
3. kumaanisha kwamba kumwitw yeye ni kuyafuatisha matendo yake na sifa yake katika maisha ya kila siku (pamoja na matukio ya ibada).

Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO yenye kuwarejelea wale wanaendele kuwa na uhusiano pamoja na Yesu. Hili jina katika Kiebrania ilikuwa njia ya kuithibitisha sifa ya mtu. Ikiwa waamini wanaliitia jina la Yesu ili waokolewe na kuliakisi jina lake kama wafuasi, yawapasa kuamini na kuishi na kufa kama yeye!

## MADA MAALUMU: JINA LA BWANA

Hili lilikuwa fungu la kawaida la Agano Jipya lililohusu uwepo wa mtu binafsi na nguvu ya Mungu wa Utatu iliyofanya kazi ndani ya Kanisa. Haukuwa utaratibu wa miujiza ya kichawi, bali mvuto wa sifa ya Mungu inayoonekana ndani ya Yesu.

Mara nyingi fungu hili linamrejelea Bwana Yesu kama Bwana (kama vile Flp. 2:11)

1. kwa yule aliye na weledi wa imani katika Kristo (kama vile Rum. 10:9-13; Matendo 2:21,38; 8:12,16; 10:48; 19:5; 22:16; 1 Kor. 1:13,15; Yakobo 2:7)
2. kwa yule anayetoa pepo (kama vile Mt. 7:22; Marko 9:38; Luka 9:49; 10:17; Matendo 19:13)
3. kwa ajili ya uponyaji (kama vile Matendo 3:6,16; 4:10; 9:34; Yakobo 5:14)
4. katika tendo la huduma (kama vile Mt. 10:42; 18:5; Luka 9:48)
5. wakati wa kulirekebisha kanisa (kama vile Mat. 18:15-20)
6. wakati wa kuwahubiri watu wa Mataifa (kamavile Luka 24:47; Matendo 9:15; 15:17; Rum. 1:5)
7. katika maombi (kama vile Yohana 14:13-14; 15:7,16; 16:23; 1 Kor. 1:2)
8. kama njia ya kuurejea Ukristo (kama vile Matendo 26:9; 1 Kor. 1:10; 2 Tim. 2:19; Yakobo 2:7; 1 Pet. 4:14)

Cho chote tufanyacho kama wapiga mbiu, wahudumu, wasaidizi, walioponywa, watoa pepo, n.k. tunakifanya katika sifa Yake, nguvu Zake, utabiri Wake—katika Jina lake (yaani, Flp. 2:9-10)!

◙ **"auache uovu"** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Huenda hili linaweza kuwa dokezo la Hes. 16:26-27 katika Agano la Kale la Kiebrania. Katika muktadha huu ni dhahiri kuwa hili linaurejelea uhusiano na miungu ya walimu wa uongo na wafuasi wao (yaani, "vya udongo . . . vingine havina," 2 Tim. 2:20; 3:5).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 2:20-26**

**[20] Basi katika nyumba kubwa havimo vyombo vya dhahabu na fedha tu, bali na vya mti, na vya udongo; vingine vina heshima, vingine havina. [21] Basi ikiwa mtu amejitakasa kwa kujitenga na hao, atakuwa chombo cha kupata heshima, kilichosafishwa, kimfaacho Bwana, kimetengenezwa kwa kila kazi iliyo njema. [22] Lakini zikimbie tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi. [23] Walakini uyakatae maswali ya upumbavu yasiyo na elimu, ukijua ya kuwa huzaa magomvi. [24] Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; [25] akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu awape kutubu na kuijua kweli; [26] wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa Ibilisi, ambao hao wametegwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake.**

**2:20 "nyumba kubwa"** Muktadha wa papo kwa papo kwa nguvu yanamaanisha kwamba hii ni sitiari yenye kuzungumza (kama vile Yohana 14:2).

◙ **"vingine vina heshima, vingine havina"** Wengine wanaliona hili kama lenye kueleza aina mbalimbali za ujuzi, sifa na karama (kama vile Rum. 9:19-24; 1 Kor. 12:12-31) za waamini bali wengine wanaliona hili kama lenye kuhusiana na wavurugaji wa 2 Tim. 2:22-23.

**2:21 "ikiwa mtu amejitakasa"** Hii ni SENTENSI AMRISHI DARAJA LA TATU yenye kumaanisha tendo lenye umuhimu, bali baadhi ya viwango vya bahati kama mtu mweye matendo ya hiari.

Hili neno "amejitakasa" ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI huenda linahusiana na wongofu au kugeuka kutoka kwa walimu wa uongo. Hili neno ambatani *ek* + *kathairō* linatumika hapa tu na katika1 Kor. 5:7. Waamini wanaouchaguzi katika kujihusisha kwao na katika kutumika katika kazi ya Ufalme.

◙ **"kujitenga"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU yenye kumaanisha mambo kadhaa:

1. walitakaswa kwa wakati uliopita na hali kaida iliendelea (WAKATI TIMILIFU)
2. walitakaswa na Mungu (IRABU TENDWA)

Itambue hali ya mtu kuamua kujitakasa na usemi wa tendo la Mungu. Utakaso ni vyoye tendo la ki-Ungu na tendo la kibinadamu. Mwelekeo huu una sifs bainishi ya uhusiano wa agano katika mambo yote yanayoshughulikiwa na Mungu kwa wanadamu. Mara nyingi huuangalia mwanzo wake na kuweka mipango, lakini mwanadamu yampasa kuihitikia vema na kuendelea kuhitikia.

## MADA MAALUMU: UTAKASO KATIKA AGANO JIPYA

Kitabu cha Agano jipya kinadai kwamba wenye dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16, 19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumto mtu hatiani).

Lakini Agano Jipya pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, ni utakaso.

| Mwitikio wa Awali | Ufanano na Kristo Endelevu |
|---|---|
| Matendo 26:18 | Warumi 6:19 |
| Warumi 15:16 | 2 Kor. 7:1 |
| 1 Wakorintho 1:2-3; 6:11 | Waefeso 1:4; 2:10 |
| 2 Wathesalonike 2:13 | 1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2 |
| Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12 | 1 Timotheo 2:15 |

| | |
|---|---|
| 2 Petro 1:2 | 2 Timotheo 2:21<br>1 Petro 1:15-16<br>Waebrania 12:14 |

◙ **"kimfaacho Bwana"** Hili ni neno la Kiyunani ambapo tunalipata neno a Kiingereza "dhalimu."Hili linam rejelea mmiliki wa mtumwa (kama vile mst. wa 24) mwenye mamlaka kamili kwa mwingine (kama vile 1 Tim. 6:1-2; Tito 2:9; 1 Pet. 2:18).

Waamini wanaojitakasa wanamfaa Bwana. Walimu wa uongo hawafai!

◙ **"kimetengenezwa kwa kila kazi iliyo njema"** Hii ni KAULI TENDWA YA KATI au KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU. KITENZI hiki kinapatikana hapa tu na katika nukuu toka Isaya katika 1 Kor. 2:9 (yaani., Isa. 64:4 na 65:17). Kazi zilizo njema hazitufanya tukubalike au kutuleta kwa Mungu (yaani., Efe. 2:8-9), bali pale tunapokutana naye katika Kristo ndiyo matokeo yatarajiwayo (kama vile Efe. 2:10; Yakobo 2:14-26)! Sisi ni watu tulioumbwa kwa ufanano na Kristo, urejesho wa sura ya Mungu ambayo ilipotea katika anguko la Mwanzo 3. Maisha ya utauwa ya waamini huuthibitisha wokovu wao na kuwavutia wengine kwa Kristo. Tazama MADA MAALUM: WEMA NA UOVU katika Agano Jipya 1 Tim. 1:9.

**2:22**
**NASB, NKJV "zikimbie. . . ukafuate"**
**NRSV "Epuke. . . ukafuate"**
**TEV "Jiepushe. . .ukafanye bidii"**
**NJB "Rudi. . .ukawe makini"**

Hizi zote ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI ZA WAKATI ULIOPO. Waamini wanaendelea kuionyesha sifa ya Mungu (kama vile 1 Tim. 6:11).

◙ **"zikimbie tamaa"** Kila hatua ya maisha ina majaribu ya kipekee (kama vile Muh. 3:1-8; 11:10; 12:1-8).

◙ **"haki, na imani, na upendo"** Hizi ni sifa bainishi za Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalum katika 2 Tim. 2:19) ambazo zinahitaji kuendelezwa na kukuzwa ndani ya watu wake (kama vile 1 Tim. 1:5,14). Kwa neno "haki" tazama Mada Maalum katika Tito 2:13.

◙ **"wamwitao Bwana kwa moyo safi "** Hii ni KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO, yenye kumaanisha tendo endelevu. Katika Yoell 2:32, Matendo 2:21 na Rum. 10:9-13 kifungu hiki kinaonekana kumaanisha mwitikio wa awali, lakini katika muktadha wa waamini waliokomaa. Mahusiano yetu pamoja na waanini ya makusudi na yaliyo endelevu ni moja ya siri ya uaminifu, furaha, na maisha ya Mkristo yaliyo na amani. Tazama MADA MAALUM: MOYO katika 1 Tim. 1:5.

**2:23 "uyakatae"** Timotheo anaamrishwa kutokuendelea kushiriki katika mabishano na madhahanio ya walimu wa uongo yasiyo na maana (KAULI YA KATI [yenye ushahidi] SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO).

◙ **"upumbavu"** HIli neno linaweza kuakisi neno la Kiebrania/Kiaramu "uovu usio na maana" (yaani., *raca* kama vile Mt. 5:22).

◙ **"yasiyo na elimu"** Hili ni neno linalotumika kaumaanisha kuwaelekeza watoto pamoja na KIBAINISHI HASI. Mara nyingi Paulo alilitumia neno lisilo na ukanushi katika miundo mbalimbali katika Nyaraka za Kichungaji (kama vile 1 Tim. 1:20; 2 Tim. 2:25; 3:16; Tito 2:12). Hawa walimu wa uongo si wenye ufahamu na hawana mafunzo; hili ni la makusudi la hiari! Yote wanayotaka kuyatenda iliwapasa kuyajadili na kuweka dhahanio juu ya mambo yasiyo ya muhimu (kama vile 1 Tim. 1:4; 4:7; 6:4; 2 Tim. 2:14; 4:4; Tito 1:14; 3:9). Hii aina ya mjadala wa kinajivunoinarudiwa katika Nyaraka za Kichungaji.

**2:24-25** Hapa kuma mlolongo wa mambo yawapasayo waamini kuyasaidia "walioshawishika" kurudi kwa Bwana:

1. kujiepusha na magomvi (kama vile 1 Tim. 3:3; Tito 3:9)
2. kuwa mwema kwa watu wote (kama vile Tito 3:2)
3. kuwa na uwezo wa kufundisha (kama vile 1 Tim. 3:2; Tito 1:7)
4. kujishusha pale unapokosea (maneno tofautitofauti lakini yenye kufanana na yale yaliyo katika 1 Tim. 3:3; 6:11; 2 Tim. 3:10; Tito 2:2)
5. uwe mpole unapokosoa (kama vile 1 Tim. 3:3; Tito 3:2)

Kwa namna iliyo wazi Paulo anauakisi ubora muhimu wa uongozi (kama vile 1 Timotheo 3) na pia sifa ya utauwa ya kila mwamini (kama vile Tito 3:1-3).

**2:25 "washindanao naye"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO (yaani., wanaoendelea kuipinga kwa makusudi ile kweli ya ki-Utume na maadili). Tambua, hata hawa lazima wachukuliwe kama waamini wa muhimu. Ni kwa namna gani tunawachukulia wale wanaoipinga injili yenye kuzungumza jambo muhimu na kutuhusu sisi!

◙ **"ikiwezekana, Mungu awape kutubu"** Hili neno "ikiwezekana" halimo katika andiko la Kiyunani bali KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU yenye kumaanisha SENTENSI AMRISHI DARAJA LA TATU.

Jambo la kithiolojia lililohusiana na kifungu hiki ni ukuu wa Mungu wenye kuhusiana na wokovu dhidi ya mapenzi huru ya wanadamu. Je! imani na toba (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21) ni mwitikio wa mwanadamu au karama toka kwa Mungu? Kuna maandiko ambayo kwa nguvu yanamaanishakwamba hizi ni karama toka kwaMungu (kama vile Matendos 5:31; 11:18; Rum. 2:4). Kwa kuwa naamini kwamba Maandiko yote yamevuviwa (kama vile 2 Tim. 3:16) yampasa mtu kuyalinganisha maandiko yote yenye kuhusiana na suala la kithiolojia na kujitoa katika mbinu za kiuchunguzi. Ni dhahiri kwamba Mungu mmoja wa kweli yu katika kuyatawala mambo yote! Lakini amechagua kuuhusianisha uumbaji wake wa kiwango cha juu kwa namna ya agano. Mara nyingi Mungu huangalia mwanzo wake na kuweka mipango, bali mwanadamu yampasa kuhitikia na kwendelea kuhitikia. Kwa vyo vyote hili haliwezi kuwa /au swali. Mara nyingi ni vyote /na uhusiano. Tazama MADA MAALUM: AGANO katika 2 Tim. 2:1

## MADA MAALUM: TOBA KATIKA AGANO LA KALE

Dhana hii ni ya muhimusana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) amabayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

a. "kupumzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
b. "kuhuzunika" (m.f. Mwa. 6:6,7)
c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Num. 23:19; Ayubu 42:5-6)
d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa.

6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hiii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [AJ]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Maro 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nacham*r linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi na Bathsheba (kama vile 2 Samueli 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahitajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

◙ **"kuijua kweli"** Njia ya kuielekea kweli (*alētheia*) na maarifa (*epignōsis*) haipatikani katika (1) uzao wa Kiyahudi au (2) madhahanio ya Ujuzi wa uongo bali injili ya Yesu Kristo (kama vile 2 Tim. 3:7; 1 Tim. 2:4; Tito 1:1). Tazama Mada Maalum : Kweli katika 1 Tim. 2:4.

**2:26 "wapate tena fahamu zao"** Hii ni KAULI TENDAJI TEGEMEZI YA WAKATI ULIOPITA yenye muundo ambatani (*ana* + *nēphō*) wa neno neno *nēphalios* ("kuwa na akili") linalotumika kistiari "mwenye kiasi na busara" (kama vile 1 Tim. 3:2,11; Tito 2:2).

◙ **"hao wametegwa naye"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ya neno ambatani "kukamata" + "kuwasili" ambalo lilitumika kutega wanyama. Hapa linatumika kuwakamata wafungwa walio mateka. IRABU TENDWA na muktadha wa papo kwa papo vinambainisha Shetani kama wakala na walimu wa uongo na wafuasi wao kama wafungwa! Kadri injili inavyopenya ndani ya wanadamu (kama vile Luka 5:10), ndivyo ilivyo, kwa yule mwovu (kama vile 1 Tim. 3:7).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni sababu gani nuhinu ya mchungaji?
2. Kwa nini kuteseka ni sehemu ya Ukristo?
3. Kwa nini ufufuo ni kiini cha imani ya Ukristo?
4. Mstari wa 12b unamrejelea nani? Je, unamaanisha nini?
5. Ni kwa namna gani Timotheo anashughulika na walimu wa uongo?
6. Kwa nini mstari wa 15 ni wa muhinu sana kwa akristo wote?
7. Je! Mungu huiruhusu toba kwa wanadamu? Ikiwa ni hivyo, kwa kiasi fulani au kwa wote?
8. Nani anasemekana kuwakamata walimu wa uongo na wafuasi wao? Ni kwa namna wanaweza kuepuka?

# 2 TIMOTHEO 3

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Tabia ya watu wa Siku za mwisho | Nyakati za hatari na watu hatari | Mchungaji na Kundi (2:14-4:5) 2:20-3:9 | Siku za Mwisho | Hatari za siku za Mwisho |
| 3:1-9 | 3:1-9 | | 3:1-9 | 3:1-5<br>3:6-9 |
| Shitaka la mwisho La Timotheo (3:10-4:8) | Mtu wa Mungu na Neno la Mungu | | Maelekezo ya Mwisho (3:10-4:8) | |
| 3:10-17 | 3:10-17 | 3:10-4:5 | 3:10-4:5 | 3:10-13<br>3:14-17 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Biblia. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 3:1-9**
**1 Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. 2 Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, 3 wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, 4 wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; 5 wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao. 6 Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi; 7 wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli. 8 Na kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, vivyo hivyo na hawa wanapingana na ile kweli; ni watu walioharibika akili zao, wamekataliwa kwa mambo ya imani. 9 Lakini hawataendelea sana; maana upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote, kama vile na upumbavu wa hao ulivyokuwa dhahiri.**

**3:1 "siku za mwisho"** Kipindi hiki cha muda kinaenda na majina kadhaa.

1. siku za mwisho, Hes. 24:14; Kumb. 8:16; Dan. 2:28; 10:14
2. katika siku za mwisho, Yer. 23:20; 30:24; 49:39; Ezek. 38:8,16; Hos. 3:5; Yoeli 2:28 (Mdo. 2:17); Yohana 6:39,40,44,54; 11:24; 12:48; 2 Tim. 3:1; Yakobo 5:3
3. katika siku za mwisho, 1 Pet. 1:5

4. katika siku za mwisho, 1 Pet. 1:20
5. wakati wa siku za mwisho, 2 Pet. 3:3
6. saa ya mwisho, 1 Yohana 2:18

Wakati wa siku za mwisho ni "siku ya Bwana" (yaani, "ukamilishwaji," Mt. 13:39,40; 24:3; 28:20; Ebr. 9:26).

Wayahudi wa kipindi cha kati ya Agano la Kale na Agano Jipya waliona nyakati mbili (kwa kuanza na Mwanzo 3) na kuja kwa nyakati ya haki inayoanzishwa kwa kuja kwa Masihi katika nguvu ya Roho. Agano la Kale linasisitiza kuja kwa Masihi katika hukumu na nguvu kuanzisha nyakati mpya. Hatahivyo ilishindwa kuona (1) yule "Mtumishi Atesekaye" katika Isaya 53; (2) Mnyenyekevu aendeshaye matandiko ya farasi katika Zek. 9:9; na (3) Yule aliyetobolewa 12:10. Kutoka ufunuo unaoendelea wa Agano Jipya tunajua kwamba Mungu alipanga ujio mbili za Masihi. Muda katika ya Kuvaa mwili (kuja kwa mara ya kwanza) na kuja kwa mara ya pili kunajumuisha mpandano wa nyakati mbili za Kiyahudi. Hii inaelezwa katika Agano Jipya kwa tungo "siku za mwisho." Tumekuwa katika kipindi hiki kwa zaidi ya miaka 2000. Angalia Mada Maalum: Enzi Hii na Enzi Ijayo katika 1 Tim. 6:17. Siku za mwisho ni sasa (kama vile Mdo. 2:16-17; Ebr. 1:2; 1 Pet. 1:20; 4:7; 1 Yohana 2:18).

◙**"kutakuwako nyakati za hatari"** Hii inarejerea "maumivu ya kuzaa" ya nyakati mpya (kama vile Mathayo 24; Marko 8:13; Luka 21; Rum. 8:22; 1 Tim. 4:1).

Kumekuwepo na mjadala mkubwa kati ya wafasiri na wanathiolojia juu ya hali za jamii ya binadamu wakati Bwana atakaporudi. Kwa baadhi, nguvu ya injili (postmillennialism baada ya Milenia). Kwa wengine, Agano la Kale na Agano Jipya linatabiri juu ya hitimisho la hatari kwa historia ya wanadamu (premillennialism na amillennialism).

Mjadala wa Paulo "mtu asiye na sheria" katika 2 Wathesalonike 2 inatoa unabii juu ya kupanda kwa maovu uasi, kama zinavyofanya 1 Timotheo 4 na 2 Timotheo 3. Yesu atakuja kurejesha utaratibu na haki.

**3:2 "wenye kujipenda wenyewe"** Kwa orodha inayofanana juu ya uasi angalia Rum. 1:28-32. Tabia hizi za kibayana ni umuhimu wa uasi wa kibinadamu (inayopatikana hapa tu katika Agano Jipya) kutoka katika upendo (*philos*) + binafsi (*auto*) (kama vile Flp. 2:21).

◙**"wenye kupenda fedha"** Angalia dokezo katika 1 Tim. 3:3 na 6:10.

◙**"wenye majivuno"** Hii inaweka tabia ya wanadamu kujivuna au ujasiri juu ya mtu mwenyewe (kama vile Rum. 1:30; Yakobo 4:16; 1 Yohana 2:16)

◙**"wenye viburi"** Hii inaelezea mtu anayefikiri yeye ni mkubwa na anaelezea maneno na matendo (kama vile Luka 1:51; Rum. 1:30; Yakobo 4:6; 1 Pet. 5:5). Neno la Kiyunani *huperēphanos*. Angalia Mada Maalum: Matumizi ya Paulo ya *Huper* Ambatani katika 1 Tim. 1:14.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"waasi"** |
| **NKJV** | **"wanaokufuru"** |
| **NRSV** | **"wenye kutukana** |
| **TEV** | **"watakuwa wakitukana"** |
| **NJB** | **"wakatili"** |

Hii kibayana "wakufuru." haijulikani ikiwa wanazungumzia dhidi ya

1. Mungu/Kristo (kama vile 1 Tim. 1:13,20; 6:1; Ufu. 16:11;21)
2. malaika (kama vile 2 Pet. 2:10-12)
3. wanadamu wengine (kama vile 1 Tim. 6:4; Tito 3:2; 1 Pet. 4:4)

◙**"wasiowatii wazazi wao"** Hii inaweza kuhusiana na Amri Kumi (kama vile Kut. 20:12). Kwa Wayahudi familia zenye nguvu ilimaanisha familia imara ("siku zako zitaongezwa katika nchi"). Maelezo binafsi siku zote yanaumiza mahusiano kati ya mtu nyumbani, kanisani, kazini, n.k.

◙**"wasio na shukurani"** Hili ni neno kanushi kwa "neema". Maneno kadhaa katika orodha hii ni maneno yaliyokanushwa na KIAMBISHI HASI. Haya ni kutoshukuru, ubinafsi na watu waharibifu.

◙**"wasio safi"** Huu ni muundo kanushi wa neno *hosios*, ambayo inarejerea juu ya mtu anayefanyia kazi sheria zote za Mungu na hivyo alifikiri alikuwa mwenye haki na mtauwa (kama vile Tito 1:8) na safi (kama vile 1 Tim. 2:8). *Hosios* lilitumika kuelezea Yesu katika Mdo. 2:27; 13:35 (nukuu kutoka katika Zab. 16). Katika Ebr. Heb. 7:26 ni tabia ya Yesu, Kuhani wetu Mkuu. Paulo analitumia kuelezea matendo yake mwenyewe kuwaelekea waumini wa Thesalonika (kama vile 1 The. 2:10).

**3:3**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"asiye na upendo"** |
| **NRSV** | **"asiye na ubinadamu"** |
| **TEV** | **"watakuwa si wema"** |
| **NJB** | **"wasio na moyo"** |

Hili ni neno la Kiyunani kwa ajili ya upendo wa asili uliokanushwa (kama vile Rum. 1:31). Inarejerea kwa kukosa ubinadamu au familia.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"isiyopatanishwa"** |
| **NKJV** | **"asiyesamehe"** |
| **NRSV** | **"asiyetafta amani"** |
| **TEV** | **"asiyerehemu"** |
| **NJB** | **"asiyetaka suluhu"** |

Hili ni neno la Kiyunai kwa ajili ya kutengeneza makubaliano au mkataba, kanushi (kama vile Rum. 1:31). Inarejerea kwa watu ambao hawako tayari kutengeneza au kurejesha mahusiano.

◙**"wasingiziaji"** Hili ni neno la Kiyunani kwa "wazushi" (*diaboloi*) ambalo pia ni nono kwa ajili ya shetani (Kiebrania) au Shetani (Kiyunani). Angalia dokezo katika 1 Tim. 3:11.

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"bila kiasi"** |
| **NRSV, NJB** | **"badhirifu"** |
| **TEV** | **"katili"** |

Hili ni neno la Kiyunani *kratos* likimaanisha "imara, nguvu, uweza," katika hali ya kukanushwa. Linapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Watu hawa wanakosa kiasi (kama vile Mt. 23:25; 1 Kor. 7:5).

◙**"wakatili"** Hili ni neno la Kiyunani "kulinda, pole au jema," katika hali ya ukanushi. Toleo la NJB lina "isiyotaarabika." Inapatikana hapa tu katika Agano Jipya.

◙**"wachukiao mema"** Hili ni neno la Kiyunani *philos* + *agathos* (yaani mpenzi wa vizuri, kama vile Tito 1:8), katika hali ya ukanushi. Linapatikana hapa katika Agano Jipya. Watu hawa ni maadui wa kila kilicho chema na chenye kupendeza.

**3:4 "wakaidi"** Hili ni neno ambatani la Kiyunani "kutoa zaidi" ambayo ilitumika kisitiari kwa ajili ya "msaliti" (kama vile Luka 6:16; Mdo. 7:52).

◙**"wasiojali"** Hili ni neno la Kiyunani ambatani la *pros* + *piptō* linalotumika kisitiari kwa kutofikiri na hivyo kutenda kiuwendawazimu (kama vile Mdo. 19:36).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"lijivunalo"** |
| **NKJV** | **"lenye kiburi"** |
| **NRSV** | **"asumbuliwaye na majivuno"** |
| **TEV** | **"asumbuliwaye na kiburi"** |
| **NJB** | **"lenye wazimu wa kiburi"** |

Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU ambayo inaashiria kuletwa na hali ya nguvu ya nje; hapa, yule muovu. Ni nahau inayohusiana na uongo kwa kupofushwa na uvumi (kama vile 1 Tim. 3:6; 6:4).

◙**"wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu"** Paulo ametumia ambatani kadhaa pamoja na *philos*:
1. wanaojipenda wenyewe (2 Tim. 3:2)
2. wapenda fedha (2 Tim. 3:2)
3. wasiopenda mazuri (2 Tim. 3:3)
4. wapenda anasa (2 Tim. 3:4)
5. wampendao Mungu (2 Tim. 3:4)

Badala ya kujikita kwaa Mungu na mapenzi Yake, watu hawa wakuwa wenye kujiangalia wao wenyewe tu na utashi wao binafsi (kama vile Flp. 3:19).

**3:5 "wenye mfano wa utauwa lakini wakikana nguvu zake"** Hii ni KAULI YA KATI ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU (kama vile Isa. 29:13; Rum. 2:20; Tito 1:16). Hii ni hali iliyotulia ya kujielezea mapenzi yake yenyewe. Elimu ya kitaasisi inaweza kuwa jukumu la kikatili! Kwa "utauwa" angalia Mada Maalumu katika 1 Tim. 4:7.

◙**"waepuke watu wa namna hiyo"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile 2 The. 3:6). Timotheo yuko tayari na anaendelea kukwepa aina hii ya watu. Hii kidhahiri ni rejea kwa walimu wa uongo na wafuasi wake (kama vile 2 Tim. 2:19,20).

**3:6 "wale wajiingizao katika nyumba za watu"** Kibayana hii ni "kunyemelea" (kama vile Mt. 7:15; Yuda 1:4). Neno linapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Walimu hawa wa uongo walikuwa wakichukulia nafasi ya wanawake wa nyumbani wasiokuwa na taarifa na wasio kuwa na ulinzi.

◙**"kuchukua mateka"** Hii ni KAULI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hii kibayana ni "kukamata kwa njia ya mkuki" (kama vile Efe. 4:8; Ufu. 13:10). Manabii hawa wa uongo wanaendelea kutrumia mbinu hii ya kutongoza familia kupitia mke aliyekuwa akishinda nyumbani wakati wa mchana.

| | |
|---|---|
| **NASB, TEV,** | |
| **NET** | **"wanawake dhaifu"** |
| **NKJV** | **"wanawake wasiojiheshimu"** |
| **NRSV, NJB** | **"wanawake wapuuzi"** |

Hii *gunaikaria* ambayo ni aina ya muundo wa kijumuishi cha *gunē* (mwanamke). Hakika namna gani inatakiwa ieleweka bado kuna maswali lakini inaonekana kuwa na kisawe kanushi (kama vile BAGD 168). Sehemu inayobaki ya 2 Tim. 3:6 na 2 Tim. 3:7 ni maelezo ya "wanawake hawa wadogo." Linapatikana hapa tu katika Agano Jipya.

Haijulikani ikiwa hawa wanawake ni wanawake wa kanisani au wanawake waishio tu katika jamii (dokezo katika 3:3 na 1 Tim. 5:6).

◙**"wenye mizigo ya dhambi"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU. Hii inaonekana kuhusian ana tatizo la "vijana" wajane vijana watongozwao na uovu (kama vile 1 Tim. 5:6).

◙**"waliochukuliwa na tamaa"** Hii ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI TIMILIFU. Hii inamaanisha wanawake waliendelea kuongozwa na mwitikio wa kishetani (kama vile Tito 3:3).

**3:7** Muktadha wa ghafla na KITENZI CHA WINGI KISICHO NA UPANDE inatengeneza miundo mara katika 2 Tim. 3:6 na mara mbili katika 2 Tim. 3:7 thibitisha utangulizi kama "wanawake dhaifu" wa 2 Tim. 3:6. Maelezo ya namna gani ya dhambi na hila!

Kwa kuzungumza kiujumla walimu wa uongo wa kila kizazi wanaundwa na tabia za

1. unyanyasaji wa kingono
2. unyanyasaji wa kifedha
3. unyanyasaji wa kiufunuo (Mungu anazungumza na mimi tu!)

**3:8 "Yane na Yambre"** Haya ni majina ya kijadi ya wachawi wa Farao katika Kut. 7:11,22; 8:7,18; 9:11. Majina yao yanafundishwa kutoka katika Dini ya Kiyahudi ya walimu, na hasa Targum ya Jonathan, lakini hayatajwi katika Agano la Kale. Paulo mara kwa mara anatumia desturi za kiualimu wa kiyahudi (kama vile 1 Kor. 10:4).

◙**"hivyo watu hawa pia wanaipinga kweli"** Hii ni KAULI YA KATI ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Walimu hawa wa uongo walikuwa na tatizo na mamlaka na kuendelea kupinga mafundisho ya Kitume. Angalia Mada Maalum: Kweli katika 1 Tim. 2:4.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"wenye wenye akili yas ukengeufu"** |
| **NKJV** | **"watu wenye akili ya upotofu"** |
| **NRSV** | **"watu hawa wenye akili za upotofu"** |
| **TEV** | **"watu ambao akili zao hazifanyi kazi"** |
| **NJB** | **"akili zao zimeharibiwa"** |

Hii ni KAULI TENDWA YA WAKATI TIMILIFU kutoka katika ambatani *kata* + *patheirō*, ikimaanisha mtu ambaye amefanyika na kuendelea kupotoka kupitia nguvu ya nje (yaani Shetani au mapepo) ikipelekea kukataliwa kwao wenyewe kwa ukweli kwa mapenzi yao wenyewe (kama vile 1 Tim. 6:5 Tito 1:15).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"waliokataliwa kuhusu imani"** |
| **NKJV** | **"wasiothibitishwa kuhusu imani"** |
| **NRSV** | **"imani ya uongo"** |
| **TEV** | **"wale walioshindwa katika imani"** |
| **NJB** | **"wenye imani ya uongo"** |

Hili ni neno *dokimazō* with likiwa na kisawe cha majaribu pamoja na mtazamo juu ya uthibitisho uliokanushwa. Hawa walishindwa jaribu la imani (kama vile Rum. 1:28; 1 Kor. 9:27; 2 Kor. 13:5-7; Tito 1:16; Ebr. 6:8). Haya ni maelezo ya kushangaza ya imani iliterereka! Angalia Mada maalum: Maneno ya Kiyunani kwa "Majaribu" na Visawe vyake katika 1 Tim. 6:9; pia dokezo MADA MAALUM: UKANAJI WA IMANI *(APHISTĒMI)* katika 1 Tim. 4:1.

**3:9 "wataendelea sana"** Hii inaweza kurejerea malimu wa uongo na wafuasi wao kwasababu KITENZI hiki hiki kinatumiwa juu yao katika 2 Tim. 2:16 na 3:13. Maana yake ya mzizi ni kutangulia katika kitu fulani (yaani, 2:16 katika utauwa na 3:13 katika kudanganya na kudanganywa).

◙**"kama vile upumbavu wa hao ulivyokuwa dhahiri"** "Kwa matunda yao mtawatambua" (kama vile Mt. 7:20; 1 Tim. 5:24). Uzima wa milele una tabia zinazoonekana kama ilivyo imani ya uongo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 3:10-17**
**[10] Bali wewe umeyafuata mafundisho yangu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani, na uvumilivu, [11] na upendo, na saburi; tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyonipata katika Antiokia, katika Ikonio, na katika Listra, kila namna ya adha niliyoistahimili, naye Bwana aliniokoa katika hayo yote. [12] Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa. [13] lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. [14] Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza**

**kwao; [15] na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. [16] Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; [17] ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.**

**3:10-11** Mstari wa 10 ni tofauti na maisha na vipaumbele vya walimu wa uongo. Paulo anaorodhesha vitu ambavyo Timotheo vinafanana naye kihuduma:

1. Mafundisho ya Kitume ya Pulo (kama vile 1 Tim. 4:6)
2. mtindo wa maisha ya Paulo
3. kusudi la Paulo
4. Imani ya Paulo (kama vile 1 Tim. 6:11)
5. uvumilivu wa Paulo
6. upendo wa Paulo (kama vile 1 Tim. 6:11)
7. Uvumilivu wa Paulo (kama vile 1 Tim. 6:11)
8. mateso ya Paulo
9. Taabu za Paulo (kama vile 1 Kor. 4:10-13; 2 Kor. 4:7-11; 6:3-10; 11:23-28)

VITENZI vyote katika 2 Tim. 3:10-1 ni WAKATI ULIOPITA USIO TIMILIFU. Paulo alikuwa anaaksi juu ya safari zake za Kimisionari. Anazungumza kumtia moyo kwa Timotheo kwa anji ya kumkumbusha.

**3:11 "Antiokia, Ikonio na Listra"** Kutoka Mdo. 13 na 14 tunajua kwamba hili lilikuwa ni eneo la nyumbani kwa Timotheo.

**3:12** Huu ni mstari unaoshangaza kwa waaminio wa kimagharibi wa sasa. Desturi yetu imelindwa na dhiki nyingi zihusianazo na Ukristo. Lakini kukosekana kwa mateso pia kumekuja kukosa kwa nguvu na utauwa! Yesu alikamilishwa na vitu vilivyomtesa (kama vile Ebr. 5:8). Vitu ambavyo Mungu huvitumia kuendeleza watoto Wake kwenye kufanana na Kristo ni vitu vile vile ambavyo watu wa magharibi ya kisasa! Afya, mali na harakati za mafanikio inajenga tabia ya desturi zetu zilizo na uharibifu na ziznzoshikiliwa.

Tazama inayofuiata inasema "wote"! Taabu ni kawaida kwa watu wa Mungu wakitafta kuishi kwa ajili yake katika ulimwengu ulionaguka; ndio,kawaida (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-2; 17:14; Mdo. 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; 2 Kor. 4:16-18; Flp. 1:29; 2 Tim. 1:8; 2:3; 3:12; 1 The. 3:3; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 4:12-19)!

Hatutakiwi kutafta taabu, lazima tuishi kitayari! Ikiwa tutakufa kila siku (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20; 1 Yohana 3:16) Kwa ajili ya Kristo, basi kifo cha kimwili haitutishi sisi tena!

**3:13 "watu wabaya na wadanganyaji"** Walimu hawa walikuwa wazushi kama wachawi wa uongo (kama vile 2 Tim. 3:8).

◙**"wataendelea"** Hiki ni KITENZI kile kile kama katika 2 Tim. 2:16.

◙**"wakidanganya"** KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Waliongoza wengine kuwapotosha kama walivyo potea wenyewe kwa uovu.

◙**"na kudanganywa"** Hii ni KAULI TENDWA YA WAKATI ULIOPO. Wale waliokamatwa na dhambi, ubinafsi na shetani kujaribu kuwakamata wengine!

**3:14 "ukae katika mambo uliyofundishwa"** Hii ni tofauti kwa 2 Tim. 3:13 na kuendelea kutia moyo 2 Tim. 3:10-12. Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO (kama vile 2 Tim. 2:13; Tito 1:9).

**3:15 "tangu utoto"** Hii inaonesha mafunzo ya kidini ya Timotheo ya nyumbani (kama vile. 2 Tim. 1:5). Haijulikani ikiwa hii inarejerea kwa Dini ya Uyahudi au Ukristo.

◙**”maandiko matakatifu"** Hii inaweza kujumuisha zaidi ya Agano la Kale, lakini mstari wa 16 unatuonesha kwamba Agano la Kale linachomaanisha hapa.

◙**"ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu wokovu"** Hii inaonesha kusudio la msingi la maandiko ni ukombozi kwa mwanadamu. Pia inaonesha kwetu mbinu za ukombozi ambao ni mwitikio wa imani ya mwanadamu kwa Masihi wa Mungu. Hii ndio sababu ya mahubiri ya Kitume (*kerygma*). Hatahivyo mstari wa17 unaonesha kwamba mafundisho (ambayo lazima katika hili andiko inarejerea kwa Andiko la Kale kwasababu Agano Jipya halikuwa kamilifu au katika mzunguko) lina kusudio la mwisho — akiwakamilisha watakatifu kwa ajili ya mtindo wa maisha yanayofanana na Kristo. Paulo mara kwa mara alitumia Agano la Kale kutia moyo waamini kuishi maisha ya kitauwa. Agano la Kale hayafanyi kazi kwa "kuhesabiwa haki" (kama vile Wagalatia 3), lakini haifanyika kazi "kutakaswa." Angalia Mada maalum katika 1 Tim. 1:8.

## MADA MAALUMU: MAFUNDISHO YA KANISA LA KWANZA

Kuna maoni mengi kuhusu Ukristo. Siku zetu hizi ni siku za wingi wa dini, kama ilivyokuwa karne ya kwanza. Binafsi, kwa pamoja nayajuisha na kuyakubali makundi yote yale yanayodai kumfahamu na kumwamini Yesu Kristo. Wote hatukubaliani kuhusu hili au lile lakini kimsingi ukristo ni kumhusu Yesu. hata hivyo, kuna makundi yanayodai kuwa wapo wakristo ambao wanaonekana “kufanana.” Ni kwa vipi naweza kuelezea tofauti?
Sawa, kuna njia mbili:

A. Kitabu kinachoweza kusaidia kujua kile makundi ya madhehebu ya kisasa yanaamini (kutoka katika maandiko yao) *The Kingdom of the Cults* na Walter Martin.
B. Hotuba ya makanisa ya awali, hasa wale kupitia Mtume Petro na Paulo katika kitabu cha Matendo, wanatupatia maelezo ya msingi kwa vipi waandishi wa karne ya kwanza waliovuviwa waliuelezea Ukristo kwenye makundi. “matamko” haya ya awali au “mafundisho” (ambacho kitabu cha matendo ni mhutasari wake) yanaendana na neno la Kiyunani *Kerygma.* Ufuatao ni ukweli halisi wa injili kuhusu Yesu katika Matendo ya Mitume:
    1. Kutimiliza nabii nyingi za Agano la Kale- – Mdo. 2:17-21,30-31,34; 3:18-19,24; 10:43; 13:17-23,27; 33:33-37,40-41; 26: 6-7,22-23
    2. Alitumwa na YHWH kama alivyoahidi- Mdo. 2:23; 3:26
    3. Miujiza iliyotendeka kuthibitisha ujumbe wake na kudhihilisha huruma ya Mungu- – Mdo. 2:22; 3:16; 10:38
    4. Waliofunguliwa, wasiomilikiwa- Mdo. 3:13-14; 4:11
    5. Kusurubishwa – Mdo. 2:23; 3:14-15; 4:10; 10:39; 13:28; 26:23
    6. Alifufuliwa kuja uzimani- Mdo. 2:24,31-32; 3:15,26; 4:10; 10:40; 13:30; 17:31; 26;23
    7. Ameinuliwa mkono wa kulia wa Mungu Baba- Mdo 2:33-36; 3:13,21
    8. Atakuja tena mara ya pili – Mdo. 3:20-21
    9. Alichaguliwa kuwa hakimu- Mdo. 10:42; 17:31
    10. Akamtuma Roho Mtakatifu- Mdo. 2:17-18,33,38-39; 10:44-47
    11. Mwokozi wa kila aaminiye- Mdo. 13:38-39
    12. Hakuna mwingine aliye mwokozi- Mdo. 4:12; 10:34-36

Hapa kuna baadhi ya njia za kukubali kwenye hizi nguzo za ukweli:

1. Tubu – Mdo. 2:38; 3:19; 17:30; 26:20
2. Amini – Mdo. 2:21; 10:43; 13:38-39
3. Ubatizwe – Mdo.2:38; 10:47-48
4. Mpokee Roho – Mdo. 2:38; 10:47
5. Yote yatakujilia- Mdo.2:39; 3:25; 26:23

Mpango huu ulitumika kama tamko la kanisa la mwanzo, ingawa waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaweza kuacha sehemu au wakasisitiza wengine hasa katika maandiko yao. Injili yote ya Marko kwa karibu inafuata dhana ya mafundisho. Marko kiutamaduni anaonekana kama kuitengeneza hotuba ya Petro, iliyohubiriwa huko Roma, katika injili iliyoko kwenye maandishi. Injili zote za Mathayo na Luka zinafuata muundo wa Marko.

**3:16 "kila andiko"**Hakuna KIAMBATA. Inaweza kufasiriwa "kila andiko" (NET Bible), lakini hii inaweza kumaanisha kwa baadhi kwamba ni kweli iliyotengwa (mapendekezo). Mapigo ya mafunzo ya Biblia za kisasa "andiko lililohakikiwa" mbinu ya ukalimani ambayo inaharibu muktadha wa kifasihi na kusudio la mwandishi aliyevuviwa.

◙**"lenye pumzi ya Mungu"** Hii kibayana "iliyovuviwa na Mungu." Ni kwa namna gani na nani na kwanini viko wazi! Katika 2 Pet. 1:21 roho ni shabaha ya uvuvio, lakini hapa yupo Baba. Wote wanatenda kazi katika hili eneo!

Huu ni ukweli wa muhimu namna hiyo na kwamba ningependa kuongeza katika maoni yangu kutoka 2 Petro 1:20-21 (angalia **www.freebiblecommentary.org**.)

**1:20 "andiko"** Hii ni moja ya mistari kadhaa katika Agano Jipya ambayo inazungumza juu ya ufunuo binafsi wa Mungu na maandiko ya Agano Jipya (yaani Maandiko).

1. Mathayo 5:17-19
2. 1 Wakorintho 2:9-13
3. 1 Wathesalonike 2:13
4. 2 Timotheo 3:16
5. 1 Petro 1:23-25
6. 2 Petro 1:20-21
7. 2 Petro 3:15-16

Umuhimu wa haya yote ni kwamba maandiko yanatoka kwa Mungu na ya Mungu, sio ya kibinadamu katika asili. Mungu alivuviwa waandishi (kama vile 2 Pet. 1:20-21) na maandiko yao (kama vile 2 Tim. 3:16).

◙**"jambo la tafsiri yake mwenyewe"** Tungo hii hakika inaelezea mvutano uliopo uliosababishwa na walimu wa uongo katika makanisa. Inawezekana kwamba walikuwa wakinukuu Maandiko na hivyo kuweka akili zao juu yake (ambayo pia ni kawaida leo).

Katika muktadha ni ngumu kujua ikiwa tungo hii inarejerea kwa (1) waandishi wa Agano la Kale au (2) walimu wa uongo wa sasa. Ikiwa uamuzi wa kwanza unazungumzia dhana ya kithiolojia ya uvuvio (kama vile 2 Tim. 3:16). Mstari unaofuata unaonekana kuthibitisha ufasiri huu. Ikiwa uamuzi wa pili unazungumzia dhana ya kithiolojia (yaani kwamba Roho inaongoza waamini katika ufasiri wa Biblia).

Lazima ielezewe kwamba dhana za kiinjilisti za "ukuhani wa mwamini" siku zote inaeleweka kama uwezo utolewao na Roho kufasiri Biblia kwa ajili ya mtu mmoja. Hatahivyo Kibiblia tungo inarejerea kwa kanisa kama nguvu ya kukamilisha Agizo Kuu, kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6. Tazama katika Agano la Kale (kama vile Kut. 19:6) na Agano Jipya "ukuhani wa waaminio" iko katika WINGI (yaani jumuiya nzima), sio kwa mtu mmoja mmoja.

**1:21 "watu waliongozwa na Roho Mtakatifu"** Hii kibayana "kuchukuliwa," ambayo ni KAULI TENDWA ENDELEVU YA WAKATI ULIOPO. Hii inaongeza msisitizo kwenye kweli kwamba Biblia ni ujumbe wa Mungu, sio ujumbe wa kibinadamu! Ni kweli kwamba Biblia ni maneno ya kibinadamu lakini wanadamu walikuwa kipekee wakiongozwa na Roho. Biblia haisemi ukweli wote kwakuwa hakuna mwanadamu awezaye kuelewa kwamba kiwango cha ukweli lakini ni wa kutumainiwa, ukweli wa kutosha kuhusu Mungu juu ya dhambi kuhusu wokovu kuhusu maisha ya utauwa na kuhusu umilele.

mbinu hasa ya uvuvio inatofautiana.

1. kuthihirishwa kwa mwili
2. Urim na Thummin/nyingi
3. ndoto
4. maono
5. mzubao
6. malaika
7. matendo ya kiuwakilishi
8. matukio maalumu na ufasiri

Swali linabakia (1) je Mungu anatoa maudhui na mwandishi mwanadamu anatengeneza namna ya kuyawakilisha (2) Je Mungu anatoa vyote?"

◙**"yafaa kwa. . ."** Neno la Mungu (maandiko) yanatambuliwa kwa maneno mawili:

1. Mungu alilipulilizia uhai
2. yenye kuleta faida
    a. kwa (*pros*) mafundisho
        (1) chanya, 2 Pet. 3:10; 1 Tim. 5:17
        (2) kanushi, 2 Pet. 4:3
    b. kwa (*pros*) kukemea
    c. kwa (*pros*) kusahihisha
    d. kwa (*pros*) mafunzo (nidhamu ya mtoto, kama vile Ebr. 12:5,7,8,11) katika haki
    e. kwamba (*hina*) mtu wa Mungu awe mkamilifu, 2 Pet. 3:17
    f. akiwezeshwa kwasababu ya (*pros*) kila kazi njema, 2 Pet. 3:17

Neno "andiko" siku zote linarejerea kwa Agano la Kale. Agano la Kale linafanya kazi katika "utakaso" lakini sio "kuhesabiwa haki" (kama vile Wagalatia 3). Wokovu (kuhesabiwa haki) iko katika Kristo kupitia imani (kama vile 2 Pet. 1:14).
Mistari hii miwili ni vipengele pacha vya Agizo Kuu.

1. kuwafanya mataifa (Mt. 28:19)
2. kuwafundisha wao (Mt. 28:20)

Lazima viende vyote! Makuzi (Kufanana na Kristo) ndilo lengo!

◙**"katika haki"** Angalia Mada Maalum katika 2:12.

**3:17 "ili kwamba"** Hii ni TUNGO YA KI-KUSUDI (yaani, *hina*) ambayo inatafsiriwa "ili kwamba."

◙**"itoshayo"** Neno hili linapatikana hapa tu katika Agano Jipya. Inamaanisha "kamilifu, yenye uwezo, bingwa, au inayotosheleza kwa ukamilifu."

◙**"kuwajenga"** "enye utoshelevu" (*artios*) na "inayowezeshwa" (*exartizo*) are VITENZI TAMBUZI inayotumika kuwezeshwa kwa ajili ya kitu fulani kwa ajili ya jukumu lililotolewa (kama vile Efe. 4:12). Inazungumza juu ya kupewa karama, ikifanya kazi kwa ajili ya kukomaza (yaani kufanana na Kristo) ambayo inaletwa na Roho kupitia Maandiko (2 Tim. 3:16). Wokovu unaletwa na kazi ya Kristo na imani/mwitikio wa mwanadamu kwa kuamini (kama vile 2 Tim. 3:15).

◙**"kwa kila kazi njema"** Kile ambacho Mungu ametuitia (kama vile Efe.. 2:0), Anatuwezesha kwa ajili ya (kama vile 2 Tim. 2:21)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.
Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je tungo ya "siku za mwisho" inarejerea nini?
2. Ni walimu gani wa uongo ambao Paulo anawarejerea? Elezea kile ambacho walikiamini.
3. Orodhesha vitu tisa ambavyo Paulo anamuomba Timotheo kumuiga katika mistari ya 10-11.
4. Mistari ya 15-17 inazungumza nini juu ya uvuvio?
5. Ni kwa namna gani Neno la Uzima — Yesu linahusiana na Neno la kuandikwa — Biblia?

# 2 TIMOTHEO 4

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Shitaka la mwisho Kwa Timotheo (3:10-4:8) | Kuhubiri neno | Mchungaji na kundi la kondoo (2:14-4:5) 3:10-4:5 | Maagizo ya mwisho (3:10-4:8) 3:10-4:5 | Shutuma nzito |
| 4:1-5 | 4:1-5 | | | 4:1-5 |
| | Kuaga kwa Paulo | Ushawishi wa mwisho | | Jioni ya maisha ya Paulo |
| 4:6-8 | 4:6-8 | 4:6-8 | 4:6-8 | 4:6-8 |
| Maagizo binafsi | Mtume aliyeachwa | | Maneno binafsi | Ushauri wa mwisho |
| 4:9-15 | 4:9-16 | 4:9-15 | 4:9-13<br>4:14-15 | 4:9-15 |
| 4:16-18 | | 4:16-18 | 4:16-18 | 4:16-18 |
| | Bwana ni mwaminifu<br>4:17-18 | | | |
| Salamu za Mwisho | Uje kabla ya wakati wa baridi | | Salamu za mwisho | Kuagana na kutakiana heri |
| 4:19-22 | 4:19-21 | 4:19-21 | 4:19-21a | 4:19-21a |
| | Kuagana | | 4:21b | 4:21b |
| | 4:22 | 4:22 | 4:22a<br>4:22b | 4:22 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 4:1-5**
**1 Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; 2 lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. 3 Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; 4 nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo. 5 Bali**

**wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiliza huduma yako.**

**4:1 "Nakuagiza"** Paulo anaendelea kupanga kazi za Timotheo na kumuonya katika matendo (kama vile. 1 Tim. 5:21; 6:13; 2 Tim. 2:14; 4:1). Kumbuka hii ni nyaraka ya mwisho ya Paulo kabla hajafa (mwishoni mwa 67 B.K. au mwanzoni mwaka wa 68)!

◙ **"mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu"** Baba na Mwana wana muundo wa muunganiko wa kisarufi ambao unatilia mkazo usawa wao (tazama MADA MAALUM:UTATU katika Tito 3:6). Viongozi wa kanisa wanaishi na kutumika kwenye uwepo wa Mungu na Kristo wake.

◙ **"atakayewahukumu"** Hiki ni cheo cha Agano la kale na kazi ya YHWH imetumika hapa kwa ajili ya Yesu. Hii inaonyesha uungu wake kamili (kama vile. Mat. 25:31na kuendelea; Mdo. 10:42; 17:31; Rum. 2:16; 1 Pet. 4:5); kristo kama mwakilishi wa Baba kwenye uumbaji (kama vile. Yn. 1:3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2), hivyo pia, atakuwa mwakilishi wa Baba kwenye hukumu.

◙ **"walio hai na waliokufa"** Hii inarejelea hukumu ya Yesu kwa uumbaji wote wenye ufahamu (kama vile. Flp. 2:10). Tungo ile ile imeonekana kwenye Mdo. 10:42 na 1 Pet. 4:5. Baadhi yao watakuwa hai nyakati za ujio wa pili (kama vile. 1 Thes. 4:13-18; wengine watakuwa na Bwana (kama vile. 2 Kor. 5:8); na baadhi (waovu) watakuwa jehanamu (kama vile. Ufu. 20:13; Mat. 11:23; Luka 16:23).

## MADA MAALUM: WAFU WAKO WAPI? *(SHEOL/HADES, GEHENNA, TARTARUS)*

I. Agano la Kale
   A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol)* (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)
   B. Tabia za shimoni (*sheol*)
      1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22
      2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
      3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
      4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
      5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
      6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
      7. panahusiana na *utelekezaj*i (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa*. . .*Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
      8. panahusiana na “shimo lefu” (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
      9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*,Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
      10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
      11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
      12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11

II. Agano Jipya
   A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)
   B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheo*l)
      1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
      2. imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14

3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (*Gehenna*), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Luk 10:15; 16:23-24
4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Luk 16:23

C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)
1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Luk 23:43
2. Sehemu ya waovu iitwayo "kwenye vifungo vya giza",iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa "shimoni" Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3

*D. Gehenna*
1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, "bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalem). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YWHW (Kama vile Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.
3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza,kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
   a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk 9:43
   b. Mahali pa milele, Mk 9:48 (Mt. 25:46)
   c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
   d. panafanana na *Sheol,* Mt. 5:29-30; 18:9
   e. Panaainisha waovu kama "wana wa Jehanamu" Mt. 23:15
   f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
   g. Dhana ya *Gehenna* inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa ndo mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).
   h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41

E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (*sheol),* kuzimu(*hades)* na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa
1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezewa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

A. Agano jipya halifundishi juu ya "zinaa ya nafsi," ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa
1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili

3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla

B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo
1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
2. Ibrahamu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk 12:26-27; Luk 16:23
3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
6. Paulo anadai kuwa waumini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.
1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Heb. 4:14; 7:26
3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Heb. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)

B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).

C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemo (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia

A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*
B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

◙ **"kwa kufunuliwa kwake"** kwa dhahili hii ni *epifania*. Ni dhana ya kuwasilisha "kung'aa, angavu, mng'ao, au utukufu." Yumkini inaaksi dhana ya Agano la kale ya uwepo wa Mungu kwenye *wingu la Shekinah* la utukufu kipindi cha safari ya kutangatanga jangwani cha historia ya wana wa Israeli. Hili ni neno la sifa kwenye nyaraka za kichungaji kwa ajili ya ujio wa pili (kama vile. 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 1:10; 4:1,8; Tito 2:11,13; 3:4; 2 Thes. 2:8). Tazama mada maalumu katika Tito 2:13.
Paulo anamuonya Timotheo afanye mambo ya uhakika katika nuru kwa ukweli wa siku ya hukumu/siku ya ufufuo. Ujio wa pili unamaanisha kuwatia moyo waaminio kwenye kila umri, ingawa itakuwa dhahili kwenye kizazi kimoja pekee. Waaminio ni lazima waishi kila siku kama itakiwavyo, kama vile ndio mwisho!

◙ **"kwa ufalme wake"** hii inarejelea utawala wa Mungu kwenye mioyo ya waaminio sasa kwamba atakamilisha juu ya uumbaji wote (kama vile. Mt. 6:10). Hapa tena, ufalme wa Mungu anapewa Mwana. Yesu kristo anaelezewa kwenye kazi tatu za matukio ya siku za mwisho: (1) hakimu; (2) yeye ajae; na (3) mfalme.

## MADA MAALUM: UFALME WA MUNGU

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israel (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10;

44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masiha akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Bethelehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi (“Agano Jipya,” kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mko 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luka 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Marko 9:1; Luk 21:31; 22:16,18).

Katika usambamba wa mihitasari kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, “ufalme wa Mungu.” Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika mioyo wa watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Huu unaakisishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mt.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani., Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika mioyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). katika injili ya Yohana “uzima wa milele” ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masiha wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipya linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya mioyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19)! Waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu “uliotayari” dhidi ya “ule ambao bado” (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

**4:2 “lihubiri neno”** huu ni mfuatano wa tisa wa kwanza kwenye KAULI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Ujumbe wetu (*logos*) ni Yesu (kama vile Kol. 4:3). Yeye ni injili! Yeye ni "neno" (Yn 1:1).

◙ **“uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa”** hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU. Kwa dhahiri ni "wakati ukufaao" (*eukairōs*) na "wakati usiokufaa" (*akairōs*). Hii inaelezea “mamlaka makubwa” ya Ukristo (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Akiwa kwenye mashaka ashirikiane injili! Mara zote inafaa!

◙ **“karipia"** ni dhahili “watendao dhambi uwakemee" (kama vile 1 Tim. 5:20; Tito 1:13; 2:15).

◙ **“kemea”** Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU nyingine (kama vile. Luka 17:3; 23:40).

◙ **“kuonya"** hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU nyingine. Hii ni asili ile ile kama "tia moyo." Kemea au kuonya bila kutia moyo na uvumilivu sio Ukristo (kama vile 2 Tim. 3:10; 1 Tim. 1:16).

◙ **"kwa uvumilivu wote"** tazama muhtasari katika 1 Timotheo 1:16.

**4:3 "Maana utakuja wakati"** hii inaaksi siku za Paulo, kwa maana ya kila siku, na siku pekee za mwisho (kama vile. 2 Tim. 3:1; 1 Tim. 4:1-2).

◙ **"watakapoyakataa mafundisho yenye uzima"** maneno mengi kwenye nyaraka za kichungaji pia yanapatikana kwenye maandiko ya Paulo. Inawezekana kwamba Paulo alimtumia Luka kama mwandishi kuandika hizi nyaraka. Neno "uzima"linamaanisha "imara" na limetumiwa mara nyingi na Luka (kama vile. Luka 5:31; 7:10; 15:27, n.k.). Ni maelezo yaliyozoeleka ya mafundisho na imani kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile 1 Tim. 4:6; 6:3; 2 Tim. 1:13; 4:8; Tito 1:9,13; 2:1,2,8).

◙ **"ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe"** tungo hii inarejelea kwa walimu wa uongo (kama vile 2 Tim. 4:4) na wafuasi wao. Wanasikia kile tu wanachotaka kusikia!

◙ **"watajipatia waalimu makundi makundi"** wanapenda kusikia

1. wale wanaokubaliana nao (kama vile. Yer. 5:31)
2. wale wafundishao mambo mapya na ya kukisia
3. walimu wengi tofauti (mara nyingi huudhuria semina mpya)

**4:4 "watajiepusha . . . kuzigeukia"** neno la kwanza limetumia upotovu kwenye Tito 1:14 (kama vile. 2 Thes. 2:11) au kuacha kwenye 2 Tim. 1:15.
Neno la pili limetumika mara nyingi kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile. 1 Tim. 1:6; 5:15; 6:20; 2 Tim. 4:4). Haya yote yameonekana kwenye dhana ya Agano la kale haki kama mtawala (au sambamba); maneno yote kwa ajili ya dhambi ni ukengeufu kutoka katika mpangilio. Hawa walimu wa uongo wameacha mafundisho ya uzima na kuzigeukia hadithi!

◙ **"yaliyo kweli "** tazama mada maalum: Ukweli katika 1 Tim. 2:4.

◙ **"hadithi"** dhana hii imetumika mara nyingi kwenye nyaraka za kichungaji (kama vile. 1 Tim. 1:4; 4:7; Tito 1:14; 3:9; 2 Pet. 1:16). Inawezekana inarejelea

1. wenye ujuzi *aeons* (viwango vya kimalaika kati ya mungu mkuu na kiumbe kidogo cha kiroho chenye mwili)
2. uzao wa kimasihi wa kiyahudi
3. baadhi ya injili isiyotakatifuzwa"

Kwa ajili ya mjadala mzuri wa maana tofauti ya "hadithi"na vidokezo vyake tazama G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, uk. 219-242.

**4:5** Hii ni tofauti nyingine kati ya matendo ya Timotheo na walimu wa uongo.

**NASB** **" uwe na kiasi katika mambo yote "**
**NKJV** **"angalia mambo yote"**
**NRSV** **"mara zote uwe na kiasi"**
**TEV** **"kuwa na nidhamu katika kila hali"**
**NJB** **"kuwa imara nyakati zote"**

Hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Hii hairejelei uzuiaji wa mvinyo lakini kuwa na hasira kiasi. Tazama muhtasari kamili katika 1 Tim. 3:2.

**NASB** **"vumilia mabaya"**
**NKJV** **"vumilia mateso"**
**NRSV, TEV** **"vumilia maumivu"**

Kuna mfuatano wa KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU tatu kwenye kifungu hiki. Neno hili limetumika mara tatu kwenye 2 Timotheo (kama vile. 2 Tim. 1:8; 2:3,9; 4:5). Inarejelea kunyimwa na kuteswa kwa sababu ya kuhusika na huduma ya injili.

◙ **"fanya kazi ya mhubiri wa Injili"** hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA ISIOTIMILIFU ya pili kwenye kifungu hiki. NOMINO "uinjilisti" imetumika mara tatu pekee kwenye Agano Jipya.

1. mabinti saba wa Filipo (kama vile. Mdo 21:8)
2. kipawa cha kiongozi wa kanisa la mahali (kama vile. Efe. 4:11)
3. na hapa

Neno “injili” (*euangelion*) kwa dhahili linamaanisha "habari njema"; mwinjilisti (*euanelistēs*) ndiye anaehubiri injili. Mwinjilisti ni kipawa cha kiroho kwa kanisa (kama vile. Efe. 4:11) na uinjilisti ni uwajibikaji kwa kila mwamini (kama vile. 1 Pet. 3:15; Kol. 4:6). Waaminio sio tu kwamba wanathibitisha mamlaka ya Yesu (kama vile. Mat. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo 1:8) lakini kuishi siku kwa siku!

◙ **"timiliza huduma yako"** hii ni KAULI TENDAJI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ya tatu. Huduma ya injili bila kuwa na uinjilisti sio huduma kamili (kama vile. Kol. 4:17). Uinjilisti ni moyo wa Mungu, kusudi la sadaka ya Kristo, na kazi ya mwanzo ya Roho.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 4:6-8**
**6 Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. 7 Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; 8 baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.**

**4:6 "mimi sasa namiminwa"** hii ni KAULI TENDWA ELEKEZI YA WAKATI ULIOPO. Tungo hii imetumika kwenye Fil. 2:17 ya sadaka ya divai ya Agano la kale (kama vile. Kut. 29:40; Hes. 15:4-7,9-10; 28:7,10,14,15,24). Paulo anayaona maisha yake kama sadaka kwa Kristo.

◙ **"wakati wa kufariki kwangu umefika"** hii ni KAULI TIMILIFU ELEKEZI YA HALI YA KUENDELEA. Neno hili *analusis* (kiingereza "uchambuzi") hupatikana hapa kwenye Agano Jipya pekee, lakini muundo wa KITENZI umetumika mara kadhaa kurejelea merikebu iliyolegezwa kutoka kwenye minyororo (kama vile. Luka 12:36). Ni sitiari ya kifo kwenye Fil. 1:23. Hii ni nyaraka ya mwisho aliyoiandika Paulo kabla ya kukatwa kichwa, kati ya mwaka 67-68 B.K (Nero alijiua mwenyewe kwenye mwaka wa 68 B.K ).

**4:7 "Nimevipiga vita vilivyo vizuri"** hii moja ya KAULI TIMILIFU YA KATI ELEKEZI tatu. Paulo ametumia mwana riadha (1 Kor. 9:27; Fil. 3:13-14) na kijeshi (kama vile. Efe. 6:10-18) sitiari ya kuelezea huduma yake. Ambayo alimtia moyo Timotheo kufanya (kama vile. 1 Tim. 1:18; 6:12) alitenda mwenyewe.

◙ **"mwendo nimeumaliza"** hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI ELEKEZI YA HALI YA KUENDELEA ya pili. Paulo alijua kifo chake kimekaribia sana. Alitimiza unabii wa Anania kwenye Mdo. 9:15 (kama vile Mdo. 26:32). Alihubiri aina zote zilizotajwa na Kaisari.

◙ **"Imani nimeilinda”** Hii ni KAULI TIMILIFU TENDAJI ELEKEZI YA HALI YA KUENDELEA. Inarejelea kwa

1. mafundisho
2. uaminifu
3. mwana riadha kama sitiari ya kutunza sheria (kama vile. 1 Kor. 9:27)

**4:8 "taji ya haki"** hii yote (1) sio yetu lakini haki ya kushutumiwa kwa ajili ya Kristo, na/au (2) maisha ya waaminio kama Kristo. Neno linarejelea shada la maua la sifa kwa ushindi wa mwana riadha. Tunapata jina la kiingereza "Stephen" kutoka kwenye neno la kiyunani. Kuna taji kadhaa zinatolewa kwa waaminio wa Agano Jipya:

1. taji ya kudumu milele (1 Kor. 9:25)
2. taji ya haki (2 Tim. 4:8)
3. taji ya uzima (Yakobo 1:12; Ufu. 2:10)
4. taji ya utukufu (1 Petro 5:4)
5. taji ya dhahabu (Ufu. 4:4)

Tazama MADA MAALUM:HAKI katika Tito 2:12.

◙ **"ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki "**neno "Bwana" linaweza kutumiwa kwa YHWH kwa sababu anaitwa hakimu (kama vile. Mwa. 18:25; Zab. 5:6: 94:2; Yoeli 3:12; Ebr. 12:23; Yak 4:12) au kwa Yesu kwa sababu hukumu yake inahusiana na "kufunuliwa kwake" (kama vile. 2 Tim. 1:10; 4:1,8; 1 Tim. 6:14; Tito 2:13). YHWH amemweka Yesu kama hakimu (kama vile Mt. 25:31-46; Mdo. 17:31; 2 Kor. 5:10; tazama muhtasari katika 2 Tim. 4:1).

◙ **"atanipa siku ile"** hii ni nyakati za mwisho (matukio ya siku za mwisho) hatimaye (kama vile. 2 Tim. 1:18; 4:1). Kwa dhahili Paulo anaamini kwamba waaminio watakuwa na Bwana katika mauti (kama vile. 2 Kor. 5:8), lakini thawabu na ushirika kamili utasubulia siku ya ufufuo (kama vile. 1 Thes. 4:13-18).

◙ **"bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake"** hii inarejelea shauku ya matumaini kwa waaminio juu ya ujio wa pili wa Bwana. Hakuna hofu zaidi. Ni furaha! Ni ishara ya ukristo wa kweli!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 4:9-15**
**[9] Jitahidi kuja kwangu upesi. [10] Maana Dema aliniacha, akiupenda ulimwengu huu wa sasa, akasafiri kwenda Thesalonike; Kreske amekwenda Galatia; Tito amekwenda Dalmatia. [11] Luka peke yake yupo hapa pamoja nami. Umtwae Marko, umlete pamoja nawe, maana anifaa kwa utumishi. [12] Lakini Tikiko nalimpeleka Efeso. [13] Lile joho nililoliacha kwa Karpo huko Troa, ujapo ulilete, na vile vitabu, hasa vile vya ngozi. [14] Iskanda, mfua shaba, alionyesha ubaya mwingi kwangu; Bwana atamlipa sawasawa na matendo yake. [15] Nawe ujihadhari na huyo, kwa sababu aliyapinga sana maneno yetu.**

**4:9 "Jitahidi kuja kwangu upesi"** Paulo alikuwa mpweke (kama vile 2 Tim. 4:21; Tito 3:12) na inawezekana alikuwa na matatizo la macho (kama vile. 2 Kor. 12:7), ambayo ilikua vigumu kwake kuwa peke yake.

**4:10 "Dema aliniacha"** muktadha wa kihistoria wa Paulo akiwa gerezani, mapema kabla hajakatwa kichwa, yumkini alielezea matendo ya Dema. Inatia mashaka kwa namna gani kuachwa kwa Paulo kunasimulia imani yake kwa Kristo.

**4:10 "akiupenda"** KITENZI hapa (KAULI TENDAJI ENDELEVU YA WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU) ni *agapaō*. VITENZI *agapaō* na *phileō* ni visawe kwenye Agano Jipya (muhtasari wa Yohana 3:35; 5:20; 11:3,5).

◙ **"ulimwengu huu wa sasa"** hii ni wazi "wakati huu wa sasa". Tazama mada maalum katika 1 Tim. 6:17. Dema mara moja alichagua umilele. Uvutaji huu wa dunia ni mkubwa mno, lakini ni wa kupita tuu (kama vile. 1 Yn 2:15-17).

◙ **"akasafiri kwenda Thesalonike"** linganisha Filemoni 24 na Mdo. 20:4. Artistarko na pia inawezekana Dema alitoka Thesalonike.

◙ **"Kreske amekwenda Galatia"** kuna machapisho mbalimbali ya Kiyunani yanayohusika na safari ya Kreske.

1. Asia ndogo (Uturuki magharibi) Galatia jimbo la Rumi (kama vile. MSS A, D, F, G)
2. kusini mwa Ufaransa, baadae ikaitwa Gaul (Galatia, kama vile. MSS א, C)
3. Galilaya ya Palestina (kama vile Vulgate, Coptic, na Armenian versions)

Toleo la United Bible Societies' fourth (UBS[4]) la *The Greek New Testament* linatupatia "Galatia" (#1) “B" inamaanisha daraja la kawaida. Ikiwa #2 inasaidia jambo kwamba Paulo alitembelea mashariki mwa Mediterrania.

◙ **"Tito amekwenda Dalmatia"** alikuwa mmoja wa wawakilishi waaminifu wa kitume wa Paulo (kama vile. Kor. 3:2; 7:6; 12-12; 8:6,16,23; 12:18; Gal. 2:1,3; Tito 1:4). Dalmatia lilikuwa ni jimbo la Rumi mashariki mwa eneo la Illyricum (kama vile. Rum. 15:19, Yugoslavia ya zamani). Paulo alihubiri huko kwenye Mdo. 20:1. Ni kaskazini mwa Makedonia. Hii ni kazi ya mwisho ya Tito tunaisikia kwenye Agano Jipya.

**4:11 "Luka"** alikuwa ni daktari wa mataifa (kama vile. Kol. 4:14; FilemonI 1:24 na “sisi" sehemu za Matendo ya mitume). Inawezekana kwamba neno daktari yumkini likamaniisha "mwenye elimu." Ni mwandishi pekee wa Agano Jipya asiyekuwa myahudi (yaani.,injili ya Luka, Matendo ya mitume, na inawezekana mwandishi wa nyaraka za kichungaji).

◙ **"Marko"** huyu ni Yohana Marko, ambae yumkini kalamu ya mwisho ilifanyikia kwenye nyumba yake (kama vile. Mdo 12:12). Aliambatana na akina Paulo na Barnaba kwenye safari ya kwanza ya umisionari, lakini kwa baadhi ya sababu hakuambatana nao (kama vile. Mdo 15:38). Paulo na Barnaba walikuwa na mabishano juu ya kumwongeza Marko kwenye safari ya pili, matokeo ni kugawanyika kwa timu mbili (kama vile Mdo. 15:36-41). Paulo na Yohana Marko baadae walipatana (kama vile. Kol. 4:10).

**4:12 "Tikiko"** Efeso lilikuwa ni kanisa na mji ambao Paulo alitumia muda mwingi na kutia moyo. Timotheo alikuwa Efeso wakati Paulo anaandika 1 Timotheo. Tikiko alikuwa ni mjumbe wa kuaminika kwa Paulo (kama vile. Mdo 20:4; Kol. 4:7; Efe. 6:21; Tito 3:12) ambae inawezekana alibeba mzigo wa 2 Timotheo kwa Timotheo na inawezekana alikuwa mbadala wa Timotheo.

**4:13 "joho"** hili lilikuwa ni vazi zito, kubwa lililotumika kama koti na pia kama mfuko wa kulalia nyakati za kipupwe.

◙ **"Troa"** huu ulikuwa ni mji wa bandari kwenye pwani ya magharibi wa Uturuki ya sasa. Ilikuwa ni sehemu ya “Maono kwa Makedonia”ya Paulo yaliyoandikwa kwenye Mdo. 16:6-10. Ni dhahili Paulo aliimarisha kazi kule kwa wakati mmoja.

◙ **"na vile vitabu, hasa vile vya ngozi"** hata Paulo alihisi anahitaji kusoma na kujifunza. Hii "ngozi" inarejelea ngozi ya shaba ya mnyama ambayo ilitumika kwa ajili maandishi. Majina yake yamechukuliwa kutoka Pergamum yalipokuwa yakitengenezwa. Hii ilikuwa ni ghali sana lakini imara kwa ajili ya maadishi. Inawezekana yakarejelea magombo ya Agano la kale. "Vitabu" yumkini vikarejelea nyaraka au hati halali. Hata hivyo, hii yote ni makisio.

**4:14 "Iskanda"** hili ni jina lililozoleka, hivyo hatuna uhakika kama alikuwa ni yeye
1. Mtu mwingine ametajwa kwenye Mdo. 19:33-34
2. mwalimu wa uongo ametajwa kwenye 1 Timotheo 1:20, pamoja na Hymenaeus
3. Iskanda mwingine asiyefahamika

Yeye ni mfano mwingine wa kinyume na injili, kama ndani ya kanisa au nje.

◙ **"Bwana atamlipa sawasawa na matendo yake"** Hii ni kanuni ya kiroho. Mungu ni mwenye haki na maadili na hivyo hata uumbaji wake. Mwanadamu aliharibu mwenyewe kanuni za Mungu. Tunavuna tulichopanda. Huu ni ukweli kwa ajili ya waaminio (lakini hauathiri wokovu) na wasioamini (kama vile. Ayu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mit.

24:12; Mhu. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; 1 Kor. 3:8; Gal. 6:7-10; 2 Tim. 4:14; 1 Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12).

◙ **"Nawe ujihadhari na huyo"** Hii ni KAULI YA KATI SHURUTISHI YA WAKATI ULIOPO. Kuwa imara na makini. Mwovu yupo na makosa! Yote yanakuja kutoka ndani na nje!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 4:16-18**
**16 Katika jawabu langu la kwanza hakuna mtu aliyesimama upande wangu, bali wote waliniacha; naomba wasihesabiwe hatia kwa jambo hilo. 17 Lakini Bwana alisimama pamoja nami akanitia nguvu, ili kwa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu, hata wasikie Mataifa yote; nami nikaokolewa katika kinywa cha simba. 18 Bwana ataniokoa na kila neno baya, na kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni. Utukufu una Yeye milele na milele. Amina.**

**4:16 "Katika jawabu langu la kwanza"** Kutoka kwenye neno hili la kiyunani, *apologia*, tunapata neno la kiingereza "(msamaha) apology."Limetumika kwenye maana ya kibali cha ulinzi (kama vile. Mdo 19:33; 22:1; 26:1,2,24). Paulo alijihami, akajieleza, na kuitangaza injili kwenye utaratibu halali mara kadhaa, katika Palestina na Rumi kote (kama vile. Mdo. 9:15).

◙ **"hakuna mtu aliyesimama upande wangu, bali wote waliniacha"** Hii yumkini imeelezwa katika 2 Tim. 4:10. Kama mioyo iliyoyeka ya wafuasi wa Yesu baada ya kukamatwa kwake, hivyo pia, wasaidizi wa Paulo walianza kuwa na hofu na wakamwacha (yaani., Dema).
Kwenye baraza la kirumi siku za Paulo kulikuwa na uchunguzi wa mwanzo wa makosa kabla ya hukumu kutolewa. Ni dhahili kwenye huu utaratibu hakuna hata mmoja aliyeshuhudia badala ya Paulo.
Kuna masimulizi ya Kiyunani ya NJEO ya VITENZI.
1. WAKATI USIOTIMILIFU – MSS A, C, D[2,3], F, G, L
2. WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU – MSS א, D[*] (kwenye andiko la UBS[4] )

Fasiri ya andiko la Bruce Metzger (uk. 649) imetaja kwamba utata huu huu unapatikana kwenye 2 Tim. 4:10,13, na 20.

◙ **"naomba wasihesabiwe hatia kwa jambo hilo"** Paulo anaaksi maneno ya Yesu kutoka pale msalabani (kama vile. Luka 23:34) na maneno ya Stefano kwenye Mdo. 7:60, lakini tambua pia kuhusika kwa tungo kwenye 2 Tim. 4:14.

**4:17 "Lakini Bwana alisimama pamoja"** Yesu aliahidi kuwa pamoja nasi kwenye Mt. 28:20. KITENZI kile kile kimetumika kumtia moyo Paulo kwa uwepo wa kiroho kwenye Mdo. 23:11 na 27:23 (tambua pia Mdo 18:9).

◙ **"akanitia nguvu"** Paulo mara nyingi amezungumza Kristo akimtia nguvu (kama vile. Efe. 3:16; Flp. 4:13; Kol. 1:11; 1 Tim. 1:12; 2 Tim. 2:1).

◙ **"ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu"** Paulo alitumwa kama mtume kwa mataifa (kama vile. Mdo 9:15; 22:21; 23:11; 26:17; Rum. 1:5; 11:13; 15:16; Gal. 1:16; 2:7; Efe. 3:1-8; 1 Tim. 2:7).

◙ **"nami nikaokolewa katika kinywa cha simba"** tangu Paulo, kama raia wa Kirumi, hakuweza kutolewa auawe na wanyama wa mwituni, hii inaweza kuwa ni Nahau ya Agano la kale kwa ajili ya (1) Mungu kuwakomboa waaminio kutoka kwa maadui zao au (2) Mungu kuwakomboa kutoka katika kifo. Soma Zaburi 7:2; 22:21 na 35:17. Inawezekana mashitaka ya Paulo yaliisha bila hukumu.
Mara kadhaa kwenye Agano Jipya watu wameelezewa kama wanyama.
1. Mathayo 10:16
    a. waaminio – kondoo, nyoka, na hua

   b. wasioamini –mbwa mwitu
2. Luka 13:32 – Herode kama bweha
3. Mt. 15:26-27; Fil. 3:2; 2 Pet. 2:22; Ufu. 22:15 – mbwa wametumika kwa ajili ya mataifa, walimu wa uongo, wasioamini

**4:18 "Bwana"** Kwenye mstari huu (na 2 Tim. 4:14), hii inarejelea kwa YHWH, lakini kwenye mstari wa 17 (na 2 Tim. 4:1) inarejelea kwa Yesu. Yesu ni chaguo bora zaidi katika matukio yote kwenye sura ya 4.

**NASB " ataniokoa na kila neno baya "**
**NKJV "atanikomboa kutoka kila kazi mbaya"**
**NRSV "ataniokoa kutoka kila shambulio la mwovu"**
**TEV "ataniokoa na kila mwovu"**
**NJB "ataniokoa kutoka majaribu ya mwovu"**

Paulo alitambua ya kwamba Bwana yuko pamoja nae, kwa ajili yake, na ndani yake. Pia alitambua kwamba mwanadamu aliye kinyume ana shetani au asili ya kipepo (kama vile. Efe. 6:10-19). Tangazo la injili mara zote huambatana na upingaji wa uovu!
Tungo hii inavutia zaidi na fumbo la maneno ambalo limejitokeza kwa ukaribu kunyongwa kwa Paulo!

◙ **"kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni"** tazama MADA MAALUM:ENZI HII NA ENZI IJAYO katika 2 Tim. 3:1.

◙ **"Utukufu una Yeye milele na milele"** Paulo mara nyingi alimalizia kwa kusifu (yaani.,mifano miwili mizuri, Rum. 11:36; Efe. 3:14-21).

◙ **"Amina"** tazama mada maalum katika Tito 2:12.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 4:19-21**
**[19] Nisalimie Priska na Akila, na wale wa nyumbani mwa Onesiforo. [20] Erasto alikaa Korintho. Trofimo nalimwacha huko Mileto, hawezi. [21] Jitahidi kuja kabla ya wakati wa baridi. Eubulo akusalimu, na Pude, na Lino, na Klaudia, na ndugu wote pia.**

**4:19 "Priska na Akila"** mwanamke huyu (pia aliitwa Priscilla) ametajwa kwa mara ya kwanza kwenye Mdo 18:18,26; Rum. 16:3 na hapa; mme wake ametajwa kwa mara ya kwanza kwenye Mdo. 18:2 na 1 Kor. 16:19. Inawezekana mwanamke ametajwa kwanza, ambaye kwa kiwango cha juu, kwa sababu alikuwa ni Mrumi mwema. Yumkini alikuwa ni mwenza imara sana. Walikuwa ni watengeneza mahema (au wafanyakazi wa ngozi) kama Paulo na walikuwa ni marafiki wema na watenda kazi kwenye injili.

◙ **"Onesiforo"** tazama muhtasari katika 2 Tim. 1:16-18.

**4:20 "Erasto"** jina hili hili pia limetumika kwenye Mdo. 19:22 na Warumi 16:23, lakini inawezekana asiwe mtu mmoja Yule yule.

◙ **"Trofimo nalimwacha, hawezi"** mtu huyu ametajwa kwenye Mdo. 20:4; 21:29 na inawezekana kwenye 2 Kor. 8:19-22.
Kuna maswali mengi sana tunapenda kuwauliza waandishi wa Agano Jipya. Jambo moja ambalo waaminio wanafikiria juu ya uponyaji wa mwili. Kwenye Mdo. (kama vile. Mdo. 19:12; 28:7-9) Paulo alikuwa na uwezo wa kumponya, lakini hapa na kwenye 2 Kor. 12:7-10 na Fil. 2:25-30, inaonekana kutoweza. Kwa nini baadhi waliponywa na sio wote, na je kulikuwa na uhusiano wa muda wa kufungwa kwa dirisha la uponyaji?

Kwa hakika naamini kwenye nguvu za Kimungu, Baba mwenye huruma aponyae mwili kama vile roho, lakini kwa nini kipengele hiki cha uponyaji kinaonekana sasa na kiko wazi wakati uliopita? Sifikilii kwamba inamuunganiko na imani ya mwanadamu, kwa hakika Paulo alikuwa na imani (kama vile. 2 Kor. 12). Nahisi kwamba uponyaji na kuamini miujiza inathibitisha uaminifu na uhalali wa injili, ambao bado ungali ukitenda ulimwenguni pale unapotangazwa kwa mara ya kwanza. Hata hivyo, nahisi kwamba Mungu anatutaka tuenende kwa imani na sio kwa kuona. Pia, magonjwa ya kimwili mara nyingi yameruhusiwa kwenye maisha ya waaminio;

1. kama adhabu ya muda kwa ajili ya dhambi
2. kama matokeo ya maisha kwenye ulimwengu ulioanguka
3. ili kuwasaidia waaminio makuzi ya kiroho

Tatizo langu ni vigumu kuelewa ni ipi inahusika! Maombi yangu kila jambo lifanyike kwa ajili ya mapenzi ya Mungu sio kwa ukosefu wa imani, lakini anajalibu kuruhusu neema, kazi ya huruma ya Mungu itatenda kwenye kila maisha.

◙ **"huko Mileto"** huu ni mji wa bandari magharibi mwa Asia ndogo (magharibi mwa Uturuki), kusini mwa Efeso.

**4:21 "Jitahidi kuja kabla ya wakati wa baridi"** Paulo alikuwa mpweke na ni dhahili alikuwa na matatizo ya macho. Usafiri ulisimaa nyakati za baridi, hivyo hakuna hata mmoja angeweza kwenda kwake baada ya kuanza majira ya dhoruba (kama vile. Tito 3:21).

◙ Hatukufahamu chochote juu ya hawa waaminio kutoka sehemu zingine za Agano Jipya. Oh, lakini Mungu alitenda!
Kuna utamaduni wa kanisa la mwanzo (yaani orodha ya makasisi wa Rumi kutoka Irenaeus) kwamba mtu aitwaye "Linus" alikuwa ni kiongozi wa kanisa huko Rumi mwishoni mwa miaka ya 60 hadi mwishoni wa miaka ya 70.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 TIMOTHEO 4:22**
***22*** **Bwana na awe pamoja na roho yako. Neema na iwe pamoja nanyi.**

**4:22** Hii ni dhahili iliandikwa kwa mkono wa Paulo kuonyesha asili ya nyaraka (kama vile. 2 Thes. 2:2; 3:17).

◙ **"Bwana"** toleo la NKJV lina "Bwana Yesu Kristo," inafuatia toleo la MSS א[2], C, D, K, L, P, na maandiko mengi madogo na tafsiri. Muundo kamili kama huu umejitokeza kwenye toleo la KJV, 2 Tim. 4:1. Toleo la UBS[4] lina kiasi cha andiko fupi "B" (kwa uhakika), inafuatia toleo la MSS א[*], F, G, na Kilatini cha kale na tafsiri za Koptiki.
Kuna utata wa dhahili kwa baadhi ya waandishi kwenye jina hili. Toleo la MS A lina "Bwana Yesu," ambalo pia linapatikana kwenye baadhi Kilatini cha kale na tafsiri za Vulgate. Kwa jambo hili, sentensi ya mwisho ina miundo nane kwenye machapisho ya Kiyunani (fasiri ya maandiko ya Metzger, uk. 651).

◙ **"awe pamoja na roho yako"** KIWAKILISHI hiki "yako" ni UMOJA, inarejelea kwa Timotheo (kama vile. Filemoni 1:25). Hapa neno "roho" ina "r" ndogo inarejelea kwa Timotheo.

## MADA MAALUM: ROHO (*PNEUMA*) KATIKA AGANO JIPYA

Neno la Kiyunani "roho" limetumika katika njia mbali mbali kwenye Agano Jipya. Hapa kuna baadhi ya maelezo yenye upambanuzi na mifano.

A. Mungu wa Utatu (tazama Mada Maalumu: Utatu)
   1. wa Baba (kama vile Yohana 4:24)
   2. wa Mwana (kama vile Rum. 8:9-10; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11)
   3. wa Roho Mtakatifu (kama vile Marko 1:11; Mt. 3:16; 10:20; Yohana 3:5,6,8; 7:39; 14:17; Matendo 2:4; 5:9; 8:29,35; Rum. 1:4; 8:11,16; 1 Kor. 2:4,10,11,13,14; 12:7)
B. wa nguvu ya maisha ya mwanadamu

1. wa Yesu (kama vile Marko 8:12; Yohana 11:33,38; 13:21)
2. wa mwanadamu (kama vile Mat. 22:43; Matendo 7:59; 17:16; 20:22; Rum. 1:9; 8:16; 1 Kor. 2:11; 5:3-5; 7:34; 15:45; 16:18; 2 Kor. 2:13; 7:13; Flp. 4:23; Kol. 2:5)
3. mambo ambayo Roho huzalisha ndani na kupitia roho za wanadamu
    a. isiyo roho ya utumwa dhidi roho ya kuasili - Rum. 8:15
    b. roho ya unyenyekevu – 1 Kor. 4:21
    c. roho ya imani – 2 Kor. 4:13
    d. rohoa ya hekima na ufunuo katika maarifa Yake – Efe. 1:17
    e. isio roho ya woga dhidi ya nguvu, pendo, na heshima – 2 Tim. 1:7
    f. roho ya ukengeufu dhidi ya roho ya ukweli – 1 Yohana 4:6

C. wa ulimwengu wa kiroho
1. viumbe vya kiroho
    a. walio wazuri (yaani, malaika, kama vile Matendo 23:8-9; Ebr. 1:14)
    b. walio waovu (yaani, pepo wabaya, kama vile. Mt. 8:16; 10:1; 12:43,45; Matendo 5:16; 8:7; 16:16; 19:12-21; Efe. 6:12)
    c. pepo (kama vile Luka 24:37)
2. roho ya utambuzi (kama vile Mt. 5:3; 26:41; Yohana 3:6; 4:23; Matendo 18:25; 19:21; Rum. 2:29; 7:6; 8:4,10; 12:11; 1 Kor. 14:37)
3. mambo ya kiroho (kama vile Yohana 6:63; Rum. 2:29; 8:2,5,9,15; 15:27; 1 Kor. 9:11; 14:12)
4. karama za kiroho (kama vile 1 Kor. 12:1; 14:1)
5. uvuvio wa Roho (kama vile Mt. 22:43; Luka 2:27; Efe. 1:17)
6. Viungo ya kiroho (kama vile 1 Kor. 15:44-45)

D. uainishaji
1. mtazamo wa ulimwengu (kama vile Rum. 8:15; 11:8; 1 Kor. 2:12)
2. mchakato wanadamu wa kufikiri (kama vile Matendo 6:10; Rum. 8:6; 1 Kor. 4:2)

E. wa ulimwengu wa kimwili
1. wingu (kama vile Mt. 7:25,27; Yohana 3:8; Matendo 2:2)
2. pumzi (kama vile Matendo 17:25; 2 The. 2:8)

Ni dhahiri kwamba neno hili linapaswa kufasiriwa katika upande wa mazingira ya sasa. Kuna maana mbalimbali ya vivuli ambavyo vinaweza kurejerewa (1) ulimwengu wa kiroho; (2) ulimwengu usioonekana; (3) pamoja na watu wa ulimwengu huu wa kiroho au ulimwengu dhahiri.

Roho Mtakatifu ni sehemu ile ya Utatu ambaye ni mtendaji mkuu katika hatua hii ya historia. Enzi mpya za Roho zimekuja. Vyote vilivyo vizuri, vitakatifu, vya haki, na vinavyohusiana Naye kweli kweli. Uwepo Wake, karama, na huduma ni muhimu katika ukuzaji wa injili na mafanikio ya Ufalme wa Mungu (kama vile Yohana 14 na 16). Havutii upande wake Mwenyewe, bali kwa Kristo (kama vile Yohana 16:13-14). Anasadikisha, hushawishi, hubatiza, anabatiza, na anawakomaza waamini wote (kama vile Yohana 16:8-11).

◙ **"Neema na iwe pamoja nanyi"** KIWAKILISHI hiki "nanyi" ni WINGI. Ingawa nyaraka zote za kichungaji zinamwelezea kila mmoja, zilimaanisha zisomwe kwa sauti kwenye makanisa ya nyumbani (kama vile. 1 Tim. 6:21; Tito 3:15).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Uinjilisti ni nini?
2. Je kila Mkristo ni shahidi kwa maneno?

3. Je mistariya 5-8 inadokeza kwamba alitarajia kufa?
4. Ni nini kilitokea kwa Dema?
5. Kwa nini Paulo hakumponya Trofimo?
6. Kwa nini sentensi ya mwisho ya kitabu ni wingi?

# TAFASIRI SAHIHI ZA ISTILAHI ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexanda mkuu (336-323 K.K) na ikadumu mpaka miaka ya (300 K.K-B.K 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

## I. NJEO

A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa “utimilifu” au “utoutimilifu”
   1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
   2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.

B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
   1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
   2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
   3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
   4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
   5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
   6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno “okoa.” Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- “okolewa” (Rum 8:24)

2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- “ameokolewa na matokeo yake yanaendelea” (Efe 2:5,8)
3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (cf. 1Kor 1:18; 15:2)
4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (cf. Rum 5:9,10; 10:9)

C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
   1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
   2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
   3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
   4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “ Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt.3:5)
   5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale….wata...”(Mt. 5:4-9).

## II IRABU

A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
   1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
   2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
   3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
   4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;

1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: "kajiangika mwenyewe" (Mt 27:5)
2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: "shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru" ( 2 Kor 11:14)
3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: "walishauliana wao kwa wao" (Mt 26:4)

## III. DHAMIRA (au "NAMNA")

A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI Y A UCHAGUZI).

B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna <u>pekee</u> ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.

C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno "ingalikuwa", "ingaliweza", "yawezekana" au "yenye uwezo".

D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. "yawezekana isiwe" (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano (kama vile Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1 Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes. 1:38, 20:16, Mdo. 8:20 na 1Thes. 3:11

E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.

F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.

G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au "kisichotambulika" cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993
D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

## V. NOMINO

A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.

B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;

1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI "kuwa" au "kufaa"
2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, "aina gani?" mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza "ya/za"
3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza "kutoka".
4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ya".
5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza "ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na"
6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno "kwa" au "enye"
7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali "kwa umbali gani" au "kwa namna gani"
8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

## VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.

B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament

1. Viunganishi vya wakati
   (a) *epei, epedē,hopote, hōs, hote, hotan (*TEGEMEZI)- "lini"
   (b) *heōs- "*wakati"
   (c) *hotan, epan (*TEGEMEZI)- "kila, wakati wowote"
   (d) *heōs, achri, mechri (*Tegemezi)- "mpaka"
      a. *priv (*kitenzijina)- "kabla"
      b. *hōs*- "tangu", "lini", "kama".
2. Viunganishi venye mantiki
   a. Kusudi/dhumuni
      1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs (*TEGEMEZI) *hōs*- "ya kwamba", "kuwa"

2) *hōste(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- "kuwa"
3) *pros(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- "kuwa"

b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
   (1) *hōste(*ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- "ili kwamba", "hivyo"
   (2) *hiva(*TEGEMEZI)- "ya kwamba"
   (3) *ara-* "kwa kiasi hicho"

c. Chanzo au sababu
   1) *gar(*chanzo/athari au sababu/hitimisho)- "kwa", "kwa sababu ya"
   2) *dioti, hotiy- "*kwa sababu ya"
   3) *epei, epeidē, hōs-* "tangu"
   4) *dia(*ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- "kwa sababu ya"

d. Maamuzi
   (1) *ara, poinun, hōste-* "kwa hiyo"
   (2) *dio(*KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- "kwa sababu ipi", "kwa nini", "kwa hiyo basi"
   (3) *oun- "*kwa hiyo basi", "kwa kiasi hicho", "hatimaye", "hivyo basi"
   (4) *tinoun-* "kufuatana na"

e. –a kinyume au tofauti
   (1) *alla(* yenye KINYUME thabiti)-"lakini", "isipokuwa"
   (2) *de- "*lakini", "ingawa", "bado", "kwa upande mwingine"
   (3) *kai- "lakini"*
   (4) *mentoi, oun- "ingawa"*
   (5) *plēn-* "hata hivyo" (haswa katika Luka)
   (6) *oun- "ingawa"*

f. Ulinganifu
   (1) *hōs,kathōs (*ingiza vishazi linganifu)
   (2) *kata(*kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper)*
   (3) *hasos(*katika Kiebrania)
   (4) *ē- "kuliko"*

g. Enye mlolongo au mtiririko
   (1) *de- "*na", "sasa"
   (2) *kai- "*na"
   (3) *tei-* "na"
   (4) *hina, oun- "*kile"
   (5) *oun- "*kasha"(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo
   a. *alla- "*kwa hakika", "naam", "kwa kweli"
   b. *ara- "*hakika", agharabu", "kweli"
   c. *gar- "*lakini kweli", "agharabu", "hakika"
   d. *de- "*hakika"
   e. *ean- "*hata"
   f. *kai*- "hata", "hakika", "kweli"
   g. *mentoi- "*hakika"
   h. *oun*- "kweli", "kwa hali zote"

VII.

A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.

B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno "kama." Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa "tangu"(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)

C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa "inayopingana na ukweli". Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
   1. "kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng'ang'ania yeye, lakini hawezi (Thes. 7:39)
   2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
   3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)

D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi "hiki". Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16

E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

## VIII. VIZUIZI

A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: "msijiwekee hazina yenu duniani…………"(Mt. 6:19); "msisumbukie maisha yenu………." ( Mt. 6:25); "wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi……."(Rum. 6:13); "wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe. 4:30) na "tena msilewe kwa mvinyo…………………"(Efe. 5:18)

B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa "udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo" baadhi ya mifano: "msidhani ya kuwa…….."(Mt. 5:17); "msisumbuke………"(Mt. 6:31); "msiuonee haya……….."(2Tim 1:8)

C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. "kamwe, katu" au "kwa hali yeyote ile". Baadhi ya mifano: "kamwe, hataonja mauti………"(Yoh. 8:51); "hakika, kamwe……….."(1Kor 8:13)

IX

A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno "wale, Yule,ile" kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya "muonyeshwaji", ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda

1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: "Mungu ni Roho" Yoh 4:24, "Mungu ni nuru" 1Yoh 1:5; "Mungu ni upendo" 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno "a" herufi ya kwanza ya alfabeti au "an" mbadala wa "a" kwenye irabu zinazoanza na herufi kama "e", "h". Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
   1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
   2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

## X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
   1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
      a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
      b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
      c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
   2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
      a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) SIFA
      b. VITENZI elekezi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) KISHAMILISHI
         (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
         (5) KIRAI HUSISHI
      c. Virai vya NOMINO
         (1) NOMINO
         (2) KIVUMISHI
         (3) KIRAI HUSISHI
   3. Mpanglio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
      a. "walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika" (Gal 2:9) kirai "mkono wa kuume wa shirika" imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
      b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.

c. "ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi" (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na

1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: "mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe……."(Mt 28:20)
2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
   a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
   b. Yohana 14:1 (maada mpya)
   c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
   d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: "usifiwe utukufu wa neema yake" (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
   a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama "lala" kwa kifo (Yoh 11:11-14) au "nyayo" kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)
   b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama "ufalme wa mbingu" (Mt 3:21) au "sauti toka mbinguni" (Mt 3:17)
   c. Maumbo ya hotuba
      (1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)
      (2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)
      (3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)
      (4) Kejeli (Gal 5:12)
      (5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)
      (6) Mvumo unaokaa kati ya maneno
         (a) "kanisa"
            i. "kanisa" (Efe 3:21)
            ii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)
            iii. "Kuitwa" (Efe 4:1,4)
         (b) "huru "
            i. "Mwanamke huru" (Gal 4:31)
            ii. "uhuru" (Gal 5:1)
            iii. "huru" (Gal 5:1)
   d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana
      (1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno "chakula" (Yoh 4:31-34)
      (2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno "hekalu" (Yoh 2:19; Mt 26:61)
      (3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno "chukia" (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)
      (4) "wote" dhidi ya "wengi". Linganisha Isa. 53:6 ("wote") na 53:11 & 12 ("wengi"). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.
5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: "Bwana Yesu Kristo".
6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*
   a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa "sawa"
   b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- "mwenyewe jinsia ya ME" "mwenyewe jinsia ya KE" au "yenyewe/chenyewe"

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:
    1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.
    2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa "neno kwa neno" (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na "mfanano wa karibu" (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)

       Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.
    3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).
    4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.
        a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901
        b. Young's Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.
Mhutasari ufuatao utahusika

I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
   A. Agano la Kale
   B. Agano Jipya
II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya "maoni dhaifu" pia yanaitwa "uhakiki wa maandiko"
III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye

I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale
1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na "Herufi Aristeas." Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao " Esene". Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
   a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, "Kama vile wengi watakavyo shangazwa <u>Naye</u>."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, "Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa <u>Nawe</u>."
      (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
         (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, "hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye"
         (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, "hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi"
   b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
      (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, "ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama."
      (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, "ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana……"
   c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
      (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), "Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.''

(2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), "Ataona —ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki."

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili A.D., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania א (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya"Maandishi ya Kialekzandria."
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alexandrianus, kijulikanacho kama "A" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alexandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama "B" au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya "Maandishi ya Kialekzandria."
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama "C" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama "D" au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama "Maandishi ya Magharibi." Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
   a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
      (1) $P^{75}$,$P^{76}$ ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
      (2) $P^{46}$ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
      (3) $P^{72}$(yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
      (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
      (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
      (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni א,C, L, W, 33
   b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
      (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
      (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
      (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsri za kale za Kisiria
      (4) Andiko D la Machapisho ya kale "Bezae" ilifuata aina ya maandishi haya
   c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
      (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS

(2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
(3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
(4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya

d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
(1) kwanza inaonekana katika Mrko tu
(2) baadhi ya shuhuda zake ni $P^{45}$ na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea
1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
(1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
(2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
2. makusudi
a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)
1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
*a.* kitabu cha J. Harold Greenless, *Inroduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia" (uk. 68).

*b.* W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* ( Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo "angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri." Criswell alisema "Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa…Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza…" Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa "kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu" pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda ( Mt. 27 na Matendo 1): "Ni maoni tofauti ya kujinyonga," Criswell alisema "Kama iko katika Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia."Criswell aliongeza, "Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu…"

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)
   A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi
      1. *Biblical Critcism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
      2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
      3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

# FAHARASA

**Uasilishaji.** Hili ni moja kati ya maoni ya kale ya uhusiano wa Yesu na Uungu. Kimsingi inadai kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida kwa kila namna na alichukuliwa na Mungu kwa kazi maalumu katika ubatizo wake (Mt. 3:17; Marko 1:11) au katika ufufuo Wake (kama vile Rum.1:4).Yesu aliyaishi maisha haya kama mfano ambao Mungu, kwa kiasi chake, (ubatizo, ufufuo) uliyomuasilisha Yeye kama "mwana" Wake (Rum.1:4 Flp. 2:9). Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na maoni ya watu wa karne ya nane. Badala ya Mungu kuwa mwanadamu (umbo la kibinadamu) akalirejeresha hili na sasa mwanadamu anakuwa Mungu!
Ni vigumu kusema namna gani Yesu, Mungu Mwana, Uungu uliokuwepo kabla alivyozawadiwa au kuwa mbadala kwa ajili ya maisha yenye mfano. Kama Yeye alikuwa tayari ni Mungu, ni kwa namna gani Yeye alitolewa kama zadiwa? Kama Yeye alikuwa na utukufu wa Kiungu wa awali ni kwa namna gani Yeye angeliheshimiwa zaidi? Ingawa ni vigumu kwetu sisi kutambua, kwa namna Baba alivyomuheshimu Yesu katika dhana maalumu ya ukamilifu Wake wa kuyatimiza mapenzi ya Baba.

**Shule ya Alexandria.**Njia hii ya ukalimani wa kibiblia ilikuzwa katika Alexandria, Misri katika karne ya pili B.K. Inatumia misingi ya kanuni za ukalimani ya Philo, ambaye alikuwa mfuasi wa Pilato, mara nyingi inaitwa njia ya kiistiari. Ilitawaliwa katika kanisa hadi wakati wa Marekebisho. Watetezi wake zaidi walikuwa Origen na Augustine. Tazama Moisea Silva, *Has The church Misred The Bible?* (Academic, 1987)

**Ufuasi wa Alexandria.**Haya ni machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano kutoka mji wa Alexandria, Misri ikijumuisha Agano la Kale, lililothibitishwa, pamoja na Agano Jipya. Ni moja ya ushahidi wetu mkubwa katika Agano Jipya zima la Kiyunani (isipokuwa sehemu za kitabu cha Mathayo, Yohana, na II Wakorintho). Wakati ambapo machapisho haya, ambayo yanapewa alama "A, na machapisho ya alama "B" (ya Vatican) yanaafiki juu ya usomaji unaofikiriwa kuwa ya mwanzo na baadhi ya wasomi.

**Istiari.** Hii ni aina ya ukalimani wa kibiblia ambayo kiasili ulianzishwa ndani ya dini ya Kiyahudi huko Alexandria. Ilienezwa na Philo wa Alexandria. Msukumo wake wa msingi ni shauku ya kufanya uhusiano wa Maandiko na utamaduni wa mtu au mfumo wa kifalsafa kwa mpangilio wa historia ya Biblia na/ au muktadha wa maandishi. Inatafuta uficho au kweli ya kiroho nyuma ya kila kifungu cha maandiko. Inapaswa kukubaliwa kwamba Yesu, katika Mathayo 13, na Paulo, katika Wagalatia 4, alitumia istiari kuiwasilisha kweli. Kwa hali yoyote, hii, ilikua katika muundo wa taipolojia (uanishi), na si istiari halisi.

**Uchanganuzi wa misamiati.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti ambacho kinamruhusu mtu kutambua kila muundo wa Kiyunani katika Agano Jipya. Ni mkusanyiko, katika mpangilio wa alfabeti za Kiyunani, wa kimuundo na maelezo ya msingi. Katika muunganiko kwa tafsiri mbalimbali, unaruhusu usomaji wa wasio Wayunani kuchambua visarufi vya Agano la Kale la Kiyunani kimsamiati na kimuundo.

**Ushabihiano wa Maandiko.** Hiki ni kifungu kinachotumika kueleza wazo kwamba Biblia nzima imefunuliwa na Mungu, na ni, kwa hiyo sio mkanganyiko bali ukamilifu. Ukubalifu wa dhanio hili ni msingi kwa matumizi yanayo fanana na vifungu vya maneno katika kufasiri maandiko ya biblia.

**Utata.**Hii inarejea juu ya mashaka ambayo yanaleta matokeo katika nyaraka zilizoandikwa ambapo kuna maana mbili ziwezekanazo au zaidi au wakati vitu viwili au zaidi vinakuwa vikirejewa kwa wakati mmoja. Inawezekana kwamba Yohana anatumia utata huu kwa makusudi.

**Elimu ihusuyo tabia ya mwanadamu.** Inamaanisha kuwa na "tabia zinazohusiana na wanadamu." neno hili linatumika kueleza lugha zetu za kidini kumuhusu Mungu. Linatokana na neno la Kiyunani kumuhusu mwanadamu. Inamaanisha kwamba tunazungumza kuhusiana na Mungu kana kwamba Yeye alikuwa mwanadamu. Mungu anaelezwa katika umbo la mwili lionekanalo, kijamii, maneno ya kisaikolojia ambayo yanahusiana na wanadamu (kama vile Mwa. 3:8; II Wafalme 22: 19-23). Hii, hakika ni mshabihiano pekee. Hata hivyo maarifa yetu kumhusu Mungu, ingawa ni kweli, lakini yamewekewa mipaka.

**Shule ya Antiokia.**Hii njia ya ufasiri wa kibiblia ilianzia huko Antiokia, Syria katika karne ya tatu B.K. kama kuonyesha hisia juu ya utaratibu wa kiistiari wa Alexandria, huko Misri. Msingi wa msukumo wake uliangalia maana ya kihistoria ya Biblia. Ilitafasiri Biblia kama fasihi ya kawaida ya mwaadamu. Shule hii ilikuwa imejumuishwa katika ubishi kumhusu Kristo kama alikuwa na asili mbili (mafundisho kuhusu uwili wa Yesu) au asili moja (Mungu kamili na mwanadamu kamili). Ilitambuliwa kama maoni ya kupinga Ukristo kwa Kanisa Katoriki la Rumi na kuhamishiwa Uajemi lakini shule ilikuwa na umuhimu mdogo. Misingi ya kanuni zake za ufasili wa kibiblia baadaye ikawa kanuni za ufasili wa watu walioleta mageuzi kwenye dini ya Kiprostanti (Luther and Calvin).

**Kutabaini.** Hii ni moja miongoni mwa njia tatu za uwasilishaji wa neno uliotumika kudokeza uhusiano kati ya misitari ya ushairi wa Waebrania. Unahusiana na misitari ya ushairi yenye kukinzana kimaana (kama vile Mit. 10:1; 15:1).

**Fasihi ya mafunuo.** Hii ilikuwa ni namna tanzu ya Wayahudi wenye nguvu, hata kuonekana ya kipekee. Ilikuwa ni aina ya uandishi wenye mafumbo uliotumika nyakati za uvamizi na umiliki dola yenye nguvu ya Kiyahudi. Inafikiriwa kwamba mtu, muumbwaji aliyekombolewa na Mungu na kuyatawala matukio ya ulimwengu, na kwamba Israeli ina upendeleo maalumu na uangalizi kutoka Kwake. Fasihi hii inahaidi ushindi mkuu na kupitia juhudi pekee za Mungu.

Ni ishara kuu na ya ubunifu sana yenye maneno ya mafumbo. Mara nyingi ilieleza ukweli katika rangi, tarakimu, maono, ndoto, upatanishi wa kimalaika, alama za siri za maneno, mara nyingi uwili wa vitu kati ya mema na mabaya.

Baadhi ya mifano tanzu hapa ni (1)katika Agano la Kale, Ezekieli (sura ya 36-48), Danieli (sura ya 7-12), Zekaria; na (2) Katika Agano Jipya, Mathayo 24;Marko 13; II Wathesalonike 2 na Ufunuo.

**Mtetezi.**Hili linatoka katika mzizi wa neno la Kiyahudi "ulinzi wa kisheria." Haya ni mafundisho ndani ya theolojia ambayo yanatafuta kutoa ushahidi na uwiano wa hoja za kifikra kwa imani za Kikristo.

**Haki ya kutangulia.**Kimsingi huu ni ukaribu wa maana ya neno "dhanio." Inahusisha ufikiliaji wa wa maana za awali zilizokubalika, kanuni au nafasi iliyosadikika kuwa kweli paspo uchambuzi au uchunguzi.

**Ufuasi wa Arius.**Arius alikuwa mhudumu ndani ya kanisa huko Aexandria, Misri katika karne ya tatu na mwanzoni mwa karne ya nne. Alikubali kwamba Yesu alikuwepo hapo kabla lakini si kwa Uungu (si sawa na asili ya Baba), huenda kwa kufuata Mithali 8:22-31. Alipingwa na askofu wa Alexandria, ambaye alianza (B.K. 318) mabishano yalidumu kwa miaka mingi. Ufuasi wa Arius ulikuja kuwa kanuni rasmi katika Kanisa la huko Mashariki. Baraza la Nicaea katika 325 B.K.walimshtumu Arius na kuutetea usawa na Uungu kamili wa Mwana.

**Jamii ya watu wakuu.** Alikuwa mmoja wa wanafalsafa wa kale wa Ugiriki, mwanafunzi wa Pilato na mwalimu wa Iskanda Mkuu.Ushawishi wake, hata sasa, umefika maeneo mengi yanayofundisha mafunzo ya kisasa. Hii ni kwa sababu alisistiza maarifa ni kupitia uchunguzi na upambanuzi. Hii ni moja ya itikadi ya njia za kisayansi.

**Miandiko binafsi.** Hili ni jina lililotolewa kwa maandishi ya mwanzo ya Biblia. Maandiko haya asilia yaliyoandikwa kwa mkono yote yamepotea. Baadhi tu ya nakala zimesalia. Hiki ndio chanzo cha utofauti wa maandishi mbalimbali katika machapisho ya Kiebrania na Kiyunani.

**Maandiko ya asili ya karne ya sita.** Haya ni machapisho ya Kiyunani na Kiratini ya karne ya sita B.K. Yanasanifiwa na alama "D." Imejumuisha Injili na Matendo na baadhi ya Nyalaka za Jumla. Inabainishwa na nyongeza nyingi za maandishi yenye ueledi. Inaunda msingi wa "uundaji wa maandiko"ambayo ni tamaduni za machapisho makuu ya Kiyunani nyuma ya toleo la King James Version.

**Upendeleo.** Hili ni neno linalotumika kueleza maelezo yenye nguvu kuhusiana na jambo au mtazamo fulani. Ni mtizamo ambao uadilifu ndani yake hauwezekani kungalia kitu au maoni Fulani. Ni madhara ya kieneo.

**Mamlaka ya Kibiblia.** Ni neno lililotumika katika maana maana ya kipekee. Linaelezwa kama uelewa wa kile alichokisema mwandishi asilia katika siku zile zake na kutumia ukweli huu katika siku zetu. Mamlaka za Kibiblia mara nyingi zinaelezwa kuitazama Biblia yenyewe kama kiongozi chetu chenye mamlaka. Hata hivyo, katika hali ya sasa, utafasiri sio sahihi. Nimeweka mipaka juu a dhana ya Biblia kama ilivyotafsiriwa na kanuni za njia ya historia ya kisarufi.

**Orodha ya vitabu vya Agano Jipya.**Hili ni neno linalotumika kuelezea maandishi yanayosadikiwa kuvuviwa kipekee. Limetumika kuangalia maandiko yote ya Agano la kale na Agano jipya.

**Kristo kama kitovu.**Ni neno lililotumika kuonyesha Kristo kama kitovu cha mambo yote. Na lilitumiwa kuunganisha dhana ya kwamba Yesu ni Bwana wa Biblia zote, Mawazo ya Agano la Kale dhidi yake na utimilifu wa malengo yake.

**Fasiri.**Hii ni aina pekee ya utafiti wa kitabu. Inatoa kwa pamoja usuli wa kitabu cha Biblia. Pia inajaribu kuelezea maana ya kila kipengele cha kitabu. Baadhi inatazamisha matumizi, wakati mwiingine zinahusiana na andiko katika hali ya kiufundi. Vitabu hivi ni vya manufaa, lakini lazima vitumike baada ya mtu kufanya uchunguzi wake wa awali. Tafsiri za watoa maoni lazima zisikubalike kuhakiki. Ukilinganisha fasiri nyingi toka kwa mitizamo ya wanathiolojia tofauti utaona inasaidia.

**Itifaki.** Hii ni aina ya chombo cha utafiti kwa usomaji wa Biblia. Inaorodhesha kila utokeaji wa neno katika Agano Jipya na la Kale. Inasaidia katika njia tofauti: (1) kubainisha maneno ya Kiebrania au Kiyunani yaliyoko nyuma ya maneno ya kiingereza: (2) kulinganisha kurasa ambapo neno lile lile la Kiebrania au Kiyunani limetumika: (3) kuonyesha mahali ambapo maneno mawili tofauti ya Kiebrania au Kiyunani yametafasiriwa kwa neno lie lile la kiingereza: (4) kuonyesha mwendelezo wa kutumia maneno fulani katika vitabu fulani au maandishi: (5) inasaidia mtu kupata somo katika Biblia (cf. Walter Clark's *How to use New Testament Greek Study Aids*. kurasa za 54-55).

**Magombo ya Bahari ya Chumvi.** Inarejerea mlolongo wa maandiko ya kale yaliyoandikwa katika Kiebrania na Kiarama ambayo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mwaka 1947. Palikuwepo na maktaba za kidini ya Kiyunani ya karne ya kwanza. Msukumo wa umilikaji toka Rumi na vita ya kinazi vya miaka ya sitini viliwasababisha wao kuficha magombo yaliyokuwa yamefungashwa ndani ya vyungu kwenye mapango au mashimo. Inatusaidia sisi kuelewa muundo wa kihistoria wa palestina ya karne ya kwanza na kuthibitisha maandiko ya mossoretes kuwa yako sahihi kwa kiasi fulani enzi ya awali kabla ya Yesu K.K

**Mambo yaliyofasiliwa.** Njia hii ya kimantiki au ufikiliaji inatokana na kanuni ya pamoja ya matumizi maalumu kwa njia ya wazo. Hii ni kinyume toka ufikiliaji wa mambo yaliyofasiriwa, ambayo yanaangazia njia ya kisayansi toka kwenye uchunguzi maalumu kwenda hitimisho la pamoja (nadharia)

**Mbinu pembuzi.**Hii ni njia ya kufikilisha ambapo kile kinachoonekana kuleta mkanganyiko au mafumbo huwekwa pamoja katika hali ya mkazo, ikitafuta jibu la pamoja ambalo linajumuisha pande zote za fumbo. Mafundisho mengi ya Biblia yana upembuzi unaofanana, kuamuliwa kabla-mapenzi huru, ulinzi-ustahimilivu, imani-kazi; uwamuzi-ufuasi; uhuru wa Mkristo-uwajibikaji wa Mkristo

**Wayahudi waliotawanyika katika mataifa mengine.**Hili ni neno la kiufundi la Kiyunani lililotumiwa na wapalestina wa Kiyahudi kuelezea wayahudi wengine walioishi nje ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi.

**Mlinganyo wa nguvu.** Hii ni nadhalia ya ufasili wa Biblia. Tafasili ya Biblia inaweza kuangaliwa kama mwendelezo toka ushirika wa "neno kwa neno", mahali ambapo neno la Kiingereza lazima liwekwe kwa kila neno la Kiyunani au Kiebrania, kwenye "ufasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa angalizo la chini ya neno au kifungu cha awali. Katika nadharia hizi mbili ndipo pana "mlinganyo wa nguvu" unaojaribu kuchukua neno la mwanzo kwa umakini wake, lakini limefasiliwa katika miundo ya visarufi vya kisasa na nahau. Majadiliano mazuri ya kweli ya hizi

nadharia mbali mbali za fasili zinapatikana katika makala ya Fee na Stuart *How to Read the Bible For Its Worth,* uk. 35 na katika Robert Bratcher's utangulizi katika Biblia ya TEV.

**Kutofuata mfumo.** Neno hili linatumika katika mahusiano ya uhakiki wa maandiko. Unarejerea kitendo cha kuchagua usomaji toka machapisho tofauti tofauti ya Kiyunani ili kufika kwenye neno linalotakiwa kuwa karibu na maandiko ya mwanzo.

**Kupotosha maana.** Hili neno ni kinyume cha neno fasili ya maandiko. Kama fasili ya maandiko ni "kuondoa" kulingana na kusudio la mwandishi wa awali, basi neno hili litamaanisha "kuingiza" wazo la kigeni.

**Elimu ya asili na historia ya neno.** Hii ni dhana ya usomaji wa neno unaojaribu kuyakinisha maana ya awali ya neno. Kutokana na chanzo cha maana hii, utumiaji wa kipekee unaotambulika kirahisi katika ufasili, elimu ya asili na historia ya neno sio kiini cha mtizamo, mbali na maana ya wakati ule ule na utumiaji wa neno.

**Fasili ya maandiko.** Hili ni neno la kiufundi kwa utendaji wa kutafasili kifungu maalumu. Inamaanisha "uondoaji nje" (wa neno) ukidokeza kwamba dhumuni letu ni kuelewa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika uelewa wa muundo wa kihistoria, mazingira ya kifasihi, sintaksi na maana ile ile ya neno.

**Namna ya Uwasilishaji.** Hili ni neno la Kifaransa ambalo limedokeza aina mbali mbali ya fasihi. Msukumo wa neno hili ni mgawanyiko wa miundo ya fasihi katika namna mbali mbali ambazo zinashirikishana tabia za aina moja. Usimuliaji wa kihistoria, mashairi, mithali, ufunuo na uandikishaji.

**Maarifa ya utambuzi/mafunuo.** Zaidi ya maarifa tulionayo kuhusu imani potofu yameletwa toka maarifa ya utambuzi wa maandiko katika karne ya pili. Ingawa mawazo ya awali yalikuwepo katika karne ya kwanza (na kabla). Baadhi ya maelezo ya mafunuo ya kinazi ya Valentino na Cerinthin ni (1) mwili na roho vyote vilikuwepo kabla. mwili ni mwovu, na Roho ni nzuri. Mungu, ambaye ni Roho hawezi kuhusishwa moja kwa moja na mwili mwovu (2) kuna asili (*eons au* daraja la kimalaika*)* kati ya Mungu na mwili. Wa mwisho au wa chini alikuwa YAHWE wa Agano la kale, ambaye aliuumba ulimwengu (*kosmos*); (3) Yesu alikuwa mwanzilishi kama YAHWE lakini akiwa juu ya viwango, karibu na Mungu wa kweli. Wengine walimweka juu zaidi lakini bado yu chini kuliko Mungu na hakika asiye na mwili wa Kiungu (kama vile 1:14). Kwa vile mwili ni mwovu, Yesu asingelikuwa na mwili wa kibinadamu na bado akawa na hali ya Kiungu. Alikuwa ni nafsi ya kufikirika (kama vile 1 Yoh 1:1-3; 4:1-6); na (4) wokovu ulipatikana kupitia imani katika Yesu pamoja na maarifa maalumu, yaliyojulikana na watu maalumu. Maarifa (maneno ya siri) yalihiiitajika kupitia ulimwengu wa kimbingu. Washikiliaji sana wa kisheria za Kiyahudi nao pia walihitaji kumfikia Mungu. Walimu wa uongo wenye maarifa ya utambuzi walitetea miundo miwili kinzani ya kimaadili (1) baadhi ya stadi za maisha hazikuhusiana na wokovu. Kwao wokovu na utakaso ulifumbwa kwenye maarifa ya siri (neno la siri) kupitia ulimwengu wa kimalaika (*eons)*; au (2) kwa wengine stadi ya maisha ilikuwa muhimu katika wokovu. Walisisitiza miundo ya maisha kama kielelezo cha utakaso wa kweli.

**Kanuni za ufasili.** Hili ni neno la kiufundi kwa kanuni zinazoongoza ufasili wa maandiko. Ni seti ya mwongozo maalumu na sanaa/kipawa. Kibiblia, au takatifu, kanuni za ufasili zimegawanyika kwa namna mbili; kanuni za ujumla na kanuni maalumu. Hizi zinahusiana na aina tofauti za fasihi zinazopatikana katika Biblia. Kila aina tofauti (tanzu)zina mwongozo wake wa kipekee lakini zinashirikiana na baadhi ya dhana na namna ya utafasili.

**Uhakiki juu ya maandiko.** Hii ni namna ya utafasili wa kibiblia ambao unatazamisha kwenye muundo wa kihistoria na umbo la fasihi hasa hasa katika kitabu cha Biblia.

**Nahau.** Neno hili linatumika kwenye vifungu vinavyopatikana katika tamaduni tofauti zenye maana maalumu na sio vilivyohusiana na maana ya kawaida ya maneno binafsi. Maana ya mifano ya kisasa ni: "ilikuwa ni vizuri sana" au "umeniua". Biblia pia inajumuisha aina hizi za vifungu.

**Nuru.**Hili ni jina lililotolewa kwenye dhana kuwa Mungu aliongea na mwanadamu. Dhana nzima kwa kawaida imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda kwenye historia ya binadamu: (2) uvuvio-ametoa utafasili sahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) nuru –ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Kudukiza.** Hii ni njia ya kimantiki au kufikiria inayotoka sehemu Fulani na kuenea sehemu yote. Ni njia ya kutegemea majaribio ya kisasa. Kimsingi, huu ni mjongeo wa watu wenye hadhi ya juu.

**Unasaba.** Hii ni aina ya chombo cha uchunguzi kinachoruhusu wale wasiojua lugha za kibiblia kuchunguza maana yake na muundo. Inaweka tafasili ya kiingereza kwenye ngazi ya neno kwa neno chini ya lugha ya awali ya kibiblia. Chombo hiki kinajumuishwa na "misamiati ya kiuchunguzi" ambayi inatoa miundo na maelezo ya msingi ya Kiebrania na Kiyunani.

**Uvuvio.**Hii ni dhana ya kwamba mungu aliongea na mwanadamu kwa kuwalinda waaandishi wa kibiblia kwa usahihi na uwazi ili kuweka kumbukumbu ya mafunuo yake. Dhana nzima imeelezewa kwa namna tatu: (1) ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) uvuvio-ametoa utafasiri wasahihi wa matendo yake na maana yake kwa watu Fulani waliochaguliwa kuweka kumbukumbu ya mwanadamu: na (3) Nuru-ametoa roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa mafunuo yake.

**Lugha ya maelezo.** Hii inatumika pamoja na nahau pale Agano la Kale lilipoandikwa. Inaongelewa juu ya dunia kwa namna jinsi vitu vinavyotokea kwenye milango mitanmo ya fahamu. Sio maelezo ya kisayansi hata yakamaanisha kuwepo.

**Ushikiliaji sana wa sheria.** Mwenendo huu umeainishwa kwa msisitizo zaidi juu ya sheria au matambiko. Unajaribu kutegemea juu ya utendaji wa mwanadamu kama njia ya ukubalifu kwa Mungu. Unajaribu kushusha uhusiano na kuinua utendaji, mwote ambamo dhana muhimu ya mahusiano ya kimaagano kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mtenda dhambi.

**Tafasili sisisi.** Hili ni jina jingine la mlengo wa kimaandiko na njia za kihistoria za za kanuni za ufasili toka Antiokia. Ina maana kwamba utafasili unahusika katika maana dhahili za lugha ya mwanadamu, ingawa inaendelea kutambua uwepo wa lugha za kitamathali.

**Fasihi tanzu.** Hii inarejerea kwenye miundo ya utofauti ili kwamba mawasiliano ya uwanadamu yanaweza kuchukuliwa kama vile ushairi au simulizi za kihistoria. Kila aina ya fasihi ina nji/namna yake maalumu ya kanuni ya ufasili kwa kuongezea kwenye kanuni za pamoja kwa fasihi zote zilizoandikwa.

**Sehemu ya fasihi.** Hii inarejerea mgawanyo wa lengo kuu la kitabu cha Kibiblia. Inaweza kuundwa na misitari, aya, au ibara chache. Ni kijumuishi pekee chenye kiini cha somo.

**Lower criticism- Uhakiki wa kawaida wa maandiko.**

**Maandiko ya asili.** Neno hili linahusiana na nakala mbali mbali za Agano jipya la Kiyunani. mara nyingi limegawanyika katika aina tofauti kwa (1) nyenzo iliyotumika kuandikiwa kwayo (mafunjo, ngozi) au (2) muundo wenyewe wa uandishi. Limefupishwa kwa neno "MS" (umoja) au "MSS" (wingi).

**Andishi la kidesturi la Kiebrania la Biblia ya Kiyahudi.** Hii inarejerea karne ya nane B.K. maandiko ya asili ya Kiebrania ya Agano la kale yalitolewa na vizazi vya wasomi wa Kiyahudi ambayo yalijumuisha alama za irabu na mihtasari mingine ya maandiko. Yanatengeneza msingi wa neno kwa Agano letu la kale la Kiingereza.

**Mshabihiano wa neno.** Huu ni namna ya msemo ambao jina la kitu linatumika mbadala wa kitu kingine kinachofanana nacho. Kwa mfano " birika linachemka" ki uhalisia inamaanisha "maji yaliyeko kwenye birika yanachemka".

**Orodha ya vitabu vya Agano jipya.** Hii ni orodha ya vitabu vya sheria za kanisa la Agano jipya. Iliandikwa huko Rumi kabla ya mwaka 200 B.K. Inatoa vitabu ishirini na saba kama vile vile vya Agano Jipya la Waporostanti. Hii wazi kabisa inaonyesha makanisa madogo madogo ya mahali katika sehemu mbali mbali za milki ya Rumi kulikuwa "kiutendaji" pamewekwa sheria za kanisa kabla ya baraza kuu la kanisa la karne ya Nne.

**Ufunuo wa asili.** Hii ni namna ya Mungu mwenyewe kujifunua kwa mwanadamu. Unajumuisha utaratibu wa kiasili (Rum 1:19-20) na dhamila adilifu (Rum 2:14-15). Umeongelewa katika Zaburi 19:1-6 na Warumi 1-2. Unatofautishwa toka kwenye mafunuo maalumu, ambayo kwa mungu mwenyewe ni muhimu kujifunua katika Biblia na mwanae pekee Yesu wa Nazareti. Uangaliaji huu wa kithiolijia unasisitizwa tena na mwenendo wa "dunia ya zamani" kati ya wanasayansi wa Kikristo (kama vile maandishi ya Hagh Ross) wanatumia uangaliaji huu kwa kuthibitisha kuwa kweli yote ni kweli ya Mungu. Ulimwengu ni mlango ulio wazi wa maarifa ya kumjua Mungu; ni tofauti toka kwa ufunuo maalumu (Biblia); unawapa wanasayansi uhuru wa kufanya uchunguzi juu ya utaratibu wa kiasili. Kwa maoni yangu , hii ni fursa mpya ya ajabu kushuhudiwa juu ya wanasayansi wa ulimwengu wa magharibi.

**Ufuasi wa Nestory.** Nestory alikuwa ni mkuu wa familia ya Constantino kwenye karne ya tano. Alifundishwa huko Antiokia ya Syria na kuthibitisha kwamba Yesu ana asili mbili, moja ni mwanadamu kamili na nyingine ni Mungu kamili. Maoni haya yalichepushwa toka kwenye mtizamo wa asili wa mtu mmoja wa Orthodox kutoka Alexandria. Kusudio kubwa la Nestory lilikuwa ni cheo cha "mama wa Mungu" alichopewa Maria Magdalena. Nestory alipingwa na Cycil wa Alexandria na, kwa kuwekwa matatani juu ya mafundisho yake huko Antiokia. Antiokia yalikuwa makao makuu ya mtazamo wa kihistoria wa visarufi vya maandiko kwa utafasili wa Kibiblia, wakati Alexandria yalikuwa makao makuu ya shule Nne zilizotengwa kwa ajili ya utafasili. Nestory hatimaye aliondolewa toka ofisini na kukimbilia mafichoni.

**Mwandishi wa awali.** Hii inarejerea wandishi halisi wa maandiko

**Mafunjo/Magombo.** Haya yalikuwa aina mojawapo ya nyenzo toka Misri zilizotumika kuandikiapo maandiko. Yalitengenezwa kwa majani au magome ya miti. Ni nyenzo ambazo nakala za zamani Agano la Kale la Kiyunani zilihifaziwapo.

**Vifungu Mlinganyo**. Ni sehemu ya mtazamo kuwa yote yaliyomo kwenye Biblia yametoka kwa Mungu na, kwa hiyo, ni ufafili wake mahsusi na mlinganyo wa kweli wa kimafumbo. Hili pia ni la msaada pale mtu anapojaribu kutafasili kifungu kisicho wazi au kigumu. Pia inamsaidia mtu kupata kifungu kilicho wazi juu ya somo husika vile vile mtazamo wote wa kimaandiko juu ya somo husika.

**Ufafanuzi/fasili.** Hili ni jina la nadhalia ya utafali wa Biblia. Utafasili wa Biblia unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa mahusiano wa "neon kwa neon" ambapo neon la Kiingreza laweza kuweka kwa kila neon la Kiebrania au Kiyunani kwenye "fasili" ambapo tu wazo limetafasiliwa kwa mtizamo wa kawaida wa neon au kifungu cha awali. Kati ya nadhalia mbili hizi "mlinganyo wa nguvu" ambao unajaribu kuchukuawa kwa umakini andiko la awali lakini likatafasiliwa katika muundo wa kisasa wa kisarufi na nahau. Kweli kabisa mjadara mzuri wa nadhalia hizi mbali mbali za utafasili zinapatikana katika chapisho la Fee na Stuart *How to Read the Bible For All Its Worth, Uk. 35.*

**Aya.** Huu ni msingi wa ufasili wa fasihi moja kinadhalia. Unajumuisha wazo moja kuu na mwendelezo wake. Tukibaki na musukumo wake mkuu hatutatazama juu ya udogo wake au uzuri wa kusudi la mwandishi wa awali.

**Uparokia.** Hii inahusiana na mapendeleo yaliyofungiwa kwenye muundo wa tamaduni/ thiolojia ya kawaida. Haitambui asili ya mapokeo ya kweli yaliyobadilika ya Kibiblia au matumizi yake.

**Fumbo.** Hii inarejerea kweli zile zinazoonekana kuleta mkanganyiko, nab ado zote zikabaki kuwa kweli, ingawa bado zinakinzana. Zinaunda kweli kwa kuwakilisha toka pande zilizo kinyume. Kweli nyingi za Kibiblia zinawakilishwa kimafumbo (au kiupembuzi). Kweli za Kibiblia sio kama nyota zilizotengana, zimetengenezwa kwa ukilimio wa sehemu za nyota.

**Pilato.** Alikuwa ni mmoja ya wanafalsafa wa Ugiriki ya kale. Falsafa yake kwa kiasi kikubwa ulisababisha kanisa la mwanzo kupitia wasomi wa Alexandria, Misri na baadaye, Augustino. Alituma ujumbe kuwa kila kitu duniani ni kiini macho na ni mfano tu wa kielelezo asili wa vitu vya rohoni. Baadaye wanathiolojia wakasawazisha "mtizamo/mawazo" ya Pilato na ulimwengu wa kiroho.

**Dhanio.** Hili linarejerea uelewa wa jambo tulilowaza kabla. Mara nyingi tunaunda wazo au hukumu kuhusu mambo hata kabla hatujatazamisha maandiko yenyewe. Uelekezaji huu vile vile hujulikana kama upendeleo, kujitanguliza mbele, kudhania au kuelewa kabla.

**Uhakiki wa maandishi.** Hiki ni kitendo cha kutafasili maandiko kwa nukuu za kifungu bila kuangalia mazingira ya haraka au ukubwa wa mazingira katika fahisi moja. Hii inaondoa vifungu toka kwa kusudio la mwandishi wa awali na mara nyingi unahusha jaribio la kuhakiki maoni binafsi wakati huo likithibitisha mamlaka ya Kibiblia.

**Ualimu wa dini ya Kiyahudi.** Ngazi hii ya maisha ya watu wa Uyahudi yalianza walipokimbilia Babel (586-538 K.K). kama ushawishi wa makuhani na hekalu ulivyoondolewa, masinagogi ya kawaida yakawa mtizamo wa maisha ya Kiyahudi. Hivi vitovu vya kawaida vya tamaduni za Kiyahudi, ushirika, kuabudu na elimu ya Biblia ikawa mtizamo wa maisha ya kidini kitaifa. Katika siku za Yesu, hii "dini ya wandishi" ilikuwa sambamba na ile ya makuhani. Katika kuanguka kwa Yerusalem mwaka wa 70 B.K muundo wa kiandishi, ukitawaliwa na mafalisayo, walidhibiti mwelekeo wa maisha ya kidini ya Kiyahudi. Inachagizwa na utafasili wa kiutendaji, na wa kisheria wa Torah kama ulivyoelezwa katika tamaduni za Talmud.

**Ufunuo.** Hili ni jina lililopewa kwenye dhana ya kwamba Mungu amesemezana na mwanadamu. Wazo zima mara nyingi limeelezewa katika maneno matatu- (1) Ufunuo-Mungu ametenda katika historia ya mwanadamu (2) Uvuvio-Ametoa tafasili sahihi ya matendo yake na maana yake kwa mtu Fulani aliyemchagua kuweka kumbukumbu ya mwanadamu (3)Nuru-Amempa Roho wake kumsaidia mwanadamu kuelewa ukaribu wake.

**Elimu-maana.** Hii imerejerea kipimo halisi cha maana kinachohusiana na neno. Kimsingi ina vidokezo mbali mbali vya neno katika mazingira tofauti.

**Maandiko ya kale ya Kiyunani.** hili ni jina lililopewa tafasili ya Kiyunani ya Agano la kale la Kiebrania. Mafundisho ya zamani yanasema kuwa yaliandikwa kwa siku 70 na wasomi sabini wa Kiyahudi kwa ajili ya maktaba ya Alexandria, Misri. Tarehe ya kimapokeo ilikuwa 250 K.K (kiukweli yawezekana ilichukua zaidi ya miaka Mia kumaliza kuandika). Tafasili hii ni muhimu kwa sababu (1)inatupatia andiko la kale kulinganisha na andiko la Kiebrania (2) inatuonyesha sisi hali ya utafasili wa Kiyahudi katika karne ya pili nay a tatu K.K (3) inatupatia uelewa wa umasihi wa Kiyahudi kabla ya kumkataa Yesu. Kifupi chake ni "LXX".

**Machapisho ya asili.** Haya ni machapisho ya asili ya Kigiriki ya karne ya Nne B.K Yalivumbuliwa na msomi wa Kijerumani, Tischendorf, katika nyumba ya mtawa Catheline, kwenye eneo la kimila la mlima Sinai. Maandishi haya yameundwa na herufi ya kwanza ya Kiebrania ya alfabeti inayoitwa "*eleph*" (א). Yanajumuisha Agano la Kale na Agano Jipya kwa pamoja.

**Kujitakasa.** Hili neno ni kisawe chenye istiari katika maana kuwa linakwenda mpaka kwenye historian a mazingira ya fasihi ya kifungu na kulifasili katika msingi wa jambo lingine.

**Visawe.** Hii inarejerea maana yenye kariba au mfano wa maana moja (ingawa kiukweli hakuna maneno mawili yenye elimu-maana kamili iliyopishana). Kwa karibu sana yanahusiana kiasi kwamba moja linaweza kuwa mbadala wa lingine katika sentesi bila kupoteza maana. Pia yanatumika kuunda moja kati ya miundo mitatu ya mlinganyo wa ushairi wa Kiebrania. Kwa maana hii inarejesha mistari miwili ya ushairi ambayo inaelezea kweli ile ile (cf. Zab 103:3).

**Sintaksi.** Hili ni neno la Kiyunani linalirejeresha muundo wa sentesi. Inahusiana na namna ya sehemu ya sentesi zinaweza wekwa pamoja kuleta maana kamili.

**Usanisi.** Hii ni moja ya maneno matatu yanayohusiana na aina ya ushairi wa Kiebrania. NenO hili linaongelea juu ya mistari ya ushairi uluojengwa juu ya mwingine katika maana moja, wakati mwingine huitwa "taaluma ya mabadiliko ya hali" (k.v. Zab 19:7-9).

**Thiolojia mpangilio.** Hii ni hatua ya utafasili ambayo inajaribu kuhusisha ukweli wa Biblia katika hali ya pamoja na mlingano. Ina mantiki zaidi kuliko historia tupu, ni uwasilishaji wa thiolojia ya Kikristo kwa namna ( Mungu, mtu, dhambi,wokovu).

**Buku la taratibu na kanuni za Kiyahudi.** Ni wadhifa uliokuwapo kwa ajili ya upangaji wa simulizi za kanuni na taratibu za Kiyahudi. Wayahudi wanaamini ulitolewa kwa Musa kwa kusimuliwa na Mungu kwenye mlima Sinai. Ki-ukweli inaelekea kuwa ni mkusanyiko wa hekima za walimu wa Kiyahudi kwa miaka mingi. Kuna matoleo mawili tofauti yaliyo andikwa juu ya Talmud: ya Babel na fupi la kiparestina ambalo halikwisha.

**Uhakiki wa tofauti za kiuwandishi.** Huu ni usomaji wa maandiko wa Biblia. uhakiki wa maandiko ni muhimu kwa sababu hakuna maandiko ya mwanzo yaliyopo na nakala zilizopo zinatofautiana toka moja hadi nyingine. Unajaribu kuelezea utofauti na kufika (karibu iwezekanavyo) na maneno ya awali kabisa ya miandiko ya Agano la kale na jipya. Mara nyingi unaitwa "uhakiki wa asili ya neno".

**Upokeaji wa Maandiko.** Usanifishaji huu ulianzia kwenye toleo la Elzevir la Agano jipya la Kiyunani katika mwaka wa 1633 B.K Kimsingi ni muundo wa Agano jipya la Kiyunani lililozalishwa toka kwenye maandiko machache ya asili ya Kiyunani na matoleo machache ya Erasmo ya Kilatini (1510-1535), Stephano (1546-1559) na Elzevir (1624-1678). Katika *An Introduction to the Textual Criticism of The New Testament uk. 27 cha A.T Robertson* anasema "andiko la Byzantine kiutendaji ni aina ile ile ya uundaji wa maandiko. Andiko la Byzantine ni la thamani ya chini kati ya familia tatu ya maandiko ya awali ya Kiyunani (Kimagharibi, Alexandria na Byzantine). Inajumuisha mkusanyiko wa makosa ya karne nyingi za maandiko na nakala za mkono. Hata hivyo, A.T Robertson alisema uundaji wa maandiko umetunza kwa ajili yetu andiko sahihi kimalidhawa (uk.21). Mapokeo haya ya maandiko ya asili ya Kiyunani (hasa Erasmo, toleo la tatu la 1522) yanatengeneza msingi wa toleo la King James la mwaka 1611 B.K

**Sheria za Musa.** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya "ufundishaji". Lilitokea kuwa wadhifa rasmi wa maandishi ya Musa (Mwanzo mpaka Kumbu kumbu la Torati). Kwa Wayahudi ulikuwa ni mgawanyo wa kimamlaka wa kanuni za kanisa la Kiebrania.

**Uanishaji.** Hii ni aina ya urasimishaji wa wa utafasili. Mara nyingi unahusisha kweli ya Agano jipya inayopatikana katika vifungu vya kale kwa njia ya analojia. Namna hii ya kanuni za ufasili ilikuwa ni dalili kubwa ya njia za Alexandria. Kwa sababu ya matukano ya aina hii ya utafasili, mtu lazima aweke ukomo wa matumizi yake kwa mfano mahsusi ulioandikwa katika Agano jipya.

**Maandiko ya Vatican.** Haya ni maandiko ya asili ya Kiyunani ya karne ya Nne B.K . Yalipatikana kwenye maktaba ya Vatican. Uwasili wake unajumuisha vitabu vyote vya Agano la kale, ufunuo na Agano jipya. Hata hivyo, sehemu zingine zilipotea( Mwanzo, Zaburi, Waebrania, Filemon na Ufunuo). Inasaidia maandiko ya asili kubadilisha miandiko ya maneno ya awali. Tena yameundwa kwa herufi kubwa "B".

**Tafasili ya Biblia ya Kilatini.** Ni jina la tafasili ya Biblia ya Kilatini ya Jerome. Ilikuwa ndio msingi au utafasili wa "kawaida"wa kanisa Katoriki la Rumi. Lilifanyika mwaka 380 B.K

**Hekima ya Fasihi.** Hii ni fasihi tanzu iliyozoeleka enzi za kale karibu na pande za Mashariki (na ulimwengu wa kisasa). Kimsingi lilikuwa ni jaribio la kuelekeza kizazi kipya juu ya mwongozo wa maisha ya ushindi kupitia ushairi, mithali, au insha. Ilielezewa zaidi kwa watu binafsi kuliko kwenye jumuiya iliyoungana. Haikutumia viini macho kuweka historia, lakini ilisimamia uzoefu na uchunguzi wa maisha katika Biblia, Ayubu kupita Wimbo ulio Bora, anasadiki uwepo na ibada ya YAHWE, lakini mtizamo huu wa ulimwengu wa kidini sio wa wazi kwa uzoefu wa kila mtu kila wakati.

**Picha ya ulimwengu na Mtizamo wa Kidunia.** Haya ni maneno mwandani. Yote yana dhana ya kifalsafa kuhusiana na uumbaji. Neno "picha ya ulimwengu" inarejerea "kwa namna gani" juu ya uumbaji wakati "mtizamo wa kidunia" unahusiana na "nani." Maneno haya yote ni muhimu kwenye utafasili pale mwanzo 1-2 inaposhughulika hasa hasa na nani, na sio kwa namna gani juu ya ulimwengu.

**YAHWE/YEHOVA.** Hili ni jina la Agano la Mungu katika Agano la kale. Linaelezewa katika kitabu cha Kutoka 3:14. Ni muundo wa KISABABISHAJI wa neno la Kiebrania "kuwa" ambalo Wayahudi waliogopa kulitamka jina hili ili wasilitamke bure; kwa hiyo, walitumia jina lingine badala yake yaani "Adonai" likimaanisha "Bwana". Hivi ndivyo jina la Agano limetafasiliwa katika Kiingereza.

# KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milelekwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”. Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa

kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

"Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo."